# Ustaarabu Wa Watu wema 2

Othman Nuri TOPBASH



ERKAM PUBLICATIONS




Istanbul – 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

# Ustaarabu wa watu wema - 2

Othman Nuri Topbash

**Jina la Asili :** Asr-ı Saadet'ten Günümüze Faziletler Medeniyeti - 2

**Mwandishi :** Othman Nuri Topbash

**Msimamizi Mkuu :** Abdi Mohamed Adam

**Mfasiri :** Hemedi Dhuli Hemedi

**Mhariri :** Ibrahimu H. Kabuga

**Msanifu jalada :** Sarkhan Isgandarov

**Kupangiliwa vizuri na** Sarkhan Isgandarov, Nijat Garibov

**ISBN:** 978-9944-83-714-9

**Mchapaji:** Erkam Printhouse

**Anuani:** Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir, Istanbul, Turkey

**Simu:** (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748

**Barua pepe:** info@islamicpublishing.org

**Tovuti:** www.islamicpublishing.org

**Language :** Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

# Ustaarabu Wa Watu wema

## - 2 -

**Othman Nuri TOPBASH**

ERKAM PUBLICATIONS

**YALIYOMO**

## SEHEMU YA PILI
## MWENENDO WA KIISLAMU NA
## SILKA YA MOYO


1. Upendo ........ 9
    a. Kumpenda Mwenyezi Mungu (Mahabbatullah) ........ 10
    b. Kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ........ 30
    c. Kuwapenda waislamu wenzetu ........ 80
    d. Kuvipenda viumbe vyote ........ 92
2. Hofu na matumaini ........ 108
3. Tazim au unyenyekevu ........ 131
4. Kuheshimu amana ya mtu na kuchunga ahadi ........ 151
5. Sadaqat (Uaminifu na kujitolea) ........ 168
6. Kuikubali hali yako ........ 181
7. Tawakkul na kujisalimisha ........ 196
8. Ihsan na kuwa macho ........ 216
9. Tawadhu' (Unyenyekevu) ........ 230
10. Hilm na Musamahah (upole na uvumilivu) ........ 254
11. Kuwa na dhana njema katika kila kitu ........ 268

12. Ukarimu na kujiepusha na ubinafsi ....................................277
13. Qanaat na Istighna (Kukinai na kutosheka)..........................301
14. Kujitenga na dunia ..................................................................319
15. Subira na ushupavu.................................................................340
16. Hamd (Kusifu) na Shukur (Kushukuru)................................354
17. Shajaa’ (Ujasiri).........................................................................370
18. Istiqama (Msimamo) ...............................................................386
19. Shukurani na utii.......................................................................394
20. Kujihifadhi na kuwa na staha ................................................411
21. Akili (Fatanah) na utambuzi (Firasah) .................................428
22. Kuutakasa moyo na roho .......................................................448

# Sehemu ya 2




# Mwenendo Wa Kiislamu Na Silka Ya Moyo

**1. Upendo**

Upendo ndio unaofanya maisha kuwa ya kupendeza, yenye amani na furaha. Unga wa uwepo wetu imekandwa na chachu ya upendo. Upendo ni moja ya fadhila kubwa ambazo Mola wetu amewapa waja wake. Hii ndio sababu hatuna budi kuelekeza mapenzi yetu kwenye zile nyoyo ambazo zimeelewa maana ya urafiki. Hatahivyo ni jambo la kusikitisha kuona watu wengi wanapoteza mapenzi yao kwa kupitia matamanio ya kidunia yenye kupita. Na ni ipi thamani ya moyo ambao umekuwa mgumu kiasi cha kushindwa kuhisi mapenzi ya Mwenyezi Mungu?

Jalaluddin Rumi anatoa mfano ufuatao kama somo kwa wale wanaochezea mtaji wao wa mapenzi kwa upuuzi na ambao wamenyang'anywa mapenzi ya Mwenyezi Mungu:

*'Wale wanaoipa dunia hii nyoyo zao ni kama wawindaji ambao wanawinda kivuli. Ni vipi mtu ataweza kukamata kivuli? Muwindaji mpumbavu alidhani kivuli cha ndege ndiye ndege mwenyewe na kujaribu kumkamata. Hata ndege mwenyewe aliyekuwa kwenye tawi alishangazwa na mpumbavu huyu.'*

Lengo letu kuu ni kukutana na Mwenyezi Mungu. Kusahau hili na kutekwa na vitu vya kupita kama mali, utajiri, cheo, familia ya mtu au watoto, ni kuuteketeza moyo wa mtu. Mshairi mmoja ameelezea jambo hili kama ifuatavyo:

*"Ondoa mdomoni mwako vyote kinyume na Mwenyezi Mungu, ili ukweli ujidhihirishe.*

*Sultani hawezi kuingia kwenye ngome mpaka iwe imejengwa vizuri"*

Ushindi wa Majnun katika safari yake kuelekea kwa Mwenyezi Mungu ulitokana na kutotekwa na Laila, ambaye alienea katika fikra zake. Kwa maneno mengine ni kwamba hakumfanya Laila kuwa ndio kikomo cha mapenzi yake. Alitoka kwenye mapenzi ya kiistiari (ya bandia) na kuelekea kwenye mapenzi ya kweli, mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Bila shaka hili ni jambo gumu ambalo watu wengi wanalishindwa. Laila anaweza kusimama badala ya vitu vingi- jinsia tofauti, mali, cheo na hadhi. Vipenzi hivi ambavyo vinaitwa 'vipenzi vya mfano', havina budi kufanywa kuwa madaraja au ngazi kuelekea kwenye mapenzi ya kweli.

### a. Kumpenda Mwenyezi Mungu *(Mahabbatullah)*

Mtu anampenda mtu mwingine kiasi kwamba anayependwa anathamini mapenzi yake. Hii ndio sababu moyo wa mwanadamu unaweza kufikia mapenzi ya hali ya juu ikiwa ataelekeza mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu. Kwani Mwenyezi Mungu pekee ndiye anayestahiki mapenzi ya kweli, Ambaye ndiye chanzo cha mapenzi yote. Haya ni kwa sababu:

- Aliyeumba kila kitu, ambaye anatoa riziki kwa viumbe vyote, ambaye anavilinda na kuvisimamia ni Mwenyezi Mungu, mwenye ukamilifu na nguvu.

- Anawapenda mno waja wake. Alimuumba Adam mbinguni katika umbile bora na kwa umakini wa hali ya juu. Pia anapenda waja wake waingie peponi. Majibu ya upendo ni upendo.

- Amemrahisishia mja njia za kukutana naye na njia ya kupata mapenzi yake.

- Yeye ni mmiliki wa hii dunia na kesho akhera.

- Mwishoni mtu atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi na atakosa pa kukimbilia, pa kujificha na msaidizi kinyume na Yeye. Uzuri ulioje wa ulinzi na usaidizi wa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.

- Zaidi ya fadhila zote hizi, Mwenyezi Mungu ametufanya kuwa miongoni mwa watu ndani ya umma wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anayempenda kuliko mitume yote, na ametupatia kitabu kilicho bora zaidi, Qur'an tukufu.

- Hivyo sharti la utumishi wetu kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ni kuelekeza mapenzi yetu kwake.

Bila shaka upendo utajidhihirisha kwa namna tofauti kwa kila kipenzi cha Mwenyezi Mungu. Ndio maana Rumi akawa chanzo cha maana na hekima, ambapo vyote vilikuwa vikimimika kutoka kinywani mwake kama lulu hadimu zilizomo kwenye kina cha bahari ya maneno yake na mapenzi yaliyokuwa yakiunguza moyo wake. Hallaj-i Mansur alifadhilishwa kwa kujaaliwa kukutana na Mwenyezi Mungu akhera kutokana na kupenda kwake kufa shahidi. Kwa miaka mingi Bahauddin *Nakshibend* alijishugulisha na kusaidia wanyama wenye vidonda na waliojeruhiwa, kusafisha mitaa na kuwasaidia wagonjwa ambao watu wengine walikuwa nao mbali. Kwa njia alijitolea mali yake yote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kufikia kuwa bahari ya kumfahamu Mwenyezi Mungu na kupata radhi zake. Njia zao zilikuwa tofauti lakini ubora wa nyoyo zao ulikuwa sawa daima. Yani kuwa na upendo na mapenzi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewatuma watu wake wema kwenda kwa wanadamu. Kila mmoja amekuwa akidhihirisha mambo mbalimbali na wamekuwa kama maua ambayo yamejaa ufahamu na mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Kwa kifupi ni kwamba muumini ambaye anampenda Mwenyezi Mungu hana budi kufahamu na kutambua kuwa ki ukweli hamiliki kitu chochote hapa duniani. Mapenzi yanahitaji kujitolea na hivyo hayawezi kuoana na umiliki. Inamaanisha kuwa yeyote anayependa hana budi kuwa tayari kutoa chote alichonacho kwa ajili ya ampendae. Mapenzi yanazaa kawaida ya moyo kuwa tayari kutoa vyote mali na nafsi. Haya yanafanyika kutokana na uzito wa mapenzi yaliyopo. Ndio maana watu wanatoa vitu vyao vya thamani kubwa kutokana na kiwango chao cha mapenzi. Kwa kutegemea uzito wa mapenzi ya mtu, yanaweza kujidhihirisha yenyewe katika hali ya mtu kujitolea hata maisha yake kwa ajili ya ampendae.

Furaha ni kwa wale wanaoshikamana na mapenzi kwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake zaidi ya vitu vingine vyote na hawadanganyiki na maua ya uongo yaliyomo ndani ya pori na bustani zenye magugu mengi.

***Matukio ya wema***

Bila shaka kilele cha watu katika kumpenda Mwenyezi Mungu ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ[1] aliyebarikiwa. Katika kutafuta mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alikuwa akirudia mara kwa mara dua ifuatayo ya nabii Daud عليه السلام ndani ya swala zake:

‘*Allahumma inni as'aluka hubbika wa hubba man yuhibbuka wa'l 'amiliilladhi yuballighunni hubbaka. Allahumma'j'al hubbaka ahabba ilayya min nafsii wa ahliy wa minal maa'il baarid*’

‘Ewe Mwenyezi Mungu! Naomba unijaalie mapenzi juu yako, mapenzi ya wale wanaokupenda na amali zitakazoniwezesha

1. ﷺ katika kiarabu ni kifupisho cha "*sallallahu alayhi wa sallam*" na kinamaanisha "Rehema na amani ziwe juu yake". Meneno haya husemwa kila jina la Mtume linapotajwa (maelezo ya mfasiri).

kupata mapenzi yako. Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie nikupende zaidi ya roho yangu, familia yangu, mali zangu na maji ya baridi' (Tirmidhi, Dawat, 72/3490).

Dua nyingine ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kama ifuatavyo:

'Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie mapenzi yako na mapenzi ya yeyote ambaye mapenzi yake yatakuwa yana faida mbele yako. Ewe Mwenyezi Mungu! Jaalia neema ulizonipa na yale ninayoyapenda kuwa nguvu ya kunifanya nikupende Wewe na kufanya matendo ambayo Utayaridhia. Ewe Mwenyezi Mungu! Jaalia vitu ambayo nimekuomba lakini bado hujanipa kuwa njia ya kukuelekea Wewe kwa utii na akili yangu kushughulishwa na mambo unayoyapenda' (Tirmidhi, Dawat, 73/3491).

❁

Ni jambo la kawaida kuwa kipenzi haachi kumuongelea na kumfikiria yule ampendae wakati wote. Hivyo hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa katika hali ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu katika kila hali na alikuwa akimuomba Mola wake katika kila hatua yake na huku akitafakari juu ya sifa zake, nguvu na udhihirisho wa ukubwa wake na neema alizomjaalia. Hivyo dua alizoomba katika nyakati tofauti na mahali tofauti, kama vile alipokuwa akienda mahali, aliporudi, alipokaa, aliposimama, alipoanza jambo lolote na alipomaliza, zilifikia idadi kubwa kiasi kwamba maswahaba zake hawakuweza kuzihifadhi zote na ndio sababu walimuomba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ awape dua fupi na nzuri.

❁

Uzuri ulioje wa simulizi ifuatayo inayotutaarifu jinsi mtu anavyoweza kupata mapenzi ya Mola wetu na kupata radhi zake na unyenyekevu wa hali ya juu:

Siku moja maswahaba waliobarikiwa walimuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

'Tunawaona waumini wawili, mmoja yupo ndani ya unyenyekevu mkubwa (khushu) na mwingine yupo kinyume na hali hii. Ni ipi sababu ya tofauti hii?'

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*'Muumini ambaye ameonja raha ya imani atakuwa na unyenyekevu mkubwa. Mwingine hatakuwa nao'.*

'Kama ni hivyo basi ni vipi mtu atapata raha ya imani? Ni vipi mtu atafikia hali hiyo?' wakauliza.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

'*Inaweza kufikiwa kwa kubakia kwenye mapenzi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu*'

Wakati huu maswahaba wakauliza:

'Vizuri, mapenzi ya Mwenyezi Mungu yanapatikana vipi?'

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

'Yanapatikana kwa kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Ndio maana hamna budi kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake kwa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake' (Senderusi, Kashf-i Ilahi, II, 651; Halabi, Mawsuatu al-Ahadith, VI, 492/16010).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliishi katika uhai wake wote akimpenda na kujitolea kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Alisubiri wakati wa kuungana na Mola wake kwa furaha

ambayo mtu angelikuwa nayo katika usiku wake wa harusi. Mke wake, Aisha ﵂[2] anasimulia:

'Wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yupo katika nyakati zake za mwisho, akiwa amelaza kichwa chake kilichobarikiwa juu ya kifua changu. Nilikuwa nikiomba "Ewe Mola wa wanadamu! Ondosha maradhi. Wewe ndiwe daktari wa kweli na mponyaji pekee". Kwa upande mwingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akisema:

*"Hapana! Ewe Mwenyezi Mungu! Niunganishe na mbora wa marafiki (Rafîk-ı A'lâ). Ewe Mwenyezi Mungu! Nisamehe! Nishushie rehema zako! Niunganishe na mbora wa marafiki". (Ahmad, VI, 108, 231)*

Katika masimulizi mengine Aisha anaendelea kusimulia:

'Katika siku alizokuwa na afya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mara kwa mara akisema:

*"Hakuna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyeondoka hapa duniani bila ya kuonyeshwa mafikio yake akhera. Kisha anaacha achague ama abakie hapa duniani au aende kule alikopangiwa".*

Alipoumwa na kukaribia mauti aliweka kichwa chake juu ya paja langu kisha akazimia. Alipozinduka akageuza macho yake kuelekea kwenye dari na kusema:

*"Ewe Mwenyezi Mungu! Mbora wa marafiki!"*

Kisha nikasema:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hatuhitaji sisi!" Nikagundua kuwa hii hamu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni dalili kuwa

2. ﵁ ni kifupi cha *radiyallahu anhu* (kwa wanaume) *anha* (kwa wanawake). Linamaanisha 'Mwenyezi Mungu awe radhi naye' na linatumika kama ishara ya heshima kwa maswahaba wa Mtume Muhammad ﷺ. (Maelezo ya mfasiri).

kile alichokuwa akituambia akiwa hai kinakuwa kweli' (Bukhari, Maghazi, 84; Ahmad, VI, 89).

❁

Mjadala ufuatao ambao ulifanyika kati ya malaika wa mauti na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakati wa kifo chake unaonyesha kwa uwazi zaidi namna alivyompenda Mwenyezi Mungu.

Ulipofika wakati wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuiga dunia Malaika wa mauti aliomba ruhusa ya kuingia. Pia Jibril alikuwepo pale, akamuambia Mtume:

'Ewe Ahmad! Huyu ni malaika wa mauti. Yupo hapa na anaomba ruhusa ya kuingia. Kamwe hajaomba ruhusa ya mtu yeyote kabla yako. Na kamwe hataomba ruhusa ya mtu yeyote tena. Mruhusu aingie!'

Malaika wa mauti akaingia na kusimama pembeni ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ewe Ahmad! Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amenituma nije kwako na ameniamuru nitii kila amri yako. Kama utaniamuru niitoe roho yako nitaitoa, lakini kama utaniamrisha kinyume chake nitakuachia roho yako".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akauliza:

*"Utafanya hivyo kweli?"*

Malaika wa mauti akajibu:

"Nimeamrishwa nitii kila neno lako".

Wakati ule Jibril عليه السلام akasema:

"Ewe Ahmad! Mwenyezi Mungu Mtukufu anakuruhusu"

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

“Yaliyo kwa Mwenyezi Mungu ni bora na yenye kudumu. Ewe malaika wa mauti! Njoo ufanye kile ulichoamrishwa kukifanya! Chukua roho yangu.” (Ibn Sa’d, II, 259; Haythami, IX, 34-35; Balazuri, Ansabu al ashraf, Egypt 1959, I, 565)

Mifano mingi kutoka kwa Mitume wengine inaweza kutolewa ili kuonyesha mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Tunataja baadhi yake kama ifuatavyo:

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alimjaalia nabii Ibrahim idadi kubwa ya kondoo. Siku moja Jibril عليه السلام alimtokea akiwa katika umbile la mtu na kumuuliza:

‘Kondoo hawa ni wa nani? Unaweza kuniuzia mmoja wapo?’

Ibrahim عليه السلام akajibu:

‘Kondoo hawa ni wa Mola wangu. Kwa sasa nimemilikishwa mimi. Ukimtaja Mwenyezi Mungu mara moja, utachukua watatu, kama utamtaja Mwenyezi Mungu mara tatu utawachukua wote!”

Jibril akamtaja Mwenyezi Mungu mara tatu kama ifuatavyo:

“*Subbuhun Quddusun Rabbunaa wa Rabbu’l malaaikati wa al ruhi*”

‘Mola wetu, na Mola wa roho na Malaika Mtukufu ameepukana na kasoro zote na ni msafi na yuko juu ya udhaifu wa namna zote”.

Nabii Ibrahimu عليه السلام akasema:

‘Wachukue wote, sasa ni wako’. Kisha Jibril akasema:

“Mimi si mwanadamu. Mimi ni Malaika. Siwezi kuwachukua’.

Nabii Ibrahimu عليه السلام akajibu:

‘Wewe ni malaika na mimi ni rafiki wa Mwenyezi Mungu. Hakunisaidii mimi kuchukua kile nilichokwisha kukitoa’

Upesi Nabii Ibrahimu ﷺ akawauza kondoo wote. Akanunua mali na kuzifanya wakfu kwa ajili ya masikini na wenye kuhitaji.

Nabii Ibrahimu ﷺ alijaribiwa katika maisha yake yote, mtoto wake na mali zake. Katika nyakati zote hizi alionyesha unyenyekevu na mapenzi ya hali ya juu. Alifikia kilele cha utumishi kama *Khalilullah* (Rafiki wa Mwenyezi Mungu).

❁

Kisa cha swahaba ambaye mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu yalijidhihirisha yenyewe katika kusikiliza maneno ya Mwenyezi Mungu ni hiki kifuatacho:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimchagua swahaba huyu kuongoza kikosi cha msafara. Swahaba yule aliyebarikiwa aliwaongoza marafiki zake katika swala lakini kila mara alimalizia kisomo chake kwa kusoma Surat Ikhlas. Waliporejea Madina walimuambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu juu ya suala hili. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

'*Muulizeni kwanini alifanya hivi*'. Marafiki zake walipomuuliza sababu ya kufanya hivi, yule swahaba akasema:

'Sura hii inahusu sifa za Mwingi wa Rehema, ndio maana napenda kuisoma'.

Baada ya kujua hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*'Muambieni Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anampenda pia'* (Bukhari, Tawheed, I).

❁

Wakati Ammar ibn Yasir ؓ anatembea pembezoni mwa mto wa Furati ili kwenda kujiunga na msafara alionyesha mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Lau ingelikuwa kujirusha katika mlima ule kungelikuwa ni njia ya kupata radhi zako nisingelisita kufanya hivyo. Lau ingelikuwa kujirusha ndani ya moto mkubwa kungelikuwa ni njia ya kupata radhi zako ningelifanya hivyo upesi. Ewe Mola wangu! Lau ingelikuwa kujirusha ndani ya bahari na kufa kungelinisogeza karibu zaidi kwenye radhi zako, ningelifanya hivyo mara moja. Ewe Mwenyezi Mungu! Hapa ninapambana ili kupata radhi zako tu. Ninakuomba unijaalie nisipatwe na madhara. Wewe pekee ndiye ninayekuomba" (Ibn Sa'd, III, 258).

❁

Abdullah ibn Omar ﷺ alikuwa mmoja wa matajiri na mwenye miongoni mwa maswahaba wakubwa. Kamwe hakuruhusu mali zake zijikusanye na hivyo alisambaza kila alichopata kuwapa masikini. Alikuwa akitoa mali zake zitumike katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alikuwa ameanza kuwafanya wawe huru watumwa wote waliokuwa kwenye hali nzuri hasa wale aliogundua kuwa wameanza kuswali. Mmoja wa marafiki zake alimtahadharisha kuwa baadhi ya watumwa aliowaacha huru wanakuja msikitini si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali kwa ajili ya kuachwa huru. Abdullah akatoa jibu lifuatalo lililo zuri, ambalo lilionyesha mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliyokuwa nayo moyoni mwake:

'Tunaweza kudanganywa na wale wanaoamua kutudanganya kwa kupitia kwa Mwenyezi Mungu' (Ibn Athir, Usdu'l Ghabah, III, 343).

❁

Fudayl ibn Iyadh alikuwa ni mtu mwenye elimu na mwema, ambaye alikuwa akitoa machozi mara kwa mara katika kumhofia Mwenyezi Mungu. Pia alikuwa ni msimulizi wa *hadith* mwenye kuaminika. Siku moja Fudayl alikutana na Shi'vane Hatun ambaye pia alikuwepo wakati ule. Shi'vane Hatun alikuwa ni mwanamke aliyekuwa katika ibada wakati wote na ambaye aliachana na raha

zote za dunia. Alikuwa akitoa machozi kutokana na mapenzi na hofu ya Mwenyezi Mungu. Fudayl alimuambia:

'Niombee'.

Shi'vane Hatun alitoa jibu lifuatalo:

'Ewe Fudayl! Je hakuna ukaribu kati yako na Mwenyezi Mungu ambao utafanya maombi yako yajibiwe kiasi kwamba unaniomba nikuombee?'

Baada ya kusikia maneno haya Fudayl akashindwa kujizuia na kuanza kulia kwa sauti. (Ibn Jawzi, Sifatu as Sahaba, IV, 56).

❁

Kabla ya kuhukumiwa, Hallaj-i Mansur aliomba dua iliyoonyesha kiwango chake cha usafi wa moyo na mapenzi aliyokuwa nayo kwa Mwenyezi Mungu:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Waja wako wamekusanyika pamoja ili kuniua kutokana na ukaribu wao kwako na kujitolea katika dini. Naomba uwasamehe. Kwani kama ungelikuwa umewajaalia mambo ambayo umenijaalia mimi, wangelikuwa na maamuzi tofauti na haya. Kama ungelikuwa umeficha kwangu mambo ambayo umeyaficha kwao, basi nisengeliwadhihirishia mambo hayo. Ewe Mola wangu! Wasamehe. Kwani wao ni sababu ya kunikutanisha na Wewe".

Imesimuliwa kutoka kwa wale walioshuhudia hali ya kiimani ya Hallaj kwamba wakati amening'inizwa juu ya kiunzi tayari kwa kunyongwa Shetani alimjia na kumuambia:

'Ulisema "Ana" ("Mimi") na mimi nilisema "Ana" ("Mimi")[3]. Itakuwaje neno hili ambalo wote tumelitamka kuwa sababu ya kupata rehema na wakati huo huo mimi kulaaniwa?

3. Maneno *Ana al Haqq* yanayomaanisha "Mimi ni kweli au Mimi ni haki"ni maneno yaliyosemwa na Hallaj. Kwa shetani pindi alipoulizwa na Allah kuwa

Hallaj alimjibu Shetani yafuatayo:

"Kwa kusema "Mimi" ulijiona ni bora kuliko Adam na kujivuna. Wakati mimi niliposema "*Ana al Haqq*", niliangukia kwa Mwenyezi Mungu. Majivuno ambayo yanakutukuza wewe mwenyewe ni ishara ya moto. Wakati kutojiona na kuangukia kwa Mwenyezi Mungu ni kiashirio cha udhalili wa mtu. Ndio maana kuna rehema kwangu na laana na kuharibikiwa juu yako".

Imesimuliwa kuwa Hallaj alimuambia yafuatayo Ibrahim ibn Fatik ambaye siku moja alimtembelea:

'Ewe mwanangu! Baadhi ya watu wanadhania kuwa nimekufuru na baadhi wanadhania kuwa mimi ni mtakatifu. Wale wanaonitangazia kuwa mimi ni mwenye kukufuru wananifurahisha zaidi na wanamfurahisha zaidi Mwenyezi Mungu kuliko wale wanaosema kuwa mimi ni mtakatifu".

Alipoulizwa ni kwanini alijibu:

'Wale wanaoamini kuwa mimi ni mtakatifu wanafanya hivyo kutokana na mawazo yao mazuri juu yangu wakati wale wenye hoja kuwa mimi ni kafiri, wanaamini hivyo kutokana na bidii yao katika dini. Yule anayeonyesha bidii katika dini anapendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu kuliko yule anayetoa mawazo mazuri tu'

❀

Jalalluddin Rumi alionyesha kwa uzuri kuwa kuunguzwa kwake na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, kuharibikiwa kwake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (*fana fillah*), maisha yake ya akhera pamoja na Mwenyezi Mungu (*baka billah*) na moto uliounguza ndani ya moyo wake, usingiliweza kuzimwa hata na kifo.

---

"Mimi ni nani na wewe ni nani?" alijibu kwa ujeuri: *"Ana ana wa anta anta"* (Mimi ni mimi na Wewe ni Wewe) (Maelezo ya mfasiri).

"Baada ya kifo changu fungueni kaburi langu na angalieni moshi utokao kwenye sanda yangu kutokana na moto unaowaka ndani yangu! Kinachotufanya tuogope kifo ni huu mwili ambao ni kama kiota. Pindi utakapofungua mwili kwa 'mapenzi' kama ambavyo ungefanya kwa chaza, je utaweza kuona namna kifo kinavyofanana na lulu..."

Moja ya sifa muhimu ya marafiki wa Mwenyezi Mungu ni namna wanavyoungua kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Rumi alikuwa akiwatafuta wapenzi hao wa kweli ambao walifariki katika hali ya kumpenda Mwenyezi Mungu kama alivyoonyesha katika maneno yaliyopita. Aliyaelezea haya kama ifuatavyo:

'Ninamtafuta mpenzi ambaye miale itokayo moyoni mwake itaweza kuwasha siku ya hukumu na joto litokalo moyoni mwake liweze kubadili moto kuwa majivu..."

❁

Siku moja Maruf-i Karhi aliulizwa na mmoja wa marafiki zake:

'Ewe Maruf! Ni kipi kinachokupelekea kufanya ibada sana?'

Maruf akawa kimya. Rafiki yake akaendelea:

'Je ni kwa sababu ya kukumbuka mauti?' akauliza.

Maruf-i Karhi akajibu:

'Ni kitu gani hiki mnachokiita kifo?'

'Je ni kufikiria kuhusu kaburi na maisha ya kaburi?'

'Ni kitu gani hiki mnachokiita kaburi?'

Rafiki yake bado akaendelea:

'Je ni hofu ya moto wa Jahannam au matumaini ya kupata pepo?' Kisha Maruf akatoa jibu lifuatalo lenye kuvutia:

'Vyote hivi ni vya nini? Mwenyezi Mungu aliyetukuka ambaye anashikilia vitu vyote hivi ni Mola Mtukufu ambaye kama utakuwa na mapenzi na shauku kubwa naye, utasahau vitu vyote hivi ulivyotoka kuvitaja' (Babanzade Ahmad Naim,"Islam Ahlakinin Esaslari, Istanbul," 1963 ukurasa 66).

❁

Hali ifuatayo ya Majnun ina mguso katika kuonyesha hali za wale ambao wamejikita katika kumpenda Mwenyezi Mungu:

Siku moja Majnun aliugua kutokana na kutengana na Leila. Wale waliokuwa karibu naye walimuita daktari ili atafute tiba yake. Daktari alipowasili akasema:

'Hakuna suluhisho lingine bali kumchanja atoke damu'. Aliufunga mkono wa Majnun ili auchanje. Alipoweka wembe kwenye mkono wake tu Majnun akasema kwa sauti:

"Daktari acha. Chukua malipo yako na uondoke. Kama nitakufa kutokana na maradhi haya basi niache nife. Hakuna hasara. Kuna tatizo gani kwa mwili huu uliochakaa kufa?"

Daktari akamuuliza Majnun kwa mshangao:

'Huogopi simba wanaonguruma jangwani lakini unahofia kutolewa damu yako?'

Jibu la Majnun likawa kama ifuatavyo:

'Sio wembe ninaouhofia...dunia nzima inajua kuwa uvumilivu na ujasiri wangu ni mkubwa kuliko mlima wa miamba. Mimi ni mtu nisiyeogopa chochote na ambaye sina hata robota la majani makavu katika dunia hii. Kama mwili wangu wenye kufa muda wowote haukupata maumivu basi hautapumzika. Kama majeraha ndio tiba ya mapenzi yangu; basi ningelikimbilia kujeruhiwa...

Hata hivyo mwili wangu umejawa na Laila; ndani yangu hakuna kingine kinyume na Laila. Huu mwili wangu ambao ni kama mama wa lulu umebeba sifa za lulu ndani yake. Na hivyo ndivyo ewe daktari. Nahofia wakati unanichanja wembe wako unaweza ukamkata Laila na ninahofia kwamba utamjeruhi yeye... Kwani waja maalum wa Mwenyezi Mungu wanajua kuwa hakuna tofauti kati ya Laila na mimi".

Baada ya miaka kadhaa Laila akajitokeza kwa Majnun lakini Majnun alimpuuzia. Laila akamuambia:

"Je si kwa sababu yangu ulipotea jangwani?"

Majnun akajibu:

"Kivuli kilichokuwa kikimuita Laila kiliyeyuka na kutoweka".

Laila, ambaye wakati fulani alikuwa ndiye malengo ya maisha yote ya Majnun amewakilisha tu hatua katika safari ya kuelekea kwenye mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Pindi Majnun alipopata sehemu yake katika mapenzi ya Mwenyezi Mungu, ukweli ambao alikuwa akiutafuta, nafasi ya Laila ikifikia mwisho.

Laila, ambaye ametajwa katika masimulizi ya Mathnawi, ni ishara ya upendo mtakatifu ambao unabadilishwa na kuwa mapenzi matakatifu na mtu ambaye amezama kwa Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine Laila ni tufe la mapenzi matakatifu ambayo yanafanya nyoyo kuchanganyikiwa na kuharibu utashi wa mwili. Ndio maana kama matukio ya kimapenzi yanayoanza na Laila na kuishia kwenye amani ya Mwenyezi Mungu, basi yatakuwa ni ya thamani.

❁

Majnun alienda jangwani kwa ajili ya Laila na kutokana na upendo wake kwake. Wakati fulani alimtomasa na kubusu macho ya mbwa ambaye manyoya yake yalikuwa yamepukutika

na ambaye mdomo wake ulikuwa ukitiririsha mate. Mtu mmoja aliyeyaona haya hakuweza kuvumilia na hivyo akamuambia:

'Ewe Majnun mchafu! Ni uwendawazimu gani huu? Kwa nini unamkumbatia na kumbusu mnyama huyu?'

Majnun akajibu:

"Wewe si chochote bali muonekano. Wewe ni umbile na mwili kutoka kichwani mpaka chini, je utawezaje kuelewa ninachokifanya? Ingia ndani na uangalie, yani zama kwenye roho yangu na kisha uiangalie kwa kupitia macho yangu. Je unajua huyu mbwa ana wema gani? Kuna siri takatifu iliyo ndani ya mbwa huyu ambayo hujaifahamu. Mwenyezi Munguameficha ndani ya moyo wake hazina ya upendo na utii kwa mmiliki wake. Angali pia, kati ya vijiji vyote, ameenda na kukifanya kijiji cha Laila kuwa ndio nyumbani kwake na amekuwa mlinzi wa kijiji kile...!

Usimdharau huyu mbwa, angalia moyo wake. Yeye moyoni mwangu ni Qitmir aliyebarikiwa. Yeye ni mwenza wa furaha yangu na huzunu yangu. Nisingelibadilisha hata mwele yake moja kwa simba wengi. Zingatia moyo wake, roho yake na undani wake ili uone wema wake. Kwangu mimi hata sakafu ambayo mguu wake umekanyaga inanipendeza kwa sababu amechagua kijiji cha Laila kuwa nyumbani kwake..."

Moyo unaoungua kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu utawapenda viumbe wake wote kutokana na mapenzi haya. Vitu vyote vinavyomkumbusha yeye juu ya Mwenyezi Mungu vinawakilisha kitu cha thamani kubwa kutokana na kiwango cha ukaribu wake kwake.

❁

Mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu anasimulia tukio lifuatalo ambalo linaonyesha matunda ya upendo kwa Mwenyezi Mungu:

"Nilikuwa ninapita katikati ya ardhi pana na yenye kusikitisha ndipo nikamkuta mchungaji. Alikuwa akiswali kwa unyenyekevu mkubwa wakati mbwa mwitu wanamlindia kondoo wake. Nilishangazwa. Nikamsubiria amalize swala yake kisha nikamuuliza:

"Ewe mchungaji! Inawezekanaje mbwa mwitu wamekuwa marafiki wa kondoo? Imekuwaje roho ya unyama na ukatili iliyopo ndani yao iondoke na kukaliwa na amani na upendo?"

Yule mchungaji mwema ambaye uso wake ulikuwa uking'aa kutokana na kumsujudia Mwenyezi Mungu, alitoa jibu lifuatalo:

"Ewe msafiri mgeni! Maajabu ya urafiki kati ya hawa mbwa mwitu na kondoo unatokana na mmiliki wa kweli wa wachungaji, wanyama wao na mbwa mwitu. Hii ni hali ya maajabu ya mapenzi".

❁

Mtu anateketeza vitu vyake vyote kwa ajili ya ampendae. Tukio lifuatalo lililosimuliwa na Molla Jami (matendo yake yakubaliwe) ni mfano wa hili:

Wakati fulani kulikuwa na kijana mmoja katika kikao cha majadiliano cha bwana wetu, Mawlana Sadeddin Kashgar. Kijana huyu alikuwa mbele katika adabu, upweke na upendo kwa Mwenyezi Mungu. Hata hivyo alikuwa ametekwa na mapenzi ya kiwiliwili kama mimi. Hivyo aliigawa hazaina ya mapenzi yaliyokusanyika ndani ya kifua chake na kumhamishia mwanamke.

Alinunua zawadi iliyokuwa na thamani kubwa iliyotengenezwa kwa dhahabu na almasi, kisha akaiweka katika njia ambayo alijua kuwa mrembo yule angepita, kisha alijificha pale karibu ili mtu mwingine asije akaichukua. Mpango wake ni kwamba mpenzi wake angelipita pale na kuiona ile zawadi na kuichukua. Lakini asingelijua imetoka wapi na kwa namna gani. Nilipolifahamu hili nikamuambia:

"Ajabu iliyoje ya jambo unalolifanya. Unakiacha katika njia yake kitu hiki ulichokipata kwa tabu nyingi. Lakini hata kama atakiona na kukichukua, hatafahamu kimetoka kwa nani na kwanini amepewa. Fanya kitu angalau ajue kwamba kimetoka kwako".

Yule kijana huku akitokwa na machozi akajibu:

"Unasemaje? Hujui kwamba ninajua ajabu ya kitu ninachokifanya? Sitarajii malipo ya kitu ninachokifanya. Sitaki ahisi wajibu wowote kwangu kwa sababu ya zawadi hii".

Nikashtushwa kutokana na jibu lake. Kama mapenzi haya yaliyoelekezwa kwa mwanadamu yanaweza kuonyesha ulaini na uzuri, sasa ni vipi itakuwa kwa wale walio na 'mapenzi ya Mtukufu wao'.

❁

Kwa kifupi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

'Mwenyezi Mungu ni mzuri na anapenda vizuri' (Muslim, Iman, 147).

Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye mmiliki wa uzuri wote uliotuzunguka, pia ndiye chanzo cha mapenzi ya kweli. Kwa sababu Yeye ni *Al-Waduud*[4]. Jina hili tukufu la Mwenyezi Mungu linamaanisha 'ambaye anapenda mno'[5] na pia 'ambaye anapendwa mno'. Ndio maana jukumu la muumini ni kuwa mlango wa rehema ambayo inaingiza mapenzi matakatifu moyoni. Kwani kama muumini hataweka mapenzi anayohisi kwa Mola wake (*mahabbatullah*) juu ya vitu vingine kinyume na Mwenyezi Mungu, basi hawezi kuambiwa ameifuata '*Sirat al-Mustaqim*' (njia iliyoon-

4. Angalia Al Buruj, (aya 14).
5. Fakhruddin Ar-Razi, Mafatihu'l ghayb (at Tafsir al-Kabir), Beirut, 1990, XXXI, 112).

yooka) kikamilifu’. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika aya ndani ya Qur’an:

**“Na katika watu wapo wanao chukua waungu wasio kuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana. Na laiti walio dhulumu wakajua watakapoiona adhabu kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu!”**(Al-Baqara, 2:165).

Hali hii ambayo ni muhimu mno kwa muumini imeelezewa katika aya nyingine kama ifuatavyo:

“**Sema: Ikiwa baba zenu, na wenenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyo yachuma, na biashara mnazo ogopa kuharibika, na majumba mnayo yapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Jihadi katika Njia yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu alete amri yake. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wapotovu**” (Al-Tawba, 9:24).

Ili kufikia hatua hii ya *mahabbatullah* (kumpenda Mwenyezi Mungu) ni lazima umtambue Mwenyezi Mungu katika moyo wako, yani kuwa sababu ya udhihirisho wa *Asma al-Husna* au Majina yake Mazuri.

Kumkumbuka Mwenyezi Mungu (*dhikrullah*) ni njia ya kukupandisha kuelekea kwenye *mahabbatullah*. Hata hivyo kupanda huku kutategemeana kiwango cha ubora wa *dhikr* inayofanywa, yani ni kwa namna gani inagusa moyo.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

“Dalili kwamba mtu anampenda Mwenyezi Mungu ni pale mtu anapopenda kumkumbuka Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi” (*dhikrullah*) (Suyuti, II, 52).

Ili kuendelea katika uelekeo wa *mahabbatullah*, mtu anahitajika kuwa na moyo unaojitosheleza na wenye kuweza kuyathaminisha. Jambo hili linaweza kupatikana kwa kujifunzia kwenye mapenzi ya wanadamu. Ndio maana mapenzi ya miongoni mwa wanadamu yanathaminiwa kwani ni kama maandalizi ya moyo ikiwa yatafanywa ndani ya mipaka ya sheria, ndio maana yanaitwa 'mfano wa mapenzi'. Kama mtu anavyoipenda familia yake...

Kuendelea na hali hii na kufikia kwenye hali ya inamaanisha kutimia kwa lengo la kuumbwa mwanadamu na kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Kwani lengo kuu la maamrisho mbali mbali aliyoletewa mtu kwa kupitia Uislamu ni kuwa '*wasil ilallah*', yani namna ya kufika kwa Mwenyezi Mungu. Na jambo muhimu mno la kufanikisha hili ni upendo. Matendo mengine ni matokeo ya huu upendo.

Muumini ambaye atakuwa na ataepushwa mbali na uovu unaotokana na nafsi yake mwenyewe na vitimbi vya Shetani, na ataishi kwa kupenda kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu pekee. Kurasa za kitabu cha ulimwengu kitafunguliwa kwake na viumbe vyote vitafanya urafiki na yeye. Yani atakuwa na uwezo wa kumuangalia kiumbe kwa kupitia 'macho' muumba. Na atatazama kwa macho ya utambuzi, hekima na kuzijua siri za ulimwengu. Baada ya kutekeleza majukumu yake ya wajibu kwa unyenyekevu mkubwa, ambayo ni kiwango cha chini cha majukumu yanayohitajiwa na Mwenyezi Mungu, kisha atajaribu kuongezea kwa ibada za sunnah kutokana na mapenzi na shauku kubwa itokayo moyoni mwake, licha ya kuwa si lazima kwake. Atafanya haya kwa namna bora, unyenyekevu na ari. Kwa kuziweka mbali starehe za dunia ataijua siri ya utamu wa imani.

**b. Kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu**

*Rehema na amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu ziwe juu ya bwana wa hapa duniani na kesho akhera, Muhammad Mustafa!*

*Rehema na amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Mjumbe wa wote wanadamu na majini, Muhammad Mustafa!...*

*Rehema na amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu ziwe juu ya kiongozi wa miji miwili mitakatifu, Muhammad Mustafa!*

*Rehema na amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu ziwe juu ya babu wa Hasan na Hussain, Muhammad Mustafa!*

Hatua za upendo wa wanadamu zinaweza kufikia kilele kwa kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Hakuna mtu katika wanadamu ambaye anastahiki mapenzi zaidi yake. Haya ni kwa sababu:

– Kuwepo kwa viumbe vyote kunatokana na mapenzi ya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi juu ya Mtume.

– Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ndio sababu ya watu na majini kuujua ukweli wa Mwenyezi Mungu na hivyo kuwa sababu ya wao kuokolewa na adhabu ya kesho akhera.

– Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amewaletea waja wake neema ya Quran na Uislamu kwa kupitia moyo safi wa Mtume.

– Alipata maumivu makali mno kwa ajili ya umma wake na alipitia majaribu na mateso ambayo hakuna mwanadamu mwingine aliyewahi kupitia.

– Amejawa na mapenzi makubwa na huruma kwa waumini. Yeye ni bahari ya wema. Anajali zaidi umma wake na anajisikia uchungu mno pale umma wake unapopata mateso ya aina yoyote.

– Yeye ni mbora na mfano mzuri wa utumishi.

– Yeye ndio njia muhimu mno ya kuwawezesha waja kumfahamu Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi.

– Miongoni mwa Mitume yote, ni yeye pekee ambaye Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ameapia kwa maisha yake, ("'La'amruka' – Ninaapa kwa maisha yako"), ili kuufanya umma wa waislamu uzingatie mfano mzuri wa maisha ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

– Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amejaalia utii kwa kipenzi chake kitukufu kuwa sharti la kupata mapenzi yake na msamaha. Anasema katika aya ndani ya Qur'an:

"**Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu**" (Al'i Imran, 3:31).

– Kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ndio sababu ya kuokolewa kutokana na adhabu ya kesho akhera: **Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha** (Al-Anfal, 8:33).

– Cha muhimu kuliko yote ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anampenda na amefadhilishwa kwa kuitwa na Mwenyezi Mungu 'Kipenzi Changu' (*Habîbullah*). Heshima iliyoje, hivyo tumpende kipenzi cha Mwenyezi Mungu.

Hivyo hatuna budi kulikita jina tukufu la kiongozi huyu Mtukufu ndani ya nyoyo zetu. Hatuna budi kulifanya hili kwa maneno ya upendo ambayo hayawezi kufutwa. Hatuna budi kumtumia salamu ili nyoyo zetu ziweze kuhisi thamani aliyopewa.

Hata hivyo hatuna budi kuweka akilini kuwa lengo kuu si kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa pekee.

Bali anayestahiki kuelekezewa mapenzi ya thati ni Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi, Muumba wa ulimwengu mzima. Hivyo kumpenda kipenzi chake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndio njia ya pekee ya kutupeleka kwenye kumfahamu na kumpenda Mwenyezi Mungu.

***Matukio ya wema***

Maswahaba watukufu walimsikiliza na kumtii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kutokana na mapenzi yao kwake. Walikuwa wakitii katika kila neno lake, amri yake na hata ishara ndogo vipi kutoka kwake, kwa kutumia maneno yafuatayo:

'Mama yangu, baba yangu, mali zangu na uhai wangu ni kwa ajili yako Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!'...

Waliridhika sana wale walioweza kugusa ngozi yake:

'Angalia! Nimeitumia hii mikono yangu miwili kufanya makubaliano na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu' (Ibn Sa'd, IV, 306; Haythami, VIII, 42).

Mfano ni Abu Asma As-Shami رضي الله عنه:

Alikuja kwa Mjumbe aliyebarikiwa kama muwakilishi. Akawa amejifunza misingi ya Uislamu ili akawafundishe watu katika kabila lake alilokuja kuliwakilisha. Akaushika mkono wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu uliobarikiwa na kuutingisha katika kufanya makubaliano. Lazima atakuwa ameguswa baada ya kuugusa mkono wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kutamani kuhisi baraka za joto la mkono ule milele. Abu Asma akaahidi kutoshikana mikono na mtu mwingine tena. Na hivyo hakugusa mkono wa mtu mwingine mpaka alipokufa. (Ibn Hajar, Al-Isabah, IV, 7).

❁

Kiwango cha mapenzi walichokuwanacho maswahaba kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni kikubwa mno kiasi kwamba maswahaba wakike walikuwa wakiwakaripia watoto wao kwa kutokaa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa muda mrefu. Pindi Hudhayfa ﵁ alipokosa kumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa masiku kadhaa mama yake alimkasirikia na kumkemea. Hudhayfa anasimulia tukio hili kama ifuatavyo:

Siku moja mama yangu aliniuliza:

“Ni lini mwisho wako kumuona Mtume?”

‘Sijamuona kwa masiku kadhaa’. Alikasirika sana na kunikaripia kwa hasira.

Nikasema:

‘Mpendwa mama! Acha! Usikasirike! Ngoja niende kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu sasa hivi. Nitaswali naye swala ya isha na nitamuomba atuombee msamaha mimi na wewe’... (Tirmidhi, Manaqib, 378; Ahmad, V, 391-2).

❁

Jabala, ambaye ni kaka wa Zayd ibn Harith ﵁, anaelezea mapenzi waliyokuwanayo maswahaba juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kama ifuatavyo:

‘Siku moja nilienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa na kusema:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Mrudishe kaka yangu Zayd kwangu”.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu:

“Huyu hapa. Kama anataka kurudi kwako sitamzuia”. Hata hivyo Zayd alikataa ombi langu na badala yake akasema:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Siwezi kumchagua mtu yeyote zaidi yako”.

Baadae nikajifunza kuwa huu msimamo wa Zayd ni sahihi zaidi yangu. (Tirmidhi, Manaqib, 39/3815).

Baada ya kiapo cha pili cha Aqaba, Mus’ab ﷺ, ambaye alikuwa mkuu wa kabila, alienda kwanza kwenye nyumba ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kabla ya nyumba yake. Alipeleka habari kuwa watu wa madina wanaingia katika Uislamu kwa kiasi kubwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifurahia sana habari hizi.

Mama yake Mus’ab ambaye ni pagani alipogundua kuwa mwanae ameenda kwanza kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akakasirika sana. Kwa upande mwingine Mus’ab akasema:

‘Nisingeliweza kwenda kwa yeyote yule mwingine kabla ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Nisingeliweza kumuwekea mtu mwingine kipaumbele wakati yeye yupo hai’.

Baada ya kuomba ruhusa kwa Mtume, alienda kwa mama yake na kumkaribisha katika Uislamu (Ibn Sa’d, III, 119).

❁

Wakati Abu Bakr ﷺ na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wanaelekea kwenye pango la Thawr wakati wakuhamia Madina, Wakati mwingine Abu Bakr alikuwa akitembea mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na wakati mwingine nyuma yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamuuliza:

*“Ewe Abu Bakr! Kwa nini unafanya hivi?”*

Abu Bakr akajibu:

‘Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nikadhania kuwa maadui zako wanaweza kukukamata kutokea nyuma yako basi natembea

nyuma yako, kisha nikadhania kwamba wanaweza kukuvamia kutokea mbele, basi naanza kutembea mbele yako'.

Mara wakafika katika pango la Thawr. Abu Bakr akasema:

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Subiri hapa nisafishe pango'. Akaingia ndani ya pango na kulisafisha. Alipohisi tundu kwa kutumia mikono yake alichana kipanda cha joho lake na kuzibia tundu lile. Kwa namna hii aliitumia sehemu yote ya juu ya joho lake kuzibia matundu, hata hivyo likawa limebaki tundu moja. Akaliziba kwa kisigino chake na kumuita Mtume:

'Sasa unaweza kuingia ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu'.

Ilipofika asubuhi na kumuona Abu Bakr hana kitu juu ya mwili wake akamuuliza kwa mshangao:

*"Nguo zako zikowapi ewe Abu Bakr?"*

Abu Bakr akamueleza alichokifanya usiku wake. Kutokana na kuguswa mno na jambo hili la kiimani, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akanyanyua mikono na kuanza kumuombea Abu Bakr.[6]

Wapagani wa kiqureishi walipofika nje ya pango lile, Abu Bakr al Siddiq akaanza kupata wasiwasi na kumuambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

'Kama nikiuawa, hakuna tatizo kwani mimi si chochote bali mtu mmoja. Lakini chochote kikikupata wewe basi huu umma wote utakuwa umevurugwa'.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawa amesimama kuomba wakati Abu Bakr analinda. Abu Bakr akasema:

'Watu wa makka wanakutafuta. Kwa jina la Mwenyezi Mungu siihofii nafsi yangu. Bali nahofia watakudhuru wewe'.

6. Angalia Hakim, III, 7/4268; Ibn Kathir, Al Bidaya, III, 222-3; Ali al-Kari, Mirkat, Beirut, 1992, X, 381-2/6034; Abu Nuaym, Hilya, I, 33).

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa ﷺ akamuambia rafiki yake aliye ndani ya pango:

"Ewe Abu Bakr! Usijali. Kwa hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja nasi" (Ibn Kathir, al-Bidaya, III, 223-4; Diyarbekri, Tarikhu' al-khamis, Beirut ts, I, 328-0).

❀

Wakati fulani wakati wapo ndani ya pango la Thawr, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilaza kichwa chake juu ya miguu ya Abu Bakr na kupitiwa na usingizi mwepesi. Wakati ule Abu Bakr alikuwa ameliziba tundu lililobaki wazi kwa mguu wake.

Baada ya Muda mfupi, kutokana na mtihani wa Mwenyezi Mungu huku Abu Bakr akiwa na hofu pale alipo nyoka alimtokea na kumgonga na kumtemea sumu. Licha ya maumivu makali aliyoyahisi hakutikisika akihofia asije akamuamsha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hata hivyo hakuweza kuzuia matone machache ya machozi kutoka kwenye macho yake. Moja ya matone haya ya lulu likadondokea uso wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Akaamka na kumuuliza:

*"Una nini ewe Abu Bakr? Nini kimetokea?"*

Abu Bakr alijaribu kumtoa wasiwasi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa kujibu:

'Hakuna tatizo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', baada ya kusihiwa na Mtume, akalazimika kusema.

'Mama yangu na baba yangu watolewa kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nyoka amegonga mguu wangu'.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatema mate kidogo kwenye mguu wa Abu Bakr. Mara ikawa kana kwamba hakuna kilichomtokea, maumivu na mahangaiko ya Abu Bakr yakaisha.

Miaka kadhaa baadae, baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kufa, sumu hii ilianza kusambaa na kuwa sababu ya kifo cha Abu Bakr (*Bayhaki, Dalail an-Nubuwwa wa Ma'rifai Ahwali Sahibi as-Shariyya*, ta'lik: Abdulmu'ti Kal'aci, Beirut, 1985, II, 477; Ibn Kathir, al-Bidaya, III, 223).

❀

Omar ؓ alipowasikia watu wakisema yeye ni khalifa bora kuliko Abu Bakr alisema:

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, usiku ule mmoja wa Abu Bakr ni bora kuliko uongozi wote wa Omar! Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipoiacha nyumba yake na kwenda pangoni alikuwa pamoja na Abu Bakr tu... (Hakim, III, 7/4268).

❀

Bara ؓ anasimulia namna baba yake alivyokuwa anapenda kusikia kumbukumbu yoyote ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

Abu Bakr al-Siddiq ؓ alinunua tandiko la farasi kutoka kwa baba yangu kwa dirham tatu na kumuambia:

'Muambie Bara alipeleke nyumbani kwetu'. Baba yangu akasema:

'Hapana! Hapana mpaka unihadithie namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyotoka Makka na kuhamia Madina'.

Kisha Abu Bakr akamsimulia safari ya kuhama kwao kwa urefu. (Bukhari, As-habu an-Nabi, 2; Ahmad, 1, 2).

❀

Baada ya jeshi la waislamu kusimama katika makao yao makuu katika Badr, Sa'd ibn Muadh alitoa hotuba ifuatayo ambayo inaonyesha mapenzi yake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na namna alivyokuwa akinyenyekea katika kila amri yake:

'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ngoja tukutengenezee mahali pakupumzikia. Na wanyama wako wawe karibu yako. Kisha tukapigane na maadui. Uzuri ulioje Ikiwa Mwenyezi Mungu atatupa nguvu na ushindi! Kama itakuwa kinyume chake basi wewe utampanda farasi wako na kurudi kwa ndugu zetu tuliowaacha nyuma. Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Wanakupenda kama tunavyokupenda sisi. Kama wangelikuwa wanajua kuwa unakuja kupigana hakuna ambaye angebaki nyuma. Mwenyezi Mungu atawalinda kwa sababu yako. Wao ni watii kwako na watapigana katika njia yako'

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamsifu Sa'd kumuombea wema. Sa'd ؓ akachomoa upanga wake na kumlinda katika mlango wa ile sehemu ya kupumzikia aliyotengenezewa.

❁

Abdurrahman Ibn Awf ؓ anasimulia tukio lifuatalo lenye mazingatio ambalo linaonyesha namna maswahaba wote waliobarikiwa, wazee kwa vijana walivyokuwa wanampenda Mtume:

'Katika siku ya Badr niliangalia kuliani kwangu na kushotoni kwangu. Nilijikuta niko nyuma ya vijana wawili wa kianswar. Sikufurahiswa sana na hili. Nilitaka kuwa pamoja na watu wenye nguvu zaidi. Mmoja wao bila ya kutaka rafiki yake asikie, akaniambia:

"Ewe mjomba! Je ukimuona Abu Jahl unaweza kumtambua?" Nikajibu:

"Ndio naweza. Utamfanyia nini?" Kijana akajibu:

"Kutokana na kusikia kwangu kuwa anaapa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ambaye Mikononi Mwake anashikilia nguvu ya kuwepo kwangu kwamba kuwa nikimuona sitaachana naye mpaka mmoja wetu afe".

Nilipigwa na butwaa kutokana na maneno ya kijana huyu. Yule kijana mwingine akasema maneno yale yale. Baada ya pale nikahisi furaha kuwa pamoja nao. Baada ya muda mfupi nikamuona Abu Jahl akitembea ndani ya uwanjwa wa mapambano, nikawaambia:

“Yule ndiye mtu mliyekuwa mkimuulizia”.

Upesi wale vijana wakachomoa mapanga yao na kumkimbilia Abu Jahl, huku wakimuelekezea panga zao. Vijana hawa wawili walikuwa ni Muadh ibn Afra na Muadh ibn Amr (Bukhari, Maghazi, 10; Muslim, Jihad, 42).

❁

Wakati fulani wakati Mtume Muhammad ﷺ amejeruhiwa katika vita vya uhud alisema:

“Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi analighadhibikia kabila lililojeruhi uso wa Mjumbe wake”.

Sa’d ibn Abi Waqqas akasema:

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu niliposikia jambo hili nikapandwa na shauku ya kumuua mtu aliyemjeruhi, shauku ambayo sijawahi kamwe kuipata katika jambo lingine.

Ikawa aliyemjeruhi ni kaka yangu, Utba ibn Abi Waqqas“.

Siku ili Sa’d رضي الله عنه ambaye moyo wake ulikuwa umejawa na mapenzi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, alipangua safu za wapagani na kujaribu kumuua kaka yake. Hata hivyo kila mara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimzuia kufanya vile.

❁

Talha ibn Ubeydullah anasimulia:

Maswahaba walipotawanyika katika Uhud, wapagani walikuja na kumzunguka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu pande zote

ili wamshambulie. Sikujua nimtetee vipi na kutokea upande upi-kutokea mbele, kutokea nyuma, kutokea kuliani mwake au kushotoni mwake. Nilichomoa upanga wangu na kuanza kuwafukuza maadui nikianzia mbele na kuja nyuma mpaka wakasambaratika. (Waqidi, I, 254).

❁

Wakati mwingine wakati wa vita vya uhud, mmoja wa wapiga mishale mahiri miongoni mwa wapagani, Malik ibn Zuhayr, aliulekeza mshale wake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Talha ibn Ubeydullah alipogundua kuwa mshale umeelekezwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaukinga kwa mkono wake na kujeruhiwa kidole. (Ibn Sa'd, III, 217).

Wakati fulani baadhi ya maswahaba kutoka Muhajirina na answar walimzunguka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ambaye walimpenda zaidi kuliko uhai wao; wakaweka kiapo kwa Mwenyezi Mungu kuwa watakufa mashahidi kwa ajili yake:

"Uso wangu uwe ngao ya uso wako, na mwili wangu uzuie mwili wako. Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yako wakati wote. Kamwe hatutakuacha ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!" na baada ya kusema yale walipigana mpaka mwisho (Ibn Sa'd, II, 46; Waqidi, I, 240).

❁

Abu Talha ؓ alikuwa ni mpiga mishale mahiri mno. Katika siku ya vita vya Uhud mishale yake miwili au mitatu ilivunjika. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamuambia kila aliyempitia na mfuko wa mishale:

*"Mpeni Abu Talha mishale yenu".*

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawa ananyanyua kichwa chake ili kuwaangalia wapagani walio nyuma yake. Abu Talha akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako. Usinyanyue kichwa chako. Mshale kutoka kwa wapagani unaweza kukuchoma. Acha kifiua changu kiwe ngao ya kifua chako. Acha chochote kitakacholengwa kwako kinikute mimi badala yako" (Bukhari, Maghazi, 18).

❁

Ili kumlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Qatada ibn Nuuman ؓ alikuwa akisimama mbele yake na kuwarushia wapagani mishale mpaka upinde wake upinde. Mara alichomwa na mshale jichoni. Mboni yake ikadondoka kwenye mashavu yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipomuona Qatada akiwa hivi macho yake yakajawa na machozi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akachukua mboni ya jicho la Qatada na kulirudishia mahali pake. Baada ya pale lile jicho likawa zuri zaidi na kuwa na uoni mkali zaidi ya lile lingine (Hakim, III, 334/5281; Haythami, VI, 113; Ibn Sa'd, III, 453).

❁

Ummu Umara ؓ alikuwa ni mmoja wa maswahaba wa kike aliyemlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika vita vya Uhud kwa kutumia upinde na mshale. Waliporejea Madina baada ya vita, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Wakati wa vita kila nilipokuwa nikiangalia pembezoni mwangu nilikuwa nikimuaona Ummu Umara anapigana karibu yangu"* (Ibn Hajar, Al-Isaba, IV, 479).

Ummu Umara Hatun alichaguliwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika mambo mbalimbali. Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuombea. Wakati fulani alimuambia Mtume:

"Niombee kwa Mwenyezi Mungu nije kuwa jirani yako peponi". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Ewe Mwenyezi Mungu! Mjaalie awe rafiki yangu na jirani yangu peponi"*. Baada ya hili Umma Umara akasema:

"Tokea sasa bahati yoyote mbaya itakayonikuta katika dunia hii haina madhara" (Waqidi, I, 273; Ibn Sa'd, VIII, 415).

❁

Wakati wa vita vya Uhud, kundi la waumini lilisikia uvumi kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amekufa na kupatwa na fadhaa kubwa na kuchanganyikiwa. Anas ibn Nadr ؓ akawapigia kelele kwa kuwaambia:

"Kuna tatizo gani mkifa au mkiishi kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amekufa? Njooni mpigane na muwe mashahidi kama yeye alivyofanya". Kisha akawashambulia wapagani. Baada ya muda mfupi aliuawa baada ya kupata majeraha zaidi ya themanini (Ahmad, III, 253; Ibn Hisham, III, 31).

Vita vya Uhud vilipomalizika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtuma mmoja wa maswahaba zake akamtafute Sa'd ibn Rabi ؓ ili ajue yuko katika hali gani. Kadiri yule swahaba alivyojaribu kumtafuta hakumpata na kadiri alivyopiga kelele kumuita hakuitikiwa. Kwa matumaini ya mwisho akaita kuelekea walipolazwa mashahidi na waliojeruhiwa:

"Ewe Sa'd! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amenituma. Ameniamuru nikutafute nijue kama upo hai au umekufa".

Wakati ule Sa'd alikuwa anapumua pumzi yake ya mwisho na hakuwa na nguvu ya kujibu. Hata hivyo aliposikia kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ana wasiwasi juu yake, alikusanya nguvu zake zote na kufanikiwa kusema kwa sauti ya chini:

“Mimi ni miongoni mwa waliokufa”. Ni jambo la wazi kuwa alikuwa anaelekea akhera. Yule swahaba akakimbia kuelekea pale Sa’d alipolala. Alimkuta na kuona mwili wake uko vipande vipande kutokana na majeraha mbali mbali ya panga. Alifanikiwa kusikia maneno yafuatayo ambayo yalionyesha kilele cha mapenzi aliyokuwa nayo kwa Mtume:

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, wakati bado macho yako yanaweza kutikisika, lakini ukaacha kumlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutokana na maadui na ukaruhusu apate madhara basi hakuna sababu utakayoweza kuitoa mbele ya Mwenyezi Mungu” (Muwatta, Jihad, 41; Hakim, III, 221/4906; Ibn Hisham, III, 47).

❁

Wanawake wa Madina walikuwa wametoka nje ya mji wakitumaini kuwa watapata habari kutoka kwenye uwanja wa vita. Aisha alikuwa miongoni mwao.

Aisha alipowasili Harra alimkuta Hind bint Amr, mwanamke aliyekuwa mwema. Hind alikuwa amebeba miili ya mashahidi akiwemo mumewe, Amr ibn Jamuh, mwanae Hallad, na kaka yake Abdullah juu ya ngamia. Aisha akamuuliza:

“Kuna habari gani huko?”

Hind bint-i Amr akatoa jibu lifuatalo lililo zuri kabisa:

“Habari njema, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yuko hai! Hali ya kuwa yuko hai habari nyingine mbaya hazina umuhimu”... (Waqidi, I, 265; Ibn Hajar, Fath al-Bari, Daral Fikr, ts., III, 216; Ibn Abdiller, al-Istiab, Cairo, ts., III, 1168).

❁

Tukio jingine kutoka Uhud linaelezewa hapa chini:

Katika siku ya Uhud, Habari moja ilitiukisa mji wa Madina, ilisemekana kuwa ‘ Muhammad ﷺ ameuawa’.

Makelele yakalipuka ndani ya mji na vilio vikapaa mpaka angani. Kila mtu akawa anaelekea barabarani ili kujaribu kupata habari kutoka kwa wale wanaorejea. Pindi Sumayra Hatun, ambaye ni miongoni mwa Answar, alipopata habari kuwa watoto wake wawili, baba yake, mumewe na kaka yake wamekufa, yule mwanamke aliyebarikiwa hakushtushwa bali alikuwa na shauku ya kupata habari juu ya jambo linalomtia wasiwasi. Nini kimemtokea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

“Kuna chochote kilichomtokea?” aliendelea kuuliza.

Maswahaba waliobarikiwa wakajibu:

“Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni mzima. Yuko hai, kama ambavyo ungelipenda”.

Sumayra Hatun akasema:

“Sitapumzika mpaka nimuone, nionyesheni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu”.

Walipomuonyesha upesi akamsogelea na kusema yafuatayo huku ameshika joho lake:

“Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hakuna jambo lingine muhimu hali ya kuwa wewe uko hai” (Waqidi, I, 292; Haythami, VI, 115).

Hivyo kilele cha mapenzi juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kujitolea na mifano ya wema imeonekana kwa hawa waumini ambao nyoyo zao zilijawa na mapenzi yake.

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alienda kuwatembelea mashahidi wa Uhud. Huku akiwaashiria mashahidi akasema:

*"Nashuhudia imani yao na utii wao"*.

Abu Bakr ؓ akauliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je sisi si ndugu zao? Kama walivyokuwa waislamu, je sisi hatukuingia kwenye Uislamu? Je hatukupigana jihad kama wao walivyopigana?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Ndio unachosema ni kweli, lakini sijui ni jambo gani mtalizusha baada ya mimi kuondoka"*.

Abu Bakr, ambaye hakuweza kutengana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hata muda mchache, akaanza kutokwa na machozi na kisha akauliza:

"Unamaanisha mimi nitakuwa hai baada ya wewe kuondoka ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?" akionyesha wasiwasi na huzuni aliyokuwa anahisi katika kuishi bila yeye (Muwatta, Jihad, 32).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwatuma waalimu kwenda kuwafundisha Uislamu makabila ya jirani. Pia Makabila ya Adal na Kare walimuomba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ awatumie mwalimu. Kikundi cha watu kumi kikatoka kuyaendea makabila haya. Hata hivyo waliangukia kwenye mtego. Wanane kati yao wakauawa na wawili wakafanywa watumwa. Kisha Zayd ibn Wasina na Hubayb walitolewa na kupewa washirikina wa Makka ambao nao kwa matokeo yake wakawaua. Kabla ya Hubayb kuuawa aliulizwa:

"Je hutamani kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ angelikuwa katika nafasi yako na wewe ukaachiwa huru?"

Huku akimuangalia vibaya Abu Sufyan ambaye aliuliza swali, Hubayb akajibu:

"Sahau kwa mimi kuwa na familia yangu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuchukua nafasi yangu, Nisingelitamani hata atobolewe na mwiba ili niwe huru".

Abu Sufyan alipatwa na mshangao juu kitendo hiki cha mapenzi ya hali ya juu na kusema:

"Inastaajabisha! Kamwe sijapata kuona watu wawili wakipendana kama maswahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wanavyompenda Mtume wao" (Waqidi, I, 360; Ibn Sa'd, II, 56).

Kabla ya Hubayb kuuawa aliomba salamu za amani zilizojawa na mapenzi zitumwe kwa Mtume.

Lakini nani angeweza kuzipeleka? Akageuzia macho yake mbinguni kwa udhalili na kuomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Hapa hakuna mtu atakayeweza kupeleka salamu za amani kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hivyo nakuomba uzipeleke salamu zangu za amani kwake".

Wakati ule Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa amekaa pamoja na maswahaba zake ndani ya Madina, akasema 'Wa alayhissalam' ('Na juu yake iwe amani'). Baada ya maswahaba zake kumsikia, wakamuuliza kwa mshangao:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Umemuitikia nani salamu?"

Akajibu:

*"Nimeitikia salamu ya amani kutoka kwa ndugu yangu Hubayb. Aliyeniletea ni Jibril ambaye yupo hapa"*.

❀

Wakati mwingine upendo wa maswahaba kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ulikuwa mkubwa kiasi kwamba hawakuweza kushirikiana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ miongoni mwao. Ka'b ibn Ujra ﵁ anasimulia tukio lifuatalo:

"Siku moja tulikuwa tumekaa mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndani ya msikiti wake. Kulikuwa na kundi kutoka answar, muhajirina na wana wa Hashim. Tukaanza kushindana: "Ni kina nani kati yetu ambao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anawapenda zaidi?" Sisi, Answar wakasema:

"Tulimuamini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tulimfuata, tulipigana dhidi ya maadui zake. Kwa hiyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anatupenda sisi zaidi".

Ndugu zetu miongoni mwa muhajirina wakasema:

'Tulihama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Tuliziacha familia zetu na watoto wetu. Tuliziacha mali zetu. Pia tulishiriki kwenye vita ambavyo mlipigana. Hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ (lazima) atupende zaidi'.

Ndugu zetu kutoka kwa wana wa Hashim wakasema:

"Mlikuwa mnasema kitu? Mlikuwa mnazungumzia nini?"

Wote tukarudia tulichokisema. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akayaambia makundi yote:

*"Mko sahihi. Nani anaweza kueleza kinyume na hayo?"* Baadae akasema: *"Je mtapenda nihukumu kati yeni?"*

"Bila shaka ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Baba zetu na mama zetu watolewe kwa ajili yako". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

*"Ni nyinyi enyi answar. Mimi ni ndugu yenu".*

Kwa furaha answar wakasema:

"Allahu Akbar (Mwenyezi Mungu ni Mkubwa zaidi). Tunaapa kwa Mola wa Al-Kaaba (tumemshinda) tumempata".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Enyi muhajirina! Mimi ni mmoja wenu".

Muhajirina kwa furaha wakasema:

"Allahu Akbar! Tunaapa kwa Mola wa Al-Kaaba tumemshinda (yeye ni wetu)".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Enyi wana wa Hashim! Nikirudi kwenu, nyinyi mnatoka kwangu na mlikuja kwangu".

Kutokana na furaha wana wa Hashim wakasema:

"Allahu Akbar! Tunaapa kwa Mola wa Al-Kaaba yeye ni wetu".

Hivyo wote tulitoshelezwa. Kila kundi lilifurahi na kutosheka na nafasi waliyopewa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. (Haythami, X, 14).

❀

Kukipenda kila alichokipenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ilikuwa ni furaha kubwa kwa maswahaba zake. Anas ؓ anasimulia:

"Siku moja fundi cherehani alimualika Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwenye chakula alichokiandaa. Nikaungana naye. Mwenyeji akaleta mezani mkate uliotengenezwa kwa, supu iliyo na nyama choma. Nilimuona akitafuta vipande vya tokea pande mbali za chakula. Tokea siku ile nikapenda kula". (Bukhari, At'imah, 33, Buyu' 30; Muslim, Ashriba 144; Muwatta, Nikah, 51).

Kukipenda kile ambacho kipenzi chako anakipenda ni dalili ya wazi ya upendo wa mtu.

❁

Hali ifuatayo ya Abu Bakr ﷺ ni mfano mzuri wa mapenzi na hisia: Pindi Makka ilipokombolewa alimpeleka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ baba yake ambaye ni kipofu na mzee kwa matumaini kuwa angeingia katika Uislamu. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipowaona akasema:

"Ewe Abu Bakr! Kwa nini umemleta baba yako kikongwe tokea huko mpaka hapa na kumsababishia tabu? Si tungeliweza kumfuata?".

Abu Bakr ﷺ akajibu:

"Nimemleta kwako kwa kuwa nilitaka apate malipo ya Mwenyezi Mungu".

Pindi Abu Quhafa, ambaye ni baba wa Abu Bakr ﷺ alipotoa mkono wake (kuushika mkono uliobarikiwa wa Mtume) ili kukubaliana naye, Abu Bakr ﷺ akashindwa kujizuia na akaanza kutokwa na machozi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomuuliza Abu Bakr kwa nini analia, huku machozi yakitiririka mashavuni mwake Abu Bakr akajibu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Natamani huu mkono ambao kwa sasa unakuja kwako kufanya makubaliano ungelikuwa mkono wa mjomba wako Abu Talib na si baba yangu ili Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi awe amekuridhisha wewe na si mimi. Ungelikuwa na furaha kiasi gani! Kwani ulimpenda sana na ulitamani aingie kwenye Uislamu..." (Haythami, VI, 174; Ibn Sa'd, V, 451).

❁

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoenda kuhiji alikuwa akisimama kuwaongoza waislamu kwenye swala katika vituo

mbali mbali njiani. Baadae waislamu wakajenga misikiti katika maeneo haya kama alama ya utii na mapenzi na kuweka kumbukumbu yake daima. (Ibn Sa'd, II, 173).

❁

Maswahaba walionyesha mifano mingi ya wema juu ya vitu vya Mtume, ambavyo waliviona kuwa na baraka kubwa. Wakati wa Hijja ya kuaga wakati nywele za mbele za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ zinakatwa, Khalid ibn Walid alimsihi Mtume:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nipe baadhi ya nywele zako mimi na si mwingine. Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako!'[7] Alipopewa zile nywele akazichana na kuziweka mbele ya kofia yake. Kutokana na baraka za nywele hizi hakuna mtu aliyeweza kumshinda katika vita. Khalid amesema:

"Nikienda na nywele hizi, sehemu hiyo tumeiteka" (Waqidi, III, 1108; Ibn Athir, Usdu al-ghabah, II, 111).

❁

Siku moja swahaba wa kike alimpelekea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ joho alilokuwa amelifuma mwenyewe. Akamwambia:

"Nimelifuma hili kwa mikono yangu mwenyewe ili ulivae".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akilihitaji joho lile hivyo alilivaa na kwenda kwa maswahaba zake. Mmoja wao alipomuona akasema:

"Uzuri ulioje wa joho hili! Je unaweza kunipa na mimi nilivae ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

7. Hapa Abu Bakr alikuwa anafikiria kile ambacho Khalid aliwafanyia waislamu katika vita vya Uhud, vita vya Handak na Hudaybiya. Alikuwa anafikiria mambo hayo na pale nilipomuona katika hali ile nilipigwa na bumbuwazi.

"Sawa". Baada ya kukaa nao kwa muda akaenda nyumbani kwake na kulikunja na kumtumia yule mtu. Maswahaba wakamuambia yule mtu:

"Hukufanya jambo zuri. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alilivaa joho lile kwa kuwa alikuwa analihitaji. Na wewe ulimuomba huku ukijua kuwa yeye kamwe hakatai anapoombwa".

Swahaba akafafanua kama ifuatavyo:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu sikumuomba lile joho ili nilivae bali liwe ndio sanda yangu".

Na hapo ndipo joho lile likaishia kuwa sanda yake (Bukhari, Janaiz 28, Buyu 31, Libas 18).

❀

Sahl ibn Sa'd ؓ anasimulia tukio lifuatalo ambalo linaonyesha namna ambavyo hata watoto wadogo walivyokuwa na kiwango kile kile cha kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliletewa kinywaji. Akanywa kidogo. Upande wake wa kulia alikuwa amekaa mtoto na upande wake wa kushoto walikuwepo maswahaba wakubwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipotaka kutoa kitu alikuwa akianzia upande wake wa kulia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamsemesha yule mtoto kwa hisia, upole na heshima:

"Je utaniruhusu nianze kutoa kinywaji hiki kwa wakubwa kwanza (upande wangu wa kulia)?"

Mtoto yule mwenye akili alitoa jibu lifuatalo lenye kustaajabisha ambalo lilimstaajabisha kila mtu pale na ambalo lilikuwa somo kwa watu wote:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nisingeliweza kamwe kuruhusu mtu mwingine anichukulie kitu ambacho umenipatia wewe".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akampatia kinywaji yule mtoto kwanza. (Bukhari, Ashriba 19).

❁

Ulipofika muda wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuiaga dunia ilikuwa ndio chanzo cha mfadhaiko na machungu makubwa kwa maswahaba, kutokana na kumpenda zaidi ya nafsi zao. Anas ibn Malik ﷺ anasimulia:

'Pindi maradhi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yalipozidi uchungu uliongezeka. Binti yake, Fatima ﷺ alipoona hali hii alimuambia:

"Ewe baba! Naona unahisi maumivu makali!" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"Binti yangu, Baada ya leo hakutakuwa na maumivu zaidi kwa baba yako".

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipofariki Fatma akalia na kusema yafuatayo:

"Ewe baba mpendwa ambaye kinyume na yeye hakuna aliye karibu zaidi na Mola wake.

Ewe baba mpendwa ambaye alikubali mwito wa mola wake.

Ewe baba mpendwa ambaye makazi yake ni pepo ya Firdaws[8].

Ewe baba mpendwa. Tutakaa na habari za kifo chako na rafiki yako Jibril tu".

8. *Firdaws* ni moja wapo ya madaraja ya pepo.

Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuzikwa, Fatma akatoa masikitiko yake juu ya kufiwa kama ifuatavyo:

"Imekuwaje mikono yenu ikawa na haraka kumfukia kwa udongo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Nyoyo zenu zimewezaje kulikubali hili?" (Bukhari, Maghazi, 83; Darimi, Muqaddima, 14. Angalia Ibn Majah Janaiz, 65).

❁

Siku moja Abdullah ibn Zayd al-Ansari ﷺ alienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusema yafuatayo huku akitokwa na machozi:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nakupenda zaidi ya ninavyoipenda roho yangu, mali zangu, watoto wangu na familia yangu. Kama nisingeliweza kuja kukuona basi ningelitamani kufa".

Kutokana na hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamuuliza:

"Kwa nini unalia?"

Abdullah ibn Zayd akajibu:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninalia kwa kuwa nimefikiria kuwa siku moja wewe utakufa na sisi tutakufa. Wewe utakuwa katika daraja la juu pamoja na Mitume wengine wakati sisi hata kama tutaingia peponi tutakuwa katika daraja la chini, hivyo nilikuwa ninalia kwa kufikiria kuwa sitaweza kukuona".

Mtume, ambaye ndiye bahari ya huruma alikaa kimya kwa muda bila kujibu. Wakati ule aya ifuatayo ikashushwa:

"**Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!**" (Nisaa 4:69).

Siku moja wakati Abdullah ibn Zayd anaishughulikia bustani yake mtoto wake akaja huku anakimbia na kuhema na kumletea habari kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ameiaga dunia. Dunia ya Abdullah ikamgeukia kichwa chini miguu juu. Akaomba dua ifuatayo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Naomba uchukue uoni wangu ili nisiweze kuona kitu kingine tofauti na kipenzi changu pekee, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"

Abdullah akajibiwa dua yake na hivyo kupoteza uoni kuanzia pale. (Angalia Qurtubi, V, 271).

❁

Kuna swahaba mwingine ambaye alipoteza uoni kutokana na kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuwa na hisia kama za Abdullah ibn Zayd. Baada ya kupoteza uoni wake baadhi ya rafiki zake wakaenda kumpa pole. Akawapa jibu lifuatalo kutokana na kumpa pole kwao:

"Nilikuwa nayahitaji macho yale ili nimuone Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Kuna tatizo gani sasa kama ameondoka na mimi nina macho swala mzuri kuliko wote" (Ibn Sa'd, II, 313).

Baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, maswahaba wakawa kama mishumaa inayoungua na kuyeyuka kutokana na huzuni waliyokuwa nayo. Siku ile maswahaba walichomwa kwa maumivu ya kutengana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na hivyo wakawa wanatangatanga. Hata Omar رضي الله عنه alipoteza fahamu kwa muda. Abu Bakr رضي الله عنه alikuwa na wakati mgumu katika kujaribu kuwapooza. Nyoyo zile za mapenzi hazikuweza kuvumulia kutomuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hata kwa siku moja. Itawezekanaje kuvumilia kwa kutoweza kumuona tena.

❁

Baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ Bilal hakuweza tena kusoma adhana kutokana na huzuni aliyokuwa nayo, ingawa alikuwa na sauti nzuri mno. Kutokana na kusisitizwa na maswahaba wengine alijaribu kuisoma lakini alipokuwa anaangalia katika mimbari ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiitumia kusimamia, na kisha akakosa kumuona, basi alikuwa akipata kizuizi katika koo lake, na hivyo sauti yake kushindwa kutoka vizuri na matokeo yake kushindwa kuisoma adhana. Aliondoka Madina na kwenda Syria ili ajaribu kuzima moto wa mapenzi uliokuwa unawaka ndani yake. Siku moja alimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika ndoto na kumuambia:

*"Utengano ulioje ewe Bilal? Je huu sio wakati kwa wewe kunitembelea?"*.

Bilal akaamka akiwa na majonzi na upesi akaondoka kuelekea Madina. Akaenda kwenye kaburi la Mtume.

Wakati analia mbele ya kaburi la Mtume, wajukuu wa Mtume, Hasan na Hussein wakaja. Bilal akawakumbatia na kuwabusu. Wakamuambia:

"Ewe Bilal! Tunatamani kusikia adhana kutoka kwako" Waliposisitiza akaanza kuisoma. Wakati ule Madina ikatikisika. Alipofikia mstari 'Nashuhudia kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu', kila mtu, mwanamne na mwanamke, wakatoka na kuelekea kwenye msikiti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakidhani kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amefufuka. Tangia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ afariki watu wa Madina hawakupata kulia kama walivyolia siku hiyo (Ibn Athir, Usdu al-ghabab, I, 244-5; Dhahabi, Siyar, I, 357-8).

Swahaba huyu aliyebarikiwa, ambaye alimpenda mno Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifariki ndani ya Damascus wakati akiwa na umri wa zaidi ya miaka sitini. Wakati anakufa alisema:

"Mwenyezi Mungu akipenda kesho naenda kukutana na rafiki yangu mpendwa- Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na marafiki zake". Baada ya kuyasikia haya, mke wake akaanza kulia:

"Ewe mpenzi". Hata hivyo Bilal, ambaye moyo wake ulikuwa umejawa na shauku akasema:

"Ubora ulioje, uzuri ulioje". (Dhahabi, Siyar, I, 359).

Watu hawa walikumbatia tangazo la Mtume- 'Utakuwa pamoja na yule unayempenda'. Walijaribu kuongeza mapenzi yao kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambayo yalikuwa ndio rasilimali yao na njia pekee ya utulivu. Anas رضي الله عنه amesema:

"Baada ya neema ya kuwa Muislamu hakuna habari nyingine njema zaidi ya 'Utakuwa pamoja na yule unayempenda' ambayo ilitufurahisha zaidi. Na hivyo nampenda Mwenyezi Mungu, nampenda Mjumbe wake, na Abu Bakr na Omar. Ingawa sikuweza kufanya matendo mema waliyoyatenda, lakini natumaini nitakuwa nao" (Muslim, Birr, 163).

Siku moja wakati Omar رضي الله عنه anatembelea mitaa ya mji aliona mshumaa unawaka kwenye nyumba moja. Alipoikaribia ile nyumba alimuona bibi kizee anaviringisha pamba na huku anasoma shairi lifuatalo:

"Amani na Baraka za watu wema ziwe juu ya Muhammad Mustafa. Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Na watu wote wema wakutumie salamu za rehema juu yako. Ulikuwa ukifanya ibada nyakati za usiku na kutokwa na machozi katika masaa ya alfajiri. Hata hivyo kifo kinamkuta mtu yeyote kwa awamu. Ah! Lau kama ningelifahamu kama nitakutana na kipenzi changu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika maisha ya kesho akhera".

Omar alianza kulia baada ya kusikia shairi hili lenye mguso. Kisha akagonga mlango. Yule bibi kizee akamuuliza yeye ni nani.

'Ni Omar ibn Khattab' Omar akajibu. Yule bibi kizee akamuuliza kwa shauku:

"Omar atakuwa anataka nini kwangu muda huu wa usiku?"

Omar akajibu:

"Kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu tafadhali fungua mlango, usiogope"

Pindi Yule bibi alipomfungulia mlango Omar akamwambia:

"Tafadhali unaweza kulisoma tena shairi ulilotoka kulisoma muda si mrefu?"

Yule bibi akafanya vile. Alipofikia mstari wa mwisho akamwambia:

"Naomba uniweke na mimi miongoni mwenu". Kisha yule bibi akasoma tena mstari wa mwisho wa shairi kama ifuatavyo:

"Lau kama ningelifahamu kama nitakutana na kipenzi changu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika maisha ya kesho akhera mimi pamoja na Omar. Ewe Mwenyezi Mungu mwingi wa kusamehe! Msamehe Omar". Kisha Omar akaondoka akiwa ameridhika mno. (Ali al-Muttaki, XII, 562/35762).

❀

Baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kamwe Fatma hakuonekana akitabasamu tena. (Ibn Sa'd, II, 312).

Hakuna wakati ambao Abdullah ibn Omar رضي الله عنه alilitaja jina la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ bila ya kulia. (Ibn Sa'd, II, 312).

Anas رضي الله عنه alisema:

"Sijawahi kuota ndoto ambayo sikumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wangu kipenzi" (Ibn Sa'd, VII, 20).

Kwa sababu Anas ndiye aliyemfahamu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ zaidi kuliko watu wengine, aliishi vile vile kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyoishi na pia alikuwa akiswali kama yeye. Wakati wote alikuwa na fimbo ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kipande cha nywele zake. Alipokufa hii fimbo iliwekwa pembeni yake na hiki kipande cha nywele kiliwekwa chini ya ulimi wake, kutokana na ombi lake.

❁

Pale maswahaba waliobarikiwa walipomzungumzia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ walitumia maneno ya upendo kama vile 'kipenzi' na 'rafiki yangu'. Haya yaliwapa raha kubwa[9]. Kila kitu katika uso wa dunia kilikuwa kikiwakumbusha kuhusu rafiki yao kipenzi. Abu Dharr alisema:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa kuhamia kwake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwenye ulimwengu mwingine kumetuacha katika hali ambayo pindi tunapomuona ndege akipiga mabawa yake tunakumbuka hadith ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Kwani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa alisema:

*"Mambo yote yameshaelezwa kwenu yakiwemo yale yanayowasogeza karibu na pepo, na yale yanayowaweka mbali na Moto"*. (Ahmad, V, 153, 162; Haythami, VIII, 263)

❁

Ukbah ibn Haris ؓ anasimulia:

Siku moja Abu Bakr ؓ alikuwa amemaliza kuswali swala ya adhuhur na kuondoka msikitini. Akaanza kutembea pamoja na Ali. Wakakutana na Hasan, mjukuu wa Mtume, akiwa anacheza

9. Bukhari, Tahajjud 33, Sawm 60; Muslim, Mûsairin 85, 86; Abu Dawud, Witr 7; Nasai, Siyam 81, Qiyamu'l Layl 28; Ibn Majah, Sadaqat 10; Darimi, Sawm 38; (Ahmad V, 159, Ibn Sa'd, IV, 229).

pamoja na watoto wengine. Upesi Abu Bakr akamshika na kumuweka kwenye mabega yake na kusema:

"Baba yangu atolewe kwa ajili yako. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu hakika wewe unafanana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na si Ali", Ali akawa anawaangalia huku ametabasamu (Bukhari, Manaqib, 23).

❁

Pindi maswahaba walipokuwa wanahadithia *hadith* kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ walikuwa makini mno wasije wakasema jambo ambalo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakulisema. Amr ibn Maymuna anasimulia:

"Kamwe sikuwahi kukosa mazungumzo ya Ibn Mas'ud kila Alhamisi usiku. Katika mazungumzo haya kamwe sikuwahi kumsikia akisema 'Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema' kutokana na hofu yake. Hata hivyo usiku mmoja miongoni mwa masiku haya alianza kuongea kwa kusema 'Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema'...kisha akainamisha kichwa chake na hakumalizia maneno yake. Baada ya kusubiri kwa muda nikamuangalia. Vifungo vya shati lake vilikuwa vimefunguliwa na machozi yalikuwa yakimtiririka. Akasimama huku mashavu yake yamevimba. Baada ya kusimama vile kwa muda akaendelea:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema...au alisema jambo kama hili, au alisema jambo sawa..." (Ibn Majah, Muqaddima 3).

❁

Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kufariki kila Abu Bakr ؓ alipohadithia hadith alianza kulia kwa kumkumbuka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na alipata tabu kuongea. Abu Huraira ؓ anaelezea hali yake kama ifuatavyo:

"Siku moja Abu Bakr ؓ alipanda mimbar na kusema:

'Wote mnajua kuwa mwaka uliopita Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisimama hapa niliposimama sasa"...Kisha akaanza kulia. Kisha akarudia maneno yake lakini akaanza kulia tena. Akajaribu tena kwa mara ya tatu lakini hakuweza kujizuia, akaanza kulia tena..." (Angalia Tirmidhi, Dawat, 105).

❁

Aisha رضي الله عنها anasimulia pindi baba yake, Abu Bakr رضي الله عنه alipokuwa kitandani anaumwa na mauti yamemkaribia. Akaelezea furaha aliyokuwa nayo baba yake juu ya hisia za kwenda kukutana na rafiki yake wa kipekee, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa.

"Siku moja wakati baba yangu yuko kwenye kitanda cha mauti aliuliza:

"Leo ni siku gani?"

"Jumatatu", tukamjibu.

"Kama nikifariki leo msingojee mpaka kesho (kunizika). Kwani kwangu bora wa masiku ya mchana na usiku ni yale yaliyo karibu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ (yani wakati wa kukutana naye haraka iwezekanavyo)" (Ahmad, I, 8).

Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kufariki, Abu Bakr رضي الله عنه alijikuta kama mgeni katika dunia hii. Wakati huu ambao anakaribia kufa alikuwa na furaha kutokana na kuelekea kwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake.

❁

Wakati baadhi ya maswahaba waliokuwa wanampenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kutamani kukutana naye kwa haraka, walipokuwa wanaumwa, maswahaba wengine waliwaonea wivu kwa kuwa ilimaanisha kuwa walikuwa wanakaribia kukutana

na Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake mapema. Walikuwa wakituma salamu iliyojaa upendo kwa kupitia wagonjwa wale. Mfano mmojawapo ni wa Muhammad ibn Munkadir ؓ ambaye siku moja alimtembelea Jabir alipokuwa mgonjwa mno. Alipogundua kuwa anakaribia kufa, Muhammad ibn Munkadir akamwambia Jabir (ambaye alikuwa ana shauku ya kuwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu):

"Chukua salamu zetu umpelekee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ". (Ibn Majah, Janaiz 4).

Maswahaba waliwapenda ndugu na vipenzi vya Mtume. Kwa mfano Omar alikuwa na sahani tisa ambazo alikuwa akiweka ndani yake matunda, njugu na vitu vingine na kuwatumia wake za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kisha mwishoni alikuwa akimtumia binti yake. Kama kulikuwa na chochote kilichopungua katika sahani hii, alikuwa akiijazia kutoka kwenye mgao wake (Muwatta, Zakat 44).

❀

Siku moja Omar alitoa dirham 3500 kwa ajili ya Usama, mtoto wa Zayd ibn Harith, mtumwa ambaye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuachia huru. Na akampa mtoto wake mwenyewe Abdullah dirham 3000.

Abdullah akapinga mgao huu kwa kusema:

"Kwa nini umemzidishia Usama zaidi yangu? Hajashiriki katika vita vingi zaidi yangu".

Omar ؓ akatoa jibu lifuatalo lililoonyesha namna alivyokuwa akitoa kwa haki na uzuri wa moyo wake:

"Mwanangu! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimpenda baba wa Usama zaidi ya alivyokuwa akimpenda baba yako. Na pia alimpenda zaidi Usama kuliko wewe. Hii ndio sababu nimewapa kipa-

umbele vipenzi vya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu juu ya vipenzi vyangu mwenyewe" (Tirmidhi, Manaqib, 39/3813).

❁

Anas ﷺ anasimulia tukio lifuatalo:

"Siku moja nilikuwa katika safari pamoja na Jarir ibn Abdullah[10]. Jarir akaanza kumhudumia, nikamwambia:

"Tafadhali usifanye hivyo". Akanijibu:

"Niliwaona watu kutoka Answar wakimtumikia na kumhudumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na mimi nikaahidi kuwa pindi nitakapofanya urafiki na mtu yeyote kutoka Answar nitamhudumia" (Bukhari, Jihad 7; Muslim, Fadail-as Sahaba, 181).

Mapenzi yaliyoje!...

Maswahaba wengi walikuwa wakiishi na kumbukumbu za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kwa mfano Abu Mahzura ﷺ alikuwa hazikati nywele zake za mbele wala kuzigawanya. Hili ni kwa sababu siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alizigusa nywele zake.

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimwambia mwanamke kutoka Gifari:

*"Chukua chombo chenye maji, tia chumvi ndani yake. Kisha fulia kitambaa chenye matone ya damu".*

10. Jarir ibn Abdullah alikuwa kiongozi wa kabila la Bajila ndani ya Yemen. Alikuwa amekuja Madina mwaka wa 10 wa hijiria katika mwezi wa Ramadhani, yani miezi mitatu baada ya kifo cha Mtume. Alikuja pamoja na kundi la watu 150 kwa ajili ya kuja kuingia kwenye uislamu. Alikuwa anampenda Mtume sana. Na Mjumbe wa Allah ﷺ pia alikuwa anampenda sana na alikuwa anatabasamu kila alipokuwa anakutana naye.

Yule swahaba mwanamke alichukua ushauri huu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuutumia kwa mapenzi makubwa katika maisha yake yote, na kamwe hakufua nguo zake bila ya kuweka chumvi. Na alipokufa alisema aoshwe kwa maji yenye chumvi. (Abu Dawud, Taharah, 122/313).

Mapenzi yaliyoje. Haya ni mapenzi ambayo kamwe hayakufifia katika kipindi chote cha maisha na yaliongezeka kadiri ya muda ulivyoenda.

❁

Siku moja mishipa ya mguu wa Ibn Omar ilikaza. Abdurrahman ibn Sa'd ambaye alikuwa karibu naye akamwambia:

"Litaje jina la yule unayempenda kuliko wote". Kisha Ibn Omar akasema:

"Ewe Muhammad!" Mara mguu wake ukapona (Ibn Sa'd, IV, 154).

❁

Katika kuashiria mapenzi makubwa waliyokuwanayo umma wake juu yake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema yafuatayo:

*"Miongoni mwa wale wanaonipenda kutakuwa na kundi la watu ambao watanifuata. Wataziacha mali zao na familia zao ili waweze kuniona"* (Muslim, Jannah, 12; Hakim, IV, 95).

Hivyo wamepita marafiki wengi wa Mwenyezi Mungu tokea enzi za neema mpaka leo ambao wamechomwa na mapenzi ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

Abdullah ibn Mubarak anasimulia:

"Siku moja nilikuwa pamoja na Imam Malik. Alikuwa akisimulia baadhi ya *hadith* kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Wakati anaongea mara nge akaja na kumuuma kwa mfu-

lululizo. Rangi ya uso wake ilibadilika na kusawajika lakini aliendelea kusimulia *hadith* za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Somo lilipoisha na watu kuondoka nikamwambia:

"Ewe Abu Abdullah! Leo kulikuwa na kitu tofauti kwako"

"Ndio", akajibu. "Nge aling'ata tena na tena lakini nilivumilia. Jambo hili liliwezekana kutokana na mapenzi na unyenyekevu nilionao kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" (Munawi, III, 353; Suyuti, *Miftahu al-Jannah*, uk. 52).

Imam Malik (rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) aliishi kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Kutokana na kumheshimu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakuweza kupanda mnyama ndani ya Madina wala hakuweza kujituliza. Alipokuwa imam katika *Rawdah* (chumba kilichopo kwenye msikiti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambacho ndicho alichofia), wakati wote alikuwa akiongea kwa sauti laini. Siku moja wakati Khalifa Abu Jafar Mansur alipoongea kwa sauti kubwa, upesi akamuonya:

"Ewe Khalifa! Shusha sauti yako eneo hili. Onyo la Mwenyezi Mungu lililetwa kwa watu ambao ni wema zaidi yako" na kisha akasoma aya ifuatayo:

"**Enyi mlio amini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyo semezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui**" (Hujurat, 49:2).

❀

Tokea alipokuwa na umri mdogo Imam Malik alikuwa makini mno katika kuonyesha heshima juu ya *hadith* za Mtume. Aliweka umuhimu mkubwa katika kuonyesha unyenyekevu mkubwa ili kuzihifadhi kwa usahihi na alijaribu kuzisikiliza kwa utulivu na katika hali ya amani. Ndio maana kamwe hakusikiliza hadith

aliyosimuliwa huku amesimama, wala hakuhudhuria masomo ya *hadith* huku akiwa kwenye dhiki, huzuni au hajitambui. Alihofia kukosea wakati wa kusimulia *hadith* yoyoye. Siku moja aliulizwa:

"Je umewahi kusikia hadith iliyosimuliwa na Amr ibn Dinar?"

Akajibu:

"Nilimuona akisimulia *hadith* na huku watu wamesimama pembeni yake wanaandika (anachokisema). Hata hivyo sijawahi kuikubali hadith yoyote aliyoindika mtu wakati amesimama".

Imam Malik alikuwa ni mtu mwenye kuheshimika, kwani alikuwa na tabia njema katika hali zake zote na wakati wa masomo yake. Ama wakati anatoa fatwa au wakati anasimulia hadith kutoka kwa Mtume, uso wake ulikuwa uking'aa. Pindi alipotaka kusimulia *hadith* kutoka kwa Mtume, alikuwa akichukua udhu, akijiandaa na kuvaa vazi lake lililo bora kuliko yote. Alipotaka kuisoma hadith alikuwa akikaa katika mimbar.

Pindi watu walipomjia katika nyumba yake mtumishi wake alitoka nje na kuwaambia:

"Imam anauliza: Je mnataka kusikiliza hadith au mnataka kuuliza kuhusu jambo la kisheria?". Ikiwa walitaka kuulizia kuhusu mambo ya kisheria basi Imam alitoka nje na kujibu maswali yao. Lakini kama walitaka kusikiliza *hadith*, alikuwa akiwaambia 'kaeni chini'. Kisha alikuwa akienda na kuchukua udhu, akijipulizia manukato mazuri, akivaa mavazi mapya, akifunga kilemba chake na kisha kupanda juu ya mimbar ambapo hutoa somo lake la *hadith* kwa unyenyekevu mkubwa. Pale ndani huchoma ubani na moshi wake ulikuwa ukitoa harufu nzuri mpaka mwisho wa somo.

❁

Abida as-Salmani alikuwa mmoja wa wasambazaji wakubwa wa *fiqh* na *hadith* kutoka katika karne ya *Tabi'een*[11].

Aliingia kwenye Uislamu miaka miwili kabla ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuiaga dunia, lakini hakubahatika kumuona. Maneno yafuatayo kutoka kwa Abida yanaonyesha mapenzi waliyokuwa nayo waislamu wa mwanzo juu ya Mtume:

"Kipande cha nywele kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni bora zaidi kwangu kuliko hazina yote iliyopo ndani ya dunia" (Ahmad, III, 256).

Baada ya kuyasoma maneno ya Abide as- Salmani yalitotajwa hapo juu, nae mwanachuoni maarufu aitwae Zehebi akaonyesha mapenzi yake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kama ifuatavyo:

"Maneno ya Abide ambayo yanaonyesha kukipa kwake kipaumbele kipande kimoja cha nywele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu dhidi ya dhahabu yote na fedha inayomilikiwa na watu ni dalili ya kilele cha mapenzi. Kama mwanachuoni huyu mkubwa ameweza kuyasema maneno hayo miaka hamsini baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kufa, na sisi tungesemaje kama miaka 700 baada ya kifo chake tungepata unywele wake mmoja au kipande cha kandambili yake au kipande kimoja cha kikombe chake cha udongo alichokitumia kunywea maji?

Kama angetokea tajiri na kutaka kutumia sehemu kubwa ya mali zake ili kukipata kitu hicho je ungeliweza kumtazama kama mtu anayetumia mali yake vibaya au anayeipoteza? Bila shaka hapana. Usijizuie kutumia chochote ulicho nacho ili uutembelea msikiti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambao aliujenga kwa mikono yake mwenyewe na kumtumia salamu za amani kutokea

11. *Tabi'een* ni kizazi cha pili cha Waislamu baada ya maswahaba. Ni wale waislamu waliowaona maswahaba katika uhai wao, lakini sio Mtume. (Maelezo ya mfasiri).

karibu na chumba chake kilichoneemeka ndani ya mji wenye kupendwa kuliko miji yote.

Ukifika Madina uangalie kwa shauku mlima wake alioupenda wa Uhud na wewe pia uupende. Kwani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa ﷺ aliupenda mno mlima wa Uhud. Tembelea mara kwa mara *Rawdah* yake na sehemu alizokaa na angalia mpaka uutosheleze moyo wako. Kwani huwezi kuwa muumini (wa kweli) mpaka umpende mtu huyu zaidi ya unavyoupenda uhai wako, mtoto wako, kila kitu unachokimiliki, na watu wote hapa duniani…” (Dhahabi, Siyar, IV, 42-3).

❃

Mmoja wa wanafunzi wa Imam Shafii’, Rabi ibn Sulayman anasimulia:

Siku moja Imam Shafii’ aliniambia:

“Rabi, ipeleke barua hii kwa Ahmad ibn Hambal na kisha unirudishie majibu”

Nikaichukua barua na kwenda Baghdad. Nilikutana na Ahmad ibn Hambal katika swala ya alfajiri ambayo tuliiswali wote. Pindi Imam Ahmad alipotoka kwenye mihrabu nikampa ile barua na kumwambia:

“Barua hii inatoka kwa ndugu yako kutoka Misri, Imam Shafii”. Akaniuliza:

“Je unafahamu barua inahusu nini?”

Nikajibu kuwa sifahamu.

Kisha Ahmad ibn Hambal akaichukua barua, akaondoa kifuniko na kuanza kuisoma. Mara macho yake yakajawa na machozi. Nikamuuliza:

“Ewe Imam. Kuna nini? Barua inasemaje?” Akasema:

"Imam Shafii' alimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa katika ndoto. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimwambia:

"Mwandikie barua Ahmad ibn Hambal na umtumie salamu zangu za amani. Atakumbwa na uchochezi na ataombwa asema kuwa 'Qur'an imeumbwa'. Kuwa makini na usikubali matakwa yao. Mwenyezi Mungu atalifanya jina lake likumbukwe na kutukuzwa mpaka siku ya mwisho'.

Nikamwambia:

"Ewe Imam! Uzuri ulioje wa habari hii kwako!"

Kutokana na furaha Imam akavua shati lake na kunipa. Nilipopata majibu nikaondoka kuelekea Misri. Nilimpa barua Imam Shafii naye akasema:

"Tusingelipenda kuchukua shati lako alilokupa. Lakini angalau lichukue na ulizamishe kwenye maji na kisha utupe maji hayo ili na sisi tupate mgao wa baraka za shati hilo". (Angalia Ibn al-Jawzi, Manaqibu'l Imam Ahmad ibn Hanbal, (thk, Abdullah ibn Abdulmuhsin at Turki) Cairo 1409 uk 609-610).

❁

Mwanachuoni wa hadith na ambaye ni *mujtahid* (mwenye kufanya jitihada katika dini), Imam Nawawi alifanya kila jambo lake katika maisha yake kwa kumfuata Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na alikuwa kitu kimoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kiasi kwamba alikuwa hali tikiti maji katika maisha yake yote kwa sababu hakujua kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikula tikiti maji kwa kulikata au kwa kulivunja.

❁

Pia ni muhimu kuelezea mapenzi ya Imam Bushiri juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

Siku moja muandishi maarufu wa Qaswida za Burda, Imam Bushiri, wakati yuko njiani anarudi nyumbani kwake alikutana na babu ambaye alikuwa amejitenga na dunia. Yule babu akamwambia:

“Ewe Bushiri! Je ulimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu katika ndoto usiku wa kuamkia leo?” Imam Bushiri akamjibu:

“Hapana sikumuona”.

Yule babu hakusema jambo lingine akaondoka. Hata hivyo maneno yale yaliwasha moto wa mapenzi na shauku ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa katika moyo wake. Usiku wake Imam akamuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika ndoto kiasi kwamba akaamka kwa furaha na amani ndani ya moyo wake. Kutokana na hili akaanza kuandika aya za kumsifu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambazo zilisababisha kupata wapenzi wengi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambao waliingia kwenye bahari ya mapenzi ya Mtume.

Baadae nusu ya mwili wake ukapooza kiasi cha kushindwa kutembea wala kusogea. Ni wakati ule ndipo alipoandika Qaswida Burda ili kumuomba Mwenyezi Mungu amponye. Usiku aliomaliza kuandika Qaswida alimuona tena Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwenye ndoto na kumsomea zile Qaswida. Alipomaliza kuzisoma Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasugua miguu ya Imam Bushiri iliyopooza kwa mikono yake iliyobarikiwa. Upendo ulioje aliokuwa nao kiasi kwamba alipoamka akakuta miguu yake imepona na hivyo akamshukuru Mwenyezi Mungu.

Kutokana na kurudishiwa afya yake, asubuhi yake akaenda msikitini kwa furaha kubwa. Njiani alikutana na Shaykh Abu’ ar-

Reja, ambaye alimwambia:

“Ewe Bushiri! Tafadhali unaweza kunisomea *Qaswida* zinazomsifu Mtume Muhammad ﷺ, furaha ya ulimwengnu?”

Imam Bushiri akamuuliza:

"Nina *Qaswida* nyingi ambazo zinamsifu Mtume. Ni ipi unayotaka nisome?"

Shaykh Abu' ar- Reja akasema:

"Ninataka unisomee ile uliyoisoma mbele ya Mtume. Kwani nimeona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiifurahia sana *Qaswida* hiyo".

Imam Bushiri akashangazwa kwani hakujua kuwa kuna mtu mwingine aliyeisikia Qaswida ile (Angalia Ilhan Armutcuoglu, "Qasida-i Burda Manzum Tercumesi," Konya 1983,p 7-10).

❁

Sayyid Ahmad Yasavi alikuwa ni mtu mwema mno ambaye alikuza nuru ya Uislamu na mng'ao wake katika nyoyo, kuanzia Asia ya kati mpaka Balkans. Alipofikisha miaka 63 alijichimbia mwenyewe kaburi lake na kusema:

"Baada ya umri huu sitaki kuishi tena juu ya ardhi". Kutokana na masimulizi inasemekana kuwa aliishi miaka 10 iliyobaki katika maisha yake ya ibada na uongofu ndani ya kaburi hili, kwa matumaini ya kuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu".

❁

Aliyeitwaa India, Gazneli Mahmud, alikuwa na mtumishi aliyempenda aitwae Muhammad. Wakati wote alikuwa akimuita kwa jina lake. Siku moja hakumuita mtumishi wake kwa jina lake lakini kwa jina la baba yake. Mtumishi wake akaumizwa na kitendo hiki cha Sultan Mahmud na kuvunjwa moyo wake. Alipomuuliza kwa nini alimuita vile, Gazneli Mahmud akamjibu:

"Mwanangu mpendwa! Nimekuwa nikikuita kwa jina lako kila siku. Na katika siku zote hizo nilikuwa na udhu. Lakini kwa

sasa sina udhu. Ndio maana niliona aibu kukuita jina lako. Na ndio maana nikakuita kwa jina la baba yako”.

❁

Dola ya Uthmainiyya ilikuwa dola, taifa zima lilipambwa kwa mapenzi ya Mtume. Kuanzia mchungaji mpaka Sultan, walikuwa wakimswalia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pindi jina lake litajwapo na kuweka mikono yao kwenye moyo kuonyesha unyenyekevu wao kwake. Walikuwa wakisimama pindi wasikiapo tungo za mazazi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika *Mawlid-i Sharif*[12]. Namna hii ya heshima imekuwa desturi. Kamwe hakupita Sultan wa Uthmainiyya ambaye hakuchukua udhu pale alipopata ujumbe kutoka Madina, au kuubusu na kuifuta karatasi yake juu ya macho yao au kuusoma huku wamesimama.

Kwa kuongezea ni kwamba wale watu wa Dola ya Uthmainiyya ambao walikuwa wakiukarabati msikiti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ walihakikisha kuwa hawanyanyui jiwe lolote bila ya kuwa na udhu na kuanza kwa ‘Bismillah’ (Kwa jina la Mwenyezi Mungu). Walikuwa na maadili mazuri mno kiasi kwamba walikuwa wakifunika nyundo zao kwa kitambaa ili kuzuia wasiisumbue roho ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Hii ni mifano ya tabia njema na heshima ambayo haijawahi kuonekana kabla yake.

*Surre Alayi*[13] ambalo lilitumwa kwenda Madina katika kipindi cha Uthmainiyya, lilikuwa linapokaribia na kuingia katika mji linasimamishwa na watu kujiandaa kwa ajili ya kuingia katika ukanda

12. Mawlud-i Sharif ni jarida lililobeba mashairi yanayoelezea mazazi na sifa za Mtume.
13. “*Surra Alayi*” lilikuwa ni tamasha lililokuwa linafanyika kila mwaka kabla ya kipindi cha Hijja ndani ya mwezi wa Rajab. Vifurushi vya fedha, dhahabu na zawadi nyingine vilikuwa vikitolewa na matajiri wa Istanbul na kupewa masikini wa Makka na Madina.

wa kiimani wa Madina. Walikuwa wakiswali swala ya *istikhara*[14] na kisha kuingia kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu huku wakiwa wamepokea kiashirio cha kiroho. Wakati wa kurudi nchini kwao, walikuwa wakienda na udongo uliobarikiwa kutoka Madina kutokana na sifa zake za kutibu na baraka zake.

Vishada vinavyoweza kuonekana juu ya vilemba vya Sultan wa kiuthminiyya katika visanamu mbalimbali, ambavyo vinatoa picha ya wakati ule, vinaashiria mafagio. Kwa kupitia mafagio haya, walimaanisha kuwa wao walikuwa wafagizi wa *Haramayn-Sharif* (miji miwili mitukufu ya Makka na Madina) na hivi ndivyo walivyojiweka. Pia Sultan wa kiuthminiyya walikuwa wakitumia fedha zao binafsi kuwalipa wale waliochukua jukumu la kusafisha *haramayn*.

❁

Alama nyingine ya mapenzi makubwa na heshima juu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa ni kuweka ncha za nywele za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na ndevu zake juu ya mimbar za msikiti. Ziliviringishwa katika matabaka 40 na kuwa ukumbusho Mtukufu. Zilipewa jina la '*Sakal-i Sharif*', na zimekuwa chanzo cha baraka na rehema kwa umma kwa karne nyingi.

❁

Yavus Sultan Selim Han aliitwaa Misri na kupewa uongozi wa eneo la Hijaz. Siku ya ijumaa tarehe 20 mwezi wa pili ndani ya msikiti wa Malik Mueyyed mtoaji wa hotuba ya ijumaa alimtaja kama:

'*Hakimu al-haramayn ash Sharifayn*' yani 'Mtawala wa sehemu mbili zilizobarikiwa za Makka na Madina'. Upesi Yavuz akamkatisha na huku anatokwa na machozi, akasema:

14. Swala ya *Istikhara* ni swala inayoswaliwa na mtu pindi anapotaka kufanya maamuzi juu ya jambo fulani (Maelezo ya mfasiri).

"Hapana, hapana! Sio hivyo. Sema '*Khâdimu al-Haramayn*' *ash Sharifayn*', 'mtumishi wa sehemu mbili zilizobarikiwa'. Kisha akaondoa zulia na kusujudu katika sakafu katika kumsifu Mola wake. Na katika kuonyesha kuwa yeye ni 'mtumishi wa sehemu mbili zilizobarikiwa' akaweka kishanga kilicho na umbo la ufagio na kukiweka juu ya kilemba chake.

Baadae maneno aliyomwambia Piri Pasha, ambaye alimpa ugavana wa ardhi hizi zilizobarikiwa, ni alama ya mapenzi yake ya kweli kwa Mtume:

"Pasha! Usultani wa Makka na Madina uko mikononi mwa watoto watukufu wa Bwana wa Ulimwengu. Sikuzichukua ardhi hizi mbili kwa nguvu ya kijeshi. Walinionyesha utii uliotokana na umoja wao wa kiislamu na ubora wao, tabia zao njema na wema wao. Sina budi kulipa fadhila hizi. Ninamsifu Mwenyezi Mungu usiku na mchana ili jina langu likumbukwe katika ardhi hizi zilizo-bariki

❁

Wa wakati wa kusoma hotuba ya ijumaa. Siwezi kubadilisha-na furaha hii kwa ufalme wa dunia nzima. Kwa hiyo msiwanyime chochote muhimu watu wa *al Haramayn ash Sharifayn*. Na kuwa makini usiingilie mambo ya nchi hizi mbili zilizobarikiwa".

Kwa karne sasa mababu zetu wameonyesha heshima ya hali ya juu na mapenzi juu ya vitu alivyovimiliki Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na vitu vya kumbukumbu yake. Ili kuona baadhi ya mifano yenye kustaajabisha juu ya jambo hili, itatosha tukiangalia historia ya amana tukufu, huduma ambayo mababu zetu waliiheshimu sana.

Masultani wa dola ya Uthmainiyya ambao hawakutamani kuwa mbali na , joho lililobarikiwa la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hata kwa dakika chache, walitembea nalo kokote wali-

poenda kwa njia mbalimbali. Kilijengwa chumba ndani ya kasri la Istavroz, sehemu ambayo lilikuwepo kasri la Beylerbeyi, ili kulihifadhi joho hilo, kama ilivyofanyika katika kasri la zamani la Edirne, na kama ilivyo leo katika kasri la Topkapi.

Pia joho lililobarikiwa lilipelekwa vitani. Kisanamu chenye kuonyesha moja wa misafara hii ni muhimu mno. Kinachoweza kuonekana kutokana na kisanamu hiki ni kwamba joho hili lililobarikiwa lilibebwa na walinzi mbalimbali waliokuwa wakiteuliwa katika kipindi chote cha safari.

❀

Mehmed wa tatu, mmoja wa masultani wa dola ya Uthmainiyya, alikuwa ni Sultani mkali na mwenye hasira sana. Licha ya hivi lakini alijawa na mapenzi ya Mtume. Kila jina la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ lilipotajwa alikuwa akisimama upesi na kuonyesha mapenzi na unyenyekevu wake kwake. Pindi Mehmed wa tatu alipoenda kwenye msafara wa Egri alibeba bango na joho lililobarikiwa. Alipoona askari wa kiislamu wanapoteza matumaini katika hatua moja ya vita wakati wakiwa na tishio la kushindwa, mshauri wa Sultani, Sadeddin Efendi, akamwambia:

"Sultani wangu! Katika hali kama hii, inatakiwa wewe, kama Sultani wa familia ya Othman na Khalifa katika njia ya Mtume, ulivae joho lililobarikiwa na umuombe Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi". Hivyo akampa ruhusa ya kuvaa joho lililobarikiwa. Kisha Mehmed Sultan wa tatu akamswalia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusema '*Mwenyezi Mungu ni Mkubwa*' kisha akalivaa joho lile lililobarikiwa. Matokeo yake akawa chanzo cha kuwatia moyo askari wake na kupelekea ushindi.

Pindi Sultani Ahmed wa kwanza alipokuwa anajenga msikiti wake, aliamuru alama za miguu ya Mtume Muhammad ﷺ ziletwe kwenye kaburi la Ayyub Sultan. Zilitolewa kwenye kaburi la

Sultan Kayitbay kutoka Misri. Pindi msikiti ulipoisha akaamuru ziwekwe kwenye msikiti huo. Hata hivyo usiku ambao walikuwa wakihamisha alama zile, aliota ndoto ambayo inaweza kuelezewa kama ifuatavyo:

"Kulikuwa na mkusanyiko mkubwa wa masultani wakiwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa ambaye alikaa miongoni mwao katika nafasi ya hakimu. Kulitengenezwa aina fulani ya mahakama ambamo Sultan Kayitbay alikuwa anamshitaki Sultan Ahmet. Alikuwa analalamika kuwa amechukua alama za miguu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuzipeleka Istanbul. Zile alama zilikuwa sababu ya watu kulitembelea kaburi lake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akiwa kama hakimu akaamuru zile alama zirudishwe mara moja..."

Sultan Ahmet aliamka huku akiwa na hofu kubwa na kutishika. Akawaendea baadhi ya wanachuoni na mashekhe, wakiwemo Aziz Mahmud Hudayi na kuwaomba wamtafsirie ndoto yake. Wakamwambia:

"Sultan wangu! Ndoto yako iko wazi mno. Haihitaji kutafsiriwa. Amana lazima irudishwe upesi".

Sultan Ahmet wa kwanza, ambaye alimpenda sana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitii jambo lile mara moja, kwa uangalifu mkubwa na huzuni aliamuru zirudishwe. Hata hivyo aliachwa anaungua moyoni kutokana na mapenzi yake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na ndipo akatengeneza mfano wa nyayo zilizobarikiwa kwa kutumia marumaru. Akaagiza ziwekwe kwenye kilemba chake kama chanzo cha ustawi. Mistari ifuatayo ambayo aliiandika mwenyewe inaonyesha mapenzi aliyokuwa nayo kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa:

*Kama ningeliweza ningelifanya alama tukufu za nyayo za Mfalme wa Mitume kuwa taji juu ya kichwa chake daima.*

*Mmiliki wa nyayo hizo ni waridi la utume.*
*Hivyo gusisha uso wako kwenye waridi hilo, ewe Ahmad...*

❁

Abdulaziz Han alikuwa ni Sultan mwingine aliyempenda sana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Siku moja alituma barua yenye kutia uchungu ikimuelezea Mtume, ipelekwe Madina na kuwekwa kwenye *Rawda Mutahhara*[15]. Baadhi ya mistari kutoka kwenye barua hiyo ni hii ifuatayo:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwenye kurehemu.

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye ni mmoja.

Na rehema na amani ziwe juu yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

Na rehema na amani ziwe juu yako ewe kipenzi cha Mwenyezi Mungu.

Na rehema na amani ziwe juu yako ewe Mtume wa umma huu!...

Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu...Wewe ndiye rafiki wa kweli. Wewe ni mfano wa wema na ukarimu. Wewe ni yule ambaye juu yako Mwenyezi Mungu amesema: '*Kama si wewe, Nisingelikuwa nimeumba ulimwengu*'. Wewe ni chanzo cha furaha kwa viumbe vyote. Muombezi wetu, kimbilio letu. Yule ambaye kila kitendo chake ni cha wema na chenye kurehemewa. Hata vumbi la nyayo zako linang'aa. Mwalimu mkuu wa viumbe vyote. Kila amali yako ilikuwa nzuri. Upendo wako unajaza ulimwengu mzima. Wewe ndiye mwisho wa Mitume na ndio kimbilio lao.

15. Barua hii inaweza kupatikana kwenye kasri la Topkapi ndani ya chumba cha Hirka-i Saadet.

Wewe ndiye kiongozi wetu katika siku ya hukumu na muombezi wa wakosefu walio ndani ya umma wako. Wewe ndiye uliyeweza kuonyesha vizuri zaidi Umoja wa Mwenyezi Mungu na pambo la Mitume. Wewe ndiye hakimu wa baraza la Mitume na Mtume kwa wale wanaoingia katika njia ya Mwenyezi Mungu, mwingi wa huruma. Wewe ni kipenzi cha mwingi wa Rehema.

Ewe Muhammad Mustafa! Ni wewe ambaye unapewa sifa zote hizi...

Licha ya udhaifu wangu nilipata ujasiri wa kupangusa uso wangu mchafu juu kaburi lako lenye kung'aa, mnyororo wake wenye kung'aa, na udongo safi katika ardhi yako. Nimefanya hivi kwa udhalili, staha na heshima. Nimeonyesha ujasiri wa kuleta jambo langu kwenye mlango wako wenye kutoa harufu nzuri, kwa mwili wangu wenye madhambi wenye kustahiki adhabu, miongoni mwa maelfu ya hisia za aibu na staha, ili kuonyesha huzuni yangu kwa heshima...

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu kwa kunifanya kuwa miongoni mwa umma bora wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa utii, furaha, heshima na imani. Umma wa kipenzi cha Mwenyezi Mungu ambaye ni mkarimu na mwenye kuneemeshwa...

Naomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu kutokana na madhambi yangu yote. Naomba msamaha tena na tena...

Tuonee huruma! Tuonee huruma! Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!...Usituache...

Ewe baba wa Fatma Zahra رضي الله عنها. Rehema na amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu ziwe juu yako.

Ewe babu wa Hasan na Hussein! Rehema na amani ziwe juu yako.

Ewe bwana wa wale waliokuja kabla yako na baada yako. Rehema na ziwe juu yako...[16]

❁

Sultani Abdulhamid Han aliagiza reli ya Hijaz ijengwe ili waislamu kutoka dunia nzima waweze kusafiri kwa wepesi kwenda *Haramayn*. Ili kuendana na desturi za Mtume, aliagiza vituo vijengwe kila mahali ambapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipumzika wakati wa misafara yake. Kwa namna hii reli ilwapeleka watu mpaka Madina katika mandhari ya upendo.

❁

Wasifu na kumbukumbu ya sifa ambazo washairi waliandika katika kuonyesha mapenzi yao kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu vilijaza vitabu. Mshairi aitwae Nabi anaelezea mapenzi yake kwa namna nzuri zaidi:

*"Sababu iliyonifanya nikusifu ni hii- ni kwamba hata miti, mawe, mimea na viumbe visivyo hai vimeingia kwenye utukufu wako na kuongea na wewe".*

❁

Ni kweli kwamba muda baada ya muda hata wanyama na mimea, na wanadamu pekee, wameonyesha mapenzi makubwa juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mfano wa hili unatolewa na Safina رضي الله عنه, ambaye alikuwa mtumwa aliyeachwa huru na Mtume:

"Nilikuwa nasafiri baharini na kisha boti niliyoipanda ikavunjika vipande vipande. Nilishikilia kipande kimoja cha mbao ambacho kilinipeleka mahali ambapo kuna miti mingi na ambapo simba wanapatikana. Simba mmojawapo akanisogelea ili anirarue. Nikamwambia:

16. Hilmi, Aydin, "Hirka-i Saadet Dairesi ve Mukaddes Emanetler", Istanbul 2004, pg 272-5.

"Ewe mwenye njaa! Mimi ni mtumwa wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nchi yangu ni fulani, na nimepatwa na jambo fulani..."

Mara simba akasimama, akainamisha kichwa chake na kunisogelea. Akanisukuma kwa mabega yake mpaka nikajikuta nimetoka nje ya miti mingi. Baada ya kunifikisha kwenye barabara kuu akaanza kukoroma kwa furaha. Nikagundua kuwa alikuwa akiniaga. Na hicho ndicho cha mwisho kukiona" (Hakim, III, 702/6550; Abdurrazzak, XI, 281-2; Tabarani, VII, 94).

❁

Maneno mengi zaidi na mifano isiyo na idadi inaweza kutolewa kuhusu kilele cha mapenzi waliyokuwa nayo umma wa Mtume. Tuliyoyaelezea ni kama tone kwenye bahari yenye kina kirefu.

Kwa hakika tunafahamu kuwa ukizungumziwa wema katika umma wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, unatokana na mapenzi yao kwake. Ni cheche za mapenzi yaliyo ndani ya nyoyo zao. Wema huu unajumuisha moyo wao kufanya ibada, ustaarabu wao, kuboresha tabia zao, uzuri wa nyoyo zao, mng'ao wa sura zao, fasaha katika maongezi yao, uzuri wa hisia zao, na uzuri wa mitazamo yao.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa ndiye chanzo pekee cha rehema na mapenzi ambayo yanaweza kuwapeleka kwenye bahari ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Ndio maana mapenzi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yanachukuliwa kuwa sawa na mapenzi kwa Mwenyezi Mungu, utii kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni sawa na utii kwa Mwenyezi Mungu na uasi dhidi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kama uasi kwa Mwenyezi Mungu.

**Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atujaalie mgao wa utukufu wa kiimani kutoka katika moyo wa kiimani wa muongozaji**

**pekee katika njia iliyonyooka, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa. Tujaalie nyoyo zetu ziwe zenye kudhihirisha mapenzi kwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie sisi sote tupate uombezi wake. Amin...**

**Kama unaridhia, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!**

**Tusaidie, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!**

**Tuombee, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!**

**c. Kuwapenda waislamu wenzetu**

Kadiri mapenzi kwa Mwenyezi Mungu yanavyoongezeka kwa mja, inakuwa ni sharti kwamba mapenzi haya yasambae kwanza mpaka kwenye nuru ya Muhammad, na kisha kwenye utukufu wake, kisha kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu, na kisha yasambae na kukijumuisha kila kiumbe kilichotukuzwa na Mwenyezi Mungu kulingana na madaraja yao. Hivyo katika kumgeukia Mwenyezi Mungu, mduara wa upendo unakuwa ndio chanzo cha uponyaji na rehema katika nyoyo. Hivyo waumini wanapokuwa katika mambo yao hawana budi kuwa makini ili wasitoke nje ya mduara huu wa rehema na upendo. Hii ni njia na matokeo ya kumpenda Mwenyezi Mungu na kujisogeza karibu yake.

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anasema katika Qur'an tukufu kwamba waumini wote ni ndugu. (Al Hujurat 49:10). Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatujulisha kuwa haiwezekani kuifikia imani ya kweli bila ya kuasisi mapenzi imara miongoni mwa ndugu wa kiimani. Ili kuasisi mapenzi haya, anaushauri umma wake kutoleana salamu miongoni mwao.[17]

17. Muslim, Iman 93-4

Kuwapenda waumini wenzako ni tabia ya wema ambayo Mwenyezi Mungu anapendezwa nayo mno. Furaha ya hapa duniani na kesho akhera pia inategemea mapenzi haya. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Siku ya kiama Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atasema:*

*Wako wapi wale waumini ambao walionyesha mapenzi miongoni kutokana na kunitii Mimi? Katika siku hii ambayo hakuna kivuli, nitawafunika kwenye kivuli changu mwenyewe, na nitawalinda"* (Muslim, Birr, 37).

*"Kuna makazi yenye nuru kwa wale waliopendana ili kupata radhi zangu, makazi ambayo hata Mitume na Mashahidi watakuwa na shauku nayo"*[18]. (Tirmidhi, Zuhd, 53/2390).

Katika hadith nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatufahamisha kwamba siku ya kiama, wakati ambapo hakutakuwa na kivuli, lakini wale waumini ambao walipendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na ambao walikuwa pamoja na kutengana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu watakingwa na kivuli cha arshi ya Mwenyezi Mungu[19]. Huu ni ushahidi wa undugu katika nyakati za shida na tabu.

Kukataa kuongea na ndugu wako wa kiislamu ni jambo lenye kuonyesha dharau ambalo kamwe halikubaliki. Kuhusiana na suala hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Si ruhusa kwa Muislamu kukataa kuongea na ndugu yake katika Uislamu kwa zaidi ya siku tatu. Zikipita siku tatu tokea*

18. Kutokana na ufafanuzi wa hadith kilichomaanishwa katika maneno "Shauku ya Mitume na mashahidi" sio kwamba kundi hili la watu litakuwa juu ya Mitume na mashahidi lakini ni katika kuonyesha hali ya utukufu kwa wale wanaopendana kwa ajili ya Allah, imeelezewa hivi kama namna ya kuwapa moyo.
19. Bukhari, Adhan, 36

*waache kuongea basi mmoja wao atakapokutana na mwenzake amtolee salamu. Kama ndugu yake ataitikia salamu basi wote wawili watapata malipo. Kama hataitikia basi yeye ndiye atakayepata dhambi. Na yule aliyemtolea salamu atakuwa amesamehewa"* (Abu Dawud, Adab, 47/4912).

*"Yeyote atakayekataa kuongea na Muislamu mwenzake kwa mwaka mmoja atahesabika sawa na aliyemwaga damu yake"* (Abu Dawud, Adab, 47/4912).

Kutokana na Mtume, matendo yaliyofanywa na mja yanapandishwa kwa Mwenyezi Mungu ama katika siku ya jumatatu au alhamisi. Mwenyezi Mungu anasamehe madhambi ya waja wake wote isipokuwa wale waliokataa kuongea na ndugu zao waislamu na wale waliomfanyia Mwenyezi Mungu washirika. Anawaambia malaika wawaache mpaka wapatane. (Muslim, Birr, 35-36; Abu Dawud, Adab, 47).

***Matukio ya wema***

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimshika mkono Muadh na kumwambia:

"*Ewe Muadh! Naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa nakupenda*". Muadh ؓ akajibu:

"Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Na wewe pia nakupenda, tena sana". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

*"Ewe Muadh. Nakuusia kutoacha kuleta dua ifuatayo kila baada ya swala: 'Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie nikukumbuke, nikushukuru na niwe miongoni mwa waja wako wema"* (Ahmad, V, 244-5; Abu Dawud, Witr, 2; Nasai, Sahw, 60; Tirmidhi, Zuhd, 30).

Uzuri ulioje wa mapenzi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimpenda Muislamu mwenzake Muadh, na kama alama ya upendo huu akamuusia jambo lenye faida kwake.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kuna watu miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu ambao si Mitume, wala mashahidi, lakini siku ya kiama watawekwa katika sehemu ambazo hata Mitume na mashahidi watawaangalia kwa tamaa".*

Maswahaba wakauliza:

"Ni watu gani hao na ni matendo gani mema waliyoyafanya? Tufahamishe ili tuwapende na kuwa nao karibu, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"Hao ni wale watu ambao ingawa hawana udugu wa damu miongoni mwao, wala mahusiano ya kibiashara au kiuchumi, lakini bado wanapendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu nyuso zao ninang'aa na wapo juu ya nguzo za nuru. Pindi wengine wapopata hofu, wao hawahofu, na pindi wengine wanapopata huzuni , wao hawahuzuniki".

Kisha akasoma aya ifuatayo:

"**Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika. Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu. Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko kufuzu kukubwa**" (Yunus, 10:62-64).

❁

Abu Idris al-Hawlani (Mwenyezi Mungu amrehemu) anasimulia:

Nilipoenda kwenye Msikiti wa Damascus nilimkuta kijana mmoja akiwa na sura ya bashasha. Alikuwa amezungukwa na kikundi cha watu. Watu walipotofautiana katika jambo lolote upesi walienda kwa yule kijana kuomba msaada na kukubali maoni yake. Niliuliza huyu kijana ni nani. Waliniambia alikuwa ni Muadh ibn Jabal ﷺ.

Siku iliyofuata nilienda msikitini mapema iwezekanavyo. Nilipofika pale nilimkuta yule kijana tayari ameshafika na anaswali. Nilimsubiri mpaka alipomaliza kisha nikamsogelea na kumsalimia kwa maamkizi ya amani na kisha nikamuambia:

“Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu! Nakupenda”.

“Je unanipenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?” akaniuliza.

“Ndio kwa ajili ya Mwenyezi Mungu” nikamjibu. Kisha akaniuliza mara mbili:

“Je unanipenda kweli kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?” Nyakati zote mbili nilimjibu:

“Ndio ninakupenda kweli kwa ajili ya Mwenyezi Mungu”. Kisha akashika joho langu na kunivuta kuelekea kwake na kuniambia:

“Nakupongeza. Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema:

*“Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amesema: ‘Wale wanaopendana kwa ajili yangu, na wale wanaokusanyika kwa ajili yangu, na wale wanaotembeleana kwa ajili yangu na wale wanaotoa sadaka na kutenda mema kwa ajili yangu…Watakuwa miongoni mwa wale waliopata mapenzi yangu”* (Muwatta, Sha’r, 16).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisimulia kisa kifuatacho chenye kuonyesha namna mtu atakapompenda Muislamu mwenzake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu atakavyowezeshwa kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

*"Siku moja mtu mmoja aliondoka kwa lengo la kumtembelea ndugu yake katika Uislamu aliyekuwa akiishi katika kijiji kingine. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alimteua malaika na kumpa jukumu la kumuangalia yule mtu njiani. Yule mtu alipomjia malaika, malaika akamuuliza:*

*'Unaenda wapi?'*

Yule mtu akajibu:

*'Ndugu yangu katika Uislamu anaishi katika kijiji kile. Naenda kumuona'.*

Malaika akamuuliza:

*'Je kuna chochote unachotegemea kufaidika kutoka kwa huyo rafiki?'*

Yule mtu akajibu:

*'Hapana, hapana. Ni kwa kuwa tu nampenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Mimi ni Mjumbe niliyetumwa kwako kukupatia habari njema'* (Muslim, Birr, 38; Ahmad, II, 292).

❁

Anas ibn Malik ؓ anasimulia tukio lifuatalo linaloelezea namna mtu mwenye udugu wa kweli wa kiislamu anavyoweza kuipata pepo.

Siku moja tulikuwa tumekaa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa, akasema:

*"Mtu wa peponi atakuja hapa sasa hivi".*

Tulipoangalia tukamuona mtu kutokana na Answar, ambaye ndevu zake zinadondosha maji ya udhu na huku amebeba viatu vyake katika mkono wake wa kushoto. Siku iliyofuata Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akayarudia maneno yake, na yule mtu akajitokeza tena vile vile. Siku ya tatu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akayarudia maneno yake, na yule mtu akajitokeza kama ilivyokuwa kwa siku ya kwanza. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliponyanyuka na kuondoka, Abdullah ibn Amr akanyanyuka na kumfuata yule mtu na kumuomba:

"Nimetofautiana na baba yangu na nimeapa kutokwenda kwake kwa siku tatu. Je unaweza kuniruhusu niishi na wewe katika kipindi hiki?"

Yule mtu akamjibu:

"Sawa".

Baadae, Abdullah ibn Amr ؓ akatuambia:

"Nilikuwa naye kwa masiku yale matatu. Lakini sikupata kumuona akiamka kuswali usiku. Lakini alikuwa akifanya dhikr na kutaja takbir mpaka ulipofika muda wa swala ya alfajiri. Kamwe sikumsikia akiongea jambo lolote lile ila lililo la kheri. Baada ya usiku wa tatu, nilihisi kana kwamba nimedharau matendo yake pindi nilipomwambia:

"Ewe mja wa Mwenyezi Mungu! Hakukuwa na tofauti kati yangu mimi na baba yangu. Lakini nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema yafuatayo mara tatu kuhusu wewe: '*Mtu wa peponi atakuja sasa hivi mbele yenu*'. Na wewe ulijitokeza katika nyakati zote tatu. Nilitaka kukaa na wewe ili nijue unafanya nini, na nilitaka kuiga mfano wako. Hata hivyo sijaona kuwa umefanya jambo lolote kubwa lisilo la kawaida. Ni amali gani inayokufanya ufikie daraja ambalo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakusifu nalo?"

Yule mtu akajibu:

“Hakuna zaidi ya ulichokiona”.

Nilipotaka kuondoka akasema:

“Sina matendo mengine zaidi ya uliyoyaona. Hata hivyo kamwe siwawekei kinyongo ndugu zangu waislamu (Moyo wangu umejawa mapenzi kwa waislamu wote). Na kamwe sikionei wivu chochote kizuri alichopewa mtu mwingine na Mwenyezi Mungu”.

Kisha nikamwambia:

“Hili ndilo lililokuwezesha kufikia daraja hili” (Ahmad, III, 166).

Huu ni moyo Muislamu ambaye anawaangalia waumini wote kama ndugu zake wa damu na anakaa nao kwa wema...

❁

Zubayr ibn Awwam ﵁ anasimulia tukio kubwa la udugu lililotokea katika vita vya Uhud.

“Wakati wa vita vya Uhud mama yangu alitoa masweta mawili aliyokuja nayo na kusema:

“Nimeleta masweta haya ili uweze kutengenezea sanda kwa ajili ya ndugu yako Hamza”.

Tukachukua masweta yale na kuelekea mahali ambapo Hamza ﵁ alilazwa. Pembeni yake tulimkuta shahidi kutoka Answar na hakuna sanda iliyopatikana kwa ajili yake. Tukajisikia vibaya kumfunika Hamza kwa masweta yote mawili na kumuacha huyu mtu bila sanda. Tulimfunika Hamza kwa sweta mojawapo na tukaliacha sweta jingine kwa ajili ya yule mtu kutoka Answar. Tukapiga kura kupata ni nani angelipata sweta kubwa na nani angelipata sweta dogo” (Ahmad, I, 165).

Hiki ni kisa cha kweli chenye kuonyesha kuwa udugu wa kiislamu unaweza kuupita udugu wa damu.

❁

Ibn Omar ﷺ anazungumzia nyoyo zilizopevuka wakati wa enzi ya neema kwa maneno yafuatayo mazuri:

"Tumeishi katika nyakati ambazo hakuna hata mmoja miongoni mwetu aliyejiona bora kama fedha na dhahabu zaidi ya ndugu zao waislamu" (Haythami, X, 285).

❁

Muumini hana budi kujihusisha na ndugu wake wa kiislamu, na pia hana budi kuwa makini naye na kusumbuliwa na kile kinachomsumbua. Yani amfikirie kabla hajajifikiria mwenyewe. Na ajaribu kumkidhia haja zake. Tunaweza kuona mfano bora wa jambo hili kwa kupitia matendo ya Dawud al-Tai.

Siku moja mwanafunzi alikuwa akipata huduma yake alimwambia:

"Nimeandaa nyama; je unaweza kula pamoja na mimi?"

Alipoona mwalimu wake yupo kimya akampelekea ile nyama. Hata hivyo Dawud al- Tai (roho yake itakaswe) hakutaka kuiangalia nyama ile na akasema:

"Je kuna habari gani kuhusu yatima fulani na fulani, mwanangu?" Yule mwanafunzi wake akavuta pumzi kidogo na huku akiashiria kuwa walikuwa katika hali mbaya, akasema:

"Kama unavyowafahamu, mwalimu" Kisha yule rafiki mkubwa wa Mwenyezi Mungu akasema:

"Kama ni hivyo, wapelekee hii nyama". Yule mwanafunzi wake mwaminifu ambaye alitaraji bwana wake angelikula nyama aliyoindaa alisema:

"Imekuwa muda mrefu tangu ule nyama, bwana".

Kadiri alivyojitahidi kusisitiza, lakini Dawud al- Tai hakukubali bali alisema:

"Mwanangu! Kama mimi nitaila nyama hiyo, kitakachotekea ni kwamba baada ya muda mfupi itatolewa. Lakini kama mayatima hao wataila, itapandishwa mpaka kwenye enzi tukufu ya Mwenyezi Mungu na kubaki huko milele, (yani nitapata malipo makubwa kutokana nayo)..."

❁

Hivyo wale wenye urafiki na Mwenyezi Mungu pia wana urafiki na viumbe wengine wote, na hasa kwa waislamu wenzao. Wanawaangalia ndugu zao waislamu kwa upendo na huruma kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wanakuwa na mapenzi makubwa juu yao. Mapenzi haya yanaongezeka mno kiasi cha kuwafanya watake kusaidia watu wote. Hata wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa, ambaye alikuwa katika kilele cha urafiki, alipopigwa mawe kule Taif, alikuwa anawaombea uongofu watu wa ardhi ile.

Katika kisa cha Habib an- Najjar, kinachosimuliwa katika Surat Yasin ndani ya Qur'an, pindi mapazia ya dunia hii yalipofungwa kwake, na pazia la utukufu kufunguliwa kwake, alionyesha huruma kwa wale waliompiga mawe kwa kusema:

**"Akaambiwa: Ingia Peponi! Akasema: Laiti watu wangu wangeli jua. Jinsi Mola wangu Mlezi alivyo nisamehe, na akanifanya miongoni mwa walio hishimiwa"** (Yasin, 36:26-7).

Jambo hili linaonyesha huruma na upendo ndani ya moyo wa muumini ambaye alitaka uongofu juu ya watu wale wale waliomfanya afe shahidi.

❁

Abu al-Hasan Harakani anaonyesha hisia zake kuhusu udugu wa kiislamu kama njia ya kudhihirisha neema alizojaaliwa:

"Kama ingetokea mwiba umechoma kidole cha yeyote yule, kuanzia Turkestan mpaka Damascus, ingelikuwa kana kwamba kidole changu ndicho kilichochomwa. Na kama yeyote yule anagonga mguu wake kwenye jiwe, ni kana kwamba mguu wangu ndio ulioumia. Huwa nahisi maumivu yao. Kama kuna huzuni kwenye moyo wa mtu mwingine, basi moyo huo ni wangu".

❁

Sahl ibn Ibrahim, anatoa mfano mwingine wenye kustaajabisha kuhusu udugu wa kiislamu kama ifuatavyo:

"Nilikuwa na urafiki na Ibrahim ibn Ethem. Siku moja nikawa mgojwa mno. Ibrahim ibn Ethem alitoa kila alichokuwa nacho kwa ajili ya afya yangu. Kisha nikaanza kupata nafuu. Wakati fulani nilimuomba chakula ambacho nilikuwa na hamu nacho mno. Kwa kuwa hakuwa amebakiwa na chochote cha kunipa, aliuza kipando chake ili aniridhishe. Nilipopona kabisa tulihitaji ngamia twende mahali na hivyo nikamuuliza:

'Ewe Ibrahim, ngamia wako yuko wapi?'

Ibrahim ibn Ethem akajibu:

'Tulimuuza'. Kwa sababu afya yangu haikuniruhusu kutembea nilimuuliza:

'Sasa tutapanda nini?'

'Nitakubeba' alisema na kisha kunibeba mgongoni mwake kwa umbali wa vituo vitatu.

❁

Baada ya Istanbul kutwaliwa, Fatih Sultan Mehmed aliwauliza makasisi fulani waliokuwa wakweli ambao waliwekwa gerezani

katika utawala wa Byzantine, maoni yao na ugunduzi wao kuhusu dola ya Uthmainiyya. Wakamjibu kuwa wangeliweza kutoa maoni baada ya muda wa uchunguzi na upembuzi.

Makasisi wale walitembelea kila mahali, ili kutekeleza jukumu walilopewa. Siku moja asubuhi na mapema waliingia kwenye duka moja kwa ajili ya kununua kitu. Muuza duka akawaambia:

"Mabwana, tayari nishafanya mauzo yangu ya kwanza kwa siku ya leo. Nendeni mkanunue kwa jirani yangu pale ambaye ndio anaanza kuuza".

Tukio hili la udugu wa kiislamu likawashangaza...hatuwezi kuuonea wivu moyo mzuri kama huu, moyo uliotwaharishwa kutokana na faida za ibada na kumfikiria Muislamu mwenzake kama anavyojifikiria yeye mwenyewe.

❃

Kwa ufupi, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anataka waislamu wawe kama mikono miwili inayooshana. Urafiki wa kweli kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni pale ambapo watu wawili wanaishi katika moyo mmoja. Jukumu la udugu wa kiimani na maisha yale wanaofanya juhudi katika kuudumisha kwa ari na kujitolea litaendelea hata baada ya maisha yao ya kiwiliwili kupita. Wakati wote watakumbukwa kwa huruma. Kama muhajirina, answar na waumini wote waliofanya nyoyo zao kama misingi...

Katika siku hizi za usasa, jukumu muhimu kuliko yote la udugu ambalo litakuwa sababu ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu ni kuwatendea wema na kuwa na huruma juu wale wanaotafuta uongofu, kwa madhaifu, mayatima na wasiojiweza katika mandhari ya udugu uliojaa upendo.

### d. Kuvipenda viumbe vyote

Viumbe vyote vimeumbwa ili vimtumikie mwanadamu. Kila kitu kipo kwa ajili yake ili apate somo na amekabidhiwa yeye katika maisha haya ya dunia. Ndio maana ni jukumu la kimaadili kwa mwanadamu kuvipenda viumbe vyote.

Nyuki anaishi ili atoe asali yake kwa mwanadamu. Kondoo wanatumia maisha yao yote kwa ajili ya kutupatia nyama, maziwa, sufi na ndama. Pia paka na mbwa wanamtumikia mwanadamu. Kama udhihirisho wa utukufu wa Mwenyezi Mungu na uzuri wake, nyoka, tandu, nge na viumbe wengine kama hao ni kwa ajili ya kutukumbusha juu adhabu ya Mwenyezi Mungu na pia wana majukumu mengine mbalimbali katika ulimwengu. Hivyo wao pia ni neema aliyopewa mwanadamu. Mawe, udongo, miti, mawingu, milima na malisho vyote viliumbwa kwa ajili ya mwanadamu...

Qur'an tukufu inatueleza:

"**Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri**" (Al-Jathiyya, 45:13).

Kuvikandamiza viumbe ambavyo viliumbwa kwa ajili ya kututii sisi ni upumbavu ambao utakuja kutuletea madhara. Kuwa wakatili kwa wanyama ni dhambi kubwa ambayo itatupelekea kuwajibika siku ya kiama.

Qur'an tukufu inatueleza:

"**Na hapana mnyama katika ardhi, wala ndege anaye ruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha kwa Mola wao Mlezi watakusanywa**" (Al-Anam, 6:38).

Kwa upande mwingine, kuvipenda viumbe vyote kwa kuwa wao ni zao la Muumba, ni jukumu la lazima kwa mja.

Viumbe wengine wana haki katika dunia hii na neema zake. Kuvunja haki zao kutasababisha kuwajibika kwa hali ya juu siku ya kiama.

Mshairi aitwae Firdawsi anasema yafuatayo katika shairi lake linalojulikana kwa jina la *Shahname*:

*'Usimjeruhi hata sisimizi aliyebeba kipande cha ngano. Kwani hata yeye ana uhai. Na uhai ni mtamu na wenye kupendeza'.*

Mtume Muhammad ﷺ amekataza bila sababu yoyote ile kuwaua wanyama kwa ajili ya kujifurahisha. Ameyasema haya katika *hadith* ifuatayo:

*"Yeyote anayemuua shorewanda kwa ajili ya kujifurahisha atamsikia huyo shorewanda siku ya kiama akilia kwa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:*

*'Ewe Mola wangu! Fulani aliniua bila sababu yoyote, wala kwa ajili ya faida yoyote'* (Nasai, Dahaya, 42).

***Matukio ya wema***

Abdullah ibn Mas'ud رضي الله عنه anasimulia:

'Siku moja tulikuwa katika safari pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kisha akatuacha kwa ajili kwenda kukidhi haja zake. Wakati ule tukamuona ndege akiwa na makinda yake mawili. Tukayachukua makinda yake na kisha yule ndege akaanza kurukaruka huku akilia kwa sauti. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliporudi na kuliona jambo lile akasema:

*'Yeyote aliyeyachukua makinda ya ndege huyu dhaifu na kumtesa ayarudishe mara moja'* (Abu Dawud, Jihad, 112/2675, Adab 163-4).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa amekaa pamoja na maswahaba zake, mtu mmoja alimsogelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ huku akiwa na kitu amekifunika mikononi mwake, na kisha akamwambia Mtume:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Nilipokuwa njiani kuja kwako nilipita kwenye miti mingi na kusikia makinda yakipiga kelele. Nikayachukua upesi na kuyafunika na nguo yangu. Kisha mama yao akaja na kuanza kurukaruka juu yangu. Niliyafungua yale makinda kisha mama yao akaja na kukaa nao pale. Kisha nikayafunika tena na kuja nayo kwako".

*"Yarudishe mara moja"*, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuamuru. Kisha yule mtu akayarudisha. Na yule mama yao badala ya kukimbia kimbia na kuyaacha peke yao akawa anakaa nayo. Baada ya kuyaona haya, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akawauliza maswahaba zake:

*"Mnashangazwa na upendo wa huyu mama kwa makinda yake, si ndio?"*

"Ni kweli ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", walijibu. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Ninaapa kwa Mtukufu ambaye amenituma kuleta ukweli, kwamba huruma ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake ni kubwa kuliko huruma ya ndege kwa makinda yake. Yachukue na uyarudishe ulipoyakuta ili yawe pamoja na mama yao"*.

Swahaba akayarudisha upesi (Abu Dawud, Janaiz).

❀

Siku moja Aisha رضي الله عنها alimpanda ngamia aliyekasirika. Alijaribu kumtuliza kwa kumpeleka mbele na nyuma kwa njia isiyokuwa nzuri. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia:

*"Kuwa mpole kwa mnyama. Kwani kokote utakapopatikana, upole utafanya kila kitu kuwa kizuri. Jambo lolote lisilo la upole ni baya"* (Muslim, Birr, 78, 79).

❁

Katika mfano mzuri ufuatao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anaelezea namna ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu kwa kupitia hata amali ndogo kuliko zote:

*"Wakati fulani mtu mmoja aliyekuwa anatembea njiani alishikwa na kiu. Akaona kisima na kuingia na kunywa maji, kisha akatoka. Alipotoka tu akamuona mbwa aliyetoa ulimi nje na huku analamba ardhi iliyokuwa na umaji maji kutokana na kiu. Yule mtu akajifikiria:*

*'Huyu mbwa ana kiu kama nilivyokuwa nacho'. Kisha moyo wake mwema ukaanza kumsuta. Moja kwa moja akaingia tena kisimani, Akajaza maji kwenye kiatu chake, akakiweka mdomoni na kupanda nacho juu kisha akamnywesha maji yule mbwa. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akapendezewa sana na kitendo cha mtu yule na kuamua kumsamehe madhabi yake yote".*

Maswahaba wakamuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Je tunapata malipo kwa matendo yetu juu ya wanyama pia?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijibu:

"Kuna malipo kuhusiana na viumbe vyote vyenye uhai" (Bukhari, Shurb, 9; Muslim, Salam, 153).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alienda kwenye bustani la mtu kutoka Answar na kumuona ngamia akiwa pale. Yule ngamia alipomuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaanza kulia kwa uchungu na huku machozi yakimtiririka. Mtume ﷺ

akamsogelea yule ngamia na kuanza kumpapasa taratibu nyuma ya masikio yake. Yule ngamia akatulia. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza:

*"Huyu ngamia ni wa nani?"* Kijana mmoja kutoka Madina alimsogelea na kumwambia:

"Ngamia huyu ni wa kwangu ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuuliza:

*"Je humuogopi Mwenyezi Mungu? Mwenyezi Mungu amekupa huyu mnyama. Lakini amenilalamikia kuwa unamuacha na njaa na huku amechoka sana"* (Abu Dawud, Jihad, 44/2549).

❁

Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amewaonya watu kuhusu maongezi yasiyo ya msingi na kusababisha madhara pindi wanapokuwa wamewapanda wanyama wao.

*"Jihadharini na kutumia migongo ya wanyama kama mimbar zenu. Mwenyezi Mungu amewapa wanyama hao ili wawahudumie kwa kuwapeleka sehemu ambazo ni vigumu kwenu kwenda wenyewe. Na amewaumbia ardhi kwa ajili yenu ili muishi juu yake. Hivyo angalieni mahitaji yenu kwenye ardhi (yani shukeni juu ya migongo ya wanyama wenu na mpate mahitaji yenu chini)"* (Abu Dawud, Jihad, 55/2567).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitoka nje mapema asubuhi kwenda kujisaidia. Akamuona ngamia amepiga magoti kwenye mlango wa msikiti. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipopita tena sehemu ile katika nyakati za mchana akamuona tena yule ngamia kama alivyokuwa asubuhi. Akauliza:

*"Yuko wapi mmiliki wa ngamia huyu?"*

Walimtafuta mmiliki wa ngamia yule lakini hawakumpata. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikasirika kwa kumuona ngamia ameachwa akiwa na njaa na kiu kisha akasema:

*"Muogopeni Mwenyezi Mungu na msimtese mnyama huyu dhaifu ambaye hawezi kutoa sauti na kulalamikia shida zake. Wapandeni wanyama hawa pale tu watakapokuwa imara, wenye nguvu na wameshiba".* (Ahmad, IV, 181).

❁

Sahl ibn Amr ؓ anasimulia:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipopita karibu na ngamia ambaye amenyonyoka manyoya ubavuni mwake kiasi kwamba mifupa yake inaonekana, akasema:

'Muogopeni Mwenyezi Mungu juu ya wanyama hawa ambao hawawezi kuongea. Wapandeni pale wanapokuwa wameshiba, na waleni pale wanapokuwa wameshiba" (Abu Dawud, Jihad 44/2548).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuona mtu akimchinja kondoo. Baada ya kumlaza kondoo chini kwa ajili ya kumchinja, yule mtu akaanza kunoa kisu chake (mbele ya yule kondoo). Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuonya yule mtu kuhusu jambo hili baya na kutojali:

*"Je unataka kumuua huyu kondoo tena na tena? Je hukuweza kunoa kisu chako kabla ya kumlaza chini?"* (Hakim, IV, 257, 260/7570).

❁

Siku nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipita mahali na kumuona mnyama aliyekuwa amewekwa alama usoni mwake kwa kuchomwa, kisha akasema:

"Mwenyezi Mungu amlaani yule aliyemuweka alama mnyama huyu usoni mwake" (Muslim, Libas, 107).

❁

Siku moja wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaenda Makka, aliiacha Madina katika hali ya *ihram*[20]. Akawasili mahali paitwapo Usaya, ambayo ni sehemu kati ya Ruwaysa na Arc. Hapa alimuona swala amejikunja na kulala kivulini. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaamuru maswahaba zake wasipumzike muda mrefu mbele ya yule swala wasije wakamkosesha uhuru na kumtia wasiwasi (Muwatta, Hajj, 79; Nasai, Hajj, 78).

❁

Wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na maswahaba zake wanaenda kuitwaa Makka walionyesha mfano mwingine wa kustaajabisha wa namna ya kuishi na wanyama. Pia jambo ni udhihirisho wa kuwaangalia wanyama kama Mwenyezi Mungu anavyoridhia. Alipokuwa akisafiri kutokea Arc kwenda Talub akiwa na jeshi la askari elfu moja, alimuona mbwa aliyekuwa amejinyoosha kwa ajili ya watoto wake ambao wananyonya. Upesi akamuita Juayl ibn Suraka kutoka kwa maswahaba zake na kumuweka amlinde mbwa yule pamoja na watoto wake. Akaonya jeshi hili la waislamu lisije likamtisha mama wala watoto wake (Waqidi, II, 804).

❁

Mfano mwingine wenye kuonyesha uangalifu unaochukuliwa juu ya wanyama unasimuliwa na Anas ibn Malik ambaye alikulia chini ya uangalizi wa Mtume.

"Pindi tuliposimama mahali kwa ajili ya kupumzika, kwanza tulishuka juu ya ngamia na kuwaacha wapumzike na kutulia kabla

20. Ihram ni hali ya maandalizi kwa ajili ya kutekeleza ibada ya hijja kwenye Al-Kaaba (Maelezo ya mfasiri).

ya kuanza kumtukuza Mwenyezi Mungu (kwa kuswali swala zetu za faradhi) na kufanya ibada nyingine" (Abu Dawud, Jihad, 44/2551).

Wanachuoni wa kiislamu wamekubaliana kuwa pindi msafiri anapopumzika, hana budi kuwalisha wanyama wake kabla ya yeye mwenyewe kula na wamefikia kusema kuwa jambo hili ni *mustahab* (kitendo chenye kulipwa) (Abu Dawud, Sunan, III, 51).

❁

Siku moja ibn Omar ﵄ alipita mahali walipokuwa vijana wa kiquraysh ambao wanamrushia ndege mishale. Walipomkosa walikuwa wakimlipa fedha mwenye ndege yule. Wale vijana walipomuona ibn Omar walisambaratika. Ibn Omar akawapigia kelele:

"Ni nani aliyefanya kitendo hiki? Mwenyezi Mungu amlaani. Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimlaani yeyote anayemchukua mnyama na kumfanya kuwa shabaha yake na kumpiga" (Bukhari, Dhabaih, 25; Muslim, Sayd, 59).

❁

Bayazid Bistami alikuwa mfasi wa moyo na mnyenyekevu kutokana na uzito wa mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu yaliyompelekea kuhisi maumivu ya viumbe vyote ndani ya moyo wake.

Siku moja rafiki huyu wa Mwenyezi Mungu alimuona punda akitokwa na damu nyuma yake kutokana na kupigwa. Wakati ule damu ikaanza kuvuja kwenye miguu ya Bayazid Bistami.

Wakati mwingine alipokuwa safarini, rafiki huyu wa Mwenyezi Mungu alipumzika chini ya mti na kisha akaendelea na safari yake. Alipokuwa njiani aliwaona sisimizi wachache waliotoka kwenye ile sehemu aliyokuwa amepumzika wakitembea kwenye mabegi yake. Ili kutowatenganisha na makazi yao mapya na kuyapotea, aliwarudisha wote ndani ya begi. Kisha akarudi pale

mahali alipokuwa amepumzika na kuwaweka sisimizi wale katika makazi yao ya mwanzo.

❀

Rafiki mkubwa wa Mwenyezi Mungu aitwae Shah-i Nakshibend, anatuambia mfano wake mzuri juu ya tabia yake kwa wanyama:

Katika masiku yangu ya mwanzo ya utafutaji, nilikutana na mmoja wa waja wa Mwenyezi Mungu waliokuwa vipenzi vyake aitwae Emir Kulal. Wakati ule nilikuwa katika mapenzi makubwa na Mwenyezi Mungu. Aliniambia:

"Tazamia katika kupendwa na watu. Wahudumie wanyonge na madhaifu. Walinde wanyonge na waliokata tamaa. Wao ni watu wasio na kipato kutoka kwa watu wengine. Wakati huo huo wanabakia katika hali ya kuridhika nyoyoni mwao, wanakuwa na staha na unyenyekevu. Watafute watu hao.

Nilitii amri hii ya mtu huyu mwema. Nilifanya juhudi juu ya kile alichoniambia kwa muda mrefu. Baada ya pale rafiki yule wa Mwenyezi Mungu akaniagiza nitafute wanyama kisha niwatibu magonjwa yao. Akanishauri kufunga majeraha yao na kuyasafisha. Pia akaniusia kuyafanya haya yote kwa nia safi na moyo safi.

Nikalitekeleza jukumu hili pia. Nilifanya kila alichoniambia katika namna ile ile aliyoniambia. Baada ya muda nilifikia katika hali ambayo pindi nikimuona mbwa barabarani ninasimama na kumpisha apite na kamwe sipigi hatua kumtangulia".

Kisha akaniagiza nikae na mbwa kwa upendo na heshima ili nipate radhi za Mwenyezi Mungu kwa kupitia huduma hii. Aliniambia:

"Utakuwa na furaha kubwa wakati unawahudumia mbwa hao".

Niliyachukulia maagizo yake kama bahati kubwa kwangu. Niliweka juhudi yangu yote katika kuyafuata. Nilielewa maana ya maagizo yake na nikawa nasubiria bishara njema ambayo ingelikuja. Nilienda kwa mbwa mmoja miongoni mwao. Nilipatwa na hali ya ajabu. Niliposimama mbele yake, kuna kitu kikanifanya nilie. Ilikuwa kana kwamba mbwa yule alikuwa ni Qitmir wa watu wa pangoni...

Wakati ninatokwa na machozi alilala chini na huku amenyanyua miguu yake inaelekea angani. Kisha akaanza kutoa sauti za huzuni na kuanza kulia na kunung'unika. Nikanyanyua mikono yangu ili niombe na kisha kwa unyenyekevu na udhalili nikasema:

"Amin". Kana kwamba alinielewa, yule mbwa akanyamaza na kuondoka.

Ilikuwa ni siku nyingine miongoni mwa masiku yale, niliondoka nyumbani na kwenda mahali. Njiani nilimuona mnyama ambaye rangi yake ilikuwa ikibadilika kutokana na rangi ya jua. Alikuwa katika raha ya kiimani isiyoonekana. Matokeo yake nikapatwa na hali ya raha isiyo na kifani. Nikasimama mbele yake kwa adabu na heshima kisha nikanyanyua mikono yangu. Wakati ninafanya vile yule mnyama aliyebarikiwa akawa anabadilika kutoka hali moja hadi nyingine, huku akiwa amezama kwenye ulimwengu mwingine. Kisha akalala chini huku uso wake umeelekea angani. Wakati yuko katika hali hii nikasema:

"Amin".

❁

Siku moja Sultani Suleiman aliulizia fatwa (hukumu ya kisheria) kutoka kwa Shaykh al-Islam, Abu as-Suud ili awaue sisimizi waliokuwa wakimaliza mipea ndani ya bustani la kasri. Ombi lake lilikuwa kama ifuatavyo:

Je itakuwa sawa kuwaua sisimizi ambao wanaharibu miti?

Abu as-Suud alijibu ombi la fatwa kwa aya ifuatayo:

"Kesho wakisimama mbele ya mahakama ya Mwenyezi Mungu wataomba watendewe haki kutoka kwa Sulayman"

Sulayman Mkuu alikuwa ni kiongozi mwenye ufahamu mkubwa na uwezo, mwenye akili sana na kiongozi mwenye mpangilio katika mambo yake, mwanachuoni na alimu mashuhuri. Licha ya hayo yote lakini alisita kumchukulia hatua sisimizi kutokana na kufunzwa maadili ya hali ya juu.

❁

Pertevniyal Valide Sultan aliamuru msikiti wa Valide ujengwe ndani ya Aksaray Istanbul. Baada ya kifo chake, mtu mwema mmoja alimuona katika ndoto akiwa amefikia daraja zuri na kumuuliza:

*"Je ni kwa sababu ya msikiti uliojenga ndio maana Mwenyezi Mungu amekupandisha daraja?"*

Pertevniyal Valide Sultan alijibu:

"Hapana".

Yule mtu mwema akamuuliza kwa mshangao:

"Kama ni hivyo basi ni amali gani ilikupelekea kufikia daraja hilo?"

Valide Sultan akatoa jibu lifuatalo:

"Ilikuwa ni siku yenye mvua kubwa. Tulikuwa tunaenda kuutembelea msikiti wa Ayyub Sultan. Nilimuona mtoto mdogo wa paka mwenye manyoya mengi akihangaika ndani ya kidimbwi kidogo cha maji pembezoni mwa barabara. Nilisimamisha gari letu la farasi na kumwambia mtumishi wa kike aliyekuwa karibu yangu:

"Nenda ukamchukue yule mtoto wa paka vinginevyo atakufa"...

Kwa kutotaka kwenda kumchukua alimuambia:

"Ewe Sultani wangu! Nguo zangu na zako zitapakwa matope".

Sikutaka kumpinga hivyo nikashuka kwenye gari, nikatembea kwenye matope na kwenda kumuokoa yule mtoto wa paka. Alikuwa akitetemeka kwa baridi. Nilimuonea huruma sana, nikamchukua na kumpakata ili apate joto. Baada ya muda mfupi kiumbe yule dhaifu akarudi kwenye uhai na kurudia katika hali yake ya kawaida.

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amenijaalia kuwa katika daraja hili tukufu kutokana na hicho kitendo changu kidogo cha huruma niliyoinyesha kwa yule mtoto wa paka.

Wakati mwingine jambo dogo la wema na lisilo na umuhimu linaweza kuvuta huruma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kiasi kwamba ikawa ndio sababu ya kupata fadhila kubwa na rehema. Ndio maana mwanadamu hana budi kutoona hana sababu ya kufanya jambo la wema kutokana na udogo wake. Siku zote mwanadamu ni mhitaji, katika dunia hii na kesho akhera, anahitaji rehema za Mwenyezi Mungu zinazotokana na matendo mema, yawe makubwa au madogo.

❁

Baba yangu, Musa Topbash Efendi (roho yake itakaswe) anasimulia tukio lifuatalo linalohusu kufanya urafiki na viumbe vyote:

Kama miaka 40 iliyopita hivi tulipanga chumba ndani ya Madina pamoja na kiongozi wangu wa dini, Sami Ramazanoglu (roho yake itakaswe). Wakati ule nyumba zilikuwa zikijengwa kwa matofali yaliyokaushwa na jua. Tulikuwa tumeandaa chumba cha kiongozi wangu kwa ajili ya kupumzikia. Alipoingia tulimuona

nyoka amejikunja kwenye kona ya chumba. Kinyume na matakwa yetu tulichanganyikiwa na kuingiwa na hofu. Hata hivyo alikuwa ametulia.

"Mwacheni huyu kiumbe wa Mwenyezi Mungu na msimguse" akatuambia.

Baada ya muda mfupi tukaona yule nyoka ametoweka.

❁

Musa Efendi (roho yake itakaswe) anasimulia:

"Ilikuwa ni kipindi cha hijja. Tulikuwa pamoja na kiongozi wangu wa dini Sami Efendi na familia yake ndani ya Makka, karibu na msikiti wa Baytullah, ndani ya nyumba ya Abdussettar kutoka Turkestan, katika kitongoji cha Ajyad. Chumba cha Sheikh kiligeukia mtaa, wakati vyumba vyetu vilikuwa ni vya ndani. Wakati fulani mchana alikuja kwenye mlango wa chumba chetu na kusema:

"Inaonekana nje kuna mtu anahitaji chakula".

Upesi nikaandaa chakula na kutoka nacho nje ili nimpe masikini lakini nilipotoka nje sikumuona mtu yeyote. Nikachukulia kuwa hakusubiri sana akaondoka, nikageuka na kuingia ndani. Dakika nane au kumi baadae Sami Efendi (roho yake itakaswe) akaja tena mlangoni mwetu na kusema:

"Yule mhitaji amerudi tena na anasubiria".

Nilipoandaa tena chakula na kwenda mlangoni sikumkuta mtu yeyote bali mbwa aliye na njaa, ulimi wake ukiwa umening'inia nje na huku amekaza macho. Mara moja nikakiweka kile chakula chini mbele yake. Atakuwa alikuwa na njaa mno kwani alikimaliza chote".

Hii ni neema na staha ya watu hao wema. Sami Efendi hakutumia neno ‘mbwa’ bali ‘mtu’ kwa yule mbwa aliyekuwa na njaa. Wakati mwingi hakutumia neno ‘kiumbe’ alipokuwa anazungumzia juu ya wanyama, bali hutumia neno ‘mja wa Mwenyezi Mungu’. Kwani mwenendo mzuri wanaouonyesha kwa Muumba wao ni wa kweli, na huwa na moyo mzuri, moyo ambao umetii kikamilifu na kujitolea kwa ajili ya Muumba wake.

❁

Dini yetu tukufu ya Uislamu inatutaka tuvitendee wema viumbe vyote, vilivyo hai na visivyo hai, katika kila nafasi na kwa namna yoyote ile. Faini mbalimbali zimewekwa kwa baadhi ya matendo unapokuwa ndani ya mipaka mitukufu ya Makka au unapokuwa katika *ihram*[21], matendo yenyewe ni kama vile kukata miti, kung’oa mimea yoyote ile au magugu, kuwinda, na hata kumuonyesha muwindaji lilipo windo. Kwa namna hii ni kwamba haitakiwi kwa waumini wanapokuwa ndani ya mipaka mitukufu kuifanyia mimea na viumbe vingine vyote hata dhambi ndogo kuliko zote na kufikia katika hali ya ‘kutodhuru chochote’ kwa upana wa neno lenyewe.

Kwa kupitia mafunzo mbalimbali yaliyopatikana katika kipindi chote cha Hijja, muumini hufikia katika hali ya uchamungu kiasi kwamba atafikia mahali atajitenga na namna zote za uharibifu, dhambi na mabishano. Hataweza kung’oa hata magugu. Pindi wote wanawake na wanaume watakapotekeleza matendo yote ya hijja yakiwemo tawaf (Kuizunguka al-ka’bah), sa’y (kutembea mara saba kati ya vilima vya Safa na Marwa) na wakfa (kusimama katika vituo kadhaa), watahifadhiwa kutokana na madhambi, uharibifu na mabishano na kuendelea kuinamisha macho yake...

21. Ihram ni jina linalowakilisha mashuka meupe yanayovaliwa na mahujaji wakati wa hijja. Pia ni hali ambayo mahujaji kuanzia pale wanalazimika kufuata kanuni maalum katika mipaka mitakatifu. (Maelezo ya mfasiri).

Umakini huu katika Uislamu hauishii tu ndani ya mipaka mitukufu na katika hali ya ihram. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema:

"Mwenyezi Mungu ataweka motoni kichwa cha yeyote yule atakayekata mti wa sidr" (Abu Dawud, Adab, 158-9/5239).

Abu Dawud alipoulizwa kuhusu *hadith* hii alitoa jibu lifuatalo:

"*Hadith* hii imefupishwa na maana yake ni: Mwenyezi Mungu ataingiza motoni kichwa cha huyu afuatae: yeyote atakayekata mti wa sidr bila haki mti ambao kivuli chake kinawanufaisha wasafiri na wanyama katika vilima na vitongoji".

❁

Tukio lifuatalo lina mafunzo muhimu kwa ajili yetu sote. Linaonyesha namna mapenzi na kujali kunakotokana na Uislamu kunavyosambaa kwa wanadamu, wanyama na hata mimea:

Siku moja Abu ad-Darda ﵁, ambaye ni mmoja wa maswahaba wakubwa, alipokuwa katika harakati za kupanda miti ndani ya Damascus. Mtu mmoja aliyemuona akifanya vile alimsogelea na kusema yafuatayo kwa mshangao:

"Licha ya kuwa unajinadi kuwa rafiki wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, lakini umeshughulishwa na kupanda miti". Abu ad-Darda alitoa jibu lifuatalo:

"Subiri kidogo. Usifanye haraka kunihukumu! Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema:

"Yeyote atakayepanda mti ambao watu na viumbe wengine wa Mwenyezi Mungu watakula matunda yake, mti huo utachukuliwa kuwa sadaka" (Ahmad, VI, 444).

Bila shaka, tofauti na hili, kuidhuru mimea na viumbe vingine ni jambo linalozalisha dhambi yake lenyewe. Mababu zetu

wamelidhihirisha jambo hili vizuri mno kama ifuatavyo: 'yeyote anayekata mti ulio hai ni sawa na yule anayekata vichwa vya watu'.

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwashauri watu wapande miti na kufanya mazingira yao kuwa kijani. Alikuwa ni mfano wa kuigwa kwa maswahaba zake. Ibn Abbas ؓ anasimulia:

Siku moja wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anapita karibu na makaburi mawili alisema:

"Wote wawili wanaadhibiwa, lakini si kwa sababu ya dhambi waliyoiona kuwa kubwa machoni mwao. Bali mmoja anaadhibiwa kwa kuwasengenya watu, na wa pili kwa kutochukua tahadhari ya kujiepusha na cheche za mkojo wakati wa kujisaidia".

Kisha akaagiza aletewe tawi angavu la mtende, kisha akalivunja mara mbili na kulipanda kila moja kichwani mwa kila kaburi. Kisha akaendelea kusema:

"Natumaini haya yatawapunguzia baadhi ya adhabu, hali ya kuwa hayajakauka" (Muslim, Taharah, 111).

Hata jani angavu liko katika hali ya dhikr (kumkumbuka Mwenyezi Mungu) ingawa sisi hatujui hilo. Qur'an tukufu imetueleza:

"**Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye maghfira**" (Isra, 17:44).

❁

Kwa kifupi ni kwamba, wakati mwingine radhi za Mwenyezi Mungu zinaweza kupatikana katika jambo kubwa, la wastani au wakati mwingine zinaweza kufichwa katika amali ndogo kuliko

zote. Ni hivyo hivyo kwa adhabu zake. Hivyo hatuna budi kuviendea viumbe vyote vya Mwenyezi Mungu kwa upole, huruma na upendo na kukimbilia kuwasaidia wanapohitaji msaada.

Uislamu unatuamuru kuvifanyia wema na kuvipenda viumbe vyote hai,yani wanadamu, wanyama na mimea. Mwanadamu ana jukumu kwa kila kimoja wapo. Uzuri wa Uislamu ni kuelewa upendo na huruma inayohitajika kwa viumbe vyote. Muislamu ni kama mto mrefu uliobeba baraka kwa viumbe hai elfu moja na moja- wanyama, miti, waridi na kinega. Unapoelekea na katika maisha ya milele na katika bahari ya ukutanishi (*wuslat*).

Ilivyo vigumu kwa jua kutotoa joto ndivyo ilivyo kwa roho za watu wema kutohisi chochote kwa viumbe vingine. Huruma ni hazina tukufu iliyosambazwa ulimwenguni kote. Na chanzo cha huruma na upendo ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wale wasio na huruma ni kama wale waliopoteza ufunguo wa hazina kuu, yani mlango wa furaha.

Wale marafiki wa haki, ambao wamekipata chanzo cha upendo, yani Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, watabakia kuwa marafiki wa viumbe vyote daima. Hawatachukuliwa kuwa wamekufa bali uhai wao utaendelea hata baada ya kufa kwao. Rafiki wa Mwenyezi Mungu aitwae Yunus Emre analizungumzia jambo hili vizuri zaidi:

*Wamepiga adhana katika kifo cha Yunus*

*Lakini ni mwili tu ndio unaokufa, mpenzi wa kweli kamwe hafi...*

**2. Hofu na matumaini**

Moja ya sifa kubwa ya wale waumini ambao wamefikia kwenye ukamilifu wa imani zao ni hofu yao juu ya Mwenyezi Mungu, inayotokana na unyenyekevu na upendo wao kwake. Kiuhalisia

hofu juu ya Mwenyezi Mungu ni hofu na shauku anayokuwa nayo mja kuwa atapoteza mapenzi yasiyo na mwisho, furaha na za Mwenyezi Mungu, mambo ambayo Mola wetu anayo juu yetu. Ndio maana nyoyo za wale waumini walio makini ambao wamejizatiti katika imani zao, hutetemeka kwa shauku pale linapotajwa jina la Mwenyezi Mungu. Pia hali hii inazaa sifa nyingine kubwa, kama vile mahusiano sahihi na Mwenyezi Mungu, usafi wa moyo na *taqwa* (uchamungu). Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuambia katika Qur'an:

"**Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi**" (Al-Anfal, 8:2).

"**Na kila umma tumewafanyia mahala pa kuchinjia mihanga ya ibada ili walitaje jina la Mwenyezi Mungu juu ya vile walivyo ruzukiwa katika wanyama wa mifugo. Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu, Ambao, anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hutetemeka, na wanao vumilia kwa yanao wasibu, na wanao shika Sala, na wanatoa katika tulivyo waruzuku**" (Hajj, 22:34-35).

Pindi elimu, ufahamu na mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu yanapoongezeka kwa mtu, hali kadhalika hofu ya mtu huyo kwa Mwenyezi Mungu inaongezeka kwa namna hiyo hiyo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

"Ufahamu wangu juu ya Mwenyezi Mungu ni mkubwa kuliko wenu na mimi ndiye ninayemhofia Yeye zaidi" (Bukhari, Adab, 72: Muslim, Fadail, 127).

Siku nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliulizwa:

"Ni sauti ya aina gani na kisomo cha namna gani ambacho ni bora kuliko vyote pindi isomwapo Qur'an?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu:

*"Sauti na kisomo cha yule ambaye katika sauti yake mnahisi hofu ya Mwenyezi Mungu"* (Darimi, Fadail al-Qur'an, 34).

Wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu, hawaogopi chochote kingine. Hofu kwa Mwenyezi Mungu ni nuru ya furaha ndani ya nyoyo zao.

Waumini wanaomuogopa Mwenyezi Mungu ni wale ambao wanamfurahia Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anawaridhia. (Al Bayyina, aya 8). Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaalika waja kama hawa kwenye pepo mbili. (Al Rahman, 46).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Muumini ambaye ametokwa na machozi kutokana na kumhofia Mwenyezi Mungu, hata kama ni madogo kama nzi lakini yakaweza kulowesha mashavu yake, hatoingia motoni"* (Ibn Majah, Zuhd 19).

*"Yeyote anayetokwa na machozi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu hatoingia motoni mpaka maziwa yarudi kwenye ziwa la mama. Vumbi linalopatikana katika njia ya Mwenyezi Mungu na moshi wa moto wa Jahannam haviwezi kukutana kamwe"* (Tirmidhi, Zuhd, 8/2311).

*"Kuna matone mawili na alama mbili ambazo Mwenyezi Mungu anaziridhia zaidi ya kitu kingine chochote: Matone mawili ni machozi yanayodondoka kutokana na hofu juu ya Mwenyezi Mungu, na matone ya damu yanatoka katika njia ya Mwenyezi Mungu. Alama mbili ni alama anayoipata mtu kutokana na kupambana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na alama inayotokana na kutekeleza ibada za faradhi"* (Tirmidhi, Fadail al- Jihad, 26/1669).

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amewakaripia wale wenye nyoyo ngumu, ambao wamekosa hofu juu ya Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

"**Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi; kwani kuna mawe yanayo timbuka mito, na kuna mengine yanayo pasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huanguka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayo yafanya**" (Baqara, 2:74).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Ewe Mwenyezi Mungu, Ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyo na manufaa, kutoka kwa mtu asiyekuogopa (Wewe), kutoka kwa mtu ambaye kamwe hariziki, na kutokana na dua isiyojibiwa"* (Muslim, Dhikr, 73).

Yeyote asiyemuogopa Mwenyezi Mungu yuko chini kuliko wanyama na madini. Kwa upuuzi huo huo mababu zetu walisema: 'Muogope yule asiyemuogopa Mwenyezi Mungu'. Ukweli ni kwamba hilo ni shauri lao tu kuogopesha watu. Kutokana na nyoyo zao ngumu, kiza cha ujinga wao na ukosefu wa hisia haupatikani hata kwa viumbe visivyo na uhai.

Ni kweli kwamba kutokana na utukufu wa Mwenyezi Mungu, hata viumbe ambavyo vinachukuliwa kuwa havina uhai vinapitia kwenye hatua za kumhofia Mwenyezi Mungu. Ukweli wa jambo hili unaonekana katika aya ifuatayo:

"**Lau kuwa tumeiteremsha hii Qur'ani juu ya mlima, basi bila ya shaka ungeli uona ukinyenyekea, ukipasuka kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Na hiyo mifano tunawapigia watu ili wafikiri**" (Al-Hashr, 59:21)[22].

22. Malengo ya tamko hili ni kuonyesha umuhimu wa yaliyomo ndani ya Qur'an na ukubwa wa jukumu la mwanadamu ambaye ndiye ameshushiwa. Pia

Ndani ya moyo wa muumini hakuna budi kuwa na hofu itakayompelekea kupata radhi na mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kuepushwa na moto; na wakati huo huo kuwa na matumaini ya kupata msamaha na huruma yake isiyo na mwisho. Inamaanisha kuwa moyo wa muumini hauna budi kuzunguka kati ya hofu na matumaini. Hisia hizi za hofu na matumaini zinaelezewa kama *'bayn'al- hawfi wa al-raja'*, (kati ya hofu na matumaini). Muumini hana budi kuhifadhi usawa huu ndani ya moyo wake kwa kupitia swala za mara kwa mara, kutambua hali yake ya udhaifu na kutafuta ulinzi kwa Mwenyezi Mungu mpaka kifo kimfikie. Qur'an tukufu inatueleza:

"**Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha tengenezwa. Na muombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanao fanya mema**" (A'raf, 7:56).

"**Hao wanao waomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kwendea kwa Mola wao Mlezi - hata miongoni mwao walio karibu mno - na wanataraji rehema zake na wanaikhofu adhabu yake. Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi yafaa kutahadhari nayo**" (Isra, 17:57).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kama muumini angelijua kikweli kweli uzito na namna ilivyo adhabu ya Mwenyezi Mungu, kamwe asingeliweza kutumainia*

tunaweza kupata maana ifuatayo kutoka kwenye aya hiyo: Kama milima ingelipewa utambuzi kama wa mwanadamu, ungeliinama kwa unyenyekevu na hofu mbele ya nguvu na Ukubwa wa Allah na uwezo wake kuundesha ulimwengu, baada ya kuzitambua sifa zake. Kutokana na kutoridhika na hili ingelikuwa tayari kujipasua ili kumtumikia Allah. Kwa upande mwingine mwanadamu anazikana hisia za mzigo aliojitwisha mabegani mwake na anapoteza uhai wake bila manufaa yoyote.
Hivyo ili mtu apate hofu na mapenzi juu ya Allah hana budi kuuweka moyo wake mbali na madhambi na kuupamba kwa uchamungu.

*pepo. Na kama kafiri angelitambua kikweli kweli huruma ya Mwenyezi Mungu, basi asingeliondoa matumaini ya kuingia peponi"* (Muslim, Tawba, 23).

*"Pepo ipo karibu na kila mmoja wenu zaidi ya ilivyo kamba ya kiatu chake. Na moto viyvo hivyo"* (Bukhari, Riqaq, 29).

Hivyo njia ya kuelekea kwenye furaha na amani ya milele ni kuuweka moyo kwenye usawa kati ya hofu na matumaini juu ya Mwenyezi Mungu. Kwani mpenzi daima anahofia kumuumiza na kumpoteza kipenzi chake. Muumini pia hana budi kupoteza mapenzi ya Mwenyezi Mungu lakini daima atumaini kupata rehema zake.

***Matukio ya wema***

Anas ﵁ anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiiomba dua ifuatayo mara kwa mara:

*"Ewe mwenye kupindua nyoyo za watu. Jaalia moyo wangu ushikamane na dini yako".*

Siku moja nilimuuliza:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tumekuamini wewe na ujumbe uliokuja nao. Je una wasiwasi na sisi?" Alinijibu:

*"Ni kweli kabisa. Kwani moyo upo kati ya vidole viwili vya mwingi wa rehema. Anazipeleka anavyotaka"* (Tirmidhi, Qadr, 7/2140).

❀

Aisha ﵂ anasimulia:

Pindi aya ifuatayo iliposhushwa:

"...na wanaotoa walichonacho..." (Al-Mu'minun, 23:60-61).

Nilimuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu:

"Je aya hii inazungumzia mambo yaliyoharamishwa kama vile uzinifu, uwizi na kunywa pombe?". Akanijibu:

"Hapana, Ewe binti wa Siddiq! Kilichomaanishwa katika aya hii ni wale wanaoswali , wanaofunga na kutoa zaka lakini hawana yakini kuwa matendo yao hayo yatakubaliwa" (Tirmidhi, Tafsir, 23/3175; Ibn Majah, Zuhd, 20).

Muislamu hana budi kutoridhika na amali na mambo mazuri anayoyafanya. Hakuna njia nyingine ila kutafuta ulinzi katika rehema za Mwenyezi Mungu.

❁

Suhayl ibn Amr alikuwa mmoja wa wasemaji wa maquraysh. Alikuwa akiongea dhidi ya Uislamu katika kipindi ambacho mazungumzo ya ushawishi yalikuwa ni silaha muhimu sana. Mtu huyu alichukuliwa mateka katika vita vya Badr. Omar رضي الله عنه alimuambia Mtume:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Niruhusu niyatoe meno ya mbele ya Suhayl na kuuacha ulimi ukining'inia. Kuanzia hapo hatoweza kuongea maneno ya kukupinga mahali popote pale"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu:

*"Muache afanye hivyo ewe Omar! Siwezi kudhuru sehemu yoyote ya mwili wake kwa njia hii. Kama nikifanya hivyo, Mwenyezi Mungu ataruhusu na mimi nifanyiwe kitu hicho hicho ijapokuwa mimi ni Mtume. Usiwe na haraka, kwani siku moja anaweza kuja kutoa maneno ambayo utayasifu na kuridhika nayo"* (Ibn Hisham, II, 293).

Kitendo hiki cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kilikuwa ni somo juu ya ulazima wa kumhofia Mwenyezi Mungu na kuchukua tahadhari ya hali ya juu ya kutoghadhibikiwa naye.

Na jambo hilo lilitokea baada ya kifo cha Mtume, katika kipindi cha msukosuko ambapo watu walikuwa wakionyesha dalili za kuipa mgongo dini yao, Suhayl ibn Amr alitoa yale maneno adhimu ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyatolea habari miaka kadhaa iliyopita. Sehemu ya maneno yake ni kama ifuatavyo:

"...Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Ninajua kwamba dini hii itashinda hali ya kuwa jua na mwezi bado vinachomoza na kuzama..."

Pindi Suhayl ibn Amr alipomaliza hotuba yake, watu waliokuwa wanamsikiliza walitulia. Na pindi Omar رضي الله عنه aliposikia maneno haya ya Suhayl aliyakumbuka maneno ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na akashindwa kujizuia na kusema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Nashuhudia kwa mara nyingine tena kuwa wewe ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" (Ibn Hisham, IV, 346; Waqidi, I, 07; Beladhuri, I, 303-4; Ibn Abdulbarr, II, 669-71; Hakim, III, 318/5228).

❁

Kutokana na masimulizi ya Aisha رضي الله عنها, pale hali ya hewa ilipokuwa ya upepo mkali au angani palipoonekana mawingu meusi, uso wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ulikuwa ukibadilika rangi. Wakati mwingine alikuwa akisimama na kuyaangalia mawingu, wakati mwingine alikuwa akigeuka na kuingia nyumbani kwake na kutoka nje tena. Pindi mvua iliponyesha alikuwa na furaha sana. Alipoulizwa sababu ya haya matendo yake, alikuwa akisema kuwa ni kutokana na hofu yake kuwa adhabu iliyowater-

emkia watu wa Ad ingelikuja kwenye umma wake" (Muslim, Istiska, 14-16).

Huruma ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ juu ya umma wake ilikuwa ni kubwa kuliko huruma ya mama na baba kwa mtoto wao. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatujulisha jambo hili:

"**Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma**" (Tawba, 9:128).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema kuwa hakuna kiwiliwili kilichowahi kutishiwa kama yeye, wala kupata maumivu na madhara makubwa, wala kupatwa na njaa kali kama alivyopatwa yeye.[23]

Mahangaiko haya yalimpata ili kuwarudisha waja wa Mwenyezi Mungu katika njia yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakulalamika kuhusu chochote. Kutokana na yeye ni kwamba uongofu wa hata mtu mmoja ulikuwa ni bora zaidi kuliko kitu chochote ambacho juu yake jua linachomoza na kuzama. Alipigwa mawe kule Taif mpaka mguu wake ukaloa damu, lakini bado moyo wake ulitulia baada tu ya tukio lile mja mmoja wa Mwenyezi Mungu aliongozwa katika Uislamu.

❁

Abu Bakr as Siddiq رضي الله عنه anasimulia:

"Nilipokuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aya ifuatayo ilishushwa:

"**Si kwa matamanio yenu, wala matamanio ya Watu wa Kitabu! Anaye fanya ubaya atalipwa kwalo, wala hatajipatia**

23. Tirmidhi, Qiyamah, 34/2472

**mlinzi wala wa kumnusuru, isipo kuwa Mwenyezi Mungu**" (Nisa, 4:123).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniambia:

*"Ewe Abu Bakr! Naweza kukusomea aya iliyonishukia sasa hivi?"*

"Bila shaka ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!" nilijibu.

Alinisomea aya hiyo hapo juu. Nilihisi kana kwamba mgongo wangu umevunjika vipande viwili na kuungana tena, na kana kwamba nimepatwa na kifafa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniuliza:

"Una tatizo gani, nini kimekupata ewe Abu Bakr?"

Nilijibu, huku nikionyesha kukata tamaa:

"Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni nani kati yetu hajafanya uovu? Je ni kweli tutaadhibiwa kwa maovu tuliyoyafanya?".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akafafanua:

*"Abu Bakr! Wewe na waumini wengine mtaadhibiwa kwa makosa mliyoyafanya hapa duniani (kwa kukutana na magumu na matatizo mbalimbali), ili muweze kukutana na Mwenyezi Mungu mkiwa hamna dhambi. Kwa wengine matendo yao yatakusanyika na watapata adhabu zao siku ya kiama"* (Tirmidhi, Tafsir, 4/3039).

❁

Mfano ufuatao wenye kuonyesha hofu juu ya Mwenyezi Mungu kutoka Abu Bakr رضي الله عنه una somo kwa ajili yetu sote:

Siku moja Abu Bakr alitoka nje huku anga ikiwa haina mawingu. Akawa anaangalia angani, anaangalia maelfu ya vidhihirisho vya nguvu zilizokuwa zikionyeshwa kwa waja wa Mwe-

nyezi Mungu ili wapate mazingatio. Jicho lake lilikwama kwa ndege ambaye alikuwa ametulia kwenye tawi na huku analia kwa sauti nzuri. Abu Bakr akavuta pumzi, huku akiwa anamuangalia ndege kwa shauku alisema:

"Furaha iliyoje kwako ewe ndege. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ningelipenda kuwa kama wewe...Unatua katika mti, unakula matunda yake na kisha unaondoka. Bila ya wewe kuhesabiwa chochote na wala hakuna adhabu inayokusubiri.

Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, bora ningelikuwa mti pembezoni mwa barabara, nikisubiri ngamia kuja na kula matawi yangu na kunitafuna kabisa, kuliko kuwa mwanadamu ambaye nitawekwa mbele ya Mola wangu na kuhesabiwa" (Ibn Abi Shayba, VIII, 144).

❁

Siku nyingine Abu Bakr ؓ alipotea ndani ya fikra, akitafakari juu ya aya zinazozungumzia siku ya kiama, usawa wa mizani, peponi na motoni, malaika wakiwa katika safu, kukunjwa kunjwa kwa mbingu, milima kutawanywa, jua kufunikwa, na nyota kutawanywa. Kisha akasema yafuatayo huku akimhofia Mwenyezi Mungu:

"Vipi kama ningelitamani kuwa majani ambayo mnyama angelikuja na kunitafuna na hivyo nikatoweka kabisa". Wakati ule aya ifuatayo ikashushwa:

"**Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi atapata Bustani mbili**" (Al-Rahman, 55:46) (Suyuti, Lubabu an Nukul, II, 146; Alusi, XXVII, 117).

Maswahaba kamwe hawakukubali onyo lifuatalo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu litoke kwenye fikra zao:

"**Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu**" (Al- Imran, 3:102).

❁

Ijumaa moja Abu Bakr ﷺ aliwaendea watu na kuwambia:

"Kesho tujumuike pamoja kwa ajili ya kugawana ngamia ambao ni sadaka, hivyo mtu yeyote asije bila kuomba ruhusa kwanza".

Siku iliyofuata mwanamke mmoja akampa mumewe kamba na kumwambia:

"Chukua hii kamba na uende, nani ajuae huenda Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akatupa ngamia".

Pindi yule mtu alipofika mahali ambapo ndipo ngamia wanapogawanywa aliwakuta Abu Bakr na Omar na bila ya kuomba ruhusa akaingia. Abu Bakr alipomuona akamuuliza:

"Umefikaje hapa?" Kisha akachukua kutoka mkononi mwake na kumgonga nayo kidogo, kama onyo. Hata hivyo alijisikia vibaya mno baada ya pale. Baada ya ngamia wote kugawanywa alimuita yule mtu na kumrudishia kamba yake na kumwambia:

"Hii hapa, ichukue na unipige nayo kama nilivyokufanyia wewe".

Kisha Omar akasema:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa hilo haliwezi kufanyika. Usiache tukio hilo likaigwa na kufanywa kuwa tabia na wale watakaokuja baada yako". Abu Bakr akasema:

"Kama ni hivyo ni nani atakayeniokoa na ghadhabu za Mwenyezi Mungu siku ya kiama?".

Kisha Omar akampa ushauri ufuatao:

"Basi patana naye". Kisha Abu Bakr akamuagiza mtumishi wake amletee ngamia pamoja na nguo yake na kumpa yule mtu. Pia alimpa dinar tano. Kisha yule mtu akamsamehe Abu Bakr ﵁. (Ali al-Muttaki, V, 595-6/14058).

❁

Kulikuwa na kijana mmoja kutoka answar ambaye moyo wake ulikuwa umejawa na hofu ya moto wa Jahannam. Kila moto ulipokuwa ukitajwa alikuwa akianza kutokwa na machozi. Mara akajifungia nyumbani kwao na kuacha kutoka nje. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijulishwa juu ya suala hili na kwenda kumtembelea. Yule kijana alimuangalia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa shauku kubwa, upesi akanyanyuka na kwenda kumkumbatia Mtume. Roho yake ikatoka na hivyo akadondoka chini. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Muoshe ndugu yako na umvishe sanda. Hofu juu ya moto imepasua ini lake. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ambaye mikononi mwake anashikilia roho yangu, kuwa Mwenyezi Mungu amemlinda na moto. Yeyote anayetamani kitu atapata njia ya kukipata na yeyote anayehofia kitu ataepukana nacho" (Hakim, II, 536/3828; Ali al-Muttaki, III, 708/8526).

❁

Qasim ﵁ anasimulia:

"Kila nilipokuwa nikiondoka nyumbani kwangu nilikuwa nikisimama kwenye nyumba ya (ndugu yangu) Aisha na kumsalimia. Siku moja miongoni mwa masiku haya niliyoenda kwenye nyumba yake, alikuwa akiswali swala ya faradhi na huku anasoma aya ifuatayo:

"**Basi Mwenyezi Mungu akatufanyia hisani na akatulinda na adhabu ya upepo wa Moto**" (Al-Tur, 52:27).

Alikuwa anaswali huku amesimama na analia na kuirudia rudia hii aya. Nilisubiri mpaka nikachoka, hivyo nikaamua kwenda sokoni kununua mahitaji yangu. Nilipomaliza na kurudi, Aisha ﵂ bado alikuwa amesimama, anaswali huku analia" (Ibn al-Jawzi, Sifatu as-safwa, II, 31).

❁

Ibn Abi Mulayka amesema:

"Nilifanikiwa kuwaona maswahaba 30 wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Wote walihofia unafiki miongoni mwao. Hakuna hata mmoja wao aliyeweza kusema kuwa ana imani kama ya malaika Jibril na Mikail" (Bukhari, Iman, 36).

❁

Siku moja Abu Bakr alikutana na Handhwala na kumuulizia hali yake. Handhwala ﵁ akajibu kwa masikitiko makubwa na huzuni:

"Handhwala amekuwa mnafiki ewe Siddiq".

Abu Bakr akajibu:

"*Subhanallah* (Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu). Jambo gani hilo la kusema".

Handhwala akafafanua:

"Tukiwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anatukumbusha kuhusu mbingu na moto na inakuwa kana kwamba tunaiona kwa macho yetu. Hata hivyo pale tunapoondoka mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kurudi kwenye familia zetu na watoto wetu tunafungamana na dunia, tunasahau mengi miongoni mwa yale tuliyoyasikia. (na tunaondokewa na hali ya imani na mafanikio yanayopatikana katika maneno yake)".

Abu Bakr akasema:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, tupo katika hali moja".

Kutokana na hili tulinyanyuka kwa pamoja na kwenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwambia tatizo letu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatujibu:

*"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, ambaye mikononi mwake ameshikilia roho yangu, kuwa kama mngeweza kubakia katika hali mnayokuwa nayo mnapokuwa pamoja na mimi, na hivyo kuwa katika hali ya kuendelea kumkumbuka Mwenyezi Mungu wakati mmelala na kutembea basi malaika wangewapa mikono. Kisha akarudia maneno yafuatayo mara tatu:*

*"Ewe Handhwala! Wakati mwingine hivi, na wakati mwingine vile"* (Muslim, Tawba, 12).

Kama tulivyoona namna maswahaba wanavyojiwajibisha wenyewe kutokana na matendo yao. Licha ya magumu yote katika maisha yao, lakini shauku yao kubwa ilikuwa ni kulinda nyoyo zao zisidhoofike.

❁

Siku moja Omar ؓ alipokuwa anapita karibu na mtu mmoja alimsikia mmiliki wa nyumba akisoma Surat Tur kwa sauti ya juu. Yule mtu alipofikia kwenye aya isemayo:

"**Hakika adhabu ya Mola wako Mlezi hapana shaka itatokea. Hapana wa kuizuia**" (Al-Tur, 52:7-8).

Omar alishuka juu ya ngamia wake na kuweka sikio lake kwenye ukuta na kusikiliza. Baadae aliporudi nyumbani kwake alilala kitandani kwa muda, kutokana na kuwa mgonjwa kutokana na uzito wa onyo lililopo kwenye aya hii.[24]

❁

24. Ibn Rajab al-Hanbali, "al Takhwif min al Nar," Damascus, 1979, uk 30

Omar ﷺ amesema:

“Kama sauti ingetoka mbinguni na kusema: ‘Enyi watu. Mmoja wenu tu ndiye atakayeingia motoni’, ningelihofia kuwa mtu huyo anaweza kuwa mimi. Na kama sauti ingelisema: ‘Enyi watu. Ni mmoja wenu tu ndiye atakayeingia peponi’, ningelishangaa mtu huyo kuwa mimi”.[25]

Hii ni hali ya kiimani ya waumini, yani hali kati ya hofu na matumaini, ambayo imeamrishwa katika aya ifuatayo:

**“Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku”** (As-Sajda, 32:16).

❁

Siku moja Omar ﷺ alikuwa akifikiria kuhusu ugumu atakaokuwa nao wakati wa kujihesabu atakapokuwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Aliokota kipande cha jani kavu chini na kusema:

“Ah, bora ningelikuwa kipande hiki cha jani kavu, nikawa sipo hapa duniani. Bora mama yangu asingekuwa amenizaa, na hivyo nikasahaulika kabisa”. (Ibn Sa’d, III, 360-1).

❁

Siku moja Ali ﷺ aliulizwa:

“Ewe kamanda wa waumini. Ni kwa nini rangi ya sura yako inabadilika na unaanza kutetemeka pindi unapofika wakati wa swala?”.

Akajibu:

25. Ali al Muttaki, XII, 620/35916. Pia angalia Ibn Rajab al Hanbali, al Tahwif mina’n Nar, Damascus, 1979, uk 15.

"Huu ni wakati wa kulipa amana ambayo mbingu na ardhi vilishindwa kuichukua na milima kuonyesha udhalili wake. Sijui kama nitaweza kuitekeleza kwa usahihi".

❁

Uso wa mjukuu wa Mtume, Hasan, ulikuwa ukikwajuka kila anapochukua udhu. Siku moja mtu mmoja aliyemuona alimuuliza:

"Ewe Hasan, kwa nini uso wako unakwajuka na kuwa njano kila unapochukua udhu?"

Akajibu:

"Huu ni wakati wa kwenda mbele ya Mmiliki pekee wa nguvu, Mwenyezi Mungu aliye Mkuu na Mtukufu".

Pindi Hasan ﵁ alipokuwa akiingia msikitini alikuwa akiomba kama ifuatavyo:

"Ewe Mlezi wangu. Mja wako yuko mlangoni kwako. Ewe mwingi wa rehem. Mja wako mwenye madhambi amekuja kwako. Umewaamrisha waja wako wema wawasamehe wale waliowakosea. Kwa sababu Wewe ni mwingi wa msamaha na ukarimu. Ewe Mwenyezi Mungu. Nisamehe makosa yangu kwa huo huo msamaha na huruma yako na ujaalie rehema juu yangu".

❁

Abu Bakr Warraq alikuwa na mtoto mdogo ambaye alikuwa anajifunza Qur'an. Siku moja alirejea mapema kutoka darasani kwake, huku akiwa amekwajuka na kufadhaika, na huku anatetemeka. Abu Bakr alimuuliza kwa mshangao:

"Una tatizo gani mwanangu? Ni hali gani hii? Kwa nini umerudi mapema mno?"

Hofu juu ya Mwenyezi Mungu ilikuwa imejengeka kwa uimara ndani ya moyo mdogo wa mtoto huyu mdogo na kuacha uso wake umefifia na kupauka kama jani la vuli. Alijibu:

"Ewe baba! Leo mwalimu wetu alitufundisha aya kutoka katika Qur'an na pindi nilipoitafakari na kufahamu maana yake nilijikuta katika hali hii". Kisha baba yake akamuuliza:

"Ni aya gani hiyo?" Yule mtoto mdogo akaanza kuisoma:

"**Basi nyinyi mkikufuru, mtawezaje kujikinga na Siku ambayo itawafanya watoto wadogo waote mvi?**" (Al-Muzammil, 73:17).

Baadae mtoto yule akawa mgonjwa kutokana na tishio na hofu iliyotokana na aya hii. Akawa mgonjwa kitandani na baada ya muda mfupi akafariki. Baba yake aliguswa mno na tukio hili. Alikuwa akitembelea kaburi la mwanae mara kwa mara na kulia na kujiambia mwenyewe:

"Ewe Abu Bakr! Mwanao alijifunza aya katika Qur'an na kutokwa roho kutokana na hofu juu ya Mwenyezi Mungu. Wewe umekuwa ukiisoma Qur'an kwa muda wote huu lakini huogopi haki za Mwenyezi Mungu kama mtoto huyu".

Tukio hili linaonyesha uzito wa imani ya mtoto ambaye Mwenyezi Mungu ameweka upole na huruma moyoni mwake. Lakini pia linaashiria namna ambavyo tunahitajika kutafakari maneno Yake kwa moyo wa upole pamoja na hofu na shauku mbele ya Ukubwa wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea namna ambavyo tunaweza kufikia hali hii katika aya ifuatayo:

**"Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola wake Mlezi...Sema: Ati watakuwa sawa wale wanao jua na wale**

**wasio jua? Hakika wanao kumbuka ni watu wenye akili"** (Al-Zumar, 39:9).

Hivyo ujuzi wa kweli mbele ya Mwenyezi Mungu ni ujuzi ambao utampelekea mtu kumtambua na kumuogopa Mwenyezi Mungu. Yani ujuzi wa kweli ni ujuzi wa Mwenyezi Mungu. Ili kuupata ujuzi huo, aya hiyo hapo juu imetoa masharti matatu ambayo ni lazima yazingatiwe:

1. Kusimama usiku na kusujudu, hivyo kuweka ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya moyo.

2. Kukumbuka kifo na wakati wote kuwa katika hali ya hofu juu ya hesabu yako siku ya kiama katika kila hatua, kila wakati na katika kila kitendo chetu.

3. Kutumainia rehema za Mola wetu daima, na kuendelea kumuomba na kujikinga kwake. Watu wakubwa katika dunia hii wamekuwa wakiishi katika hali ya kuendelea kuomba dua.

❀

Mansur ibn Ammar anasimulia:

Usiku mmoja nilitoka nje nikifikiri kuwa kumekucha. Lakini nikagundua kuwa haikuwa asubuhi. Nilipokuwa ninapita karibu na nyumba ya mtu mmoja niliwasikia wakilia kwa huzuni na huku wakiomba dua ifuatayo:

"Mola wangu! Nimefanya madhambi mengi. Nimejiharibia maisha yangu. Lengo langu halikuwa kujaribu maneno yako. Bali nilijirudi *nafs* yangu. Na niliona kuwa chochote kibaya nilichokifanya, hukufanya chochote. Nilidanganywa na pazia lako. Niliten-da madhambi kutokana na ujinga. Sasa hivi najua kuwa nilifanya makosa. Ukiniadhibu nitakuwa katika hali gani? Ole wangu. Ewe Mola wangu. Siku utakapowaamuru waja wako wapite katika daraja la Sirat, baadhi yao wataangukia ndani ya Moto na baadhi

yao wataingia peponi. Sijui mja wako huyu mnyonge ataangukia katika kundi gani".

Wakati ule aya inayohusu Moto ilisikika. Kijana mmoja aliyekuwa pale ndani akasikika akikoroma na kisha hakuweza kusikika tena.

"Nastaajabu nini kimetokea?" nilijisemea. Nilipotambua ilikuwa ni nyumba gani nilirudi nyumbani. Niliporejea tena asubuhi yake nilikuta jeneza mlangoni.

Nilipoulizia kilichotokea mama yake aliniambia:

"Aliyekufa ni mwanangu. Anatoka katika ukoo wa Mtume. Ilipokuwa ikifika usiku alikuwa akiswali na kulia mpaka asubuhi. Alikuwa akitoa alichokipata mchana na kuwapa masikini. Alikuwa akisikia aya inayohusu Moto ikisomwa anashindwa kuvulimia na hivyo huanguka chini huku analia. Hivyo aliiaga dunia".

Nilimwambia:

"Mpendwa mama. Mwanao ameenda peponi. Kwani yeyote anayelia kutokana na kumhofia Mwenyezi Mungu hawezi kuingia Motoni. Vipi mtu huyu aliyetokwa roho kwa namna hii aingie Motoni? Mshukuru Mwenyezi Mungu".

❁

Yavuz Sultan Salim alikuwa Sultan aliyekuwa na hasira sana. Alikuwa akipandwa na hasira juu ya kosa au jambo lolote lililofanyika kwa uzembe. Hata hivyo uzuri wake ni kwamba hasira zake huyeyuka linapokuja suala la maamrisho ya Mwenyezi Mungu. Hofu yake juu ya Mwenyezi Mungu ilikuwa kubwa kuliko kitu chochote kile. Wakati fulani aliamuru watu arobaini wauawe ulipotokea wizi katika hazina kutokana na uzembe. Shaykh al-Islam, Zenbilli Ali Efendi alipopata taarifa ya jambo hili upesi alienda kwenye upande wa Yavuz ili azuie adhabu ile isitekelezwe bila ya

kupata ruhusa. Alisikiliza ukweli wa jambo lile kutoka kwa Sultan. Yavuz akajibu kwa ukali:

"Mheshimiwa. Ulichokisikia ni kweli lakini hata hivyo huna haki ya kuingilia kwenye masuala ya dola..."

Shaykh al-Islam, Zenbilli Ali Efendi, akamjibu kwa kiwango kile kile cha ukali:

"Sultan wangu. Nimekuja hapa kukujulisha hukumu ya kisheria. Kwa sababu jukumu letu ni kulinda maisha yako ya akhera".

Sultan Yavuz alitulia mbele ya mizani ya Uislamu, akawa mdogo kuliko unywele, na mwembamba kuliko upanga. Akasema:

"Je hakuna ruhusa ya kuua kundi moja ili kurekebisha tatizo kwa ujumla?"

Zenbilli Ali Efendi akajibu:

"Hakuna uhusiano kati ya kuwaua watu hawa na kuirekebisha jamii. Adhabu inayoendana na kosa lao ndiyo itakayosaidia..."

Sultan huyu mkubwa ambaye aliyadhibiti majeshi makubwa aliinamisha kichwa chake na kubadili maamuzi yake. Kutokana na kufurahishwa na jambo hili Zenbilli aligeuka kana kwamba anaondoka. akamwambia Yavuz ambaye alikuwa anaonekana ana shauku kubwa:

"Sultan wangu. Suala langu la kwanza lilikuwa ni kukufahamisha juu ya hukumu ya kisheria katika dini yetu. Nina suala lingine, lakini hili ni ombi tu..."

Kisha akaendelea:

"Sultan wangu. Wahalifu hawa wanawajibika katika uhalifu walioutenda. Lakini ni nani atakayesimamia familia zao zisizo na hatia wakati wakiwa jela? Ombi langu ni kwamba utenge posho

kwa ajili ya familia zao mpaka kifungo chao kimalizike". (Angalia, Mustafa Nuri Pasha, Netaij al-Wukuat, Ankara, 1987, uk 90-91).

Yavuz alikubali ombi hili la pili pia, bila shaka akiashiria utambuzi wake wa jukumu tukufu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

❁

Katika tukio lingine Zenbilli Ali Efendi alimuonya Sultan vile vile kama mwanzo. Lakini kwa kuwa Sultan alijiona yeye ndiye mwenye maamuzi alimwambia Shaykh al Islam yale yale aliyomwambia kipindi kilichopita:

"Si jukumu lako kuingilia masuala ya dola"

Bila kutishika Zenbilli Ali Efendi akajibu maneno haya ya kitisho kama ifuatavyo:

"Sultan wangu. Haya ni masuala ya kesho akhera hivyo tuna haki ya kuyaingilia. Kama hutengui maamuzi yako ya kimakosa basi jiandae na adhabu kali siku ya kiama..."

Baada ya kusema maneno haya Shaykh al Islam akageuka na kuondoka bila ya kuaga. Yavuz Sultan Selim, ambaye alikuwa anakaribia kuanza safari, alikuwa amekasirika kidogo kwani kamwe hakuwahi kuongeleshwa na mtu yeyote kama vile. Hata hivyo aliukubali ukweli na kuikubali tahadhari aliyopewa na Shaykh al Islam na hivyo alibadilisha maamuzi yake. Aliacha barua ya msamaha aje kupewa Zenbilli Ali Efendi.

Licha ya ukweli kwamba alikuwa Sultan wa dunia, hofu juu ya Mwenyezi Mungu iliyojikita moyoni mwake ilimzuia kufanya jambo kutokana na matamanio yake. Kwa upande mwingine hofu ya Sheikh juu ya Mwenyezi Mungu ilimpa ari kubwa na hivyo akaweza kuhatarisha kila kitu ili kuonya bila hofu juu ya Sultan mkali kama Yavuz.

❁

Mmoja wa mawaziri wa wakati ule alikutana na Sufi mkubwa aitwae Zunnun-i Misri na kumwambia:

"Tafadhali nisaidie. Nimeshughulishwa na kumhudumia Sultan usiku na mchana. Namtakia mema lakini nahofia atanifokea na kunikaripia".

Zunnun alitokwa na machozi na kumwambia:

"Kama ungelikuwa unamuogopa Mwenyezi Mungu kama unavyomuogopa Sultan huyu basi ungelikuwa umekubaliwa kuingia kwenye kundi la wakweli".

❁

Kwa ufupi 'Mwanzo wa mambo yote mazuri ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na msingi wa hekima ni hofu juu ya Mwenyezi Mungu'.

Yeyote anayemuogopa na kumfahamu Mwenyezi Mungu atakuwa muangalifu katika matendo yake, kwa hofu ya kutopoteza mapenzi yake na kutopata adhabu yake. Ataishi katika namna nzuri sana. Kama mja atamuogopa Mwenyezi Mungu kikweli kweli (kama anavyostahiki kuogopwa), ataonyeshwa muelekeo wa maisha yake chini ya blanketi la Uislamu na pia atakingwa kutokana na hofu za kidunia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kuna mambo matatu ambayo yatawanusuru watu: Hofu juu ya Mwenyezi Mungu, katika siri na dhahiri, kutenda haki katika nyakati za furaha na hasira, kuwa mchumi katika hali ya umasikini na utajiri. Mambo matatu yafuatayo yatampoteza mtu: mtu kuendeshwa na matamanio yake, ubahili na kutosheka na wewe mwenyewe"* (Munawi, III, 404/3471).

Kama tunataka amani ndani ya hii dunia na kesho akhera hatuna budi kumhofia Mwenyezi Mungu kwa namna anavyostahiki kuhofiwa. Pia hatuna budi kujikinga kwake wakati tumerukuu

na tumesujudu, kwa swala zetu na dua zetu, huku zinanyeshelezewa kwa machozi yetu na kutaraji rehema na msamaha wake.

**3. Tazim au unyenyekevu**

Tazim ni matokeo ya hisia fulani nzuri, kama vile taqwa (uchamungu), mapenzi, udhalili, kuthamini jambo zuri, na umakini wa moyo wenye imani. Msingi wa Uislamu unaweza kuelezewa kwa ufupi kwa fikra mbili zifuatazo:

a. *Tadhim li-amrillah* - kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa umakini mkubwa na heshima.

b. *Shafqat ala khalkillah* – kuwahurumia na kuwapenda viumbe wengine kulingana na kiwango cha ukaribu wao na Mwenyezi Mungu.

Jambo la kipaumbele kwetu ni kumnyenyekea Mwenyezi Mungu. Na alama kubwa na nzito katika hili ni kufanya ibada. Baada ya hapo ni kuwaheshimu watu kulingana na kiwango cha ukaribu wao na Mwenyezi Mungu. Qur'an tukufu inatueleza:

"**Ndio hivyo! Na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo**" (al-Hajj, 22:32).

Swala, Qur'an tukufu, adhana, kuchinja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na amana nyingine tukufu zikiwemo Al- Kaaba, vilima vya Safa na Marwa na sehemu nyingine takatifu, vyote hivi vinachukuliwa kuwa kanuni takatifu za Uislamu. Hatuna budi kuviheshimu bila kukosea, na kuviheshimu zaidi katika nyakati za Hijja na Umra (Hijja kubwa na ndogo). Kuikanyaga Al-Kaaba wakati umekaa au umelala na kuongea maneno ya upuuzi katika sehemu hizo takatifu, kusoma au kusikiliza Qur'an bila nidhamu au kuiweka chini, yote haya ni mambo mabaya ambayo yataathiri hisia za unyenyekevu wa mtu na hivyo hatuna budi kujiepusha nayo.

Mwenyezi Mungu (ambaye utukufu na ukuu ni wake) amewaahidi pepo wale wanaomheshimu Yeye, Mitume wake, watu wema na amana takatifu na pia anawamiminia rehema wakati wote. Mfano mzuri wa hili ni kwamba washirikina wa Makka hawakuadhibiwa kutokana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuwa nao[26].

Mfano mzuri wa faida kwa wale wanaoviheshimu vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu ni kisa cha wachawi wa Firauni kilichoelezewa ndani ya Qur'an. Pindi Firauni aliposhangazwa na miujiza iliyoonyeshwa na Musa عليه السلام, aliwakusanya pamoja wachawi wa Misri na kuwaahidi ujira mkubwa. Hata hivyo wale wachawi walipojaribu kushindana na Musa, walirudi nyuma kwa upole na kumpa heshima na kipaumbele yeye. Kitendo hiki cha upole walichomuonyesha Musa lazima kitakuwa kilimfurahisha Mwenyezi Mungu Mtukufu ndio maana wakati ule mbegu za uongofu zilizokuwa ndani ya nyoyo zao zikaanza kukua.

Miujiza iliyodhihirika baada ya pale ilikuwa sababu ya wao kuheshimiwa kwa imani zao. Na hii ilikuwa ni imani thabiti iliyowapelekea kutoa uhai wao bila ya majadiliano hata kidogo...

Katika kisa kifuatacho Jalaluddin al-Rumi anaelezea siri ya kuheshimu alama za Mwenyezi Mungu:

"Wale wachawi walikuja kuungana kutokana na adabu na heshima waliyoionyesha kwa Mtume yule Mtukufu, mja aliye karibu na Mwenyezi Mungu, kwa kumfaa kipengele cha kwanza.Hata hivyo wakati huo huo waliadhibiwa kwa kujaribu kushindana na Mtume yule Mtukufu ".

Tukio lingine maarufu ni ndoto ya Othman Gazi iliyotokana na heshima yake na unyenyekevu wake juu ya Quran tukufu. Ndoto hii ilitafsiriwa na sheikh Edebali ambaye baadaye alim-

26. Al Anfal, 8:33

wozesha binti yake. Hivyo ni sahihi kusema kwamba Dola ya Uthmainiyy, dola iliyotawala kwa muda mrefu duniani ilikuwa imejengwa juu ya misingi ya heshima, unyenyekevu, mapenzi, adabu na kuihudumia Qur'an.

Dola hii tukufu iliyopata nguvu kutokana na heshima kubwa iliyoweka juu ya Quran baadae ilikuja kusimamia amana takatifu na kuzihifadhi kwa heshima kubwa.Kwa kuongezea ni kwamba dola hii ilihudumia misikiti miwili mitakatifu ya Makka na Madina kwa heshima na kulingana na utukufu wake.

***Matukio ya wema***

Kutokana na masimulizi ya Abu Huraira ﵁, Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliona makohozi chini ndani ya msikiti wake yakiwa katika usawa wa Qibla. Akawageukia watu na kusema:

*"Mna matatizo gani baadhi yenu kiasi kwamba mnapomgeukia Mola wenu mnatema makohozi. Je kuna yeyote miongoni mwenu angelipenda mtu amgeukie na kumtemea usoni mwake?"* (Muslim, Masajid, 53).

❁

Pindi Junayd al-Baghdadi alipoenda kumtembelea mtu mmoja ambaye aliambiwa ni mchamungu, alimuona akitema kohozi kwenye uelekeo wa Makka. Akaondoka bila kumuona yule mtu kwani aligundua kuwa yule mtu si mwenye kufuata *Sunnah* (mwenendo wa Mtume).

❁

Kutokana na masimulizi ya Anas ﵁, kila wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoenda kujisaidia alikuwa akivua pete yake ambayo iliandikwa 'Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi

Mungu' kutokana na kumheshimu Mwenyezi Mungu (Abu Dawud, Taharah, 10/19).

❁

Katika kipindi cha Hijja wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ameelekea Al-Kaaba alinyanyua mikono yake na kuomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu. Nakuomba uongeze heshima, ukubwa na utukufu wa nyumba hii. Na pia nakuomba uongeze heshima, utukufu, unyenyekevu na wema kwa wale wanaoiheshimu katika kipindi cha Hijja kubwa na ndogo" (Ibn Sa'd, II, 173).

❁

Ndani ya Qur'an tukufu Mwenyezi Mungu anasema:

"**Na ngamia wa sadaka tumekufanyieni kuwa ni kudhihirisha matukuzo kwa Mwenyezi Mungu; kwa hao mna kheri nyingi. Basi litajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yao wanapo simama kwa safu. Na waangukapo ubavu kuleni katika hao na walisheni walio kinai na wanao lazimika kuomba. Ndio kama hivi tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu ili mpate kushukuru**" (al-Hajj, 22:36).

Hivyo wanyama waliochinjwa katika kipindi cha sherehe za Qurban pia nao ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Ndio maana hatuna budi kuonyesha heshima juu wa wanyama hawa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kama ilivyo katika ibada nyingine zote, hisia ya unyenyekevu na taqwa ndio yenye kuangaliwa. Ndani ya Qur'an tukufu Mwenyezi Mungu anasema:

"**Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamngu wenu. Namna hivi tumewadhalilisha kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyo kuongoeni. Na wabashirie wafanyao mema**" (al-Hajj, 22:37).

Tukio lifuatalo ni mfano mzuri wenye kuonyesha heshima iliyodhihirishwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa Mwenyezi Mungu juu ya wanyama waliochinjwa kwa ajili ya sherehe za Qurbani.

Waislamu walikuwa wamewasili Hudaybiya kwa ajili ya kutekeleza hija ndogo, hata hivyo washirikina waliwazuia kuingia Makka. Maswahaba walikuwa wamebeba wanyama wa kuchinja. Miongoni mwa wanyama hawa alikuwepo ngamia wa ukoosafu ambaye alichukuliwa kama ngawira katika vita vya Badr. Ngamia huyu alikuwa ni wa Abu Jahl na alikuwa na pete ya fedha katika pua yake. Pindi ngamia walipolazwa chini kwa ajili ya kuchijwa ngamia huyu alitoroka na kukimbilia Makka kwenye nyumba ya Abu Jahl. Amr Ibn Anema ﷺ alimfuata. Baadhi ya watu hawakutaka Amr amrejeshe ngamia yule na hivyo wakataka kutoa ngamia 100 ili kufidia ngamia huyu mmoja. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliposikia jambo hili alisema:

*"Kama tungelikuwa hatujaamua kumtoa kafara ngamia huyu tungelikubali ombi lenu"* (Waqidi, II, 64).

Hapa tunaweza kuona huruma na uvumilivu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na pia unyenyekevu aliouonyesha kwa Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndiye aliyekuwa na moyo laini kuliko watu wote. Haikuwa kawaida yake kukataa maombi ya halali ya watu. Hata hapa pia angelikuwa amekubali ombi la makafiri wale kama isingelikuwa heshima yake juu ya kanuni za Mwenyezi Mungu na dini yake ambavyo viko juu ya vitu vyote vingine. Ndio maana hakumtumia ngamia ambaye alikuwa ametolewa kuchinjwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa matumizi mengine.

Pia tunaweza kupata mazingatio kutokana na unyenyekevu ulioonyeshwa na marafiki wa Mwenyezi Mungu kuhusiana na kuchinja wanyama kwa ajili yake.

Shaykh Sami Efendi na marehemu Mûsa Topbas Efendi (Mwenyezi Mungu atakase nyoyo zao) walikuwa makini mno wanapokuja kwenye suala la kuchinja wanyama wao kwa ajili Mwenyezi Mungu. Walikuwa kamwe hawachinji wanyama wawili katika sehemu moja. Walikuwa wakiwaziba macho kabla ya kuwachinja. Hawakuruhusu wanyama wasukumwe na kukokotwa kwa nguvu kuelekea kwenye sehemu ya kuchinjiwa, kinyume chake kama mnyama alikuwa ni mdogo, walikuwa wakiomba abebwe vizuri na kwa upole. Walikuwa wakihakikisha kuwa kisu cha kuchinjia ni kikali. Pia walikuwa wakielekeza mnyama achinjwe kwa namna ambayo hataumia sana na damu iachwe itiririke yote. Walikuwa hawakai chini pindi mnyama anapochinjwa bali wakikuwa wakisimama mpaka damu yote itiririke chini.

Walifanya yote haya kwa sababu kuchinja mnyama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni moja wapo ya ibada ambayo nayo inahitajika kutekelezwa kwa umakini kama zilivyo ibada nyingine. Huku ni kuonyesha unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu kama shukurani kwa ajili ya neema alitujaalia, na kujitolea kila ulicho nacho katika njia yake. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi aliumba wanyama kwa manufaa ya wanadamu na kuwaacha wawatumikie. Neema zote zinazotokana nao kama vile nyama yao, maziwa, ngozi na sufi ni fadhila kubwa kwa waja wa Mwenyezi Mungu.

Kumshukuru mtu kwa ajili ya bilauri ndogo ya maji ni jambo la kiutu. Hivyo hatuna budi kuwa katika hali ya kumshukuru Mwenyezi Mungu wakati wote kwa ajili ya neema nyingi alizotujaalia. Hatuna budi kuonyesha heshima, upole, upendo na wema wakati wa kuwachinja wanyama hawa waliobarikiwa ambao Mwenyezi Mungu ametupatia kwa manufaa yetu.

Omar na Othman ﷺ walikuwa na kawaida ya kubusu nakala za Qur'an zilizobarikiwa kwa heshima kila walipoamka asubuhi. Abdullah lbn Omar pia alikuwa akichukua kitabu kitakatifu mikononi mwake, akikibusu kwa heshima kubwa na kukikumbatia kifuani mwake na huku akisema :

"Huu ni mkataba wa Mola wangu. Haya ni maagizo ya wazi kutoka kwa Mola wangu" (Kattani, II, 196-7).

Pia Ikrima ﷺ alikuwa akichukua maandiko matakatifu na kuyapitisha katika macho yake. Alikuwa akilia na kusema maneno yafuatayo katika kuonyesha unyenyekevu wake na mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

"Haya ni maneno ya Mola wangu, haya ni maneno ya Mola wangu" (Hakim, III, 272/5062).

❀

Katika kipindi cha nyuma pindi kilipotakiwa kufutwa chochote kilichoandikwa kwa wino kilikuwa kikioshwa kwa maji. Anas ﷺ ametufahamisha kuwa katika kipindi cha makhalifa wanne wanafunzi waliokuwa wakiosha aya za Qur'an hawakuwa wakimwaga maji yake mahali popote bila ya mpangilio. Bali walikuwa wakiyakusanya kwenye chombo maalum na baadae kuyamwaga pembezoni mwa kaburi au ndani ya visima visafi ambavyo hakuna mtu aliyevitumia. Pia walikuwa wakiyatumia maji hayo kwa ajili ya kutibu magonjwa. (Kattani, II, 200).

❀

Kabla ya Qur'an kushushwa watu wa Makka walikuwa wakitundika kwenye ukuta wa Al-Kaaba majina ya mashairi saba ambayo yalichaguliwa kutokana na uzuri wake na ufasaha wake . Moja ya mashairi haya lilitoka kwa Labid ibn Rabia. Kazi za Labid zilikuwa zimetundikwa katika ukuta wa Al-Kaaba kwa miaka

mingi. Pindi Labid alipoingia kwenye Uislamu alikataa kuandika au kusoma shairi lingine kutokana na unyenyekevu wake na heshima juu ya maneno ya Mwenyezi Mungu. Shairi lake la mwisho aliliandika alipoingia kwenye Uislamu (mwanzoni):

"Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia na mimi pia kulivaa vazi hili lenye kung'aa la Uislamu kabla haijafika saa iliyoahidiwa" (Ibn Abdilbar, al-Istiab, III, 1335).

❁

Siku moja nabii Suleiman عليه السلام alimtumia barua Balqis ambaye alikuwa malikia wa Sheba kwa ajili ya kumualika kwenye Uislamu. Balqis ambaye alikuwa akiabudia masanamu kwa wakati ule aliisoma ile barua na kusema:

"Enyi mabwana na waheshimiwa. Nimetumiwa barua iliyobarikiwa. Inatoka kwa Suleiman na inaanza hivi "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu"...

Baadhi ya wanachuoni wanasema kuwa kutokana na heshima yake hii aliyoionyesha kwenye barua ya Suleiman ndio maana akabarikiwa kwa kuingia kwenye Uislamu.

❁

Katika nusu ya uhai wa rafiki wa Mwenyezi Mungu, Bashir Hafi, alikuwa mtenda madhambi. Siku moja akiwa anatembea huku amelewa aliokota kipande cha karatasi kilichoandikwa 'Kwa jina la Mwenyezi Mungu'. Alikibusu na kukiweka kwenye paji lake la uso (katika kuonyesha heshima). Alikipulizia manukato na kukiweka sehemu nzuri. Usiku wake aliota ndoto ambayo alisikia sauti ikisema:

"Umelipulizia jina langu manukato mazuri na umelionyeshea heshima kubwa. Sasa kutokana na utukufu na ukubwa wangu, nitalifanya jina lako liheshimiwe hapa duniani na kesho akhera".

Baada ya ndoto hii Bashir aliamka na kutubu na kumrudia Mwenyezi Mungu kwa utii na usafi wa moyo.[27]

❁

Mababu zetu ambao walitumia kila njia kuonyesha unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi na Mjumbe wake, walilifanya jambo hili kuwa kanuni ya maisha yao. Walipokuwa wakiandika vitabu walikuwa hawaliandiki jina la Mwenyezi Mungu kwa uwazi kutokana na kuliheshimu. Kinyume chake walikuwa wakiandika kifupi chake, kama vile *bihi* ikimaanisha kwa jina lake (kwa jina la Mwenyezi Mungu) kutokana na hofu kuwa vitabu vyao vinaweza kuwekwa chini.

❁

Kutokana na masimulizi mbalimbali, siku moja mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu, Ibrahim ibn Edhem alienda kumuona Abu Hanifa. Wanafunzi waliokuwa wamemzunguka Abu Hanifa walimuangalia Ibrahim ibn Edhem kwa dharau na kiugeni. Abu Hanifa akaligundua hili na kumwambia Ibrahim ibn Edhem:

"Tafadhali mheshimiwa ingia ndani, ni heshima iliyoje kwetu".

Ibrahim alimsalimia kwa unyonge na kuondoka. Pindi Ibrahim ibn Edhem alipoondoka, wanafunzi wake wakamuuliza:

"Ni kitu gani kinamfanya mtu huyu astahiki ukubwa na heshima? Inawezekanaje mtu kama wewe ukamuita mheshimiwa?".

Kutokana na hili Abu Hanifa alitoa jibu lifuatalo lililoonyesha hisia zake za heshima kwa marafiki wa Mwenyezi Mungu na ambalo pia lilionyesha kiwango chake cha juu cha unyenyekevu:

"Yeye wakati wote anamfikiria Mwenyezi Mungu, wakati sisi tumetawaliwa na mazungumzo ya kipuuzi na usengenyaji".

27. Attar, Tadhkirat al-Anbiya, Tahran, 1372, uk 128

Abu Hanifa alikuwa amejishonea mwenyewe vazi lake kutokana na malighafi nzuri na za thamani, vazi ambalo alikuwa akilivaa wakati wa swala za usiku. Alifanya haya kutokana na unyenyekevu wake kwa Mwenyezi Mungu, hivyo akituonyesha umuhimu wa adabu na heshima katika kuziendea ibada zetu.

❁

Ahmad ibn Hambal (rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) alikuwa akimtembelea mara kwa mara rafiki wa Mwenyezi Mungu, Bashir Hafi, kwa ajili ya kuongea naye. Alikuwa akimpenda sana. Siku moja wanafunzi wake walimwambia:

"Ewe Imam! Wewe ni mwanachuoni wa Qur'an na Sunnah. Licha ya hili lakini unamtembelea yule mtu wa kawaida mara kwa mara. Je jambo hili linakufaa wewe kweli?"

Imam yule mkubwa akatoa jibu lifuatalo:

"Ni kweli kwamba katika mada mlizozitaja mimi ni bora kuliko yeye. Lakini yeye anamfahamu na kumtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu zaidi yangu".

Hivyo wote Abu Hanifa na Ahmad ibn Hambal waliwaheshimu waja wenye kumfahamu na kumtambua Mwenyezi Mungu kutokana na mapenzi na heshima waliyokuwa nayo kwake, na hivyo walijaribu kufaidika nao kwa kuwatembelea.

❁

Jangwa la Sinai ni sehemu ya hatari mno ambayo hakuna mtu yeyote aliyewahi kufanikiwa kuipita. Kutokana na ujasiri na maamuzi ya Yavuz Sultan Selim jeshi la dola ya Uthmainiyya liliingia kwenye jangwa hilo. Baada ya muda mfupi Yavuz alishuka kutoka kwenye farasi wake na kuanza kutembea. Askari wake wakastaajabu na kupatwa na hofu kubwa: "Kwa nini Sultan ameteremka kwenye farasi wake na kuanza kutembea katika jangwa

hili ambalo linatosha kuchemsha damu ya farasi”. Wakaanza kunong’onezana wao kwa wao kisha na wao wakateremka kwenye farasi wao na kuanza kutembea. Pashas wakamuuliza Hasan Can ambaye alikuwa rafiki wa karibu wa Yavuz:

“Tafadhali muulize Sultan, ni kitu gani hiki?”

Hasan Can akamuuliza Yavuz kwa shauku kubwa kuwa ni jambo gani alilokuwa akilifanya.

“Je huoni Hasan? Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatembea mbele yetu. Inawezekanaje tuwe tumekaa juu ya farasi wetu wakati Sultan wa ulimwengu anatembea kwa miguu?”

Kwa watu wa dola ya Uthmainiyya alama ya usultani kwao haikuwa taji, bali ilikuwa kuchukua upanga. Kila lilipotumika neno ‘mwenye taji’ kwenye nyaraka za dola, usultani wa Sultan ulitekelezwa kwa njia ya ahadi ya umoja na kuchukua upanga. Utaratibu huu uliendelea mpaka wakati wa Sultan wa 36 wa dola ya Uthmainiyya, Wahiduddin.

Baada ya Istanbul kutwaliwa utaratibu wa kuchukua upanga ulifanyika katika kaburi la Ayyub Al-Ansari. Sherehe iliyofanyika iliitwa “Kilic Alayi” (Sherehe ya Upanga).

Upanga aliouchukua Sultan mpya ulikuwa ni upanga ambao mwanzo ulimilikiwa na Omar رضي الله عنه, na kwa sasa umehifadhiwa katika kasri la Topkapi. Upanga huu uliwekwa kwa ajili ya Sultan huyu mpya na mtu wa dini aliyeheshimika sana kwa wakati ule. Jambo hili lilifuatiwa na dua katika hadhara na pongezi nyingi kwa Sultan. Eneo la Ayub lilichaguliwa kwa ajili ya sherehe hizi kwa sababu maswahaba wengi wa Mtume, wote waliojulikana na wasiojulikana, walikuwa wamezikwa katika eneo hili lililochukuliwa kama eneo takatifu kama ilivyo ardhi takatifu ya Haram ndani ya Makka.

❁

Katika kipindi cha Murad wa IV, mafuriko yalitokea na kuangusha kuta mbili za Al-Kaaba. Upesi mkuu wa wasanifu majengo aliyeitwa Ridhwan Aga aliagizwa kwenda Makka kukarabati uharibifu uliotokea. Baada ya kugundua tatizo, mbunifu yule alijizuia kutumia maneno kama vile 'kuanguka' na 'kubomoka' juu ya Al-Kaaba tukufu na badala yake akatoa maneno kama yafuatayo:

"Sehemu ile na ile ya nyumba ya Mwenyezi Mungu imeinama chini kusujudu".

Pia alionyesha heshima yake juu ya Al-Kaaba kwa njia nyingine nyingi, kama vile kuwa makini ili kuzuia wanyama waliobeba vitendea kazi wasichafue sehemu ile tukufu.

Kuziheshimu ardhi hizi tukufu kulianza pale dola ya Uthmainiyya ilipoingia madarakani. Wakati wa safari ya hijja kituo cha kwanza kwa watu watokao Ulaya mpaka Asia kilipewa jina '*Haram*' (Takatifu). Eneo hili bado linabeba jina hili mpaka leo na ndio mwanzo wa kuchunga taratibu muhimu unapowasili kwenye miji hii mitakatifu. Hakuna jambo lolote la kipuuzi linaloruhusiwa katika safari hii.

❁

Mnamo mwaka 1678 Sair Nabi alienda kuhiji pamoja na watu wa dola. Kundi lake lilipokaribia Madina Nabi hakuweza kulala kwa furaha. Alipomuona pasha ananyanyua mguu wake kuelekea Madina aliguswa mno na kitendo hiki na hivyo akaanza kuandika wasifu wake maarufu.

Walipokaribia Madina karibu na swala ya alfajiri, Nabi alisikia ule wasifu aliouandika ukisomwa juu ya minara ya msikiti wa Mtume.

*'Kuweni makini na kwenda kinyume na adabu za hijja mnapokuwa katika eneo hili la Mwenyezi Mungu, ambalo ni kituo*

*na ardhi iliyobarikiwa ya Mtume wake mpendwa, Muhammad Mustafa ﷺ.*

*Ewe Nabi, ingia katika eneo hili na ushikamane na Adabu zake. Hili ni eneo ambalo roho takatifu zinalifuata kama mende na kituo kilichobarikiwa ambacho Mitume wamekibusu'.*

Kutokana na kufurahishwa mno na jambo hili mshairi, Nabi, upesi akaenda kumtafuta mpiga adhana:

"Umejifunza wasifu huu kutoka kwa nani na kivipi?" Alimuuliza.

Mpiga adhana akajibu:

"Usiku Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniambia yafuatayo ndani ya ndoto:

"Mshairi kutoka kwenye umma wangu aitwae Nabi anakuja kunitembelea. Mtu huyu ananipenda na kuniheshimu sana. Msalimie kwa wasifu wake mwenyewe juu ya minara ya msikiti wangu kutokana na haya mapenzi aliyonayo kwangu".

Hivyo tulitekeleza agizo hili la Mtume"

Nabi akaanza kulia bila ya kuweza kujizuia. Alikuwa akilia na wakati huo huo akisema:

"Inamaanisha kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema kwamba mimi ni miongoni mwa umma wake. Yani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amenikubalia kuwa katika umma wake!...

❁

Sultani wa mwisho wa dola ya Uthmayniyya Abdulaziz Han, alikuwa akimheshimu na kumtii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Siku moja alipokuwa amelala juu ya kitanda chake na huku akiwa ni mgonjwa, amedhoofika na hajitambui vizuri, aliambiwa:

“Kuna ombi hapa kutoka kwa watu wa madina”. Baada ya kuyasikia haya Sultani alikusanya nguvu zake zote na kuwaambia wasaidizi wake: “Nipelekeni chini ya gorofa haraka. Ngojeni nisikilize ombi kutoka Haramayn wakati nimesimama. Ombi kutoka kwa majirani wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ haliwezi kusikilizwa huku mtu amekaa na kunyoosha miguu, hii ni kinyume na adabu”...

Kila ujumbe ulipokuja kutoka madina alikuwa akichukua tena udhu na kubusu karatasi zake na kusema “Zina vumbi lililobarikiwa la Madina”. Kisha alikuwa akimkabidhi mkuu wa waandishi ili azifungue na kuzisoma.

❁

Ni muhimu pia kuwataja mababu zetu walioonyesha heshima kwa wanachuoni na watekelezaji wa mwenendo wa mtume. Kuhusiana na kuwaheshimu marafiki wa Mwenyezi Mungu, Ertugrul Gazi alimpa ushauri mzuri mwanae Othman Gazi kwa niaba yake kama namna ya kutoa muongozo kwa wale wote ambao watakuja baada yake: “Angalia mwanangu. Unaweza kuniumiza mimi, lakini kamwe usimuumize sheikh Edebali. Yeye ni kiongozi wa dini wa watu wetu. Yeye ndiye anayetuweka katika usawa na mizani yake haizidi upende mmoja hata kwa dirham moja.

Unaweza kuniasi mimi lakini kamwe usimuasi yeye. Ukiniasi mimi nitahuzunika na kuumia, lakini ukimuasi yeye, macho yangu hayataendelea kukuangalia tena, na hata kama yatakuangalia hayataweza kukuona.

Maneno yangu si kwa ajili ya Edebali bali ni kwa ajili yako. Chukulia maneno haya kama wosia wangu wa mwisho kwako”.

❁

Othman Gazi alimpa mwanae Orhan Gazi ushauri ufuatao:

"...Daima waheshimu, wafanyie wema na kuwafadhilisha wale wanachuoni wema, ambao wanaipa serikali yetu nguvu ya kiimani. Kama unamsikia mwanachuoni mkubwa au mtu mwema kutoka nchi nyingine, mualike katika nchi yetu kwa upole na heshima kubwa. Yafanye mambo ya kiutawala na dini yaongozwe na baraka na msaada wao..."

❃

Katika kipindi cha utawala wa Orhan Gazi, rafiki wa Mwenyezi Mungu aliyekuwa na elimu kubwa aliyeitwa Geyikli Baba alikuwa akiishi katika mji wa Uludag. Baada ya kusikia umaarufu wake Orhan Gazi alimtumia mualiko. Hata hivyo rafiki huyu wa Mwenyezi Mungu ambaye alikuwa na kawaida ya kutangatanga kwenye milima pamoja na paa wake, alikataa mualiko. Kisha akatuma ujumbe akisema: "Pia Orhan asije kuniona".

Orhan Gazi alipopatwa na shauku ya kutaka kujua sababu alipokea jibu lifuatalo:

"Watu wa kanuni za Darwish ni watu wa uoni wa mbali na watu wenye nyoyo nzuri. Ni wajibu wao kutekeleza wajibu wao vilivyo. Kama wataende kinyume na kutoka kwenye njia ya haki basi dua zao hazitakubaliwa. Kwa upande mwingine nyinyi ni wadhamini wa watu. Kwa namna hiyo nyie ni askari wa mstari wa mbele lakini sisi ni askari wa maombi. Ushindi hupatikana kwa juhudi za pamoja kati ya askari wa maombi na askari wa mstari wa mbele vitani. Kama ilivyo kwa askari wa vita wanavyojiandaa kwa silaha na ujuzi wa mbinu za kivita ili kupata ushindi, pia askari wa maombi hawana budi kujiweka mbali na mapenzi na matamanio ya kidunia. Hivyo ninahofia kuwa fadhila na kitu chochote utakachonipatia kutokana na mimi kuja kwako kutapanda mbegu za kuipenda dunia ndani ya nyoyo za madaruwesh na kupunguza mapenzi ya akhera. Matokeo yake madhara yatatufikia sisi sote.

Sultani wangu! Fahamu kuwa muda utakapofika tutaonana tena kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu".

Baada ya muda mfupi Geyikli Baba alikuja Bursa na kupanda mti katika eneo la Orhan Gazi. Wakamfahamisha Sultan kuhusu jambo hili, kisha Sultan akaenda pale haraka. Geyikli Baba akamwambia:

"Tumeupanda kwa kutokana na baraka zake. Hali ya kuwa upo hapa dua za madaruwesh wenu na vizazi vyenu zipokelewe".

Licha ya mashari aliyopewa hapo kabla, Orhan Gazi alimpa Geyikli Baba mji wa Inegol na vitongoji vyake. Hata hivyo, Geyikli Baba ambaye hakuwa anahitaji chochote katika hivi alikataa na kusema:

"Mali ni za Mwenyezi Mungu peke yake. Anawapatia wale wanaostahiki. Sisi hatustahiki"

Sultan akamsisitiza. Kwa kuhofia kuwa kukataa kile alichopewa inaweza ikawa aina ya majivuno, Geyikli Baba akasema:

"Acha kipande kile cha ardhi kilicho upande ule wa kilima kiwe uwanjwa kwa ajili ya madaruwesh".

Kwa kuhofia kukosea kwa kutoonyesha heshima kwa rafiki wa Mwenyezi Mungu na kuifanya dola iwe na tabia hii, Orhan Gazi alikuwa na furaha kubwa pale Geyikli Baba alipokubali ombi lake na akaahidi kubusu mikono yake; aliibusu kwa hakika mfululululizo ...Baadae wakati wa kifo chake aliamuru kaburi lake na msikiti ujengwe. Na kaburi hili bado linatembelewa mpaka leo.

Historia ni shahidi kuwa heshima kubwa iliyoonyeshwa na masultani wa dola ya Uthmainiyya juu ya marafiki wa Mwenyezi Mungu ndio sababu kuu ya kupata usaidizi kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

❀

Heshima aliyoonyeshwa Akshamsaddin na Sultani Fatih Mehmed ilikuwa ni kubwa mno. Ilipelekea mpaka siku ambayo Istanbul ilitwaliwa akawaambia wale waliomzunguka:

“Furaha na amani ambayo mnaniona nayo leo hii haitokani na kuitwaa ngome hii. Ni kwa sababu rafiki wa Mwenyezi Mungu aliyebarikiwa, Akshamsaddin yupo pamoja na mimi wakati huu na sehemu hii...”

❁

Kamal Pasazade ambaye ni mwanachuoni maarufu katika dola ya Uthmainiyya mwanzo alikuwa askari mzuri sana lakini baadae akaacha kazi hiyo na kujishughulisha na masomo yake. Kutokana na vyanzo mbalimbali ni kwamba sababu aliyoitoa juu ya maamuzi haya ni kama ifuatavyo:

“Siku moja tulikuwa katika msafara pamoja na Sultani Bayazid. Pembezoni mwa Sultani alikuwepo mshauri wake aliyeitwa Ibrahim Pasha, na kamanda maarufu Evranosoglu. Evranosoglu alikuwa ni kamanda ambaye hakuna kamanda mwingine aliyekuwa juu yake na hakuna mtu ambaye angeliweza kukaa mbele yake katika mkusanyiko wowote. Lakini wakati ule alikuja mwanachuoni aliyevalia kanzu ya zamani iliyochakaa na kukaa mbele ya kamanda. Nilishangaa kwa kutomuona mtu yeyote akisema kitu ili kuzuia jambo hili na hivyo nikawauliza wale waliokuwa karibu yangu:

“Ni mtu gani huyu ambaye anaweza kupita na kukaa mbele ya kamanda kama Evranosoglu?”.

“Huyu ni mwanachuoni wa maadili aitwae Molla Lutfi” walinijibu.

“Mshahara wake ni kiasi gani?” Niliuliza.

“Dirham 30” walinijibu.

Nikasema yafuatayo kwa mshangao:

"Inawezekanaje mtu mwenye mshahara mdogo kama huyu akae mbele ya kamanda mkubwa kama huyu?" Kisha wakaniambia:

"Wanachuoni wanapewa heshima kubwa kiasi hicho kutokana na utukufu wa elimu yao ya dini. Na kwa namna yoyoye ile iwe ni pasha au kamanda mwenye imani, busara na adabu hawezi kufanya kinyume na haya..."

Baada ya kuyasikia haya nikagundua kuwa sistahiki kuwa miongoni mwa makamanda wale, na kwa kuhisi kuwa kwa kupitia eneo la elimu tu ndio umuhimu wangu unaweza kuonekana, nikaamua kuondoka jeshini na kujishughulisha na kusoma".

Baada ya kufanya maamuzi haya Kemal Pashazade akafikia daraja la elimu ambalo lilimpelekea kuwa mtu 'wa kipekee katika zama zao'. Baada ya kifo cha Zenbilli Ali Efendi akawa Shaykh al-Islam wa 9 katika dola ya Uthmainiyya.

❁

Siku moja wakati Sultani Ahmad Han anaenda kwa Uskudar alikutana na Aziz Mahmud hudayi sokoni. Upesi akashuka juu ya farasi wake na kumpandisha Sheikh na kuanza kutembea kwa miguu nyuma yake. Moyo wa Hudayi haukuweza kuvumilia kumuona Sultani mkubwa kama yule akitembea na hivyo baada ya muda mfupi akamwambia:

"Nilimpanda farasi huyu ili tu kutii dua ya Sheikh na amri ya Sultani wangu". Kisha akashuka kwenye farasi yule. Hivyo dua ya Sheikh wake, Uftade ikawa kweli: "Mwanangu! Mwenyezi Mungu ajaalie Masultani watembee nyuma yako..."

❁

Sultani Ahmad Han alionyesha heshima ya hali ya juu kwa Aziz Mahmud Hudayi na hakuwahi kupunguza wema wake kwake. Siku moja Aziz Mahmud Hudayi alikuwa amekaa naye ndani ya kasri wanaongea. Wakati fulani Wakamletea Aziz Mahmud Hudayi buli na bakuli lenye maji kwa ajili ya kuchukua tena udhu. Sultani akachukua lile buli kwa heshima ya mwalimu wake na kuanza kummiminia maji. Nyuma ya pazia mama yake Sultani alikuwa tayari anamsubiria huku ameshika taulo. Punde fikra zifuatazo zikamjia mama yake Sultani:

"Natamani ningeliuona muujiza wa Aziz Mahmud Hudayi". Baada ya Hudayi kupata neema ya kufahamu kile alichokifikiria mama yake alisema:

"Je haistaajabishi? Kuna watu wanatarajia kuona maajabu kutoka kwetu. Kutakuwa na muujiza gani mkubwa zaidi ya khalifa wa dunia akinimiminia maji kwenye mikono yangu wakati mama yake mpendwa anamsubiria na taulo mkononi?"

❁

Akiwa amekata tamaa kutokana na shambulio la maadui dhidi ya bandari, Mirliva Jawad Pasha alishikwa na usingizi mwepesi kutokana na kuchoka. Ndani ya ndoto alisikia sauti ikimuita kwa ulaini:

"Ewe Jawad! Unaonyesha heshima na unyenyekevu kwenye maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi, na kwa ajili hii Mwenyezi Mungu Mtukufu anakupa bishara njema ya msaada wake. Angalia baharini".

Pindi Jawad Pasha alipoangalia kivuko cheusi aliona mwanga mzito ulioandika herufi 'kaf' na 'waw'. Kisha akaamka.

Siku iliyofuata wakati anasoma Surat Fatha mbele ya kaburi alisikia sauti kutoka kwenye ndoto yake tena:

“Ewe Jawad! Tandaza baharini mabomu 26 yaliyomo kwenye ghala lenu”.

Alifurahia sana jambo lile. Alikuwa katika maajabu ya kiimani. Wakati anafikiria namna ya kulitekeleza jambo lile aliona njia ndogo mbele yake, alikuwepo mtu anayeng’aa anamuangalia. Mtu yule alimsogelea Pasha na kumuuliza kama kulikuwa na tatizo. Jawad Pasha alimueleza kila kitu kilichotokea. Rafiki yule wa Mwenyezi Mungu alimfafanulia maajabu yale kwa undani zaidi na kwa namna ambayo inaeleweka:

“Mwanangu! Ule mwangaza uliouona baharini ni ishara ya ushindi. Ni ishara kuwa makafiri watashindwa kuichukua ardhi hii. Herufi ‘kaf’ na ‘waw’ zinafanya jumla ya 26 kutokana na mahesabu yangu. Hivyo kuyatandaza mabomu hayo 26 juu ya kivuko cheusi itakuwa ndio ujanja mkubwa utakaopelekea ushindi”.

Baada ya maneno haya yule mtu mwenye kung’aa akatoweka.

Kwa kawaida mabomu yalikuwa yakitandazwa kwa wima pale bandarini, lakini kutokana na ndoto yalikuwa yanatakiwa kutandazwa sambamba na ardhi. Kwa sababu kivuko kile kilikuwa hakitumiki, kimkakati haikuwa vyema kuyatandaza kwa namna hii.

Licha ya yote haya Jawad Pasha upesi aliamuru mabomu yale yatandazwe bila kuchelewa kulingana na ufunuo ule. Jukumu hili lilitekelezwa vizuri kwa kutumia meli ya mabomu ya Nusret chini ya amri ya kapteni Hakki Bey. Mabomu yale yalilazwa usiku wa manane na yaliandikwa maneno ‘Mwenyezi Mungu ni mkubwa’. Baada ya kumaliza kazi ile asubuhi yake Kapteni Hakki Bey alikufa shahidi kutokana na shinikizo la moyo.

Siku iliyofuata pindi meli za kivita za maadui zilipowasili kwenye bandari mabomu yale yalilipuka. Matokeo yake meli hizi za maadui zikazikwa pale bandarini na hivyo shambulio la maadui likawa limezimwa kabisa.

Katika gazeti la 'Revue de Paris', toleo la mwaka 1930, Winston Churchill alilielezea tukio hili:

"Sababu kuu ya watu wengi kufa kutokana na gharama kubwa ya vita, na kuzama kwa meli 5000 za kibiashara na kivita katika vita vya kwanza vya dunia, ilikuwa ni mabomu 26 yaliyokuwa yamening'inizwa na waturuki mwishoni mwa kamba nyembamba ya chuma cha pua usiku wake".

Hizi ni baraka za kipekee kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi kutokana na heshima na unyenyekevu unaoonyeshwa kwenye maneno matukufu ya Mwenyezi Mungu...

❁

Kwa kifupi ndani ya Qur'an jambo muhimu kuliko yote lililoamrishwa baada ya imani ni kutenda amali njema. Na kinachohitajika baada ya toba ni kutenda amali njema pia. Inamaanisha kuwa kupandishwa daraja mbele ya Mwenyezi Mungu na kukubaliwa kwa toba kunategemeana na kufanya au kutofanya amali njema. Na kutenda amali njema kunajumuisha 'taadhwim li-amrillah' na 'shafkat ala khalkillah', yani kufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na kuvitumikia viumbe vyake kwa huruma na upendo.

### 4. Kuheshimu amana ya mtu na kuchunga ahadi

Neno '*amanah*' au amana linatokana na mzizi 'iman' au imani. Neno 'mu'min' ambalo ni maana ya ujumla kwa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu, na linaashiria kuwa Yeye ni chanzo cha ulinzi, anajaalia uaminifu kwa waja wake, na Yeye ndiye anayewafanya kuwa waaminifu. Pia Yeye ndiye aliwapa Mitume wake sifa ya 'uaminifu' na ndiye aliyewafanya waaminike. Kutokana na haya ni kwamba 'mu'min' ni yule mwenye imani, ambaye amepewa

amana, ambaye anasababisha uaminifu, na ambaye anaweza kuaminiwa.

Abu Musa ﷺ alisema:

"Nilimuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni nani mbora zaidi miongoni mwetu?'

Akanijibu:

"Ni yule ambaye waislamu wanasalimika kutokana na ulimi wake na mikono yake" (Bukhari, Iman 4,5, Riqaq 26; Muslim, Iman 64,65).

Kuwa muaminifu na kuchunga ahadi, yani kuheshimu maneno yako, ni moja wapo ya msingi muhimu kwa mtu na jamii kwa ujumla. Amani katika jamii inatokana na watu wake kuwa waaminifu na wenye kuchunga ahadi. Bila sifa hii hatuwezi kufanya mageuzi katika dini wala dunia.

Aya zifuatazo zinagusia hasa sifa ya uaminifu waliokuwa nao Mitume:

"**Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu Mlezi. Na mimi kwenu ni mwenye kukunasihini, muaminifu**" (Al-a'raf, 7:68).

"**Hakika mimi kwenu ni Mtume muaminifu**" (Al-Shu'ara, 26:107).[28]

Pia sifa hizi nzuri ni alama ya umma wa Muhammad. Kwani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijulikana kwa jina la 'Muaminifu' hata kabla ya kuja wito wa utume wake.

Baada ya uaminifu, sifa nyingine muhimu ni kuchunga ahadi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuamuru kuchunga ahadi tunazotoa kama ifuatavyo:

28. Pia angalia Al Shu'ara, aya ya 125,143, 162, 178; Al Duhan, aya ya 18

"**Enyi mlio amini! Timizeni ahadi. Mmehalalishiwa wanyama wa mifugo, ila wale mnao tajiwa. Lakini msihalalishe kuwinda nanyi mmo katika Hija. Hakika Mwenyezi Mungu anahukumu apendavyo**" (Al-Maida, 5:1).

"**Wala msiyakaribie mali ya yatima, isipo kuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afike utuuzimani. Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itasailiwa**" (Isra, 17:34).

Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu anaonyesha sifa za muumini ambaye ameongoka kama ifuatavyo:

"**Na ambao wanazitimiza amana zao na ahadi zao**" (Al-Mu'minuun, 23:8).

Kamwe tusisahau kuwa ahadi na mikataba ya aina zote tunayoifanya na watu pia nayo ni ahadi zilizowekwa kwa Mwenyezi Mungu. Kila mtu hana budi kushikamana na makubaliano aliyoyaweka mbele ya Mwenyezi Mungu na kuchunga ahadi kwa umakini mkubwa.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anamsifu na kumtukuza nabii Ibrahim kama ifuatavyo:

"...**Ibrahimu aliye timiza ahadi?**" (Al-Najm, 53:37).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwapa bishara njema wafanyabiashara waaminifu na wakweli kama ifuatavyo:

*"Mfanyabiashara ambaye anaongea ukweli na ni muaminifu atakuwa karibu na Mitume, watu wema na mashahidi siku ya kiama"* (Tirmidhi, Buyuu 4/1209; Ibn Majah, Tijarah, 1).

Kinyume na haya kuna maonyo makali kwa wale wasio waaminifu na wasiochunga ahadi zao. Kwa mfano Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Yeyote asiye na hata chembe ya uaminifu pia hana imani"* (Ahmad, III, 135).

❁

Mtu akishindwa kuonyesha uaminifu kwa wale wanaomzunguka ni ishara ya udhaifu wa imani, kupoteza utu na kupoteza hisia za Uislamu. Mtu hawezi kuwa muumini kwa jina tu na huku hana chochote katika ibada bali amejawa na majivuno na uovu. Omar ﵁ analizungumzia jambo hili kwa namna nzuri zaidi kama ifuatavyo:

"Msiangalie kwenye swala ambazo mtu anaswali wala funga anazofunga. Bali sikilizeni muone ikiwa akiongea anaongea ukweli na kama anapoaminiwa havunji uaminifu wake, na kama anajiegemeza kwenye dunia na hajali kuhusu halali na haramu"[29]

Pindi hali hii ya kuvunja ahadi na kutokuwa mkweli isiporekebishwa, itapelekea kufikia katika sifa mbaya kuliko zote ambayo ni unafiki. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

"Kuna sifa nne ambazo zikikutwa kwa mtu basi mtu huyo ni mnafiki kamili. Na kama akiwa na sifa moja wapo basi ana unafiki kidogo: 1. Anapoaminiwa huvunja ahadi yake; 2. Anapoongea husema uongo; 3. Anapotoa ahadi hatimizi; 4. Yule ambaye anavuka mipaka kwa kufanya uadui na maovu" (Bukhari, Iman 24; Medhalim 17; Muslim Iman 106).

Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: "Siku ya kiama nitakuwa adui wa makundi haya matatu ya watu: 1. Yule anayeapa kwa jina langu na kisha akavunja ahadi yake; 2. Yule anayemuuza mtu huru kama mtumwa na kutumia hela zake; 3. Yule anayemuajiri mfanyakazi na kuacha kumlipa baada ya kumaliza kazi" (Bukhari, Buyuu 106; Ijarah).

29. Bayhaki, Sunan al Kubra, Daru'l Fikr ts. VI, 2888; Shuab'l Iman, IV, 230, 326

Hivyo uaminifu na kuchunga ahadi ni alama za Muislamu. Muumini kutokuwa muaminifu na kuvunja ahadi zake ni sifa mbaya mno ambayo inasababisha ghadhabu za Mwenyezi Mungu na kumpelekea mtu kuwa chini zaidi ya walio chini.

***Matukio ya wema***

Ulipoangaliwa ukarimu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwekwa juu na kabila lake, na alikuwa mbora zaidi katika ukoo na mwenye tabia nzuri zaidi. Yeye ndiye aliyekuwa akishughulikia haki za majirani zake, na alikuwa mwenye upole na uvumilivu mkubwa. Yeye ndiye aliyekuwa akiaminika zaidi kuliko watu wote, na ambaye alijizuia sana kuwaumiza na kuwadhuru watu wengine. Kamwe hakuonekana akimlaumu wala kumshitaki mtu yeyote bila haki, na hakuonekana kamwe akibishana na mtu yeyote. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimkusanyia sifa zote nzuri na ubora kiasi kwamba ukoo wake ukaona anastahiki jina la *'Al-Amin'* (Muaminifu).[30]

Jina *'Al-Amin'* likawa kama jina la pili la Mtume. Na ukweli ni kwamba alipofikisha miaka 25 hili ndilo jina alilokuwa akiitwa.[31] Katika kipindi cha majadiliano kuhusu Al-kaaba, pindi Maquraysh walipomuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anakuja walifurahi na kusema: "Al-Amin anakuja!". Walikuwa wakimuamini sana na walimhusisha katika kila jambo. Tofauti na maswahaba zake ambao walikuwa tayari kutoa uhai wao, mali zao na kila kitu chao kwa ajili yake, pia maadui zake ambao walipanga kumuua hawakuweza kusema chochote dhidi ya uaminifu wake.

Washirikina pia walikuwa wakitumia jina la *Muhammad' al-Amin* wakati wote na walimpa vitu vyao vya thamani awahifadhie kinyume na wao wenyewe. Hata wakati Mjumbe wa Mwenyezi

30. Ibn Hisham, I, 191; Ibn Sa'd, I, 121
31. Ibn Sa'd, I, 121, 156

Mungu ﷺ anataka kuhamia Madina bado alikuwa na baadhi ya mali za washirikina. Na licha ya tishio la kuuawa alimuachia mali zile Ali ili azirudishe kwa wenyewe.

❁

Moja ya tukio lililompelekea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kupewa majina ya *'Al-Amin'* na *'As Sadik'* (Mtii) limesimuliwa na Abdullah ibn Abi'l Hamsa ﵁ kama ifuatavyo:

"Siku moja kabla ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hajawa Mtume nilienda naye sokoni. Nilikopa fedha kutoka kwake na kumuahidi anisubiri kidogo nitamletea. Niliondoka lakini nilisahau ile ahadi yangu. Siku tatu baadae nikakumbuka na kurudi katika ile sehemu tuliyokubaliana kukutana. Nilimkuta pale akinisubiri. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakunikaripia kwa kosa nililolifanya bali aliniambia"

*"Kijana. Umenikosesha raha. Nimekusubiria hapa kwa siku tatu"* (Abu Dawud, Adab, 82/4996).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwashinda watu wote kwa uaminifu na kuchunga ahadi, hata hivyo kusubiri kwake kwa siku tatu haikuwa kwa sababu ya fedha. Kilichomfanya apate tabu ya kusubiri kwa siku tatu ilikuwa ni hofu yake juu ya kuchunga ahadi.

❁

Hudhayfa ﵁ anasimulia:

"Mimi na baba yangu Husayl tuliondoka Makka kuelekea Madina , tulipokamatwa na kabila la Maquraysh na kuulizwa: "Mnaenda kujiunga na vikosi vya Muhammad". Tuliwaambia: "Hapana, hatuendi Madina kwa sababu hiyo, tunaenda kwa sababu nyingine". Kisha wakatuambia tuahidi kuwa hatutojiunga na vikosi vya Muhammad na kushiriki naye katika vita. Tulipowasili

Madina na kumsimulia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kilichotokea alituambia:

"Nendeni. Tutachunga ahadi yenu na kumuomba Mwenyezi Mungu msaada dhidi yao" (Muslim, Jihad, 98).

❁

Ilikuwa ni kipindi cha mkataba wa Hudaybiya na masharti yote tuliyokubaliana yalikuwa yameshaandikwa. Mara Abu Jandal, mtoto wa Suhayl ibn Amr ambaye ni muwakilishi wa Maquraysh, akajitokeza mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ huku anaburuza miguu yake iliyofungwa minyororo. Abu Jandal ؓ alikuwa akiteswa kwa kuwa aliingia kwenye Uislamu. Alibahatika kutoroka na kwenda sehemu ambayo walikuwepo waislamu. Suhayl alisisitiza kuwa mtu wa kwanza kurudishwa awe mwanae kutokana na makubaliano, kisha akampiga Abu Jandal usoni kwa fimbo. Kutokana na kuhuzunishwa na tukio lile, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliomba kwa kurudia rudia na kusisitiza kuwa Abu Jandal awe nje ya makubaliano yale na hivyo arudishwe kwake. Hata hivyo mshirikina huyu aliyekuwa na moyo mgumu hakukubaliana na hili. Abu Jandal akawa anarudishwa kwa Maquraysh, akasema kwa hasira:

"Je mtanirudisha na kunitupa ndani ya moto ule ule wa dhulma?" Waislamu wakaumia sana nyoyo na wakashindwa kuvulia na hivyo wakaanza kulia. Katika kujaribu kumtuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia Abu Jandal:

*"Abu Jandal. Tafadhali kuwa na subira zaidi. Subiria malipo ya hili kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu atawapa nafasi na namna ya kujikomboa, wote wewe na waislamu wengine dhaifu wasio na mtu wa kuwasaidia. Tumefanya makubaliano na kabila hili na tumewaahidi kwa jina la Mwenyezi Mungu. Na wao wametuahidi kwa jina la Mwenyezi Mungu.*

*Hatuwezi kuvunja ahadi zetu. Jambo hili lipo nje ya uwezo wetu"* (Ahmad, IV, 325; Waqidi, II, 607-8; Ibn Hisham, III, 367; Belazuri, I, 220).

❁

Baada ya mkataba wa Hudaybiya mtu mmoja kutoka Makka aitwae Abu Basir ؓ ambaye aliingia kwenye Uislamu, pia alitafuta hifadhi Madina. Lakini kutokana na masharti ya mkataba, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilazimika kumrudisha kwa washirikina. Mara ya kwanza Abu Basir ؓ hakuweza kuelewa maamuzi haya ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na hivyo akamuuliza kwa mshangao:

"Je unanirudisha kwa watu wenye kuabudia masanamu?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamtuliza kwa upole kwa kusema:

*"Abu Basir! Hatuwezi kuvunja makubaliano yetu. Lakini kama utakuwa na subira, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atakuonyesha njia ya kuepukana na hayo wewe na wenzako kama wewe".*

Baada ya maneno haya Abu Basir ؓ hakuwa na la zaidi la kusema na hivyo alitii maamuzi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Akaelewa hali waliyokuwa nayo waislamu wote na hivyo kujisalimisha mwenyewe kwa washirikina. Hata hivyo alijua kuwa harudi Makka bali anaenda kwenye kifo chake mwenyewe. Kwa kujua hili aliamua kujitetea na hivyo akawashambulia wale waliokuwa wakimpeleka. Alimuua Hunays, mmoja wa watu wawili waliokuwa naye, lakini yule mwingine alikimbia. Abu Basir alichukua nguo ya Hunays, mali alizokuwa nazo na upanga na kuvipeleka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Chukua moja ya tano ya mali hii na ukae nayo mwenyewe". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamjibu:

*"Nikichukua vitu hivi nitakuwa nimevunja makubaliano niliyoweka nao. Hata hivyo jambo lako ni tofauti. Kitendo ulichokifanya na mali za mtu uliyemuua ni jukumu lako"* *(Waqidi, II, 626-7).*

Kutokana na uoni wake wa mbali Abu Basir akaamua kuondoka Madina baada ya muda mfupi na kwenda kukaa katika pwani iliyopo kati ya Makka na Damascus, pwani hiyo ilikuwa ikiitwa Îs. Baada ya muda mfupi eneo lile likawa haliingiliwi na upande wowote na ikawa sehemu ya kukimbilia. Abu Jandal ؓ aliyetajwa hapo juu naye pia akawatoroka madhalimu wake na kwenda kuungana na Abu Basir. Namba ya waislamu ikafikia 300 kwa namna hii. Njia ya kibiashara kati ya Makka na Damascus sasa ikawa katika tishio. Kutokana na kuathirika na matukio haya, washirikina wa Makka wakamuomba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ waondoe kipengele kile katika mkataba. Yani wakaomba kuwa waislamu wanaotoroka Makka wakubaliwe kukaa Madina. Matokeo yake kipengele ambacho kilikuwa kigumu mno kwa waislamu kukikubali kikawa kimeondolewa kutokana na kuchunga ahadi yao.[32]

Hivyo uaminifu wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ juu ya ahadi zake ilikuwa ndio chanzo cha rehema na baraka kwa waislamu wote.

❁

Asubuhi moja katika kipindi cha kutwaliwa Haybar, Yassir ambaye alikuwa akipata ziriki yake kwa kuchunga kondoo wa mmoja wa viongozi wa wayahudi. alikuwa akichunga kondoo wake nje ya ngome, hapo alikutana na Mtume.

Baada ya kuongea naye kwa muda mfupi akakubali kuingia kwenye Uislamu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akabadilisha jina lake na kuwa 'Aslam'. Baadae Aslam ؓ akamuuliza Mjumbe

32. Angalia Bukhari, Surut, 15: Ibn Hisham, III, 372

wa Mwenyezi Mungu ﷺ awafanyie nini wale kondoo aliokuwa akiwachunga. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamjibu:

*"Wageuze na uwaongoze warejee wenyewe. Usiwe na shaka kuwa hawatafika kwa mmiliki wao"*. Aslam ﷺ akajaza changarawe mkononi mwake na kuwarushia kondoo huku akisema:

"Rudini kwa mmiliki wenu! Naapa kwa Mwenyezi Mungu sitakuwa nanyi tena tokea sasa".

Wale kondoo wakarejea kwa pamoja na kuingia kwenye ngome kana kwamba kuna mtu anawaongoza. Mapema baada ya Aslam kuingia kwenye Uislamu alishiriki katika vita na baada ya muda si mrefu akafa shahidi.[33]

Hata wakati wa vita ambapo mahitaji yamekuwa hafifu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwarudisha kondoo wa maadui zao ambao wamekuja karibu yake. Na hata mchungaji naye hakusaliti mali ya mmiliki aliyeweka naye mkataba. Na jambo hili analo pekee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ 'muaminifu' na umma wake wa waumini.

❁

Baada ya Makka kukombolewa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituma ujumbe kwa Othman ibn Talha ambaye alikuwa akiuhifadhi ufunguo wa Al-Kaaba aupeleke kwake. Kwa kuhofia kuwa ufunguo usingelirejeshwa kwake, Othman akasema:

"Ninakupa ufunguo huu kama amana ya Mwenyezi Mungu" (Waqidi, II, 833; Haythami, VI, 177).

Baada ya kuingia kwenye Al-Kaaba na kuswali, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitoa hotuba ya ushindi. Mwishoni mwa hotuba yake akauliza:

33. Ibn Hisham, III, 397-8; Ibn Hajar, al Isaba I, 38-9

"Othman yuko wapi?" Othman ibn Talha akanyanyuka. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasoma aya ifuatayo:

"**Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu. Hakika haya anayokuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona**" (Al-Nisa, 4:58).

Kisha akasema:

*"Enyi watoto wa Abu Talha. Chukueni amana hii ya Mwenyezi Mungu na muahidi kuihifadhi daima na kuwa waaminifu. Hakuna yeyote atakayeichukua kutoka kwenu ili mradi hamuwi madhalimu. Leo ni siku ya wema na kuchunga ahadi"*. Kisha akairejesha funguo kwa Othman ibn Talha. (Ibn Hisham, IV, 31-32; Waqidi, II, 837-838; Ibn Sa'd, II, 137).

Maswahaba wengi wakubwa walitarajia kuwa wangelipewa wao funguo ya Al-Kaaba, kwa kuwa waliliona jukumu la kuitumikia nyumba ya Mwenyezi Mungu ni jambo kubwa na tukufu. Lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimpa yule aliyestahiki zaidi. Kila mtu alishangazwa na wema ule na kusababisha watu wengi kuingia katika Uislamu.

❁

Kwa kuwa Makka ilikombolewa kwa njia ya amani hivyo hakuna chochote kilichochukuliwa kama ngawira[34]. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliomba akopeshwe fedha na mavazi ya chuma kutoka kwa matajiri wa Makka ili kukidhi mahitajio muhimu ya jeshi la waislamu ambalo lilikuwa kubwa mno. Baadae aliwalipa kutokana na ngawira kutoka Khawazin na kusema:

34. Abu Dawud, Kharaj, 24-25/3023

*“Matokeo ya kukopa kitu ni kushukuru na kulipa deni*” (Waqidi, II, 863; Abu Dawud, Buyu, 88/3562: Muwatta, Nikah, 44).

Tajiri aliyekuwa ametoa mikopo mwanzoni alihofia kuwa kamanda atakayeshinda angelichukua mali zake zote. Hata hivyo haukupita muda mrefu kabla ya wao kukubali kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kweli alikuwa *‘Al-amin’* au muaminifu.

❁

Pindi Musa عليه السلام alipokuja Madyan, aliwaona watu wengi wakinywesha wanyama wao. Nyuma yao kabisa walikuwepo wasichana wawili wakisubiria kunywesha wanyama wao, hawakuweza kusogea karibu mpaka wachungaji waondoke. Baada ya Musa kuwasaidia walirudi kwa baba yao na kumuelezea kilichotokea na kuomba wamualike huyu kijana aliyewasaidia. Binti mdogo zaidi akasema:

“**Akasema mmoja katika wale wanawake: Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu**” (Al-Qasas, 28:26).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatujulisha kwamba:

*“...Shuayb عليه السلام aliwaambia:*

*“Ewe binti yangu, unajuaje kama ana nguvu?” Wale wasichana wakajibu:*

*“Alichukua jiwe zito na kuliweka juu ya kisima”. Kisha Shuayb akawauliza:*

*“Vizuri, mmejuaje kuwa yeye ni muaminifu?” Binti zake wakajibu:*

*“Tulipomualika hapa nyumbani alituambia: “Tembeeni nyuma yangu na sio mbele yangu”. Kutokana na maneno yake haya tukagundua kuwa yeye ni muaminifu”* (Haythami, VIII, 203-4).

❁

Baba yake Jabir ؓ aliuawa katika vita vya Uhud na kuacha familia kubwa yenye kuhitaji msaada na madeni mengi. Jabir anaelezea:

“Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniambia:

*“Fedha za sadaka zikiwasili kutoka Bahrein nitakupatia (baadhi yake)”.*

Hata hivyo hakuna fedha yoyote iliyokuja kutoka Bahrein mpaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akafariki. Ilipowasili baadae Abu Bakr ؓ akasema:

“Kama kuna mtu yeyote ambaye aliweka ahadi na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ au alikuwa anadaiwa naye na aje karibu yetu”.

Baadae nilisogea karibu yake na kumwambia:

“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniambia kadha wa kadha”. Abu Bakr ؓ akaingiza mkono wake kwenye fedha zilizotokana na ngawira na kujaza mkono. Alipozihesabu niliona zikikaribia dinar 500. Kisha Abu Bakr ؓ akaniambia:

“Chota nyingine kama hizi mara mbili zaidi” (Bukhari, Kafalat, 3).

Abu Bakr ؓ alitekeleza ahadi iliyowekwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na hivyo kuonyesha uaminifu wake katika kuchunga ahadi.

Anas ؓ anasimulia: “Mjomba wangu Anas ibn Nadr hakushiriki katika vita vya Badr na hivyo jambo hili likamgusa sana. Alimwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Sikuwepo katika vita vya kwanza mlivyopigana na washirikina. Kama Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ataniruhusu kushiriki katika vita vingine dhidi yao, basi kwa hakika ataona nitakachokifanya”.

Vilipotokea vita vya Uhud naye alikuwepo. Pindi waislamu walipoacha nafasi zao walizopangiwa na Mtume, alisema yafuatayo huku akiwaashiria marafiki zake: "Ewe Mola wangu, Nakuomba msamaha badala yao", na huku anawaashiria washirikina alisema: "Natangaza kuwa najiweka mbali na wanayoyafanya". Kisha akasogea mbele na kukutana na Sa'd ibn Muadh ﷺ na kumwambia:

"Ewe Sa'd! Ninachotaka ni pepo. Naapa kwa Mola wa Al-Kaaba kwamba naanza kuhisi harufu ya pepo kwenye ncha ya mlima Uhud".

Baadae pindi Sa'd aliposimulia kisa hiki alisema:

"Sikuweza kufanya alichokifanya yeye ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu".

Tukamkuta mjomba wangu ameuawa. Alikuwa na majeraha zaidi ya sabini yaliyotokana na panga, singe na mishale. Washirikina walikuwa wamekata miguu yake ili asitambulike na mtu yeyote. Alikuwa dada yake pekee ndiye aliyeweza kumtambua kwa kupitia ncha za vidole vyake. Aya ifuatayo ilishushwa kuhusiana na mjomba wangu na wengine kama yeye:

**"Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo"** (Al-Ahzab, 33:23) (Bukhari, Jihad 12).

❁

Bara ibn Ma'rur ﷺ alikuwa miongoni mwa wawakilishi kumi na mbili katika mkataba wa Aqaba. Bara alimuahidi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuwa angelienda Makka katika kipindi cha Hijja. Hata hivyo ilipofika wakati wa Hijja alishikwa na maradhi na kuwa kitandani hoi. Aliiambia familia yake:

"Nigeuzieni kwenye uelekeo wa Al-Kaaba kama njia ya kutekeleza ahadi yangu kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Nilimwambia kuwa ningelienda". Kwa njia hii akawa mtu wa kwanza kuigeukia Al-Kaaba wakati wote wanaishi na baada ya kufa kwake.

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliporejea Madina alienda kwenye kaburi la Bara ibn Ma'rur ؓ pamoja na maswahaba zake. Walisimama kwenye safu na yeye akaongoza swala ya maiti kwa ajili yake, akaomba:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Msamehe, Mhurumie na uwe radhi naye" (Ibn Abdilbar, I, 153; Ibn Sa'd, III, 619-20).

❁

Hanesh ؓ amesema:

"Nilimuona Ali akiwa tayari kuwachinja kondoo wawili, nikamuuliza:

"Kwa nini unafanya hivyo?". Akanijibu:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniagiza kuchinja mnyama kwa ajili yake baada ya kifo chake. Ninatekeleza matakwa yake na nitaendelea kufanya hivyo"

❁

Khalifa, Muawiya ibn Abu Sufyan alikuwa ameweka mkataba wa amani na watu wa Byzantine. Kabla ya muda wa mkataba kuisha Muawiya akaondoka pamoja na jeshi lake kwenda kwenye ardhi za Byzantine. Alikuwa anaenda kusubiri kwenye eneo karibu nao ili apigane nao punde tu muda wa mkataba wao utakapoisha. Wakati jeshi linaelekea Byzantine, mtu mmoja aliyekuwa juu ya farasi alionekana. Mtu huyo alisema kwa sauti ya juu:

"Allahu Akbar, Allahu akbar! Ahadi lazima zichungwe na hakuna kwenda kinyume na ahadi".

Walipoangalia kwa makini waliona mtu yule alikuwa ni Amr ibn Adese ﷺ, mmoja wa waislamu wa mwanzo. Khalifa alimtuma mtu kwenda kumuuliza kuwa alimaanisha nini. Amr ﷺ akamuelezea:

*"Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema: 'Pindi mtu yeyote anapofanya makubaliano na kabila la watu, basi asiyavunje wala kuyabadili mpaka muda wake uishe au mpaka waujulishe upande mwingine juu ya kuvunja makubaliano yao".*

Baada ya kuyasikia haya, Muawiya akarudi nyuma pamoja na jeshi lake. (Abu Dawud, Jihad, 152/2759; Ahmad, IV, 111, 113, 385-6).

Hivyo tunaona kuwa hakuna tofauti kati ya ahadi iliyowekwa kwa Muislamu au asiyekuwa Muislamu. Pindi Muislamu anapofanya makubaliano na mtu hana budi kuchunga ahadi yake na kuitekeleza.

❁

Miongoni mwa watu wa dola ya Uthmainiyya, maadili mema kama vile uwerevu, kuchunga ahadi na utii vimekuwa ni sifa na tabia ambazo zimepamba nyoyo zao. Tabia hizi zilikuwa sehemu ya maisha yao. Ndio maana Ulaya maneno 'uturuki' na 'Uislamu' yanaendana. Matokeo yake pakasemwa:

"Kuwa mturuki ina maana kuwa muaminifu, mtu ambaye neno lake linaweza kutegemewa. Ilikuwa ikijulikana kuwa tofauti na nchi nyingine, watu wa dola ya Uthmainiyya kamwe hawawezi kutoa kiapo cha uongo.

Generali wa zamani wa Ufaransa aliyeitwa Comte de Bonneval, alitafuta ulinzi kwenye dola ya Uthmainiyya wakati wa

utawala wa Ahmad III. Ana yafuatayo ya kusema kuhusu alichoshuhudia:

"Waturuki wanaonyesha utii wa kidini juu ya ahadi wanazotoa".

Balozi wa Swiden alisema:

"Waislamu wa Uturuki ni waaminifu mno katika maneno yao na ahadi zao. Wanajitahidi neno Mwenyezi Mungu lisiondoke mdomoni mwao. Hakuna ushahidi mwingine unaohitajika pindi wanapotoa ahadi zaidi ya Mwenyezi Mungu kuwa shahidi wao".

Henri Mathieu, mtunzi wa kifaransa ambaye ni maarufu kwa uhasama wake na waturuki anakiri yafuatayo:

"Kushindwa kuthibitisha utu na maadili yaliyopo kwenye asili ya waturuki kama jambo la thamani kubwa kwao ni kutowatendea haki. Wao ni watu wanaoamini kuwa kuchunga ahadi zao ni jambo tukufu kwao na ambao wamekubali uaminifu na usawa kuwa misingi ya maadili".

❁

Kwa kifupi Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an tukufu:

"**Bila ya shaka wanao fungamana nawe, kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hizi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anaye tekeleza aliyo muahadi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamlipa ujira mkubwa**" (Al-Fath, 48:10).

Pindi Muislamu anapotoa ahadi hana budi kumfanya Mwenyezi Mungu kuwa shahidi yake. Hivyo kila ahadi atakayoitoa kwa watu itakuwa ahadi aliyoitoa kwa Mwenyezi Mungu. Kwa namna hiyo kinachomlazimu muumini ni kuchunga ahadi yake na kuwa

muaminifu na mtu mwenye kuweza kutegemewa , mtu ambaye wengine wanasalimika kutokana na ulimi wake na mikono yake.

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ametufahamisha kuwa Yeye ndiye mmiliki wa vitu vyote na kwamba mambo yote yanatoka kwake, na kwamba **'Mwenyezi Mungu hatovunja ahadi yake'**[35].

Hivyo pia Muislamu hana budi kuchunga ahadi zake na kuwa muaminifu. Yani hana budi kutafakari 'sifa' za Mwenyezi Mungu.

Uaminifu ni hali ya kiimani ambayo inafunika maisha ya mwanadamu kwa kiwango kikubwa na pia ni sifa ya Mitume na watu wema. Kutokana na haya imepelekea baadhi ya wachambuzi wa Qur'an kuuelezea Uislamu kuwa ni kujisalimisha na kuwa muaminifu kwa Mwenyezi Mungu kwa lolote litakalotukuta, kwa kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi.

**5. Sadaqat (Uaminifu na kujitolea)**

Moja ya tabia njema zaidi kwa Mitume ni 'sidq/sadaqat' ikimaanisha kuwa mkweli katika maneno yako na dhati yako na kuwa msafi wa moyo na mtiifu.

Wakati wote Mitume walikuwa wakihamasisha uaminifu kwa kupitia wao wenyewe, maneno yao na maelekezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika kuelezea baadhi ya tabia za Mitume, Qur'an tukufu inaeleza kuwa **'Hakika yeye alikuwa mkweli, Nabii'** (Maryam, 19:41,56).

Pia Qur'an tukufu inaeleza:

"Ili Mwenyezi Mungu awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao " (Al-Ahzab 33:24).

35. Al Bakara 2:80; Al' Imran 3:9; Al Rad 13:31; Hajj 22:47; al Mu'minun 23:27; Al Rum 30:6; al Sajda 32: 13; Al Zumar 39:20; al Qaf 50:29.

Ili mtu awe na tabia kama hii hana budi kufanya juhudi kubwa. Jambo muhimu la kuzingatiwa limetajwa katika Qur'an:

"**Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli** " (Al-Tawba, 9:119).

Ina maana kwamba kuwa pamoja na wakweli kutampelekea mtu kuwa na uaminifu na itakuwa ndio njia ya kuwa na tabia kama zao. Shaykh Sadi-i Shirazi anaelezea umuhimu wa kuwa pamoja na wakweli na kinyume chake, yani madhara ya kujitenga nao, kama ifuatavyo:

"Qitmir, mbwa wa watu wa pangoni alipata hadhi kubwa kutokana na kuwa pamoja na wakweli na matokeo yake akatajwa ndani ya Qur'an[36]. Kwa upande mwingine wake za Nuhu na Lut wataingizwa motoni kwa sababu walichagua kuwa pamoja na waovu[37]".

Siku ya kiama wakati watu wapo kwenye shida kubwa na wakati ambao hakuna mtu atakayeweza kumsaidia mwingine, uaminifu utakuwa hazina yenye thamani kubwa mno. Wale walioona kuwa tabia zao katika dunia hii zitawapelekea kulipwa kesho akhera, wakati wa hitajio kubwa, watapata amani kwa msaada wa huu uaminifu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anaielezea siku hii kama ifuatavyo:

"**Mwenyezi Mungu atasema: Hii ndiyo Siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu milele. Mwenyezi Mungu amewawia radhi, nao wawe radhi naye. Huku ndiko kufuzu kukubwa**" (al-Maida, 5:119).

36. Angalia Al Kahf 18. Kwa kuongezea ni kwamba mfasiri aitwaye Bursevi anasema kuwa mbwa wa watu wa pangoni atakuwa ni katika wanyama wachache watakaoenda peponi, kutokana na kuwa pamoja na wakweli.
37. Angalia al Tahrim, 66:10

Pia Mwenyezi Mungu anaielezea siku hiyo katika aya nyingine:

**"Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake, na wat'iifu wanaume na wat'iifu wanawake, na wasemao kweli wanaume na wanawake, na wanao subiri wanaume na wanawake, na wanyenyekevu wanaume na wanawake, na watoao sadaka wanaume na wanawake, na wanao funga wanaume na wanawake, na wanao jihifadhi tupu zao wanaume na wanawake, na wanao mdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wanaume na wanawake, Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na ujira mkubwa"** (Al-Ahzab, 33:35).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaelezea umuhimu wa ukweli kama ifuatavyo:

"*Sidq* (ukweli) unampeleka mtu kwenye wema na wema unampeleka mtu peponi. Kama mtu ataendelea kusema ukweli atakuwa miongoni mwa *Siddiqun* (wakweli). Kudanganya kunampeleka mtu kwenye dhambi na dhambi inampeleka mtu motoni. Kama mtu ataendelea kusema uongo, Mwenyezi Mungu atamuandika kwenye orodha ya waongo" (Bukhari, Adab, 69; Muslim, Birr, 103-5).

❁

***Matukio ya wema***

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ndiye kilele cha ukweli. Hata maadui zake wakubwa kama vile Abu Jahl, Ahnes ibn Sharik, Nadr ibn Haris and Abu Sufyan (ambaye baadae aliingia katika Uislamu) waliukubali ukweli huu[38]. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kamwe hakuwahi kuongea neno la uongo na hata aliweza kuongea ukweli wakati anatania.

❁

38. Bukhari, Badu al-Wahy 6; Muslim, Jihad, 74; Taberi, Tafsir VII, 240; Ibn Kathir, Al Bidaya III, 113.

Kabla ya Abu Sufyan ﷺ kuingia kwenye Uislamu alikuwa miongoni mwa maadui wakubwa wa Uislamu. Siku moja alipokuwa ameenda kufanya biashara mahali fulani alifanya majadiliano marefu na mfalme wa Byzantine aliyeitwa Heraclius. Abu Sufyan ameyaelezea majadiliano yale kama ifuatavyo:

"Heraclius aliniuliza:

"Je umewahi kumtuhumu kuwa muongo kabla ya kudai kwake kuwa Mtume?"

Nikajibu: "Hapana".

"Je amewahi kuacha kuchunga ahadi zake?" aliuliza.

Nikajibu:

"Hapana. Kwa hakika alikuwa akichunga ahadi zake lakini kwa sasa tuko katika mchakato wa kufanya naye mkataba. Hatujui atafanya nini katika kipindi hiki". Sikupata maneno mengine ya kumchafua zaidi ya haya.

Heraclius akaniuliza kwa mara nyingine tena:

"Anawaamuru mfanye nini?"

"Anatuamuru kuwa watumishi wa Mwenyezi Mungu, tusimamishe swala, tutoe sadaka, tutoe zaka, tuishi kwa wema na tushikamane na ndugu zetu". Kisha Heraclius akasema:

"Kama unayoyasema ni kweli basi si muda mrefu mtu huyo ataitawala ardhi niliyosimamia sasa" (Bukhari, Bad-u al-Wahy, 6; Muslim, Jihad 74).

❀

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

"Niahidini vitu hivi sita na mimi nitawahakikishia pepo:

1. Pindi mnapoongea, semeni ukweli!

2. Pindi mnapoahidi, chungeni ahadi zenu.

3. Kuweni waaminifu pindi mnapopewa amana.

4. Lindeni heshima yenu.

5. Yalindeni macho yenu kutokana na kuangalia yaliyokatazwa.

6. Wekeni mikono yenu mbali na vitu vilivyokatazwa" (Ahmad, V, 323).

❁

Abdullah ibn Amir ﵁ anasimulia:

"Siku moja mama yangu aliniita wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amekaa ndani ya nyumba yetu. Mama yangu akaniambia:

"Njoo nikupe kitu". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza:

*"Unafikiria kumpa nini?"*

Mama yangu akajibu:

"Nilitaka kumpa tende". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Jua kuwa kama usingelimpa chochote basi ungeliandikiwa dhambi ya kudanganya"* (Abu Dawud, Adab, 80/4991; Ahmad, III, 447).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimsogelea muuzaji sokoni. Aliweka mkono wake juu ya fungu la ngano na kugundua kuwa lina umaji maji. Akamuuliza muuzaji:

*"Ni nini hiki?"*. Yule mtu akajibu:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Lililoa kutokana na mvua”. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

*“Je ulishindwa kuweka sehemu iliyoloa juu ili watu waione. Yeyote anayedanganya si katika sisi”.* (Muslim, Iman, 164).

Hivyo waislamu kwa namna yoyote ile, katika hali zote na matendo yote hawaruhusiwi kuiacha njia ya uaminifu na ikapelekea kumdanganya mtu yeyote.

❁

Maswahaba watukufu na wale waumini wema ambao walifuata njia yao, walikuwa wakisafiri hata kwa mwezi mzima chini ya magumu ya wakati ule ili tu kukusanya *hadith* kutoka kwa msimulizi wa *hadith*. Kutokana na mafunzo kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, walifikia hali kama hii ya wema kiasi kwamba walipomuona mtu akijaribu kumuita mnyama kwa kumuonyesha mfuko mtupu usio na chakula walipoteza uaminifu juu ya mtu huyu na hawakumchukulia kuwa mtu tabia njema. Yani hawakuamini kuwa mtu yule aliyejaribu kumdanganya hata mnyama kama angelistahiki kusambaza hadith kwa sababu hakuishi kama ulivyokuwa mwenendo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ.

❁

Imam Malik (rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) anasimulia:

“Kama alivyoniambia, siku moja Luqman Hekim aliulizwa:

“Ni kipi kiini cha tabia zako na maadili yako mema tunayokuona nayo?”

Alijibu:

“Uaminifu, kutekeleza ahadi, kuachana na lisilokuhusu na kuchunga ahadi zangu” (Muwatta, Kalam, 17).

❁

Pindi mtu alipotaka kuwafahamisha washirikina juu ya matukio yaliyotokea katika safari yake ya usiku na usiku wa kupanda mbinguni, alimwambia Jibril:

"Ewe Jibril! Watu wangu hawataniamini".

Jibril عليه السلام akajibu:

"Abu Bakr atakiri utakalolisema. Yeye ni as-Siddiq". (Ibn Sa'd, I, 215).

Matokeo yake washirikina waliposikia kuhusu matukio ya kupanda mbinguni walienda moja kwa moja kwa Abu Bakr رضي الله عنه na kumwambia:

"Rafiki yako anasema kuwa eti usiku mmoja ameenda mpaka msikiti wa Aqsa na tokea pale akapanda mbinguni na kurejea Makka kabla ya asubuhi. Unasemaje kuhusu jambo hili?"

Kwa kuonyesha uaminifu wa kweli kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, Abu bakr رضي الله عنه akajibu kwa shauku kubwa:

"Kama hayo ndiyo aliyoyasema basi ni kweli. Kwani hakuna namna yoyote wala uwezekano wa yeye kudanganya. Naamini kuanzia mwanzoni chochote anachokisema na kukileta..."

Washirikina wakamuuliza kwa mara nyingine tena:

"Unakiamini anachokisema...kuwa ameenda Baytu'l Maqdis kwa usiku mmoja?"

"Ndio. Ni kipi cha kushangaza hapo? Naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa ameniambia kuwa habari kutoka kwa Mwenyezi Mungu zinamjia katika wakati wowote wa siku na mimi namuamini kwa hayo".

Baadae Abu Bakr رضي الله عنه alienda kwenye Al-Kaaba ambapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amekaa. Alisikiliza

matukio yale kutoka kwenye kinywa cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mwenyewe na kisha akasema:

"Umesema kweli ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitabasamu kwa tabasamu lililotia nuru dunia kama ishara kuwa alifurahishwa mno na uthibitisho huu wa Abu Bakr ؓ na kisha akamwambia:

*"Ewe Abu Bakr! Wewe ni Siddiq (mkweli)"* (Ibn Hisham, II, 5).

Kuanzia siku ile Abu Bakr ؓ akawa maarufu kwa jina lake la kupanga la *as Siddiq.*

Huu ndio uaminifu unaopatikana ndani ya imani... Kinachotakiwa pekee ni kutafuta ukweli na kushikamana nao.

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alinunua farasi kutoka kwa Bedui. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuomba Bedui yule amlete farasi yule nyumbani kwake ndio amlipe. Akaharakisha kumtangulia, lakini kwa kuwa Bedui alikuwa akitembea taratibu aliachwa nyuma. Katika kipindi kile baadhi ya watu wakaja kwa Bedui na kumbembeleza awauzie yule farasi na kujaribu hata kutoa kiasi kikubwa cha fedha. Hawakujua kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa tayari amemnunua farasi yule. Bedui akamuita Mtume:

"Kama unamtaka farasi huyu mchukue, kinyume chake nitamuuza". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipoisikia sauti yake akageuka nyuma na kusema:

*"Tayari nimeshamnunua kutoka kwako"*. Lakini Bedui akaanza kukataa:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu sijakuuzia".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Hapana, nimemnunua kutoka kwako"*.

Hapa Bedui akasema:

"Muite shahidi". Mara Huzayma ibn Thabit ﵁ akajitokeza mbele:

"Mimi ni shahidi kuwa umemnunua kutoka kwake" alisema.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuinamia Huzayma ﵁ na kumuuliza:

*"Wewe haukuwa na sisi wakati tunapatana, sasa unawezaje kuwa shahidi?"*. Kisha Huzayma ﵁ akasema:

"Naweza kuwa shahidi kwa kuwa nakuamini ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu".

Kutokana na uaminifu huu mkubwa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaufanya ushahidi wa Huzayma ﵁ kuwa mzito kama ushahidi uliotolewa na mashahidi wawili. (Abu Dawud, Aqdiya, 20/3607; Nasai, Buyu, 91; Ahmad, V, 215-6).

Kutokana na mapokezi haya baadae Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuuliza Huzayma ﵁:

*"Haukuwa pamoja na sisi wakati wa biashara, ni kipi kilichokupelekea kutoa ushahidi?"*

"Ninauamini ujumbe uliokuja nao na hivyo ninajua kuwa husemi chochote kile kinyume na ukweli".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Kama Huzayma ﵁ atatoa ushahidi kumuunga mtu mkono au dhidi yake basi utatosha kuwa ushahidi sawa na watu wawili"*.

Huu ni mfano mmoja tu wenye kuonyesha kilele cha uaminifu juu ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake...

❁

Ka'b ibn Malik ﵁ alikuwa akiongozana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika misafara yake yote ya kivita. Hata hivyo siku moja alichelewa kujiunga na msafara wa kuelekea Tabuk. Jeshi liliondoka na kumuacha Ka'b ﵁ Madina. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliporejea kutoka kwenye msafara ule watu wote wasioshiriki walitoa nyudhuru lakini Ka'b ﵁ na wengine wachache ndio waliosema ukweli na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu. Aya iliyowataarifu kuwa walikuwa wamesamehewa ilishuka siku 50 baadae. Kabla ya muda huu walikuwa katika mahangaiko makubwa. Licha ya upana wake dunia ilikuwa nyembamba mno kwao. Lakini kwa kuwa waliomba toba kwa moyo safi walipata msamaha wa Mwenyezi Mungu. Ka'b ibn Malik ﵁ ambaye alishikamana na ukweli na kukubali kosa lake anaelezea faida alizopata kutokana na ukweli wake kama ifuatavyo:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa neema kubwa niliyojaaliwa baada ya kuingia kwenye Uislamu ni kusema ukweli mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kunusurika kuangamizwa pamoja na waongo. Kwani Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alitufahamisha kuhusu mwisho wa wale ambao hawakushiriki katika msafara wa kivita kuelekea Tabuk na ambao walidanganya katika kutoa nyudhuru zao, katika aya ifuatayo:

"**Watakuapieni kwa Mwenyezi Mungu mtakapo rudi kwao ili muwaachilie mbali. Basi waachilieni mbali. Hakika hao ni najsi, na makaazi yao ni Jahannamu, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyachuma. Wanakuapieni ili muwe radhi nao. Basi hata mkiwa radhi nao nyiye, Mwenyezi Mungu hawi radhi na watu wapotofu**" (Al-Tawba, 9:95-96) (Bukhari, Mahazi, 79).

Baada ya vita vya Uhud wanawake wa Madina wakaenda kwenye viunga vya mji kwa matumaini ya kupata habari. Aisha ﵂ alikuwa ni miongoni mwao. Hind alikuwa amebeba miili ya mumewe, Amr ibn Jamuh, mwanae Hallad, na kaka yake Abdul-

lah, ambao waliuawa kwenye vita na akiwa anairudisha Madina. Aisha ﵂ akamuuliza:

"Kuna habari gani huko?"

Hind bint-i Amr ﵂ akajibu:

"Kuna habari njema. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yuko hai! Hali ya kuwa yuko hai habari zote nyingine mbaya hazina umuhimu". Huku akiashiria miili iliyopo juu ya ngamia Aisha ﵂ akauliza:

"Hao ni nani?" Mwanamke yule mwema akajibu:

"Kaka yangu Abdullah, mwanangu Hallad na Mume wangu Amr".

Aisha ﵂ akamuuliza:

"Anawapeleka wapi?". Hind akajibu:

"Nawapeleka Madina kwa ajili ya kuwazika".

Hind alipojaribu kumlazimisha ngamia atembee aliporomoka chini. Aisha ﵂ akamwambia:

"Je hiyo inatokana na mzigo mzito uliopo juu yake?" Hind akajibu:

"Sijui kwa nini ameanguka. Wakati mwingine anaweza kubeba mara mbili ya uzito huu. Lakini kwa sasa nahisi kitu tofauti na ngamia huyu".

Alipolazimishwa kwa mara nyingine tena akanyanyuka. Lakini alipogeuziwa Madina akaporomoka tena. Hata hivyo alipogeuziwa Uhud alianza kukimbia. Hind akarudi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuelezea kilichotokea. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

*"Ngamia ana jukumu la kutekeleza. Je Amr aliacha wosia?"*

Hind akajibu:

“Pindi Amr alipokaribia kwenda Uhud aligeukia uelekeo wa Madina na kuomba: “Ewe Mwenyezi Mungu. Nijaalie nife shahidi. Na usinirudishe katika familia yangu katika hali ya kusikitisha na kukatisha tamaa”.

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema yafuatayo katika kuonyesha utukufu wa uaminifu juu ya neno la mtu:

*“Hiyo ndiyo sababu ngamia hataweza kwenda. Enyi Answar. Yeyote kati yenu atakayeweka ahadi kwa Mwenyezi Mungu, na aitimize. Ewe Hind, mume wako Amr ni miongoni mwa wakweli. Tokea auawe malaika walimfunika kwa mabawa yao na kuangalia wapate pa kumzika. Ewe Hind! Amr ibn Jamuh, mwanao Hallad na kaka yako Abdullah watakuwa pamoja peponi”.*

Kutokana na habari hizi njema Hind akasema:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Tafadhali niombee kwa Mwenyezi Mungu nije kuwa pamoja nao”. (Waqidi, I, 265-66; Ibn Hajar, Fathu’l Bari, III, 216; Ibn Abdilbar, Al-Istiab, III, 1168).

❁

Kabla ya mkataba wa Hudaybiya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amemtuma Othman رضي الله عنه kwenda Makka kukutana na Maquraysh. Upesi Othman رضي الله عنه aliondoka kwenda Makka kama alivyoagizwa. Aliwaelezea washirikina kuwa lengo lao ni kutekeleza hijja ndogo na kurudi upesi. Licha ya hili lakini washirikina walikataa kuwaruhusu. Cha zaidi ni kuwa walimuweka Othman رضي الله عنه kizuizini na kumwambia:

“Kama unataka unaweza kufanya *tawaf* (kuzunguka) katika Al-Kaaba”...

Waislamu walikuwa na shauku kubwa na tamaa ya kufanya *tawaf* katika Al-Kaaba. Ukweli ni kwamba kulikuwa na wengi

waliomuonea wivu Othman ﷺ kwa kudhani kuwa atafanya *tawaf*. Wengine walikuwa na wasiwasi kuwa labda Othman ataonyesha uaminifu na kutokuwa mbinafsi na kukataa kufanya *tawaf* mpaka waislamu wote waruhusiwe kufanya hivyo.

Hali ikawa kama walivyodhania kundi la pili. Kama uthibitisho wa uaminifu wake, swahaba huyu muaminifu ambaye alijitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake aliwaambia washirikina:

"Hali ya kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wetu aliyebarikiwa hafanyi *tawaf*, na mimi pia sitaifanya. Nitaitembelea nyumba ya Mwenyezi Mungu pale tu yeye akiwa mbele yangu. Siwezi kuwa mahali ambapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amekataliwa"... (Ahmad, IV, 324).

❁

Licha ya kujulikana kwa tabia yake ya kughadhibika sana, Yavuz Sultan Selim Han pia alikuwa na moyo wenye hofu na laini. Hata hivyo imani juu ya umuhimu wa umoja na kuiendeleza dola yao iliwapelekea Masultani wa dola ya Uthmainiyya kufanya maamuzi magumu mno. Mfano mmoja wapo ni kwamba Yavuz Sultan Selim alilazimika kumuua kaka yake Korkut. Matokeo yake alihudhuria katika mazishi yake na kulibeba jeneza mwenyewe na kusema huku analia:

"Ewe kaka yangu! Kama usingelikuwa umefanya ulichokifanya, basi nisingelitakiwa kufanya nilichokifanya".

Alimsifu Piyale, mtumishi muaminifu wa Korkut kama ifuatavyo:

"Ninakusamehe kwa sababu ya uaminifu wako ambao ni wema mkubwa. Na kama zawadi kwa uaminifu wako nitaku-

teua kwenye nyadhifa yoyote utakayoitaka. Unaweza kuwa waziri mkuu wangu kama ukipenda".

Piyale alimshukuru na kwa kuthibitisha uaminifu wake zaidi akajibu:

"Sultani wangu! Kuanzia sasa jukumu langu ni kulilinda kaburi la bwana wangu Korkut..."

❁

Kwa kifupi muumini hana budi kuwa mkweli katika maneno yake, dhati yake na katika malengo yake na aandikwe miongoni mwa 'wakweli'. Hivyo atayaona manufaa ya ukweli wake hapa duniani na kesho akhera. Uzuri ulioje namna Ziya Pasha alivyolielezea jambo hili:

*"Ni ukweli tu ndio unaomfaa mtu, hata kama atakutana na upinzani. Kwani Mwenyezi Mungu ni msaidizi wa mambo yote ya kweli"*

**6. Kuikubali hali yako**

Vyote furaha kupita kifani na maumivu kupita kifani vinajumuisha mtego mkubwa kwenye nafsi ya mwanadamu. Kwa upande mwingine kuikubali hali yako, subira na kumtegemea Mwenyezi Mungu ni sifa za kipekee za waumini ambao wamefikia katika ukamilifu wa imani.

Kanuni kuu ya furaha ni kuwa akili inafuata mapokezi, moyo unapambwa na tabia njema na mtu anayakubali mabadiliko ya kushangaza katika maisha yake. Pia furaha ya kweli inawezekana pale tu mtu atakapokubali shida na raha katika maisha, pale mtu atakapovumilia magumu na kujaribu kujifanyia mageuzi mwenyewe na kuangalia wema wa kila jambo na kujisalimisha kwa Mola wa walimwengu wote.

Uzuri ulioje wa ushauri ufuatao kutoka kwa Luqman Hakim:

*"Mwanangu! Usiugubike moyo wako kwa huzuni na wasiwasi. Kuwa makini na tamaa. Kuwa mwenye kuikubali hali yako. Kuwa mwenye kuridhika na kile Mwenyezi Mungu alichokujaalia ili maisha yako yawe mazuri, moyo wako ujawe na furaha na uweze kupata raha ya maisha"*.

Kuwa mwenye kukubali matukio yenye kukuletea furaha na kukasirikia matukio yenye kuhuzunisha na kutia wasiwasi ni jambo lisiloendana na Uislamu. Pia hali ya kuwa mwanadamu hajafikia kilele cha ukamilifu wa imani, itakuwa ngumu kwake kuepukana na udhaifu huu wa kibinadamu. Kwa upande mwingine pindi atakapoisafisha nafsi yake na kufikia katika hali ya kutosheka, ataweza kujisalimisha bila ya kusita na kuridhika na kanuni za maumbile yake ambazo zinatokana na uwezo wa Mwenyezi Mungu, ziwe ni nzuri au mbaya. Kamwe hawezi kulalamika. Uzuri ulioje wa habari njema juu ya watu hao:

"**Ewe nafsi iliyo tua! Rejea kwa Mola wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha. Basi ingia miongoni mwa waja wangu, Na ingia katika Pepo yangu**" (Al-Fajr, 89:27-30).

Ni rahisi kwa mtu kukifanya kitu anachokipenda au alichokikubali au kukivumilia. Kilicho rahisi kitafanywa bila ugumu, katika utulivu na furaha. Kwa muumini ambaye anampenda Mwenyezi Mungu, kila kitu kitakachokuja kutoka Kwake kitakuwa kirahisi na kitatoa raha na furaha.

Wale watu wema wenye imani wataridhishwa na makadirio ya Mwenyezi Mungu. Wanafahamu kuwa hakuna jambo lolote baya litakalompata mtu ila 'limeshaandikwa' na Mwenyezi Mungu. Ndio maana kila jambo linalowapa katika dunia hii ni dogo mno ukilinganisha na maumivu ya kesho akhera.

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anawashushia watu hao amani. Kiukweli ni kwamba funuo mbalimbali kutoka kwa Mwenyezi Mungu machoni mwao ni bora mara elfu moja kuliko ndoto zenye kudanganya na mazigazi za hapa duniani. Kwani wao wamejitoa kwenye yale mambo ambayo watu wengi wanayakimbilia na kuyaona kuwa ni neema.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa amesema:

*"Ukubwa wa malipo ya mtu unatokana na uzito wa mitihani yake. Mwenyezi Mungu amejaalia mitihani iwapate wale anaowapenda. Yeyote atakayekubaliana na lolote litakalomfika basi Mwenyezi Mungu atakuwa radhi naye. Na yeyote ambaye hataridhika atakutana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu"* (Tirmidhi, Zuhd, 57/2396; Ibn Majah, Fitan, 23).

Katika *hadith* nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Mbele ya Mwenyezi Mungu muumini mwenye imani kubwa ni mbora na mwenye kumridhia kuliko muumini mwenye imani dhaifu. Lakini kote kuna wema. Huna budi kuchukua kile kitakachokunufaisha. Muombe Mwenyezi Mungu msaada na usionyeshe udhaifu. Pindi jambo lolote litakapokufika usihuzunike na kusema: 'Lau kama ningelifanya hili, hili na hili lingelikuwa limetokea' badala yake sema: 'Huu ni mpango wa Mwenyezi Mungu. Anafanya atakalo'. Kifungu 'lau kama' kinafungua mlango wa matendo yanayomfurahisha Shetani"*. (Muslim, Qadr, 34; Ibn Majah, Muqaddima, 10).

Mtu ambaye haridhiki na hali yake na anasema 'lau kama ningelifanya hili na lile', atapatwa na mambo ambayo ni kinyume na imani kama vile kutotosheka, kukataa makadirio yako na kuchukia uwezo wa Mwenyezi Mungu. Na matendo haya yanampendeza sana Shetani na yanamuangamiza mtu. Kwa upande

mwingine kuridhika na hali yako kutakupelekea kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Baada ya kutaja aina zote za furaha katika dunia hii na kesho akhera, Qur'an inasema: "**Mwenyezi Mungu amewaahidi Waumini wanaume na Waumini wanawake Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na makaazi mema katika Bustani za kudumu, na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote. Huko ndiko kufuzu kukubwa**" (Al-Tawba, 9:72).

***Matukio ya wema***

Usama ibn Zayd ﷺ anasimulia:

"Siku moja Zainab, mtoto wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtumia baba yake ujumbe:

"Mtoto wangu anakaribia kufa, tafadhali njoo". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ naye akarudisha salamu kwa binti yake, akasema:

*"Anayetoa na kuchukua ni Mwenyezi Mungu. Kila kitu kina muda wake. Mwambieni awe na subira na asubirie malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu".*

Binti yake akamtumia tena ujumbe:

"Tafadhali mwambie afanye hima aje".

Wakati huu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akanyanyuka na kwenda kwenye nyumba ya binti yake akiwa pamoja na baadhi ya maswahaba zake kama vile Sa'd ibn Ubada ﷺ, Muadh ibn Jabal ﷺ, Ubayy ibn Ka'b ﷺ and Zayd ibn Thabit ﷺ. Wakamkabidhisha yule mtoto kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alimchukua mikononi mwake. Mtoto yule mdogo alikuwa akipumua kwa shida. Machozi yakaanza kutiririka kutoka kwenye macho yaliyobarikiwa ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Baada ya kuliona hili Sa'd ibn Ubada ﷺ akauliza:

"Ni hali gani hii ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akajibu:

*"Hii ni hisia ya huruma ambayo Mwenyezi Mungu ameiweka ndani ya nyoyo za waja wake anaowapenda. Na Mwenyezi Mungu atawaonea huruma wale waja wake wenye kuhurumiana wao kwa wao"* (Bukhari, Janaiz, 33, Ayman 9, Marda 9; Muslim, Janaiz 9,11).

Salamu ya kwanza na ushauri alioutuma Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa binti yake ulikuwa katika hali ya kuridhika na makadirio ya mtu. Jambo la muhimu ni kuweza kuridhika na kujisalimisha kwenye makadirio yako wakati yanatokea licha ya uchungu. Hali ya pili ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ haikuwa kama baadhi ya maswahaba walivyokuwa wakifikiria mara ya kwanza, kuikataa qadari kwa kupiga kelele, kulia na kurarua nguo mambo ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyakemea, lakini ilikuwa ni udhihirisho wa hisia za huruma ambazo Mwenyezi Mungu amejaalia kwa waja wake.

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametufahamisha juu ya malipo ya muumini ambaye ameridhika na makadirio yake kama ifuatavyo:

*"Pindi mtoto wa mja anapofariki Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi huwaambia malaika:*

*"Je mmeitoa roho ya mtoto wa mja wangu?" Malaika hujibu:*

*"Ndio, Mola wetu". Kisha Mwenyezi Mungu husema:*

*"Je mmevunja tunda la moyo wake?"*

*"Ndio, Mola wetu" malaika hujibu kwa mara nyingine tena. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi husema:*

*"Na ni kitu gani alichokisema mja wangu?" Malaika hujibu:*

*"Alikusifu Wewe na kujikinga kwako pekee kwa kusema: 'Inna lillahi wa inna ilayhi raji'uun'...*'**Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea'** (Al-Baqara, 2:156).

*Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi husema:*

*"Kama ni hivyo basi mjengee mja wangu nyumba peponi na uiandike 'Nyumba ya kusifu"* (Tirmidhi, Janaiz, 36/1021).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ameeleza:

*"Pindi mja anapokuwa mgonjwa, Mwenyezi Mungu hutuma malaika wake wawili na huwaambia:*

*"Nendeni mkaangalie, ni kipi mja wangu anawaambia wasaidizi wake".*

*Kama wale malaika wakifika wanamkuta mja anamsifu Mwenyezi Mungu, wanatuma taarifa hii kwa Mwenyezi Mungu, (ambaye hata hivyo anajua kila kitu). Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi, ambaye alituma malaika wake kwa lengo kuwa mashahidi juu ya matendo ya mja husema:*

*"Kama nitachukua roho ya mja wangu, kumuingiza peponi ni haki yake kwangu. Kama nitamponya, ni haki yake kwangu kumbadilishia mwili wake kwa ulio bora zaidi, kubadili damu yake kwa iliyo bora zaidi, na kumsamehe madhambi yake" (Muwatta, Ayn, 5).*

❁

Abu Huraira رضي الله عنه anasimulia:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaambia maswahaba zake:

*"Ni nani atakayechukua haya maneno yangu na kuwafundisha wengine ili waishi kulingana nayo?"*

Upesi nikanyanyuka juu.

"Mimi nitafanya hivyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akanishika mkono na kuniambia mambo matano yafuatayo:

*"Kuwa makini na vitu vya haramu na utakuwa mja wa Mwenyezi Mungu mwenye kufanya ibada".*

*"Kama utatosheka na kile Mwenyezi Mungu alichokupangia, basi utakuwa mtu tajiri kuliko wote".*

*"Mfanyie wema jirani yako na wewe utakuwa muumini wa kweli".*

*"Wapendelee wenzako kile unachokipendelea wewe ili uwe Muislamu bora".*

*"Usicheke kupita kiasi, kucheka sana kunaua moyo".* (Tirmidthi, Zud, 2/2305; Ibn Majah, Zuhd, 24).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amekaa pamoja na Abu Bakr ﵁. Abu Bakr alikuwa amevaa joho kuu kuu. Lilikuwa kuu kuu mno kiasi kwamba alilifunga kwa vipande vya mbao kifuani kwake.

Wakati ule Malaika Jibril akajitokeza. Alimsalimia kwa maamkizi ya amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kumwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni hali gani hii ya Abu Bakr? Amevaa nguo kuu kuu na ameifunga pembe zake kwa vipande vya mbao?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Ewe Jibril! Alitumia kila kitu alichokuwa nacho kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu kabla ya kuitwaa Makka, hiyo ndiyo sababu iliyomfanya awe katika hali hii"*. Kisha Jibril akasema:

"Mpe maamkizi ya amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Mwambie: 'Mola wako anakuuliza: Je unanifurahia kutokana na hali hii ya umasikini na uhitaji uliyokuwa nayo au unalalamika juu ya hali hii?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimgeukia rafiki yake na kumwambia:

"*Ewe Abu Bakr! Jibril yuko hapa na amekuletea maamkizi ya amani kutoka kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Mola wetu anataka kujua ikiwa unaridhika na hali yako ya umasikini na uhitaji uliyokuwa nayo hivi sasa, na hivyo unamfurahia Mwenyezi Mungu au una malalamiko yoyote?*".

Abu Bakr ؓ hakujua cha kufanya kutokana na furaha aliyokuwa nayo mbele ya hisani hii. Alijihisi ulimi umefungwa. Alilia na kulia kwa muda kisha akasema:

"Je mimi ni wa kulalamika kwa Mola wangu? Ninamridhia Mola wangu! Ninamridhia Mola wangu! Ninamridhia Mola wangu!" (Abu Nuaym, Hilya, VII, 105; Ibn al-Jawziya, Sifat as-Safwa, I, 249-250).

❀

Kutokana na mapokezi mbalimbali tunakuta kuwa siku moja nabii Yunus عليه السلام alimuuliza Malaika Jibril:

"Je unaweza kunionyesha mtu mwenye kufanya ibada kupita watu wote kwenye uso wa dunia?"

Jibril alimuonyesha mtu ambaye mikono yake na miguu yake imeoza kutokana na ukoma na ambaye amepoteza jicho moja. Licha ya yote haya mtu yule alikuwa akiendelea kusema:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Chochote nilichopewa kwa kupitia mikono hii na miguu ni kutoka kwako. Chochote kilicho mbali na mimi ni wewe uliyekifanya kiwe mbali na mimi. Ewe Mwenyezi Mungu. Umebakiza jambo moja tu la kunifanyia, na jambo lenyewe ni kunikutanisha na wewe"

❁

Nabii Ayub (a.s) alikuwa akipitia wakati mgumu katika maradhi yake. Mke wake Rahima Hatun aliniambia:

"Wewe ni nabii. Kwa nini humuombi Mwenyezi Mungu akurudishie afya na ustawi wako kiasi kwamba uwe huru na maradhi haya?" Ayub akajibu:

"Ni siku ngapi zimepita tukiwa na afya njema na ustawi?" Rahima Hatun akajibu:

"Miaka 80". Kisha Ayub akasema:

"Ewe Rahima! Mwenyezi Mungu Mtukufu amenijaalia miaka 80 ya afya. Kipindi cha kuumwa kwangu ni kidogo mno ukilinganisha na kipindi nilichokuwa na afya. Kutokana na hali hii naona aibu kulalamika kwa Mwenyezi Mungu kuhusiana na maradhi yangu. Tunafurahia sana pale ambapo Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapotujaalia neema, sasa kwa nini tusiwe na subira pale tunapofikwa na mitihani kutoka kwake? Nimeridhika na Mola wangu".

Mwenendo huu wa nabii Ayub ni mfano mzuri wa ukinaifu. Licha ya tabu zote alizozipata lakini alijizuia na kulalamika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu ugonjwa wake na kumuomba amjaalie afya na ustawi, ameyafanya haya kwa kuhofia kukosa radhi za Mwenyezi Mungu juu ya makadirio yake. Hata hivyo kutokana kusisitizwa mno na mkewe akaamua kuomba dua ifuatayo:

“**Na Ayyubu, alipo mwita Mola wake Mlezi, akasema: Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unaye rehemu kuliko wote wanao rehemu**” (Al-Anbiya 21:83).

Kutokana na dua hii Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alimuondolea kadhia ile kama ukumbusho wa huruma Yake kwa wale waja wake wanaokinai katika utumishi wao. Alimtibu na kumjaalia tena mali na watoto. Katika kuonyesha uvumilivu na shukurani na kuridhika na hali uliyonayo, Mwenyezi Mungu Mtukufu amemsifu nabii Ayub kama ifuatavyo: **“Na shika kichwa cha vijiti tu mkononi mwako, kisha ndio upigie nacho, wala usivunje kiapo. Hakika tulimkuta mwenye subira, mbora wa waja, kwa hakika alikuwa mwingi wa kutubu”** (Sa’d, 38:44).

❁

Katika kisa kifuatacho Rumi anatuelezea namna upendo na urafiki wa kweli unavyowezekana pale mtu atakapoonyesha wema juu ya maumivu na magumu atakayoyapata kutoka kwa rafiki yake na kwa kukubaliana na hali yake:

“Siku moja marafiki wa karibu walienda kumtembelea mtu mmoja na huku wamebeba tikiti maji kama zawadi. Yule mtu akamuita mtumishi wake aliyekuwa mtiifu mno kwake aliyeitwa Luqman, alikuwa akimpenda sana mtumishi huyu na alimfanya kuwa msiri wake.

Pindi Luqman alipofika pale bwana wake alikata kipande cha tikiti maji na kumpa. Luqman alikila kipande kile utadhani kilikuwa ni asali au sukari. Alikila kwa namna ya furaha na raha kiasi kwamba wale waliomuona nao wakapata hamu ya kulila na hivyo wakamuonea wivu. Bwana wake akampa kipande cha pili kutokana na furaha aliyoipata mtumishi wake mtiifu kwa kile kipande cha kwanza. Mwishoni kikabaki kipande kimoja tu cha tikiti maji. Kisha bwana wake akasema:

"Ngoja nile kipande hiki nione tikiti maji lina utamu kiasi gani". Lakini mara tu baada ya kulila mdomo wake nusu uungue kutokana na uchungu wa tikiti maji lile. Mara ulimi wake ukaota malengelenge na koo lake likaathirika pia. Akamwambia Luqman:

"Ewe mtumishi wangu mpendwa. Uliwezaje kuila sumu hii kana kwamba ilikuwa ni kitu kitamu mno? Umewezaje kukichukulia kitu hiki kisichoweza kuvumilika kuwa ni neema? Ni subira gani hii? Nani anajua ni kiasi gani cha maumivu uliyoyavumilia kwa ndani ili kuwa na subira na kujizuia kukunja sura yako. Je wewe ni adui wa roho yake iliyo nzuri? Kwa nini hukusema chochote? Kwa nini angalau hukusema: 'Tafadhali samahani sitakula sasa hivi'?"

Luqman akajibu:

"Nimekula chakula hicho kitamu kutoka kwenye mikono yako ewe bwana wangu. Nimepokea chakula hicho hadimu kimwili na kiroho kutoka kwako kwa namna ambayo ni aibu kwa kushindwa kuonyesha fadhila. Nitawezaje kusemea kitu ulichonipa kwa mikono yako mwenyewe kuwa: "Hiki ni kichungu hivyo siwezi kukila". Hata hivyo chochote kichungu kinachotoka kwenye mikono yako kwangu ni kitamu. Kwani kila kiini hai katika mwili wangu kimelishwa na mali zako".

Kisha Luqman akaendelea kuonyesha hisia zake kwa raha na kwa maneno yaliyojawa na upendo:

"Bwana wangu. Kama nitakuja kulalamika juu ya kitu chochote chenye maumivu kutoka kwako basi acha nitupiwe uchafu. Inawezekanaje mkono wako ambao daima uko katika hali ya kutoa usababishe maumivu? Ni kwa kupitia upendo maumivu yanakuwa utamu na shaba inabadilika na kuwa dhahabu. Kwa kupitia upendo mawingu na ukungu vinaondolewa na kuacha uwazi. Upendo unayafanya magonjwa yasiyotibika yatibike. Upendo

unakipa uhai kilichokufa. Upendo unawageuza masultani kuwa watumwa. Upendo unageuza magereza kuwa bustani la mawaridi. Upendo unaleta nuru kwenye nyumba zenye giza. Kutokana na upendo moto unakuwa nuru. Kutokana na upendo mwanamke mbaya anakuwa mwanamwali mrembo. Kutokana na upendo wasiwasi, hofu na huzuni vinakuwa furaha. Wale walioiacha njia na wanyang'anyi wanakuwa viongozi wa furaha kutokana na upendo. Ni kutokana na upendo ndio maana ugonjwa unabadilishwa na kuwa afya na ustawi. Kutokana na upendo huzuni inakuwa rehema".

Hii ni alama ya wazi ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na hali ya ukinaifu wa kweli.

❁

Kila Omar ibn Abdulaziz alipokuwa anaulizwa:

"Unapenda kitu gani?" alikuwa akijibu:

"Ninapenda chochote kilichopo kwenye qadari yangu. Ninapenda qadari ya Mwenyezi Mungu"...

❁

Majadaliano yafuatayo kati ya bwana na mtumishi wake ni muhimu kuyafahamu:

Siku moja mtu mmoja alimnunua mtumwa. Mtumwa yule alikuwa ni mtu mwema na muumini wa kweli. Baada ya bwana yule kumpeleka mtumwa yule nyumbani mjadala ufuatao ulianza kati yao:

Bwana akasema:

"Ungependa kufanya nini hapa nyumbani?"

Mtumwa akajibu:

“Chochote utakachoniambia nifanye”

“Ni nguo za aina gani unazopenda kuzivaa?” bwana yule akamuuliza.

Mtumwa akajibu:

“Chochote utakachonipa nivae”.

“Ungependa kulala katika chumba gani?” aliulizwa tena.

“Chumba chochote utakachonipangia nilale” mtumwa alijibu.

“Ni ipi kati ya kazi zangu ungelipenda kuifanya?” aliulizwa tena.

“Kazi yoyote utakayopenda niifanye” mtumwa alijibu.

Baada ya jibu hili la mwisho, bwana yule alitafakari kidogo na kisha huku machozi yanamtiririka usoni mwake akasema:

“Lau kama ningelijisalimisha kwa Mola wangu kwa namna hii, furaha iliyoje ningekuwa nayo!...

Wakati ule mtumwa akasema:

“Ewe bwana wangu. Je mtumwa anaweza kutekeleza matakwa yake na kujichagulia tofauti na matakwa ya bwana wake?”

Kisha bwana wake akasema:

“Ninakuacha huru. Uko huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo ningelipenda ukae na mimi ili nikutumikie kwa uhai wangu na mali zangu”...

Yeyote anayemfahamu Mwenyezi Mungu kikweli atajisalimisha kwake kwa mapenzi ya kweli, na kama ataridhika na alichokadiriwa naye, basi ataweka pembeni uwezo wake na uhuru wa kuchagua. Atakachosema pekee ni:

"Mimi ni nani kuomba kitu chochote kile kwa Mwenyezi Mungu"...[39]

❁

Siku moja mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu aitwae Sunbul Sinan Efendi aliwauliza wafuasi wake:

"Hebu fikirieni kana kwamba Mwenyezi Mungu amewapa mamlaka ya kutawala ulimwengu huu, mngelifanya nini?"

Wanafunzi wake walistushwa na swali hili ambalo kamwe hawajawahi kukutana nalo. Hata hivyo hawakutaka kuwa watovu wa nidhamu kwa kuacha kulijibu hivyo walitoa michango yao mbalimbali:

"Mwalimu, nisingelimuacha hata kafiri mmoja aishi katika uso wa dunia".

"Ningelifuta uovu wote".

"Ningeliwaondoa wale wote wanaokunywa pombe".

Hata hivyo mmoja miongoni mwao alikuwa kimya na hakujibu kabisa. Mwalimu wake alimgundua na kumuuliza huku anamuangalia:

"Mwanangu. Na wewe ungelifanya nini?"

Yule mwanafunzi ambaye uso wake ulikuwa umefifia, kutokana na maadili yake na unyenyekevu wake mkubwa alisema:

"Mwalimu wangu. Je kuna kasoro katika usimamizi wa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi juu ya ulimwengu huu kiasi cha kunitaka mimi nifanye kitu tofauti? Utaratibu wa Mwenyezi Mungu unaendelea kufanya kazi bila hata mimi kutambua. Inawezekanaje katika dunia hii akili yangu dhaifu, yenye mipaka na nyembamba

39. Abdulqadir Gaylani, "Al Fathu al-Rabbani". Istanbul 1987, uk 421

ikathubutu kusema: “Ningelibadili kile na kile na ningelifanya kile na kile”...kisha akashusha macho yake kutokana na aibu.

Hata hivyo mwalimu wake alifurahishwa mno na jibu hili zuri. Akamuangalia mwanafunzi wake kwa tabasamu na uso wenye kung’aa na kumwambia:

“Sasa suala letu limeisha na limefika mahala pake”.

Tokea pale mwanafunzi huyu akawa anafahamika kama “Merkez efendi” (Bwana wa kituo) na jina lake la kweli la Musa Muslihiddin likasahaulika.

❁

Kwa ufupi ni kwamba kuridhika katika hali aliyonayo mtu ni udhihirisho wa mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu na uaminifu wake Kwake. Kuridhika na chochote unachopewa na Mwenyezi Mungu ni wema mkubwa ambao wale waja wa Mwenyezi Mungu waliowekwa mbali na wivu na uroho na ambao wanamtambua Mwenyezi Mungu ndio pekee wanaoweza kuwa nao.

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anajua kilicho bora kwa mja wake, zaidi ya mja mwenyewe anavyofahamu. Ndio maana njia salama ni kuridhika na makadirio ya Mwenyezi Mungu na kuonyesha shukurani katika hali zote. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatoa tahadhari ifuatayo:

“**Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui**” (Al-Baqara, 2:216).

### 7. Tawakkul na kujisalimisha

Neno tawakkul lina maana ya kumtumainia mtu mwingine, kumteua mdhamini na kuweka amana yako kwa huyo mdhamini.

Moja ya majina mazuri ya Mwenyezi Mungu ni *'Al-Wakil'*. Jina hili lina maana zifuatazo: 'Ambaye anashughulikia matatizo yaliyopelekwa kwake (katika njia nzuri mno), Ambaye anashughulikia mambo kwa namna iliyo bora, Ambaye anategemewa, na Ambaye anaongoza na kutawala kila kitu'.

Bila shaka chanzo ambacho hatuna budi kukitegemea katika mambo yetu yote ni kile ambacho hakifi na chenye nguvu zisizo na mipaka. Itakuwa haina maana kumuamini yeyote kinyume na huyu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an:

"**Na mtegemee Aliye Hai, ambaye hafi. Na umtukuze kwa sifa zake. Na yatosha kwake kuwa yeye ni Mwenye khabari za dhambi za waja wake**" (Al-Furqan, 25:58).

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapenda sisi waja Wake tumtegemee Yeye pekee. Ndani ya Qur'an anasema:

"**Mitume wao wakawaambia: Sisi kweli si chochote ila ni wanaadamu kama nyinyi. Lakini Mwenyezi Mungu humfanyia hisani amtakaye katika waja wake. Wala sisi hatuwezi kuleta uthibitisho ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na juu ya Mwenyezi Mungu ndio wategemee Waumini**" (Ibrahim, 14:11).

"**Na humruzuku kwa jiha asiyotazamia. Na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake**" (al-Talaq, 65:3).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kama mngeliweza kumtegemea Mwenyezi Mungu vizuri basi mngelikuwa mnapata riziki kama ndege ambao wanaondoka kwenye viota vyao wakiwa na njaa na kurudi huku wameshiba"* (Tirmidhi, Zuhd, 33/2344; Ibn Majah, Zuhd, 14).

Tukija kwenye kujisalimisha, neno hili lina maana ya kukubaliana na lolote litakalokufika bila ya kupinga na hivyo kuwa katika amani. Kujisalimisha ni suala la moyoni ambalo linahusiana na kujiweka mbali na wasiwasi wa aina yoyote juu ya mambo yanayotokana na Mwenyezi Mungu. Kunahusiana na kujitenga na matamanio ya kidunia ambayo yako kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu, matamanio ambayo yako kinyume na usafi wa moyo, na laana ya kupinga qadari na hukumu za kiislamu. Katika aya ndani ya Qur'an tunafahamishwa kuwa:

"**Na lau kuwa tumewaamrisha: Jiueni, au tokeni majumbani kwenu, wasingeli fanya hayo ila wachache tu miongoni mwao. Na lau kama wangeli fanya walio waidhiwa ingeli kuwa bora kwao na uthibitisho wa nguvu zaidi**" (An Nisa, 4:65).

Neno '*taslimiyat*' au *kujisalimisha* lina mzizi ule ule sawa na neno '*islam*'. Ndio maana ili kuwa Muislamu wa kweli na kuwa mtumishi wa kweli wa Mwenyezi Mungu kutawezekana kwa kupitia kwenye kujisalimisha kwake. Hii inatokana na ukweli kuwa Mwenyezi Mungu (mwenye kutukuzwa na kuhimidiwa) anakasirika pale anapomuona mja wake anamtegemea mwingine kinyume na Yeye.

Kujisalimisha ni kitendo cha utii kinachotokana na upendo. Ilikuwa ni kwa sababu ya utii na kujisalimisha ndio maana nabii Ibrahim عليه السلام hakupumbazwa na uhai wake, mali zake au mwanae. Katika ibada zake hasa hijja ni alama kubwa ya kuonyesha utegemezi wake kwa Mola wake, na ibada hii itaendelea mpaka siku ya mwisho. Ulimi wa nabii Ibrahim ulikuwa unadhihirisha kilichokuwa ndani ya moyo wake na mara kwa mara alikuwa akiomba:

"**Na Mola wake Mlezi alipo mwambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote**" (Al-Baqara, 2:131).

Lengo la tasawwuf ambayo inachukulia upendo ambao ndio kiini cha Uislamu kama msingi wake, ni kuasisi hisia za kujisalimisha na kuridhika na Mwenyezi Mungu kwa kumfanya mja kuishi chini ya muongozo Mtukufu na kumkurubia Mwenyezi Mungu kwa kila pumzi. Madhara na ulaghai wa nafsi ambao unatokana na wasiwasi, hofu na maumivu ambayo yamesambaa katika hii dunia yenye kupita, yataanza kuondoka kutokana na kuridhika na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu. Uzuri ulioje namna Hakki Erzurumi anavyolielezea suala hili:

*Mtegemee Mwenyezi Mungu*
*Jisalimishe na upate amani*
*Ridhika na kila anachokupa*
*Acha tuone Mwenyezi Mungu amekuandalia nini*
*Chochote kitakachokuwa, kitakuwa ni kheri kwako*

***Matukio ya wema***

Siku moja Bedui alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuuliza:

"Ewe Mtume! Je nimfunge ngamia wangu ndio nimtegemee Mwenyezi Mungu au nimtegemee Mwenyezi Mungu bila ya kumfunga ngamia wangu?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Kwanza mfunge ngamia wako kisha ndio umtegemee Mwenyezi Mungu"*. (Tirmidhi, Qiyamah, 60/2517).

❁

Kutokana na mapokezi ya Ummu Salama ؓ, kila Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa akiondoka nyumbani kwake alikuwa akihakikisha kuwa anauelekeza uso wake mbinguni na kuomba dua ifuatayo:

*"Kwa jina la Mwenyezi Mungu! Ninamtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mwenyezi Mungu, ninajikinga kwako kutokana na kumpoteza mtu au mimi kupotezwa, kumtelezesha mtu au kutelezeshwa, kumdhulumu mtu au kudhulumiwa, na kuonyesha ujinga au kuwa muathika wa ujinga wa wengine"* (Abu Dawud, Adab, 102-3/5094; Tirmidhi, Dawat 35).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa kwenye msafara wa kivita alifika sehemu yenye bonde lenye miti mingi wakati wa mchana, akawaambia askari zake wapumzike pale na hivyo askari wake wakasambaa ili kutafuta kivuli. Na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pia alipata kivuli chini ya mti uliokuwa ukiitwa Semure ambao ulikuwa na majani mengi, kisha akapumzika pale na kuning'iniza upanga wake kwenye mti.

Sehemu ya tukio hili iliyobaki inasimuliwa na Jabir ؓ kama ifuatavyo:

"Baada ya kulala kwa muda mfupi tukasikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akituita na hivyo tukaamua kumkimbilia. Tulipofika pale alipokuwepo tulimkuta Bedui karibu yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Nilipokuwa nimelala huyu Bedui alikuja na kuchukua upanga wangu. Nilipoamka nikakuta ameshauchomoa kwenye ala yake na ameushika mkononi. Kisha akaniambia:*

*"Sasa ni nani atakayekuokoa kutoka mikononi mwangu?" Nikarudia mara tatu:*

*"Mwenyezi Mungu".* (Bukhari, Jihad, 84, 87; Muslim, Fadail, 13).

Ingawa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikutana uso kwa uso na kifo lakini hakupata hofu yoyote kutokana na kumtegemea kwake Mwenyezi Mungu na pia aliweza kusema maneno yafuatayo kwa ujasiri: "Mwenyezi Mungu ataniokoa". Baada ya yule Bedui kuyasikia maneno haya upanga ulidondoka kutoka mikononi mwake na akajisalimisha. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakumuadhibu Bedui huyu ambaye alikuwa anajaribu kumuua bali kinyume chake alimuelezea kuhusu Uislamu na kumshauri aingie kwenye Uislamu. Yule Bedui ambaye alistaajabishwa sana na kitendo kile cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliporudi kwenye kabila lake hakuweza kujizuia kuwaambia watu wake:

"Nimetoka kwa watu bora miongoni mwa watu wote". (Ibn Kathir, al-Bidaya, IV, 87).

❁

Abu Bakr as Siddiq رضي الله عنه anasimulia:

"Tulipokuwa pangoni pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika safari yetu ya kuhamia Madina, nilihisi miguu ya washirikina ikikanyaga juu ya pango na hivyo nikamwambia Mtume:

"Ewe Mtume. Kama mmoja wao mtainama na kuangalia kwa hakika atatuona".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Ewe Abu Bakr, unaonaje pale wanapokuwepo watu wawili na wa tatu wao akawa ni Mwenyezi Mungu?"* (Bukhari, Tafsir, 9/9; Muslim, Fadail as-Sahaba, 1).

❁

Ismet ibn Malik رضي الله عنه anasimulia:

Tulikuwa tukimlinda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ usiku kucha mpaka ilipoteremka aya ifuatayo:

**"...Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri"** (Al-Maida, 5:67)(Suyuti, Lubabu'n Nukul, I, 148).

Aisha ؓ anasimulia:

"Siku moja usiku Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alishindwa kulala. Nikamuuliza:

"Kuna tatizo gani ewe Mtume?" Akanijibu:

*"Je hakuna mtu yeyote mwema ambaye anaweza kuja kutulinda usiku wa leo?"* Wakati tunaendelea kuongea tukasikia sauti za mapanga nje. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Ni nani hao?"* Sauti ikajibu:

"Sisi ni Sa'd na Hudhayfa ewe Mtume. Tumekuja kukulinda. Baada ya pale Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akapata usingizi. Nikawa ninasikia sauti ya upumuaji wake wa kawaida. Wakati ule aya: **"...Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu"** iliteremka. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akachomoza kichwa chake nje ya hema na kusema:

*"Sasa mnaweza kwenda, kwani sasa hivi Mwenyezi Mungu ananilinda"*.[40]

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akichukua tahadhari na ndio amtegemee Mwenyezi Mungu. Baada ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kumuahidi kumlinda hakuendelea tena kuwa na wasiwasi wowote na hivyo akaweka utegemezi wake wote kwa Mwenyezi Mungu.

❀

40. Wahidi, "Esbabu' Nuzul'I Qur'an," thk: Kemal Besyuni Zaglul, Beirut 1990, uk 204-5

Kutokana na masimulizi ya Abu Said Al-Hudri ﷺ, siku moja mtu mmoja alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia kuwa kaka yake anasumbuliwa na tumbo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Mpatie shira ya asali anywe"*.

Yule mtu akafanya kile alichoelekezwa. Baada ya muda mfupi akarudi na kusema:

"Nilimpatia asali anywe lakini haikumsaidia bali hali yake ilizidi kuwa mbaya". Yule mtu alienda na kurudi kama hivi mara tatu. Mara ya mwisho Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

*"Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaongea ukweli na tumbo la kaka yako linadanganya"*. Baada ya pale yule alipompatia kaka yake asali anywe kwa mara nyingine tena alipona. (Bukhari, Tibb, 4; Muslim, Salam 91).

Kwa maneno haya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaashiria kwenye ukweli uliotolewa kwenye aya: **"...ndani yake kuna matibabu kwa wanaadamu. Hakika katika haya ipo Ishara kwa watu wanao fikiri"** (Al-Nahl, 16:69), na akashauri watu wajitegemeze na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu. Baadae swahaba mwingine naye akapona kwa kufanya kama hivi.

Kutokana na masimulizi ya Abdullah ibn Abbas, nabii Ibrahim alisema maneno yafuatayo pindi alipoingizwa ndani ya moto:

**"Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa"** (Al'i-Imran, 3:173).

Maneno haya pia aliyasema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pindi alipoambiwa awe katika tahadhari kwani washirikina

wamemzunguka. Kutokana na meneno haya imani za waumini zilipanda. Hivyo walionyesha unyenyekevu mkubwa mbele ya Allah.[41]

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu waislamu, watu ambao wanamtegemea Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

**"...Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa. Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu"** (Al'i Imran, 3:173-174). (Wahidi, uk 135).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametufahamisha kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atawahifadhi na kuwalinda wale waliomtegemea Yeye katika hii dunia na kesho akhera na kwamba wataingia peponi bila ya hesabu wala adhabu:

*"Nimeonyeshwa mataifa ya watu waliopita. Nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa na kundi dogo la watu watatu au watano. Nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mwingine akiwa na watu wawili. Na nikamuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye hana mtu kabisa. Wakati ule kundi kubwa la watu likaja mbele yangu. Nikadhani kuwa lilikuwa ni kundi la watu wangu. Wakaniambia: 'Hawa ni watu wa Musa, angali angani'. Nikaangalia na kuona mkusanyiko mkubwa kupita kiasi. 'Hawa ni watu wako. Kuna watu elfu 70 miongoni mwao ambao wataingia peponi bila ya kupelekwa kwenye hesabu na bila kuadhibiwa", walisema.*

Ibn Abbas ؓ amesema:

41. Angalia Bukhari, Tafsir, 3/13.

"Wakati ule Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alinyanyuka na kwenda nyumbani kwake. Maswahaba waliokuwepo pale wakaanza kujadili kuwa watu hawa elfu 70 ni kina nani. Baadhi yao wakasema: 'lazima watakuwa ni wale waliokuwa wakiongea na Mtume', wengine wakasema: 'watakuwa ni wale waliozaliwa baada ya Uislamu na ambao kamwe hawajapata kuujua ushirikina'. Wengine wakatoa maoni mengine. Wakati bado wanaendelea kulijadili jambo hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akarudi. Maswahaba zake wakamuuliza:

"Tunajadiliana kuhusu ni nani atakayeingia peponi bila ya hesabu wala adhabu". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Wao ni wale watu ambao hawalaani wala hawasababishi kulaaniwa, ambao hawakuwa wanaamini katika bahati mbaya, na ambao wanamtegemea Mola wao".*

Baada ya kuyasikia haya Ukkasha ibn Mihsan ؓ akasimama upesi na kusema:

"Tafadhali ninaomba uniombee na mimi niwepo kwenye kundi hilo ewe Mtume".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Wewe ni miongoni mwao"*.... (Muslim, Iman, 374; Bukhari, Riqaq, 50).

❁

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwajaribu nabii Ibrahim, mwanae Ismail na mkewe Hajar kwa mitihani mikubwa kiasi kwamba wameandikwa kwenye historia kama mifano ya kuigwa katika kujisalimisha. Kwa ajili yao Mwenyezi Mungu amefanya hijja ndogo na kubwa kuwa alama ya usafi wa nyoyo zao katika kujisalimisha kwa Mola wao.

Pindi Mwenyezi Mungu alipomfanya Ibrahim rafiki yake Malaika walimuuliza:

"Ewe Mola wetu. Inakuaje Ibrahim awe rafiki yako? Yeye ana roho, mali na watoto. Moyo wake utaegemea kwenye vitu hivyo..." Baadae walishuhudia tukio lifuatalo lililokuwa funzo na mtihani mkubwa kwa Ibrahim:

Pindi nabii Ibrahim alipokaribia kutupwa ndani ya moto malaika walipata wasiwasi. Baadhi yao wakamuomba Mwenyezi Mungu kama wanaweza kwenda kumsaidia Ibrahim. Malaika wakamuuliza Ibrahim kama alikuwa ana ombi lolote. Aliwaambia:

"Msiingilie kati ya marafiki wawili".

Baadae Jibril akamuuliza:

"Je unanihitaji mimi?"

Ibrahim akamjibu:

"Sina haja na wewe. Mwenyezi Mungu ananitosha, na Yeye ni mbora wa walinzi".

Matokeo ya kujisalimisha huku kwa huyu rafiki wa Mwenyezi Mungu na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu pekee, kulipelekea Mwenyezi Mungu kuuamrisha moto hata kabla ya Ibrahim kurushwa ndani yake:

**".....ewe moto, kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!"** (Al-Anbiya, 21:69).

Kutokana na amri hii sehemu ambayo nabii Ibrahim aliangukia ikawa kama bustani la mawaridi. Na Ndani yake kukawa kunavuma upepo mwanana kabisa.

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasimulia:

"Nabii Ibrahim ﷺ aliwaleta Makka Hajar na mtoto wake mdogo Ismail ambaye bado alikuwa ananyonya...Aliwapeleka pale mkewe na mwanae na kuwaacha na mfuko wa tende na chupa ya maji kwa sababu ambayo haifahamiki kwetu lakini yenye hekima kubwa. Pindi Ibrahim alipogeuka kwa ajili ya kuondoka, Hajar akamuita:

"Ibrahim! Unaenda wapi na kutuacha hapa kwenye bonde ambalo halina watu wa kuongea nao wala wa kuwaona, na hakuna chochote cha kula wala kunywa?"

Alilirudia swali lake mara nyingi lakini Ibrahim alibakia kimya. Kisha Hajar akamuuliza:

"Je Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuamrisha kufanya hivi?" Hapa Ibrahim akajibu:

"Ndio. Mwenyezi Mungu ameniamrisha kufanya hivyo". Hajar akapata utulivu kutokana na jibu hili, na katika kuonyesha kilele cha kujisalimisha kwake kwa Mwenyezi Mungu akasema:

"Kama ni hivyo basi Mwenyezi Mungu atatulinda na hatatuacha tuangamie..."

Kisha akageuka na Ibrahim akaondoka zake. Alipofika sehemu ya Seniyye na kuona haoni mtu yeyote akageuzia uso wake kwenye Al-Kaaba na kunyanyua mikono yake na kuomba:

"**Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya zangu katika bonde lisilo kuwa na mimea, kwenye Nyumba yako Takatifu, ewe Mola wetu Mlezi, ili washike Sala. Basi zijaalie nyoyo za watu zielekee kwao, na waruzuku matunda, ili wapata kushukuru**" (Ibrahîm, 14:37) (Bukhari, Anbiya 9).

❀

Ismail alikuwa amefikia umri wa kuchezacheza na alikuwa katika hatua ambayo anapendwa sana. Hata hivyo Ibrahim alikuwa

anatakiwa amtoe kafara mwanae kutokana na ahadi aliyokuwa ameiweka kwa Mwenyezi Mungu. Pindi walipomaliza maandalizi waliondoka. Kwa mara nyingine tena malaika walikuwa hawana utulivu:

"Nabii anamchukua nabii mwingine kwa ajili ya kwenda kumtoa kafara", walisema.

Ismail عليه السلام alimwambia baba yake:

"Ewe baba yangu! Fanya kama ulivyoamrishwa. Mwenyezi Mungu akipenda utanikuta katika miongoni mwa wenye kusubiri. Kinoe kisu chako vizuri; unikate kwa haraka; nitakufa kwa urahisi... na usiangalie uso wangu pindi utakaposhika kisu. Labda huruma ya ubaba itakucheleweshа na kutekeleza ahadi yako kwa Mwenyezi Mungu. Wasiwasi wangu ni kwamba utahisi maumivu ya kumtoa kafara mtoto wako kwa mikono yako mwenyewe na utanikosa katika maisha yako yote yaliyobaki..."

Wakati wote baba na mtoto wapo katika hali hii ya kujisalimisha, malaika Jibril akaja kuwaokoa. Akakifanya kisu kuwa butu na kushuka na kondoo kutoka peponi kwa ajili ya kutolewa kafara badala ya Ismail. (Angalia Taberi, Tarih, I, 275; Ibn Athir, al Kamil, I, 112; Hakim, II, 606/4040).

❁

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuelezea juu ya kujisalimisha kwa nabii Musa na kumtegemea kwake Yeye kama ifuatavyo:

**"Na akaja mtu kutoka mwisho wa mji akipiga mbio, akasema: Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuuwa. Basi toka! Hakika mimi ni katika wanao kupa nasaha. Basi akatoka, naye ana khofu, akiangalia huku na huku. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niokoe na watu madhalimu"** (Al-Qassas, 28:20-21).

Hivyo Musa alidhirisha utegemezi wake wa kweli kwa Mwenyezi Mungu:

Kwanza alichukua hatua, akatafuta suluhisho likifuatiwa na kuchukua tahadhari na kisha kuyaacha matokeo kwa Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine ni kwamba alikuwa katika hali ya maombi, kujisalimisha na kuridhika. Huku ndiko kumtegemea Mwenyezi Mungu kikweli kweli...

❁

Katika kipindi ambacho watu wa Yemen wanaenda kuhiji walikuwa hawabebi chakula wakiwa safarini huku wakiamini kuwa huku ndiko kumtegemea Mwenyezi Mungu:

"Tunaenda kutembelea nyumba ya Mwenyezi Mungu. Kwa hakika Yeye atatulisha".

Walipofika Makka walijikuta wanaomba watu wengine. Kisha aya ifuatayo ikateremka: "...**Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamngu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili!**" (Al-Baqara, 2:197).

Omar ﵁ alikuwa akiwafokea wale waliokuwa hawafanyi kazi, hawafanyi juhudi yoyote na wavivu na ambao walikuwa wakisema: "Sisi ni watu ambao tunamtegemea Mwenyezi Mungu". Alikuwa akiwaambia: "Nyinyi ni watumiaji wa mali za watu wengine na hivyo hamuwezi kuchukuliwa kuwa ni watu wenye kumtegemea Mwenyezi Mungu. Anayemtegemea Mwenyezi Mungu kikweli kweli ni yule ambaye anapanda mbegu katika ardhi na kisha anamtegemea Mwenyezi Mungu" (Ibn Rajab Al-Hanbali, 'Jami al Ulum wa al Hikam' Amman 1990, 650).

❁

Abu Huraira ﵁ anasimulia hadith ifuatayo yenye mafunzo makubwa kwetu:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituelezea kuhusu hali nzuri ya mtu kutokana na wana wa Israel. Mtu huyo alimuomba mtu mwingine amkopeshe dinar elfu moja. Yule aliyeombwa mkopo alisema:

"Niletee mashahidi na mimi nitakupa fedha hizo mbele yao". Yule aliyekuwa anaomba mkopo akasema:

"Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi yetu". Kisha mkopeshaji akasema:

"Kama ni hivyo basi mlete mdhamini wako". Yule mkopeshwaji akasema:

"Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mdhamini wangu". Kisha mkopeshaji akasema:

"Umesema kweli" na kisha akampatia fedha kwa muda fulani.

Yule akaenda kwenye safari ya baharini na kutimiza mahitaji yake. Kisha wakati anataka kurudi ili akalipe fedha za watu kwa muda waliokubaliana alitafuta mashua ya kumrudisha lakini hakuipata. Huku akiwa amekata tamaa alipata gogo la mti, akalichukua na kulitoboa na kuziweka dinar elfu moja pamoja na karatasi yenye anuani ya yule aliyemkopesha na kisha akaliziba na kwenda kwenye ukingo wa bahari na kusema:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Unajua kuwa nilikopa dinar elfu moja kutoka kwa fulani. Aliponiuliza juu shahidi nilimwambia kuwa "Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi". Na aliridhika Wewe kuwa shahidi yetu. Na pindi alipohitaji mdhamini, Nilimwambia: "Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mdhamini wangu". Na aliridhika kwa Wewe kuwa mdhamini wangu. Na sasa nimejitahidi kutafuta mashua lakini sikupata. Hivyo nazitegemeza hizi fedha kwako".

Kisha akalirusha lile gogo ndani ya bahari. Kisha lile gogo likaelea juu ya bahari na kupotea kwenye uoni wake. Kisha yule mtu akaondoka sehemu ile na kuendelea kutafuta mashua.

Baada ya muda mfupi yule mkopeshaji akawa anasubiria mashua ili arudishiwe fedha zake. Hakukuwa na mashua yoyote lakini aliona gogo lililokuwa limebeba fedha zake. Alilichukua kwa lengo la kwenda kulitumia nyumbani kwake. Alipolipasua aliona barua pamoja na fedha.

Baada ya muda mfupi yule mtu aliyekuwa amekopa alipata mashua na kurejea kwenye makazi yake. Akafikiria kuwa huenda yule mtu hakuliona lile gogo lililokuwa na fedha hivyo akachukua dinar nyingine elfu moja na kwenda nazo kwa yule mtu.

“Nilitafuta mashua kwa muda mrefu kwa ajili ya kukurudishia fedha zako lakini sikuipata kabla ya kuipata hii mashua niliyokuja nayo sasa hivi”. Yule mtu aliyekuwa amemkopesha akasema:

“Je hukunitumia chochote?”

“Nimekuambia nilitafuta mashua lakini sikuipata” alijibu.

Kisha mkopeshaji akasema:

“Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amenilipa ile fedha badala yako na ameileta kwangu ikiwa ndani ya gogo kama malipo ya usafi wako wa moyo. Matokeo yake hizo dinar elfu moja ulizokuja nazo sasa hivi ni zako. Sasa unaweza kurudi kwa amani huku ukiwa una dinar zako elfu moja”. (Bukhari, Kafalat I, Buyuu 10).

Pindi Mwenyezi Mungu anapokuwa mdhamini katika jambo, kinachoonekana hakiwezekani kinaweza kufanyika kwa urahisi. Kinachotakiwa kwa mja ni kumuamini Yeye kwa moyo safi na kikweli kweli...

❁

Kutokana na masimulizi ya Ibn Abbas رضي الله عنه siku moja Omar ibn Khattab رضي الله عنه aliondoka na kuelekea Damascus. Alipofika sehemu iitwayo Serg alikutana na kamanda wa jeshi aliyeitwa Abu Ubayda ibn Jarrah pamoja na marafiki zake waliokuwa chini yake. Kamanda yule akamtaarifu kuwa ugonjwa wa tauni umeanza kuingia ndani ya Damascus. Omar رضي الله عنه akamwambia Ibn Abbas:

"Waite muhajirina wa kwanza waje hapa". Omar akakutana nao na kuwaambia kuwa kuna mlipuko wa ugonjwa wa tauni ndani ya Damascus. Walitofautiana juu ya nini cha kufanya. Baadhi yao walisema:

"Umekuja hapa kwa lengo fulani; hatudhani kuwa ni sawa kwa wewe kurudi sasa hivi". Wengine wakasema:

"Waislamu wengine na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wako pamoja na wewe. Hatudhani kuwa ni sawa kwa wewe kuupata ugonjwa huu na kurudi nao".

Omar رضي الله عنه akawaambia:

"Mnaweza kwenda". Kisha akamgeukia Ibn Abbas na kumwambia:

"Waite Answar waje hapa".

Kama ilivyokuwa kwa muhajirina na Answar nao wakafikia kwenye makubaliano yale yale. Kisha Omar akawaambia nao waondoke.

"Sasa waite watu wazima katika muhajirina kutokana na Maquraysh walio hapa na ambao walihamia Madina kabla ya Makka kukombolewa". Nilienda kuwaita. Hakuna hata wawili kati yao walioacha kukubaliana na hivyo wakasema:

"Tunadhani huna budi kuwarudisha watu ili usirudi na huu ugomjwa wa tauni". Kisha Omar رضي الله عنه akamuita kila mtu na kusema:

"Nitakuwa juu ya mnyama wangu itakapofika asubuhi. Na nyinyi pia fanyeni hivyo". Abu Ubayda ibn Jarrah ﵁ akauliza:

"Je unaikimbia qadari ya Mwenyezi Mungu?" Omar akajibu:

"Je kuna mtu mwingine yeyote aliyelisema hili kinyume na wewe ewe Abu Ubayda!"

Omar hakutaka kumpinga Abu Ubayda.

Kisha akaendelea kusema:

"Ndio. Tunaikimbia qadari ya Mwenyezi Mungu na kwenda kwenye qadari ya Mwenyezi Mungu. Ungelisemaje kama ungelikuwa una ngamia kadhaa na kwenda nao kwenye bonde lililokuwa na pande mbili, upande mmoja una malisho na mwingine hauna. Na kisha unawaachia ngamia wako wakale sehemu yenye malisho na kisha unawaachia wakale sehemu isiyokuwa na malisho. Je hali hizi zote mbili zisingelikuwa ni qadari ya Mwenyezi Mungu?"

Wakati ule Abdurrahman ibn Awf ﵁ ambaye hakuwepo kwa ajili ya kwenda kushughulikia baadhi ya mahitaji yao alikuja na kusema:

"Nina ufahamu kidogo juu ya jambo hili. Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema:

*"Kama mkisikia kuwa sehemu fulani ina tauni msiingie sehemu hiyo. Kama ugonjwa wa tauni unalipuka sehemu na wewe upo pale basi usijaribu kuukimbia ugonjwa kwa kuondoka sehemu ile"*. Baada ya kuyasikia haya Omar ﵁ alimsifu Mwenyezi Mungu na kuendelea na safari yake ya kuondoka Damascus. (Bukhari, Tibb 30; Muslim, Salam, 98).

Tukio hili linaelezea vizuri kuhusu utegemezi na qadari ndani ya Uislamu. Kujiingiza wewe mwenyewe na waumini katika hatari kwa kufahamu hakuendani na kumtegemea Mwenyezi Mungu.

Kwa maneno mengine kujisalimisha kunaruhusu kuchukua tahadhari lakini sio kuweka mategemeo yako juu yake.

❀

Mayyit-zade ambaye aliishi katika kipindi cha Sultani Ahmad wa kwanza, alikuwa mwanachuoni mkubwa katika dola ya Uthmainiyya ambaye alikuwa maarufu kutokana na mwenendo wake mwema na busara zake. Sababu iliyomfanya apewe jina la 'Mayyit-zade' ambalo lina maana ya 'mtoto wa marehemu' ilikuwa ni kutokana na tukio lifuatalo ambalo lilimpata kutokana na utukufu wake:

Baba yake Mayyit-zade alikuwa askari hodari. Kama ilivyokuwa kwa mashujaa wengine aliitwa kushiriki kwenye msafara wa kivita wa Egri wa mwaka 1596 uliandaliwa na Sultani Mehmed wa tatu. Lakini wakati ule mke wake alikuwa mjamzito na alikuwa anakaribia kujifungua. Hata hivyo baba huyu hodari ambaye alithaminisha kupigana katika njia ya Mwenyezi Mungu zaidi ya vitu vingine alijiandaa kwa ajili ya safari na kumuomba mkewe amsamehe. Alinyanyua mikono yake kwa unyenyekevu na kuielekeza kwenye mahakama tukufu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Akamuomba Mola wake huku machozi ya huruma yakimtiririka machoni mwake:

"Ewe Mola wangu! Ninaenda kwenye vita vitakatifu katika njia yako. Sina mwingine zaidi yako. Ninamtegemeza kwako huyu mtoto wangu ambaye anatarijiwa kuzaliwa muda si mrefu na huyu mke wangu muaminifu ambaye amehangaika kwa muda mrefu. Tafadhali naomba umlinde kwa rehema na fadhila zako".

Kisha yule baba shujaa akarukia farasi wake upesi na kutoweka eneo lile. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu na rehema zake jeshi la dola ya Uthmainiyya lilishinda.

Wakati wanarudi nyumbani yule baba shujaa alimuomba kamanda wao amruhusu arudi moja kwa moja nyumbani kwake. Lakini alipowasili nyumbani kwake hakukuta mtu. Wakati alitarajia kuwa mke wake lazima angekuwa ana taarifa za ushindi wao kutokana na kusambaa kwa taarifa kote na hivyo alitarajia angelikuwa anamsubiria yeye. Huku akiwa na wasiwasi na shauku kubwa alikimbilia kwa majirani ili kuwauliza kuhusu mke wake. Pindi majirani zake walipomuona baba mtu walimuangalia kwa masikitiko na kusema:

"Ewe mwerevu. Mwenyezi Mungu aubariki ushindi wenu na ayafanye maisha yako yawe ya neema".

Kutokana na kuelewa maana ya sentensi hii maumivu makali yakaushika moyo wake na akawa anaongea bila ya kujitambua:

"Hapana, haiwezekani". Kisha akasema kwa upole:

"Haiwezekani. Nilimtegemeza mtoto wangu kwa Mola wa walimwengu. Yeye ni mbora wa walinzi..."

Baba yule aliyekuwa na huzuni alikaa kimya kwa muda mrefu na kuwaangalia wale waliokuwa karibu yake. Kisha akasema:

"Bila shaka Mwenyezi Mungu ni mwingi wa huruma na ni mbora wa wale wanaolinda na kuhifadhi; nionyesheni kaburi la mke wangu upesi".

Wote kwa pamoja wakaenda makaburini. Alipoonyeshwa kaburi aliweka sikio juu yake na kuanza kusikiliza. Kisha akapiga kelele:

"Ndio, ninaweza kusikia kilio cha mtoto wangu!"

Baba yule aliyekuwa na huzuni alikamata sepetu na koleo na kuanza kufukua lile kaburi. Wale waliokuja naye wakaanza kumsaidia kutokana na wao pia kusikia kilio cha mtoto kutoka ndani

ya kaburi. Pindi walipomaliza kufukua kaburi kitendo kilichokuwa kinawasubiri ni cha kustaajabisha na cha kushtua:

Ndani ya kaburi kulikuwa na maiti ya mama ambaye alikuwa amejifungua mtoto mzuri ambaye alikuwa ameshikilia kwenye kifua cha mama yake. Yule baba mpiganaji vita wa siku nyingi alimkamata upesi mtoto wake na kumshikilia kifuani mwake. Akabusu mashavu yake kama mawaridi tena na tena. Kisha akamfunga mtoto wake na kisha akaomba dua ya kumuaga mke wake na kisha akalifukia kaburi kwa uangalifu. Wote waliokuwa pale walishtushwa na muujiza huu na hivyo wakawa wanamsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na hofu kubwa. Huku macho yake yakiwa yamejawa na machozi baba alisujudu na kumsifu Mola wake. Alikuwa na huzuni ya kufiwa na mkewe lakini wakati huo huo alikuwa na furaha juu ya mtoto wake.

Mtoto huyu alikulia katika mazingira ya kujifunza na ya kimaadili. Alikuja kuwa mwanachuoni mkubwa aliyekuwa maarufu katika ardhi zote za dola ya Uthmainiyya. Wakati wote alikuwa akijulikana kama 'Mayyit-zade' kutokana na kilichokuwa kimemtokea. Yeye alikuwa baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, aliyejaa busara na umakini, na pia ni matokeo ya ujisalimishaji wa kweli.

❁

Kwa ufupi kupata amani ya moyo ndani ya dunia hii na kupata furaha ya milele kesho akhera itawezekana pale mtu akatakapotambua ukubwa wa Mwenyezi Mungu na kujitegemeza na kujisalimisha kwake, na kuridhika na kile ambacho Mwenyezi Mungu amemjaalia. Nyoyo ambazo zinamtii Mwenyezi Mungu, zinajisalimisha kwake na ambazo zimeridhiwa naye zinakuwa ni chanzo cha busara, wema na ustawi. Kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kikweli na kujitegemeza na kumtii Yeye kunategemea ikiwa mtu ana moyo uliojawa na furaha ya imani. Ni kutokana na upendo na kupanda daraja kwa moyo ndio mwanadamu anaweza kumgeukia

Mola wake mzima mzima na kuuweka mbali moyo wake dhidi ya kushikama na dunia na vyote vilivyopo ndani yake.

Kujisalimisha kwa mja kwa Mola wake kunaendana na kumfahamu na imani yake Kwake. Kutokana na kuwa kiini cha utumishi, kujisalimisha ni jambo muhimu lenye kuufanya moyo ujikurubishe kwa Mwenyezi Mungu. Kujikurubisha huku huanza kwa imani na huendelea kuongezeka kadiri ufahamu juu ya Mwenyezi Mungu unavyoongezeka. Rumi anaelezea siri ya kufikia daraja la *'fana fillah'* (kujitoa au kujipoteza kwa Mwenyezi Mungu) ambayo ni kama kujisalimisha moja kwa moja:

"Maji ya bahari hubeba kichwa cha maiti aliyejisalimisha moja kwa moja juu yake. Je inawezekanaje yule aliye hai na huku ana wasiwasi hata kidogo mno ajitoa kwenye bahari? Vivi hivi kwa kupitia fumbo ya *'kufa kabla hujafa'*, kama unakufa huku ukiwa umejiweka mbali na sifa zako za kibinadamu, basi bahari ya maajabu itakunyanyua na kukubeba".

### *8. Ihsan* na kuwa macho

*Ihsan* inamaanisha ufahamu na utambuzi wa muumini kuwa yuko chini ya usimamizi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, yani yuko chini ya uangalizi wa jicho lenye kuona kama 'kamera tukufu'. *Ihsan* ni kupandishwa madaraja kwa zile roho ambazo zipo karibu na Mwenyezi Mungu.

Ukweli kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anaona kitendo cha kila mtu na kwamba atawaita kwa ajili ya kuwahesabu pindi wakati utakapofika umeelezewa katika aya zifuatazo ndani ya Qur'an:

"**Tena tutawasimulia kwa ilimu; wala Sisi hatukuwa mbali**" (Al-Araf, 7:7).

"**Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anajua siri zao na minong'ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua sana ya ghaibu?**" (Al-Tawba, 9:78).

**"Ewe mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikawa ndani ya jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu atakileta. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliyo fichika, Mwenye khabari za yote"** (Luqman, 31:16).

Katika maisha yetu ya kila siku watu wengi hujizuia na kusema na kufanya mambo mabaya pindi wanapoona kuna jozi ya macho inawaangalia. Na hii kutokana na jozi dhaifu ya macho ambayo hayawezi hata kuwaadhibu...vihi hivi kwa muumini ambaye anaishi katika hali ya *ihsan* anatambua kuwa Mwenyezi Mungu anamuona na anajua kila kitu anachokifikiria, anachokisema na anachokifanya.

Maana nyingine ya *ihsan* ni kutekeleza chochote unachokifanya katika njia bora iwezekanavyo.

Moja wapo ya mambo ya muhimu katika kujiandaa na pumzi ya mwisho ni kujijengea hisia ya *ihsan* ndani ya moyo. Yani kuukurubisha moyo wako kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuhisi kuwa wakati wote upo chini ya uangalizi wake. Ukurubishaji huu wa moyo unaweza kujengwa kwa kupitia kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi.

Hatua ya pili katika kufikia kwenye hali ya ihsan na kuwa macho ni kutafakari juu aya zifuatazo kutoka kwenye Qur'an:

"**Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita; kisha akakaa vyema juu ya enzi. Anayajua yanayo ingia katika ardhi na yanayo toka humo, na yanayo teremka kutoka mbinguni, na yanayo panda humo. Naye yu pamoja nanyi popote mlipo.**

**Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayo yatenda**" (Al-Hadid, 57:4).

"**Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake**" (Qaf, 50:16).

"**Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa**" (Al-anfal, 8:24).

Juu suala hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema:

*"Daraja la juu la imani ni kufahamu kuwa Mwenyezi Mungu yuko na wewe popote ulipo"* (Haythami, I, 60).

Hakuna shaka kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakati wote alikuwa katika hali ya *'ihsan'*, usiku na mchana, katika nyakati za shida, na katika nyakati za wepesi na raha, katika nyakati za vita na katika nyakati za amani. Hali yake ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wote, swala zake na dua zake, ibada zake za faradhi alizoendelea kuzitekeleza, kuswali kwake usiku mpaka vifundo vya miguu yake vikavimba, umakini wake katika kutekeleza haki za watu wengine, ugawaji wake wa haki na usawa katika nyakati zote na mambo yake mengine ya wema ni ushahidi wa kutosha juu ya kuwa kwake katika hali ya *ihsan*.

Omar ibn Khattab رضي الله عنه anasimulia hadith ifuatayo (ambayo inaitwa hadith ya Jibril) ambayo inaonyesha namna walivyotaarifiwa na kufundishwa juu ya hali ya *ihsan*:

"Siku moja tulipokuwa tumekaa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitokea mtu mmoja aliyekuwa amevaa mavazi meupe mno na ambaye nywele zake zilikuwa nyeusi kupita kia-

si. Hakuwa na dalili ya kuwa msafiri na hakuna yeyote kati yetu aliyekuwa anamfahamu. Kisha mtu akakaa mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kugusanisha magoti yake na magoti ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuweka mikono yake kwenye magoti yake mwenyewe na kisha akamuuliza:

"Ewe Muhammad! Uislamu ni nini?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Uislamu ni kushuhudia kuwa hakuna mungu mwingine ila Mwenyezi Mungu na kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kusimamisha swala tano, kutoa sadaka, kufunga bila ya kukosea katika mwezi wa Ramadhani na kutembelea Al-Kaaba kwa mwenye uwezo".*

Yule mtu akasema:

"Umesema kweli".

Tukaona ni kitu cha ajabu kuwa yeye anauliza swali na kisha anathibitisha jibu. Kisha yule mtu akauliza:

"Na imani ni nini?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Ni kumuamini Mwenyezi Mungu, malaika*

*wake, vitabu vyake, Mitume yake na siku ya mwisho. Ni kuamini qadari na heri na shari inayotokana nayo".*

"Umesema kweli" yule mtu akasema tena.

"Baada ya hayo ni *ihsan* ni nini?" aliuliza.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Ihsan ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona. Na ingawa wewe humuoni lakini yeye anakuona".*

Yule mtu akarudia:

"Umesema kweli". Kisha akauliza:

"Je ni lini kiama kitasimama?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Anayeulizwa hana ufahamu zaidi kuhusu jambo hili kuliko yule anayeuliza"*. Kisha yule mtu akauliza:

"Kama ni hivyo basi ni zipi dalili zake?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Mjakazi atamzaa bwana wake, utakuta wachunga mbuzi masikini wakishindana kujenga majengo mazuri huku wako peku"*[42].

Kisha yule mtu akaondoka bila ya kusema chochote. Nikasimama kama nilivyokuwa kwa muda kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniuliza:

"Ewe Omar, Je unajua ni nani alikuwa ananiuliza maswali hivi punde?" Nikajibu:

"Mwenyezi Mungu na Mjumbe waje wanajua zaidi".

Akajibu:

*"Alikuwa ni Jibril. Alikuja kuwafundisha dini yenu"* (Muslim, Iman, 1,5 Bukhari, Iman 37 Tirmidhi, Iman, 4; Abu Dawud, Sunan 16).

❁

42. Hivi ndivyo hadith (mjakazi atamzaa bwana wake) ilivyotafsiriwa; yani mama watazaa watoto waasi ambao watawafanya wazazi wao kuwa kama watumwa wao. Katika suala la wachungaji walio pekupeku na wasio na nywele ambao watajenga majengo marefu na mazuri, ni ishara ya kuongezeka kwa starehe na utajiri, na watu ambao walikuwa masikini wanakuwa matajiri kiasi cha kushindana kujenga majengo makubwa na ya kifahari. Dunia itatoa utajiri wake kwa mwanadamu, na itakuwa fedha na mali ndio kipimo cha thamani ya mtu na watu watapenda kutumia na kuonyesha utajiri wao.

Wanachuoni wamesema kuwa *hadith* hii ndio kiini cha *sunnah*. Hivyo kufikia kwenye ukamilifu wa Uislamu na imani ya mtu kunategemeana na kufikia katika hali ya *ihsan*. Hivyo dini ya muumini ambaye hajafikia kwenye hali ya *ihsan* inakuwa na upungufu. Imani ya namna hiyo ni sawa na mti usio na matunda ambao hauwezi kuendelea kuwepo. Kuna uwezekano mkubwa kuwa utakuja kukauka muda si mrefu.

Pia *hadith* hii inathibitisha wazi kuwa *tasawwuf* ambayo iko kwenye moyo wa imani na Uislamu, na ambayo haiwezi kutengwa na vitu hivyo, inalenga kujenga hali ya *ihsan* ndani ya moyo wa muumini.

Ukweli ni kwamba furaha kubwa kwa mja wa Mwenyezi Mungu ni kwa yeye kuwa pamoja na Mola wake. Muumba wa ulimwengu mzima anapenda kuwa na waja wake wakati wote na katika kuthibitisha hili Anasema yafuatayo ndani ya Qur'an:

"**Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto**" (Al-Imran, 3:191).

Kwa upande mwingine mtu ambaye hajaiunganisha akili yake na moyo na ambaye kichwa chake kimezungukwa na matamanio ya nafsi yake hataweza kuhisi raha inayopatikana kwa kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Yani atakuwa amekosa kitu bora na furaha.

Furaha na raha ya ibada na kutochoka kutokana na kuzitekeleza inaweza kupatikana kwa kupitia *ihsan* pekee. Yeyote ambaye hana hisia ya hii ihsan ndani ya moyo wake basi atachoka mapema kutokana na kuswali na swala itakuwa ni jambo lenye kumchosha. Kama atakuwa ni tajiri basi atajizuia na kutoa sadaka na zaka na ku-

wasaidia masikini. Haya ni kutokana na kujiweka kwake mbali na usimamizi wa Mwenyezi Mungu na hivyo hawezi kuhisi ladha ya imani. Kutokana na haya tunaweza kusema kuwa swala iliyoswaliwa vizuri, sadaka iliyotolewa kutoka moyoni, funga iliyotekelezwa kwa mapenzi, hijja iliyotekelezwa kwa hamasa, moyo uliotegemaa ambao uko kati ya matumaini na hofu, mwenendo mwema na kila wema wa aina nyingine unatokana na baraka za hali ya *ihsan*.

***Matukio ya wema***

Abdullah ibn Abbas ﵁ anasimulia:

Siku moja nilikuwa nimekaa nyuma ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ juu ya ngamia wake. Akaniambia:

*"Mwanangu. Nitakupa ushauri"*. Kisha akaendelea:

*"Tii maamrisho ya Mwenyezi Mungu na Yeye atakulinda. Kama unajitahidi kumridhisha Mwenyezi Mungu juu ya mambo yote, basi utamkuta Mwenyezi Mungu yuko mbele yako. Kama unataka kitu muombe Mwenyezi Mungu. Kama unahitaji msaada wa kitu chochote basi muombe Mwenyezi Mungu akusaidie"* (Tirmidhi, Qiyamah, 59/2516).

Na katika masimulizi mengine:

*"Jihadhari na maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu na hivyo utamkuta Mwenyezi Mungu yuko mbele yako. Mfahamu Mwenyezi Mungu kwa kushikamana na maamrisho yake wakati upo katika raha na Yeye atakutambua (na kukusaidia) pindi utakapokuwa kwenye matatizo…"* (Ahmad, I, 307).

Maneno haya ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yanatoa mukhtasari mzuri wa kiini cha hali ya *ihsan* na dalili zake.

❁

Siku moja Abdullah ibn Omar ﷺ alikuwa ameenda kwenye vitongoji vya Madina pamoja na baadhi ya marafiki zake. Wakaandaa meza ya chakula kwa ajili yake. Wakati ule akajitokeza mchungaji na kuwasalimia. Ibn Omar akamwambia:

“Njoo mchungaji na tule pamoja”. Yule mchungaji akajibu:

“Nimefunga”. Kisha Ibn Omar akamuuliza:

“Inakuwaje umefunga katika joto kali kiasi hiki lenye kuumiza? Na huku unachunga kondoo?”

Baadae, katika kuangalia umakini na *taqwa* ya mchungaji akamshauri yafuatayo:

“Je huwezi kutuuzia kondoo mmoja na sisi tukakulipa na kukupa nyama ambayo utaitumia kufuturia?”

Yule mchungaji akajibu:

“Hawa sio kondoo wangu. Ni wa bwana wangu”. Kisha Ibn Omar akasema:

“Unaweza kumwambia kuwa umepoteza mmoja. Bwana wako atajuaje vinginevyo?” Yule mchungaji akanyanyua kichwa cheke na kidole chake na kuashiria mbinguni na kusema:

“Na Mwenyezi Mungu naye yuko wapi?”

Ibn Omar aliachwa ameguswa na *ihsan* na utambuzi wa mchungaji huyu. Akafunikwa na mawazo huku anatafakari maneno ya mchungaji. Akawa anajisemea mwenyewe: *Mchungaji amesema: “Na Mwenyezi Mungu naye yuko wapi?” Mchungaji amesema: “Na Mwenyezi Mungu naye yuko wapi?”*

Pindi aliporejea Madina alituma kikosi kwenda kwa bwana wa yule mchungaji na kununua wale kondoo na mchungaji. Baada ya kumuacha huru yule mchungaji pia alimpatia kundi la kondoo. (Ibn Athir, Usdu al-Ghabah, III, 341).

Hivyo baadhi ya baraka na malipo ya ihsan na kumtambua Mwenyezi Mungu vinaweza kuonekana hapa hapa duniani... Nani ajuae ni malipo kiasi gani yatakuwepo kesho akhera?

❁

Kama ilivyokuwa kawaida yake Omar ؓ siku moja alikuwa anatembea katika mitaa ya Madina katikati ya usiku. Mara akasimama. Alishughulishwa na malumbano yaliyokuwa yakisikika kutoka kwenye nyumba moja wapo ya zile alizozipita. Mama alikuwa akimwambia binti yake:

“Binti yangu. Ongeza maji kwenye maziwa ambayo tutayauza kesho”.

Yule binti akajibu:

“Mama mpendwa, je khalifa wetu hakutukataza kuchanganya maji na maziwa?”

Yule mama akamfokea binti yake:

“Je khalifa atafahamu vipi katika nyakati hizi za usiku kuwa tumeongeza maji kwenye maziwa yetu?”

Lakini haikusaidia kitu. Yule binti ambaye moyo wake ulikuwa hai kutokana na upendo na hofu ya Mwenyezi Mungu hakukubaliana na ulaghai huu wa mama yake.

“Mama mpendwa! Tufanye khalifa hawezi kutusikii. Je Mwenyezi Mungu naye pia hawezi kutuona? Ni rahisi kuuficha ulaghai huu kwa watu lakini lakini inawezekanaje kuuficha kwa Mwenyezi Mungu ambaye ni Muumba wa ulimwengu, ambaye anaona na kujua kila kitu...?”

Jibu hili la binti huyu kwa mama yake lilimgusa mno Omar ؓ. Huyu alikuwa msichana mwenye maadili na moyo ulio hai na uliojawa na ukweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu na hofu kubwa juu

yake. Omar akapangilia yule msichana awe mchumba wa mwanae kutokana na kutambua uchamungu wake usio wa kawaida, na hakumuona kuwa ni binti mwingine wa muuza maziwa wa kawaida. Na matokeo yake mtu maarufu kwa jina la Omar ibn Abdulaziz ambaye ni khalifa wa tano alizaliwa kutokana na ukoo huu. (Angalia Ibn Jawzii', Sifatu as-Safwa, II, 203-4).

Mfano huu unaonyesha kuwa ihsan inaweza kwenda mbali zaidi na kuwa sababu ya neema na kheri kwa jamii nzima.

❁

Wakati wa ukhalifa wa Omar ﵁ siku moja alimtuma Muadh ﵁ kwenda kwenye kabila la watu wana wa Kilab. Alikuwa anatakiwa atoe fedha yoyote inayotakiwa kutolewa kutoka kwenye hazina ya dola, pia kutoa kila mali iliyokuwa inatakiwa kutolewa na kuchukua mali kutoka kwa matajiri na kuwapa masikini na mafakiri.

Muadh ﵁ alitekeleza jukumu lake kwa umakini mkubwa na moyo wake wote, kisha akarejea na mchapo mtamu. Pindi aliporudi alibakiwa na kilemba shingoni mwake katika bidhaa za kiduni. Kilemba hiki alikuwa nacho kabla ya kuondoka. Wakati fulani mke wake alishindwa kuvumilia na hivyo akamwambia:

"Watu ambao wanachukua jukumu hili huchukua malipo kiasi fulani na kurudi na zawadi kwenye familia zao. Wewe zawadi zako ziko wapi?"

Muadh ﵁ akajibu:

"Kulikuwa na aliyenisindikiza popote nilipoenda na kamwe hakuniacha. Alihesabu kila kitu nilichochukua na kutoa".

Mke wake akapandwa na hasira:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuaminisha katika kila kitu. Na Abu Bakr naye pia alifanya vivo hivyo. Sasa hivi Omar

amekuja na amekutuma pamoja na msindikizaji? Na amekufuata katika kila kitu ulichokifanya?"

Maneno haya yalimfikia mke wa Omar na kutoka pale yalifikia masikio ya Omar ﵁ mwenyewe. Akamuita Muadh ﵁ na kumuuliza kwa upole:

"Ni nini hiki ninachokisikia ewe Muadh? Sikumtuma mtu yeyote aje kukusindikiza lakini sasa nasikia kinyume chake? Je unadhani sikuamini?"

Jibu la Muadh ﵁ lilikuwa ni lenye kuvutia mno:

"Ewe kiongozi wa waumini! Hii ilikuwa sababu pekee niliyoweza kumpa mke wangu. Na pindi niliposema msindikizaji sikumaanisha alitoka kwako. Nilimaanisha kuwa nilikuwa ninaangaliwa na Mwenyezi Mungu. Sikutaka kukosa malipo na hivyo sikuchukua chochote katika jukumu uliloniagiza kulifanya kama malipo, ingawa kuna ruhusa hiyo..."

Omar ﵁ alielewa alichokimaanisha kwa maneno haya. Muadh hakutaka kuchukua chochote katika dunia hii kwa ajili yake. Hata hivyo ili kumridhisha Muadh Omar alimpatia zawadi kutokana na mali zake na kumwambia:

"Chukua hiki na uende ukairidhishe familia yako"

❁

Mfano mwingine mzuri wenye kuonyesha bayana uzuri wa *ihsan* na kumtambua Mwenyezi Mungu ni huu ufuatao:

Siku moja mhubiri alikuwa anatoa hotuba kuhusu akhera. Miongoni mwa waliokuwepo kwenye mkusanyiko ule alikuwa ni Sheikh Shibli. Mhubiri alikuwa anazungumzia juu ya maswali ambayo Mwenyezi Mungu atakuja kutuuliza siku ya kiama:

“Mtaulizwa- elimu yenu mliitumiaje? Mtaulizwa- mali zenu mlizitumia kwenye nini? Na pia mtaulizwa kuwa uhai wenu mliutumiaje? Je mlikuwa mkifanya ibada? Je mlikuwa waangalifu katika kujizuia na haramu na kuchukua kilicho cha halali tu?” Akaendelea kuorodhesha vitu vyote tutakavyokuja kuulizwa.

Maelezo mengi sana yalitolewa lakini kiini cha mambo kilisahaulika na hivyo Sheikh Shibli akamuita yule mhubiri:

“Ewe mhubiri. Umesahau swali muhimu kuliko yote. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atauliza: **Ewe mja wangu! Nilikuwa pamoja na wewe katika kila jambo. Je Wewe ulikuwa na nani?”**

❁

Wakati mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu aliyeitwa Abu Bakr Kattani (roho yake itakaswe) alipokuwa juu ya kitanda cha mauti aliulizwa ni amali gani njema ambayo aliifanya katika uhai wake. Alitoa jibu lifuatalo lenye kuvutia:

“Kama ningelikuwa sifahamu kuwa mauti yangu yanakaribia nisingeliongelea amali zangu kutokana kuhofia kujionyesha. Kwa miaka yote arobaini nimekuwa nikiangalia mlango wa moyo wangu. Nilijaribu kutoufungua kwa ajili ya yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu. Ikapelekea moyo wangu kufikia mahali ambapo haukuweza kutambua chochote kingine kinyume na Mwenyezi Mungu”.

❁

Kutokana na masimulizi mbalimbali, siku moja nabii Issa عليه السلام alikutana na mgonjwa ambaye ngozi yake ilikuwa na rangi mbili na panja lake la kichwa limechakaa. Yule mtu alikuwa hautambui ugonjwa wake na alikuwa akijiambia mwenyewe:

“Ewe Mola wangu! Sifa nyingi na shukurani ziwe juu yako kutokana na kuniepusha na wasiwasi ambao umewapa watu wengi...”

Ili kutambua kiwango cha utambuzi na ukamilifu wa imani ya mtu huyu, nabii Issa akamuuliza:

"Ewe mtu. Je ni wasiwasi gani ambao Mwenyezi Mungu amekuepushia?"

Yule mgonjwa akajibu:

"Ewe roho wa Mwenyezi Mungu! Ugonjwa wa hatari kuliko yote ni kwa moyo kumpuuzia na kumuacha Mwenyezi Mungu. Namshukuru Mungu kuwa niko katika furaha ya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndio maana siutambui ugonjwa ulioko mwilini mwangu..."

❁

Siku moja kulitokea uvumi kuwa Sheikh Muhammad Nur al-Arabi ambaye ni mwanachuoni wa kisufi maarufu katika karne ya 19, alikana kuwa mwanadamu hakuwa na uwezo wowote, yani alikataa fikra ya *'juz'i irada'* au uwezo pungufu wa mwanadamu. Baada ya Sultani Abdulmajid Han kulisikia jambo hili aliagiza mtu huyu aalikwe ili aje kumuuliza juu jambo hili. Agizo hili lilitekelezwa na hivyo Sheikh alialikwa kwa ajili ya mazungumzo. Pindi alipoulizwa juu ya suala lililokuwepo mezani alijibu kama ifuatavyo:

"Sikukana kuwa hakuna uwezo pungufu kwa ujumla wake. Lakini mimi nilisema kwamba kwa baadhi ya watu uwezo huu ni kama haupo. Kwani kwa marafiki wakubwa wa Mwenyezi Mungu ambao wakati wote wako mbele ya Mwenyezi Mungu, kwao kufanya jambo kwa uwezo wao ni kama haiwezekani, hivyo ni kana kwamba hawana kabisa huo uwezo pungufu. Watu hawa hawafanyi mambo kama wanavyotaka wao bali kulingana na matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye wako ndani ya ufalme wake. Kinyume chake wangelifanya mambo ambayo yangewapelekea kuingia kwenye makosa.

Kwa mfano kwa sasa tupo mbele ya Sultani. Kama tukiambiwa 'njooni', basi tunakuja, na kama tukiambiwa 'nendeni', tunaondoka. Haiwezekani tukafanya kile tunachotaka sisi kutokana na matakwa yetu kinyume na ya Sultani ambaye yuko mbele yetu. Lakini angalia watu wasiojali na viumbe wengine; wao wapo huru na wanafanya watakalo".

Kutokana na kutosheka na majibu haya, Sultani akamuonyesha Sheikh ukarimu mkubwa.

Wale watu wa *ihsan* na utambuzi ambao wanaishi huku wanafahamu kuwa Mwenyezi Mungu daima yupo na anawaangalia katika kila jambo lao, watakuwa katika hali ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na si kwenye matamanio ya nafsi zao katika mambo yote...

❁

Kwa ufupi *ihsan* na kuwa macho ni kiini na tunu ya imani. Matunda ya kumtambua Mwenyezi Mungu kama vile *khushu* (unyenyekevu), *ikhlas* (usafi wa moyo) na *taqwa* (uchamungu) miongoni mwa mambo mengine katika ibada na tabia vyote vitawezekana endapo moyo wa mtu utakuwa umefikia kwenye hali ya *ihsan*. Jambo lolote jema ambalo litafanywa katika hali ya 'kumuona' Mwenyezi Mungu Mtukufu litapelekea *ikhlas* na *taqwa* kuchanua na *khushu* kuwa matunda yake. Kuwa katika njia iliyonyooka hata pale ambapo watu hawakuoni na kujizuia na maovu hata pale unapokuwa mbali na jicho la mwanadamu kutawezekana pale tu mtu atakapotambua kuwa 'Mwenyezi Mungu ananiona popote nilipo na wakati wowote'. Ndio maana Usufi unalenga kwenye kufikia hali hii katika misingi na njia zake zote. Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni watafutaji wa hali hii katika maisha yao yote.

Hivyo kinachotulazimu sisi ni kupandisha daraja la nyoyo zetu kwa kiasi cha kuwa katika hali ya utambuzi na uouni wa uan-

galizi wa Mwenyezi Mungu juu yetu wakati wote. Kisha tupime mwenendo wetu dhidi ya *ihsan* aliyokuwa nayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kisha kuipa muelekeo kama inavyostahiki.

**"….Hakika rehema ya Mwenyzi Mungu iko karibu na wanao fanya mema"** (Al-A'raf, 7:56).

### 9. Tawadhu' (Unyenyekevu)

Tawadhu' ni kunyenyekea na kutambua uduni wako mbele ya Mwenyezi Mungu. Mtu anaweza akajaaliwa elimu, wadhifa na mali, lakini isije ikampelekea kuwakandamiza wengine ambao hawakujaaliwa vitu, ikiwa ni kimwili au kiakili na kujinadi kuwa mbora kuliko wao.

Mshairi mmoja ameligusia jambo hili vizuri:

*"Usijikweze kwa mali zako au utajiri, na usiseme 'je kuna mwingine kama mimi?*

*Kwani upepo uliopo kila mahali unaweza kuja na kubeba kila kitu"...*

Kila wakati na kila kesho vinatoka kwa Mwenyezi Mungu na hakuna yeyote ajuae ni lipi litampata baadae.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an: **"Na watwae kwa upole wanao kufuata miongoni mwa Waumini"** (Shu'ara, 26:215).

"**Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: Salama!"** (Furqan, 25:63).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Mwenyezi Mungu ameniamrisha yafuatayo:*

*Onyesha unyenyekevu kiasi kwamba hatokei mmoja wenu akajivuna mbele ya wenzake na pia asijitokeze yeyote miongoni mwenu akamkandamiza mwingine"* (Muslim, Jannah, 64).

*"Yeyote anayeonyesha unyenyekevu mbele ya mja wa Mwenyezi Mungu kwa lengo pekee la kupata radhi za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamnyanyua daraja"* (Ibn Maja, Zuhd, 16).

Nabii Idris ﷺ alikuwa akiwapa watu wake ushauri kwa maneno ya hekima. Moja wapo ya sehemu za hekima zake ni kama ifuatavyo:

"Kadiri daraja la mtu mwenye akili linavyopanda, ndivyo unyenyekevu wake unavyoongezeka".

Yusuf-i Asbat anaelezea namna ya kuimarisha hali ya *tawadhu'*, ambayo ni aina fulani ya 'udhalili', kama ifuatavyo:

"Kila unapoondoka nyumbani kwako asubuhi muangalie kila utakayekutana naye kuwa bora zaidi yako. Tawadhu' ni kwamba unakubali jambo la kweli unaloambiwa bila kujali linatoka kwa nani, na kuwaona wale walio chini yako kuwa juu yako. Wafanye wale ambao wanakupuuzia na wale ambao wanakusifu kuwa sawa mbele ya macho yako..."

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atawapa furaha kesho akhera wale ambao hawakujisifu kwa ufahari na majivuno katika dunia hii, ambao hawakusababisha madhara wala uasi, na ambao nyoyo zao zimejawa na mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Wale ambao walijiweka mbali na baraka za *tawadhu'* na kushikamana na tabia mbovu hawakuweza kukwepa kuwa kama Firauni. Kwa hali hiyo hatuna budi kushikamana na tawadhu' na kujiweka mbali na tabia za kudharau wengine.

Qur'an tukufu inatueleza:

"**Hayo ndiyo makaazi ya Akhera, tumewafanyia wale wasio taka kujitukuza duniani wala ufisadi. Na mwisho mwema ni wa wachamngu**" (Qasas 28:83).

Pia mshairi mmoja amelielezea jambo hili vizuri sana:

*"Mbegu ambayo haijapandwa ardhini haiwezi kuota (ndivyo hivyo pia ilivyo) huruma ya Mwingi wa Rehema hustawi kwa mtu ambaye ni mnyenyekevu".*[43]

Maswahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kamwe hawakuitumia vibaya nafasi yao hapa duniani waliyopewa na Mwenyezi Mungu na kamwe hawakujisifu kwa majivuno na ufahari kama njia ya kuonyesha wadhifa wao. Waliiga utaratibu wa unyenyekevu kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuufanya kuwa ndio kanuni ya maisha yao. Mji wa Madina ulijengwa na familia takriban mia nne, lakini ndani ya miaka kumi mipaka yake ilifika Iraq na Palestina. Wakati wa kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kulikuwa na vita kati ya watu wa Byzantine na Persian. Ngawira zilikuwa zikimiminikia ndani ya Madina. Hata hivyo hali ya maswahaba miaka kumi iliyopita, yani kujitenga na dunia, maisha yao ya staha, uchumi wa nyumba zao na ari yao ya kutoa, havikubadilika hata kidogo. Walihofia kuwa raha wanayoipata kutokana na imani yao ingeliharibiwa ndio maana walikuwa makini kupita kiasi kuhusiana na kutozitumia neema za kidunia kwa malengo yao binafsi. Hii ndio sababu iliyowafanya waelekeze maisha yao kwenye kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

***Matukio ya wema***

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alitumwa kama rehema kwa walimwengu wote na ambaye alikuwa sababu ya

43. Kama mbegu haijapandwa kwenye udongo haiwezi kuota na kukua. Vivi hivi rehema za Allah haziwezi kustawi na kuwaangukia wale wenye kujivuna na kujiona lakini kinyume chake ni kwa wale wenye unyenyekevu na staha.

kuumbwa kwa ulimwengu, alifanikiwa kuihifadhi hali yake ya tawadhu' na unyenyekevu licha ya kuwa na maadili bora na tabia njema. Alikuwa akirudia mara kwa mara:

"La fakhr" au "Sijisifu".

Wakati fulani maswahaba walikuwa wakiongea wao kwa wao. Walikuwa wakielezeana namna wanavyostaajabishwa na namna Mwenyezi Mungu alivyofanya urafiki na mwanadamu aliyemuumba mwenyewe, yani nabii Ibrahim, na namna gani aliongea na Musa, na namna gani nabii Issa alikuwa neno lake na uwezo wake, na namna alivyomchagua nabii Adam. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuja na kuwasikia. Alithibitisha yale waliyokuwa wakijadiliana kwa kusema: "Ndio, mambo yako kama hivyo mnavyosema". Kisha akataja sifa zake mwenyewe za kipekee:

*"Mimi ni kiongozi wa Mitume yote, lakini sijisifu! Mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wa mwisho, lakini sijisifu! Nitakuwa wa kwanza kuwaombea umma wangu na maombezi ndiyo yatakayokuwa ya kwanza kujibiwa, lakini siyasemi yote haya kwa ajili ya kujisifu"* (Darimi, Muqaddima, 8).

*"Siku ya kiama ambapo ardhi itakuwa imepasuliwa, nitakuwa wa kwanza kufufuliwa, hata hivyo siyasemi haya kwa ajili ya kujisifu. Bango la sifa nitapewa mimi lakini sijisifu kwa hili. Nitakuwa kiongozi wa watu wote siku ya kiama, lakini hakuna kujisifu. Nitakuwa wa kwanza kuingia peponi lakini siifanyi hii iwe sababu ya mimi kujisifu"* (Darimi, Muqaddima, 8. Pia angalia Tirmidhi, Manaqib, 1/3616).

❀

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa na trei la chakula lililoitwa 'Garra', trei ambalo lilikuwa likiwatosheleza watu wanne tu. Baada ya kumaliza swala ya dhuhur, trei lile lililetwa mbele yao likiwa na 'tirit', aina ya mkate uliotowezwa kwenye supu.

Maswahaba wakalizunguka. Idadi yao ilipokuwa imeongezeka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipiga magoti pembeni yao. Bedui mmoja aliyemuona alisema:

"Ni mtindo gani huu wa kukaa?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amenifanya kuwa mja mwema, na sio kiongozi katili"*. Kisha akaendelea:

*"Anzeni kula kuanzia pembezoni mwa sahani. Msianzie kati-kati, kufanya hivyo kutapelekea chakula chetu kibarikiwe"* (Abu Dawud, At'ime, 17/3773).

❁

Abdullah ibn Jubayr رضي الله عنه anasimulia:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akitembea pamoja na maswahaba zake. Mtu mmoja alimsogelea na kumkinga na jua kwa kutumia aina fulani ya kizuizi. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipogundua kuwa kumejitokeza kivuli alinyanyua kichwa chake na kuona kuwa kinasababishwa na kizuizi kile. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimwambia yule mtu akiachie kile kizuizi, kisha akakichukua na kukiweka chini na kusema: "Mimi ni mwanadamu kama nyinyi" (Haythami, IX, 21).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Inatosha kwa dhambi ya mtu kuweza kuonekana na watu"*

Aliulizwa:

"Hata kama ataonekana kuwa mwema ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Hata kama yeye ni mwema, isipokuwa kwa lile lililohifadhiwa na Mwenyezi Mungu. Kama atagundulika kuwa muovu, basi hali hii ni mbaya vile vile"* (Tabarani, Kabir, XIII, 138/14971. Pia angalia Tirmidhi, Qiyamah, 21/2453).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakutaka kuchukuliwa tofauti na marafiki zake. Wakati fulani walipokuwa katika msafara wa kivita, aliwaomba maswahaba zake wamchinje na kumpika kondoo. Mmoja wa maswahaba zake akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, niachie mimi nimchinje"

Mwingine akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, niachie mimi nimchune".

Mwingine akasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, niachie mimi nimpike".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Kama ni hivyo niacheni mimi nikatafute kuni"*.

Maswahaba zake wakasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Tutalifanya na hilo pia. Usijichoshe".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Ninafahamu kuwa mnaweza kunifanyia kazi zangu. Lakini sitaki kupewa kipaumbele dhidi yenu. Kwani Mwenyezi Mungu*

*aliye juu zaidi hapendi waja wake wapewe kipaumbele miongoni mwa marafiki zake”*.[44]

Kuingia kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndani ya Makka baada ya kuikomboa ni mfano mwingine wa unyenyekevu wa hali ya juu. Maswahaba waliokuwepo wakati ule wameelezea kama ifuatavyo:

“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa kiongozi wa jeshi ambalo liliingia Makka baada ya kuikomboa. Ushindi ulikuwa umepatikana kwa urahisi mkubwa na wakati anaingia Makka akiwa juu ya ngamia wake, alikuwa ameinamisha kichwa chake chini mno kutokana na unyenyekevu kwa Mola wake, kiasi kwamba ndevu zake zikawa zimegusa tandiko la ngamia. Kiuhalisia alikuwa anasujudu kama shukurani. Wakati wote akawa anasema:

*“Ewe Mwenyezi Mungu. Hakuna maisha ila maisha ya kesho akhera”* (Waqidi, II, 824, Bukhari, Riqaq, I).[45]

❀

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ameenda kumuaga Muadh ibn Jabal رضي الله عنه ambaye alikuwa amemteua kama gavana wa Yemen. Pamoja naye walikuwepo baadhi ya maswahaba kutoka Muhajirina na Answar. Muadh رضي الله عنه alikuwa juu ya mnyama wake wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu yuko pembeni yake anatembea kwa miguu. kutokana na kujisikia vibaya, Muadh رضي الله عنه akamwambia Mtume:

---

44. Kastallani, “al Mawahibu al-Ladunniyye,” Misri, 1281, I, 385)
45. Mjumbe wa Allah ﷺ alikuwa akiyarudia maneno haya mara kwa mara katika kuonyesha umuhimu wa akhera ukilinganisha na dunia. Kutokana na masimulizi mengine inasemekana kuwa aliyarudia maneno haya wakati wa ujenzi wa Masjid-i Nabawi (Msikiti wa Mtume), wakati mitaro inachimbwa wakati wa vita vya Handak, Wakati wa kuingia Makka baada ya kuitwaa na wakati alipoona kundi kubwa la waumini katika siku ya Arafa wakati wa hijja ya kuaga.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Mimi niko juu ya mnyama halafu wewe unatembea kwa miguu. Je naweza kushuka chini ili nitembee pamoja na wewe na maswahaba zako?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamtuliza na kumuonyesha ni jambo gani lilikuwa kichwani mwake:

*"Ewe Muadh! Ni matarajio yangu kwamba hizi hatua ninazozipiga ziwe hatua zilizopigwa katika njia ya Mwenyezi Mungu"*.[46]

Hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ni mfano mzuri mno wa unyenyekevu. Hofu yake haikuwa juu yake binafsi. Jambo pekee lililokuwa likimshughulisha, kiasi cha kumzeesha lilikuwa ni juu ya watu kuongozwa na kupata furaha hapa duniani na kesho akhera.

❁

Anas ؓ alikulia chini ya malezi ya Mtume. Kila alipokuwa akipita karibu na watoto alikuwa akiwasalimia na kusema:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pia alikuwa akiwasalimia watoto kama hivi" (Bukhari, Isti'zan, 15; Muslim, Salam, 15).

Katika mapokezi mengine, Anas anasema:

"Katika moja ya masiku yale wakati wa utoto wangu wakati ninacheza pamoja na mtoto mwingine, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitusogelea na kututolea salamu. Kisha akanishika mkono na kunituma mahali mara moja. Yeye mwenyewe akanisubiria chini ya kivuli cha ukuta mpaka niliporejea" (Abu Dawud, Adab, 135-13/5203).

Kingine tulichojifunza kutoka kwa Anas ؓ ni kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwatembelea Answar mara kwa mara. Alipokuwa akifika kwenye nyumba zao alikuwa

46. Diyarbakri, "Tarihu'l Hamis," Beirut ts. II 142.

akiwasalimia watoto, akiwashika vichwa vyao na kuwaombea. (Nasai, Sunan al-Kubra," VI, 90).

❁

Anas ﵁ anasimulia:

"Kijakazi yeyote ndani ya Madina alikuwa ana uwezo wa kushika mkono wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kwenda naye popote alipotaka" (Bukhari, Adab, 61).

Siku moja mwanamke mmoja aliyeitwa Ummu Zufer, ambaye alikuwa amechanganyikiwa kidogo, alienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kuna kitu ninataka unifanyie".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"Hakuna shida. Fanya tukutane popote unapopapenda kwa ajili ya kukusaidia". Kisha akasogea pembezoni mwa barabara na kumsikiliza yule mwanamke na kisha kumtatulia shida yake" (Muslim, Fadail, 76; Abu Dawud, Adab, 12/4818).

❁

Aisha ﵂ ambaye ni mke wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliulizwa:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akifanya nini anapokuwa nyumbani?"

Aisha akajibu:

"Alikuwa akiisaidia familia yake na muda wa swala unapofika huenda kuswali" (Bukhari, Athan 44, Nafaqat 8, Adab 40).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akishughulikia mahitaji yake na kuisaidia familia yake. Kuhusiana na mada hii tunaweza kumalizia kama ifuatavyo:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akifua nguo zake, akiwakamua kondoo maziwa, akishona nguo zake, akikarabati viatu vyake, akifagia nyumba yake, akimfunga ngamia wake na kumpa chakula chake, akila pamoja na watumishi, akifinyanga udongo pamoja nao na kubeba vitu alivyovinunua sokoni. Siku moja Abu Huraira ؓ alipojaribu kumbebea nguo alizonunua Mtume, alimwambia:

*"Ni vizuri zaidi kwa mtu kubeba vitu vyake mwenyewe. Pale tu atakaposhindwa ndio ndugu yake Muislamu anaweza kumsaidia"* (Haythami, V, 122).

Omar ؓ na Ali ؓ ambao waliishi kama alivyokuwa akiishi Mtume, walikuwa wakizunguka masokoni kwa ajili ya kununua mahitaji ya nyumba zao, hata walipokuwa makhalifa.

❁

Aisha ؓ kwa mara nyingine anasimulia tukio lifuatalo ambalo linaonyesha namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyokuwa akimsaidia majukumu ya nyumbani kwa unyenyekevu mkubwa:

"Usiku mmoja familia ya baba yangu, Abu Bakr ؓ, ilitutumia mguu wa kondoo. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliushikilia wakati ninaukata, au niliushikilia na yeye akaukata".

Mtu mmoja aliyekuwa akisikiliza aliuliza:

"Mliyafanya haya katika giza, taa ikiwa imezimwa?"

Aisha ؓ alijibu:

"Kama tungelikuwa na mafuta ya kuweka katika taa, tungelitoweza mkate wetu ndani yake na kuula. Mwezi mmoja ulikuwa

ukipita bila ya familia ya Muhammad ﷺ kupata hata mkate wa kula na hakuna vyungu vilivyokuwa vikichemka jikoni mwao" (Ahmad, VI, 217; Ibn Sa'd, I, 405).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kama nikikaribishwa nyama ya mguu au mtulinga, ninaenda haraka sana. Kama nikipewa zawadi ya nyama ya mguu au mtulinga, haraka mno naikubali".* (Bukhari, Hibe 2, Nikah 73; Muslim, Nikah 104).

Hivyo ukubwa wa zawadi sio muhimu. Lengo ni kumfurahisha mwenzako na kuongeza upendo wake kwako. Ili mtu afikie hatua hii ya moyo hana budi kujivisha joho la unyenyekevu.

❁

Kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakukua na kitu kikubwa zaidi ya kuwa mtumishi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Masimuliza yanayofafanua itikadi hii ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kama ifuatavyo:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amekaa pamoja na Malaika Jibril wanaongea. Wakati ule Malaika mwingine akashuka kutoka mbinguni. Jibril akamwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuwa malaika huyu ndio mara yake ya kwanza kushuka katika ardhi. Yule malaika akasema:

"Ewe Muhammad! Mola wangu amenituma kwako. Anakuuliza ikiwa unataka kuwa Mtume mfalme au Mtume mtumishi".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuangalia Jibril ambaye alisema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nyenyekea kwa Mola wako"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

“Nataka kuwa Mtume mtumishi”. (Ahmad II, 231; Haythami, IX, 18, 20).

Hivyo alikuwa mfano wa kuigwa juu ya unyenyekevu. Baada ya chaguo hili utumishi ukawa nyadhifa ya kuheshimika ambayo mwanadamu ataihitaji. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaonya wale waliomuonyesha unyenyekevu kupita kiasi:

*“Msinitukuze zaidi ya ninavyostahiki kutukuzwa. Kwani kabla ya kunituma kama Mjumbe, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi alinifanya kuwa mtumishi”.* (Haythami, IX, 21).

Hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alionyesha thamani na ubora wa kuwa mtumishi wa Mwenyezi Mungu.

❁

Licha ya kuwa na asili ya ukali, Khalifa wa pili Omar رضي الله عنه alikuwa mtu mnyenyekevu mno. Alikuwa akivaa nguo yenye viraka, akibeba maji na chakula na kuvipeleka kwenye nyumba za wajane na mayatima, akilala kwenye mkeka, na pia alikuwa akiwasugua na kuwaosha ngamia wake kwa mikono yake mwenyewe. Katika kipindi ambacho alikuwa khalifa, alikuwa akizunguka mitaani nyakati za usiku kwa ajili ya kusikiliza malalamiko ya watu. Abu Mahzura رضي الله عنه anasimulia juu ya unyenyekevu wake kama ifuatavyo:

“Siku moja nilipokuwa nimekaa karibu na Omar ibn Khattab رضي الله عنه, Safwan ibn Ummaya alileta bakuli la chakula na kuliweka mbele ya Omar. Omar akawaita masikini, wahitaji na watumwa waliokuwa wakiishi karibu naye. Wote walikuja na kula pamoja na Omar. Wakati wanakula Omar alisema:

“Mwenyezi Mungu hatawajaalia mafanikio wale wanaojisikia vibaya kula pamoja na watumwa”. Kutokana na haya Safwan ibn Ummaya akasema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Sisi hatuhisi aibu kula pamoja nao. Hata hivyo tunawapa wao kipaumbele juu yetu kiasi kwamba tukiwa na chakula kitamu na kizuri tunawapa wao" (Ali al-Muttaki, IX, 198/25650).

❁

Wakati mwingine katika ukhalifa wa Omar ﷺ, alikuwa anatembea pamoja na Jarud ibn Mualla, mmoja wa maswahaba, wakakutana na Khawlah ibnt-i Sa'laba. Khawlah ambaye alikuwa msichana mdogo wakati wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, kwa sasa alikuwa bibi kizee. Aya za mwanzoni mwa surat '*Mujadila*' zilishushwa kutokana na malalamiko yake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuhusu mume wake. Pindi swahaba huyu wa kike alipomuona Omar akataka kumpa ushauri:

"Ewe Omar!"

Omar aliposimama, Khawlah akamwambia yafuatayo:

"Tulikuwa tukikuita 'bwana mdogo Omar' kwa muda mrefu. Kisha ulipokuwa tukakuita 'kijana Omar'. Kwa sasa tunakutambua kama 'Omar, kiongozi wa waumini'. Ewe Omar, muogope Mwenyezi Mungu na ujishughulishe na matatizo ya watu. Kwani yeyote anayehofia adhabu ya Mwenyezi Mungu, chochote kilicho mbali kinakuwa karibu.Yule anayehofia kifo atakuwa makini kutopoteza nafasi yoyote aipatayo".

Omar aliguswa sana na maneno haya na kuanza kulia. Jarud ambaye alimuonea huruma Omar alimgeukia Khawlah na kumwambia:

"Hayo yanatosha wewe mwanamke! Umeshamuuzi kiongozi wa waumini". Hata hivyo Omar alimgeukia na kumwambia:

"Muache aendelee. Muache aseme anachotaka. Unajua huyu mwanamke ni nani? Huyu ni Khawlah, aliyetukuzwa na Mwenyezi

Mungu aliye juu zaidi, ambaye alisikia malalamiko yake tokea kwenye kiti chake kitukufu cha enzi. Naapa kwa Mwenyezi Mungu hata kama angelitaka kuniweka hapa usiku kucha, ningelienda kuswali na kurudi na kuendelea kumsikiliza".[47]

Huu ni ushahidi wa mfano wa hali ya unyenyekevu kwa muumini kama Omar ﷺ, ambaye alikuwa wa pekee katika tabia hasa katika masuala kama vile hofu juu ya Mwenyezi Mungu, heshima na mapenzi kwa Mwenyezi Mungu, ukweli, haki na kuwajibika.

❁

Katika mtindo wake wa kipekee Jalaluddin al-Rumi anatuelezea tukio lifuatalo ambalo ni mfano mzuri wa unyenyekevu wa Omar ﷺ, na ambao una mafunzo kwa watu wote:

Siku moja msafara kutoka Rumi ulikuja Madina kwa ajili ya mkutano wa kisiasa. Aliulizia lilipokuwa kasri la Omar. Alipewa jibu lifuatalo:

"Wadhifa wa khalifa una maana 'kiongozi wa waumini', na licha ya kuwa utawala wake inawezekana kuwa ulisambaa duniani kote, lakini hana kasri kwa jina lake. Kinyume chake moyo wake ndio kasri lake lenye kung'aa. Alikuwa na kijumba kidogo ambacho ndimo alipokuwa akiishi, kijumba hicho ni sawa na cha watu wapweke, masikini na wanaotangatanga, ambacho wanakitumia kujihifadhi. Lakini kutokana na udhaifu wa macho yako hutaweza kuliona kasri hilo la kiimani na lisilojiegemeza katika dunia na lililopo ndani ya moyo wake".

Msafara wa warumi ulitishika na maneno haya. Aliacha mzigo wake, farasi wake na zawadi zake na kuanza kumtafuta Omar al-

47. Angalia Mehmed Zihni Efendi, "Meshur Kadinlar," Istanbul ts., I, 250; M. Yasar Kandemir, I. Luti Cakan, Rasit Kucuk, "Riyadhus Saliheen – Translation and Exegesis," III, 508.

Faruq. Alimuulizia kila mahali. Kutokana na kushindwa kumpata akawa anamunyamunya mwenyewe kwa kustaajabu:

"Inamaanisha kuna mtawala katika ardhi hii ambaye anaweza kutoonekana na watu kama roho..." Hata hivyo aliendelea kumtafuta khalifa yule.

Mwisho wake mwanamke wa kiarabu akamwambia:

"Khalifa unayemtafuta yupo pale chini ya mtende. Wakati kila mtu analala katika kitanda chake na juu ya godoro (laini), yeye anafanya kinyume chake kwa kulala kwenye udongo. Nenda na ujionee mwenyewe 'kivuli cha Mwenyezi Mungu', kimelala chini ya kivuli cha mtende ule..."

Msafara ukahisi namna fulani ya utukufu kuhusu Omar aliyelala na roho yake ilikuwa ikisogea kwa upole. Alistaajabishwa na hisia hizi mbili za upendo na hofu ambazo licha ya kuwa tofauti, zilikutana kwenye roho yake mwenyewe. Alijiambia mwenyewe:

"Mimi ni mtu niliyekutana na wafalme na kusifiwa nao. Ingawa sijawahi kuona utukufu wa namna hii kwao, upendo na hofu juu ya mtu huyu imenifanya nipoteze fahamu.

Khalifa huyu amelala hapa bila ulinzi wowote na bila upanga. Na bado mimi nipo hapa nimesimama mbele yake, huku mwili wangu unatetemeka. Ni hali gani hii? Jambo hili linawezekanaje? Hofu hii lazima itoke kwa Mwenyezi Mungu. Haiwezi ikatoka kwa huyu mtu hapa aliyevalia joho duni..."

Mjumbe yule wakati yupo katika hali hii ya kuchanganyikiwa, mara Omar ﷺ akaamka. Mjumbe yule akamsalimia Omar kwa heshima kubwa. Khalifa akamuitikia salamu. Kisha akaanza kuongea na mjumbe yule, akimualika kwenye kasri la nafsi yake ambalo ndani yake alipata furaha. Aliukarabati na kuutibu moyo wake ambao mwanzoni ulikuwa umeharibika. Aliongea nae kwa maneno ya ufasaha, mazito na ya hekima.

Kadiri alivyokuwa akisikiliza, mjumbe yule alishuhudia hali na viwango mbalimbali. Mjumbe yule ambaye alikuja kwa Omar ﵁ kama mgeni sasa akawa rafiki mpendwa. Alijisikia furaha sana kutokana na maneno aliyokuwa akiyapokea kutoka kwa Omar. Alijisahau kuwa yeye ni mjumbe ambaye amekuja kutoa na kupokea ujumbe.

Kutokana na kujihisi raha ya aina yake, Omar ﵁ aliendelea kuongea naye. Alizungumzia vituo ambavyo nafsi haina budi kuvipitia na safari ya kiroho. Alizungumzia muda katika upeo wa muda, hali takatifu za marafiki wema wa Mwenyezi Mungu, na thamani isiyo na mipaka ya roho iliyoletwa hapa duniani.

Matokeo yake nuru ya imani ikamulika moyo wa mjumbe yule na akaamua kutoa shahada mbele ya khalifa. Hivyo akajiunga kwenye msafara (wenye furaha) unaoelekea kwenye furaha ya milele.

❁

Siku moja Ahnaf ibn Qays ﵁ alienda kumtembelea Omar ﵁ akiwa pamoja na viongozi wakubwa wa waarabu. Walipowasili walimkuta akikimbia huku na kule akiwa amelikunja joho lake juu ya tumbo. Omar ﵁ alipomuona Ahnaf akamwambia:

“Njoo unisaidie. Ngamia aliye chini ya dola ametoroka. Unajua ni watu wangapi wenye mgao wao kwenye ngamia huyu?”

Kisha mtu mmoja akamwambia:

“Ni kipi unachokihofia zaidi? Je huwezi kumteua mtumishi akamkamate ngamia huyo?”. Omar ﵁ akamjibu:

“Je kuna mtumishi bora zaidi yangu?”

Uzuri ulioje wa tabia yake! Namna gani ulivyokuwa ufasaha wake na unyenyekevu wake hali ya juu...

❁

Wakati Salman ﷺ alipokuwa gavana wa Madain, mtu mmoja aliyetoka kwenye kabila la watoto wa Taym aliwasili kutoka Damascus. Alikuwa amebeba mzigo mkubwa wa mitini. Pia Salman ﷺ alikuwa na nguo na joho duni. Watu wa Damascus walikuwa hawamfahamu Salman ﷺ. Alipomuona katika hali hii alimwambia:

"Njoo ubebe hivi vitu".

Salman ﷺ akauchukua mzigo ule na kuubeba mabegani mwake. Watu walipomuona walimtambua na kumwambia yule mtu:

"Mtu huyu aliyekubebea mzigo wako ni gavana wetu".

Yule mtu kutoka Damascus upesi akaomba msamaha:

"Samahani, sikujua kama ni wewe". Hata hivyo Salman ﷺ akajibu:

"Hakuna ubaya uliofanyika. Lakini sitaweka mzigo wako chini mpaka niufikishe kwenye nyumba yako" (Ibn Sa'd, IV, 88).

❁

Siku moja mjukuu wa Mtume, Hussain ﷺ alikuwa akitembea mitaani akawakuta masikini wakila vichembe vya mkate. Wale masikini wakamuita:

"Ewe mja wa Mwenyezi Mungu. Njoo ule pamoja nasi..."

Kutokana na kuwa mtu mnyenyekevu, Hussain alikubali ombi lao. Upesi akateremka juu ya farasi wake na kuanza kula kile walichokuwa wanakula. Pindi walipomaliza kula mjukuu huyu mzuri wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Nimekubali ombi lenu. Na nyinyi sasa njooni ninawakaribisha nyumbani kwangu..." Kisha nao wakaenda wote kwa pamoja kula kwenye nyumba ile iliyobarikiwa mno.

❁

Wanachuoni wakubwa wa umma huu Mtukufu wa waumini wana mifano yao wenyewe yenye kuonnyesha unyenyekevu. Siku moja khalifa Harun al-Rashid alimuuliza Imam Abu Yusuf juu ya jambo fulani.

Abu Yusuf akajibu:

"Sifahamu" Msaidizi wa khalifa akamwambia Abu Yusuf:

"Wewe unalipwa mshahara mzuri na marupurupu na bado unasema: 'Sifahamu".

Abu Yusuf akajibu:

"Mshahara wangu unalingana na ufahamu wangu. Kama ningelipewa mshahara kwa vitu vyote nisivyovijua basi katika hazina kusingelikuwa na fedha ya kutosha kunilipa mimi..."

Katika kukiri udhaifu wake, Al-Ghazzali pia naye alionyesha unyenyekevu kama huu:

"Kama ningelichukua vitu vyote nisivyovifahamu ukilinganisha na vitu vyote ninavyovifahamu na kuvikanyaga, basi kichwa changu kingeligusa anga".

❁

Wakati bado Khalid al-Baghdadi ni mwanafunzi na bado hajakabidhiwa leseni ya kufundishia, lakini tayari alikuwa akijulikana kwa ufahamu wake na alivuta umakini wa watu wote. Siku moja gavana wa Sulaymaniye, Abdurrahman Pasha alimtembelea na kustaajabishwa na ufahamu wake na busara zake, akamwambia:

"Chagua shule yoyote iliyopo Sulaymaniye na mimi nitakuteua uwe mwalimu wake". Hata hivyo kutokana na kuheshimu taratibu za elimu na kwa kutokabidhiwa leseni ya kufundishia

hakukubali ombi hili na kinyume chake akasema: “Mimi sina sifa za kuikubali nafasi hiyo”.[48]

Yildirim Bayazid Han aliwaalika masheikh na wanachuoni wakubwa akiwemo Amir Bukhari kwenye ufunguzi wa Ulu Cami (Msikiti mkubwa ndani ya Busra).

Ilikuwa ni ijumaa asubuhi na watu wote walikusanyika kwa ajili ya sherehe. Muda mfupi baadae Yildirim Bayazid Han akawasili na kumwambia Amir Bukhari, mwanae wa kambo:

“Ewe Amir! Njoo ufungue milango ya msikiti na uongoze swala. Ukiwa mmoja wa watu wakubwa katika jamii hii, unastahiki heshima hii”.

Amir Bukhari akakataa ombi hili kwa staha kubwa na kusema:

“Hapana Sultani wangu! Huna budi kumpa nafasi hii Sheikh Abu Hamiduddin”

Hata hivyo Bayazid Han hakuwahi kumsikia mtu huyu, akauliza:

“Ni nani huyo?”

Amir Bukhari Akajibu:

“Sultani wangu. Utakuwa umewahi kumsikia mtu aitwae Somuncu Baba ambaye ni mwoka mikate. Alijitolea mikate mingi wakati wa ujenzi wa Ulu Cami. Mtu huyu si mwingine zaidi ya Abu Hamiduddin ambaye ni rafiki mkubwa wa Mwenyezi Mungu”.

Kutokana haya Sultani akakubali ombi lake. Kisha Amir Bukhari akasimama na kumtambulisha Somuncu Baba kwenye mkusanyiko ule na kumkaribisha kwenye mimbar. Kutokana na kujihisi vibaya Somuncu Baba akamwambia Amir Bukhari:

48. Heyet, “Islam Alimleri Ansiklopedisi,” Istanbul, ts. Turkiye Gazetesi Publica-tions, XVIII, 78

“Ewe kiongozi wangu! Sasa umefanya nini? Umenionyesha kwa watu...” huku taratibu anasogea kwenye mimbar kwa unyenyekevu mkubwa.

Siku ile Somuncu Baba akiwa juu ya mimbar alitoa sherehe saba tofauti za sura ya ufungnuzi wa Qur’an, Al-Fatha. Baada ya pale aliondoka Bursa na kumchukua mwanafunzi wake Haji Bayram-i Wali na kwenda naye kuhiji, hatua iliyomlazimu baada ya siri yake kufunuliwa kwa watu.

❁

Tarehe 15 mwezi wa pili ndani ya mwaka 1517, Yavuz Sultan Selim Han aliingia kwenye kasri la Mamluk kutokana na sherehe kubwa iliyokuwa ikifanyika ndani yake. Wana historia wa wakati ule wanaelezea namna watu walivyompokea Yavuz ndani ya Misri kama ifuatavyo:

“Watu walimiminika kwenye mitaa na wengine kukimbilia kwenye madirisha yao kwa ajili ya kumuona mtu huyu. Walidhania kuwa angelikuwa tofauti, walifikiria kuwa mavazi yake na kilemba chake vingekuwa tofauti na wale waliomzunguka. Hata hivyo Yavuz hakuwa mbele ya sherehe zile, bali alikuwa katikati pamoja na mashujaa. Mavazi yake na kilemba chake havikuwa tofauti na vya watu waliomzunguka. Alikuwa akitembea kwa unyenyekevu mkubwa huku akiangalia mbele”.

❁

Baada ya safari ya Misri, Yavuz Sultan Selim Han alirejea Istanbul mchana kwa kupitia Uskudar. Baada ya kupata habari kuwa watu wa Istanbul wanamsubiria wampokee kwa sherehe kubwa na kumsifu alimwambia mkufunzi wake binafsi Hasan Can:

“Acha kiza kiingie, na kila mtu arudi nyumbani kwake, na mitaa ibakie mitupu ndio na mimi niingie Istanbul. Tusikubali

pongezi za wanadamu, kusifu kwao na mapambo ya ushindi yakazishinda nafsi zetu na kutupeleka chini..."

Hivyo tumemuona Yavuz- simba mwenye kuogopesha katika jangwa la Sinai; muumini mwenye kutokwa na machozi na mnyenyekevu katika milango ya Misri; na daruwesh ambaye ameiwajibisha nafsi yake kwa lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Alimsomea Hasan Can mistari ifuatayo:

*Kuwa Sultani wa dunia ni jambo dogo mno.*
*Kuwa mwema ni bora kuliko mambo yote...*

❁

Pindi habari za ushindi mkubwa uliopataikana Kanije zilipofika kwenye kasri, Sultani III, Mehmed Han alifurahi mno na kuamua kumpa wadhifa wa uwaziri mkuu Tiryaki Hasan Pasha ambaye alikuwa mhusika mkubwa katika ushindi ule. Kwa kuongezea ni kwamba alimtumia Pasha zawadi nyingi za thamani na barua iliyoandikwa kwa mwandiko wake mwenyewe.

Huku akiisoma barua hii mbele ya maveterani wa vita, Tiryaki Hasan Pasha pia alionyesha unyenyekevu wa hali ya juu licha ya ushindi wake mkubwa. Aliwaambia wale waliomzunguka kwa staha kubwa:

"Sultani wa dola yetu amenichagua mimi kuwa waziri mkuu na isitoshe amenitumia barua iliyoandikwa kwa mkono wake mwenyewe kama zawadi juu ya kuihami kwetu Kanije. Hata hivyo tulichokifanya ni jukumu letu. Je mzee huyu anastahiki kweli uwaziri mkuu katika dola kubwa kama ile? Mwenyezi Mungu ailinde dola yetu na taifa letu!"

❁

Bwana mkubwa Sinan ambaye alikuwa kipaji kikubwa cha usanifu wa majengo katika dola ya Uthmainiyya, mwenyewe ali-

jiona kama sisimizi mdogo mno mbele ya Mwenyezi Mungu licha ya kuwa na mafanikio makubwa. Haya ni kwa sababu alikuwa kiongozi mwenye unyenyekevu mkubwa.

Mimar Sinan aliweka juhudi zake zote katika kuhakikisha kuwa msikiti wa Sulaymaniye unabakia wima mpaka siku ya kiama. Aliomba dua nyingi juu suala hili na matokeo yake kwa rehma za Mwenyezi Mungu alitengeneza mchoro wa msikiti usiokuwa na mfano wake. Hata hivyo ulipofika wakati wa kujitengenezea mwenyewe kaburi lake aliliweka kwenye pembe ya msikiti kama ishara ya staha. Licha ya kujenga misikiti maarufu na mizuri lakini hakujisifu na kujikweza. Licha ya kusaini jina lake kama 'Ser-Mimaran-i

Hassa' (Mkuu wa wasanifu majengo), pia alitumia majina kama vile 'Mur'i Natuvan' (sisimizi dhaifu), 'Al-Fakiru'l Hakir' (Masikini duni). Vile vile katika ukamilishaji wake wa mchoro mkubwa wa msikiti wa Selimiye, aliombwa kuandika jina lake kwenye kisahani ili kikawekwe kwenye mlango wa msikiti. Akajibu kama ifuatavyo:

"Mimi ni nani mpaka mliweke jina langu kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu!..." Hivyo alionyesha imani ya hali ya juu ambayo ilikuwa sawa na uzuri wa kazi zake...

Siku moja Sultani Ahmad Han alimtumia mwalimu wake mpendwa Mahmud Hudayi zawadi yenye thamani kubwa. Hata hivyo, Mahmud Hudayi hakuikubali zawadi ile. Kwa kuwa Sultani Ahmad Han aliahidi kuitoa zawadi ile akaamua kumtumia Sheikh wa wakati ule, Abdulmajid Siwasi. Yeye aliikubali. Baadae Sultani Ahmad Han alipomtembelea Abdulmajid Siwasi alimwambia:

"Bwana wangu! Mwanzoni nilimtumia zawadi hii mwalimu Mahmud Hudayi lakini aliikataa. Lakini wewe umeikubali".

Kwa kuelewa sababu ya jambo lile, Siwasi alitoa jibu lifuatalo zuri:

"Sultani wangu! Bwana mkubwa Hudayi ni ndege Mtukufu ambaye hakubali kula mizoga".

Sultani aliridhishwa na jibu hili na baada ya siku chache akaenda kumtembelea bwana Hudayi. Akamwambia:

"Bwana wangu. Bwana Abdulmajid aliikubali zawadi yangu ambayo wewe uliikataa".

Bwana Hudayi akamjibu huku ametabasamu:

"Sultani wangu! Bwana Abdulmajid ni bahari yenye kina kirefu. Tone dogo la uchafu litakalodondoka kwenye bahari hiyo kubwa haliwezi kuathiri utwaharifu wake".

Uzuri ulioje wa mfano huu wenye kuonyesha adabu za kiislamu na uzuri ulioje wa unyenyekevu uliopo ndani yake...

Daktari wa kifaransa aliyeitwa A. Brayer ambaye aliishi Istanbul kwa miaka mingi na ambaye kwa umakini mkubwa aliangalia maisha ya kijamii ya watu wa dola ya Uthmainiyya, ana yafuatayo ya kusema:

"Kutokana na staha na maadili yao, tabia za kujiona na kujisifu zilitoweka kwa waislamu wa uturuki. Kwani kujiona na kujisifu ni tabia mbili hasi ambazo Uislamu umezikemea kwa nguvu. Wakati wote waislamu wanaonyana wao kwa wao juu ya mambo yafuatayo:

"Usitembee juu ya ardhi kwa majivuno na usiwape watu mgongo kutokana na kiburi".

"Mwenyezi Mungu anamchukia yule anayejisifu kupita kiasi na kufanya kiburi".

"Kuwa mpole katika matendo yako na ongea kwa sauti laini"

"Majivuno yanatokana na ujinga, kamwe mwanachuoni hajivuni".

"Unyenyekevu unampa mtu heshima".

Ni kutokana na haya ndio maana kuna heshima na utukufu kwenye dola ya Uthmainiyya, lakini wakati huo huo hakuna majivuno wala kujionyesha. Wakati wote wanaongea kwa ulaini. Kamwe huwezi kuhisi mazingira ya udikteta katika maongezi yao. Pia kuna uzuri na wepesi katika huduma zao".

Hivyo hali hii ya kiakili iliyopo katika maisha ya kijamii ya dola ya Uthmainiyya inaweza kuonekana kwenye jamii nzima kuanzia kwenye watu wa chini kabisa mpaka kwa Sultani. Hivyo kuanzia mwanzoni mpaka kuanguka kwake, Masultani wa dola ya Uthmainiyya kila walipohudhuria hotuba ya ijumaa, walikuwa wakiwaamuru askari wao wawaambia:

"Usiwe na kiburi Sultani wangu; Mwenyezi Mungu ni mkuu kuliko wewe..." Walilifanya onyo hili rasmi kuwa desturi yao.

Kwa ufupi ni kwamba kuna manufaa mengi kwa mtu kuwa mnyenyekevu. Mtu mnyenyekevu ni mkarimu. Mtu mkarimu ni mwenye huruma. Mtu mwenye huruma ni mwenye furaha na shauku ya kuwahudumia viumbe wengine. Na hii ni njia ya kupata radhi za Mola wetu. Mtu aliye mbali na Unyenyekevu anakosa sifa zote hizi nzuri.

Kwani ufahamu na utambuzi ukiingia kwa mtu mnyenyekevu ataweza kutofautisha kati rafiki na adui.

Unyenyekevu ni sifa muhimu sana kwani inamsafisha mtu, inakuza utumishi wake kwa Mwenyezi Mungu na inapendezesha tabia yake. Rumi amesema yafuatayo:

"Hata wakati wa majira ya kuchipua hamtaweza kuona uhai ukitoka kwenye mwamba mgumu. Kuweni wanyenyekevu kama

ardhi ili maua na mawaridi ya rangi zote yaweze kuchanua kutokea ndani yenu”.

Ukweli ni kwamba viumbe wanaotembea juu ya ardhi wanaiponda na kuacha vumbi. Hata hivyo ardhi kutokana na unyenyekevu mkubwa inalilowesha na kulisafisha vumbe lote. Na kutokea ndani yake inachanua mimea ya aina mbali mbali ambayo ni chakula kwa viumbe wanaotembea juu yake. Hivyo ndivyo moyo wa muumini unavyotakiwa kuwa. Hauna budi kutafakari juu ya uzuri wote uliopo juu yake na kuuwasilisha kwa watu na viumbe wote kwa njia ya shairi zuri lenye kuvutia.

### *10. Hilm* na *Musamahah* (upole na uvumilivu)

*Hilm* ni neno linalomuelezea mtu ambaye hahisi uchungu ndani ya moyo wake hata kwa wale wanaomuumiza kwa namna fulani. Huku ni kuwa na subira na uvumilivu juu ya wengine.

*Hilm* au huruma na upole ni tabia anazozipenda zaidi Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Haya ni kinyume na ghadhabu. Ukatili na ukali ambavyo ni kinyume na *hilm*, ni tabia mbaya mno ambazo zinawadhuru watu, ambazo zinawafanya watu kuwa na hofu na chuki na kukengeuka. Hivyo *hilm* ni moja ya sifa za Mitume. Yeyote ambaye si halim au hana huruma na upole, hawezi kutekeleza jukumu muhimu kama hili la utume. Kutokana na kulielewa suala hili kutoka kwenye vitabu na kisha kushuhudia hali ya upole na huruma kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, wanachuoni wengi wa kiyahudi waliingia kwenye Uislamu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anasema yafuatayo ndani ya Qur’an:

**“Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombee maghfira, na shauriana nao katika**

**mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea"** (Al'I Imran, 3:159).

Uislamu umeikubali kama kanuni muhimu kujipamba na msimamo wa wastani, bila ya kuvuka mipaka hasa katika masuala kama vile kuwafundisha wanadamu na kutangaza dini. Kanani hii inaweza kupatikana kwa kupitia sifa ya *hilm* pekee.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatufahamisha kuwa Yeye ni *Al-Halim*, yani mwenye kumiliki *hilm*. Na hivyo mikusanyiko yote ya Mitume, wanadamu wapole kuliko wote, ilitawaliwa na tabia kama vile huruma, elimu, staha, subira, kumtegemea Mwenyezi Mungu na uaminifu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitaka kanuni hii ya upole na uvumilivu utawale maisha yake yote. Aliongelea ubora wa tabia hii kuwepo kwenye biashara kama ifuatavyo:

"Mwenyezi Mungu amrehemu yeyote atakayeonyesha wepesi katika masuala ya kununua, kuuza na kudai kulipwa deni lake" (Bukhari, Buyuu', 1; Ibn Maja, Tijaarah, 28).

Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Wakati fulani kulikuwa na mtu ambaye anawakopesha watu fedha. Alimwambia mtumishi wake (aliyekuwa akikusanya madeni):*

*"Ama utakutana na mtu akiwa katika shida kubwa (ambaye tumemkopesha fedha), upesi msamehe deni lake; kisha na sisi tutarajie kuwa Mwenyezi Mungu atatusamehe madhambi yetu'*

*Mara yule mtu akarejea kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akiwa amemsamehe madhambi yake yote"* (Bukhari, Anbiya, 54; Muslim, Musakat, 31; Bukhari, Buyu' 18).

*Hadith* nyingine ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni hii ifuatayo:

*"Katika siku ambayo hakutakuwa na kivuli, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamfunika (atamlinda) yule ambaye anamuongeza muda yule anayemdai, (au ambaye anamfutia deni kabisa)"* (Muslim, Zuhd, 74).

Hata hivyo haya hayamaanishi kuwa yeyote anayekopa fedha aitumie vibaya nafasi hii ya tabia ya wema kwa mtu anayemkopesha fedha. Mada ya kukopa fedha ni muhimu mno kiasi kwamba kila mtu alipofariki na kuletwa kwenye mazishi, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa kwanza akiuliza:

"Je mtu huyu alikuwa na madeni?", kama alikuwa nayo, alikuwa akiamuru madeni hayo yalipwe ndio amswalie maiti na kama madeni hayakulipwa alikuwa hamswalii maiti.

Kwa upande mwingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa wakati wote akiwavumilia sana waislamu wapya na wale wasiopata nafasi ya kujifunza vya kutosha kuhusu dini. Hivyo huruma na upole ni sifa mbili muhimu mno kwa watu wote wema ambao wamefungamana na mwenendo wa Mtume.

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimwambia Ashajj kuhusu watoto wa Abdulqays:

*"Mna sifa mbili ambazo zinapendwa sana na Mwenyezi Mungu: hilm (asili ya upole) na kuwa makini katika matendo yenu"* (Muslim, Iman, 25,26).

Luqman Hakim alisema:

"Ewe mwanangu! Vitu vitatu vinaweza kuonekana kutokana na vitu vingine vitatu: *Hilm* wakati wa hasira; ushupavu katika uwanja wa vita; na udugu wakati wa matatizo".

Kama zilivyo sifa nyingine za wema, pia upole na uvumilivu vina thamani kubwa. Kumdhulumu mtu kutokana na upole wake na kuonyesha uvumilivu juu ya ukiukwaji wa sheria za Mwenyezi Mungu kamwe si msimamo sahihi wa kuwa nao. Mwenendo huo ni elekevu[49] na ni mbaya kwani unawapelekea watu waovu kufuata matamanio yao zaidi.

***Matukio ya wema***

Abu Said al-Khudri ﷺ anasimulia:

Wakati fulani Bedui alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kutaka alipwe deni lake na alifanya hivi kwa ukali mno. Alisema:

"Sitakuachia mpaka unilipe deni lako". Maswahaba wakamfokea yule Bedui kwa kumwambia:

"Huna aibu! Unajua unaongea na nani?" Yule Bedui akajibu:

"Ninataka haki yangu". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaambia maswahaba zake:

*"Kwa nini hampo kwenye upande wa yule aliye kulia?"* Kisha akamgeukia Khawlah bint-i Kays na kumwambia:

*"Kama una tende kavu naomba unilipia deni langu; kitakapofika kipindi cha mavuno ya tende zetu nitakulipa"*.

Khawlah akajibu:

"Kwa namna yoyote ile! Na baba yangu atolewe kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!".

Mwanamke yule akamkopesha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ tende kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ naye akalipa deni

49. Maneno Hilmi khimari yanaashiria utiifu wa mnyama.

lake kwa yule Bedui. Pia akamkaribisha chakula. Yule Bedui akasema yafuatayo katika kuonyesha shukrani zake:

"Umenilipa deni lako vizuri. Mwenyezi Mungu akulipe kwa ukamilifu"

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Wale wanaolipa madeni yao ni bora miongoni mwa watu. Katika jamii ambayo watu dhaifu hawawezi kupata haki zao bila kuumizwa haitaendelea"* (Ibn Majah, Sadaqa, 17).

Kama tulivyoona, Maisha ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yamejawa na tabia nzuri mno na ni kiigizo kwa wanadamu katika kila hali itakayomfika. Tunachotakiwa kufanya ni kumsoma vizuri na kufanya juhudi kufuata nyayo zake.

❁

Jubayr ibn Mut'im رضي الله عنه anasimulia:

Wakati tunarejea kutoka kwenye vita vya Hunayn, baadhi ya mabedui wa kiarabu ambao walikuwa wanatembea pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakaanza kusisitiza wapewe mgao wao wa ngawira. Mara wakamsimamisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ chini ya mti wa Semura ambapo joho lake lilisokotwa kwenye tawi la mti. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisimamisha ngamia wake na kusema:

*"Nirudishieni joho langu! Hata kama ningelikuwa na wanyama wengi kama miti hii mnayoiona hapa ningelifanya mgao na nyinyi wote. Na mngeliona kuwa mimi si mchoyo, muongo au muoga!"* (Bukhari, Jihad 24, Khumus 19).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mpole na mvumilivu hata kwa watu ambao ndio wameingia kwenye Uislamu na hivyo hawajaingiza nyoyoni mwao ulaini na upole wa dini.

❁

Anas ﷺ anasimulia:

"Kamwe sikuwahi kugusa kitu chochote, iwe ni atlasi au hariri, ambacho kilikuwa laini kuliko mikono ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kamwe sikuwahi kunusa manukato mazuri kuliko manukato ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Nilimtumikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa miaka kumi. Kamwe hakuwahi kuniambia hata 'oof'. Kamwe hakuniuliza juu ya jambo nililolifanya: "Kwa nini umefanya hivyo?" wala hakuwahi kuniuliza juu ya jambo nisilolifanya: "Je umeshindwa kufanya kadha wa kadha?" (Bukhari, Sawm 53, Manaqib 23; Muslim, Fadail 82).

Hivyo ndivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyomfunza na kumuelimisha Anas, kihali na kivitendo, Anas ambaye alikabidhiwa kumlea akiwa na umri wa miaka kumi. Pia hii ni njia ya kujifunzia katika tasawwuf. Mtu hupenda mwenendo fulani na tabia fulani za mtu na kuanza kumuiga mtu huyo. Kwani kawaida ya kuiga ni moja wapo ya desturi za msingi katika asili ya mwanadamu. Ndio maana ukuaji wa kiwiliwili na kiroho kwa mtu- ikiwa ni hasi au chanya- vinaathiriwa na mtu anayempenda na ambaye ndiye anamuiga.

Muawiya ibn Hakam ﷺ anasimulia:

Tulipokuwa tukiswali katika jamaa nyuma ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, mtu mmoja alipiga chafya. Upesi nikasema: "Yarhamukallah"[50]. Watu wakaanza kuniangalia kwa hasira. Kisha nikawaambia:

"Kuna tatizo gani? Kwa nini mnaniangalia kiasi hicho?"

Kisha wakaanza kupiga piga magoti yao kwa mikono yao. Nilipogundua kuwa wanajaribu kuninyamazisha nikapandwa na hasira lakini nikabakia kimya.[51]

50. *Yarhamukallah* ni maneno yanayotamkwa pindi mtu anapopiga chafya, na linamaanisha 'Mwenyezi Mungu akurehemu' (Maelezo ya mfasiri).

51. Kufanya kitendo kinyume na swala unapokuwa ndani ya swala ni jambo

Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Sijapata kuona mwalimu mzuri kama yeye, ama kabla yake au baada yake. Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakunifokea wala kunipiga. Baada ya swala aliniambia kwa upole:

*"Hii ibada tunayoitekeleza inaitwa swala. Wakati tupo ndani ya swala haturuhusiwi kuongea maneno yoyote yanayohusiana na dunia hii. Kwani swala inahusisha kumtukuza na kumsifu Mwenyezi Mungu na kusoma Qur'an*".

Kisha nikamwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ndio hivi karibuni nimeingia kwenye Uislamu..." (Muslim, Masajid, 33).

❁

Mwanachuoni mmoja wa kiyahudi aliyeitwa Zayd ibn Sa'na alikuwa anachunguza ikiwa maandiko yaliyomhusu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wa mwisho yaliyokuwa ndani ya taurati yalikuwa yanaendana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Siku moja alimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akitoka nyumbani kwake akiwa pamoja na Ali ؓ akaanza kumfuatilia. Wakati ule mtu mmoja aliyevalia kama Bedui alimsogelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nimewaambia kabila kadha wa kadha kuwa kama wataingia katika Uislamu, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atawazidishia riziki zao. Kisha wakaingia kwenye Uislamu. Lakini kwa bahati mbaya wakakutana na ukame. Kwa sasa wapo katika hali mbaya mno. Kwa sasa nahofia kuwa

lisilokubalika. Hata hivyo hatuna budi kumchukulia kama dharura huyu swahaba ambaye alipandwa na hasira na maswahaba aliowakasirikia kwa kuonyesha tabia ile. Haya yaliweza kutokea kwa sababu wakati ule jamii ilikuwa na watu wapya katika uislamu na ambao ndio walikuwa wanaanza kujifunza kuhusu ibada na taratibu zake.

kwa kuingia kwao kwenye Uislamu kutokana na matarajio ya kidunia kutawafanya warudi katika dini zao za zamani pindi matarajio yao yasipotimia. Kama utapenda kuwasaidia basi nitawapelekea chochote utakachonipatia".

Alipoona hii ni nafasi muafaka ya kumjaribu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ, Zayd ibn Sa'na ambaye alikuwa akisikiliza maongezi haya aliwakatisha na kusema:

"Ewe Muhammad! Kama utaamua kuwasaidia watu hawa basi nitakubaliana na wewe nikukopeshe".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikubali mkopo wa dinar 80 kutoka kwa mtu yule na kumpa yule swahaba kwa ajili ya kuwapelekea wale watu. Kisha akamwambia:

*"Nenda upesi ukawasaidie".*

Siku nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa pamoja na Abu Bakr ؓ, Omar ؓ na baadhi ya maswahaba wengine walikuwa wamebeba maiti kwa ajili ya kwenda kumzika Jannatu al-Baqi[52]. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuongoza swala ya maiti kwa ajili ya mtu yule, Zayd akamsogelea na akamvua joho lake kwa nyuma. Akiwa bado hajafahamu ni kwa nini Zayd amefanya vile, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu huku amestaajabu akaangalia joho lililokuwa limedondoka na kisha kwenye uso ulioghadhibika wa Zayd. Huku akiwa tayari amepanga maneno ya kusema, Zayd akaanza kumwambia Mtume:

"Je hutalipa mkopo wako ewe Muhammad? Nyinyi wana wa Abdulmuttalib wakati wote mnachelewesha kulipa madeni yenu".

Hata hivyo muda wa mkopo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliokopa kwa Zayd ulikuwa bado haujaisha.

52. Jannatu al-Baqi ni eneo la makaburi maarufu ndani ya Madina lililopo mita 100 kutoka kwenye msikiti wa Mtume.

Zayd ambaye ndiye anasimulia tukio hili ana yafuatayo ya kusema:

"Kisha nikageuka kumuangalia Omar. Nilipomuona amepandwa na hasira, moyo wangu ukashtuka kidogo. Omar akaniangalia na kusema:

"Ewe adui wa Mwenyezi Mungu! Ni kweli haya maneno yako unamwambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Umemvunjia heshima na unaongea maneno machafu. Ninaapa kwa Yule aliyemtuma kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba kama ungelikuwa humdai ningelikata kichwa chako"...

Omar hakuweza kuvumilia kuona myahudi anamtukana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Baada ya kuona namna Omar alivyoghadhibika, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatabasamu na kusema:

*"Tulia ewe Omar! Wakati huu mimi na mtu huyu tunategemea aina tofauti ya tabia kutoka kwako. Ungelitakiwa unishauri nilipe deni langu katika njia bora na ungelikuwa umemshauri huyu mtu aombe fedha zake kwa maneno mazuri zaidi, ingawa bado nina siku tatu zimebaki kabla ya kulipa deni langu. Sasa simama na unilipie deni langu. Na mpe fedha ya ziada kwa kuwa umemtisha"*.

Baada ya kupokea zaidi ya kile alichotoa, Zayd alikiri kwa Omar:

"Angalia ewe Omar! Kila mara nilipomuangalia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu niliweza kuona ishara za utume katika uso wake. Hata hivyo mpaka leo nilikuwa sina uhakika ikiwa alikuwa nazo au hakuwa nazo sifa mbili. Je alikuwa akiwasamehe wale waliomtendea ubaya? Na je upole wake na huruma yake ilikuwa ikiongezeka kadiri ubaya dhidi yake ulipoongezeka? Na hivyo leo hii nimeyajaribu yote haya. Na sasa nina uthibitisho thabiti kuwa yeye ndiye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyekuwa akisubiri-

wa. Shuhudia kuwa ninamkubali Mwenyezi Mungu kuwa Mola wangu, Uislamu kuwa dini yangu, Muhammad ﷺ kuwa Mtume wangu na ninajitolea nusu ya utajiri wangu kuwa sadaka kwa ajili ya umma wa Muhammad".

Omar ؓ alifurahi mno kutokana na kusilimu kwa Zayd na akamuonya kwa upole:

"Huna utajiri wa kututosha waislamu wote. Angalau sema kuwa unatoa sadaka kwa ajili ya baadhi ya waislamu".

Katika kusahihisha maneno yake ya mwanzo, Zayd akasema:

"Umesema kweli. Natoa nusu ya utajiri wangu kwa ajili ya baadhi ya waislamu" (Hakim, III, 700/6547).

❁

Tabia na heshima ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ viliwavutia watu wengi na namna alivyokuwa na upole, uvumilivu na subira. Kwa rehma za Mwenyezi Mungu aliweza kusambaza Uislamu katika ukanda wote wa Uarabuni ndani ya muda mfupi.

Miongoni mwa wafungwa waliochukuliwa katika msafara wa kivita wa Abdullah ibn Jahs kwenda kwa Batn-i Nahla alikuwepo Hakem ibn Kaysan. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimkaribisha Hakem katika Uislamu.

Alimuelezea kwa kirefu uzuri wa Uislamu. Alirudia tena na tena ili kumuondoa wasi wasi. Licha ya juhudi yote hii ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu lakini Hakem hakuingia kwenye Uislamu. Jambo hili lilimuudhi sana Omar ؓ.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Unaendelea kuongea naye nini? Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika hawezi kuingia kwenye Uislamu. Niruhusu nimkate shingo yake atangulie Motoni, ambamo ndimo hatima yake". Hata hivyo Mjumbe wa Mwe-

nyezi Mungu ﷺ aliendelea kumuelezea Hakem kuhusu Uislamu. Ikafikia mahali Hakem akafungua masikio yake na kuuliza:

"Uislam ni nini?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"Ni kumtumikia Mwenyezi Mungu bila ya kumfanyia washirika na kushuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mjumbe wake".

Kisha Hakem akasema:

"Nimeshaingia kwenye Uislamu".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawageukia maswahaba zake na kuwaambia:

"Kama ningelikubaliana na mapendekezo yenu, sasa hivi mtu huyu angelikuwa ni wa motoni".

Kisha Omar ؓ akasema:

"Nilipomuona Hakem ameingia kwenye Uislamu, nilihisi kana kwamba wakati wangu uliopita na ujao vyote vinanikandamiza kwa pamoja. Nikajiambia mwenyewe: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anajua vizuri zaidi yako sasa kwa nini umeenda kinyume naye". Kisha nikajituliza mwenyewe kwa kusema: "Hata hivyo lengo langu pekee lilikuwa ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake". Hakem aliingia kwenye Uislamu. Na naapa kwa Mwenyezi Mungu alikuwa Muislamu mzuri sana. Alipambana katika njia ya Mwenyezi Mungu na kufa shahidi pale Bi'r-i Mauna" (Ibn Sa'd, IV, 137-138; Waqidi, I, 15-16).

❁

Abu Huraira ؓ anasimulia tukio lifuatalo:

"Mmoja wa mabedui alijisaidia ndani ya msikiti wa Mtume. Upesi maswahaba wakaanza kumkaripia. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Muacheni huyo mtu. Mwagieni ndoo ya maji mahali alipojisaidia. Mliletwa kurahisisha mambo, na si kufanya mambo kuwa magumu"* (Bukhari, Wudu', 58; Adab 80).

❁

Anas ﷺ anasimulia:

"Siku moja nilikuwa ninatembea pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Alikuwa amevalia joho lililotengenezwa kwa kitambaa kutoka Najran, ambacho kilikuwa kigumu mno na kizito. Bedui mmoja akamsogelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuvuta joho lake kikatili. Kitendo hiki cha yule Bedui kiliacha alama nyekundu kwenye shingo ya Mtume. Baadae yule Bedui akasema:

"Ewe Muhammad! Amuru baadhi ya mali ya Mwenyezi Mungu ambayo iko kwako nipewe mimi".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamgeukia yule Bedui na kutabasamu. Baadae akakubali kutekeleza alichoambiwa na Bedui yule. (Bukhari, Khumus 19, Libas 18, Adab 8; Muslim, Zakat 128).

Uvumilivu na upole ulioje...

❁

Siku moja wakati Abu Darda anazunguka katika mji aliwaona watu wakimnyanyasa mtenda dhambi kwa maneno makali mno. Akawauliza:

"Kama mngelimuona mtu amedondoka kisimani, je msingelijaribu kumsaidia?".

Wale watu wakajibu:

"Ndio tungelimsaidia" Kisha Abu Darda akawaambia:

"Kama ni hivyo basi msimnyanyase ndugu yenu. Na mtukuzeni Mwenyezi Mungu kwa kuwapa uzima".

Wale watu wakamuuliza:

"Je wewe hujamkasirikia huyu mkosefu?"

Swahaba huyu mwema ambaye alilelewa chini ya usimamizi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawajibu:

"Mimi sijamkasirikia yeye, bali matendo yake. Pindi atakapoachana na makosa yake bado ataendelea kuwa ndugu yangu" (Abdulrazzak, XI, 180; Abu Nuaym, Hilya I, 225).

❁

Wakati wa kipindi cha Mtume ﷺ kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Abdullah. Mtu huyu ambaye alijulikana kama 'Khimar' alikuwa akimfanya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ acheke kutokana na vichekesho vyake. Hata hivyo wakati mwingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akimuadhibu kwa sababu ya kunywa kwake pombe...

Siku moja baada ya kipindi kingine cha kumuadhibu na baada ya yeye Abdullah kuondoka, wale waliokuwepo pale wakaomba dua dhidi yake kwa kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu mlaani mtu huyu". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawageukia na kuwaambia:

*"Msiseme maneno hayo. Msimsaidie Shetani dhidi ya ndugu yenu. Naapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa nafahamu kuwa mtu huyu anampenda Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Badala ya kumlaani hamna budi kumuombea: "Ewe Mwenyezi Mungu, Msamehe madhambi yake. Ewe Mwenyezi Mungu mhurumie mtu huyu"* (Bukhari, Hudud, 4, 5; Abu Dawud, Hudud 35).

Tukio hili ni ushahidi tosha juu ya upole na uvumilivu vilivyotokana na wema, huruma na upendo aliokuwa nao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa watu wake.

❁

Kipindi fulani wakati Rabi ibn Haysam alipokuwa anaswali farasi wake mwenye thamani ya dirham elfu 20 aliibiwa mbele ya macho yake. Lakini badala ya kumfuata mwizi aliamua kumalizia swala yake huku akiwa na amani moyoni mwake.

Baada ya marafiki zake kusikia juu ya hasara ile kubwa walienda kumpa pole. Rabi ibn Haysam aliwaambia:

"Nilimuona mwizi akimfungua farasi wangu. Hata hivyo wakati ule nilishughulishwa na jambo muhimu zaidi na ninalolipenda. Ndio maana sikumkimbiza mwizi yule".

Baada ya kuyasikia haya wale marafiki zake wakaanza kumlaani mwizi yule. Rabi ibn Haysam akawaambia:

"Tulieni kwani hajanidhuru mimi. Ameidhuru nafsi yake mwenyewe. Nadhani inatosha kwa masikini yule kujidhuru yeye mwenyewe, sisi tusimdhuru" (Angalia Babanzade Ahmad Naim, Islam Ahlakinin Esaslari," uk 85-6).

Uzuri ulioje wa kilele cha upole na huruma...Hii ni hali ya kipekee ya marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao waliangalia uumbaji kwa kupitia Muumba wao...

❁

Siku moja Imam Sha'bi', ambaye alikuwa mmoja wa Tabi'ina wakubwa alimwambia maneno yafuatayo mtu mmoja muovu ambaye alikuwa amemtukana:

"Kama unachokisema ni cha kweli, basi Mwenyezi Mungu anisamehe! Ikiwa wewe ni muongo, basi Mwenyezi Mungu akusamehe!"

Uzuri ulioje wa mfano huu wa wema mkubwa...

❁

Kwa ufupi ni kwamba upole na uvumilivu ambavyo ni matokeo ya tabia nzuri kama vile wema, huruma na upendo, ndio kiini cha mahusiano ya kijamii. Mambo haya ni maamrisho matukufu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na ndivyo zilivyokuwa tabia za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alisema:

*"Yeyote ambaye amejaaliwa rifk (upole na wema) amepewa neema kubwa sana. Lakini yeyote ambaye hana rift amenyimwa neema kubwa"* (Tirmidhi, Birr, 67/2013).

**11. Kuwa na dhana njema katika kila kitu**

Kuwa na husn-i zann (dhana njema) ni kufikiria chanya, kutumaini mazuri, kujiweka mbali na fikra hasi na dhana mbaya au fikra mbaya. Waislamu watakapofanikiwa kufungamana na dhana njema kwa watu wengine watalindwa dhidi ya kuangukia kwenye makosa.

Aya ifuatayo kutoka kwenye Qur'an tukufu inafunga milango yote inayompelekea mtu kuwadhania wengine vibaya:

**"Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu"** (Hujurat, 49:12).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Jichungeni na dhana. Kwani dhana au tuhuma zisizo na ushahidi ni maneno mabaya mno. Msichunguze wanachokisema wengine, msitafute makosa ya watu wengine na msijikweze na*

*kujisifu miongoni mwenu. Msioneane wivu kati yenu, msichoko-zane miongoni mwenu na msipeane migongo nyinyi kwa nyinyi. Enyi waja wa Mwenyezi Mungu! Kuweni kama ndugu kama vile Mwenyezi Mungu alivyowaamrisha..."* (Muslim, Birr, 28-34).

Hadith nyingine ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kama ifuatavyo:

*"Na asitokee yeyote katika maswahaba wangu kuja kuniambia kasoro za mwingine. Ninataka kuwa na moyo safi mbele yenu"* (Abu Dawud, Adab, 28/4860).

Kuwa na dhana njema kwa wengine ni jambo rahisi ambalo haligharimu chochote. Kinyume chake kunamuepushia mtu majukumu na kuchoka. Khalifa wa nne, Ali رضي الله عنه amesema:

"Kuweni na dhana njema juu ya waja wa Mwenyezi Mungu. Mkifanya hivyo mtakuwa mmejipunguzia mzigo mkubwa".

Ili kuwa na dhana njema juu ya wale waliotangulia mbele ya Mwenyezi Mungu, waislamu hawana budi kuamini kuwa watasamehewa. Kufikiria kinyume chake hakuna faida kwa yeyote.

Kila mtu hana budi kuendelea kuwadhania wengine wema na kuwa na uvumilivu juu ya hilo. Ikiwa ukweli wa mambo haujulikani ni jukumu la waislamu kudhaniana mazuri na kuwa na fikra chanya kati yao. Kwani tutakuja kuhukumiwa kutokana na dhana zetu hasi. Kinyume chake ni kuwa hata kama tutakuwa tumekosea kwa kumdhania mtu mazuri, hatutohukumiwa kwa hilo. Hasara yetu itakuwa ni kukosea kulikotokana na dhana yetu njema. Lakini kama tutamdhania mtu kwa ubaya au tutamshuku mtu yeyote tutalazimika kuwajibika kutokana na matendo yetu haya.

***Matukio ya wema***

Kutokana na masimulizi ya Abdullah ibn Amr ﵁, wakati wa kutekeleza moja ya mizunguko ya Al-Kaaba, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliizungumzia Al-Kaaba kama ifuatavyo:

"*Usafi ulioje uliokuwa nao na uzuri ulioje wa harufu yako! Utukufu ulioje uliokuwa nao na ukubwa ulioje wa heshima iliyo juu yako. Ninaapa kwa mwingi wa Rehema ambaye ameishikilia roho yangu mikononi mwake kuwa thamani ya muumini mbele ya Mwenyezi Mungu ni kubwa kuliko thamani yako wewe. Thamani ya mali na damu ya muumini iko sawa. Hatuna chochote bali dhana njema kwa waumini*" (Ibn Majah, Fitan, 2).

Hivyo kwa waumini kujipamba na dhana njema juu ya wengine ni kanuni muhimu katika Uislamu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipata shida sana kutokana na tukio la *Ifk*[53] ambalo lilisababishwa na fitina na utesi wa wanafiki. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaendea mke wake aitwae Zaynab bint Jahsh ﵂ na mjakazi wa Aisha ﵂ aitwae Barira ﵂ na kuwaomba maoni yao kuhusu Aisha ﵂[54]. Wote walishuhudia wema wake. Aisha ﵂ ana yafuatayo ya kusema kuhusiana na suala hili:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa analichunguza suala hili alimuuliza Zaynab bint Jahsh ﵂ juu ya maoni yake kwangu:

*"Ewe Zaynab, je unajua nini kuhusiana na suala hili, na ni nini ulichokiona?"*

Akajibu:

53. Tukio hili linahusisha kashfa ambayo washirikina walimzushia Aisha ﵂ ambaye ni mke wa Mtume.
54. Bukhari, Shahadah 16

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninajilinda kutokana na kile ambacho masikio yangu hayajakisia na macho yangu hayajakiona. Sijui chochote kuhusu Aisha zaidi ya wema".

Miongoni mwa wake za Mjumbe a Mwenyezi Mungu ﷺ, Zaynab alikuwa ni mtu ambaye kutokana na baadhi ya matendo yake mema alionekana kuwa mpinzani wangu. (Kama angelikuwa amepata nafasi angelinisemea kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ili aonekane yeye ni bora zaidi kwake). Hata hivyo kutokana na uchamungu wake na imani yake ya dini Mwenyezi Mungu alimuepushia kuwa miongoni mwa watu walionizushia" (Bukhari, Shahadah, 15, 30; Muslim, Tawba, 56).

Uzuri ulioje wa mfano wa husn-i dhann...Wakati watu wengi wangeliweza kuangukia kwenye makosa, lakini Zaynab alijikinga chini ya mwamvuli wa husn-i zann na aliepushiwa adhabu kali iliyowapata wale waliomzushia Aisha ؓ. Baadae aya zikashuka kwa ajili ya kumsafisha Aisha kutokana na uzushi ule. Pia zilishushwa aya zilizobeba onyo kali kwa wazushi na wale waliojitenga na dhana njema. Ikafahamika kuwa kama Mwenyezi Mungu angelikuwa hasamehi, basi wote wangeliadhibiwa katika njia mbaya kabisa. Kurudiwa mara nyingi maonyo na vitisho hivi inatosha kutuonyesha namna ulivyo ubaya wa dhana na tuhuma za uongo. Aya hizo zinasema yafuatayo:

**"Kwa nini mlipo sikia khabari hii, wanaume Waumini na wanawake Waumini hawakuwadhania wenzao mema, na kusema: Huu ni uzushi dhaahiri?"** (Al-Nur, 24:12).

**"Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema yake katika dunia na Akhera, bila ya shaka ingeli kupateni adhabu kubwa kwa sababu ya yale mliyo jiingiza"** (Al-Nur, 24:14).

❁

Pia wakati wa kipindi cha tukio la Ifk , Ummu Ayyub ambaye alikuwa mke wa Abu Ayyub al-Ansari alimuuliza mumewe:

"Je umesikia watu wanayoyasema kuhusu Aisha?" Abu Ayyub akajibu:

"Ndio nimesikia. Lakini yote ni uongo na mambo ya kutengeneza".

Kisha akamuuliza mke wake:

"Je wewe ungeliweza kufanya kitendo kibaya kama hicho?" Akajibu:

"Hapana! Naapa kwa Mwenyezi Mungu kamwe nisingeliweza kufanya hivyo".

Kisha Abu Ayyub ﵁ akamwambia:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Aisha ni bora zaidi yako" (Ibn Hisham, III, 347; Waqidi, II, 434).

Uzuri ulioje wa mfano juu ya dhana njema katika kizazi kile cha kuigwa...

❁

Ibn Mas'ud ﵁ anasimulia yafuatayo:

"Ukimuona ndugu yako anatenda dhambi usimsaidie Shetani kwa kusema maneno kama: "Ewe Mola! Mharibu mtu huyu. Ewe Mwenyezi Mungu! Mlaani mtu huyu".

Badala yake sema: "Ewe Mola! Msamehe mtu huyu na umuongoze katika njia iliyonyooka". Kama maswahaba wa Mtume Muhammad ﷺ kamwe hatukusema chochote kumuhusu mtu yeyote aliyekufa ambaye hatukujua alikufa katika hali gani. Kama alikufa vizuri, tulikuwa tukisema: "Amekutana na kheri". Kama

alikufa vibaya tulikuwa tunahofia kusema chochote juu yake" (Abu Nuaym, Hilya, IV, 205).

❁

Mtu aliyekuwa amemtembelea Abu Dujana ﵁ ambaye alikuwa mgonjwa kitandani aliona uso wake uking'aa kwa nuru, akamuuliza:

"Kwa nini uso wako unang'aa kiasi hicho?". Akajibu:

"Nina matendo mawili:

"La kwanza ni kwamba ninakaa kimya juu ya mambo yasiyonihusu na la pili ni kwamba moyo wangu uko mbali na kuwadhania vibaya waumini wenzangu. Huwa nina dhana njema kuhusu kila muumini" (Ibn Sa'd, III, 557).

❁

Jalaluddin al-Rumi anaelezea kwa sitiari kuhusu tabia mbaya na zenye kuangamiza ambazo zinajificha ndani ya mwanadamu kama vile dhana, wivu na husda kama ifuatavyo:

Wakati fulani Sultani aliwanunua watumwa wawili. Ili kutambua uwezo wao na nyoyo zao alianza kuzungumza na mtumwa wa kwanza. Yule mtumwa alimpa Sultani majibu ambayo kwa watu wengine wangelitafakari kwa muda na kwa ugumu juu ya majibu yale. Sultani alifurahishwa mno na uelewa, akili na maneno matamu ya mtumwa huyu. Kisha akamuita yule mtumwa mwingine.

Yule mtumwa mwingine akaenda mbele ya Sultani. Mdomo wa mtumwa yule ukawa unatoa harufu mbaya na meno yake yalikuwa meusi kutokana na kupuuzia kwake. Ingawa Sultani hakupendezwa sana na muonekano wa nje wa mtumwa yule alianza kuzungumza naye ili kujua tabia yake na undani wake:

“Kutokana na muonekano wako na harufu ya kinywa chako kaa mbali kidogo, lakini sio mbali sana. Ngoja kwanza tutafute tiba ya mdomo wake; wewe ni rafiki na mimi ni mganga mwenye ufahamu mkubwa. Haikubaliki kwetu kukudharau au kukufedhehesha. Kaa chini na utuhadithie baadhi ya visa ili tuweze kufahamu uwezo wako wa kufikiria”.

Kisha Sultani akamgeukia yule mtumwa wa kwanza na kumwambia:

“Sasa nyanyuka na uende hamam ukajisafishe vizuri”.

Baada ya rafiki yake kuondoka, akamgeukia yule mtumwa wa pili ambaye alikuwa akiongea naye na kumwambia maneno yafuatayo kwa lengo la kumjaribu:

“Huyu rafiki yako niliyetoka kuongea naye muda si mrefu ameniambia mambo mengi kuhusu wewe. Lakini mimi nakuona hauko kama alivyosema yeye. Mtu huyu mwenye husda alijaribu kunifanya nikuchukie wewe. Rafiki yako huyu amesema yafuatayo kukuhusu wewe: “Yeye ni mwizi. Yeye si muaminifu. Anakaa pamoja na wahalifu na pia hana utu”. Je wewe una lipi la kusema kumhusu yeye?”

Yule mtumwa wa pili akamjibu Sultani kama ifuatavyo:

“Siwezi kusema kuwa amedanganya mtu huyu mwenye uelewa mkubwa na msema ukweli. Kinyume chake kutokana na maneno yake nitajaribu kubadilika kwa kuona kuwa ninaweza kuwa na kasoro hizo. Sultani wangu! Labda ameona kasoro nyingi juu yangu bila ya mimi mwenyewe kuzitambua”.

Sultani akamwambia yule mtumwa:

“Kama alivyoniambia kasoro zako, na wewe sasa niambie kasoro zake”. Yule mtumwa akajibu:

"Sultani wangu! Ukweli ni kwamba yeye ni rafiki yangu mwema. Moyo wangu unanizuia kutofunua kasoro zake. Ndio maana ninachoweza kukuambia ni hiki: Kwa muono wangu kasoro zake si kasoro bali ni wema. Yeye ni mfano wa kuigwa katika upendo, uaminifu na utu. Yeye ni mtu mwenye msimamo, akili na urafiki wa kweli. Yeye ni mkarimu na anawasaidia wahitaji. Yeye ni mkarimu mno kiasi cha kuweza kutoa uhai wake kama ikimlazimu kufanya hivyo. Tabia nyingine ya rafiki yangu ni kwamba yeye si mtu mwenye majivuno. Yeye anampenda kila mtu nani adui wa nafsi yake mwenyewe"

Kisha Sultani akamwambia yule mtumwa:

"Usimsifu rafiki yako kupita kiasi na usijaribu kujisifu mwenyewe kwa kupitia kwake. Kwani na yeye nitamjaribu na wewe utakuja kujutia maneno yako".

Kisha mtumwa yule akasema:

"Kwa hakika hapana, sikumsifu kupita kiasi. Sifa za rafiki yangu yule ni nyingi zaidi ya nilizozitaja. Hizi nilizokuambia ndio tabia za rafiki yangu. Hata hivyo sina la kufanya kama hutaniamini. Moyo wangu unanilazimu kuyasema hayo".

Pindi yule mtumwa wa kwanza aliporejea kutoka hamam Sultani alimuita na kumwambia:

"Mwenyezi Mungu akupe afya na neema zisizo na kikomo. Hata hivyo ubora ulioje kama hutakuwa na sifa mbaya ambazo rafiki yako ameniambia. Kisha wale walioiona sura yako nzuri watafurahia sana. Kisha itakuwa sawa kwa hazina yote ya ulimwengu kukuangalia wewe".

Yule mtumwa akamwambia:

"Sultani wangu! Tafadhali niambie ni kipi alichokisema mtu huyu asiye na busara?"

Sultani akajibu:

"Kwanza kabisa ameniambia kuhusu unafiki wako. Ameniambia ijapokuwa unaonekana kama tiba lakini ukweli ni kwamba wewe mwenyewe ni laana".

Baada ya kuyasikia maneno haya kutoka kwa Sultani alipandwa na hasira sana kiasi kwamba akaanza kutoa mapovu mdomoni mwake, na uso wake ukageuka na kuwa mwekundu kutokana na hasira. Yule mtumwa akaanza kumsema vibaya rafiki yake bila hata mipaka. Alisema:

"Mwanzoni alikuwa rafiki yangu, lakini nikakuta ananuka mdomo sana. Alikuwa kama mbwa katika nyakati za njaa. Mara nyingi alikuwa akila taka taka".

Yule mtumwa wa kwanza alianza kuongea kama filimbi katika kumsema vibaya rafiki yake. Alianza kutoa ubaya uliokuwa umejificha ndani yake. Kisha Sultani akamwambia yule mtumwa: "Inatosha". Kisha akauweka mkono wake kwenye mdomo wa Yule mtumwa na kusema:

"Sasa nimeona tofauti kati yenu. Mdomo wake ulikuwa ukinuka kutokana na ugonjwa kwenye mwili wake. Lakini nafsi yako wewe inatoa harufu mbaya. Ewe nafsi inayonuka, sogea. Rafiki yako atakuwa kiongozi wako na wewe utafuata atakachokuamrisha. Utajifunza kutoka kwake tabia njema, utu na namna ya kuongea. Jifunze kutokana na wema wake. Jiweke mbali na dhana na husda. Wewe ni mtu mwenye kusikitisha sana, uko kama mtu ambaye amejifunga jabali kwenye tumbo lake; huwezi kuogelea wala kutembea nalo".

Yule mtumwa wa pili ambaye alitoa maneno mazuri kuhusu rafiki yake alipata neema za kiroho na kimwili kutokana na kuwa kwake katika kilele cha wema. Kwa upande mwingine yule mtumwa wa kwanza ambaye alitoa maneno mabaya na kutekwa

na hasira zake bila ya kujua ukweli wa mambo alidharaulika na kufedheheka na kukutana na hasara kubwa.

❁

Hivyo cha muhimu ni kwamba kuwa na dhana jema juu ya watu ni matunda ya kuwaangalia viumbe kwa kupitia Mwenyezi Mungu. Kuwatakia watu heri na kuangalia upande wao wa wema ni sifa muhimu sana ambayo itampelekea mtu kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kupendwa na watu.

**12. Ukarimu na kujiepusha na ubinafsi**

Ukarimu ni kumpa mtu kitu ambacho wewe unacho lakini mwenzako hana. Kilele cha ukarimu ni *isar* au kutokuwa na ubinafsi au kujitolea. Maana nzuri ya *isar* inaweza kupatikana katika aya ifuatayo iliyopo ndani ya Qur'an:

**"Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu. Basi Mwenyezi Mungu atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha"** (Al-Insan, 76:8-11).

Ukarimu ni zao la huruma inayotokana na imani. Na huruma ni kukimbilia kuwasaidia wengine ili kukidhi haja zao.

Hata hivyo ukarimu sio kutumia mali bila mpangilio. Mwenyezi Mungu anawaneemesha waja wake kwa umakini na kwa kujua umuhimu wake. Katika suala hili Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuambia yafuatayo:

**"Wala usiufanye mkono wako kama ulio fungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi"** (Al-Isra 17:29).

Ukarimu ni moja ya sifa za Mwenyezi Mungu. Moja ya jina lake ni 'Al-Kareem', lenye kumaanisha 'Anayetoa bila mipaka na mwingi wa kutoa'[55]. Majina mengine ya Mwenyezi Mungu kama vile Rahman, Rahim, Wahhab, Latwif, Tawwab, Gaffar, Afuww, Rauf na Hadi pia yanaonyesha ukarimu wa Mwenyezi Mungu katika maeneo mbalimbali.

Tunaelezwa yafuatayo katika hadith:

*"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ni Al-Jawwad, yani Yeye ni mwingi wa ukarimu na neema na ndio maana anapenda ukarimu. Anapenda tabia njema na anachukia tabia mbaya"* (Suyuti, I, 60).

*"Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Twayyib, yani Anapenda uzuri na vizuri. Yeye ni Twahir, Anapenda usafi. Yeye ni Karim, Anapenda uadilifu. Yeye ni Jawwad, Anapenda ukarimu"* (Tirmidhi, Adab, 41/2799).

Ili kuwa na fungu katika ukarimu wa Mwenyezi Mungu, muumini hana budi kuwa kama mwezi katika usiku wa kiza, yani awe mpole, afikirie wengine, mwenye huruma, mwema, moyo wa kutoa, na awe na moyo safi. Mwenyezi Mungu anasema yafuatayo katika aya ndani ya Qur'an:

**"Enyi mlio amini! Toeni katika tulivyo kupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhaalimu"** (Al-Baqara, 2:254).

**"...Na chochote mtakacho kitoa Yeye atakilipa. Naye ni Mbora wa wanao ruzuku"** (Al-Saba, 34:39)

Ali ﷺ ana yafuatayo ya kusema:

"Watu wamelala na pindi wanapokufa huamka..." (Ajluni, Kashfu al-Hafa, II, 312/2795). Kama hatutaki kuamka tukiwa mikono

55. Angalia Initar verse 6

mitupu katika maisha ya milele na ikiwa hatutaki kukosa malipo, hatuna budi kuandaa kipato chetu kwa ajili ya maisha ya kesho akhera kwa kujipamba na tabia ya ukarimu na kujiepusha na ubinafsi ndani ya dunia hii. Rumi amelielezea jambo hili vizuri mno:

"Maisha ya dunia hii si chochote bali ndoto. Kupata manufaa katika dunia hii ni sawa na kutafuta hazina ndani ya ndoto yako. Utajiri wa dunia hii unaendelea kurithishwa vizazi baada ya vizazi na kubakia ndani ya dunia hii".

"Malaika wa mauti humuamsha mtu mjinga aliyelala ili aichukue roho yake. Kisha mtu huyo husikitika juu ya jitihada kubwa aliyoifanya katika kumiliki mali ndani ya dunia hii, mali ambayo si kitu cha uhakika cha kumiliki. Hujuta mno, lakini huwa amechelewa na muda huwa umeshakwisha..."

Hivyo ndivyo yanavyokuwa maisha ya hapa duniani, na ndivyo yanavyokuwa maisha ya kesho akhera...

Tunaelezwa katika aya ndani ya Qur'an:

**"Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema? Wala Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapo fika ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda"** (Al-Munafiqun, 63:10-11).

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu wale waja wake walio wakarimu na ambao nyoyo zao zimeamka kama ifuatavyo:

**"...wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa"** (Al-Hashr, 59:9).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye kamwe hakuwahi kukataa ombi la mtu yeyote[56] ameeleza wema wa wale walio na tabia ya ukarimu kama ifuatavyo:

*"Ukarimu ni kama mti ambao matawi yake yananing'inia katika dunia hii kutokea peponi. Yeyote atakayeshikilia tawi moja wapo basi litampeleka peponi. Kwa upande mwingine ubakhili ni kama mti ambao matawi yake yananing'inia kwenye Moto kutokea hapa duniani. Na yeyote atakayeshikilia tawi moja wapo basi litampeleka motoni..."* (Bayhaqi, Shuabu'l Iman, VII, 435).

*"Hali ya mkarimu ukiilinganisha na ya mbakhili ni kama hali za watu wawili waliovaa vazi la chuma kuanzia vifuani mwao mpaka kwenye mitulinga yao. Kadiri mtu mkarimu anavyotoa basi vazi lake linatanuka na kurefuka kiasi cha kuziba vidole vyake vya miguu na kufuta nyayo zake. Pindi mtu mbakhili anapotaka kutoa kitu basi vazi lake linasinyaa na kumzuia; kadiri anavyojitahidi kulitanua lakini haisaidii kitu"* (Bukhari, Jihad 89, Zakat 28; Muslim, Zakat 76-77).

*"Mtu mkarimu yupo karibu na Mwenyezi Mungu, pepo na watu; na yupo mbali na Moto. Na mtu mbakhili yupo mbali na Mwenyezi Mungu, pepo na watu, na yupo karibu na Moto. Mtu mkarimu ambaye ni mjinga anapendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu zaidi ya mtu bakhili anayefanya ibada wakati wote"* (Tirmidhi, Birr, 40/1961).

*"Wakati wote msamehe mtu mkarimu, kwani Mwenyezi Mungu humshikilia mkono pindi anapoyumba"* (Haythami, VI, 282).

Asma ﵂, ambaye ni binti wa Abu Bakr ﵁ anasimulia kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimwambia:

56. Angalia Bukhari, Adab 39; Muslim, Fadail, 56.

*"Usikaze nyuzi za mfuko wako wa fedha, kwani Mwenyezi Mungu anaweza kukibana kile alichokupa"* (Bukhari, Zakat, 21).

*"Toa na usiendelee kuhesabu, isije ikapelekea Mwenyezi Mungu akahesabu vile alivyokupa na kukuzuia navyo. Usifiche fedha zako kwenye chungu vinginevyo Mwenyezi Mungu atazificha na wewe usizione"* (Muslim, Zakat, 88).

Kuwafikiria wengine zaidi yako mwenyewe, ukarimu, usafi wa moyo na ukweli, vyote ni matokeo ya kukua kiimani. Ukarimu na kuwafikiria wengine ndivyo vitakavyomuweka mtu mbali na dunia na vishawishi vyake ambavyo vinachafua amani na imani ya moyo.

Rumi ameelezea tena vizuri manufaa ya ukarimu na ubaya wa ubakhili kama ifuatavyo:

"Ukarimu ni tawi la mti wa peponi. Huzuni iliyoje kwa yule anayeliachia tawi hili. Yule anayepanda mbegu hana budi kwanza kukisafisha chumba chake cha kupandia hizo mbegu, na baadae mavuno yake yatakuwa makubwa. Lakini yule asiyefanya hivyo atapelekea mbegu zake kuwa chakula cha panya".

"Kama watu warembo wanavyotafuta vioo vya kujitazamia visafi, ndivyo pia mtu mkarimu anavyowatafuta watu masikini na dhaifu. Uzuri wa watu warembo huonekana kwenye kioo kama uzuri wa watu wanaotoa unavyodhihirika mbele ya masikini na walala hoi".

Pia leo hii tunawahitaji watu ambao wanahamasisha kwa kila namna ukarimu na kuwasaidia wengine. Tusisahahu kuwa na sisi tungeliweza kuwa katika nafasi ya watu masikini na wasiojiweza. Ndio maana tuna deni la shukurani kwa Mola wetu, hivyo hatuna budi kuwa wakarimu, kuwasaidia wagonjwa, walalahoi, wapweke, wahitaji na wenye njaa.

Hebu tugawane na wahitaji neema tulizojaaliwa ili zile nyoyo tunazoziridhisha na kuzifurahisha zituzidishie imani zetu ndani ya dunia hii, na zitusaidie na kutupa furaha kesho akhera.

***Matukio ya wema***

Anas ﵁ anasimulia:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akitoa kila alichokuwa akiombwa kwa ajili ya Uislamu. Siku moja alimpa mtu mmoja aliyemjia kundi kubwa la kondoo. Yule mtu aliporejea kwenye kabila lake aliwaambia:

"Enyi watu. Kimbilieni kuingia kwenye Uislamu. Kwani Muhammad anatoa mali nyingi bila ya kuhofia umasikini wala uhitaji".

Ukweli ni kwamba baadhi ya watu waliingia kwenye Uislamu kwa ajili ya kupata manufaa ya kidunia. Hata hivyo haikuchukua muda mrefu kabla ya Uislamu haujawa wenye thamani kwao zaidi ya dunia na kila kitu kilichopo ndani yake. (Muslim, Fadail, 57-58)

❁

Ingawa Safwan ibn Umayya, mmoja wa viongozi wa wapagani wa kiquraish, alikuwa bado hajaingia kwenye Uislamu lakini alipambana bega kwa bega pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika vita vya Hunayn na Twaif.

Walipokuwa wanapita karibu na ngawira zilizokuwa zimekusanywa pale Jirana, Safwan aliiangalia sehemu ya ngawira zile kwa matamanio. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomuona alimuuliza:

*"Je ngawira hizo zinakupendeza?"*

"Ndio" Safwan alijibu.

“Zichukue, zote ni zako”

Safwan alijisikia vibaya na kusema:

“Hakuna moyo unaoweza kuwa na ukarimu kama moyo wa Mtume”. Kisha akatoa shahada na kuwa Muislamu. (Waqidi, II, 854-55).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa katika kilele cha wema. Alikuwa akitoa mara nyingi na kuwapa watu kwa lengo la kurekebisha udhaifu wao na alikuwa akifanya juhudi ya kuwaongoza.

❁

Abdullah ibn Abbas ﷻ anasimulia:

“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndiye aliyekuwa mkarimu kupita wote. Ukarimu wake ulikuwa ukiongezeka katika kipindi cha Ramadhani, wakati alipokuwa anakutana na Jibril. Jibril alikuwa akikutana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika kila usiku ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani na walikuwa wakisomeana Qur’an. Ndio maana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mkarimu mno kuliko upepo unaovuma bila ya kizuizi” (Bukhari, Bad’u al-Wahy 5, 6, Sawm 7; Muslim, Fadail 48, 50).

❁

Wakati fulani mtu mmoja alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nina njaa”.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatuma ujumbe kwa mmoja wa wake zake atume kitu kwa ajili ya kula. Hata hivyo huyu mama wa waumini alisema:

“Naapa kwa yule aliyekutuma kuwa Mtume kuwa nyumbani hatuna chochote isipokuwa maji”.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipogundua kuwa hali ilikuwa ni ile ile hata kwa wake zake wengine aliwageukia maswahaba na kuwaomba:

“Je kuna yeyote kati yenu anaweza kumkubalia mtu huyu awe mgeni wake usiku wa leo?”

Mtu mmoja kutoka Answar akasema:

“Mimi nitamchukua ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu” Kisha akamchukua yule mtu muhitaji na kumpeleka nyumbani kwake. Alipofika alimwambia mke wake:

“Je tuna chochote kwa ajili ya kula?” Mke wake akamjibu:

“Hapana, kuna chakula cha kuwatosha watoto wetu tu”.

Kisha yule swahaba akasema:

“Kama ni hivyo washughulishe watoto kwa kitu chochote. Na kama wataulizia kitu cha kula walaze kitandani. Pindi mgeni wetu atakapoingia ndani utazima taa na tutajifanya kama tunakula pamoja naye”.

Kisha wakakaa chini kwa ajili ya kula. Yule mgeni akala na kushiba na wao wakaenda kulala na njaa.

Asubuhi yake swahaba huyu akaenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kumuona alimwambia:

*“Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amependezwa na jambo ulilomfanyia mgeni wako jana usiku”* (Bukhari, Manaqibu’l Ansar, 10; Tafsir, 59/6; Muslim, Ashribah, 172).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichinja kondoo. Baada ya kumgawanya kwa watu wengi kisha Mjumbe wa Mwe-

nyezi Mungu ﷺ akamuuliza Aisha ni kipi kilichokuwa kimebakia. Pindi Aisha alipomjibu:

"Umebakia mtulinga pekee", Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Unamaanisha tuna malipo ya kila kitu isipokuwa mtulinga".* (Tirmidhi, Qiyamah, 33).

Inamaanisha kuwa mali yetu halisi ni ile tuliyoitoa...

❁

Siku moja masikini mmoja alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuomba kitu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema:

*"Sina chochote cha kukupa lakini nenda kanunue chochote unachohitaji kwa jina langu na mimi nitakilipia nitakapopata".*

Omar ؓ ambaye hakukubali Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aingie katika madeni alisema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kama ungelikuwa na kitu ungelitoa lakini Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yako kwa lile lililo nje ya uwezo wako".

Uso wake uliobarikiwa ulionyesha namna alivyokuwa hakuridhishwa na maneno haya ya Omar. Kutokana na haya mtu mmoja wa kianswar alisema:

"Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Achana na hayo! Usihofie kuwa Mwenyezi Mungu atakupunguzia malipo yake".

Maneno haya ya swahaba huyu yalimfurahisha sana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumfanya atabasamu na kusema:

*"Haya ndiyo niliyoamrishwa kuyafanya"* (Haythami, X, 242).

Uzuri ulioje wa mfano huu wa moyo msafi...muumini kumliwaza Muislamu mwenzake ni sababu ya amani kubwa ndani ya moyo wake.

❁

Mmoja wa viongozi wa Tabi'een, Abdullah al-Harawi alikuwa akifahamu hali ya ukarimu aliokuwa nao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Hata hivyo alitaka kufahamu zaidi. Siku moja alipokuwa Aleppo alikutana na Bilal Habeshi ؓ, msomaji adhana wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Baada ya kuipata fursa hii alimuuliza Bilal kuhusiana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ:

"Ewe Bilal! Nielezee namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alivyokuwa akitoa".

Bilal ؓ akaelezea kama ifuatavyo:

"Tokea siku ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipotumwa na Mwenyezi Mungu kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mpaka siku alipokufa nilikuwa nikiangalia mambo yake mbalimbali. Kwa mfano pale Muislamu alipomjia na kumuona kuwa ni masikini, alikuwa akiniagiza niende kukopa na kumnunulia yule mtu chakula na mavazi. Siku moja mpagani mmoja alikuja kwangu na kuniambia: "Ewe Bilal. Mimi ni mtu tajiri na mwenye fursa nyingi. Kuanzia sasa usiende kwa yeyote mwingine kuomba mkopo bali njoo kwangu". Niliamua kufanya vile. Siku moja nilikuwa nimeshachukua udhu na niko tayari kusoma adhana, mara nikamuona yule mpagani akiwa pamoja na kundi la wafanyabiashara. Aliponiona aliniita:

"We Bilal"

"Kuna nini?" nikajibu. Yule mtu akanikunjia sura na kuniangalia vibaya na kuanza kutoa maneno makali:

"Ni muda gani sasa tokea mwanzo wa mwezi?" aliuliza.

Nikajibu:

“Si muda mrefu”.

Kisha akasema:

“Yamebakia masiku manne tu. Siku hiyo ikifika nitataka unipatie ninachokudai. Sikukupa fedha zile kwa ajili yako wala kwa ajili ya yule mtu, bali nilikupa wewe ili uje kuwa mtumwa wangu. Utapeleka kondoo wangu kuwachunga kama ulivyokuwa ukifanya mwanzoni”.

Nilipoyasikia maneno yale nilikasirika sana. Nikaenda kusoma adhana. Baada ya kumaliza kuswali swala ya isha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alirejea kwenye familia yake. Nikamuomba ruhusa ya kuongea naye akanikubalia na kuniruhusu kuingia kwake. Kisha nikamwambia:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Mama yangu na baba yangu watolewe kwa ajili yako. Unamkumbuka yule mpagani niliyeenda kuomba mkopo kutoka kwake? Amesema hili na hili. Si wewe wala mimi nina namna ya kumlipa mtu huyu. Atakuja kunidhalilisha mimi. Naomba uniruhusu nikatafute hifadhi kwenye kabila moja wapo ya yale yaliyoingia kwenye Uislamu hivi karibuni. Niruhusu nikakae nao mpaka hapo Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atakapokujaalia mali mali ya kuweza kulipa deni langu”.

Baada ya kupata ruhusa kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu niliondoka mpaka nyumbani kwetu. Kisha nikaweka upanga wangu, singe yangu, mkuki wangu na viatu chini ya kichwa changu, nikageuzia uso wangu angani na kulala. Nilikuwa na mfadhaiko kiasi kwamba sikuweza kupata usingizi kwa haraka. Nilipokaribia kupata usingizi tu mara nikasikia mtu akiniita nje:

“Ewe Bilal. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anakuita”.

Nikasogea kwenye mlango wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na sikuona kingine bali ngamia wanne waliobebeshwa mizigo. Niliomba ruhusa ya kuingia na kisha nikaingia ndani. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniambia:

*"Habari njema ewe Bilal. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amenitumia mali hii ili nilipe deni lako"*. Nikamsifu Mwenyezi Mungu, kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniambia:

*"Je hukuona ngamia wanne mbele ya mlango?"*

"Nimewaona" nikajibu.

*"Wote ni wako pamoja na walichokibeba. Wametumwa na kiongozi wa Fedek. Wachukue na uende ukalipe deni lako"*.

Nilitekeleza kile alichoniambia Mtume. Niliwatua mizigo yao na kuwapa chakula na kisha nikaenda kusoma adhana ya alfajiri. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kumaliza kuongoza swala nilienda kwenye makaburi ya Baqi, nikanyanyua mikono yangu mpaka masikioni mwangu na kusema kwa sauti:

"Yeyote anayemdai chochote Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aje sasa hivi nimlipe".

Kwa kuuza ile mizigo iliyokuja na ngamia wale niliweza kupata fedha ambayo nililipa madeni yote ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kiasi kwamba hakubakia yeyote katika uso wa dunia ambaye alikuwa akimdai Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Pia nilibakiwa na kiasi fulani cha fedha. Ilipofika jioni nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekaa msikiti peke yake. Nilimtolea salamu kisha akaniuliza:

*"Nini kimetokea? Umefanya nini?"*

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amelipa madeni yote ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na sasa huna deni lolote" nilijibu.

"Je kuna chochote kilichobakia?" aliniuliza.

"Ndio, dinar mbili" nilijibu.

"Kama ni hivyo niokoe kutokana na hizo dinar mbili kwa kuzitoa. Sitarejea kwenye familia yangu mpaka uniondoshee mzigo wa hizo dinar mbili na kuniacha huru".

Kwa kuwa hakukuwa na mtu yeyote aliyekuja ili nimpe zile dinar, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisubiria pale msikiti kwa muda mrefu. Mara ilipokaribia usiku watu wawili waliokuwa kwenye farasi walikuja. Niliwachukua na kuwapeleka sokoni na kuwanunulia chakula na mavazi kwa kutumia dinar zile mbili. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kumaliza kuongoza swala ya isha aliniita na kuniuliza:

*"Umekifanyia nini kile ulichokuwa umebakia nacho?"*.

"Mwenyezi Mungu amekuweka huru" nikajibu.

Baada ya kusikia jibu langu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akatoa takbir "Mwenyezi Mungu ni mkubwa".

Alimsifu Mwenyezi Mungu kutokana na kuwekwa huru na hofu ya kufa akiwa na amana ya zile dinar mbili. Kisha alinyanyuka na kuondoka na mimi nikamfuata nyuma. Alimtembelea kila mtu wa familia yake na kumsalimia. Baada ya hapo akarudi nyumbani kwake.

Na hivi ndivyo ilivyokuwa ewe Abdullah. Hili ndilo jibu la swali lako" (Abu Dawud, Haraj, 33-35/3055; Ibn Hibban, Sahih, XIV, 262-264).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mkarimu mno kiasi kwamba alikuwa akikopa kwa ajili ya kuwasaidia wengine. Ni kiasi gani na sisi kama umma wake tumemuiga kwa ukarimu wake?

Mshairi ameelezea kilele cha ukarimu na kujiepusha na ubinafsi kama ifuatavyo:

"Kama angelikuwa hana kingine mkononi mwake isipokuwa uhai na nafsi yake angelivitoa kwa yeyote ambaye angelimuomba. Ndio maana yeyote ambaye angelimuomba angelitakiwa kumuogopa Mwenyezi Mungu na kuwa mkweli katika ombi lake".

Mshairi mwingine amesema:

"Kama siku moja mtu anaufananisha ukarimu wako na mawingu atakuwa amekosea katika kukusifu kwake. Kwani mawingu yanatoa huku yanalia wakati wewe unatoa huku unatabasamu".

Hivyo hiki ndicho kiwango cha ukarimu aliokuwa nao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Alikuwa akitoa kila alichokuwa nacho kwa hiari yake mwenyewe katika njia ya Mwenyezi Mungu. Khalid-i Baghdadi ametoa ulingano kuhusu kilele cha ukarimu wa Mtume:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mfano mzuri wa kuigwa katika ukarimu kiasi kwamba bahari zinatoa lulu kwa ajili ya uwepo wake, rubi zinatoka kwenye mwamba mgumu na mawaridi yanachanua kutoka kwenye miba. Kama tabia yake nzuri ingelitajwa kwenye bustani basi kusingelibakia hata chipukizi la waridi ambalo lisingelitabasamu, yani lisingelifunguka na kuchanua"[57].

❁

Kujitolea kwa Aisha ﵂, mke wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kulikuwa kwa kipekee. Wakati Omar ﵁ anakaribia kukata roho baada ya kuchomwa alimuita mwanae Abdullah na kumwambia:

"...Nenda kwa Aisha, mama wa waumini na umwambia kuwa Omar anamtakia amani. Usithubutu kusema 'kamanda wa waumini' anakutakia amani. Kwani leo hii mimi si kamanda wa waumini

57. Khalid-i Baghdadi, Divan, trans Sadreddin Yuksel, Istanbul 1977, uk 65-66.

tena. Kisha mwambie: “Omar ibn Khatab anakuomba ruhusa ya kuzikwa pembezoni mwa marafiki zake wawili”.

Abdullah ﵁ anaendelea:

“Niliomba ruhusa ya kuingia nyumbani kwa Aisha ﵂ na kisha nikamtolea salamu. Alikuwa analia, nikamwambia:

“Omar anakutakia amani na anakuomba aruhusiwe kuzikwa pembezoni mwa marafiki zake wawili”.

Aisha akajibu:

“Nilikuwa nimebakisha sehemu pembezoni mwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa ajili yangu mwenyewe. Hata hivyo leo ninamuachia Omar badala yangu”. (Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na Abu Bakr wote walizikwa kwenye chumba cha Aisha. Aisha alitaka azikwe kwenye sehemu iliyobaki karibu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na baba yake).

Niliporejea Omar aliambiwa:

“Abdullah huyu hapa, amesharudi”. Omar ﵁ alijaribu kunyanyuka kwa furaha na shauku:

“Ninyanyue” alisema. Alimshikilia mtu mwingine kama kizuizi na kuniuliza:

“Umekuja na habari gani?”

“Ombi lako limekubaliwa. Aisha amekupa ruhusa”.

Baada ya kuyasema haya naye alisema:

“Alhamdulillah (Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu). Hakukuwa na jambo lingine muhimu kwangu zaidi ya hili. Pindi roho yangu itakapochukuliwa nipelekeni pale. Mtakapofika mpeni tena salamu zangu na kisha mwambieni “Omar anaomba ruhusa”.

Kama atawaruhusu basi ingieni ndani, na kama hatawaruhusu basi mtanipeleka kunizika pamoja na waislamu wengine makaburini".

Alipokufa walimchukua na kumpeleka kwenye chumba cha Aisha. Abdullah akamtolea salamu na kusema:

"Omar anaomba ruhusa". Mheshimiwa Aisha akajibu:

"Muingize ndani". Upesi aliingizwa ndani na kuzikwa pembezoni mwa marafiki zake watukufu. (Bukhari, As-habu al-Nabi 8, Janaiz 96, Jihad 174, Tafsir 59/5, Ahkam 43).

Tabia tukufu ya kutoa aliyokuwa nayo Aisha رضي الله عنها na upole, maadili na heshima ya Omar رضي الله عنه vilikuwa vya hali ya juu kiasi kwamba maneno hayawezi kuzielezea.

❁

Zaynab ibnt-i Jahsh رضي الله عنها, mke mwingine wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mwanamke mwenye maarifa makubwa katika kazi za mikono. Alikuwa akipata fedha kwa kupitia shughuli hii na kuitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaambia wake zake:

"Mwenye mkono mrefu ndiye atakayeungana na mimi mapema zaidi".

Aisha رضي الله عنها anaelezea:

"Kutokana na matamanio yetu na shauku ya kuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu tulikuwa tukipima mikono yetu ili tujue ni nani kati yetu atakuwa wa kwanza kuungana na Mtume. Ilikuwa baada ya pale ndipo tulipogundua kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliposema 'mwenye mkono mrefu' alimaanisha Zaynab. Kwani yeye ndiye aliyeweza kutengeneza vitu kwa mikono yake na alikuwa mkarimu mno katika kuwasaidia watu wengine" (Muslim, Fadail as Sahaba, 101)

❁

Baada ya kuhamia Madina, kila familia ya Madina (*Answar*[58]) iliichukua familia ya waislamu wapya waliowasili kutoka Makka (*Muhajirah*[59]). Kutokana na haya kulionekana makubaliano kati yao ya kufanya kazi kwa ushirikiano na kugawana mapato yao. Answar walitoa kiasi kikubwa cha ardhi na kumkabidhi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na yeye Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliigawanya kwa *Muhajirah*. Answar au wasaidizi walienda mbali zaidi kwa kutoa vifuatavyo:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Chukua mitende yetu na uigawanye kwa Muhajirun".

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokataa jambo hili Answar waliwageukia Muhajirina na kuwaambia:

"Kama ni hivyo chukueni jukumu la kuimwagilia na kuisimamia mitende ili tuje kugawana mavuno". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokubaliana na jambo hili pande zote mbili zikasema:

"Tumesikia na tumetii" (Bukhari, Harth 5).

Ni kiasi gani tunahitaji mwenendo huu Mtukufu katika dunia ya leo ambayo ina masikini wengi...

❁

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipowasili Madina Muhajirina walimwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kamwe hatujawahi kuona watu wakarimu na wenye kutoa kama kabila hili tulilohamia. Yeyote mwenye mali nyingi anatoa zaidi na yule mwe-

58. Answar ni jina walilopewa waislamu wa Madina na linamaanisha 'Wasaidizi'.
59. Muhajirah lilikuwa ni jina walilopewa kundi la kwanza la waislamu ambao waliacha nyumba zao na kuhamia Madina pamoja na Mtume na linamaanisha wahamiaji. (Maelezo ya mfasiri).

nye mali kidogo anajitolea kile kile alichonacho na kuwasaidia watu. Wametuondolea mashaka yote ya maisha na wametufanya washirika katika utajiri wao. Tunahofia kuwa watapata malipo yote na kutoacha chochote kwa ajili yetu".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

"Hapana. Hali ya kuwa mnawaombea kwa Mwenyezi Mungu na kuendelea kuwasifu kwa kile walichowafanyia, na nyinyi pia mtapata malipo yenu" (Tirmidhi, Qiyamah, 44/2487)

❁

Jabir ؓ anaelezea ukarimu wa Answar kwa Muhajirina kama ifuatavyo:

"Kila Answar walipokusanya mavuno yao ya tende waliyagawa katika mafungu mawili. Kisha walikuwa wakiweka tende nyingi kwenye fungu moja na kuweka tende chache kwenye fungu lingine. Kisha walikuwa wakiweka majani ya minazi katika lile fungu dogo ili lionekane kubwa kinyume na lilivyokuwa. Kisha walikuwa wakiwaambia Muhajirina: "Chukua fungu lolote unalotaka". Kwa kufikiria kuwa fungu kubwa linabidi kwenda kwa Answar, Muhajirina walikuwa wakichagua lile fungu lililokuwa linaonekana kuwa dogo. Kwa namna hii Muhajirina walikuwa wakipata tende nyingi. Na Answar nao walijihakikishia kuwa wanapata fungu dogo..." (Haythami, X, 40)

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amewagawia Muhajirina ngawira zilizokuwa zimechukuliwa kutoka Bani Nadir. Alikuwa hajampa chochote yeyote miongoni mwa Answar licha ya kuwepo watu watatu wenye kuhitaji. Baadae aliwageukia Answar na kuwaambia:

*"Kama mnataka viacheni vile mlivyowagawia Muhajirina mwanzoni viwe vyao na nyinyi mchukue ngawira hizi. Na kama mkitaka chukueni kile mlichokitoa na muache ngawira hizi zote kwa ajili yao".*

Kisha Answar wakatoa jibu lifuatalo lenye kuashiria ukarimu wao na kipaumbele chao kwa ndugu zao waislamu juu ya wao wenyewe:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Sisi tutawapa ndugu zetu Muhajirina sehemu ya mali zetu na nyumba zetu na pia tutawaachia ngawira zote"

Kutokana na hili aya ifuatayo ilishushwa kwa ajili ya kutoa bishara njema ya uongofu kwa wale waja wa Mwenyezi Mungu waliojitolea kwa moyo safi:

**"Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio hamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyo pewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji. Na mwenye kuepushwa uchoyo wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa"** (Al-Hashr, 59:9) (Al-Razi, XXIX, 250; Qurtubi, XVII, 25).

Hivyo moyo wa muumini hauna budi kuhisi amani wakati wa kutoa kama walivyokuwa Answar na kutohofia kuwa mali zao zitapungua.

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anataka kuigawa ardhi ya Bahrain kwa ajili ya kuwapa Answar. Answar walionyesha kujitolea kusikokuwa na mfano:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Usitupatie chochote mpaka uwapatie ndugu zetu Muhajirina mara mbili ya hiki"

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Enyi Answar! Kwa kuwa mmewapendelea ndugu zenu Muhajirina juu yenu na hamtaki chochote, basi kuweni na subira juu mitihani ya hii dunia mpaka mnifikie kwenye chemchem ya Kawthar*[60]*. Kwani baada yangu utakuja wakati ambao watu wengine watapendelewa juu yenu"* (Bukhari, Manaqibu'l Ansar 8)

❁

Siku moja wakati Aisha ﵂, mke wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa amefunga, masikini mmoja alimjia na kumuomba kitu. Aisha ﵂ hakuwa na chochote pale nyumbani isipokuwa kipande cha mkate. Alimwambia mtumishi wake:

"Mpe huyo mtu mkate".

Yule mtumishi akasema:

"Hakuna chochote isipokuwa hiki kipande cha mkate kwa ajili ya kufuturia".

Aisha ﵂ akasema tena:

"Mpe huyo mtu huo mkate".

Yule mtumishi anaendeleza kisa:

Kutokana na amri ya Aisha nilimpatia yule masikini ule mkate. Ilipofika usiku mtu mmoja alitutumia sehemu ya kondoo aliyepikwa. Aisha aliniita na kuniambia:

"Mchukue huyu, huyu ni mtamu zaidi ya mkate wako" (Muwatta, Sadaqa 5)

Tunaambiwa katika aya ndani ya Qur'an kuwa "**Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja wake, na anazikubali sadaka, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa**

60. *Kawthar* ni chemchem au mto kutoka peponi , mto ambao ndio chanjo cha mito yote ya peponi (Maelezo ya mfasiri).

**kupokea toba na Mwenye kurehemu?”** (Al-Tawba, 9:104). Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapa waja wake kulingana na madaraja ya nyoyo zao.

❁

Wakati fulani swahaba mmoja alipewa zawadi ya kichwa cha kondoo. Alimwambia mtoaji wa zawadi: “Ndugu yangu, familia ile na ile zinahitaji zaidi yetu” na kisha akaichukua na kuipeleka kwenye familia aliyoambiwa. Familia ile ikaitoa kwa familia nyingine... wakaendelea kufanya vile mpaka ikapitia nyumba saba na mara mwishowe ikarudi kwenye nyumba ya yule swahaba wa kwanza. (Hakim, II, 526).

❁

Tukio lifuatalo lililohadithiwa na Huzayfa al-Adawi رضي الله عنه ni la kuzingatia katika kutafakari juu ya ukarimu na kujitolea kwa maswahaba hata wakati wa pumzi zao za mwisho.

“Tulikuwa katika vita vya Yarmuk. Ukali wa mapambano ulizidi na wale waislamu waliokuwa wamejeruhiwa kwa panga na mishale walianza kudondoka chini kwenye mchanga wa moto mmoja baada ya mwingine na hatimaye kufariki. Baada ya muda mfupi nilikusanya nguvu zangu ili nimtafute mtoto wa mjomba wangu. Baada ya kuzunguka huku nikimtafuta katika wale waliojeruhiwa mwishowe nilifanikiwa kumpata. Lakini kwa bahati mbaya mtoto wa mjomba wangu alikuwa amelala kwenye dimbwi la damu na hakuweza kuongea hata kwa macho yake. Niliashiria kwenye chombo cha maji niliyokuwa nimekuja nayo na kumuuliza:

“Je unahitaji kunywa maji?”

Ilikuwa wazi kuwa alikuwa akihitaji yale maji kwani mdomo wake ulikuwa umekauka kwa joto. Hata hivyo hakuwa na nguvu za kujibu. Macho yake yalikuwa yanaashiria hali yake ya maumivu.

Nilifungua kile chombo cha maji na wakati nakaribia kumpa mara nikasikia 'aagh' kutoka kwa wale majeruhi wenzake.

Mara tu baada ya kusikia kilio hiki cha maumivu, mtoto wa mjomba wangu akajitoa nafsi yake na kuniashiria kwa macho yake kuwa nimpe yule majeruhi mwingine.

Nikakimbia juu ya ule mchanga wa moto na kumfikia yule mtu. Nilikuta mtu yule ni Hisham ibn As. Nikamuuliza:

"Je unahitaji kunywa maji?" Aliashiria 'ndio' kwa macho yake. Wakati anataka tu kunywa mara tukasikia sauti nyingine ya 'aagh, aagh'. Hisham akaashiria kuwa nimpelekee maji mtu yule.

Nilipomfikia alikuwa tayari ameshafariki. Upesi nikarudi kwa Hisham lakini nilipotaka kumpa maji mara naye akakata roho.

Nilijifikiria mwenyewe kuwa naweza kumuwahi mtoto wa mjomba wangu na kisha nikamkimbilia. Lakini haikupangwa kuwa kama nilivyotarajia kwani alikuwa ameshakata roho juu ule mchanga wa moto...nilibakia na kile chombo cha maji kikiwa kimejaa vile vile baada ya kukipitisha kwa mashahidi watatu.[61]

Baadae Hudhayfa alizungumzia hali aliyokuwa nayo wakati ule:

"Nilikuwa na uzoefu mkubwa katika maisha yangu. Lakini hakuna jambo lililokuwa limenigusa kuliko hili. Ingawa hatukuwa na udugu wa damu na hawa maswahaba watatu lakini hali yao ya kujitolea, huruma yao na namna walivyopendeleana wao kwa wao iliacha alama kubwa ndani ya kichwa changu. Ile ilikuwa ni imani ya hali ya juu ambayo niliweza kuishuhudia kwa umakini mkubwa. Watu hawa waliweza kuyaaga maisha huku wanaonyesha wema ule ule waliokuwa nao katika maisha yao yote na wali-

61. Angalia Qurtubi, XVII, 28; Zaylai, Nasbu ar-Raye, II, 318; Hakim, III, 270/5058.

onyesha uelewa wao juu ya aya: "**msife ila nanyi ni Waislamu"**[62] kichwani mwao.

❁

Mpinzani mkubwa wa Sufi, Gulam Khalil alikuwa anawapinga sufi wote. Alisababisha kundi la masufi kukamatwa na kupelekwa Khalifa, miongoni mwao alikuwepo Abu al-Hussain an Nuri. Kutokana na hukumu iliyokuwa imetolewa na Khalifa Abbasi wakati ule iliwapelekea kuuawa. Wakati muuaji anataka kumkata kichwa mmoja wa madaruwesh, Abu al-Hussain an Nuri alisogea mbele yeye mwenyewe na kwa furaha. Watu walishangazwa na kitendo hiki. Yule muuaji akasema:

"Ewe shujaa. Umekuja mbele mwenyewe lakini huu upanga sio wa kukimbilia. Bado zamu yako haijafika, kwa nini una haraka hivyo?". Abu al-Hussain akajibu:

"Mimi ni mtu nisiyekuwa na ubinafsi. Kitu chenye kupendwa na chenye thamani kubwa ni uhai wenyewe. Ninataka kuitoa hii nafasi yangu ya mwisho ya uhai kwanza ili ndugu zangu waendelee kuishi kidogo zaidi. Kwetu sisi muda wa kuvuta pumzi moja zaidi ni jambo la thamani na lenye kupendeze zaidi kwetu kuliko miaka elfu moja ya huko akhera. Kwani hapa ni sehemu ya kutumikia, na huko ni sehemu ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu. Na kuwa karibu na Mwenyezi Mungu kunapatikana kwa kumtumikia yeye. Licha ya haya ninataka kujitolea pumzi zangu za mwisho kwa ajili ya marafiki zangu".[63]

❁

Baada ya kifo cha Othman Ghazi, Aladdin Bey ambaye alikuwa akiungwa mkono na viongozi miongoni mwa machifu na

62. Angalia Al'I Imran, 3:102.
63. Hujwiri, "Kashfu'l Mahjub," tafsiri. Sulayman Uludag, Istanbul 1996 uk 302.

ambaye alihitajika kuchukua enzi kutokana na desturi zao, alimchagua ndugu yake Orhan Bey badala yake na kusema:

"Ndugu yangu! Wewe una dua na ulinzi kutoka kwa mababu zetu. Wakati alipokuwa hai alikuchagua kuongoza jeshi. Hivyo unastahili kuwa mtawala".

Alaaddin Bey ambaye alionyesha ukarimu wa hali ya juu na kujitolea alikuwa msaidizi mkubwa wa ndugu yake na alikuwa waziri mkuu wake.[64]

❁

Tarehe 10 mwezi wa kumi mwaka 2005 Pakistani ilitikiswa na tetemeko kubwa la ardhi na zaidi ya watu 70000 walikufa. Wale waliokuwa wamebaki walikabiliwa na njaa na umasikini. Tarehe 24 mwezi wa kumi na moja kijana mmoja mdogo kutoka Uturuki aliwatumia barua ifuatayo. Ndani yake alitangaza kujitolea nusu ya mali yake kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zake waislamu, hivyo kuonyesha kilele cha ukarimu:

"Mimi ni mtoto wa masikini. Sina baba na mama yangu ni mgonjwa. Tuna lira mbili kwa ajili ya kununulia mkate, lakini ninawatumia moja wapo ya hizi lira kwa sababu leo nimepata kipande kingine cha mkate kwenye takataka. Tutakitumia kipande hicho kufuturia. Tafadhali wanunulia mkate watoto walioathirika na tetemeko la ardhi kwa kutumia lira hii moja. Fedha hii ni ya halali na safi. Sikuweza kutuma fedha yote kwa sababu naihitaji hii iliyobaki kwa ajili ya kununulia stempu. Nawaomba radhi"[65].

Ukarimu na wema ulioje...upepo mwanana unaovuma kutoka kwenye zama za neema...

❁

64. Ziya Nur Aksun, Ottoman History, Istanbul 1994, I, 36.
65. Angalia http://www.presidentofpakistan.gov.pk/NewsEventImagePopUp.aspx?ImageID=129 (28/12/2005)

Kwa ufupi ni kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa katika kilele cha ukarimu katika nyakati zote, wakati wa mali na umasikini. Alikuwa akiwashauri maswahaba zake kuwa wakarimu na kutoa wakiwa matajiri au masikini. Katika hadith ifuatayo anaelezea namna ukarimu usivyopunguza mali ya mtu:

"Kila siku ambayo jua linachomoza malaika wawili huita: "Enyi watu njooni kwenye rehema za Mola wenu. Kiasi kidogo cha mali kinachokutosheleza ni bora kuliko mali nyingi ambayo itakupoteza". Viumbe vyote husikia maneno haya isipokuwa watu na majini.

Kila siku ambayo jua linazama malaika wawili wanachukua nafasi yao wale wa kwanza na kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu, mpe mafanikio yule anayetoa na mpe maharibiko yule asiyetoa". Pia maneno haya nayo yanasikiwa na kila kiumbe kinachoishi juu ya ardhi isipokuwa watu na majini" (Ahmad, V, 197).

Hivyo mafanikio ya kweli ni kuujaza moyo kwa hisia za ukarimu na kutoa ili kuufanya kuwa bahari na kubadili neema za hii dunia ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia na kuwa utajiri wa kesho akhera. Kutokana na kipengele hiki tunagundua kuwa utajiri wa kweli ni ule ambao mmiliki wake anautanguliza peponi; na roho nzuri ni ile inayotumika kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

### 13. Qanaat na Istighna (Kukinai na kutosheka)

Kanaat au kukinai ni kuridhika na kile alichokupangia Mwenyezi Mungu, kutosheka na kinachokutosheleza, kukidhi mahitaji ya mtu kwa kiasi kidogo na kutosheka na kiwango chochote cha mali alichojaaliwa mmoja wetu. Na sio kutamani alichokuwa nacho mwingine, na hivyo kufuta ulafi.

Wanadamu wameletwa katika dunia hii kwa ajili ya kujaribiwa na hivyo hawana budi kutosahau lengo lao la kuumbwa na kuwa makini katika utafutaji wao wa riziki. Kila mtu hana budi kujitahidi kubadili mali na fursa ambazo Mwenyezi Mungu amemjaalia na kuwa mtaji kwa ajili ya kesho akhera. Kwani Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amechukua Mwenyewe jukumu la kutoa riziki kwa viumbe vyote, na anapenda wakinai na kutosheka. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an:

**"Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha"** (Hud, 11:6).

**"Na tumekujaalieni humo vitu vya maisha yenu, na ya hao ambao nyinyi sio wenye kuwaruzuku."** (Hijr, 15:20).

**"Hakika nyinyi mnaabudu masanamu badala ya Mwenyezi Mungu, na mnazua uzushi. Hakika hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawakumilikiini riziki yoyote. Takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu, na mumuabudu Yeye, na mumshukuru Yeye. Kwake Yeye ndio mtarudishwa"** (Al-ankabut, 29:17).

**"Hakika hii ndiyo riziki yetu isiyo malizika"** (Saad, 38:54).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwasifu watu wenye kukinai kama ifuatavyo:

*"Amefaulu Muislamu ambaye amejaaliwa riziki ya kutosha na akarizika na neema ambazo Mwenyezi Mungu amemjaalia"* (Muslim, Zakat, 125).

Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiomba dua ifuatayo:

*"Ewe Mwenyezi Mungu! Ipe familia ya Muhammad riziki ambayo itawatosheleza kukidhi mahitaji yao"* (Muslim, Zakat, 126).

Mtu tajiri ambaye bado hajatosheka hatulii na anakabiliwa na mahangaiko zaidi kuliko alivyo mtu masikini na fakiri. Kadiri anavyozidi kupata mali kamwe hatosheki na daima anataka zaidi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amewaelezea wale wenye udhaifu katika kukinai kama ifuatavyo:

*"Hata kama mwanadamu angelipewa bonde lililojaa dhahabu angelihitaji lingine. Hakuna kitakachomtosheleza isipokuwa udongo. Hata hivyo Mwenyezi Mungu anakubali toba ya yule anayetubia"* (Bukhari, Riqaq, 10; Muslim, Zakat 116-119).

Hivyo kila mtu hana budi kutubia kwa dhambi ya kutotosheka. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amewashauri watu juu ya suala hili kama ifuatavyo:

"Yeyote miongoni mwenu atakayemuangalia mwingine ambaye yuko juu yake, pia ageuze macho yake na kuwaangalia wale walio chini yake" (Bukhari, Riqaq, 30).

Luqman Hakim anatoa ushauri ufuatao:

"Mwanangu! Usiujaze moyo wako wasiwasi na hofu. Jihadhari na uroho na ulafi wa mali. Kikubali kile ulichopangiwa. Ridhika na kile ambacho Mwenyezi Mungu amekujaalia na maisha yako yatastawi, moyo wako utajawa furaha na utapata raha ya maisha"

Hata hivyo tusielewe vibaya kukinai kana kwamba Uislamu unahimiza kuacha kufanya kazi na kuwa wavivu na kufikia mahali ambapo mtu anawategemea wengine. Kukinai ni suala la moyoni na tabia ya mtu. Muislamu hana budi kutafuta kipato chake kwa njia za halali na safi na kutekeleza majukumu yake ya kiuchumi na kuwasaidia wale wanaomzunguka.

Sifa nyingine nzuri ya watu wema ni *istighna*, au kujiepusha na kuomba. Istighna inamaanisha kutosheka, kuwa na utajiri wa moyo, kutosheka na kile ambacho Mwenyezi Mungu amekujaalia,

kutotarajia chochote kutoka kwa wengine na kutotaja shida zako kwa wengine. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

"Malaika Jibril alikuja kwangu na kusema: "Ewe Muhammad! Ishi utakavyoishi lakini mwishoni utakufa. Penda utakachokipenda lakini mwishoni itakubidi utengane nacho. Jitume katika jambo lolote na mwishoni utaona matokeo yake. Fahamu kuwa heshima ya muumini ipo katika kusimama usiku na kuswali; na utu wake uko katika kutowaomba watu wengine" (Hakim, IV, 360-361/7921).

*Istighna* ni sifa ya nyoyo za wale watu wema na wenye nyoyo safi ambao wamejiweka huru kutokana na asili yao na kufikia kwenye ukamilifu wa imani. Huu ni utajiri wa moyo. Huku ni kujizuia na kujishusha na kuvionea wivu vile walivyonavyo wengine na kutosheka na kile ulichonacho.

Katika hadith nyingine tunafahamishwa kuwa: "Kukinai ni hazina ambayo kamwe haiishi" (Daylami, III, 236/4699). Hivyo kama inavyohitajika katika hadith hii, istighna ni pale moyo unapofikia kwenye hali ya amani kwa kuwa na imani ya hali ya juu kutokana na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Moyo uliopambwa kwa istighna na kukinai hupata amani kutokana na hofu na wasiwasi wa kidunia. Hapa nafsi hutambua maisha ya milele na kwa muumini starehe za dunia zenye kudanganya hufikia mwisho. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamfanya asihitaji kingine chochote isipokuwa Yeye Mwenyezi Mungu pekee kwa kupitia sifa yake ya *'Al-Mughni'*[66].

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Yeyote atakayejikuta katika shida na kuitaja shida yake kwa wengine basi shida yake haitaisha kamwe. Lakini yeyote atakayeishitakia shida yake kwa Mwenyezi Mungu basi inataraji-*

66. *Al Mughni* ni moja miongoni mwa majina matukufu ya Allah na linamaanisha 'mwenye kutajirisha' (Maelezo ya mfasiri).

*wa kuwa shida yake itatuliwa ama hapo hapo au baadae"* (Tirmidhi, Zuhd, 18/2326; Abu Dawud, Zakat 28/1645).

Istighna si kuhusu mali, utajiri na hazina pekee. Ni kuuchunga moyo kutokana kuvitegemea zaidi viumbe na kumsahau Mola wake.

***Matukio ya wema***

Mara nyingi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alikuwa mwenye kukinai kupita watu wote, alikuwa akiwaambia maswahaba zake waahidi kuwa hawataomba chochote kutoka kwa mtu yeyote. Sawban ؓ anasimulia:

"Wakati fulani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Yeyote atakayeniahidi kuwa hatoomba chochote kutoka watu nitamhakikishia kuipata pepo"*.

Kisha nikamwambia:

"Mimi ninaahidi"

Sawban ؓ ambaye ndiye swahaba aliyeisimulia *hadith* hii anasema kuwa kuanzia siku ile kamwe hakuomba chochote kutoka kwa mtu yeyote katika kipindi chote cha uhai wake. (Abu Dawud, Zakat, 27/1643).

Hadith hii inaonyesha fadhila za kujiepusha na utegemezi kwa wengine. Maruf-i Karhi amesema yafuatayo katika kuonyesha namna tasawwuf ilivyo na mkazo mkubwa katika suala la kukinai na *istighna*:

"*Tasawwuf* ni kupokea ukweli na kuondoa tamaa juu kile alichonacho mwenzako"

❁

Tukio lifuatalo lililosimuliwa na Awf ibn Malik ؓ ni la kuzingatia mno katika kujua namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyokuwa akiwafundisha maswahaba zake kuhusu kukinai na *istighna*:

“Kikundi cha watu saba au nane walikuwa wamekaa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Akatuuliza:

*“Je hamtoweka makubaliano na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?”* wakati muda si mrefu ndio tulitoka kufanya makubaliano. Tukasema:

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tayari tumeshafanya makubaliano na wewe. Sasa ni kipi hicho unachotaka tuweke tena makubaliano na wewe?” Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*“Ahadi kuwa mtamuabudu Mwenyezi Mungu na hamtafanyia washirika, na kuwa mtasimamisha swala tano kila siku, na kuwa mtatii, na-* huku amepunguza sauti yake akasema- *hamtaomba chochote kutoka kwa mtu yeyote”*. Naapa niliwaona watu ndani ya kundi hili ambao hata kama mijeledi yao ingelidondoka wakiwa juu farasi wasingeliweza kumuomba mtu yeyote awaokotee” (Muslim, Zakat, 108).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyarudia maneno yake mara tatu huku amepunguza sauti yake akiashiria umuhimu wa jambo hili.

❁

Pale Abu Bakr ؓ alipokuwa akidondosha vitu vilivyokuwa juu ya ngamia wake alikuwa akisimamisha ngamia wake mara moja na kushuka chini na kuviokota yeye mwenyewe. Wale waliomzunguka husema:

“Kama ungelituamrisha sisi tukuokotee tulingelikuokotea”.

Abu Bakr ؓ hutoa jibu lifuatalo:

“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ameniamrisha kamwe kutoomba chochote kutoka kwa mtu yeyote” (Ahmad, I, 11).

❁

Amr ibn Taglib ؓ anasimulia:

“Siku moja ngawira- au watumwa- zililetwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kutokana nazo aliwagawia baadhi na kuwanyima baadhi. Hata hivyo alipofikiwa na manung’uniko ya wale wasiopewa ch*ochote alimsifu Mwenyezi Mungu na kisha akasema:*

*“Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa ninawapa baadhi na kuwanyima wengine. Ukweli ni kwamba wale nisiowapa wanapendeza zaidi kwangu kuliko wale ninaowapa. Ninawapa wale watu ambao ninaona nyoyoni mwao hakuna subira na ni walafi. Na ninawanyima wale ambao ninaona kukinai na wema nyoyoni mwao. Amr ibn Taglib ni mmoja miongoni mwao”.*

Kisha Amr ibn Taglib ؓ akasema:

“Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa yale maneno ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniambia yalikuwa na thamani kubwa mno kwangu kuliko dunia nzima” (Bukhari, Jum’a 29, Humus 19, Tawheed 49).

❁

Omar ؓ anasimulia:

“Mara kwa mara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akinipa mshahara kutokana na kuhudumia kwangu katika vita na nilikuwa nikimwambia:

“Kwa nini usingelimpa fedha hizi mtu mwingine ambaye anahitaji zaidi kuliko mimi?”. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akijibu:

"Chukua. Unaweza kupokea fedha unazopewa bila ya wewe kuzitaka au kuzimezea mate. Zichukue fedha hizi wewe mwenyewe na kama ukitaka utazitoa kwa yeyote. Lakini usitafute fedha kinyume na hivi" (Bukhari, Zakat, 51)

❁

Pindi kabila la Bani Tujib lilipotaka kurejea katika nchi yao baada ya kumtembelea Mtume, aliwafanyia ukarimu mkubwa katika vitu alivyowapa kuliko makabila mengine na kisha akawauliza:

*"Kuna yeyote miongoni mwenu ambaye hajapata chochote?"*

"Ndio, tulimuacha nyuma yetu kijana ambaye ni mdogo kuliko sisi kwa ajili ya kutuangalizia vipando vyetu" walijibu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akawaambia:

*"Mleteni hapa"*. Walipoenda kule vilipokuwa vipando vyao wakamwambia yule kijana:

"Nenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu upate zawadi yako. Tumeshachukua zawadi zetu na kumuaga kabisa". Yule kijana alipofika kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamwambia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, Mimi ninatoka kwenye kabila la watoto wa Abza. Ninatoka kwenye kundi ambalo ulikuwa nalo muda si mrefu, kundi ambalo uliitatulia shida zao . Je na mimi pia utanitatulia shida yangu?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

"Una shida gani?"

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, shida yangu sio kama ile ya marafiki zangu. Ninakuomba uniombee kwa Mwenyezi Mungu anisamehe madhambi yangu, anihurumia na kunizidishia imani katika moyo wangu"

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Ewe Mwenyezi Mungu. Msamehe madhambi yake, mhurumie na kumzidishia imani katika moyo wake!"* Kisha akaamuru na yeye apewe zawadi kama wale wenzake.

Lile kabila la Bani Tujib likarejea nchini mwao. Baadae kundi moja kutokana na watu hawa lilikutana na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa Mina wakati wa Hijja. Wakamwambia Mtume:

"Sisi tunatoka kwenye kabila la watoto wa Abza". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alikuwa mfano wa kuigwa katika uaminifu aliwauliza:

*"Yule kijana mliyekuja naye mwaka jana anaendeleaje?"*

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Hatujapata kumuona mtu mwenye kukinai kwa kile ambacho Mwenyezi Mungu amemjaalia kama kijana yule. Kama watu wangelitaka kugawana dunia yule kijana asingelijisikia hata kidogo kutokana na jambo hili", walijibu. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuyasikiliza maneno haya kutokana na furaha aliyokuwa nayo alimsifu Mwenyezi Mungu na kumuombea kheri kijana yule.

Kijana huyu akaja kuwa mfano wa kuigwa katika jamii yake kutokana na tabia yake nzuri. Aliendelea kuishi kama mtumishi wa Mwenyezi Mungu ambaye hakuipa thamani dunia hii na ambaye aliridhika mno na kile ambacho Mwenyezi Mungu alimjaalia. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kufariki yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza katika kuwakumbusha watu kuhusu Mwenyezi Mungu na dini yao, wakati ambao watu wengi wa Yemen waliipa mgongo dini yao ya Uislamu. Kutoka katika kabila lake hakuna hata mtu mmoja aliyeipa mgongo dini yake kutokana na yeye. Baadae Abu Bakr رضي الله عنه alitakiwa amchunguze yule kijana. Aliwaulizia watu kuhusu kijana yule na kumuandikia barua

gavana wa sehemu ile akimshauri kuwa akae na kijana yule kwa wema. (Ibn Qayyim, III, 650-652; Ibn Sa'd, I, 323).

❁

Mkataba waliowekeana kati ya Muhajirina ambao walitoka Makka na kuhamia Madina, na Answar wa Madina ulikuwa ni jambo la kipekee ambalo mfano wake haukuwahi kuonekana katika historia. Ilifikia kwa Answar kutangaza mali zao zote na kuzitoa kwa ajili ya kugawana na ndugu zao Muhajirina nusu kwa nusu. Kutokana na haya Muhajirina ambao nyoyo zao zilikuwa hazina ya ukinaofu, walionyesha kutotaka chochote kutoka kwao na kufikia kusema:

"Mwenyezi Mungu abariki mali zako na utajiri wako kwa ajili yako ewe ndugu yangu, kwa mimi itatosha kunionyesha njia ya kuelekea sokoni" (Bukhari, Buyu'u, 1)

❁

Siku moja mtu mmoja masikini kutoka kwa waislamu wa Madina alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuomba chakula.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuuliza:

*"Je huna chochote nyumbani kwako?"*

Yule mtu akajibu:

"Ndio tunacho. Tuna kitambaa ambacho sehemu tunaitumia kwa ajili ya kujifunikia sisi wenyewe na sehemu tunaitumia kwa ajili ya kutandikia kwenye sakafu, na pia tuna buli la maji"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

"Kaniletee hivyo vitu". Yule mtu akaenda na kumletea kile kitambaa na buli la maji. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akavi-

chukua vitu vile mikononi mwake na kuwauliza watu waliokuwa karibu yake:

*"Ni nani atapenda kuvinunua vitu hivi?"*

Mmoja miongoni mwa maswahaba akasema kuwa yeye alikuwa tayari kuvinunua kwa dirham moja. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akanadi tena kwa mara kadhaa:

*"Hakuna yeyote mwingine ambaye ataweza kutoa zaidi?"*

Baadae akaviuza kwa swahaba ambaye alikuwa tayari kuvinunua kwa dirham mbili. Kisha akampa yule masikini zile fedha na kumwambia:

*"Nenda ukanunue chakula kwa ajili ya familia yako kwa dirham hii. Na kwa hii iliyobaki nenda ukanunulie shoka na kisha ulilete kwangu".*

Pindi yule mtu aliporudi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa na shoka, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilichukua na kuliwekea mpini kwa kutumia mikono yake mwenyewe na kisha akamwambia yule mtu:

*"Sasa unaweza kwenda. Kakate kuni kwa shoka hili na kisha uziuze. Fanya hivyo kwa siku kumi na tano kisha urudi kwangu".*

Baada ya siku kumi na tano yule mtu akarudi kwa Mtume. Alikuwa amepata dirham kumi na hivyo akaweza kununua chakula na mavazi kwa ajili yake na familia yake.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alifurahishwa sana na jambo hili, akamwambia:

*"Jambo hili ni zuri zaidi kwako kuliko kuomba kwako ambako kunaweza kuwa doa kwako siku ya kiama..."* (Abu Dawud, Zakat, 26/1641; Ibn Majah, Tijarah, 25).

Muislamu hana budi kuwa na tabia ya kumuelekeza Muislamu mwenzake njia nzuri itakayoweza kumpatia kipato. Na masikini hawana budi kujiepusha na kuomba kwa watu wengine badala yake wajitahidi kufanya kazi katika njia iliyoelekezwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

❁

Abu Said ﷺ alikuwa mmoja miongoni mwa maswahaba waliokuwa wakifunga mawe kwenye matumbo yao kwa ajili ya kupunguza njaa. Mama yake alimwambia:

"Simama na uende kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Kamuombe chochote. Fulani na fulani walienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kusaidiwa. Na fulani na fulani pia walienda na kupewa sadaka. Sasa na wewe nenda, unaweza ukarejea na chochote".

Abu Said ﷺ akamjibu mama yake:

"Acha tusubiri kidogo na kutafuta chochote. Kama hatutapata chochote tutaenda". Kadiri alivyotafuta lakini hakuweza kupata chochote cha kula. Kutokana na kutokuwa na kingine cha kufanya aliamua kwenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Alipofika pale alipokuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimkuta anatoa mawaidha na yeye akaamua kukaa na kumsikiliza. Katika mawaidha yake alikuwa anazungumzia kuhusu yafuatayo:

*"Mwenyezi Mungu atamfanya yule asiyeomba na akahifadhi heshima yake kuwa mtu asiye tegemezi kwa kiumbe chochote..."*

Baada ya kuyasikia maneno haya, Abu Said ﷺ hakuweza kuomba tena chochote kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na hivyo akarejea nyumbani kwao akiwa mikono mitupu. Anaielezea hali yake baada ya pale kama ifuatavyo:

"Baada ya kurudi nyumbani kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ nikiwa mikono mitupu Mwenyezi Mungu Mtukufu alitushushia riziki yetu na mambo yetu yakawa mazuri kiasi kwamba hakukuwa na yeyote katika Answar ambaye alikuwa tajiri kuliko sisi" (Angalia Ahmad, III, 44).

Huu ndio umuhimu wa kuweza kumfahamu Mola wako vizuri. Umuhimu wa kufahamu kuwa Mola wetu ni *Al- Razzak*, Mwenye kutoa riziki, ambaye anagawanya riziki kwa waja wake. Kadiri tunavyomuamini, tunavyomtegemea na kujisalimisha kwake ndivyo nyoyo zetu zinavyozidi kuridhika na kupata amani zaidi.

❁

Hakim ibn Hizam ﷺ anasimulia:

"Siku moja nilienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kumuomba anipe sehemu ya ngawira walizokuwa wamezipata. Alinipatia ngamia mia moja. Nilimuomba aniongezee akaniongezea wengine mia moja. Nikamuomba tena zaidi akaniongezea wengine mia moja. Kisha akaniambia:

*"Ewe Hakim! Kwa hakika hizi mali zinavutia na kupendeza. Zitabarikiwa kwa yeyote atakayezichukua bila ya hisia za uroho. Yeyote atakayezichukua kwa uroho na tamaa hazitakuwa na baraka yoyote kwake. Mtu huyo ni kama yule ambaye anakula tena na tena na kamwe hatosheki. Mkono unaotoa ni bora kuliko mkono unaochukua".*

Kutokana na haya nikasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu ambaye amekuleta na dini ya kweli kuwa kamwe sitakubali chochote kutoka kwa mtu yeyote kinyume na wewe hali ya kuwa niko hai".

Kisha Hakim ﷺ akawachukua wale ngamia mia moja wa kwanza ambao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimpatia na kuwaacha wale waliozidi. Ikafika siku ambayo Abu Bakr ﷺ (wakati wa ukhalifa wake) alitaka kuzigawanya ngawira na hivyo akamuita Hakim ili ampe. Hata hivyo Hakim alikataa kuchukua chochote kutoka kwake. Mara nyingine tena Omar ﷺ (wakati wa ukhalifa wake) alimuita Hakim ili ampe ngawira, lakini Hakim ﷺ hakukubali kupokea kitu chochote kutoka kwake pia. Kutokana na haya Omar ﷺ akawaambia watu:

"Waislamu, naomba mumuangalie Hakim. Ninampa mgao ambao Mwenyezi Mungu amempangia kutokana na ngawira lakini yeye anakataa". Hivyo ikawa baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ Hakim ﷺ kamwe hakupokea chochote kutoka kwa mtu yeyote. (Bukhari, Wasaya 9; Waqidi, III, 945).

Huu ni mfano wa kipekee wa kutambua namna ya kukinai kwa kile ulichonacho, kuwa mbali na utegemezi kwa watu wengine na kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ...

❁

Ahmad ibn Hanbal ambaye alifahamika kwa uchamungu wake na kujiweka mbali na anasa za dunia, siku moja aliulizwa:

"Kipi ni bora, utajiri au umasikini?"

Akajibu:

"Endelea kwenda sokoni (yani fanya biashara zako) na usiwe tegemezi kwa wengine. Siujui ubora mwingine zaidi ya kutowategemea watu"

Siku moja Ibrahim ibn Adham alimuona mtu akilalamikia umasikini akamwambia:

"Je walikupa umasikini bila ya kuulipia kiasi kwamba unaulalamikia hivyo?"

Yule mtu akauliza kwa mshangao:

“Ewe mheshimiwa. Je kuna namna ya kuwajibika kwenye umasikini?”

❁

Ibrahim ibn Adham akamjibu:

“Ndio, pindi nilipoiona thamani ya umasikini niliitoa ardhi yangu Belh kwa hiari yangu na kwa furaha kwa ajili ya kuununua umasikini”

Jambo lililokusudiwa hapa ni kuwa tajiri katika ukinaifu kwa kuondokana na uroho wa nafsi. Watu masikini wenye subira na matajiri wenye kushukuru wako sawa mbele ya radhi za Mwenyezi Mungu. Thamani ya umasikini ulioambatana na subira haina kipimo...

❁

Siku moja Abu Hazim aliulizwa:

“Una mali kiasi gani?”

“Nina vitu viwili: cha kwanza ni kwamba nimeridhika na kile alichonijaalia Mwenyezi Mungu; na cha pili ni kwamba mimi si tegemezi kwa watu”.

“Kama hivyo wewe ni masikini”, aliambiwa.

Akajibu:

“Nitakuwaje masikini wakati mbingu na ardhi na vyote vilivyopo kati yake ni vya Mwenyezi Mungu, na mimi ni mja wake mwema?”

Umasikini wa kweli ni wa moyo uliojiweka mbali na Mwenyezi Mungu. Moyo uliopewa neema ya kuwa karibu na Mwenyezi

Mungu ndio moyo tajiri kuliko nyoyo zote duniani. Na ule ulio mbali na Mwenyezi Mungu ndio ulio chini kuliko zote.

❀

Kisa kifuatacho kinaonyesha ubora wa ukinaifu na *istighna* na pia kimebeba somo kwa ajili yetu sote:

Wakati fulani ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani ulipofika muda wa kufuturu, mtu mmoja ambaye sura yake ilikuwa imejawa na utukufu ambao haujawahi kuonekana na watu kamwe aliwasili kwenye sehemu ya kuchomea mikate. Baada ya watu kupungua alimwambia mwoka mikate:

"Mwanangu, Sikuweza kupata kipato changu cha leo, je unaweza kunipatia robo ya mkate ambao nitakulipa kesho kama nitakuwa bado hai?"

Sauti yake ilikuwa ikitetememka na uso wake ulikuwa mwekundu. Yule mwoka mikate akamjibu:

"Bila shaka mheshimiwa; nitakupatia mkate mzima, huna haja ya kunilipa". Hata hivyo yule mzee akasema:

"Hapana mwanangu, robo inatosha...Inawezekana wakaja wahitaji wengine watatu kwa ajili ya mkate. Hata hivyo hii itapelekea robo ya uso wangu kuwa wekundu. Siwezi kuchukua zaidi ya hicho. Na sharti langu katika kuchukua robo ni ili kesho nikulipe".

Yule mwoka mikate akampatia robo ya mkate huku akiwa amestaajabishwa na jambo lile. Yule mtu akauchukua mkate ule, akaubusu na kuondoka taratibu huku akiwa kimya. Alipofika mbele kidogo akatokewa na mbwa. Mbwa yule alikuwa akimuangalia mzee yule kwa macho yenye kudhihirisha njaa yake. Mtu yule aliyebarikiwa akasema: "Ina maana nusu ya mkate huu ni kwa ajili yako" na kisha akampatia yule mbwa nusu ya ile robo. Baada ya pale akaenda msikitini na kufungulia swaumu yake kwa

kile kipande kilichokuwa kimebaki na maji. Kisha akamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema aliyokuwa amemjaalia.

Siku iliyofuata muuza duka alimwambia:

“Mheshimiwa, naomba uchukue hizi chupa za maji na kisha uzijaze kwa maji ya chemchem ile na kisha uziingize ndani”. Kisha yule mtu akampa lira moja kwa shughuli hii.

Kisha mzee yule wa kipekee akaenda kwa mwoka mikate upesi na kumlipa senti 25 kwa ajili ya ile robo ya mkate. Mwoka mikate hakutaka kuzichukua lakini mtu yule mwema alisisitiza mno kiasi kwamba akashindwa kukataa zaidi; alilazimika kuzichukua zile fedha huku akiwa amejawa na machozi.

Huyu ni mtu ambaye alikuwa mfano wa kuigwa katika ukinaifu na kutoomba ovyo. Pia alikuwa mja wa Mwenyezi Mungu aliye mkarimu ambaye aliweza kutoa sehemu ya mkate wake licha ya kuwa masikini na hivyo kuonyesha huruma kwa viumbe vya Mwenyezi Mungu.

❁

Ifuatayo ni mifano miwili ya ukinaifu na istighna ambayo tuliishuhudia katika taasisi ya Aziz Mahmud Hudayi ndani ya Istanbul:

Taasisi yetu ilikuwa katika harakati za kumsaidia mama na mwanae. Mwanae alikuwa amepooza lakini alikuwa ameshamaliza chuo kikuu. Siku moja yule mama alikuja kwenye taasisi yetu na kutushukuru kwa kusema:

“Kuanzia sasa sitaendelea kupokea msaada wowote kutoka kwenu. Mnaweza kuwasaidia watu ambao watakuwa na shida zaidi yangu, kwani mwanangu ameshafariki. Zile fedha za mwisho kupokea nilizitumia katika mazishi ya mwanangu. Sasa hivi nimeachwa mwenyewe na ninaweza kujisimamia mwenyewe. Tafad-

hali wapeni zile fedha ambazo mngelinipa mimi wahitaji wengine ambao wapo katika hali kama niliyokuwa nayo mwanzoni".

Familia nyingine ambayo tulikuwa katika harakati za kuisaidia ilikuwa ni familia kutoka Uholanzi. Mama alikuwa amefiwa na mumewe na watoto wake wakaachwa yatima. Siku moja aliiandikia taasisi yetu barua ya shukurani, barua ambayo ndani yake kuliandikwa:

"Sasa nimelipa madeni ya mume wangu. Nimemuokoa kutokana na kuwaingizia madeni watu wengine. Kwa sasa naweza kuendelea kwa juhudi zangu mwenyewe".

Hivyo utu hauhusiani na utajiri wala umasikini; utu wa kweli ni lulu iliyo ndani ya moyo wa mtu.

❁

Mja wa Mwenyezi Mungu hana budi kujiepusha na utegemezi kwa wengine, lakini pia asikae mbali na neema ambazo zinamfikia kutoka kwa Mwenyezi Mungu. *Hadith* ifuatayo inalielezea suala hili vizuri zaidi:

"Nabii Ayub عليه السلام alikuwa amelivua joho lake kwa ajili ya kulifua, mara fungu la dhahabu likadondoka mbele yake. Upesi akaanza kuzijaza kwenye lile joho lake. Kutokana na haya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akamuita:

"Ewe Ayub! Je sikukutoa kwenye matamanio ya kidunia ambayo ninakuona nayo sasa hivi?" nabii Ayub akajibu:

"Ninaapa mbele ya utukufu wako kwa hakika ulinitoa Ewe Mola wangu. Lakini sikutoka kwenye kuhitajia baraka zinazonifikia kutoka kwako" (Bukhari, Ghusul, 20)

❁

Siku moja Hasan Basri alimuomba Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi kama ifuatavyo:

"Ewe Mwenyezi Mungu! Naomba unifanye nihitaji zaidi kutoka kwako. Na usinidhoofishe kwa kunifanya nisikutegemee Wewe". (Baqillani, I'jazu al-Qur'an, Beirut 1998, uk 107).

❁

Kwa ufupi ni kwamba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema kuwa utajiri wa kweli unatambulika kutokana na utajiri wa moyo na sio kwa utajiri wa mali.[67] Hivyo kila mtu ni tajiri kulingana na kiwango chake cha ukinaifu na *istighna*. Kutokana na hadith tunafahamishwa kuwa ukinaifu ni hazina ambayo haiishi kamwe[68]. Waumini wa kweli ni wale ambao wanayo neema hii ya utajiri na wanaitumia.

**14. Kujitenga na dunia**

*Zuhd* ni kujitenga na raha zote za dunia, yani kutozipa thamani yoyote na kuupamba moyo wako kwa ibada na kuwatendea wema watu wengine. Matokea yake vitu vingine vyote kinyume na Mwenyezi Mungu vinakuwa havina umuhimu ndani ya moyo.

*Zahid* au mwenye zuhd ni yule mtu ambaye anajikinga na hata vitu vyenye kutia wasiwasi tu na hivyo kuepukana na madhambi, na pia ni yule mtu ambaye kutokana na mapenzi yake na hofu aliyo nayo juu ya Mwenyezi Mungu anazitumia neema za dunia hii katika njia za wema.

Watu wema katika Uislamu daima wamekuwa wakionyesha utumishi wa hali ya juu kwa Mwenyezi Mungu ndani ya nyoyo zao, na wamekuwa wakiishi kwa *zuhd* na istighna, tabia ambazo

67. Ahmad, II, 389
68. Bayhaqi, Kitabu az-Zuhd, Beirut 1996, II 88.

zilidhihirisha kujitenga kwao na dunia na raha zake. Hivyo katika dunia yao kila kitu kimepoteza thamani mbele yao isipokuwa mapenzi na hofu juu ya Mwenyezi Mungu. Kwa namna hii tunaona kuwa *zuhd* ni kama ngao imara ambayo inawakinga dhidi ya mapenzi na uroho wa vitu vya dunia hii, vitu ambavyo humpelekea mtu kusahau maisha ya kesho akhera.

Dunia hii yenye kudanganya pamoja na vivutio vyake na raha zake vimewafanya watu wengi waikumbatie. Kinachotakiwa kwa watu ni kuiweka dunia nje ya nyoyo zao na kunufaika nayo kwa kuifanya iwe sehemu ya kuchuma kwa ajili ya kesho akhera. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameyaelezea maisha ya dunia hii pamoja na mapambo yake kama ifuatavyo:

**"Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua. Na akhera kuna adhabu kali na maghfira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu"** (Al-Hadid, 57:20).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Thamani ya dunia hii ikilinganishwa na thamani ya akhera ni kana kwamba mmoja wenu amezamisha kidole chake ndani ya bahari na kisha akakitoa na kuangalia ni kiasi gani cha maji ilichotoka nacho"* (Muslim, Jannah 55).

*"Yeyote atakayependelea zaidi maisha ya akhera, Mwenyezi Mungu atampandisha daraja na atamuongoza katika mambo yake na watu wote watamheshimu na kumfuata. Lakini yeyote ambaye ataweka malengo yake katika hii dunia, Mwenyezi Mungu atamuwekea umasikini kati ya macho yake mawili na atamvurugia*

*mambo yake. Matokeo yake hakuna atakachopata katika dunia hii zaidi ya kile alichopangiwa".* (Tirmidhi, Qiyamah, 30/2465).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amewapa watu katika umma wake ushauri ufuatao unaohusu kujiweka mbali na dunia na kushukuru juu ya neema ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia:

*"Waangalie wale ambao hali zao ni mbaya kuliko yako, na usiwaangalie wale ambao hali zao ni bora kuliko yako. Jambo hili ni bora kwako kwani litakupelekea kutodharau neema ambazo Mwenyezi Mungu amekujaalia"* (Muslim, Zuhd, 9).

Wakati mwingine *zuhd* na *taqwa,* sifa ambazo ni alama za wale walioiga njia ya maisha ya Mitume katika kuishi kwao na katika matendo yao, watu wengi wanashindwa kuzielewa. Watu wengi wanajua kuwa zuhd na taqwa ni kujitoa kabisa katika neema na utajiri wa dunia. Wakati kuweza kutekeleza majukumu ya kiuchumi ni aina moja wapo ya ibada yenye kupendeza mbele ya Mwenyezi Mungu. Neno *'infaq'* au kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu kumetajwa mara nyingi ndani ya Qur'an tukufu. Nguzo mbili za Uislamu, *zakat* na *hajj*, zitaweza kutekeleza tu pale mtu atakapokuwa na amefikisha '*nisab*' (kiwango cha chini ambacho mtu akifikisha atawajibika kutoa *zakat*). Hadith ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuwa 'mtu anayetoa ni bora kuliko mtu anayepokea' pia inamshawishi mtu kuwa na angalau kiwango cha chini au *nisab* ili kuweza kutekeleza matendo haya ya kiibada. Kwa namna hii *zuhd* haiwezi kwenda kinyume na mambo ambayo dini imeyapendekeza.

Sharti la *zuhd* na *taqwa* ni kujiweka mbali na tamaa za neema za kidunia pale utakapohisi kuwa zinaweza kukupelekea kuangukia kwenye madhambi au kupuuzia ibada. Hata hivyo hii istighna ni kitu kinachotakiwa kuwa ndani ya moyo na sio kuonekana katika matendo ya mtu au katika muonekano wake wa nje. Inamaanisha kuwa *zuhd* na *taqwa* vinahusiana na kushiriki katika

kuzitumia neema za duniani bila ya kuupelekea moyo kuzama katika neema hizo. Kwa mtizamo huu *zuhd* sio umasikini bali ni hali ya moyo ambayo kila muumini hana budi kuwa nayo, akiwa ni tajiri au masikini. Ikiwa mtu anaishi katika umasikini wa hali ya juu kutokana na makadirio ya Mwenyezi Mungu lakini moyo wake ukaegemea kwenye dunia, hawezi kuchukuliwa kama mtu mwenye *zuhd* na *istighna*. *Zuhd* na *istighna* hazimaanishi kuwa mtu analazimika kuridhika na kidogo alicho nacho kwa kigezo kuwa ndicho kiasi alichokadiriwa na Mwenyezi Mungu, lakini zinamaanisha kuuchunga moyo wako kwa namna yoyote ile usije ukawa mtumwa wa dunia.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ameielezea zuhd vizuri zaidi kama ifuatavyo:

"*Zuhd* ya hapa duniani sio kuhalalisha vile vilivyoharamishwa wala kujiweka mbali na mali na utajiri. Bali *zuhd* ya hapa duniani ni kuitegemea mali iliyopo kwa Mwenyezi Mungu kuliko kutegemea ile iliyopo mikononi mwako; pia ni kutarajia malipo makubwa kutokana na mtihani wowote utakaokupata" (Tirmidhi, Zuhd, 29/2340).

***Matukio ya wema***

Iyas ibn Sa'labe ﵁ anasimulia:

"Siku moja maswahaba walikuwa wanajadiliana juu ya dunia karibu na Mtume. Kutokana na majadiliano yao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaambia:

*"Je hamsikii? Je hamsikii? Kwa kawaida kuishi kama hivyo kunatokana na imani ya mtu; Kwa kawaida kuishi kama hivyo kunatokana na imani ya mtu"* (Abu Dawud, Tarajjul, 1/4161; Ibn Majah, Zuhd 4).

Yani kuishi kama *zahid,* kwa unyenyekevu na kuridhika...

❁

Kutokana na masimulizi ya Aisha, siku moja mwanamke mmoja wa kianswar alikuja kwake na kuona kuwa kitanda cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakikuwa na chochote zaidi ya godoro jembamba lililokuwa limekunjwa. Kisha akakimbia nyumbani kwake upesi na kurudi na godoro lililojazwa sufi. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoona kuwa kitanda chake kimebadilika hakufurahishwa na jambo lile akamwambia Aisha:

*"Ewe Aisha! Lirudishe godoro hili kwa mwenyewe. Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa kama ningelipenda Mwenyezi Mungu angeliifanya milima ya dhahabu na fedha ije kwa ajili yangu na kuitiisha kwangu"* (Ahmad, Kitabu az Zuhd, uk 30).

❁

Abdullah ibn Mas'ud رضي الله عنه anasimulia:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amelala juu ya mkeka. Alipoamka ule mkeka ulikuwa umeacha alama katika mwili wake. Tukamwambia:

"Ewe Mtume. Si tukuletee godoro?" akajibu:

*"Nina kipi cha kufanya na dunia hii? Mimi ni kama msafiri ndani ya dunia hii, msafiri ambaye anapumzika chini ya mti na kisha anaendelea na safari yake na kuuacha ule mti nyuma yake"* (Tirmidhi, Zuhd, 44/2377)

❁

Siku moja Abu Huraira رضي الله عنه alikuwa anatembea akakutana na kundi la watu ambao mbele yao kulikuwa na nyama ya kondoo wa kuchoma. Watu wale walimkaribisha lakini yeye hakutaka kula hivyo akawaambia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliondoka katika dunia hii bila ya hata kipande cha mkate wa shairi tumboni mwake" (Bukhari, At'ima, 23)

❁

Siku moja Sahl ibn Sa'd ؓ alisema:

"Tokea siku aliyopewa utume mpaka siku anakufa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuwahi kuuona unga uliochekechwa". Akaulizwa:

"Je wakati wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ watu walikuwa wakitumia unga wa kuchekecha?"

Sahl akajibu:

"Tokea siku atumwe kama Mtume mpaka siku alipokufa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kamwe hakuwahi kuliona chekeche".

Wakamuuliza:

"Sasa walikuwa wakichekecha vipi unga wa shairi?"

Sahl akajibu:

"Tulikuwa tukiiponda shairi na kuitawanya. Kisha tulikuwa tukipuliza kwa ajili ya kuondoa makapi; na kisha tulikuwa tukinyunyizia maji ule unga na kuukanda" (Bukhari, At'ima, 23).

❁

Anas ؓ anasimulia kuwa:

"Siku moja bidhaa kutoka Bahrain zililetwa kwa Mtume. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

"Zileteni na mziingize msikitini".

Wakati ule mali ilikuwa kubwa kuliko zile zilizokuwa zikiletwa kwake katika nyakati nyingine. Alienda kuswali bila ya hata kuiangalia. Baada ya kumaliza kuswali alisimama mbele ya mali ile na kuigawanya kwa kila mtu aliyemuona pale...Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuondoka sehemu ile mpaka alipohakikisha kuwa ameigawanya mali yote na hakuna hata dirham moja iliyokuwa imebakia. (Bukhari, Salat 42, Jizya 4, Jihad 172)

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaonya baadhi ya wake zake waliokuwa wameegemea kwenye mapambo ya dunia kwa aya kutoka ndani ya Qur'an. Aliwaambia wachague kati ya mapambo ya hii dunia au Mwenyezi Mungu, Mjumbe wake na maisha ya akhera. Kisha akajitenga nao kwa muda wa mwezi mmoja. Baada ya tukio hili lililojulikana kama 'Ila' aya ifuatayo ilishushwa:

**"Ewe Nabii! Waambie wake zako: Ikiwa mnataka maisha ya dunia na pambo lake, basi njooni, nitakupeni kitoka nyumba, na kukuacheni mwachano mzuri"** (Ahzab, 33:28-29).

Kutokana na jambo hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaanza na Aisha kwa kumwambia yafuatayo:

*"Nataka kuzungumza na wewe kuhusu jambo fulani, lakini usiharakishe kunipa jibu. Unaweza kunijibu baada ya kuiona familia yako"*. Aisha akamuuliza:

"Ni jambo gani hilo ewe Mtume? Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamsomea aya iliyotajwa hapo juu. Kisha Aisha akajibu upesi:

"Je nikaione familia yangu katika jambo linalohusu kipaumbele changu kwako? Kamwe siwezi! Ninamchagua Mwenyezi Mungu, Mjumbe wake na maisha ya akhera". Wake wengine wa

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ walijibu hivi hivi. (Muslim, Talaq, 29)

❁

Mtumwa aliyeachwa huru na Mtume, Thawban ؓ anasimulia:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kila alipotaka kuondoka kwa ajili ya safari alikuwa akimuaga binti yake Fatma ؓ baada ya kuwaaga watu wote. Na mtu wa kwanza kumuona baada kurudi alikuwa ni Fatma. Ilikuwa ni wakati ambao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amerejea kutoka katika moja ya safari zake. Fatma alikuwa amefunga pazia mlangoni mwake na alikuwa amewavalisha bangili watoto wake wawili Hasan na Hussein. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawa amewasili kwenye nyumba ya Fatma lakini hakuingia ndani. Fatma akagundua kuwa sababu iliyomfanya Mtume

asiingie ndani ni kile alichokiona. Upesi akalivuta na kuliondoa lile pazia (lililokuwa limepambwa) na kuwavua watoto wake zile bangili. Akatoa bangili moja iwe yao wote wawili. Hasan na Hussein wakaanza

kulia na kwenda kwa Mtume. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akazichukua zile bangili zote na kumwambia Sawban:

*"Ewe Sawban. Chukua hizi bangili na umpelekee fulani na fulani. Hasan na Hussein ni miongoni mwa Ahlul Bayt*[69]*. Sitaki watumie mapambo haya ya hii dunia, mapambo yao ni yale ambayo Mwenyezi Mungu atawapa (kesho akhera). Ewe Sawban nenda na ununue mkufu uliotengenezwa kwa mfupa kwa ajili ya Fatma na bangili mbili zilizotengenezwa kwa mfupa pia kwa ajili ya watoto wake".* (Abu Dawud, Tarajjul, 21/4213).

69. Watu katika familia ya Mjumbe wa Allah ﷺ (Maelezo ya mfasiri).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitaka watu wa Ahlul Bayt waishi maisha ya kawaida, ya unyenyekevu wa hali ya juu na kujitenga na mapambo ya dunia ili wawe mfano kwa umma wake.

❁

Abu Dharr ؓ anasimulia:

“Siku moja tulikuwa tunatembea pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika kitongoji cha Harra ndani ya Madina, tukauona mlima wa Uhud. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*“Ewe Abu Dharr!”* Na mimi nikaitikia:

“Ndio ewe Mtume. Ninakusikiliza”. Akajibu:

*“Kama ningelikuwa na dhahabu mfano wa mlima huu hapa wa Uhud, kusingelinifurahisha kabisa. Sitaki siku tatu zipite nikiwa nina fedha bila ya kulipa madeni hata kama dinar moja- Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaonyeshea kitendo cha kutoa kwa kunyoosha mkono wake mbele yake, kuliani kwake, kushotoni mwake na nyuma yake- Ningelipenda kukigawa kile nilichokuwa nacho na kuwapa waja wa Mwenyezi Mungu”.*

Kisha akatembea mbele kidogo na kusema:

*“Wale wenye mali nyingi hapa duniani watakuwa na malipo madogo kesho akhera. Isipokuwa kwa wale wanaotoa kama hivi kwa kuwapa wale walio kuliani mwao, kushotoni mwao na nyuma yao. Lakini kwa hakika watu hao ni wachache kiasi gani”* (Bukhari, Istikraz 3, Riqaq 14; Muslim, Zakat 32)

❁

Siku moja mtu mmoja alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kusema:

“Ewe Mtume. Naomba uniambie amali ambayo nikiitenda Mwenyezi Mungu atanipenda na watu pia watanipenda”.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

*“Jiweke mbali na raha za dunia, wala usiigombanie Mwenyezi Mungu atakupenda na jiweke mbali na vilivyo kwa watu na wala usivionee wivu hapo watu watakupenda”* (Ibn Majah, Zuhd, 1)

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alienda sokoni. Alifuatana na maswahaba. Njiani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliona mzoga wa ndama na huku masikio yake yamekatwa. Akaushika masikio na kusema:

*“Ni nani kati yenu atakuwa tayari kuununua mzoga huu kwa dirham moja?”* Maswahaba zake wakajibu:

“Tusingelikuwa tayari kumchukua hata kwa bei ndogo kuliko hiyo, kwani hatakuwa na manufaa kwetu”.

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawauliza:

*“Je kuna yeyote miongoni mwenu atakubali kuuchukua bure?”* Wakajibu:

“Tunaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa hata kama angelikuwa mzima basi angelikuwa na kasoro kwani hana masikio. Sasa ana faida gani sasa hivi wakati ameshakufa?” Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*“Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu dunia hii ina thamani ndogo kuliko huu mzoga wa mbuzi mnaououna mbele yenu”* (Muslim, Zuhd, 2)

❁

Kutokana na masimulizi ya Amr ibn Awf ﷺ, siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimtuma Abu Ubaydah ibn Jarrah ﷺ kwenda Bahrain kukusanya *jizya*[70]. Abu Ubaydah ﷺ akarudi kutoka Bahrain pamoja na fedha za *jizya*. Answar waliposikia kuwa Abu Ubaydah ﷺ amerudi wakakusanyika pamoja kuswali swala ya alfajiri pamoja na Mtume. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomaliza swala na kunyanyuka kwa ajili ya kuondoka wale Answar wakamsogelea. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipowaona katika hali hii alitabasamu na kusema:

*"Naona mmesikia kuwa Abu Ubaydah amerejea na fedha kutoka Bahrain".*

"Ndio ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu" wakajibu:

*"Pendeni kuwaridhisha wengine na fanyeni vitu ambavyo vitawaridhisha wengine. Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa sihofii umasikini juu yenu. Bali ninahofia kuwa dunia itawekwa juu yenu kama ilivyowekwa juu wale waliokuwa kabla yenu, na mtaanza kuipigania kama ilivyokuwa kwa wale waliokuwa kabla yenu. Na ninahofia kuwa dunia hii itawaangamiza kama ilivyowaangamiza wale waliokuwa kabla yenu"* (Bukhari, Riqaq 7; Muslim, Zuhd 6)

❁

Mfano ufuatao una somo zuri katika kuonyesha hatari ya kuegemea katika dunia na kusahau akhera:

Katika kipindi cha utawala wa Muawiyya jeshi la kiislamu likiongozwa na Abdurrahman, mtoto wa Khalid ibn Walid, liliondoka kwa matumaini ya kwenda kuitwaa Istanbul kama zilivyokuwa habari njema zilizotolewa na Mtume. Wakati wa Byzantine wanapigania nyuma na ngome yao, akajitokeza mtu mmoja

70. *Jizya* ni kodi ambayo makafiri wanalazima kulipa kwa ajili ya kulindwa na waislamu (Maelezo ya mfasiri).

miongoni mwa Answar na kukimbiza farasi wake kuelekea katikati ya jeshi la Byzantine. Kwa mshangao na kwa kuikumbuka aya isemayo: "Msizitie nafsi zenu katika maangamizi", waumini walioliona hili wakaanza kusema:

"La ilaha Illallah! Muangalieni. Anajipeleka mwenyewe katika maangamizi". Kutokana na jambo hili Abu Ayyub Al-Ansari akasema:

"Enyi waumini, isieleweke vibaya. Aya hii ilishushwa kwa ajili yetu sisi Answar. Pindi Mwenyezi Mungu alipomsaidia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wake kwa kuifanya dini yake iongoze sisi tulisema: "Ngoja sasa tukae na kuzisimamia mali zetu". Kutokana na jambo hili Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akamshushia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aya ifuatayo:

**"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. Na fanyeni wema. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema"** (Al-Baqara,2:195).

Kilichomaanishwa katika aya hii juu ya maneno "msijipeleke katika maangamizi" ni kutoweka juhudi yako yote katika kushughulikia mali za kidunia kama vile mabustani na mazao na kupuuzia na kuacha juhudi zako katika njia ya Mwenyezi Mungu".

Abu Ayyub Al-Ansari ؓ ambaye alilizingatia onyo hili kwa moyo wake wote kamwe hakuwahi kuziegemea starehe na raha za hii dunia. Kamwe hakuacha juhudi zake katika kumtumikia Mwenyezi Mungu na alikuja kuuawa kama shahidi karibu na ngome moja wapo ya Byzantine na akazikwa katika mji wa Ayyub ambao umebeba jina lake mpaka leo hii. (Angalia Abu Dawud, Jihad, 22/2512; Tirmidhi, Tafsir, 2/2972)

Nyumba iliyobarikiwa ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ilikuwa ya kawaida mno. Hasan Basri ambaye mama yake alikuwa mtumishi wa Ummu Salama, mke wa Mtume, alimalizia utoto wake katika nyumba hii na alielezea namna alivyokuwa anaweza kugusa dari la chumba cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakati alipokuwa mdogo[71]. Kutokana na haya ikajulikana kuwa vyumba vyake havikuwa virefu sana. Milango ya nyumba ya Mtume wetu ilitengenezwa kwa kitambaa gandamizo cheusi.[72]

Siku moja Said ibn Musayyab ambaye ni mmoja wa maimamu wakubwa katika kipindi cha Tabi'een alitoa masikitiko yake makubwa juu ya kuvunjwa kwa vyumba hivi kwa ajili ya kupanua msikiti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakati wa utawala wa Umayya:

"Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa ingelikuwa vizuri vyumba hivi vikaachwa kama vilivyokuwa. Kwa namna hii vizazi vinavyokuja na wale wanaokuja kutembelea eneo hili wangeliweza kuona namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyotosheka na kidogo na pia wasingelejaribu kupupia mali na kujivuna nazo" (Ibn Sa'd, I, 499-500).

Kuishi kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika nyumba ndogo vile haikuwa kwa sababu ya umasikini bali ni kuonyesha namna asivyokuwa ameipa hii dunia umuhimu wowote. Kama angelijilimbikizia mali hizi na kuacha kuzigawa kwa wengine angeliweza kujenga makasri makubwa makubwa. Lakini yeye alitaka kidogo na kuishi katika maisha ya unyenyekevu na hakuwa na utulivu mpaka pale alipotoa kile alichokipata. Haya ni kutokana na kufunikwa na sifa ya Mwenyezi Mungu ya '*Al-Rahman*' (Mwingi wa rehma).

❁

71. Ibn Sa'd, VII, 161; Zuheyli, I, 248.
72. Ibn Sa'd, I, 499

Nabii Suleiman ﷺ alijichukulia kuwa mtu masikini kwa sababu alifuta moyoni mwake mapenzi ya mali na utajiri. Kila alipokuwa anaamka asubuhi alikuwa anaenda kwa watu masikini na kukaa nao kwa unyenyekevu mkubwa, na alikuwa akisema:

"Inafaa kwa mtu masikini kukaa na masikini mwenzake".

❁

Kutokana na masimulizi mbalimbali tunafahamishwa kuwa nabii Nuhu ﷺ alipokaribia kufa aliulizwa:

"Ewe nabii uliyeishi kwa muda mrefu, umeionaje hii dunia?" Nuhu akajibu:

"Nimeona hii dunia ni nyumba yenye milango miwili. Niliingia kwenye mlango mmoja na kutokea kwenye mwingine" (Ibn Athir, Al-Kamil, I, 73).

Nabii Nuhu alijijengea kibanda kwa kutumia mianzi. Pindi alipoambiwa:

"Kwa nini usingelijenga nyumba nzuri zaidi ya hiyo", akajibu:

"Kwa mtu atakayekufa hii nyumba ni zaidi ya kutosha". (Abu Nuaym, Hilya, VIII, 145)

❁

Jabir ibn Abdullah ﷺ anasimulia:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimchagua Abu Ubaydah ﷺ kuwa kamanda wetu na kisha alitutuma tuende kukutana na msafara wa maquraysh. Alitupa mfuko wa tende kwa ajili ya kula. Hakupata kingine cha kutupatia. Abu Ubaydah alikuwa akitugawia tende mmoja baada ya mwingine. Mtu mmoja aliyeyasikia haya aliuliza:

"Mliwezaje kuishi kwa tende pekee?"

Jabir akajibu:

“Tulikuwa tukifyonza zile tende kama mtoto anavyonyonya maziwa ya mama yake, kisha tulikuwa tukinywa maji na kutosheka kwa siku hiyo mpaka usiku. Tulikuwa tukitikisa majani juu ya miti kwa fimbo zetu na kisha kuyalowesha kwa maji na kuyala” (Muslim, Sayd, 17).

Ingawa maswahaba waliobarikiwa hawakuwa na hata vitu vya msingi katika dunia hii, lakini kamwe hawakuwahi kulalamika juu ya hili. Na pia hawakurudi nyuma katika kuipigania dini ya Mwenyezi Mungu.

❁

Siku moja Abu Bakr ﷺ alikaribishwa kunywa asali. Hata hivyo alipokaribia kunywa alianza kulia. Wale waliokuwa karibu naye hawakuweza kuvumilia hivyo nao wakaanza kulia. Abu Bakr ﷺ alipoulizwa sababu ya kulia kwake alijibu:

“Siku moja nilikuwa pamoja na Mtume. Mara akaanza kusema *“kaa mbali na mimi, kaa mbali na mimi”* na huku anajaribu kukisukumia kitu mbali na yeye. Hata hivyo sikuweza kuona kitu chochote. Nilipotaka kujua kuna kitu gani kinaendelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*“Nilionyeshwa dunia na mapambo yake yote, kisha nikaiambia ikae mbali na mimi. Ikasogea nyuma lakini ikasema: “Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa ingawa imeweza kuniepuka na kunusuriwa kutokana na mimi lakini wale watakaokuja baadae hawataweza kunikimbia”.*

Abu Bakr ﷺ aliendelea:

“Kutokana na maneno yale nikaanza kulia kwa kuhofia kuwa ninaweza kuangukia kwenye mapenzi ya kuipenda dunia” (Abu Nuaym, Hilya, I, 30-31)

Abu Bakr ﷺ aliishi maisha ya kawaida mno katika kipindi cha ukhalifa wake. Wakati akiwa juu ya kitanda cha mauti aliacha maelekezo kuwa kipande chake cha ardhi kiuzwe ili alipiwe ule mshahara aliokuwa akipokea kutoka kwenye hazina ya dola wakati alipokuwa khalifa. (Ibn Athir, Al-Kamil, II, 428-9)

❁

Pia wakati Abu Bakr ﷺ yupo juu ya kitanda chake cha mauti aliacha maelekezo kwa binti yake Aisha ﷺ kuwa ampatie Omar ﷺ ngamia wao aliyekuwa anawatolea maziwa, chombo alichokuwa anakitumia kulowekea nguo zake kwa rangi na joho lake la pamba alilokuwa akivaa. Sababu yake ya kufanya hivi ni kuwa vitu hivi alivipata wakati akiwa anasimamia mambo ya waislamu. Baada ya kifo cha baba yake, Aisha ﷺ akavitoa vile vitu kwa khalifa mpya ambaye ni Omar ﷺ. Baada ya Omar ﷺ kuvichukua akasema:

"Abu Bakr! Rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako. Umewaacha kwa njia panda wale waliokuja baada yako" (Ahmad, Az Zuhd, uk 110-111; Suyuti, Tarih al Khulefa, Misri 1969, uk 78-9).

Katika kipindi cha utawala wa Omar ﷺ ardhi za Siria, Palestina na Misri zilitwaliwa na Iran nayo ikashirikishwa kwenye mipaka ya dola ya kiislamu. Hazina za Byzantine na Iran zikaanza kumiminika ndani ya Madina ambayo ilikuwa ndio kitovu cha Uislamu. Maisha ya waumini yakaanza kuboreka. Hata hivyo moyo wa khalifa wa waislamu, Omar ﷺ ulibakia katika hali ya kujitenga na hali hii na licha ya maendeleo ya dola na wingi wa hazina za dola lakini aliendelea kuhutubia waislamu hali ya kuwa amevaa joho lenye viraka. Alikuwa analazimika kuingia kwenye madeni mara kwa mara na kuishi katika hali ya ugumu. Haya ni kwa sababu alikuwa akichukua kiwango cha chini cha mshahara kutoka kwenye hazina na kwake kiwango hiki kilikuwa kinatosha kabisa.

Wale watu wakubwa katika maswahaba hawakuweza kuvumilia hali ile, hivyo wakafikiria kuongeza mshahara wa khalifa. Lakini walisita kulizungumzia jambo hili mbele ya Omar ﷺ hivyo wakaamua kumfuata binti yake na ambaye ni mke wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyeitwa Hafsa ﷺ. Walimuomba alipeleke jambo hili kwa baba yake bila ya kutaja majina yao. Hafsa ﷺ akalipeleka suala hili mbele ya baba yake bila ya kutaja majina yao. Kwa kuwa Omar ﷺ alishuhudia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akikaa na njaa[73] kwa masiku bila ya kupata hata tende moja kwa ajili ya kuiweka tumboni mwake, akamuuliza binti yake:

"Binti yangu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akivaa vipi na kula vipi?"

"Kile kilichokuwa cha ulazima" alijibu.

Omar akaendelea:

"Rafiki zangu wawili (Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na Abu Bakr) na mimi ni kama wasafiri watatu ambao wanasafiri katika njia moja. Wa kwanza wetu (Mtume) amefika safari yake. Wa pili (Omar) huku akifuata njia ile ile ameenda kuungana na yule wa kwanza. Na kama wa tatu wao ningelipenda kuwafikia marafiki zangu. Kama nitaenda na mizigo mingi sitaweza kuwafikia, au wewe hutaki niwe msafiri wa tatu katika njia hii?"[74]

❁

Siku moja Abu Dharr Al-Ghifari ﷺ ambaye alipenda kuishi maisha ya kawaida, ya unyenyekevu na kuwa mbali na hanasa, alipewa dinar elfu moja kutoka kwenye hazina ya dola. Lakini alitumia kiasi kidogo mno cha fedha hizi na kiasi kilichobaki alikigawa kwa masikini" (Abu Nuaym, Hilya, I, 163).

73. Angalia Muslim, Zuhd, 36
74. Angalia Ahmad, Zuhd, p 125; Shahbenderzade Ahmad Hilmi, Tar ih' i Islam, I, 367.

Swahaba huyu ambaye alikuwa akisema kuwa hesabu ya mtu aliye na dirham mbili itakuwa ngumu kuliko ya yule atakayekuwa na dirham moja. Siku moja alirudisha dinar mia tatu ambazo alitumiwa na gavana wa Damascus huku akisema:

"Je gavana hakuweza kumpata mtu aliyekuwa na shida kuliko mimi? Tuna nyumba ya kujihifadhi, kondoo tunayenufaika kutoka kwake na mtumishi wa kutuhudumia. Ninahofia kuwa na zaidi ya hivi" (Ahmad, Zuhd, uk 147)

❁

Ari ya imani baada ya kipindi cha maswahaba ilikuwa imeifunika dunia kiasi kwamba jeshi la Tariq ibn Ziyad lililokuwa na watu elfu tano liliweza kulishinda jeshi la wahispania lililokuwa na watu 90000. Tariq aliweka mguu wake juu ya hazina ya mfalme na kujiambia mwenyewe:

"Tariq! Jana ulikuwa mtumwa ukiwa na mnyororo shingoni; kisha ikafika siku ambayo Mwenyezi Mungu akakuweka huru. Kisha ukawa kamanda wa jeshi. Leo hii unajikuta kuwa mmeitwaa Andalusia na umesimama katika kasri la mfalme. Lifahamu jambo hili vizuri na usisahau kuwa kesho utajikuta upo mbele ya Mwenyezi Mungu".

Ni aina gani ya mafunzo hii ambayo inajenga imani ya mja na kumpandisha mpaka kwenye kilele cha wema. Yanaufanya moyo wake uache kuegemea kwenye neema za hii dunia na kumfanya aishi kwa kujiwajibisha mwenyewe.

❁

Siku moja mtu mmoja mwema na pia mwanafunzi wa Shaykh Naqshiband, Muhammad Parisa wakati anaelekea kuhiji alienda kwa kijana mmoja mwema ambaye alikuwa anajishughulisha na kukopesha watu fedha ndani ya Baghdad. Alihisi huzuni akifikiria

kuwa kijana yule wakati wote anajishughulisha na starehe za dunia kwa kutumia muda mwingi katika biashara. Alijifikiria kichwani mwake:

"Bahati mbaya iliyoje. Katika umri ambao anaweza kutekeleza ibada kwa wingi lakini yeye amezama katika biashara za kidunia".

Alipoenda kumchunguza alikuta kuwa moyo wa kijana huyu ulikuwa umeshikama na Mwenyezi Mungu na hapo akastaajabishwa. Wakati huu akajifikiria mwenyewe kichwani na kumsifu yule kijana kwa kusema:

"*Mashallah.* Mkono wake uko katika faida na bado moyo wake uko pamoja na kipenzi cha kweli.

Hali hii ndiyo inayojulikana kama *'halvet der encumen'*, yani kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu wakati umejumuika na watu, kuweza kumfikiria yeye tu na kuweza kuishi katika hali ya umoja ndani ya mkusanyiko.

Pindi Muhammad Parisa alipowasili Makka alikutana na mzee mmoja mwenye ndevu nyeupe ambaye alilipenda mno lile shuka la Al-Kaaba akiwa ananung'ika huku analia. Kwa mara ya kwanza alipoangalia muonekano wa nje wa yule mzee na namna alivyokuwa anamlilia Mwenyezi Mungu kwa namna yenye mguso, alifikiria katika nafsi yake:

"Lau kama ningeliweza kulia kama vile na kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu", akamuonea wivu yule mzee.

Pindi alipouchunguza moyo wake aligundua kuwa kulia kwake kote na maombi yake yalikuwa ni kwa ajili ya maslahi ya dunia. Mara moyo wake laini ukahuzunika.

Kwa kifupi ni kuwa kwenda kinyume na dunia sio katika kipindi cha umasikini tu bali ni tabia ya moyo ambayo haina budi

kubakia wakati wote. Jambo la msingi ni kuweza kuendelea kutafuta manufaa ya kidunia bila ya kupuuzia akhera yako.

❁

Hali ifuatayo ya Jalâluddin Al-Rumi ni yenye kuvutia, kwani inaonyesha ni kwa namna gani aliweza kujipamba na sifa ya *zuhd* aliyokuwa nayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutokana na mapenzi yake kwake.

Kila alipokuwa akirudi nyumbani kwake alikuwa akiuliza: "leo tuna nini cha kula?" pindi anapopokea jibu kuwa: "Hakuna kitu", alikuwa akifurahi na kusema "Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu. Leo nyumba yetu ni kama nyumba ya Mtume". Katika hali yoyote ile Rumi alikuwa akikataa sadaka na pia alikuwa akiwashawishi wanafunzi wake pia wasichukue, badala yake aliwashawishi kufanya kazi".[75]

❁

Siku moja Malik ibn Dinar alimuona kwenye ndoto Rafi' ambaye ni mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu. Alikuwa hana kitu kichwani na alikuwa anatembea peku. Alimuuliza:

"Unaenda wapi?"

Rafi' akajibu: "Namshukuru Mwenyezi Mungu kuwa nimeweza kutoroka jela".

Asubihi yake upesi Malik ibn Dinar akaenda kwenye nyumba ya Rafi' ambapo alimkuta ameshafariki.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Hii dunia ni jela ya muumini na pepo ya kafiri"* (Muslim, Zuhd, 1)

❁

75. Ali Nihat Tarlan, "Mawlana," Istanbul 1974, uk 29.

Baada ya Sultani Murad Han wa pili kukiacha kiti chake cha enzi na kumpa Manisa kwa ajili ya kutenga muda mwingi zaidi kwa ajili ya ibada aliandika shairi ambalo liliashiria kuwa alikuwa akitekeleza majukumu yake kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu pekee:

*Acha twende tukamkumbuke Mwenyezi Mungu angalau kwa siku moja au mbili. Hatukuja hapa duniani kwa ajili ya kuimiliki.*

❁

Mtu mwingine mwerevu ambaye alijipamba na tabia ya kuishi bila ya kuzipenda sana mali na utajiri na nyadhifa za kidunia na ambaye alikubali neema za hapa duniani lakini si kwa ajili ya kutosheleza nafsi yake bali kuzitumia kwa ajili ya kuwahudumia waja wa Mwenyezi Mungu, alikuwa ni Yavuz Sultan Selim Han. Siku moja aliwahutubia wale waliokuwa chini yake kama ifuatavyo:

"Kama lengo lenu ni kuendelea na uasi basi nifahamisheni na mimi mara moja nitajitoa mwenyewe serikalini. Niliupokea usultani huu kutoka kwa baba yangu kwa lengo pekee la kuutumikia Uislamu na nimewatoa muhanga kaka yangu na watoto wa mama yangu kwa ajili ya mapinduzi ya hii dunia. Niliweka makubaliano na nyinyi (bay'ah) na nyinyi mlikubali. Niliacha usingizi wangu, starehe zangu na utulivu wa nafsi katika juhudi zangu za kuijenga hii dini. Kama lengo lenu si kuudhoofisha Uislamu basi na mimi pia sina tamaa yoyote juu ya huu usultani".

❁

Kwa kifupi ni kwamba mja wa Mwenyezi Mungu hana budi kuelekea katika kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muumba wa vitu vyote. Pale moyo unapojitiisha kwa Mwenyezi Mungu hali ya *zuhd* inajidhihirisha kwa mja. Na pale *zuhd* inapojidhirisha kwa mja basi mali zote na utajiri wake vinakuwa havina

thamani mbele ya nafsi yake na vitu hivi vitapata thamani pale vitakapotumika ndani ya misingi ya Mwenyezi Mungu, yani itakapotolewa sadaka. Kwa namna hii itakuwa imerudi kwa mwenye kustahiki. Haya ni kwa sababu moyo hapa unakuwa umepambwa kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na amali njema, na amali hizi ambazo zinapendwa na kipenzi chake zinaanza kuipa nafsi yake raha ya hali ya juu.

**15. Subira na ushupavu**

*Swabr* (subira) ni pale mtu anapobakia kama alivyokuwa pindi kunapotokea mabadiliko katika mwili wake au nafsi yake na kubakia mtulivu, kuvumilia mitihani, kushindana na maumivu, kukabiliana na mahangaiko na magumu kwa upole, na kuzidhibiti hisia za kibinadamu ziwe ndani ya mipaka ya dini.

*Matanah* (ushupavu) ni pale mtu anapokabiliana na lolote linalompata kwa uimara, uvumilivu na bila ya kutetereka.

Subira ndio msingi wa tabia njema. Subira ni nusu ya imani na ufunguo wa furaha na neema. Subira ni sifa tukufu ambayo inamuunganisha mtu na neema za peponi. Subira ni kujivika amani bila ya kujiharibia uwiano wake pale utakapofikwa na matukio ambayo yatakuhuzunisha na kukusababishia maumivu. Subira ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu.

Mitume mbalimbali na watu wema walikuwa ni mifano ya kuigwa katika kusubiri na jambo hili liliwapelekea kupata msaada wa Mwenyezi Mungu. Wale watakaoweza kuvumilia maumivu ya subira watapata radhi za Mwenyezi Mungu na kuzawadiwa maisha ya milele ya peponi.

Kutafakari juu ya fadhila zilizopo katika maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu, kutafakari hekima zake na mali-

po yatakayopatikana kwa kuyafuata vilivyo kutapelekea kusubiri kuwe rahisi kwa mtu.

Sharti la kwanza la subira ni kuionyesha pale unapokutana na tukio linalolazimu kusubiri. Subira isiyoonyeshwa katika wakati wa tukio kama hili hiyo haitakuwa na malipo makubwa.

Kwa sababu subira inajumuisha nyanja zote za tabia njema inapelekea kuwa na nafasi kubwa katika dini yetu. Subira imetajwa zaidi ya mara sabini ndani ya Qur'an tukufu. Subira imeamrishwa juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na umma wake wote:

**"Enyi mlio amini! Takeni msaada kwa subira na Sala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri"** (Al-Baqara, 2:153).

**"Enyi mlio amini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa"** (Al'i Imran, 3:200).

Katika sherehe ya aya hii Elmalili Muhammad Hamdi Yazir ana yafuatayo ya kusema:

"Moja ya majina matukufu ya Mwenyezi Mungu ni Al-Swabur au mwingi wa subira. Yeyote atakayekuwa na subira atakuwa amedhihirisha nguvu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ndani yake. Na hasa pale watu hawa wenye subira watakapokuja kwa pamoja na kutengeneza umma, hapo watapata msaada wa Mwenyezi Mungu katika mambo yao yote. Mwenyezi Mungu atakuwa rafiki yao na msimamizi wao daima".[76]

Wakati wote malipo makubwa huwafikia wale walioonyesha subira kwa kiwango cha juu na wakavumilia mitihani na majanga mbalimbali yanayowapata. Tunafahamishwa haya katika Qur'an tukufu kama ifuatavyo:

76. Angalia Elmalili M. Hamdi Yazar, "Hak Dini Kur'an Dili," Istanbul 1971, I, 546.

**"Sema: Enyi waja wangu mlio amini! Mcheni Mola wenu Mlezi. Wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema. Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni kunjufu. Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu"** (Az Zumar, 39:10).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametufahamisha aina mbalimbali za Subira na ubora wake kama ifuatavyo:

*"Subira iko katika hali tatu: Subira wakati wa majanga; subira katika kumtumikia Mwenyezi Mungu na subira katika kujizuia na kutenda dhambi"* (Suyuti, II, 42; Daylami, II, 416).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametufahamisha tena kuwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amesema:

*"Pale Mwenyezi Mungu atakapomchukua duniani rafiki wa mtu ambaye anampenda, muumini ambaye ataonyesha subira na kusubiria malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu malipo yake ni pepo"* (Bukhari, Riqaq, 6).

*"Kama mja wangu atasubiri pale nitakapomjaribu kwa kuyafanya macho yake mawili yasione, basi nitampa pepo kwa niaba ya macho yake"* (Bukhari, Marda, 7; Tirmidhi, Zuhd, 58).

Subira na kuwa na msimamo ni miongoni mwa misingi muhimu katika dini yetu. Na mtihani wa subira ni miongoni mwa mitihani migumu mno. Ndio maana Abu Bakr ؓ akasema:

"Ni bora kwangu kuwa na afya na kushukuru kuliko kupewa mtihani halafu nikatakiwa kusubiri".

***Matukio ya wema***

Maisha ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yamejaa mifano mingi mizuri ya subira. Tokea utoto wake mpaka alipokufa alikutana na mambo mengi yenye kuhuzunisha na kuleta majonzi makubwa. Alimpoteza baba yake hata kabla ya kuja hapa duniani.

Alimpoteza mama yake akiwa na umri wa miaka sita na babu yake katika umri wa miaka nane na katika mwaka wa kumi wa utume wake alifiwa na mjomba wake ambaye alikuwa akimlinda. Siku tatu baada ya hili alimpoteza msaidizi wake mkubwa, mke wake kipenzi, bibi Khadija. Alimuaga mkuu wa mashahidi ambaye ni mjomba wake Hamza katika vita vya Uhud, na watoto sita kati ya watoto wake saba na wajukuu wake wengi, baadhi wakiwa katika umri mdogo na baadhi wakubwa. Aliwazika maswahaba zake wengi kwa mikono yake mwenyewe. Alipatwa na mateso, matusi, kashfa, njaa na umasikini. Alikuwa akijeruhiwa katika vita na kupatwa na homa kali mno. Hata hivyo hakuna hata moja mion-goni mwa haya lililomfanya apunguze ushupavu au msimamo wake. Alikuwa mfano wa kuigwa katika subira na alikubalika katika nyanja zote.

Ni nani miongoni mwetu ameshawazika watoto sita mion-goni mwa watoto wetu? Ni nani miongoni mwetu amewahi kuwa-shika watoto wetu wachanga na wajukuu katika mikono yake na kuwaangalia wakipata tabu katika kupumua na mwishowe wakaf-ariki? Je kuna yeyote miongoni mwetu amewahi kushuhudia mwili dhalili wa mjomba wake ukichanwa katikati na ini lake kupigwa? Kwa kifupi ni kwamba je kuna mtu mwingine tofauti na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye amejaribiwa kwa mateso makub-wa kiasi hiki na akaonyesha subira na kukubaliana nayo yote?

❁

Wakati wa kipindi cha ujinga na katika kipindi cha hijja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiweka jukwaa na kulitumia kutangazia Uislamu. Matokeo yake alifikwa na madhila, magumu na mateso makubwa. Hata hivyo alikabiliana nayo kwa subira na bila ya kulalamika kamwe. Wakati fulani alilialika kwe-nye Uislamu kabila la watoto wa Amir ibn Sa'saa kama alivyokuwa akifanya kwa makabila mengine. Walimsikiliza Mjumbe wa Mwe-

nyezi Mungu ﷺ na kumuuliza maswali lakini hawakuingia kwenye Uislamu. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipowaacha na kwenda kupanda ngamia wake, mpagani mmoja aliyejulikana kwa jina la Bayhara alimchokoza yule ngamia na kumfanya anyanyuke na kumdondosha chini Mtume. Mwanamke mmoja wa kiislamu aliyeitwa Dubaa ibnti Amir ambaye aliliona tukio hili alilofanyiwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipiga kelele kwa kusema:

"Enyi kabila la Amir. Je hakuna yeyote miongoni mwenu aliyeuona ukatili huu aliofanyiwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na akafanya chochote kumsaidia, hata kwa kunionea aibu mimi?

Watu watatu ambao walikuwa ni watoto wa mjomba wao walinyanyuka na kumpiga Bayhara. Baada ya tukio hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaombea kama alama ya shukurani zake kwao:

*"Ewe Mwenyezi Mungu, washushie watu hawa baraka zako"*. Kutokana na matokeo ya baraka za dua hii Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi aliwafanya watu wale waingie kwenye Uislamu na baadae kufa mashahidi. (Ibn Hajar, Al-Isaba, IV, 353).

Tarik ibn Abdullah Al-Muharibi anasimulia namna alivyoshuhudia subira aliyoonyesha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutokana na magumu aliyokutana nayo wakati wa kuutangaza Uislamu:

"Siku moja nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa juu ya jukwaa la Zulmajaz akiwahutubia watu:

*"Enyi watu! Semeni 'la ilaha illallah' (Hakuna Mungu apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu) muokolewe"*. Akatokea mtu mmoja na kumfuata huku akiwa na jiwe mkononi na huku anasema kwa sauti:

“Enyi watu! Kamwe msimuamini, wala msijaribu kumfuata. Mtu huyu ni muongo”. Alimrushia jiwe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kupelekea vifundo vyake vya miguu kutoa damu. Niliwauliza wale waliokuwa pale:

“Ni mtu gani huyu (anayehutubia)?” Wakanijibu:

“Huyu ni kijana kutokana na watoto wa Abdulmutwalib”. Kisha nikauliza:

“Na ni nani yule anayemfuata huku anamrushia mawe?” wakanijibu:

“Yule ni mjomba wake, Abu Lahab”.[77]

❁

Mudrik Al-Asdi anasimulia mfano mwingine unaoonyesha kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa mfano wa kuigwa katika subira:

“Siku moja nilikuwa pamoja na baba yangu tunatekeleza hijja (katika kipindi cha ujinga). Tulipofika Mina tulikutana na kikundi cha watu. Nikamuuliza baba yangu:

“Kwa nini watu hawa wamejikusanya hapa?” Akanijibu:

“Kwa ajili ya mtu yule pale ambaye amejitenga na dini ya kabila lake”. Nilipoangalia ni nani anamuashiria nilikuta kuwa ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alikuwa akisema:

*“Enyi watu! Semeni ‘la ilaha illallah’ muokolewe”.*

Baadhi ya watu walimtemea mate usoni na wengine kumrushia uchafu na bado isitoshe wengine wakawa wanamsimanga. Hali hii ikaendelea mpaka mchana. Wakati ule akajitokeza msichana mmoja ambaye mabega yake yalikuwa wazi akaja huku amebeba

77. Darekutni, Sunan, Beirut 1986, III, 44-45.

chombo chenye maji na kitambaa. Alikuwa akilia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akachukua yale maji na kunywa na mengine kunawia uso na mikono yake. Kisha akanyanyua kichwa chake na kusema:

*"Mwanangu mpendwa! Funika mabega yako kwa kitambaa cha kichwani. Usihofie kuwa baba yake ataangukia kwenye mtego na kuuawa au kuteswa"*.

Tuliulizia huyu msichana alikuwa ni nani. Wakanijibu: "Ni binti yake aitwae Zaynab". (Haythami, VI, 21).

❀

Abdullah ibn Mas'ud رضي الله عنه anasimulia:

Wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa anagawanya ngawira kutokana na vita vya Hunayn aliwagawia mgao ule baadhi ya watu zaidi ya wengine.

Alimgawia Akra ibn Habis ngamia mia moja na idadi hiyo hiyo alimgawia Uyayna ibn Hisn. Aliwagawia baadhi ya wakuu wa kiarabu zaidi ya hizo. Mmoja miongoni mwa watu waliokuwa pale akasema:

"Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu, hakuna haki katika ugawaji huu wa ngawira, na radhi za Mwenyezi Mungu hazikupatikana".

Na mimi nikasema:

"Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa ninaenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kumuambia ulichokisema". Nikaenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuambia kile alichokisema yule mtu. Uso uliobarikiwa wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ukageuka na kuwa mwekundu kutokana na huzuni. Kisha akasema:

*"Kama Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake hawana uadilifu basi ni nani mwingine atakuwa muadilifu?"* Kisha akaendelea:

*"Mwenyezi Mungu amrehemu Musa. Yeye alipata mitihani mizito kuliko hii lakini bado alisubiri"*.

Kuanzia siku ile nikaamua kuacha kumuambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yale yaliyokuwa yanasemwa na watu wengine kumhusu yeye. (Bukhari, Adab 53; Muslim, Zakat, 145)

❁

Kutokana na masimulizi kutoka kwa Anas ibn Malik رضي الله عنه, siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipita mahali na kumuona mwanamke akilia kwa sauti juu ya kaburi la mtoto wake. Akamwambia:

*"Muogope Mwenyezi Mungu na uwe na subira"*.

Yule mwanamke akajibu:

"Nenda zako na uniache peke yangu! Janga lililonikuta mimi halijakukuta wewe".

Yule mwanamke alikuwa hajamtambua Mtume. Baadae wakamwambia yule alikuwa ni Mtume. Mara tu baada ya kulisikia hili akakimbilia kwa Mtume, kwa kuwa hapakuwa na mtu wa kumzuia aliingia moja kwa moja na kumfikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuomba msamaha:

"Ewe Mtume, nilikuwa sijakutambua".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Subira ya kweli ni pale unapofikwa na msiba"* (Bukhari, Janaiz, 32)

❁

Abdullah ibn Mas'ud رضي الله عنه anasimulia:

Siku moja nilienda mbele ya Mtume. Wakati huo alikuwa ameshikwa na malaria. Nikamwambia:

“Ewe Mtume! Umefikwa na kiwango cha hali ya juu cha malaria”. Akajibu: *“Ndio, ninavumilia maumivu ambayo yanaweza kuvumiliwa na watu wawili miongoni mwenu”.*

“Hayo yamekuwa hivyo ili upate malipo mara mbili”, nikamwambia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*“Ndio, hayo ni ya kweli. Mwenyezi Mungu anasamehe dhambi ya Muislamu ambaye amechomwa mguuni mwake au anapohisi maumivu makali. Madhambi ya Muislamu huyo hudondoka kama majani yanavyodondoka kutoka kwenye mti”* (Bukhari, Marda, 3, 13, 16; Muslim, Birr, 45)

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuuliza malaika Jibril:

*“Machungu aliyoyahisi Yaqub yalifikia kiwango gani baada ya kutengana na Yusuf?”.*

Jibril akajibu:

“Alihisi machungu ambayo ni sawa na machungu ambayo wangehisi akina mama sabini baada ya kupotolewa na watoto wao”. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*“Kama ni hivyo basi alipata malipo kiasi gani?”*

Jibril akajibu:

“Malipo ya mashahidi sabini. Kwani hakumfikiria vibaya Mwenyezi Mungu hata mara moja” (Tabari, XIII, 61; Suyuti, ad Durru al Manthur, IV, 570; Yusuf, 86).

Subira ya namna hii ndio ile iliyotajwa ndani ya Qur'an kama *'Swabrun jamil'*, yani 'subira njema'.

❁

Abdullah ibn Mas'ud ﵁ anasimulia:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alianza kutuhadithia juu ya Mtume aliyetumwa kwa watu wake. Lakini watu wake walimpiga mpaka akawa anavuja damu usoni mwake. Mtume yule akawa anafuta uso wake huku anasema:

*"Ewe Mwenyezi Mungu, wasamehe watu wangu kwani hawafahamu".*

Niliweza kumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ namna alivyokuwa amebadilika wakati anatuhadithia kuhusu huyu Mtume. (Bukhari, Anbiya 54; Muslim, Jihad 104).

❁

Tukio lifuatalo lina mazingatio kwetu sote katika kuonyesha kuwa malipo ya subira ni pepo:

Siku moja Abdullah ibn Abbas alimwambia Ata ibn Abi Rabah:

"Je nikuonyeshe mwanamke wa peponi?" akajibu:

"Ndio nionyeshe". Kisha ibn Abbas akasema:

"Je unamuona yule mwanamke mweusi? Siku moja yule mwanamke alienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumwambia:

"Nina kifafa na pindi kinaponijia nguo zangu zinafunuka. Je unaweza kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili aniponye?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamjibu:

*"Kama utakuwa na subira basi pepo itakuwa yako. Lakini kama bado unataka kuponywa basi nitakuombea kwa Mwenyezi Mungu akuponye"*. Kutokana na haya yule mwanamke akasema:

"Nitakuwa na subira juu ya maradhi yangu. Lakini naomba uniombee nguo zangu zisifunuke wakati nimepatwa na kifafa?" Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuombea kwa Mwenyezi Mungu juu ya hili. (Bukhari, Marda 6; Muslim, Birr, 54).

Hivyo hii ndiyo thamani ya subira mbele ya Mwenyezi Mungu pale mtu anapopewa mitihani...

❁

Abu Said ؓ anasimulia:

"Siku moja nilikuwa nimekaa pamoja na masikini kutoka Muhajirina. Kutokana na kuwa baadhi yao hawakuwa na nguo za kujisitiri walikuwa wamekaa kwenye kivuli cha wengine kwa ajili ya kujificha. Wakati ule ule mtu mmoja akaanza kusoma Qur'an. Mara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajitokeza na kukaa na sisi. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipotokea yule mtu aliyekuwa akisoma Qur'an akaacha kusoma. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatutolea salamu na kutuuliza:

*"Mnafanya nini?"*

Tukajibu:

"Ewe Mtume! Huyo ni mwalimu wetu na anatusomea Qur'an. Tunasikiliza kitabu cha Mwenyezi Mungu".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye amewaumba watu katika umma wangu ambao nimeamrishwa niwe na subira nao"*.[78]

78. Kutokana na maneno haya Mtume alikuwa amezingatia aya ifuatayo kutoka

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akakaa pamoja na sisi kana kwamba yupo sawa na sisi. Aliashiria kwa mikono yake na kusema:

*"Tengenezeni duara"*.

Upesi lile kundi likatengeneza duara kumzunguka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kugeuzia nyuso zao kwake. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatupa habari njema ifuatayo:

"Enyi Muhajirina ambao ni masikini na wahitaji. Kuna habari njema kwa ajili yenu. Siku ya kiama mtazungukwa na nuru na mtaingia peponi nusu siku mapema zaidi ya watu matajiri katika dunia hii. Hii nusu siku ni sawa na miaka mia tano ya hapa duniani" (Abu Dawud, Ilim, 13/3666).

Na haya ndiyo malipo ya masikini mwenye kusubiri...

❁

Kutokana na masimulizi kutoka kwa Fadala ibn Ubayd رضي الله عنه tukio lifuatalo ni mfano mzuri wenye kuonyesha kilele cha subira na ushupavu waliokuwa nao wanafunzi maalumu wa Mtume, yani maswahaba mbele ya magumu na tabu mbalimbali walizokutana nazo:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa anawaongoza maswahaba zake katika swala baadhi yao walishindwa kuendelea kusimama hivyo wakazimia kutokana na kukosa nguvu kuliko-

---

kwenye Qur'an: **"Na isubirishe nafsi yako pamoja na wanao muomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimt'ii tuliye mghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamanio yake yakawa yamepita mpaka"** (al Kahf, 18:28). Hapa Allah aliye juu zaidi amemuamrisha Mjumbe wa Allah ﷺ na wale watu masikini na wahitaji ambao waliingia kwenye uislamu pamoja naye waonyeshe subira pindi wanapofikwa na mitihani na pia awe makini wakati anafanya nao mambo mbalimbali.

sababishwa na njaa. Watu hawa walikuwa ni '*Ashab-i Suffa'*[79] au watu wa benchi. Mabedui waliokuwa wanakuja kutoka jangwani walikuwa wakisema yafuatayo kuwahusu watu hawa: "wao ni wendawazimu". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomaliza kuswalisha aliwafuata na kuwatuliza kwa kuwaambaia:

*"Lau kama mngelifahamu kile ambacho Mwenyezi Mungu amewaandalia mngelitamani muwe masikini na wahitaji zaidi ya mlivyokuwa sasa"* (Tirmidhi, Zuhd, 39/2368)

❁

Abu Huraira ؓ anasimulia:

"Niliwaona watu sabini kutokana na watu wa benchi. Hakuna hata mmoja miongoni mwao aliyekuwa na nguo iliyomfunika mwili mzima. Ama walikuwa na sketi walizozivaa kwa ajili ya kuwafunika mapaja yao au walivaa majoho yaliyoweza kuwafunika kuanzia kwenye kiuno kwenda juu. Walikuwa wanafikia kufunga nguo zao shingoni mwao. Baadhi yake zilikuwa zikiwafikia kwenye miundi ya miguu yao wakati nyingine zilikuwa zikiwafikia kwenye visigino. Walikuwa wakizikusanya nguo ili kuziba sehemu zao za siri" (Bukhari, Salat, 58).

Kama tulivyoweza kuona kuwa maswahaba waliobarikiwa walikutana na magumu ya aina zote ikiwemo njaa, umasikini, vita na majanga mbalimbali ili dini ya Uislamu itufikie leo hii.

Hivyo na sisi hatuna budi kufuata nyayo zao ili kuweza kuifikisha amana hii tukufu kwa vizazi vijavyo.

❁

79. Hasa "watu wa benchi". *Ashab-i Suffa* lilikuwa ni kundi la waislamu wa mwanzo ambao hawakuwa na sehemu ya kuishi na namna yoyote ya kujiendeleza. Hivyo walikuwa wakiishi katika benchi nje ya msikiti wa Mtume (Maelezo ya mfasiri).

Abdurrahman ibn Awf ﷺ alisema:

"Uislamu ulileta maamrisho magumu ambayo yalikuwa mazito kwenye nafsi zetu. Tuliwapata wabora miongoni mwa wabora katika kukabiliana na magumu haya ambayo yaliichukiza nafsi. Kwa mfano tuliondoka Makka na kuelekea Madina pamoja na Mtume. Kuhama huku ambako kulikuwa kugumu katika nafsi zetu kukawa sababu ya utukufu na ushindi juu yetu. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anatufahamisha yafuatayo ndani ya Qur'an:

**"Kama Mola wako Mlezi alivyo kutoa nyumbani kwako kwa Haki, na hakika kundi moja la Waumini linachukia. Wanajadiliana nawe kwa jambo la Haki baada ya kwisha bainika, kama kwamba wanasukumwa kwenye mauti nao wanaona"** (Al-Anfal, 8:5-6).

Kama Mwenyezi Mungu alivyoelezea tulitoka kwenye vita vya badr pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na hapa pia Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akatupa ushindi na kutunyanyua daraja.

Kwa kifupi ni kwamba tulipata malipo makubwa kutokana na haya maamrisho magumu juu ya nafsi zetu". (Haythami, VII, 26-27).

❁

Maneno yafuatayo ambayo yanatoka kwa Muhammad Iqbal yanaonyesha ubora wa kuwa na subira na uvumilivu pale unapopatwa na mitihani:

"Siku moja swala alikuwa analalamika kwa swala mwingine:

Kuanzia sasa hivi nitakuwa ninaishi kwenye Al-Kaaba ambayo ni sehemu tukufu ya usalama. Nitalala pale na kula pale pale. Kwani hapa kwenye hizi tambarare zenye nyasi nyingi wawindaji wametega mitego yao na wanazunguka usiku na mchana kutu-

winda sisi. Ninahitaji amani kutokana na hawa wawindaji, na ninahitaji amani ndani ya moyo wangu...”

Yule swala mwingine aliyekuwa anamsikiliza akasema:

“Ewe rafiki yangu mwerevu, kama unataka kuishi ishi kwenye hatari. Pambana na uwe shupavu kuliko upanga wenye ncha ya almasi. Hatari hujaribu uimara na nguvu za mtu. Itatuonyesha ni kiasi gani miili yetu na nafsi zetu zinaweza kukabiliana na misukosuko”.

❁

Kiini cha jambo hili ni kwamba: subira ni hazina inayoweza kupatikana ndani ya mwanadamu.

Subira ni ngao imara dhidi ya majanga na matatizo mbalimbali. Subira ni sifa nzuri ambayo Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anairidhia zaidi na ameahidi malipo makubwa. Maneno ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yanatufahamisha kuwa:

*“Subira ni nuru”* (Muslim, Taharat, 1). Hii ni kwa sababu inaangaza dunia ya mtu na akhera yake.

### *16. Hamd* (Kusifu) na *Shukur* (Kushukuru)

*Hamd* ni kusifu na kutukuza ukubwa usio na mipaka aliokuwa nao Mwenyezi Mungu Mtukufu, uumbaji wake na ubainifu wa sifa zake. *Shukur* ni kumshukuru Yeye kutokana na neema na fadhila zake zisizo na mipaka kwa kupitia matamshi ya mtu, vitendo na ndani ya moyo. Maneno haya mawili yanakaribiana sana katika maana.

Kila namna ya kutukuza kunamhusu Mwenyezi Mungu pekee na sifa zote njema ni juu yake. Kumsifu Mwenyezi Mungu kutokana na neema zote alizotujaalia ni jukumu la kila Muislamu. Ingawa hili ni deni juu ya Muislamu Mwenyezi Mungu aliye juu

zaidi anatufahamisha kuwa anampenda mja wake anayemsifu[80]. Hii pia ni neema na fadhila kubwa na ni udhihirisho wa Rehma zake zisizo na mwisho.

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ndiye mwenye kustahiki kusifiwa. Qur'an tukufu inatufahamisha:

**"Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye umba mbingu na ardhi, na akafanya giza na mwangaza. Tena baada ya haya walio kufuru wanawafanya wengine sawa na Mola wao Mlezi"** (An'am, 6:1).

Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapenda waja wake wamsifu Yeye katika kila hali. Anatufahamisha ndani ya Qur'an:

**"Na sema: Alhamdulillah, Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye hana mwana, wala hana mshirika katika ufalme, wala hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu wake. Na mtukuze kwa utukufu mkubwa"** (Isra, 17:111).

**"Wito wao humo utakuwa: Subhanaka Llahumma "Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu!" Na maamkio yao humo ni "Salama". Na mwisho wa wito wao ni: Alhamdulillahi Rabbil A'lamiin "Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote"** (Yunus, 10:10).

Tunapata nafasi kumsifu Mwenyezi Mungu katika kila rakaa ndani ya swala zetu kwa kupitia aya ya kwanza ya Sura ya kwanza ndani ya Qur'an, Al-Fatiha:

**"Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote"** (Fatiha, 1:1).

Haiwezekani kutumaini wema wowote katika jambo lolote ambalo linafanywa bila ya kuanza kwa kumsifu Mwenyezi Mungu

80. Muslim, Zikir, 89

aliye juu zaidi. Katika kuwaonya watu wake kuhusu suala hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kila jambo la muhimu ambalo halitaanzwa kwa kumsifu Mwenyezi Mungu halitakuwa na baraka za Mwenyezi Mungu"* (Abu Dawud, Adab, 18/4840).

Kwa wakati huo huo *hamd* ni namna muhimu ya *dhikr* (kumkumbuka Mwenyezi Mungu). Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametuelezea ubora wa kumsifu Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

*"Twahara ni nusu ya imani. Maneno* **'Alhamdulillah'** *(Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu) ndio nguzo yake,* **'Subhanallahi wa'l hamdulillah'** *(Sifa zote njema na utukufu ni wake Mwenyezi Mungu) inajaza nafasi kati ya mbingu na ardhi kutokana na malipo yake. Swala za faradhi ni taa; sadaka ni ushahidi; subira ni nuru. Qur'an ni ushahidi ama juu yako au dhidi yako. Kila mtu anaondoka asubuhi (kwenda sokoni) kuiuza nafsi yake; baadhi yao wanaishia kuiacha huru wakati wengine wanaishia kuiangamiza"* (Muslim, Taharah 1; Tirmidhi, Dawat 85/3517).

Kama ilivyo *hamd* jukumu lingine la mja ni *shukur*. *Shukur* ni pale mja atakaporidhishwa na neema na wema ambao amejaaliwa na akasema maneno mbalimbali na kutenda matendo mbalimbali kwa moyo safi kwa ajili ya kumtumikia Mola wake ambaye ndiye aliyemjaalia yote hayo. *Shukur* ni kumjua mtoaji wa kweli wa neema zote.

Haitoshi kufahamu tu na kudhihirisha kwa maneno juu ya neema ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia ili kuchukuliwa kama waja wa Mwenyezi Mungu wenye kushukuru. Bali pia ni muhimu kutekeleza ibada zetu na kutenda amali njema kulingana na maamrisho ya Mola wetu.

Moja wapo ya mambo muhimu katika dini yetu ni kwamba sifa na shukurani ni sharti la kuwa mwanadamu. Mwanadamu

yuko kileleni katika msururu wa tabaka la viumbe kuanzia vya chini mpaka vilivyo bora zaidi, na yeye mwanadamu ameumbwa kama *'ashraf-i makhlukat'* (mbora zaidi miongoni mwa viumbe).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Shukr* (Kushukuru) ni nusu ya imani..." (Suyuti, I, 107).

Kila mwanadamu ambaye ametunza utu wake na heshima yake ambayo ndiyo aliyoumbiwa atahisi moyoni mwake wajibu huu wa kushukuru hata kwa yule aliyempatia bilauri ya maji ya kunywa. Kwa kuzingatia hili mtu kupuuzia na kutoshukuru kwa Mola wetu ambaye ndiye chanzo cha neema zote hizi ni kinyume na akili ya mwanadamu, uelewa wake na utu wake. Hali hii inaweza kusababishwa na kukosa utambuzi na hisia.

Licha ya haya kwa bahati mbaya kuna watu wengi ambao hawazingatii juu ya neema na fadhila zisizo na kifani ambazo Mwenyezi Mungu amewajaalia. Katika kuuelezea ujinga huu mkubwa Mwenyezi Mungu anatufahamisha ndani ya Qur'an:

**"Ni wachache katika waja wangu wanao shukuru"** (Saba, 34:13).

Kutoshukuru ni hali ambayo Mola wetu anaichukia sana. Pia ni sababu ya kutupunguzia neema alizotujaalia. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatufahamisha haya ndani ya Qur'an tukufu kama ifuatavyo:

**"Basi nikumbukeni nitakukumbukeni, na nishukuruni wala msinikufuru"** (Al-Baqara, 2:152).

**"Na alipo tangaza Mola wenu Mlezi: Mkishukuru nitakuzidishieni; na mkikufuru, basi adhabu yangu ni kali"** (Ibrahim 14:7).

**"Na tulimpa Luqman hikima, tukamwambia: Mshukuru Mwenyezi Mungu. Na mwenye kushukuru basi hakika anashuk-**

**uru kwa manufaa ya nafsi yake. Na aliye kufuru, basi Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Msifiwa"** (Luqman, 31:12).

***Matukio ya wema***

Kila Mtume alipokuwa akiandaa vitu mezani alikuwa akisema:

*"Ewe Mola wetu, Tunakusifu kwa moyo safi, kwa sifa zisizo na mwisho ambazo kamwe hazipungui na ambazo zitakubalika kwako na wala hazitarudishwa"* (Bukhari, At'ima, 54; Abu Dawud, At'ima 52; Tirmidhi, Dawat, 55)

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anampenda mja wake ambaye baada ya kula au kunywa chochote anamshukuru"* (Muslim, Zikr, 89; Tirmidhi, At'ima 18).

❁

Siku moja watu wawili walipiga chafya mbele ya Mtume. Akasema *'yarhamukallah'* kwa ajili ya mmoja na kutosema chochote kwa ajili ya yule mwingine. Yule mtu ambaye hakusemewa maneno haya akamuuliza Mtume:

"Pindi fulani alipopiga chafya ulisema *'yarhamukallah'*; kwa nini hukusema chochote pindi mimi nilipopiga chafya?"

*"Yule mtu alisema 'alhamdulillah' (Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu), lakini wewe hukusema kitu"* (Bukhari, Adab 127; Muslim, Zuhd, 53)

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuona Omar amevaa shati. Akamwambia:

*"Je hili shati lako ni jipya au umelifua?"* Omar ﷺ akajibu:

"Sio jipya, limefuliwa tu ewe Mtume". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Vaa kitu kilicho kipya na uishi kama mtu anayemsifu Mwenyezi Mungu, na kufa kama shahidi"* (Ahmad, II, 89).

Mara maneno haya ya kimiujiza kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yakawa kweli na Omar ﷺ akafa shahidi.

❁

Jukumu la muhimu kupita yote ambayo yanatekelezwa na mja wa Mwenyezi Mungu bila shaka ni kumsifu Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ametufahamisha ubora wa kumsifu Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

*"Mmoja miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu alisema: 'Ewe Mola wangu! Sifa zote njema ni zako, sifa zinazoendana na wewe, ukubwa wa nguvu zako na mamlaka yako'. Mja huyu akawafanya wale malaika wawili walioteuliwa kwa ajili ya kuandika amali zake washindwe kuandika malipo yanayotokana na sifa hizi. Kisha wakapanda mbinguni na kusema:*

*"Ewe Mola wetu, Mja wako amesema maneno ambayo hatujui ni namna gani tuandike malipo yake". Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akawauliza ingawa Yeye anajua zaidi kuliko mtu yeyote:*

*"Mja wangu alisema nini?" Malaika wakajibu:*

*"Ewe Mola wetu, mja wako yule alikusifu kama ifuatavyo:*

*"Ya rabbi lakal'hamdu kama yanbaghiy l'jalaali wajhika wali'a'thiymi sultaanika". (Ewe Mola wangu. Sifa zote njema ni zako, sifa zinazoendana na wewe, ukubwa wa nguvu zako na mamlaka yako).*

*Kutokana na maneno haya Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akawaambia wale malaika wawili:*

*“Yaandikeni hayo maneno ya mja wangu kama alivyoyatamka mpaka siku atakayokutana na Mimi na kisha nitampa malipo yake kutokana na hayo maneno aliyoyatamka”* (Ibn Majah, Adab, 55).

Mola wetu atujaalie utukufu wa dua hii...

❁

Abu Huraira ﷺ anasimulia:

“Nilikuwa nikiwa yatima na nilihamia Madina nikiwa masikini. Nilifanya kazi kwa Gazwan (Busra) kwa malipo ya kujaza tumbo langu na jozi ya viatu. Wakati tukiwa safarini nilikuwa nikiwakusanyia kuni na pindi walipopanda wanyama wao nilikuwa nikiwabembeleza ngamia wao kwa sauti nzuri ili waongeze mwendo; Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu kwa kuimarisha dini ya Uislamu na kwa kumfanya Abu Huraira kuwa imam” (Ibn Majah, Ruhun, 5/2445).

❁

Aisha ﷺ anasimulia:

“Usiku mmoja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliniambia:

“Ewe Aisha! Kama utaniruhusu nitautumia usiku huu kwa ajili ya kumuabudu Mola wangu”. Nikajibu:

“Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu! Ninapenda kuwa pamoja na wewe lakini ninapenda kile unachokipenda zaidi ya hiki”

Kisha akanyanyuka na kuchukua udhu wake na kuanza kuswali. Alikuwa akilia... Alikuwa akilia sana kiasi kwamba joho lake, ndevu zake na sehemu aliyokuwa akisujudia pakaloana kwa

machozi. Wakati akiwa katika hali hii Bilal ﷺ alikuja na kumuita kwa ajili ya swala. Alipomuona analia alimwambia:

"Ewe Mtume. Kwa nini unalia wakati Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amekusamehe madhambi yako yaliyopita na yajayo?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Je nisiwe mja mwenye kumsifu zaidi? Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa nimefunuliwa aya hizi na kwamba ni huzuni kubwa kwa yule ambaye anazisoma aya hizi lakini hazitafakari".* Kisha akasoma aya zifuatazo kutoka kwenye Qur'an:

**"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto"** (Al-Imran, 3:190-191)

❁

Pale Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoona kuwa neema alizojaaliwa yeye hakujaaliwa mtu mwingine alikuwa akimsifu Mwenyezi Mungu mara moja. Siku moja alienda kumtembelea mtu mmoja aliyekuwa amepooza na pindi alipoona hali yake upesi alishuka juu mnyama wake na kusujudu kwa kuonyesha shukurani. (Haythami, II, 289).

Dalili kuwa mtu anampenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni kuwa anaendelea na tabia yake njema popote pale. Ni mara ngapi tumesujudu kutokana na matukio mbalimbali tunayokutana nayo ambayo yana mazingatio ndani yake?

❁

Sa'd ibn Abi Waqqas ﷺ anasimulia:

"Siku moja niliondoka Makka kwa ajili ya kwenda Madina pamoja na Mtume. Tulipofika sehemu iliyokuwa inaitwa Azwara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alishuka juu ya ngamia wake. Kisha akanyanyua mikono yake mbinguni na kuomba dua kwa kitambo kiasi kisha akasujudu na kutulia kwenye sijda kwa muda mrefu. Akayarudia haya mara tatu kisha akasema:

*"Nilimuomba Mola wangu aniruhusu kuwaombea umma wangu siku ya kiama. Mwenyezi Mungu akaniahidi moja ya tatu ya umma wangu. Kisha nikasujudu kwa kuonyesha shukurani kwa Mola wangu. Kisha nikanyanyua kichwa changu kwa mara nyingine tena na kumuomba Mola wangu awasamehe watu wangu; kisha akaniahidi theluthi nyingine ya umma wangu. Kutokana na hili nikasujudu tena kwa kuonyesha shukurani. Kisha nikanyanyua kichwa changu kwa mara nyingine tena na kumuomba Mola wangu awasamehe watu wangu; kisha akaniahidi theluthi iliyobaki ya umma wangu. Kisha nikasujudu kwa mara nyingine tena kwa kuonyesha shukurani kwa Mola wangu"* (Abu Dawud, Jihad, 162/2775).

Habari njema zilizomfurahisha mno Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wetu na kumpelekea asujudu kwa kushukuru zilikuwa ni kwamba wale watu katika umma wake ambao walitenda madhambi makubwa hawatabakia katika moto milele ingawa wataadhibiwa kutokana na madhambi yao, lakini baadae wataingizwa peponi kutokana na maombezi yake. Na wale waliotenda madhambi madogo watasamehewa na kuingizwa peponi huenda hata bila ya kukutana adhabu yoyote.

Hapa hatujadili juu wale wasio na imani kabisa ikiwa wataingia peponi au la.

❁

Abdurrahman ibn Awf ؓ anasimulia tukio lifuatalo lenye kuonyesha namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyotilia

maanani suala la kumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na neema na fadhila zake:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliondoka msikitini na mimi nikamfuata bila ya yeye kujua. Alielekea kwenye shamba la mitende. Alipokuwa pale alielekea Makka na kusujudu. Alisujudu kwa muda mrefu kiasi kwamba nikadhani kuwa amekufa. Upesi nikamfuata pale alipo na kupiga magoti na kumuangalia usoni. Alinyanyua kichwa chake na kusema:

*"Kuna tatizo gani ewe Abdurrahman?"*

"Ewe Mtume. Ulitulia kwa muda mrefu kwenye sijda kiasi kwamba nikadhani kuwa umefariki ndio maana nikaamua kuja upesi kukuangalia". Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Pindi nilipoingia kwenye bustani hii nilimuona Jibril. Alinipa habari njema kuwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amesema: 'Yeyote atakayekusalimia kwa maamkizi ya amani basi nitampa mtu huyo amani. Yeyote atakayekutakia baraka basi na mimi nitambariki mtu huyo'. Hii ndio sababu iliyonipelekea kusujudu kwa ajili ya kumshukuru Mwenyezi Mungu".* (Hakim, I, 344-345/810)

❁

Bila shaka neema zote tulizonazo zinatoka kwa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Kushukuru namna neema hizi zinavyotufikia ni dalili ya uaminifu na adabu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema yafuatayo katika hadith:

*"Kama mtu atamuombea kwa Mwenyezi Mungu yule aliyemfanyia wema kama ifuatavyo: 'Mwenyezi Mungu akujaalie kila la kheri' atalipwa deni lake la shukurani katika njia iliyo bora zaidi..."* (Tirmidhi, Birr, 87/2035)

❁

Aisha رضي الله عنها anasimulia:

Mara kwa mara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiniambia:

*"Ewe Aisha, unaweza kunisomea baadhi ya mashairi uliyoyahifadhi?"*

Na mimi nilikuwa nikijibu:

"Ni aya zipi ungelizipenda ewe Mtume? Ninayafahamu mashairi mengi".

Kisha alikuwa akisema:

*"Yale yanayohusu kushukuru"*. Wakati fulani nikasema:

"Baba yangu na mama yangu watolewe kafara kwa ajili yako. Kisha nikasoma shairi lifuatalo:

"Mshike mkono mtu dhaifu na umsaidie asimame. Usiruhusu hali yake ya udhaifu ikudanganye. Itakuja siku ambayo majanga yatakufika na kukusumbua. Kisha utakuja muda ambao yule mtu dhaifu atakulipa fidia au kama atashindwa kufanya lolote angalau atakushukuru. Kwani mtu yeyote atakayekushukuru kwa jambo ulilomfanyia atakuwa amekulipa. Kama utataka kumfedhehesha mtu ambaye ni Mtukufu jua kuwa nguvu ndogo haiwezi kudhoofisha kamba iliyo imara"

Baada ya haya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Ewe Aisha! Kutokana na kile alichoniambia Jibril ni kwamba katika siku ya kiama wakati viumbe vyote vimefufuliwa, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atamuuliza mja wake ambaye alipokea fadhila kutoka kwa mwenzake:*

*"Je ulimshukuru mja wangu ambaye alikutendea wema?"*

*Atajibu:*

*"Ewe Mola wangu. Nilijua kuwa kila wema unaonifikia unatoka kwako hivyo nilikushukuru Wewe pekee". Kisha Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atasema:*

*"Hukunishukuru Mimi hali ya kuwa hukumshukuru mja wangu ambaye alikuwa sababu ya wema huo kukufikia wewe".* (Ali al-Muttaki, III, 741-742).

Katika hadith nyingine ya Mtume, Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ameonyesha uhusiano wa karibu kati ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumshukuru mtu ambaye amekufanyia wema:

*"Yeyote ambaye hawashukuru watu basi hajamshukuru Mwenyezi Mungu"* (Abu Dawud, Adab, 11/4811; Tirmidhi Birr, 31)

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema kuwa moja ya neema kubwa miongoni mwa neema alizojaaliwa mwanadamu ni moyo wa kushukuru. Sawban ﵁ anasimulia kuwa:

"Siku moja tulikuwa katika msafara wa kivita pamoja na Mtume, wakati huo aya ifuatayo ikashushwa:

**"Enyi mlio amini! Hakika wengi katika makuhani na wamonaki wanakula mali za watu kwa baat'ili na wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu"** (Tawba, 9:34). Baadhi ya maswahaba wakasema:

"Kinachotakiwa kushushwa kuhusu dhahabu na fedha tayari kimeshashushwa (hatutaweka akiba ya vitu hivyo tena). Lau kama tungelifahamu kuwa ni bidhaa gani bora zaidi tungelizikusanya baadhi yake". Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*"Kitu cha kuwa nacho kilicho bora zaidi ni ulimi wenye kumtaja Mwenyezi Mungu wakati wote, moyo uliojaa kushukuru na mke mwema ambaye anamsaidia mume wake katika imani yake"* (Tirmidhi, Tafsir, 0/3094)

❁

Nabii Daudi ﷺ alikuwa akimshukuru Mwenyezi Mungu mara kwa mara. Siku moja alisema:

"Ewe Mola wangu, nitawezaje kukusifu kikweli kweli? Kwani ninaweza kukushukuru Wewe kwa kupitia neema zako".

Akafunuliwa kuwa:

"Je unafahamu kuwa neema zote zinazokufikia zinatoka kwangu?"

Nabii Daud ﷺ akajibu:

"Ndio"

Kutokana na jibu hili Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akasema:

"Kama unaamini hivyo inatosha kwa mimi kukuridhia".[81]

❁

Siku moja Omar ﷺ alikutana na muumini ambaye alikuwa anaomba dua ifuatayo mfulululizo: "Ewe Mwenyezi Mungu nijaalie niwe miongoni mwa wale walio wachache sana".

Omar hakufahamu mtu yule alimaanisha nini kutokana na dua ile hivyo akaamua kumuuliza:

"Kwa nini unaomba kama hivyo?" Muumini yule akajibu:

81. Ibn Kathir, "Kisasu al-Anbiya," Beirut, Dara'l Qalam, uk 524.

"Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amesema: **'...Ni wachache katika waja wangu wanao shukuru'** (Saba, 34:13).

Ninatamani kuwa miongoni mwa watu hao wachache".

Omar aliachwa kwenye mshangao juu ya namna hii nzuri ya kufikiria na akajisikitikia mwenyewe:

"Majonzi yaliyoje juu yangu; kila mtu ni mjuzi na mwenye akili kuliko Omar" (Ibn Abi Shayba, Musannaf, VII, 81)

❁

Pindi Junayd al-Baghdadi alipokuwa na umri wa miaka saba mjomba wake Seriyy-i Sakati alimpeleka hijja. Katika moja ya mazungumzo yao ya busara ambayo yalikuwa yakifanyika pale Haram, walianza kujadiliana kuhusu *Shukur* au kushukuru. Baada ya kila mwanachuoni kutoa maoni yao Seriyyi Sakati alimgeukia Junayd na kumuomba atoe maoni yake. Baada ya kutulia kwa muda Junayd alitoa majibu yafuatayo yenye kuvutia:

"Shukurani sio kuzitumia zile neema ambazo Mwenyezi Mungu amekujaalia kwa maasi wala kuzitumia katika kufanya maovu" (Fariduddin Attar, uk 318).

❁

Mjadala ufuatao unaohusu shukur ambao ulifanywa kati ya Ibrahim ibn Adham na Shakik-i Belhi una mazingatio muhimu kwetu sote:

Shakik-i Belhi alimuuliza Ibrahim ibn Adham:

"Unapataje kipato chako?"

Ibrahim ibn Adham akajibu:

"Ninashukuru chochote ninachopata na pale ninapokosa chochote huwa na subira"

Kisha Shakik-i Belhi akasema:

"Mbwa wa Khurasan wanayafanya haya pia". Wakati huu naye Ibrahim ibn Adham akamuuliza:

"Vizuri, wewe unafanya nini?"

Shakik-i Belhi alitoa jibu lifuatalo:

"Sisi tunashukuru kwa chochote tunachokipata na kukitolea sadaka, na pale tunapokosa chochote pia tunashukuru na kusubiri".

❁

Haiwezekani kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zote alizotujaalia kama anavyostahiki kushukuriwa. Hata hivyo kama tutamsifu na kumshukuru kadiri ya uwezo wetu basi Mwenyezi Mungu Mtukufu atakubali hicho kidogo tulichokifanya kana kwamba kilikuwa ni kikubwa na atakuwa radhi na sisi. Bashir Hafi ambaye ni mmoja wa marafiki wa Mwenyezi Mungu ni mfano mzuri juu ya jambo hili:

Mtu huyu baada ya kufariki alionekana kwenye ndoto. Ndani ya ndoto aliulizwa:

"Mwenyezi Mungu amekuhukumu vipi?" Akajibu:

"Mwenyezi Mungu amenisamehe na kunijaalia kuingia peponi na kisha akaniambia:

"Ewe Bashir! Hata kama ungelisujudu juu ya kaa la moto kwa ajili yangu usingeliweza kunishukuru vya kutosha kutokana na mapenzi niliyoyaweka katika nyoyo za waja wangu juu yako wewe" (Kushayri, Risalah, Beirut 1990, uk 406).

❁

Andrea Dorya alishindwa na Barbaros Hayreddin Pasha pale Preveze. Kisha Andrea Dorya akalazimika kuacha manowari yao na kukimbia katika hali ngumu lakini alifanikiwa kuokoa maisha yake.

Meli za maadui zikiwa zimeshusha bendera zao pamoja na maelfu ya watumwa mbele yake, Barbaros aliingia Halij kwa kutokea Sarayburnu. Juu ya bahari kulijaa meli za kivita za maadui pamoja na watumwa wa kivita.

Sultani wao, mawaziri wake pamoja na pashas walikuwa wakiangalia mandhari hii wakiwa kwenye fukwe za Sarayburnu eneo ambalo leo hii halipo. Mmoja miongoni mwa pashas akasema yafuatayo kwa furaha:

"Sultani wangu, ninastaajabu ni mara ngapi dunia imewahi kushuhudia tukio kama hili? Lazima utakuwa unajivunia mno jambo hili"

Sultani yule maarufu alitoa jibu lifuatalo:

"Pasha! Je tunastahiki kujivunia na kujikweza juu ya jambo hili au kumsifu na kumshukuru Mola wetu ambaye ndiye aliyetujaalia ushindi huu?"

Uzuri ulioje wa mafunzo haya ya Uislamu na usafi moyo...

❁

Kwa kumalizia ni kwamba, ni jukumu letu la msingi la kuishi tukiwa na hisia za sifa na shukurani kwa Mola wetu. Na wakati huo huo kutekeleza jukumu hili kutatufanya tuwe karibu na Mwenyezi Mungu na kuongezewa neema zake. Jalaluddin Rumi ana yafuatayo ya kusema:

"Kushukuru juu ya neema uliyojaaliwa ni kuzuri kuliko neema yenyewe. Je mtu anayependa kushukuru anaweza kuacha kushukuru na kuifikiria neema yenyewe? Kuwa mwenye kushukuru

ndio roho ya neema zote. Neema ni kama ngozi au ganda. Kwa jambo la pekee linaloweza kukupeleka kwenye mlango wa rafiki yako ni shukurani. Neema zinaweza kumfanya mtu awe au asiwe mwenye kutafakari, jambo ambalo ni kinyume na utambuzi wetu. Lakini mara zote shukurani inaleta utambuzi. Fungua macho yako na uwinde neema ya kweli kwa kupitia neema ya shukurani".

**17. Shajaa' (Ujasiri)**

Neno *shajaa'* lina maana ya ujasiri katika vita, werevu, ushujaa, ushupavu wa moyo na kuonyesha ujasiri mbele ya vurugu na hatari. Hii ni njia ya wastani kati ya hisia za hasira na ghadhabu na uwoga ambao ni kinyume chake.

Kiini cha *shajaa'* ni kukubaliana na makadirio ya Mwenyezi Mungu na kujitiisha kwayo. Hii ndio sababu Muislamu ambaye anaamini kadari na anamtegemea Mwenyezi Mungu kamwe hapatwi na uwoga au udhalili.

Kutokana na masimulizi ya Sawban ﵁ Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Muda umekaribia ambapo majeshi ya wageni yatakuja kuwashambulia kama wanyama waroho ambao wanaitana wao kwa wao kwenye meza kwa ajili ya kula".*

Mmoja miongoni mwa wale waliokuwepo pale akauliza:

"Je ni kwa sababu tutakuwa na idadi ndogo ewe Mtume?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Hapana, kinyume chake ni kwamba mtakuwa wengi kiidadi. Lakini mtakuwa kama povu ambalo linajikusanya baada ya mafuriko, povu ambalo halina uzito kabisa. Mwenyezi Mungu ataondoa hofu katika nyoyo za maadui na kuweka udhaifu katika nyoyo zenu".*

“Ni udhaifu gani huo ewe Mtume?” waliuliza.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*“Kuipenda hii dunia na kuhofia kifo”*. (Abu Dawud, Malahim, 5/4297).

Hivyo tunajifunza kutokana na hayo kuwa pale ujasiri na werevu utakapoondolewa katika nyoyo za waumini na wakaamua kuikumbatia dunia na kuhofia kifo, basi watadhalilishwa na kuteswa. Kwa namna hii hawatakuwa na uzito wowote mbele za maadui zao.

***Matukio ya wema***

Hatuwezi kumfikiria mtu mwingine jasiri zaidi ya Mtume. Alionyesha subira na ujasiri katika mazingira magumu mno. Kamwe hakutekwa na hofu na uwoga au kushindwa kutekeleza majukumu yake vizuri.

Pindi Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomuamrisha Mjumbe wake ahamie Madina washirikina wa kiquraysh ambao walilifahamu jambo hili waliizunguka nyumba yake na kuchomoa mapanga yao tayari kumuua pale tu atakapotoka kwenye nyumba yake. Hata hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuonyesha hofu yoyote, akafungua mlango wake na kuwarushia mchanga kwenye vichwa vyao. Akawapita pale pale walipokuwa wamesimama huku akiwa anasoma aya za mwanzo wa surat *Yasin* na kisha akawatoroka. (Ibn Sa’d, I, 227-228).

Ali ؓ amesema:

“Wakati wa vita vya Badr tulijikinga nyuma ya Mtume. Siku ile yeye ndiye aliyekuwa karibu mno na maadui kuliko sisi sote na yeye ndiye aliyekuwa jasiri na mwerevu kuliko sisi sote” (Ahmad, I, 86).

Abdullah ibn Omar ﷠ anasimulia:

“Kamwe sikuwahi kumuona mtu mkarimu, mwerevu na jasiri kuliko alivyokuwa Mtume” (Ibn Sa’d, I, 373).

❁

Wakati wa vita vya Uhud mtu mmoja miongoni mwa wapagani alijitokeza mbele ya uwanja wa vita akiwa juu ya ngamia na kutaka mtu ajitokeze kupambana naye. Alipoona kila mtu amesogea nyuma na kushindwa kuitikia changamoto yake alirudia kuita mara tatu. Kisha Zubayr ibn Awwam ﷠ akamsogelea karibu yake. Akamrukia pale juu ya ngamia na kumkaba na kisha wakaanza kupambana. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*“Muangushe chini, mfanye aanguke chini”*. Haukupita muda mrefu mara yule mpagani akawa yuko chini. Kisha Zubayr akainama na kummalizia kabisa. Baada ya pale Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema:

*“Kama Zubayr asingelifanya vile, basi mimi ningelipambana naye pale ambapo kila mtu alikuwa amerudi nyuma”*.[82]

❁

Ubayy ibn Halef ambaye alikuwa miongoni mwa wapagani wa Makka alikuwa miongoni mwa maadui wa Uislamu wenye vurugu sana. Kabla ya kuhamia Madina alimwambia Mtume:

“Nina farasi ambaye ninamuandaa kwa chakula kilicho bora. Siku moja nitampanda na kukuchinja nikiwa juu yake”.

Wakati mwingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamjibu:

*“Mungu akipenda mimi ndiye nitakayekuchinja”*.

82. Halabi, Insanu al-Uyun, Egypt 1964, Ii, 235.

Wakati wa vita vya Uhud mpagani huyu asiyekuwa na akili alikuwa akimtafuta Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na huku anasema:

"Kama leo atakimbia basi ndio utakuwa mwisho wangu"

Huku akiwa na mawazo haya kichwani akamsogelea Mtume ili amuue. Maswahaba walitaka kumkata kichwa chake wakati bado akiwa mbali, lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Hapana, muacheni aje"*

Pindi Ubayy ibn Halef alipomkaribia Mtume, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichukua mkuki kutoka kwa mmoja wa maswahaba zake. Mara Ubayy akakimbia. Hata hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

*"Ewe mwongo, unakimbilia wapi?"*, kisha akamrushia mkuki. Ule mkuki ukamchoma kidogo Ubayy kwenye shingo. Hata hivyo licha ya kuchomwa huku kidogo alidondoka kwenye farasi wake; akabingilika mara kadhaa na kuanza kukimbilia kwenye upande wake huku akihisi uchungu mkali. Alikuwa akikimbia huku wakati huo huo akipiga kelele, macho yake yalikuwa yanakaribia kuchomoka kwenye soketi zake.

"Ninaapa kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amenichinja"

Wapagani walioenda karibu yake na kuliona jeraha lake walisema:

"Huu ni mkwaruzo mdogo tu". Hivyo hawakuona kuwa kulikuwa na umuhimu wa kumtuliza. Akasema:

"Wakati tulipokuwa Makka Muhammad aliniambia: 'Nitakuchinja'. Ninaapa kuwa hata kama angelikuwa kanitemea mate basi mate hayo yangeliniua..."

Aliendelea kulia kama ng'ombe dume anayekoroma.

Abu Sufyan akamtania kwa kumwambia:

"Unawezaje kupiga kelele kiasi hicho kutokana na mkwaruzo mdogo hivyo?"

Ubayy akamjibu:

"Je unamjua aliyenisababishie jeraha hili? Hili ni jeraha lililosababishwa na Muhammad. Ninaapa mbele ya Lat na Uzza kuwa kama haya maumivu ninayohisi sasa yangelisambazwa kwenye Hijaz nzima basi watu wote wangeliteketea. Muhammad aliniambia kuwa kwa hakika ataniua. Tokea wakati ule nilifahamu fika kuwa nitakufa kwa mikono yake na sitaweza kumkwepa".

Hivyo matokeo yake Ubayy ambaye alikuwa adui mkubwa wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akafariki siku moja kabla ya wapagani hawajawasili Makka. (Ibn Ishaq, uk 89; Ibn Sa'd, II, 4; Hakim, II, 357).

❀

Muhammad ibn Maslama ana yafuatayo ya kusema:

Nilisikia kwa masikio yangu mwenyewe na kuona kwa macho yangu mwenyewe namna waislamu walivyokuwa wanakimbilia milimani baada kutawanyika tulipokuwa Uhud. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwaita:

*"Nyie fulani na fulani. Rudini kwangu. Nyie fulani na fulani. Njooni kwangu. Mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu"* (Waqidi, I, 237).

Mwenyezi Mungu Mtukufu anafunua ukweli huu ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

**"Pale mlipo kuwa mkikimbia mbio wala hamumsikilizi yeyote, na Mtume anakuiteni, yuko nyuma yenu. Mwenyezi**

**Mungu akakupeni dhiki juu ya dhiki, ili msisikitike kwa yaliyo kukoseeni wala kwa yaliyo kusibuni. Na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayo yatenda"** (Al'i Imran, 3:153).

❁

Kutokana na mkataba uliowekwa katika siku ya Uhud waislamu walitakiwa kupambana tena na wapagani baada ya kupita mwaka mmoja. Kutokana na mkataba huu Abu Sufyan alienda kwenye mji wa Marru'z Zahran huku akiwakilisha jeshi lake. Hata hivyo hofu iligubika moyo wake na kumlazimu arudi. Kutokana na kuwa hakutaka heshima yake ishuke aliamua kumtuma mtu kwenda Madina kuwaambia waislamu kuwa kuna jeshi kubwa lililojiandaa kwa ajili ya kupambana nao, aliwaambia haya ili kuwahofisha waumini na kuwazuia wasijiingize kwenye vita.

Pindi habari hizi zilipowasili Madina Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa tayari ameshamaliza maandalizi kwa ajili ya vita na alikuwa tayari ameshatoa amri ya kwenda kwenye vita. Yule mtu aliyekuwa ametumwa kupeleka habari Madina alikuwa anafahamu kuwa Abu Sufyan aliyasema yale kwa kuhofia vita na hivyo alitaka kuwahofisha waislamu nao ili wasiende vitani. Mtu huyu naye akajitahidi kadiri ya uwezo wake kuwatia waislamu wasiwasi ili kuwazuia wasisonge mbele. Aliongezea uongo kwenye ule uongo aliopewa aufikishe na aliwaambia waislamu kuwa kama wangelienda vitani nje ya mipaka ya Makka basi mwisho wao ungelikuwa mbaya mno. Kutokana na juhudi zake na juhudi za wanafiki wengine waislamu wengi walianza kupata hofu na hivyo wakasita kwenda vitani. Kutokana na yote haya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaambia:

*"Ninaapa mbele ya Mwenyezi Mungu ambaye anashikilia uhai wangu Mikononi mwake kuwa hata kama hakuna mtu atakayeenda na mimi vitani, nitaenda Badr mimi mwenyewe"*. Baada ya

maneno yale Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akawasaidia waislamu na kuzifanya nyoyo zao imara". (Ibn Sa'd, II, 59; Waqidi, I, 386-387).

❁

Sehemu nyingine ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alionyesha ushujaa ni Hunayn. Siku ile kila mtu alikuwa anawakimbia maadui wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anaendelea kuwafuata akiwa juu ya farasi wake, akiwa hawaangalia maswahaba wake ambao walikuwa wanajaribu kumrudisha nyuma. (Muslim, Jihad, 76).

Anas رضي الله عنه anasimulia:

Katika siku ya Hunayn makabila ya Hawazin, Ghatafan na wengine walienda kwenye uwanja wa vita pamoja na watoto wao na ngamia wao. Siku ile kulikuwa na watu elfu kumi kwenye jeshi la Mtume. Watu wa Makka ambao walikuwa wamesamehewa baada ya kuitwaa Makka pia walikuwa pamoja na Mtume. Hata hivyo vita vilipoanza walianza kurudi nyuma. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliachwa peke yake. Siku ile Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliita mara mbili na hakutoa maneno yoyote kati yake. Mara ya kwanza aligeukia upande wake wa kulia na kuita:

*"Enyi Answar"*. Wakajibu:

"Ndio ewe Mtume. Habari njema ni kwamba tuko na wewe".

Kisha akageukia upande wake wa kushoto na kuita:

*"Enyi Answar"*. Wale waliokuwa upande ule wakaitikia:

"Ndio ewe Mtume. Tuko pamoja na wewe".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amepanda nyumbu mweupe. Alishuka juu yake na kusema:

*"Mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake"*. Baada ya kuyasema haya waislamu walijikusanya wao wenyewe na kuan-

za kupambana na kisha kuwashinda wapagani wote. (Bukhari, Magazi 56, Humus 19, Manaqib 14, Manaqibu al-Ansar 1; Muslim, Zakat 135).

Mtu mmoja alikuja kwa Bara ibn Azib ﷺ na kusema:

"Ewe Abu Umara! Je wote nyinyi mlikimbia katika siku ya Hunayn?"

Bara akajibu:

"Ninatoa ushuhuda kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakukimbia. Lakini wale askari ambao walikuwa na jukumu jepesi na wale ambao walikuwa hawajavaa mavazi ya kivita kwa pamoja walisogea kwenye upande wa Hawazin. Hata hivyo warusha mishale walikuwa wakiwasubiria hivyo wakaanza kuwarushia mishale. Hivyo ikawabidi watawanyike. Jambo hili liliwafanya maadui wamgeukie Mtume. Abu Sufyan ibn Haris ﷺ alikuwa akimkokota nyumbu wa Mtume. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akateremka chini na kuanza kumuomba na kumlilia Mwenyezi Mungu. Alikuwa akisema:

*"Mimi ni Mtume, sio uongo. Mimi ni mtoto wa Abdulmuttalib.*

*. Ewe Mwenyezi Mungu tushushie msaada wako".*

Kisha akawapanga askari wake. Bara akaendelea:

"Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu pale vita vilipopamba moto tulijikinga nyuma ya Mtume. Shupavu kuliko sisi sote aliweza kusimama kwenye mstari mmoja pamoja na Mtume" (Muslim, Jihad 79; Bukhari, Magazi 54, Jihad 52, 61, 97, 167).

❁

Anas ibn Malik ﷺ anasimulia:

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ndiye mzuri kuliko sisi sote, mkarimu na mwerevu kuliko watu wote. Pindi kiliposikika kilio cha hofu ndani ya Madina au ilipotokea hali ya hatari,

upesi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akimuazima farasi wa Abu Talha aliyeitwa Mandub na kwenda kwenye tukio. Hakuna siku tuliyosikia makelele ya hatari ila tulimkuta Mandub kwenye eneo lile kana kwamba ana kasi ya upepo. Usiku mmoja watu wa Madina walisikia makelele, wakaogopa na kuamua kwenda yalipotokea makelele hayo. Hata hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa tayari ameshafika eneo lile na akakutana nao njiani wakati anarudi baada ya kumaliza uchunguzi wake. Aliwaambia maswahaba zake maneno yafuatayo wakati upanga wake uko shingoni mwake:

*"Msiogope! Msiogope!"* na kisha akamzungumzia Mandub: *"Nimegundua kuwa farasi huyu anakimbia kama mafuriko makali".* (Ibn Sa'd, I, 373; Bukhari, Adab, 39).

❁

Maswahaba wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ waliobarikiwa walijitolea muhanga na kuonyesha ushujaa mkubwa wakati wa vita vya Badr. Hasa Hamza ؓ, 'simba wa Mwenyezi Mungu' alikuwa mfano wa kuigwa katika werevu na ujasiri. Alipelekea mmoja wa viongozi wa wapagani aliyeitwa Umayya ibn Halef amuulize Abdurrahman ibn Awf

ambaye alikuwa miongoni mwa maswahaba:

"Ni mtu gani yule ambaye aliweka unyoya wa mbuni kifuani mwake?"

Pindi alipojibiwa kuwa yule alikuwa ni Hamza ibn Abdulmuttalib, alisema:

"Kila tulichofanyiwa tulifanyiwa na yeye" (Ibn Hisham, II, 272).

❁

Pindi mapambano katika vita vya Uhud yalipopamba moto Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichukua upanga wake na kusema:

*"Ni nani atauchukua upanga huu?"* Maswahaba wakajibu:

"Mimi nitauchukua, mimi nitauchukua" na wakanyoosha mikono yao kwa ajili ya kuuchukua. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza kwa mara nyingine tena:

*"Ni nani atauchukua upanga huu na kuupa haki yake?"* Mara maswahaba wakasita kuuchukua.

Abu Dujana ؓ ambaye alikuwa miongoni mwa Answar alinyanyuka na kusema:

"Mimi nitauchukua na kuupa haki yake". (Muslim, Fadhailu as-Sahaba, 128).

Wakati Abu Dujana ؓ alipouchukua upanga ule alimuuliza Mtume:

"Ni ipi haki ya upanga huu ewe Mtume?".

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Haki yake ni kuwa unautumia kupambana na maadui mpaka upinde au uvunjike".*

Abu Dujana aliuchukua upanga ule na kuchukua kilemba chake chekundu na kukifunga kichwani mwake na kisha akaanza kukatisha safu za waislamu na askari wa wapagani kwa kutamba na kujivuna.

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomuona anatembea katika hali hii ya kutamba na kujivuna alisema:

*"Huku ni kutembea ambako Mwenyezi Mungu anakuchukia (wakati mtu akitembea kama hivi kutokana na kujivuna kwa ajili*

*ya nafsi yake) isipokuwa katika mazingira kama haya”.* (Ibn Hisham, III, 11-12).

❁

Shangazi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyekuwa akiitwa Safiyya ؓ alikuwepo kwenye vita vya Handak pamoja na wanawake wengine na watoto. Walikuwa katika jumba kubwa la mbao lililokuwa likiitwa Hari ambalo lilikuwa linamilikiwa na Hassan ibn Thabit. Kundi moja la wayahudi lilikuja na kuanza kurusha mishale kuelekea kwenye jumba lile na kutaka kuingia ndani. Mmoja wao alikuwa akizunguka jumba lile katika kutafuta njia ya kuingilia. Wakati ule Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pamoja na maswahaba zake walikuwa wanapambana na maadui kwenye Handak.

Pindi Safiyya ؓ alipogundua kuwa hakuna wa kuwasaidia dhidi ya tishio lile alijifunga skafu kichwani kwake vizuri na kuchukua mti mkononi mwake, kisha akafungua mlango taratibu na kumsogelea kwa nyuma yule myahudi aliyekuwa analizunguka lile jumba, kisha akampiga kichwani kwa lile jiti alilokuwa amelishika na kumuua pale pale. Pindi wayahudi walipomuona ndugu yao amekufa waliogopa sana na kusema:

“Walituambia kuwa hapa kuna wanawake tu bila walinzi”. Kisha wakatawanyika na kuondoka. (Haythami, VI, 133-134; Waqidi, II, 462).

❁

Khalid ibn Walid ؓ amesema:

“Katika siku ya vita vya Muta nilivunja panga nane kwa mikono yangu. Ni upanga mmoja tu uliokuwa mnene na mpana ambao ulitengenezwa Yemen ndio ulioweza kuhimili” (Bukhari, Maghazi, 44).

❁

Siku moja Harezm ambako palikuwa nyumbani kwa Sufi mkubwa aliyeitwa Najmaddin-i Kubra palishambuliwa na wamongolia. Najmaddin-i Kubra alikuwa ni mtu ambaye alitembea juu ya nyayo za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na maswahaba zake. Kwa kushurikiana na wanafunzi wake waliweka upinzani mkubwa lakini mwishoni walikufa mashahidi. Watu hawa walijulikana kama *alperen*. *Alperen* ni wale watu wanaoishi katika mipaka kwa ajili ya kuilinda na ambao wana shauku ya kufa mashahidi jambo ambalo lina nafasi kubwa katika desturi za *tasawwuf*. Wao ni wawakilishi muhimu wa ujasiri na ushupavu.

❁

Pindi umoja wa jeshi la msalaba lilipoingia kwenye ardhi za dola ya Uthmainiyya kwa lengo la kuwaangamiza watu katika dola ya Uthmainiyya, kuikoa Byzantine na kuichukua Jerusalem ambayo ilikuwa mikononi mwa waislamu, waliahidi kuishinda ngome ya Nigbolu iliyokuwepo kwenye fukwe ya mto Tuna.

Pindi Yildirim Bayazid alipofahamishwa jambo hili upesi alienda Nigbolu haraka kama radi kama lilivyokuwa jina lake[83]. Alienda kwa ajili ya kuwaamuru waislamu wasikubali kuiachia ngome yao. Alipanda farasi katikati ya usiku na kumuendesha kwa kuibia na kukatisha majeshi ya maadui mpaka akaifikia ngome na kisha akamuita kamanda wa ngome ile:

“Angalia Dogan!”

Dogan Bey ambaye aliitambua kwa haraka sauti ya Sultani, alijibu kwa taharuki kubwa:

“Niko kwa ajili yako ewe bwana wangu”

Sultani Yildirim Bayazid alitoa maagizo yake kwa ufupi kama ifuatavyo:

83. Neno *‘yildirim’* linamaanisha radi kituruki (Maelezo ya mfasiri).

"Dogan! Nimekuja hapa pamoja na jeshi langu. Vyovyote itakavyokuwa usije ukaisalimisha ngome hii". Na kisha akarudi kizani na kuondoka. Siku iliyofuata yalitokea mapambano makali dhidi ya jeshi kubwa la msalaba na Yildirim Bayazid akaibuka na ushindi. Mataifa yote ya ulaya makubwa kwa madogo yalikuwa yametuma askari kuungana na jeshi hili. Miongoni mwao walikuwepo mashujaa wa kifaransa elfu kumi ambao walijitamba kwa kusema: "Kama mbingu zitaporomoka basi tutazizuia kwa mikuki yetu". Lakini ushindi haukuwa wao kwani waliyeyuka mbele ya mbinu za dola ya Uthmainiyya zilizoongozwa na imani yao,

Siku ile Yildirim Bayazid alijeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili wake na pindi farasi wake alipojeruhiwa alidondoka chini. Hata hivyo hakujali juu ya hili akapanda farasi mwingine na kuongoza vita kwa nguvu zake zote mpaka walipopata ushindi.

❁

Baada ya ushindi wa Nigbolu, Yildirim Bayazid Han alichukua mashujaa na watu wakubwa kama mateka wa vita. Miongoni mwa mateka wale alikuwepo shujaa maarufu wa kifaransa aliyeitwa Fearless Jean. Yildirim Bayazid Han aliwaachia waende kwa kulipa fidia. Zaidi ni kwamba siku ambayo walikuwa wanarejea katika ardhi zao aliwaandalia karamu. Pindi walipotafakari juu ya ubinadamu wa Sultani na kujilinganisha na wao wenyewe ambao huwa huwatesa na kuwadhalilisha wafungwa wao, wote wakajisikia aibu mno na hivyo wakasema:

"Tunaapa mbele ya heshima yetu kuwa tokea sasa hatutosimama dhidi ya Sultani Anatolia na Rumelia wala hatututatumia panga zetu kupambana nao..."

Kutokana na maneno haya yaliyotolewa kama shukurani Sultani Yildirim Bayazid Han ambaye alikuwa mfano wa kuigwa

katika kuwakabili makafiri, aliwaambia wale mashujaa kwa sauti yenye kuonyesha msisitizo:

"Ninawarudishia kiapo walichokitoa Fearless Jean na marafiki zake kuwa kamwe hawatasimama kupambana na sisi. Hapana! Ninasema nendeni na mkusanye askari wapya na kisha mrudi kupambana na sisi. Fahamuni kuwa kitendo hicho kitatupelekea kupata ushindi mwingine. Kwani mimi ni Sultani ninayetambua kuwa nimekuja hapa duniani ili kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuitukuza dini yake. Hivyo msaada wa Mwenyezi Mungu uko pamoja na sisi. Na ambaye msaidizi wake ni Mwenyezi Mungu hakuna nguvu yoyote inayoweza kumshinda!..."

❁

Pindi Timurlane alipozingira ngome ya Sivas kwa tembo ambao walikuwa ni vifaru vya wakati ule, mtoto wa Yildirim Bayazid Han aliyeitwa Shahzade Ertugrul aliwakusanya watu wenye kuheshimika katika mji na kuwaambia:

"Jukumu langu ni kuwalinda kwa nguvu zangu zote. Vikosi vya Timur vinaweza kuwa imara na vingi kuliko vyetu. Hii ni mipango ya Mwenyezi Mungu. Wajibu wangu ni kupambana nao kwa werevu na kuwalinda nyinyi na hii ngome kulingana na utukufu wetu. Fahamuni kuwa Timur kamwe hawezi kuingia kwenye ngome hii labda juu ya maiti zetu..."

Baada ya Shahzade Ertugrul kuyasema haya alichukua hatua kwa kuchukua kundi la watu shupavu na kusababisha upinzani mkubwa na kupambana na jeshi la Timur kwa werevu mkubwa. Hata hivyo yeye pamoja na mashujaa wake waliuawa na jeshi la maadui ambalo liliwashambulia kama mvua.

Baada ya Tamur kumuangamiza shahzade aliwatumia ujumbe wale waliokuwa ndani ya ngome kuwa kama watajisalimisha

hatomdhuru yeyote. Hata hivyo aliwaua kikatili wale walinzi wa ngome ambao walitoka nje kutokana na kuamini maneno yake.

❁

Tukio lifuatalo ni mfano mwingine wa ushupavu wa askari wa dola Uthmainiyya:

"Kijana mmoja ambaye alikuwa katika kasi kubwa ambaye alikuwa anapeleka habari za ushindi uliotokea Preveze aliingia ndani ya kasri la Topkapi. Pindi alivuta kamba za farasi wake alibakia amesimama na miguu miwili kwa muda. Sultani Suleiman ambaye alikuwa anaangalia tukio hili akamwambia:

"Umekuja na farasi mkorofi kweli!" Yule kijana akasema:

"Sultani wangu! Mediterania kulikuwa na farasi wakorofi, lakini tuliweza kuwafuga", katika kudhihirisha ushupavu wao uliotokana na imani zao.

❁

Wakati wa vita kwa ajili Dardanelles iliamuliwa kuwa Sultani na viongozi wengine wahamishiwe Eskisehir kama tahadhari na kutokana na hofu kuwa maadui wanaweza kuingia katika bahari ya Marmara. Pindi Abdulhamid Han ambaye aliondolewa kwenye kiti chake cha enzi na kuwekwa gerezani katika kasri la Beylerbeyi, alipofahamishwa juu ya matukio haya alikataa na kwa ujasiri na ushupavu akasema:

"Mimi ni mjukuu wa Fatih Sultan Mehmed…! Kamwe sitamnyenyekea Constantine ambaye alikuwa mtawala wa Byzantine, ambaye wakati Fatih anaichukua Istanbul alipambana naye mpaka kufa huku akiwa kiongozi wa kikosi. Kama kweli adui ataingia Dardanelles- Mwenyezi Mungu aliepushe hilo- nitachukua bunduki yangu na kupambana kama askari na ikibidi nife. Adui ataweza kuingia Istanbul juu ya mgongo wa maiti yangu.

Mwambieni kaka yangu Rashad ambaye ni mkuu wa serikali kuwa naye pia asiende popote. Kama yeye na serikali yake wataondoka Istanbul, hawataweza kurejea tena...

Kutokana na msimamo huu Sultani na serikali yake walibakia Istanbul. Kwa namna hii kuondolewa kwa serikali kulizuiliwa.

❁

Msafiri wa kifaransa aliyeitwa A.L. Castellan ameelezea ushupavu wa dola ya Uthmainiyya kama ifuatavyo:

"Imani juu ya qadari imejengeka kwa uimara ndani ya vichwa vya watu ndani ya dola ya Uthmainiyya. Imani hii ndiyo inayowapelekea kuwa mashupavu; na inawaongezea ujasiri na msimamo. Kutokana na kumtegemea kwao Mwenyezi Mungu wapo tayari kuhatarisha uhai wao. Ndio maana hata pale wanapokabiliwa na hatari ya wazi hawakati tamaa.

Wanajirusha wenyewe kwenye panga na silaha nyingine za maadui zao na hata kama miili yao imejeruhiwa, ikiwa bado hawaoni kuwa mauti yao yamefika hawakati tamaa ya kuishi"

❁

Kwa kumalizia ni kwamba daima waumini wanamhofia Mwenyezi Mungu pekee na kutokana na utegemezi wao kwake hawaogopi kitu kingine chochote. Wanatekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu kwa ujasiri na ushupavu. Kwa kutumia ujasiri wao pamoja na uoni wa mbali na utambuzi wanaweza kufanya lolote. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

**"...waliokuwa wakifikisha risala za Mwenyezi Mungu na wanamwogopa Yeye, na wala hawamwogopi yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ndiye atoshaye kuhisabu"** (Al-Ahzab, 33:39).

### *18. Istiqama* (Msimamo)

Kwa maana ya ujumla neno *istiqama* linamaanisha kulielekea lengo lako moja kwa moja bila ya kujitoa wala kusita. Maana yake katika tasawwuf ni kuhifadhi haki na usafi wa mtu bila ya kuuchafua.

Maana nyingine ya *istiqama* ni kuwa mfano wa kuigwa kutokana na kumpenda vilivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kuiga mwenendo wake. Kwa kuongezea tu ni kwamba *istiqama* ni kuishi katika mazingira ya kuifuata Qur'an na *Sunnah,* kujiweka mbali na matamanio na raha za kidunia na kubakia kwenye ibada, kwenye kumtumikia Mwenyezi Mungu na kufahamu siri za kumfahamu Mwenyezi Mungu.

Kama ilivyo kwamba hakuna njia nyingine kinyume na *istiqama* ambayo inamuongoza mtu kwa Mwenyezi Mungu pia vile vile hakuna jambo la msingi zaidi ya kuhifadhi vilivyo *istiqama* yako katika kila hali kama inavyostahiki. Ndio maana *istiqama* katika njia ya Mwenyezi Mungu ni jambo kubwa mno.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapa bishara njema watu wa *istiqama* kama ifuatavyo:

**"Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyo kuwa mkiahidiwa. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinacho tamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyo vitaka. Ni takrima itokayo kwa Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu"** (Fussilat 41:30-32).

**"Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu; kisha wakatengenea, hawatakuwa na khofu, wala hawatahu-**

**zunika. Hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo, kuwa ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyatenda”** (Ahqaf, 46:13-14).

Njia ya watu wa *istiqama* ni *‘sirat al-mustaqim’* au njia iliyonyooka. Qur’an ina yafuatayo ya kusema kuhusu wale ambao wanasafiri katika njia hii iliyonyooka kama inavyostahiki:

“**Na wenye kumt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume, na kuwa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!**” (Nisa, 4:69).

Njia iliyonyooka ni njia ya wale waliochaguliwa. Kiini cha *istiqama* ni imani na uchamungu. Na mahala pa vitu hivi viwili ni moyoni. Kwa namna hii *istiqama* ni amani ya mwili kutokana na hii imani na uchamungu unaopatikana ndani ya moyo. Imani, usafi wa moyo na utulivu wa moyo inahakikisha kuwa *istiqama* inayohitajika inakuwepo wakati wote. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

“Imani haiwezi kutengemaa ikiwa ulimi na moyo havijatengemaa” (Ahmad, III, 198).

Muumini ndani ya dunia hii yenye kupita hana budi kubakia na msimamo na kamwe asitoke katika njia ya haki. Mshairi amelielezea jambo hili vizuri kama ifuatavyo:

*Usimuogope adui kwani hata moto wake hauwezi kukuunguza*
*Kuwa na msimamo na Mwenyezi Mungu hatakuangusha*

***Matukio ya wema***

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuambia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wake maneno yafuatayo kwa niaba ya umma wote:

"**Na ndio kama hivyo ndivyo inavyo kuwa Mola wako Mlezi anapo ikamata miji inapo kuwa imedhulumu. Hakika mkamato wake ni mchungu na mkali**" (Hud, 11:112).

Kutokana na aya hii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema yafuatayo:

"Surat Hud imenizeesha..." (Tirmidhi, Tafsir, 56/3297; Qurtubi, IX, 107).

Abdullah ibn Abbas ؓ amesema yafuatayo kuhusu aya hii:

"Hakujawahi kutokea ujumbe mzito aliopewa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ndani ya Qur'an kuliko aya hii"[84]

Ingawa mwanzoni aya hii ilishushwa moja kwa moja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuwia nzito mno lakini hakuwa anahofia msimamo wake binafsi kwani Mwenyezi Mungu alikuwa ameshamthibitishia msimamo wake kama ifuatavyo:

**"Juu ya Njia Iliyo Nyooka"** (Yasin, 36:4). Kilichomtia wasiwasi zaidi kiasi cha kumzeesha ni kwamba aya hii iliwahusu waumini wote.

❁

Katika hadith Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema yafuatayo:

*"Kuweni na msimamo. Hamuwezi kudhania wa kufahamu (malipo katika) jambo hili. Na fahamuni kwamba amali iliyo bora zaidi ni swala (ya faradhi)..."* (Muwatta, Taharah, 6).

❁

Sufyan ibn Abdullah ؓ anasimulia:

Siku moja nilimwambia Mtume:

84. Nawawi, "Sharhu Sahih-i Muslim", Egypt, 1981, II, 9.

"Ewe Mtume! Nielezee kuhusu Uislamu kiasi kwamba nisihisi hitajio la kumuuliza yeyote mwingine kuhusu Uislamu"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajibu:

*"Sema 'ninamuamini Mwenyezi Mungu' kisha uwe na msimamo"* (Muslim, Iman, 62).

❁

Kutokana na masimulizi ya Anas ؓ siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisoma aya ifuatayo kutoka ndani ya Qur'an:

**"Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakakwaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyo kuwa mkiahidiwa"** (Fussilat, 41:30).

Kisha akasema:

*"Watu wamekuwa wakiyasema maneno haya mara nyingi, lakini baada ya hapo wengi wao wamemkataa Mwenyezi Mungu. Yeyote atakayekufa juu ya maneno haya (yani 'Mola wetu ni Mwenyezi Mungu') atakuwa amekufa katika hali ya msimamo"* (Tirmidhi, Tafsir, 41/3250).

❁

Siku moja mtu mkubwa alikutana na mzee mmoja aliyekuwa amebeba mzigo wa kuni mgongoni mwake na huku anapata shida kutembea. Akamuangalia na kusema:

"Ewe mzee! Je umepoteza uaminifu wako kwa Mwenyezi Mungu kiasi kwamba unajisababishia ugumu kiasi hicho? Au huna mtu wa kukuangalia?"

Yule mzee alitazama juu na kunyanyua mikono yake mbinguni ili arekebishe upungufu wa imani ya yule mtu aliyekuwa akimzungumzisha na kisha akasema:

"Ewe Mlezi wangu! Zibadili kuni hizi na kuwa dhahabu"

Mara tu baada ya kusema maneno yale vile vipande vya kuni vikageuka na kuwa vipande vya dhahabu.

Yule mtu aliyeona muujiza huu mkubwa aliuliza kwa mshangao:

"Kwa nini mtu aliyefikia hali kama hiyo yako bado anaendelea kubeba kuni?". Yule mzee akamjibu:

"Mwanangu! Ninayafanya haya ili nafsi yangu ifahamu kuwa mimi ni mtumwa na isipelekee kuvuka mipaka ya utumishi kwa Mwenyezi Mungu. Kwani kukubaliwa kwa utumishi wa mtu mbele ya Mwenyezi Mungu kunatokana na kiwango cha msimamo wake..."

❁

Bayazid-i Bistami amesema:

"Kama itatokea kumuona mtu anaelea angani huku amekunja miguu yake, usiamini kuwa huo ni muujiza mpaka umuone mtu anachunga maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu na anafuata *sunnah* na anahukumu katika njia ya Mwenyezi Mungu"

❁

Bayazid-i Bistami amesema tena:

Siku moja nilivuka mto Dijla. Pindi nilipoukaribia kingo zake mbili zilikutana na kuniruhusu kupita juu yake kwenda upande wa pili. Kisha upesi nikajikusanya na kuuambia mto:

"Ninaapa kuwa kamwe siwezi kudanganyika kutokana na jambo hili. Watu wenye mashua wanavusha watu kwa nusu sarafu ya fedha. Na mimi nina miaka 30 katika amali zangu. Hivyo siwezi kupoteza miaka yangu 30 ya amali njema nilizoziandaa kwa ajili

ya siku ya kiama kwa nusu ya sarafu. Ninachohitaji kwa sasa ni Mwenyezi Mungu ambaye ni mwingi wa ukarimu na si muujiza".

❁

Siku moja wanafunzi wa Shaykh Nakshibend walimuomba awaonyeshe muujiza. Akawaambia:

"Miujiza yetu iko wazi. Niangalieni mimi, licha ya mzigo mkubwa wa madhambi ulioko mabegani mwangu lakini bado ninasimama na kutembea juu ya ardhi. Je kuna muujiza mwingine mkubwa kuliko huu?"

Baada ya pale katika kuwakumbusha kuwa jambo la msingi katika tasawwuf haikuwa kuonyesha miujiza bali kuwa katika msimamo alisema:

"Kama mmoja wenu ataingia katika bustani na kusikia majani ya miti yakimsemesha kwa kusema: 'Salamu ewe rafiki wa Mwenyezi Mungu', wala usidanganyika na kuitafakari sauti hii kwa wazi ama kwa siri. Kinyume chake wakati huo utambuzi na juhudi za mja ziongezeke".

Kisha baadhi ya wanafunzi wake wakasema:

"Mwalimu, kadiri unavyojitahidi kuificha, mara nyingi baadhi ya miujiza yako inakuwa wazi kwetu..."

Kisha mtu yule ambaye ni mfano wa kuigwa katika unyenyekevu akasema:

"Vitu hivyo mnavyovishuhudia ni miujiza ya wanafunzi wangu".

Mtu huyu alikuwa katika ya unyenyekevu mkubwa, ikimaanisha kuwa alitaka kuficha undani wake wa imani. Ndio maana hakumruhusu mwanafunzi wake aliyeitwa Husameddin Haja Yusuf aandike miujiza yake na maneno yake wakati bado yupo hai.

Watu wema katika Uislamu waliweza kufikia katika madaraja ya juu si kwa kupitia miujiza yao bali kwa kushikamana na misingi ya msimamo.

Walionyesha kuwa miujiza yao haikuwafanya wawe bora kuliko ndege wanaopaa angani au samaki wanaoogelea majini. Bali walionyesha kuwa jambo bora si kuwaiga ndege na samaki, bali ni kuishi kwa kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa utambuzi mkubwa wa utumishi wako kwake. Pia walilionyesha hili katika matendo yao na tabia zao.

Haya ni kwa sababu hawakutaka kujionyesha, marafiki wa Mwenyezi Mungu hawaonyeshi miujiza yao mpaka itokee sababu fulani. Wanajiweka katika hali kuwa watu wa mfano katika tabia njema ambayo watu wengine wanaweza kuifuata.

Ushauri ufuatao uliotolewa na Hasan-i Basri juu ya miujiza ni muhimu kuuchukua:

"Usidanganyike kwa kiwango chako kikubwa cha ufahamu, wadhifa na busara. Kumbuka ni nini kilimtokea Bel'am ibn Baura ambaye alifikia hali ya kuweza kusoma *Lawhil Mahfudh* [85] ya Mwenyezi Mungu.

Kisa cha jambo hili kimetolewa ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

"**Na wasomee khabari za yule ambaye tulimpa Ishara zetu, naye akajivua nazo. Na Shet'ani akamuandama, akawa miongoni walio potea. Na tungelitaka tungeli mtukuza kwa hizo Ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimwacha pia hupumua na kutoa ulimi.**

85. *Lawhil mahfudh* ni ubao ambao ndani yake umeandikwa ujuzi wote wa Allah (Maelezo ya mfasiri).

**Huo ni mfano wa kaumu wanao zikanusha Ishara zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatatafakari**" (A'raf, 7:175-176).

Mawlana Khalid-i Baghdadi amesema:

"Kuwa na msimamo na kufanya juhudi katika njia ya Mwenyezi Mungu ni bora kuliko kuonyesha miujiza mingi na kuvumbua siri ya vitu visivyoonekana. Na kwa kuongezea ni kwamba kama gunduzi hizi na miujiza hii si sababu ya kumuongezea mtu ari ya kushikamana na maamrisho ya dini, basi si chochote bali ni kujisababishia matatizo na madhara".

❁

Muhammad Asad (Mwenyezi Mungu amrehemu) ametahadharisha juu ya umuhimu wa msimamo hasa kwa wale watu wenye nyadhifa kubwa:

"Ama awe ni mwanachuoni au Sheikh , yeyote ambaye hatajivika kilemba cha msimamo kichwani mwake ataishia kwenye maangamizi.

Kama mgongo wako haujatwikwa mzigo wa msimamo je mshale wako wa matamanio ya kumkurubia Mwenyezi Mungu utalenga shabaha?" (Divan, Istanbul, 1991, uk 27).

Kama suala la msimamo liliwafanya wale marafiki wa Mwenyezi Mungu pamoja na miujiza yao watetemeke kwa hofu basi na sisi waumini dhaifu hatuna budi kutafakari juu ya umuhimu wake...

❁

Kwa ufupi ni kwamba msimamo ni jambo la lazima kwa kila muumini. Hata hivyo ni vigumu mno kuupata na kuuchunga. Mtu kufikia malengo yake kunatokana na kiwango cha juhudi yake katika kuutafuta msimamo, na hivyo wale watu wenye msimamo

watapata heshima kubwa na malipo yasiyo na mwisho kutokana na juhudi yao.

**19. Shukurani na utii**

Shukurani na utii ni miongoni mwa alama muhimu za Uislamu. Hizi ni miongoni mwa sifa zinazomfanya mtu kuwa mwanadamu. Hizi ni sifa za kiimani ambazo utazikuta kwa Mitume, watu wema na watu wenye maadili mazuri na humpandisha mwanadamu katika daraja la juu kabisa. Sifa hizi ni kipimo cha thamani ya mtu ambacho wanapewa wale wanaopendwa na wale wanaostahili kupendwa. Wale wasio na hisia za utii ni watu wabinafsi ambao wanazifikiria nafsi zao, furaha yao na manufaa yao.

Kwanza kabisa mwanadamu hana budi kumtii Mola wake. Hili linaweza kutekelezwa kwa kufuata maamrisho yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema yafuatayo ndani ya Qur'an:

"**Wala msiwe kama wale walio msahau Mwenyezi Mungu, na Yeye akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio wapotovu**" (Al Hashr, 59:19).

Baada ya kuonyesha utii kwa Mwenyezi Mungu, anayestahili zaidi utii baada ya Mwenyezi Mungu ni Mtume. Utii huu ni udhihirisho wa shukurani yako kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye kipaumbele chake ilikuwa ni umma wake kama alivyolidhihirisha hili katika dua zake kwa Mwenyezi Mungu *"Umma wangu, umma wangu"*. Utii huu ambao huanza pale ambapo hisia za mtu za upendo kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ zinapoongezeka, na hili linawezekana pale ambapo mtu atashikamana na *sunnah.*

Kila mtu hana budi kujipamba na hisia za utii kwa watu wakubwa katika dini hii, yani marafiki wa Mwenyezi Mungu. Kwani hawa marafiki wa Mwenyezi Mungu ndio waliosambaza

maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake na mwenendo wake mzuri mpaka kwetu.

Wale ambao tunalazimika kuwaonyesha utii si wale tu waliokwishatajwa. Kinyume chake ni kwamba tunalazimika kujenga utii ndani ya nyoyo zetu juu ya marafiki zetu na ndugu zetu katika imani. Pia hatuna budi kuonyesha uaminifu kwa mababu zetu, walio hai na waliokufa, nchi yetu na amana tulizoaminiwa kwazo, kwani zote hizi ni sifa za tabia njema na utu.

Jalaluddin Rumi ameelezea vizuri ubora wa kushukuru na utii kama ifuatavyo:

"Tabia kama vile upendo na urafiki zote zinategemea uaminifu na daima zinamtafuta mtu mtiifu. Kamwe hazikai katika moyo usio na utii.

Kalamu iliandika: "Malipo ya utii ni utii; na malipo ya ukali ni ukali" na kisha wino ukakauka.

Sultani alikuwa akikata kichwa cha yeyote aliyemsaliti hata kama alikuwa ni mwanae. Na kama mtumwa kutoka India angelitakiwa kuonyesha utii kwa Sultani basi nyoyo za watu wengine zingelimtii mtumwa yule na kumridhia...nafasi ambayo wasingeliweza kupewa mawaziri mia moja.

Na hata kama mtumwa huyo angelikuwa mbwa mtiifu aliye mlangoni basi mmiliki wa mbwa huyo angelijisikia raha na kuridhika na mbwa huyo mara mia moja zaidi na mmiliki wake angelimpapasa kwa mahaba..."

### *Matukio ya wema*

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Mimi ni matokeo ya dua ya Ibrahim, bishara njema za ndugu yangu Issa, na ndoto ya mama yangu Amina*[86]*"*. Baada ya kuyasema haya alidhihirisha utii mkubwa juu yao.

Katika mwaka uliofanyika mkataba wa Hudaybiya siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiwa katika safari ya kwenda Makka kwa ajili ya kutekeleza ibada ya umra alipita karibu na Abwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuomba Mwenyezi Mungu ruhusa ya kutembelea kaburi la mama yake (ambalo lilikuwa Abwa). Akasawazisha kaburi la mama yake kwa mikono yake iliyobarikiwa na kisha akaanza kulia kwa huzuni. Waislamu waliomuona nao wakaanza kulia. Kisha wakamuuliza ni kwa nini alifanya vile na yeye akawajibu:

*"Nilikumbuka upendo na huruma alionionyesha mama yangu vikanifanya nilie"* (Ibn Sa'd, I, 116-117; Pia angalia Muslim, Janaiz, 105, 108).

❁

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipoibariki dunia kwa kuja kwake, mwanamke aliyejulikana kwa jina la Suwayba Hatun ambaye alikuwa na mtoto aliyeitwa Masruh alimnyonyesha kwa muda fulani[87]. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye ni mfano wa kuigwa katika utii alimjali sana Suwayba Hatun pindi alipokuwa mkubwa. Pindi wote Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na mkewe bi khadija walipokuwa ndani ya Makka walimtendea wema Suwayba na kumpa vitu vingi. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipohamia Madina alikuwa akimtumia Suwayba Hatun chakula

86. Ahmad, V, 262; Hakim, II, 453. Nabii Ibrahim alimuombea Mtume Muhammad ﷺ dua ifuatayo: **'Ewe Mola Mlezi wetu! Waletee Mtume anaye tokana na wao, awasomee Aya zako, na awafundishe Kitabu na hikima na awatakase'** (Al Baqara, 2:129). Nabii Issa (amani iwe juu yake) alitoa bishara njema juu ya Mtume ambaye atakuja baada yake na ataitwa 'Ahmad' (as Saf, verse). Siku moja Amina ambaye ni mama wa Mtume aliona kwenye ndoto nuru iliyotoka kwake na kuangaza ulimwengu mzima kabla Mtume hajazaliwa. (Ibn Sa'd, I, 102).

87. Ibn Sa'd, I, 108

na nguo na kuendelea kutosheleza mahitaji yake. Katika mwaka wa saba tokea wahamie Madina na wakati wanarejea kwenye msafara kutoka Haybar Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipewa taarifa juu ya kifo cha Suwayba Hatun. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliuliza:

*"Mwanae Masruh anafanya nini?"*

Alipokea jibu kuwa:

"Alifariki kabla ya mama yake".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akauliza kama kulikuwa na ndugu zao wengine ambao walikuwa hai, akaambiwa kuwa hakukua na yeyote aliyebaki. (Ibn Sa'd, I, 108, 109).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwajali ndugu zake aliochangia nao ziwa katika maisha yake yote. Kila alipokuwa akimuona mama yake mlezi, Halima Hatun (ambaye alimnyonyesha alipokuwa mdogo), alikuwa akimuita: *"Mama mpendwa, mama mpendwa"* na kisha alimuonyesha upendo mkubwa na heshima. Alikuwa anafikia kutandika shuka lake ili akae na kutekeleza kila alilolitaka.

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa amekaa ndani ya nyumba yake alitembelewa na mume wa mama yake mlezi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ upesi akatandika sehemu ya nguo yake chini ili mgeni wake akalie. Baada ya muda mfupi mama yake mlezi naye pia akaja. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasimama kwa ajili yake na kumkalisha huku yeye yuko nyuma yake. (Abu Dawud, Adab, 119-120/5145).

Siku moja Halima Hatun alikuja Makka kwa ajili ya kumuona Mtume. Wakati ule Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amemuoa bi Khadija. Walimpokea Halima Hatun kama mgeni

wao. Halima aliwapa taarifa juu ya ukame, upungufu wa chakula na hatari iliyokuwa juu ya wanyama wao katika ardhi yao kwa wakati ule. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipomuambia mkewe juu ya hali aliyokuwa nayo yule mama yake mlezi, alimuandalia zawadi ya kondoo arobaini na ngamia wa kwenda nao na mzigo juu yake. Kwa namna hii Khadija alionyesha utii wake kwa Mtume wetu. (Ibn Sa'd, I, 114).

❁

Katika kipindi cha kuitwaa Makka wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yupo katika eneo la Abtah, dada yake Halima Hatun aliendा kumtembelea. Akamuandalia zawadi miongoni mwake ikiwemo jibini ya machunda ya maziwa na siagi. Upesi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaulizia hali ya mama yake mlezi. Alipomjibu kuwa alikuwa ameshafariki, macho ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yakajawa na machozi. Alimuuliza ni nani aliyekuwa ameachwa. Kisha baadae akaamuru mwanamke huyu apewe nguo za kuvaa, zawadi ya ngamia na dirham 200 za sarafi za fedha. Wakati anarudi kwenye nchi yake huku akiwa na furaha tele alisema:

"Ajabu iliyoje ya wewe ndugu yangu wakati ulipokuwa mdogo na sasa wakati umeshakuwa mkubwa" (Waqidi, II, 869; Beladhuri, I, 95).

❁

Pamoja na ushindi na ngawira zilizopatikana baada ya vita vya Hunayn pia walipatikana watumwa wengi. Miongoni mwa watumwa hawa alikuwemo dada aliyelelewa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyeitwa Shayma.

Aliagiza aletwe kwake na kisha akavua vazi lake la juu na kulitandika kwa ajili yake. Alionyesha ukarimu mkubwa kwa dada yake huyu ambaye alilelewa pamoja naye walipokuwa Badiye na hivyo alimkaribisha vizuri na kumkirimu. Alipokumbuka siku zao za utotoni macho yake yalijawa na machozi. Alimuuliza kuhusiana

baba yake na mama yake. Shayma akamfahamisha kuwa walikuwa wameshakufa. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamuuliza kuhusiana na ndugu zake wengine na kusema:

*"Kama unataka unaweza kubaki na mimi na hivyo ukapokea upendo na heshima. Na kama unataka ninaweza kukupatia bidhaa na ukarudi nazo kwenye kabila lako. Nitayafanya haya kwa ajili yako".*

Shayma akajibu:

"Nipatie bidhaa na uniruhusu nirejee kwa watu wangu". Baadae aliingia kwenye Uislamu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimpatia Shayma Hatun na wale ndugu zake waliokuwa bado hai ngamia na ng'ombe. Pia alimpatia mtumwa wa kike na wa kiume, watumwa ambao baadae aliwaruhusu waoane wenyewe. (Ibn Hisham, IV, 101; Waqidi, III, 913).

Baada ya muda mfupi alitangaza kuwa amewaachia huru wale watumwa walioangukia kwake na wana wa Abdulmuttalib wakiwemo ndugu zake waliochangia naye ziwa. Kisha akawaambia maswahaba zake:

*"Yeyote miongoni mwenu anayetaka kuwaridhisha ndugu zake kwa kuwaachia huru watumwa bila ya fidia na kwa ajili ya wema basi na afanye hivyo. Na yeyote asiyetaka kuwaachia huru wale watumwa walioangukia kwake waende bila ya kulipwa fidia basi tutawalipa kwa ngawira ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia kuzipata ili wawaachie huru. Kila mtu afanye atakacho..."*

Katika kuonyesha wema wa hali ya juu maswahaba wakasema:

"Na sisi pia tunaahidi kumpa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ watumwa wetu" (Bukhari, Maghazi, 54; Ibn Hisham, IV, 134-135).

Siku ile maelfu ya mateka wa vita walirudishwa kwa Hawazin bila ya kulipa chochote. Kutokana na upendo wa Mjumbe wa

Mwenyezi Mungu ﷺ maelfu ya watu walihuishwa na kubarikiwa kwa imani na hivyo wakarudishiwa uhuru wao.

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipofikisha miaka sita alienda Madina pamoja na mama yake kwa ajili ya kutembelea kaburi la baba yake. Wakati wanarudi mama yake naye akafariki katika kijiji cha Abwa. Hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaachwa yatima na hivyo akarejea Makka pamoja na mtumishi wao Ummu Ayman ﵂.

Katika kipindi chote cha maisha yake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akimtembelea mtumishi wao Ummu Ayman na alikuwa akimuita *"mama"*. Alikuwa akimpa kipaumbele na kumuonyesha upendo mkubwa na heshima na akisema: *"Yeye ni mama yangu baada ya mama yangu. Yeye ndiye pekee aliyebakia katika watu wa nyumba yangu"*.

❁

Mke wa Abu Twalib aliyeitwa Fatima Hatun alikuwa ni mwanamke mwema sana. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuhamia Madina alikuwa akimtembelea mwanamke huyu mara kwa mara na alikuwa akipata usingizi wake wa mapema asubuhi katika nyumba yake. (Ibn Sa'd, VIII, 222).

Pindi Fatima Hatun alipoaga dunia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alilia na kutokwa na machozi kutoka kwenye macho yake yaliyobarikiwa kama matone ya lulu. *"Leo mama yangu amefariki"* alisema, na kisha akafanya shati lake kuwa sanda yake. Alimuombea katika mazishi yake na kulala juu ya kaburi lake kwa muda. Alipoulizwa juu ya sababu ya kufanya kitendo hiki alijibu:

*"Baada ya Abu Twalib hakuna mtu mwingine ambaye alikuwa mwema kwangu kama alivyokuwa mwanamke huyu. Nimelifanya*

*shati langu kuwa sanda yake ili aje kuvaa mavazi ya peponi huko mbinguni. Na nililala juu ya kaburi lake ili lipate joto kwa ajili yake".*

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akiwaambia wale walioshangazwa na kuhuzunika kwake juu ya kifo cha Fatima Hatun:

*"Yeye alikuwa mama yangu baada ya mama yangu. Pindi watoto wake walipokuwa na njaa na kukunja nyuso zao yeye alikuwa ananilisha mimi kwanza, kisha anachana nywele zangu na kunipaka mafuta ya waridi. Yeye alikuwa mama yangu".* Kisha alimuombea kama ifuatavyo:

*"Namuomba Mwenyezi Mungu akusamehe na akulipe wema. Namuomba Mwenyezi Mungu akuhurumie ewe mama yangu mpendwa. Ulikuwa mama yangu baada ya kumpoteza mama yangu. Ulikuwa ukishinda na njaa ilimradi mimi nile. Ulikuwa ukinifadhilisha mimi niweze kuvaa (na bila kujiangalia wewe kwanza). Ulikuwa ukinionjesha neema tamu mno na kujinyima mwenyewe. Na ulikuwa ukiyafanya haya kwa lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kupata pepo..."* (Hakim, III, 116-117; Haythami, IX, 256-257; Ya'qubi, II, 14).

❁

Aisha anatuambia juu ya utii aliouonyesha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwa mke wake wa kwanza Khadija رضي الله عنها:

"Sikumuonea wivu mke yeyote miongoni mwa wake za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ zaidi ya ilivyokuwa kwa Khadija. Na hata sikuwahi kumuona. Hata hivyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akimkumbuka mara kwa mara. Kila alipochinja kondoo alikuwa akiwatumia marafiki wa karibu wa Khadija vipande kadhaa. Wakati mwingine nilikuwa nikimwambia:

"Ni kama hakuna mwanamke mwingine katika dunia hii isipokuwa ni Khadija". Kisha alikuwa akianza kutaja wema wake akisema:

*"Yeye alikuwa hivi na hivi..."* na kisha alikuwa akisema: *"Yeye alikuwa mama wa watoto wangu"* (Bukhari, Manaqibu al-Ansar', 20; Muslim, Fadailu as-Sahaba, 74-76).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipokuwa anatoa amri ya kuwazika mashahidi wa vita vya Uhud alisema yafuatayo kuhusiana na Amr ibn Jamuh رضي الله عنه na Abdullah ibn Amr ibn Haram رضي الله عنه:

*"Hao wawili walisimama bega kwa bega katika safu moja na walikuwa marafiki mno. Walazeni katika kaburi moja mashahidi hawa wawili ambao walipendana sana, walazeni wakaribiane"*. (Ibn Hisham, III, 49; Ibn Sa'd, III, 562).

Uzuri ulioje wa utii ulioonyeshwa hapa...

❁

Kulikuwa na mwanamke mweusi ambaye alikuwa akifagia msikiti wa Mtume. Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakumuona. Alikuwa na shauku ya kujua na hivyo akaulizia alipokuwa. Walimwambia kuwa tayari ameshaaga dunia. Akiwa mfano wa kuigwa katika utii, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Kwa nini msingenitaarifu?"* Baadae akasema: *"Nionyesheni kaburi lake"* na kisha akaenda kwenye kaburi lake na kumswalia swala ya maiti. (Bukhari, Janaiz, 67).

❁

Miaka mingi ilipita baada ya kuhamia Abyssinia. Siku moja misafara ya mtawala wa Abyssinia ilienda kwa Mtume. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwasikiliza kwa makini mno na kuwa-

kirimu yeye mwenyewe. Maswahaba zake walimwambia kuwa wao wangeliweza kuwahudumia lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatoa jibu lifuatalo lenye maana kubwa:

*"Watu hawa waliwaonyesha sehemu ya kuishi wale maswahaba waliohamia Abyssinia na pia waliwaonyesha ukarimu mkubwa. Na sasa nataka kuwahudumia na wao"* (Bayhaqi, Shuabu al-Iman, VI, 518, VII, 436).

❁

Mfalme wa Uhabeshi aliyekuwa Abyssinia aliiaga dunia ndani ya mwezi wa Rajab baada ya kurudi kutoka Tabuk. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwapa maswahaba zake taarifa za kifo cha mfalme huyu siku ile ile na kisha akasema:

*"Mswalieni swala ya maiti ndugu yenu huyu aliyefariki katika ardhi ya mbali"*. Maswahaba zake wakamuuliza:

"Ewe Mtume. Yeye ni nani? Akawajibu:

*"Ni mfalme wa Uhabeshi anayeitwa Ashama. Leo Ashama ambaye ni mja mwema wa Mwenyezi Mungu ameiaga dunia. Muombeeni ndugu yenu msamaha kwa Mwenyezi Mungu"*. Kisha akamswalia wakati yeye hayupo. (Muslim, Janaiz 62-68; Ahmad, III, 319, IV, 7).

Baadae waligundua kuwa yule mfalme aliaga dunia siku ile ile ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwapa taarifa.

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alibakia Makka kwa muda wa siku kumi na tano baada ya kuitwaa. Katika kipindi hiki baadhi ya Answar kutoka Madina walidhania kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anaweza asirudi Madina. Kwani Mwenyezi Mungu alimjaalia yeye kuweza kuitwaa ardhi ile tukufu na iliyobarikiwa, ardhi ambayo ndimo alipozaliwa na kukulia. Mjumbe wa Mwenyezi

Mungu ﷺ alipokuwa anaswali juu ya kilima cha Safa alihisi shauku hii ya Answar na hivyo baada ya kumaliza swala yake aliwafuata na kuwaambia:

*"Ni kipi hicho mnachokiongelea?"*

Walipotoa wasi wasi wao Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwaambia yafuatayo katika kuonyesha utii wa hali ya juu:

*"Enyi Answar! Ninajikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kufanya jambo hilo. Nilihamia kwenye ardhi yenu, Maisha yangu ndio maisha yenu; na kifo changu kitakuwa upande wenu".*

Baada ya maneno haya wasi wasi wa Answar ulitoweka. (Muslim, Jihad, 84, 86; Ahmad, II, 538).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuwasahau kamwe wale maswahaba zake waliopigana kwa ajili ya Uislamu kwa mali zao na nafsi zao, wala hakuwasahau wale maswahaba zake ambao walikufa mashahidi katika harakati hizi. Mara kwa mara alikuwa akizuru makaburi ya Baqi na makaburi mengine ambayo mashahidi walilala na kuwaombea. Maswahaba zake wanasimulia kama ifuatavyo:

"Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipanda juu ya mimbar. Baada ya kutoa shahada *(Ninashuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mjumbe wake)*, kitu cha kwanza ilikuwa ni kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe mashahidi wa vita vya Uhud". (Ibn Sa'd, II, 228).

Baada ya pale katika kuonyesha utii kwa Answar alisema:

*"Enyi watu. Watu wengine wanaongezeka wakati Answar wanapungua kiidadi. Ukweli ni kwamba watakuwa wachache kwa kiasi kama chumvi katika chakula. Yeyote miongoni mwenu ambaye atafikia katika nafasi ambayo atakuwa na uwezo wa kuwanufaisha*

*au kuwadhuru watu, basi na awafanyie wema Answar kutokana na wema wao na awasamehe miongoni mwao ambao wamewakosea”* (Bukhari, Manaqibu al-Ansar, 11).

*“Ninawashauri muwatendee wema Answar. Wao ni watu wangu, wasiri wangu na wadhamini wangu. Wametekeleza majukumu yote waliyopewa. Hawajapata malipo yote ya huduma yao (Watalipwa mara nyingi zaidi kesho akhera). Ndio maana hamna budi kuukubali wema walioufanya na muwakataze wasifanye maovu”* (Bukhari, Manaqibu'l Ansar, 11).

❁

Pia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakusahau kamwe muhanga waliojitolea Muhajirina na wakati anawapangia majukumu mbalimbali maswahaba zake alihakikisha wakati wote anawaangalia wale waliouunga mkono Uislamu tokea mwanzo. Miongoni mwa hawa Abu Bakr ؓ alikuwa ana nafasi maalum. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alionyesha shukurani zake kwake kama ifuatavyo:

*“Tumewalipa jaza yao wale wote waliotutendea wema, ama sawa sawa au kwa kuwazidishia. Lakini kwa Abu Bakr si hivyo. Amefanya wema mkubwa mno kiasi kwamba Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ndiye atakayemlipa jaza yake siku ya kiama. Hakuna mali ya mtu mwingine iliyokuwa na manufaa kwangu kuliko ilivyokuwa mali ya Abu Bakr. Kama ningelitakiwa kuchagua rafiki wa karibu ningelimchagua Abu Bakr. Fahamuni kwamba rafiki yenu (huku akijiashiria yeye mwenyewe) ni rafiki wa karibu wa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi”* (Tirmidhi, Manaqib, 15/3661).

❁

Abu Bakr ؓ alipokuwa khalifa alitangaza kuwa yeyote aliyekuwa ameahidiwa chochote na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ

aende akachukue na hivyo akawalipa watu hawa kwa mali iliyotoka Bahrain. (Bukhari, Kafale, 3).

Baada ya kifo cha Mtume, Ali ﷺ naye alitangaza kuwa:

"Yeyote aliyekuwa ameahidiwa kitu chochote na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ au anayemdai chochote Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aje kwangu kuchukua". Wakati alipokuwa hai alikuwa haachi kumtuma mtu aende Mina katika siku ya kuchinja na kuendelea kutoa tangazo hili. Alikuwa akimpa mtu anayekuja kwake chochote anachotaka. Hivi hivi na mwanae Hasan aliyafanya haya kama alivyofanya mwanae Hussein mpaka alipouawa. (Ibn Sa'd, II, 318).

❁

Abdullah ibn Omar ﷺ alikuwa maarufu katika utii wake juu ya kumbukumbu ya Mtume. Baada ya kifo cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ Abdullah ibn Omar ﷺ alikuwa akitembea juu ya njia ile ile aliyoitembelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumfikiria yeye. Alikuwa akikaa na kukumbuka namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyokuwa amekaa chini ya mti ule ule ambao alikaa chini yake kwa ajili ya kupumzika. Alikuwa anahakikisha kuinyeshelezea miti hii popote ilipokuwa kama ni juu ya mlima au katika tambarare ili isikauke. Yote haya yalikuwa ni ushahidi wa utii wake katika kumbukumbu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwake ﷺ .

❁

Fariduddin Atar anaelezea hali ya wale ambao wanasahau neema walizopewa na Mwenyezi Mungu na kuonyesha kutokuwa waaminifu kwa kuwa watumwa wa matamanio ya nafsi zao:

Wakati fulani kulikuwa na mbwa kwa ajili ya kuwindia ambaye alimvutia sana Sultani. Alikuwa ni mwenye kipaji na mtaal-

amu wa kuwinda. Sultani alimthaminisha na kumpenda sana na alikuwa akienda naye katika kila msafara wa kuwinda. Alimuwekea shingoni mwake kola iliyopambwa kwa vito na alikuwa akimvalisha bangili za dhahabu na fedha katika vifundo vyake vya miguu. Mgongo wake ulifunikwa kwa kitambaa kilichofumwa kwa nyuzi za fedha na hariri.

Siku moja Sultani alimchukua tena huyu mbwa na kwenda naye kuwinda pamoja na watu wengine katika kasri. Sultani alikuwa na matumaini makubwa juu ya mbwa yule wakati anasonga mbele juu ya farasi wake na huku ameshikilia kamba ya hariri aliyokuwa amefungiwa mbwa yule. Lakini mara akaona kitu ambacho kiliondoa furaha yake. Mbwa aliyekuwa anampenda sana alimsahau yeye na akawa ameshughulishwa na kitu kingine. Huku akiwa na huzuni kubwa Sultani akavuta kamba lakini mbwa akakataa na akawa anaendelea kuung'ata mfupa uliokuwa mbele yake. Kutokana na hisia za mshangao na hasira Sultani alisema:

"Unawezaje kusimama hapo mbele yangu na huku unashughulishwa na kitu kingine na kunisahau mimi moja kwa moja?"

Alikuwa katika huzuni kubwa. Utovu wa nidhamu na ukosefu wa hisia aliouonyesha mbwa yule ulimgusa mno. Hakutarajia kuja kumsamehe ingawa alikuwa ni mbwa tu. Kitendo hiki cha kutomtii kilitosha kumvunja moyo na kilikuwa kitendo kisichoweza kusameheka kutokana na heshima aliyompa na vitu alivyompa na sasa anamsahau kwa kipande cha mfupa. Alisema yafuatayo kwa hasira:

"Muacheni kiumbe huyu asiyekuwa na adabu aende zake"

Yule mbwa alielewa hasira za yule Sultani lakini alikuwa amechelewa na hana chochote cha kufanya. Wale watu waliomzunguka Sultani walimwambia:

"Sultani wangu. Tuache kwanza tumuondolee vito, dhahabu na fedha ndio tumuache aende". Hata hivyo Sultani alijibu:

“Hapana, muacheni aende kama alivyo” na kisha akaongezea:

“Muacheni aende kama alivyo. Muacheni aende na abakie mpweke kwenye jangwa kubwa, lenye kuunguza na tupu na huku akiwa na njaa na kiu; muacheni aende akakumbuke neema na vitu mbalimbali alivyoviacha na hivyo aendelee kuishi kwa maumivu...”

Kisa hiki kina mafunzo katika kutuambia zitakavyokuwa hali za wale watu wasio waaminifu ambao wanasahau neema nyingi walizojaaliwa na Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi, bila ya kuzithamini na kinyume chake wakajiangamiza wenyewe kwa faida ndogo na yenye kupita ya hapa duniani.

❁

Kazi ya kupamba kuba ya msikiti wa Sultani Suleiman alipewa mkaligrafia aliyeitwa Karahisari. Karahisari alianza kazi yake kwa juhudi kubwa katika kufananisha fani yake ya kaligrafia na mvuto wa msikiti. Alijitolea kwa kiasi kikubwa mno katika jukumu lake hili kiasi kwamba wakati anamalizia alikuwa tayari ameshapoteza nuru ya kuona katika macho yake.

Pindi msikiti ulipoisha na ukawa unakaribia kufunguliwa kwa ajili ya kufanyia ibada Sultani Suleiman alisema:

“Heshima ya kufungua msikiti wetu kwa ajili ya kufanyia ibada iende kwa mkuu wa usanifu majengo, Sinan, ambaye aliusanifu na kuujenga katika namna yenye kupendeza sana”

Msanifu majengo yule ambaye aliianza kazi yake kwa kujifunza unyenyekevu kwanza alifikiria muhanga aliojitolea mkaligrafia Karahisari na hivyo akamjibu Sultani kwa adabu kama ifuatavyo:

“Ewe Sultani wangu! Mkaligrafia Karahisari alijitolea muhanga macho yake ili kuupamba msikiti huu kutokana na utaalamu wake; matokeo yake amekuwa kipofu. Tafadhali iache heshima hii iende kwake...”

Kisha Sultani Suleiman kwa kuonyesha shukurani kubwa na katika kuwawakilisha wale waliokuwepo pale akamchagua Karahisari afungue msikiti.

❁

Mwalimu wangu wa kiajemi ambaye kwa sasa ni marehemu na ambaye mwanzoni alikuwa mkiristo lakini akaingia kwenye Uislamu baada ya kusoma Mathnawi ya Jalaluddin Al-Rumi na kuchukua jina la Yaman Dede, pindi alipoulizwa sababu ya mapenzi yake kwa Rumi alijibu:

"Mwanangu, Jalaluddin Rumi alinishika mkono na kuniongoza mpaka kwenye mlango wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliyebarikiwa, yeye ndio sababu ya mimi kuingia kwenye Uislamu. Kwa mimi kumkumbuka mtu aliyeniokoa na Moto kwa kiasi hiki hakutoshi kabisa".

Uzuri ulioje wa utii na upambanuzi huu wa fikra...

❁

Baba yetu na mwalimu wetu Musa Efendi alijulikana miongoni mwa wale waliompenda kama *'Sahibu'l Wafa'*, yani bwana wa utii. Tunaweza kusimulia mifano michache miongoni mwa mifano mingi ya utii kutoka kwa Musa Efendi kama ifuatavyo:

Alikuwa akiguswa sana pale alipoona wazee wapweke katika jamii ambao wameachwa na ukiwa wao bila ya kusimamiwa. Alikuwa akisema:

"Hatuna budi kuwachukua watu hawa na kuishi nao katika nyumba zetu, na kama haiwezekani basi hatuna budi kuwajengea sehemu zao zenye usalama".

Kwa ushirikiano na baadhi ya marafiki zake wa karibu waliweza kulifanyia kazi wazo hili. Mara kwa mara walikuwa wakiwatembelea watu hawa na kuwakidhia haja zao.

Moyo wa Musa Efendi ulikuwa ukishughulisha na hata paka katika bustani yake na alikuwa akiwapa majina kulingana na tabia zao, na alikuwa akiwahudumia kulingana na upendo wao kwa watoto wao.

Kulikuwa na nesi ambaye alikuwa akinisimamia wakati nilipokuwa mdogo, na baada ya miaka 55 nilimtafuta na kumuonyesha heshima na ukarimu.

Utii wake aliokuwa akiuonyesha kwa kiongozi wake wa kiimani aliyeitwa Sami Efendi ulikuwa ukijulikana na wote. Wakati wa sherehe za eid sehemu ya kwanza kuitembelea ilikuwa ni nyumba ya Sami Efendi. Na pia kila alipochinja mnyama wa kwanza kumpa alikuwa ni yeye. Alikuwa sababu ya Qur'an kusomwa kwa ajili yake na moyo wake ulikuwa ukiridhika sana pindi inapokuwa kila mwaka maelfu ya *'hatm-i sharif*[88]' wanapomaliza kusoma Qur'an kwa kumkusudia mwalimu wake kipenzi.

Kwa ufupi ni kwamba alitufundisha kwa kupitia tabia zake nzuri zilizokuwa zimetawala maisha yake yote namna ya kumtendea wema yule unayempenda. Kwa namna hii alikuwa kama Abu Bakr ﷺ katika upendo wake na utii.

Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie sote tuwe na tabia yake hii yenye kupendeza.

Ewe Mwenyezi Mungu! Tufanye tuwe miongoni mwa watu wema kwa kutujaalia kuwa na tabia nzuri za watu watiifu. Jaalia uaminifu na usafi wa moyo katika matendo yetu na utujaalie tuwe warithi wa pepo. Tujaalie watoto ambao watakuwa matufaha ya macho yetu na viongozi wa uchamungu. Tujaalie tuwe watiifu Kwako, kwa Mjumbe Wako, kwa mama na baba zetu, kwa nchi yetu na taifa letu na katika amana tulizoaminiwa kwazo. Tujaalie

88. H*atm-i sharif* ni kuisoma Qur'an yote.

tuishi katika mazingira ya kiimani katika hii dunia na kesho akhera kama ambavyo Wewe unaridhia …

Amin!...

**20. Kujihifadhi na kuwa na staha**

Kujihifadhi na staha ni kujichunga kutokana na kutekwa na namna zote uchu wa kinyama na maovu. Hii ndio sifa inayomtofautisha mwanadamu na viumbe vyote vingine. Kuipoteza sifa hii ni sawa na kupoteza utu wako na kuangukia katika daraja la viumbe wengine.

Kujihifadhi na kujiheshimu ni mambo muhimu kwa watu wote wema. Heshima, utu na kujiheshimu vyote vinategemea wema wa mtu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewataja watu wawili ambao walifikia kilele cha kujififadhi na machafu kama mfano wa kuigwa na waumini na pia amewasifu ndani ya Qur'an. Watu hawa ni nabii Yusuf عليه السلام ambaye kisa chake kimetajwa kwenye surat Yusuf, 'katika visa vilivyo bora zaidi'. Mtu mwingine ni Mariam ambaye ni mama wa nabii Issa, mwanamke ambaye amesifiwa katika sehemu mbalimbali ndani ya Qur'an. Qur'an tukufu inatufahamisha yafuatayo:

"**Na mwanamke aliye linda uke wake, na tukampulizia katika roho yetu, na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni Ishara kwa walimwengu**" (Al-anbiya, 21:91).

Wanaume na wanawake hao ambao wanajihifadhi watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi na watapata malipo makubwa[89]. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu wale waja wake wanaojihifadhi kama ifuatavyo:

89. Angalia al Ahzab, 33:35

"**Na ambao wanazilinda tupu zao, Isipo kuwa kwa wake zao au kwa iliyo wamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa. Lakini anaye taka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka**" (Al-Mu'minun 23:5-7).

Kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyowafundisha watu misingi ya imani na ibada, pia aliwafundisha misingi ya kimaadili katika msimamo, kujihifadhi na kuwasimamia ndugu zako. Pindi mtawala wa Byzantine aliyeitwa Heraclius alipomuuliza Abu Sufyan ni kipi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichowaamrisha watu, alijibu: "Anatuamuru kuwa waaminifu, wema na kuwasimamia ndugu zetu" (Bukhari, Badu al -Wahy, 6, Salat 1; Muslim, Jihad 74).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliweka mkazo juu ya umuhimu wa kujihifadhi kiasi kwamba alikuwa anawaapisha wanawake juu ya kuhifadhi tupu zao[90]. Aliwaambia waumini wote kuwa:

*"Yeyote atakayeniahidi kuhifadhi kilichopo kati ya midomo yake miwili (ndimi zao) na kuhifadhi tupu yake, ninamuahidi pepo"* (Bukhari, Riqaq, 23).

Kwa kuongezea ni kwamba suala la staha, kujihifadhi, twahara na ustaarabu kati ya wanawake na wanaume ni jambo lenye umuhimu mkubwa. Uislamu umekataza matendo yote maovu, kutokuwa na staha na matendo yenye kutia aibu.

Mahusiano ya aina yoyote yasiyokubalika kati ya wanaume na wanawake yanaanza kwa kuangalia. Ndio maana waumini wanawake na wanaume wameamriwa kutoangaliana kwa mapenzi na kuinamisha vichwa vyao pale wanapoongea:

"**Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao. Hakika Mwe-**

90. Angalia al Mumtihana, 60:12.

**nyezi Mungu anazo khabari za wanayo yafanya. Na waambie Waumini wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasionyeshe uzuri wao isipo kuwa unao dhihirika. Na waangushe shungi zao juu ya vifua vyao, wala wasionyeshe uzuri wao ila kwa waume zao, au baba zao, au baba wa waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzao, au iliyo wamiliki mikono yao ya kuume, au wafwasi wanaume wasio na matamanio, au watoto ambao hawajajua mambo yaliyo khusu uke. Wala wasipige chini miguu yao ili yajuulikane mapambo waliyo yaficha. Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa**" (Nuur, 24:30-31).

Aya ifuatayo ingawa wanaambiwa wake za Mitume lakini ni jambo la kuzingatiwa na waumini wa kike wote:

"Enyi wake wa Nabii! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine. Kama mnamcha Mungu basi msiregeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema. Na kaeni majumbani kwenu, wala msijishauwe kwa majishauwo ya kijahilia ya kizamani. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ wake. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baarabara" (Ahzab, 33:32-33).

Aya nyingine kutoka kwenye Qur'an inasema yafuatayo:

**"Ewe Nabii! Waambie wake zako, na binti zako, na wake za Waumini wajiteremshie nguo zao. Hivyo ni karibu zaidi kuweza kutambulikana wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu"** (Ahzab, 33:59).

Wale wanaume na wanawake ambao ni wageni kisheria pindi wanapotaka kitu kutoka kwa mwingine au wanataka kuongea cho-

chote hawana budi kujitahidi kadiri ya uwezo wao kuongea nyuma ya mlango au pazia.[91]

Watu hawana budi kujizuia na kuingia kwenye nyumba za wengine bila ya ruhusa. Pale watu wanapokuwa wanaishi katika nyumba moja hawana budi kuomba ruhusa pale wanapotaka kuingia kwenye vyumba vingine na pia hawana budi kuwafanya wahusika wafahamu kuwa wanakaribia vyumba vyao. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatufahamisha kuwa ni bora kujipamba na wema katika hali zote.[92]

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatilia uzito juu ya umuhimu wa waja wake kuwa wenye kujihifadhi na zinaa na kujipamba na tabia njema, ameliashiria jambo hili katika aya nyingi.[93] Ndio maana kuwazushia watu wema kumefanywa kuwa ni dhambi kubwa, na wahusika wameandaliwa adhabu ya *'hadd-i qazf '* (adhabu ya wazushi). Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema yafuatayo ndani ya Qur'an:

"**Hakika wanao wasingizia wanawake, wanao jihishimu, walio ghafilika, Waumini, wamelaaniwa duniani na Akhera, nao watapata adhabu kubwa**" (Nur, 24:23).

Hii ndio sababu iliyomfanya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aseme: "...Msiwatuhumu wanawake wema kwa zinaa"... (Tirmidhi, Isti'dhan, 33/2733).

Ni kweli kuwa sifa ya kipekee kwa mwanamke ni kujihifadhi kwake kutokana na zinaa. Maneno yaliyopita yanaonyesha uzito wa kumtuhumu mtu kuwa amezini. Jambo hili huwa ni uhalifu mkubwa hasa pale ambapo shahidi hakutoa ushahidi wa kutosha,

91. Angalia Ahzab, 33:53.
92. Angalia Nur, 24:58-60.
93. Angalia Nisa, 4:25; Maida, 5:5; Anbiya, 21:91; Nur, 24:4, 23; Tahrim, 66:12.

humpelekea shahidi kutiliwa mashaka juu ya taarifa aliyoitoa ambayo inaweza kumshushia mtu heshima yake ikiwa ni ya uongo.

Katika masuala mengine kama haya ni muhimu kuonyesha heshima pale mtu anapomuomba mtu mwingine kitu chochote. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewasifu waja wake wenye kujiheshimu kama ifuatavyo:

"**Nawapewe mafakiri walio zuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasio weza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiye wajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. Utawatambua kwa alama zao; hawang'ang'anii watu kwa kuwaomba. Na kheri yoyote mnayo toa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anaijua**" (Baqara, 2:273).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Masikini wa kweli sio omba omba wa kawaida ambaye amepewa kokwa moja au mbili za tende na kuondoka. Bali masikini wa kweli ni yule ambaye ingawa ana shida kubwa lakini haombi chochote kutoka kwa mtu yeyote kutokana na kulinda utu na heshima yake. Kwa ushahidi zaidi soma aya isemayo*: "***hawang'ang'anii watu kwa kuwaomba***" (Al-Baqara, 2:273). (Muslim, Zakat, 102).

*"Watu wa peponi ni wa aina tatu: 1- Gavana muadilifu na mwenye mali na ambaye anatoa sadaka; 2- Mtu mwenye moyo laini ambaye anawapenda watu wake wa karibu na waislamu; na 3- Muislamu mwenye kulinda heshima yake ambaye ingawa ana familia kubwa lakini anajizuia na kuwaomba wengine na anajizuia na kipato cha haramu"* (Muslim, Jannah 63).

*"Mwenyezi Mungu anamjaalia heshima yule ambaye anajizuia kutokana na kuwaomba wengine. Na Mwenyezi Mungu anamuokoa mtu kutokana na kuwa tegemezi kwa wengine pale anapoonyesha kuridhika na kile alichonacho"* (Bukhari, Zakat, 18).

Heshima ni moja miongoni mwa matawi ya imani na inahusiana na kujiweka mbali na mambo maovu na machafu, kufanya mambo kwa staha na bila ya kuvuka mipaka. Hisia ya utu ni msingi wa mambo yote mema na ni kinyume na mambo yote maovu na machafu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema yafuatayo kuhusu *hayâ* (kumuonea Mwenyezi Mungu haya), miongoni mwa sifa zinazopendwa mno na Mwenyezi Mungu:

*"Hayâ ni katika imani"* (Bukhari, Iman, 3).

*"Hayâ na imani vinaenda kwa pamoja, kimoja kitakapotoweka na kingine pia kitatoweka"* (Suyuti, I, 53).

*"Hayâ inapelekea kwenye wema"* (Bukhari, Adab, 77).

*"Hayâ za aina zote ni nzuri"* (Muslim, Iman 61).

*"Maneno machafu hayanufaishi chochote bali kuvunja heshima. Kwa upande mwingine hayâ na adabu vinavutia popote vinapoenda"* (Muslim, Birr, 78).

*"Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakuomba unijaalie uongofu, uchamungu, heshima na utajiri wa moyo"* (Muslim, Dhikr, 72).

Tabia za utu na staha ndizo tabia za pekee ambazo zinaweza kumlinda mtu dhidi ya mambo mabaya, maovu na fikra za tamaa za kimwili. Katika kumlinda muumini kutokana na aina zote za maovu adabu na staha vina ufanisi mkubwa kuliko sheria na sera mia moja. Katika jambo lolote lile inatosha kumuonya mtu juu ya utu na staha kwa kumwambia maneno: "Je hujionei aibu mwenyewe?"

Othman رضي الله عنه alikuwa ni mtu mwenye kuheshimika na alikuwa mfano wa kuigwa katika staha na haya. Mjumbe wa Mwe-

nyezi Mungu ﷺ anatufahamisha kuwa hata malaika walikuwa wanamuonea aibu. [94]

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewatahadharisha wale watu ambao hawana staha na ambao wanajaribu kuwaharibu wengine ili wasiwe na staha kama ifuatavyo:

"**Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui**" (Al-Nur, 24:19).

Wale ambao wanataka kuona kuwa watu wote katika jamii hawana staha watakuwa wameisababishia nchi yao na taifa lao uovu mkubwa. Watu wa namna hii ni wale ambao mwishoni wanakutana na hasara na madhara makubwa. Kwani kama ambavyo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema, kutokuwa na staha ndio sababu ya maangamizi:

"Bila shaka pindi Mwenyezi Mungu ambaye Nguvu na Utukufu ni wake anapotaka kumuangamiza mtu kwanza kabisa anamuondoshea haya. Pindi anapokuwa amemuondeshea haya basi hakuna kinachobaki zaidi ya kwenda kukutana na ghadhabu Zake. Pindi anapokutana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu, anapoteza uaminifu wake. Pindi anapokuwa kapoteza uaminifu wake anakuwa ni muovu. Pindi anapokuwa muovu anaondoshewa rehema yote. Na pindi anapokuwa kaondoshewa rehema yote, hakuna kinachokuwa kimebaki zaidi ya kulaaniwa. Na pindi anapokuwa kalaaniwa, kamba ambayo alijifunga na Uislamu inakatika moja kwa moja" (Ibn Majah, Fitan, 27).

***Matukio ya wema***

Abu Said Al-Khudri ؓ anasimulia:

94. Ahmad, I, 71; VI, 55

"Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa ni mwenye staha kuliko msichana ambaye ndio amefikia baleghe. Pale alipoona kitu ambacho hakukipenda ungeliweza kugundua kwa kuangalia uso wake uliobarikiwa" (Bukhari, Manaqib, 23; Abu Dawud, Haraj, 34-36).

Kamwe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hakuwahi kunyanyua sauti yake pindi alipokuwa anaongea. Alikuwa akipishana na watu taratibu na huku akiwa na tabasamu usoni mwake. Pale alipokuwa anasikia neno baya ambalo halikumfurahisha alikuwa hasemi kitu. Kutokana na uso wake kudhihirisha hisia zake wale waliomzunguka walikuwa makini mno na maneno yao na mienendo yao. Alikuwa hacheki kwa sauti ya juu kutokana na *hayâ*, maadili na adabu aliyokuwa nayo. Alikuwa akitabasamu tu. Alisema katika *hadith* kuwa:

*"Staha ni katika imani na mtu mwenye staha ataingia peponi! Kutokuwa na staha kunatokana na moyo mgumu; na yeyote mwenye moyo mgumu ataingia motoni"* (Bukhari, Iman, 16).

❁

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa hapigi miayo huku amemgeukia mtu usoni, haya ni kutokana na staha ya hali ya juu aliyokuwa nayo. (Munawi, V, 224).

❁

Siku moja babu wa Bahz ibn Hakim alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuuliza kuhusu kujihifadhi tupu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamjibu:

*"Hifadhi tupu yako isipokuwa kwa mkeo na mtumwa yeyote unayemmiliki"*. Mtu huyu huyu akauliza pia kuhusu suala la kuvaa wakati hakuna mtu yeyote sehemu ile. Alipata majibu yafuatayo:

*"Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi kuonewa hayâ (aibu) kuliko watu"* (Abu Dawud, Hammam, 2/4017).

Katika hadith nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kuweni makini na kuwa uchi! Kuna malaika ambao hawaachani na nyinyi isipokuwa pale mnapokuwa msalani au mnapowaendea wake zenu. Onyesheni staha mbele yao na kaeni nao kwa wema"* (Tirmidhi, Adab, 42/2800).

❁

Bila shaka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa na staha kuliko mtu yeyote mwingine. Hata kabla ya kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ sifa hii ya kipekee ilimtofautisha na wengine katika kipindi ambacho uovu ulisambaa mno kwa jamii. Mfano mzuri wa jambo hili ni huu ufuatao:

Wakati Al-Kaaba inajengwa tena Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa amebeba mawe pamoja na mjomba wake aliyekuwa anaitwa Abbas. Ili kuzuia bega lake lililokuwa wazi lisiumie Abbas alimwambia mpwa wake:

"Weka *izar* (msuli) yako kwenye bega". Alipojaribu tu kuiweka *izar* yake kwenye bega lake ngafla akadondoka chini na huku amegeuzia macho yake angani akasema:

*"Nionyeshe izar yangu"*. Akaiokota upesi na kujifunika nayo. (Bukhari, Hajj, 42).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuona mtu akioga katika sehemu ya wazi huku hajavaa nguo yoyote ya chini. Kutokana na jambo hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akapanda kwenye mimbar na kusema:

*"Mwenyezi Mungu aliyetukuka na Mwenye kuheshimiwa ni mwenye staha mno na mwenye usiri mno. Ndio maana anapenda*

*staha na kujihifadhi. Hivyo pindi yeyote kati yenu atakapokuwa anaoga na ajifunike"* (Abu Dawud, Hammam, I/4012).

❁

Miswar ibn Mahrama ﵁ anasimulia:

Nilikuwa nimebeba jiwe kubwa mabegani mwangu na huku ninatembea nalo. Nilikuwa nimevaa joho jepesi. Wakati lile jiwe liko mabegani mwangu joho langu lilinivuka. Sikuliacha lile jiwe nikatembea nalo vile vile. Kutokana na kufanya kwangu hivi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaniambia:

*"Rudi ukachukue joho lako, usitembee uchi"* (Muslim, Hayz, 78; Abu Dawud, Hammam, 2/4016).

❁

Ibn Mas'ud ﵁ anasimulia kuwa:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema:

*"Kuweni na aibu (kuweni na haya) mbele ya Mwenyezi Mungu kama anavyostahili"*. Tukasema:

"Ewe Mtume! Sifa zoye njema anastahiki Mwenyezi Mungu, sisi tuna staha mbele yake"

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akafafanua kama ifuatavyo:

*"Nilichomaanisha si hiyo aibu mnayoifikiria. Kuwa na haya mbele ya Mwenyezi Mungu kama anavyostahili ni kuhifadhi kichwa chako na viungo vingine vya mwili na kukumbuka mauti na kaburi. Yeyote anayependa maisha ya kesho akhera ajitenge na mapambo ya hii dunia na achague maisha ya akhera juu yake. Yeyote atakayefanya hivi atakuwa ameonyesha haya ya kweli mbele ya Mwenyezi Mungu kama anavyostahili"* (Tirmidhi, Qiyamah, 24/2458).

Junayd-i Baghdadi amesema:

“Staha ni kuangalia neema za Mwenyezi Mungu zisizo na kifani na kisha kutafakari namna tunavyozitumia kwa makosa”.

❁

Familia ya Firauni ambaye aliitawala Misri ilikuwa ni ya watu wenye kudhulumu na kujivuna. Pindi mwanamke mrembo alipoingia kwenye mji Firauni alikuwa akifahamishwa mara moja. Kama anakuwa ameolewa basi mume wake huuawa, na kama anakuwa na kaka basi kaka yake huombwa juu yake. Pindi nabii Ibrahim عليه السلام alipoingia ndani ya mipaka ya mji ule akiwa na mkewe Sarah kasri lilipata habari juu ya jambo hili. Waliambiwa kuwa kuna mwanamke mrembo ameingia ndani ya Misri. Kisha wakamchukua Sarah na kumpeleka kwenye kasri. Kuna hadith juu ya suala hili ambayo ni kama ifuatavyo:

“Pindi Sarah alipoingia ndani ya kasri upesi alichukua udhu na kuswali rakaa mbili. Alipomaliza akamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ifuatavyo:

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kama mimi ni miongoni mwa watu waliokuamini Wewe na Mwako na kuhifadhi tupu yangu isipokuwa kwa mume wangu basi naomba usiwaruhusu hawa makafiri wanishambulie” (Bukhari, Buyu’, 100).

Firauni alipotaka kumsogelea Sarah mara akakosa pumzi na kupooza. Hivyo Mwenyezi Mungu akamlinda Sarah kutokana na kufanyiwa uovu, kwani hali hii ilimtokea mara kadhaa.

Firauni akamuachia aende kutokana hofu na akampa zawadi ya kijakazi wake aliyeitwa Hajar. Aliwaambia wale waliomzunguka kwa mshangao:

"Mwanamke huyu ni jini. Kama atabaki na mimi kwa kitambo zaidi basi nitaangamia. Nimempa Hajar ili niepukane na madhara yake".[95]

Uzuri ulioje wa mfano huu wenye kuonyesha namna mtu anavyohifadhi staha yake, tupu yake na kuonyesha mwenendo mwema...

Qur'an tukufu inatueleza:

"**Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu**" (Al-Baqara, 2:45).

❁

Siku moja mwanamke mmoja wa kianswar alienda kwa myahudi mfua dhahabu kwa ajili ya kununua kitu. Yule myahudi akaanza kumsumbua yule mwanamke akitaka kumchafulia staha yake na heshima yake, hivyo akajaribu kumfanyia vitendo visivyo vya kimaadili. Pindi alipopiga kelele alijitokeza kumsaidia Muislamu mmoja aliyekuwa akipita na ambaye alishuhudia tukio lile, mtu yule akaanza kumshambulia yule myahudi. Kisha wakaanza kupigana mieleka. Yule Muislamu akawa mshindi kwa kumuua myahudi yule. Wayahudi waliokuwa pale karibu walimuua yule Muislamu na kumpelekea kufa shahidi. Mambo yakawa yameharibika mno na wakawa wamevunja makubaliano waliyokuwa wameyaweka pamoja na waislamu.

Kutokana na tukio hili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwakusanya wayahudi na kuwahutubia:

*"Enyi jamii ya wayahudi. Muogopeni Mwenyezi Mungu na kumbukeni maafa na adhabu iliyowakuta maquraysh, hivyo ingieni kwenye Uislamu. Kwani nyinyi (kati ya watu wote) mnafahamu*

95. Angalia uslim, Fadail, 154.

*kuwa mimi ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺniliyetumwa na Mwenyezi Mungu. Mmeliona hili katika vitabu vyenu na katika ahadi ambayo Mwenyezi Mungu aliiweka kwenu".*

Kisha alishauri makubaliano yao yafanywe upya. Hata hivyo majibu ya wayahudi yalikuwa ni ya kifedhuli mno. Kutokana na haya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺakatangaza vita na kabila la Bani Qaynuda.[96]

Huu ndio umuhimu wa heshima ya mwanamke wa kiislamu.

❁

Abu shahm رضي الله عنه anasimulia:

Siku moja nilipokuwa Madina msichana mmoja alipita mbele yangu. Nikamkaba shingoni kisha nikamuachia aende. Asubuhi ya kesho yake Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anapokea dhamana kutoka kwa watu. Nilimfuata kumpelekea dhamana yangu lakini alikataa na kusema

"Na sasa yule aliyemkaba mtu amekuja?" kisha nikasema:

"Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa kamwe sitafanya hivyo tena".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akakubali dhamana yangu. (Ahmad,V,294).

❁

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikutana na Muislamu kutoka Madina ambaye alikuwa anamshauri kaka yake aliyekuwa na aibu ili ajifunze kutokuwa na aibu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akamwambia:

96. Ibn Hisham, II, 426-329; Wakidi, I, 176-180; Ibn Sa'd, II, 28-30.

*"Muache kwani hayâ ni katika imani"* (Bukhari, Iman 1, Adab 77; Muslim, Iman 57-59).

❁

Ummu Khallad ﷺ alikuwa ni swahaba wa kike kutoka Madina. Alimtuma mwanae akapigane vita vilivyotokea kati ya waislam na kabila la kiyahudi la Bani Qaynuqa. Baadhi ya waislamu waliokuwa wamepata taarifa kuwa askari wa kiislamuu wamerejea kutoka kwenye vita na kwamba Khallad amefariki shahidi upesi walikimbilia kwenye nyumba ya Ummu Khallad kwa ajili ya kumpasha habari. Yule mwanamke wa kiislamu akachukua kilemba chake na kujifunika kwa ajili ya kwenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kujua hatma ya mwanae. Mtu mmoja aliyemuona akijifunga kilemba chake alimwambia:

"Mwanao Khallad amefariki lakini wewe umesimama hapo uanashughulishwa na kilemba chako".

Ummu Khallad katoa jibu lifuatalo zuri,jibu ambalo lilionyesha utambuzi wa mwanamke wa kiislamu:

"Nimempoteza Khallad lakini haimaanishi kuwa nimepoteza staha yangu (hayâ)".

Jibu hili la Umma Khallad lilipelekwa kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ambaye alisema:

*"Kuna malipo ya namna mbili kutokana na ushahidi wa Khallad".*

"Kwa nini ewe Mtume?" aliulizwa.

*"Kwa sababu aliuawa na wayahudi ambao ni watu wa kitabu".* (Ibn Sa'd, III, 531; Ibnu al-Asir, Usdu al-Ghabah, II, 140).

❁

Siku moja kundi la wanawake kutoka Damascus lilikuja kwa Aisha ambaye ni mke wa Mtume. Aisha akawaambia:

"Ninaamini mmekuja kutoka sehemu ambayo wanawake wanatembea njiani bila ya kujali staha yao". Wale wanawake wakajibu: "Ndio, hilo ni kweli". Aisha akaendelea:

"Lakini nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema kuwa: "Mwanamke anayetembea bila ya kujistiri katika maeneo nje ya nyumba yake atakuwa ameweka kizuizi kati yake na Mwenyezi Mungu". (Abu Hammam, 1/4010; Tirmidhi, Adab, 43/2804).

Mwanamke kama huyu anakuwa amejivua vazi la heshima na staha. Kwani Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amemuamrisha ajihifadhi kwa vazi la uchamungu. Kutokana na kitendo hiki anakuwa amevunja amri ya Mwenyezi Mungu ya kujifunika na amejizuia na kuwa mtu mwema.

❁

Pindi alipofariki mke wa mmoja wa washairi watatu wakubwa waliokuwa wakitumia mashairi ya tashtiti kutoka kwenye ukoo wa Ummayyad aliyeitwa Ferezdak, Hasan Basri alikuwepo kwenye mazishi yake. Wakati fulani Hasan Basri aliashiria kaburi na kumuuliza huyu mshairi ambaye alikuwa amewachafua watu na kujeruhi heshima yao kutokana na mashairi yake:

"Je umejiandaaje na akhera?" Mshairi huyu mkongwe akajibu:

"Kwa miaka sabini nimekuwa nikiandaa ushahidi wa imani yangu". Hasan Basri akajibu:

"Uzuri ulioje wa maadhalizi yako", kisha akaongezea:

"Hata hivyo kuna masharti katika ushahidi ya imani. Hivyo kuwa muangalifu na kuwashifu wanawake waliojihifadhi".

Siku moja mtu mmoja alimwambia Wahb ibn Munabbih:

"Je *"la ilaha illallah"* sio ufunguo wa pepo?"

Akamjibu:

"Ndio, vivo ndivyo. Lakini ni ufunguo gani bila meno? Kama ufunguo utakuwa na meno basi utaweza kufungua mlango, lakini kama hauna meno mlango utabakia umefungwa" (Bukhari, Janaiz, 1).

Meno ya ufunguo wa tawhid (kumpekwesha Mwenyezi Mungu) ni wema na matendo mema.

❁

Watu katika dola ya Uthmainiyya walihakikishwa kulindiwa heshima na utu wao. Kwa mfano katika maagizo aliyoyatoa Fatih baada ya kuitwaa Bosnia alisema:

"Askari wangu wawe makini wasije wakawepo kwenye chemchem wakati wasichana wa Kiserbia wanachota maji..."

Kwa maagizo haya Fatih alikuwa amehifadhi heshima ya askari zake na wale wakiristo waliokuwa chini ya utawala wake.

❁

Katika kipindi cha utawala wa Sultani Suleiman suala la kucheza muziki hadharani, watu kutokuwa na staha na matendo mengine maovu yalikuwa yameanza kujitokeza. Baada ya Suleiman kuyasikia haya upesi alimtumia mfalme wa Ufaransa maelekezo:

"...Nimesikia kuwa namna fulani ya burudani ya kiovu inayoitwa kunengua imeanzishwa ambapo wanawake na wanaume wanakumbatiana mbele ya watu na wanaenda kinyume na maadili na staha. Kuna uwezekano kitendo hiki cha kiovu kikasambaa mpaka kwenye taifa langu kutokana na kupakana kwetu. Hivyo punde tu utakapoipata barua hii hakikisha unasimamisha matendo hayo mara moja. Na kama hutafanya hivyo nina uwezo wa kuja huko na kusimamisha matendo hayo mimi mwenyewe".

Mwanahistoria anayeitwa Hammer ameandika kuwa kutokana na barua hii unenguaji wa hadharani ulipigwa marufuku kwa karne nzima.

❁

Mababu zetu walikuwa wakiweka visanduku vya sadaka katika wilaya za Istanbul. Visanduku hivi vilikuwa maarufu mno, ndani yake walikuwa wakiweka fedha na mahitaji mengine kwa ajili ya watu wenye shida kuja na kuchukua watakacho. Kwa njia hii wale waliokuwa wakijiheshimu mno na waliokuwa wakiona aibu ya kuomba hawakujisikia vibaya na walijiepusha na kuomba kwa watu wengine.

Visanduku hivi vya sadaka vimekuwa ni ushahidi wa namna watu walivyokuwa wakishindana katika kutenda amali njema na kuwahudumia watu. Wale waliokuwa na uwezo mkubwa walikuwa wakitoka usiku wa manane na kwenda kuweka sadaka yao kwa kupitia kwenye matundu yaliyokuwa juu ya visanduku hivi. Waliyafanya haya kutokana na msemo kuwa “mikono yao ya kulia haijui kilichotolewa na mikono ya kushoto”.

Baadae wale masikini lakini wenye kujiheshimu na wema ambao walikuwa wanaishi katika sehemu hizi walikuwa wanakuja katika visanduku hivi na kuchukua kile tu kinachowatosha bila ya kuzidisha. Na hasa wale ambao walikuwa wanafurahia kuomba omba nao ingawa walikuwa katika hitajio kubwa lakini walikuwa wakichukua kile kilichokuwa kinawatosha tu. Msafiri mmoja wa kifaransa ambaye aliandika makala kuhusu Istanbul katika karne ya kumi na saba, aliandika kuwa siku moja aliamua kutumia wiki nzima kukichunguza kisanduku kimoja wapo kilichokuwa na fedha ndani yake, lakini hakuona mtu yeyote kuja na kuchukua fedha zile.

❁

Kwa ufupi ni kwamba muumini hana budi kujiheshimu na kuwa na staha. Kwani nguvu yote ya matamanio na hisia za kidunia zinategemea katika kufikiri na kuona, hivyo hatuna budi kuzipamba nyoyo zetu kwa hisia chanya na fikra za wema ili kuhifadhi heshima na utu wako na kuweza kuiongoza nafsi. Pia kwa kuongezea ni kwamba ni muhimu sana kukaa mbali na marafiki wenye ushawishi mbaya.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kuweni na staha mbele ya wanawake wageni kwenu ili na wanawake zenu nao wawe na staha. Watendeeni wema baba zenu ili na watoto wenu nao wawatendee nyinyi wema. Pindi ndugu yako atakapokuja kukuomba msamaha kubali kumsamehe vyovyote itakavyokuwa. La sivyo hutaweza kuwa pamoja na mimi katika chemchem yangu peponi"* (Hakim, IV, 170/7258).

Staha ambayo ni pambo la mwanadamu ni kama ngao ya kiimani ambayo inamlinda mtu kutokana na aina zote za maovu. Inamfanya mtu aweze kutekeleza wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu na waja wake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ameelezea athari na umuhimu wa kuwa na staha kama ifuatavyo:

"Msemo mmoja wapo wa Mitume wa mwanzo ambao watu wengi walikuwa wakiutumia ni: kama huoni aibu basi fanya utakalo" (Bukhari, Anbiya, 54, Adab 78).

### 21. Akili *(Fatanah)* na utambuzi *(Firasah)*

Neno *Fatanah* ambalo linamaanisha akili isiyo ya kawaida ni moja kati ya sifa tano za Mitume. *Fatanah* si akili au mantiki ya kawaida bali ni utambuzi ulio zaidi ya kipaji. Ni udhihirisho wa akili juu ya utambuzi na utabiri ambao una ushirikiano na moyo.

Ili kutekeleza jukumu lao la kuhubiri dini vizuri bila ya kukosea Mitume yote ilikuwa haina budi kuwa na hii akili isiyo ya kawaida. Kinyume chake wasingeliweza kutoa ushahidi wenye nguvu ili kuthibitisha wanayoyasema na pia wasingeliweza kuwashawishi watu wayaamini yale waliyokuwa wakiwaambia.

Mitume wako juu ya watu wengine katika sifa zote na hasa katika akili, kipaji na utambuzi. Walikuwa na kumbukumbu imara, kiwango kikubwa cha utambuzi na uwezo mkubwa wa kimantiki na ushawishi. Walikuwa na uwezo wa kutatua matatizo magumu kwa urahisi mno. Walikuwa wakiongea kwa kutumia *'sehl-i mumten*[97]*i'* walipokuwa wanaelezea mambo fulani na hivyo wale waliokuwa wanaambiwa hawakupata tabu ya kuwaelewa ingawa uwezo wao wa utambuzi ulitofautiana kwa kiasi kikubwa.

Sifa nyingine ya Mitume ambayo ni firasah ina maana ya kuwa na akili ambayo inamuwezesha mtu kuongea na mwingine kulingana na uwezo wake wa uelewa. Kwani jambo ambalo linamfurahisha mtu linaweza kumhuzunisha mwingine. Hivyo kuwafundisha watu kunahitaji uwezo wa kutambua hali yao ya kisaikolojia na kuweza kutabiri matokeo kabla hayajatokea.

Tukio lifuatalo ni muhimu kwani linaonyesha namna Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alivyokabiliana na watu ambao walikuwa mbali na utambuzi na ambao walitoa hukumu bila ya kuyafahamu maamrisho ya dini vizuri na hivyo wakawa sababu ya watu kupata madhara.

Jabir رضي الله عنه anasimulia:

Wakati tulipokuwa katika msafara wa kivita mmoja wa marafiki zetu alipigwa na jiwe kichwani na kuanza kuvuja damu.

97. *Sehl-i mumteni* ni maneno ambayo ingawa kwa juu yanaonekana kuwa mepesi, marahisi na yamenyooka [yanaeleweka, yako wazi] lakini ukweli ni kwamba ni magumu kuyatengeneza na kuyaiga.

Mtu yule baadae akapoteza twahara yake (kutokana na ndoto) na hivyo akawa na janaba.

Aliwauliza wale waliokuwa karibu naye:

"Je kuna kibali cha mimi kutekeleza *tayammam* (kukusudia udongo)?"

Wakamjibu:

"Unaweza kutumia maji hivyo hatadhani kuwa kuna kibali cha namna hiyo kwako"

Yule mtu akaoga akiwa katika hali yake ya kujeruhiwa na matokeo yake akaiaga dunia. Tuliporudi kwa Mtume, alifahamishwa tukio hili.

Mtu alipandwa na hasira na kusema:

*"...tiba ya ujinga ni kuuliza. Ilikuwa inatosha kwake kutayammam na kisha kufunika jeraha lake kwa bendeji na kupangusa kwa maji juu ya bendeji ile na kisha kuonyesha viungo vilivyobaki"* (Abu Dawud, Taharah, 125/337; Ibn Majah, Taharah 93).

Hivyo ni sharti kwa kila Muislamu ambaye anafuata nyayo za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuwa na akili, kujielimisha, kuwa mwerevu, mwenye kuzingatia mambo na kuangalia mbele.

*Firasah* ni nuru ambayo Mwenyezi Mungu anaiweka ndani ya nyoyo za wale waja wake anaowapenda. Ni udhihirisho wa sifa za utambuzi, akili, ujuzi na uelewa ndani ya moyo wa mtu mwenye imani. Huku ni kutambua undani wa mambo na kuyapima kwa usahihi na kugundua kile kinachopita kwenye akili na kilichopo ndani ya moyo wa mtu kutokana na hisia na msukumo wa moyo. Hii *firasah* inaweza kuwa bahati kwa wale wanaojiweka mbali na majivuno ya nafsi na ambao wanayaangalia matukio kwa nuru ya Mwenyezi Mungu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

*"Kuweni macho na firasah ya muumini. Kwani pindi anapoangalia huangalia kwa nuru ya Mwenyezi Mungu"* (Tirmidhi, Tafsir, 15/3127).

Kutokana na hadith hii ameashiria kuwa kila *firasah* ya muumini inategemeana na kiwango cha imani yake. Hivyo *firasah* ya marafiki wa Mwenyezi Mungu, yani wale waumini wa kweli ni kubwa kuliko ile ya waumini wengine.

*Firasah* bora huanza kwa kufanya juhudi ya kufahamu siri ya mauti. Itawezekana kufahamu ukweli wa siri za hii dunia yenye kupita kwa njia ya 'kufa kabla hujafa'. Jalaluddin al Rumi amesema:

"Watu wenye akili ni wale ambao wanalia kwanza na kucheka baadae; Wapumbavu ni wale ambao kwanza wanajizamisha katika kicheko na kisha wanapiga vichwa vyao kutokana na majuto. Ewe mwanadamu! Kuwa mtambuzi na ona mwisho wa mambo yako tokea mwanzo na hivyo uokolewe kutokana na kuumia kwa majuto siku ya kiama..."

Sharti la firasah ni kwamba mtu anakula kilicho halali na anazama katika fikra za kuulea moyo. Hatua ya kwanza katika kutafakari na kuwa na moyo wenye hisia ni kuyaangalia matukio yanayokuzunguka kwa macho ya utambuzi. Mwenyezi Mungu amewaalika waja wake waangalie matukio yanayowazunguka kwa uoni wa mbali na kuchukua mazingatio, katika aya nyingi amesema:

"**Je! Hawamtazami ngamia jinsi alivyo umbwa, na mbingu jinsi ilivyo inuliwa, na milima jinsi ilivyo thibitishwa, na ardhi jinsi ilivyo tandazwa?**"[98]

98. Qaf, 6; Yunus 101; Ghashiyah 17-20; Nur, 43; Haj, 63; Ra'd 3; Anbiya 31; Nahl 65; Rum, 50; Muhammad 10…

Baada ya kuzitaja neema nyingi za Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'an, kisha Mwenyezi Mungu mara nyingi amekuwa akiwaita watu 'enyi watu wenye kuzingatia'[99]...Na anawataka wauangalie ulimwengu kwa jicho la utambuzi. Aya nyingine nyingi sawa na hizi zinauliza:

"**Basi hamfikiri? Basi hamtafakari? Basi hamtumii akili**"[100]

Hivyo mwanadamu amealikwa auangalie ulimwengu si kwa mtazamo wa kawaida usio wa kiakili bali kwa uoni wa mbali na akili ya kuelewa hekima yake.

Aya zifuatazo kutoka ndani ya Qur'an zinaonyesha umuhimu wa kuangalia mbali:

"**Hakika ilikuwa ni Ishara kwenu katika yale majeshi mawili yalipo pambana. Jeshi moja likipigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jingine kafiri likiwaona zaidi kuliko wao mara mbili, kwa kuona kwa macho. Na Mwenyezi Mungu humuunga mkono amtakaye kwa nusura yake. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye macho**" (Al-Imran, 3:13).

**"Na wakumbuke waja wetu, Ibrahim na Is-haqa na Yaa'qubu walio kuwa na nguvu na busara. Sisi tumewakhusisha wao kwa sifa ya ukumbusho wa Akhera. Na hakika wao kwetu sisi ni wateuliwa walio bora"** (Sa'd, 45-47).

"**Sema: Hii ndiyo Njia yangu - ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa kujua - mimi na wanao nifuata. Na ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina**" (Yusuf, 12:108).

99. Al'I Imran, 13; Nur, 44; Hashr, 2…
100. An'am, 50; Baqara, 219, 266; Muhammad, 24; Nisa, 82; Yasin 68…

***Matukio ya wema***

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliulizwa:

"Ewe Mtume! Je umewahi kumuabudia yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu?" Jibu lilikuwa:

"Hapana"

Kisha aliulizwa:

"Je umewahi kunywa pombe?"

Alijibu:

*"Hapana, kamwe! Hata kabla ya kukifahamu Kitabu na imani ya kweli nilifahamu kuwa vitu hivyo vilikuwa ni kinyume na imani"* (Diyarbakri, I, 254-255).

Kwa asili Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliumbwa na kupewa akili ya hali ya juu, uoni wa mbali na utambuzi.

❁

Miaka mitano kabla ya utume wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuanza maquraysh walitaka kuijenga tena Al-kaaba. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pamoja na mjombwa wake, Abbas walisaidia katika kazi hii. Ulipofika wakati wa kuweka jiwe jeusi mahali pake kila kabila lilitaka lipate heshima ya kuliweka lenyewe na hivyo yakatokea malumbano makubwa. Tukio lile lilipelekea wivu na uroho kiasi kwamba damu ikakaribia kumwagika. Watoto wa AbduDarr walileta bakuli lililojaa damu na kuweka makubaliano na watoto wa Adiy ibn Ka'b ya kupambana mpaka kufa na hivyo wakajiandaa kwa ajili ya vita. Ili kuimarisha kiapo chao walizamisha mikono yao ndani ya bakuli la damu. Maquraysh walibakia katika hali hii kwa takriban masiku manne au matano.

Mara mtu mzima kupita wote miongoni mwa maquraysh aliyeitwa Abu Umayya alisema kwa sauti ya juu:

"Enyi watu wangu. Sisi tunachotaka ni wema na wala hatutaki ubaya. Msiingie kwenye mashindano ya wivu wenyewe kwa wenyewe. Acheni kugombana. Kwa kuwa hatujaweza kusuluhisha jambo hili sisi wenyewe basi ngoja tumteue yeyote atakayekuwa wa kwanza kuingia kwenye Al-kaaba ili ahukumu kati yetu.Na wote turidhike na hukumu yake". Na kisha akawaonyesha Bani Shaybah, mlango wa Al-Kaaba.

Wakati ule ule Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akajitokeza mlangoni. Tabasamu likadhihirika kwenye uso wa kila aliyekuwa pale kwani aliyekuja alikuwa ni Muhammad muaminifu. Upendo, heshima na uaminifu wa maquraysh juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ulikuwa ukikua siku baada ya siku. Kila walipotaka kuchinja ngamia walikuwa wakimtafuta Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumuomba afanye maombi ya baraka katika jambo lile.[101]

Ndio maana punde tu walipomuona walisema:

"Angalieni, ni *Al- amin* (Muaminifu). Tunamkubali awe hakimu miongoni mwetu".

Walimuelezea tatizo lao. Kisha akamchagua mtu mmoja kutoka kila kabila na kisha akavua joho lake na kulitandika chini. Kisha akaliweka lile jiwe jeusi katikati ya joho lake na kumwambia kila mtu kutoka katika kila kabila ashikilie pembe yake. Wakalinyanyua na kulipeleka lile jiwe lililobarikiwa kwa namna ile na kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akalichukua na kuliweka mahali pake. Kwa namna hii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawa ameepusha kutokea kwa vita kati ya makabila na kuonyesha kiwango chake cha akili na uoni wake wa mbali. (Ibn Hisham, I, 209-214; Abdurrazzak, V, 319).

101. Abdurrazzak, V, 319; Ibn Kathir, Al Bidaya, II, 304.

Upevu wa akili aliouonyesha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika vita vyote alivyopigana katika njia ya Uislamu, na uoni wake wa mbali aliouonyesha katika mikataba ya amani, hasa ule wa Hudaybiya, na wakati wa kuitwaa Makka pale Hunayn, na mbinu zisizo za kawaida alizozionyesha pale Taif na haki aliyoisimamisha, vyote hivi vilikuwa ni vya hali ya juu na vitukufu kiasi kwamba hakukuwa na mtu wa kawaida ambaye angeliweza kuvifanya.

Na wakati mwingi watu wamekuwa na hamasa ya kuwaamini watu wenye uoni wa mbali na wenye hulka madhubuti.

❁

Pindi ilipothibitika kuwa nabii Yusuf hakufanya uhalifu wowote na hivyo kutaka kuachiwa huru alitumiwa Mjumbe ili ampe taarifa ile. Hata hivyo Yusuf hakutaka kuondoka jela mpaka itakapokuwa Mfalme amefahamu fika ni nini kilikuwa kimetokea, na jambo lile likawekwa wazi na kila mtu akakubali kuwa yeye hakuwekwa jela kwa haki. Kwa kutumia akili yake na kuonyesha msimamo aliwazuia wale waliokuwa wakimuonea wivu wasisababishe madhara zaidi. Alikubali kuachiwa huru kutoka jela pale tu itakapothibitishwa kuwa alifungwa kwa mashitaka ya uongo na hivyo hakutendewa haki na hivyo kuwa huru dhidi ya dhana ile ya uongo.

Hii ndio sababu waislamu hawana budi kujifunza kutoka kwa Yusuf na kuwa makini katika kuinua dhana yoyote dhidi ya wengine na kuzuia watu wasiwadhanie vibaya.

❁

Hata wakati nabii Suleiman عليه السلام alipokuwa bado mdogo alikuwa na akili ya hali ya juu na utambuzi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasimulia tukio lifuatalo ambalo linaendana na sifa hii ya nabii Suleiman:

*"...wakati fulani kulikuwa na wanawake wawili ambao walikuwa wanatembea njiani pamoja na watoto wao. Mara mbwa mwitu akatokea na kukimbia na mtoto wa mwanamke mtu mzima. Kisha yule mwanamke akamwambia yule mwanamke mwenzake (ambaye ni kijana):*

*"Mbwa mwitu amekimbia na mtoto wako". Yule mwanamke mwingine akajibu:*

*"Hapana, amemchukua mtoto wako".*

*Kisha wanawake hawa wawili wakaenda kwa nabii Daudi ili ahukumu kati yao. Nabii Daudi* عليه السلام *akahukumu kuwa mtoto ni yule mwanamke mtu mzima*[102]*. Baada ya kuondoka pale walienda kwa Suleiman ambaye ni mtoto wa nabii Daudi na kumuomba ahuku kati yao. Suleiman akawaambia:*

*"Nileteeni kisu. Akataka amgawe mtoto yule (aliyebaki) kati yao wawili".*

*Mara yule mama kijana ambaye ndiye mama halisi wa mtoto yule akasogea mbele na kusema:*

*"Hapana, tafadhali acha! Mwenyezi Mungu akurehemu. Huyu mtoto ni wa huyu mwanamke"*

*Kutokana na haya Suleiman akahukumu kuwa mtoto alikuwa ni wa yule mwanamke kijana"* (Bukhari, Anbiya, 40).

❁

102. Moja ya sifa za Mitume ni 'ismah' yani kutokuwa na dhambi. Hata hivyo hawajakingwa na '*zelle*', au kufanya makosa madogo madogo, kutokana na kuwa wanadamu. *Zelle* ni makosa yanayofanywa na Mitume bila ya kujitambua. Kuna hekima nyingi katika haya. Wakati mwingine kutokana kutokea makosa haya Allah Mtukufu huteremsha maamrisho. Wakati mwingine anataka Mitume wahisi udhaifu wao wa kibinadamu na wakati mwingine anataka kuwakumbusha watu kuwa hawa watu wasio wa kawaida nao pia ni wanadamu na wao pia wanaweza kukosea na hivyo kuzuia wasitukuzwe.

Kuna kisa kutoka kwenye kitabu *Arais-i Majalis* ambacho kiko kama ifuatavyo:

Kulikuwa na wanawake wawili ambao walikuwa na uoni wa mbali. Wote wawili walimtambua vyema nabii Musa.

Mmoja wapo ni Asia, mke wa Firauni. (Pindi Musa alipoletwa kwenye kasri akiwa kwenye kikapu, moyo wake ulimpenda na akaamua kumchukua na kumpeleka kwa Firauni na kumwambia:

"Muache mtoto huyu awe tufaha la macho yetu. Usimchinje".

Mwingine ni binti wa nabii Shuaib. Alitambua tabia nzuri ya Musa na kumwambia baba yake:

"Baba mpendwa! Muajiri ili achunge wanyama wetu. Atakuwa mbora miongoni mwa wengine ambao huwa unawaajiri, yeye ni mwenye nguvu na muaminifu mno".

Kwa uoni wake wa mbali, Safura ambaye ni binti wa Shuaib aliitambua hali ya uaminifu ya Musa kwa usahihi. Alipoulizwa aliwezaje kufanya hivi alijibu:

"Hakuangalia hata nyuso zetu. Na alipokuwa anatembea, alitembea mbele yetu. Kwa namna hii tuligundua kuwa alikuwa ni mtu muaminifu mno"

❁

Inamuwajibikia kila Muislamu kupata mgao wake wa fatanah juu ya Mitume, yani ufahamu wao unaotoka moyoni, uoni wao wa mbali na utambuzi wao na kutumia neema hii katika njia iliyo bora. Muislamu hana budi kufahamu ni kipi cha kusema na kukisema kwa mtu sahihi, kwa muda muafaka, katika njia sahihi na katika sehemu sahihi.

Kwa mfano werevu aliouonyesha Jafar Tayyar رضي الله عنه wakati anaongea na mtawala wa Abyssinia katika kumfahamisha kuhusu

Uislamu ni wenye maana sana katika kuonyesha utambuzi ambao Muislamu anatakiwa awe nao. Pindi mtawala huyu wa kikiristo alipomuomba Jafar Tayyar ﵁ amsomee baadhi ya aya ndani ya Qur'an hakukimbilia kumsomea aya ambazo zinawakemea makafiri, kinyume chake alisoma aya ambazo zimemtaja nabii Issa na mama yake Mariam. Baada ya kuzisikiliza aya hizi zenye kuvutia kwa umakini mkubwa, mtawala huyu akasema yafuatayo huku macho yake yakiwa yamejawa na machozi:

"Hakika maneno haya yametoka kwenye chanzo kile kile ambacho Issa alikitumia kutuletea ujumbe". Baada ya muda mfupi akaingia kwenye Uislamu. (Ibn Hisham, I, 358-360).

❁

Kutokana na masimulizi ya Anas ﵁ mwenyewe siku moja alipokuwa anaenda kumtembelea Othman ﵁ alimuona mwanamke mmoja njiani. Uzuri wa mwanamke yule ulimvutia sana. Wakati bado fikra za yule mwanamke zipo kichwani mwake akafika kwa Othman ﵁. Othman akamwambia:

"Ewe Anas. Unaingia kwangu wakati bado alama za zinaa zimebakia machoni mwako".

Anas ﵁ alishtushwa na maneno haya hivyo akaamua kumuuliza:

"Je kuna ufunuo ambao bado unaendelea hata baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kuiaga dunia?"

Othman ﵁ akajibu:

"Hapana, huu ni uoni wa mbali na mtazamo ulio sahihi".[103]

❁

103. Kushayri, Risale, uk 238.

Pindi Abdullah ibn Omar رضي الله عنه aliposikia kuwa Hussein رضي الله عنه ambaye ni mjukuu wa Mtume, ameondoka na anaelekea Iraq, upesi aliondoka na kumfuata. Baada ya kusafiri kwa siku tatu mwishowe alimpata na kumuuliza:

"Ewe Hussein! Unaenda wapi?"

Hussein رضي الله عنه akajibu:

"Ninaenda Iraq". Ibn Omar akamuangalia Hussein na kugundua kuwa amebeba kifurushi cha karatasi. Hussein akamwambia:

"Hizi ni barua kutoka kwa watu wa Iraq". Ibn Omar akamwambia:

"Usidanganyike na barua zao wala usiende kwao"

Kadiri Ibn Omar alivyomsisitiza Hussein asiende lakini yeye alishikilia kuwa ni lazima aende.

"Kama mimi sitaenda basi ni nani atakayeenda?" akasema. Kisha Ibn Omar akaongea na Hussein رضي الله عنه kama ifuatavyo:

"Kama ni hivyo basi ngoja nikukumbushe hadith moja ya Mtume:

Siku moja malaika Jibril alikuja kwa Mtume. Akamuacha achague ama aendelee kubaki kwenye dunia hii au aende akhera. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alichagua akhera na kuiacha dunia. Wewe ni sehemu ya Mtume. Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kuwa hakuna hata mmoja miongoni mwenu ahl'ul bayt (familia ya Mtume) ambaye ataendelea hapa duniani mpaka siku ya kiama, yani hutakuja kumiliki utajiri, mali wala wadhfa au sifa kwa muda mrefu. Kinachokuzuia kuendelea ndani ya dunia hii ni kwamba akhera ni bora zaidi kwako na tayari umeshaichagua na kuiacha hii dunia.

Hata hivyo Hussein ؓ hakukubali kurudi pamoja na Ibn Omar. Alipoona hivi Abdullah ibn Omar ؓ akamkumbatia huku anatokwa na machozi na kisha akasema:

"Namuomba Mwenyezi Mungu akulinde, unakifuata kifo chako". (Ibn Kathir, Al-Bidaya VIII, 152; Zahabi, Siyar, III, 296).

Pia kaka wa Hussein ؓ ambaye ni Hasan ؓ alimuandikia barua Muawiya ili kuondoa matatizo na mtafaruku uliokuwa umejitokeza baina ya waislamu na ili kuzuia damu ya yeyote isimwagwe. Kisha akajitoa kwenye ukhalifa.

Hivyo matukio haya yanadhihirisha uoni wa mbali wa Abdullah ibn Omar ؓ juu ya maumivu na matatizo yatakayoipata familia ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kutokana na kujitolea kwao muhanga, kuwajibika kwao na kupenda kuutumikia Uislamu.

❁

Abdulqadir Jaylani (q.a) anasimulia tukio lililomtokea yeye mwenyewe:

Siku moja niliona mwanga unanimulika machoni mwangu na huku umetanda kwenye anga yote. Nilipokuwa ninajaribu kuangalia ilikuwa ni kitu gani mara nikasikia sauti kutoka kwenye ule mwanga:

"Ewe Abdulqadir. Mimi ni Mola wako. Nimeridhia na amali zako ulizozifanya mpaka sasa kiasi kwamba nimekuhalalishia vilivyokuwa haramu".

Hata hivyo punde tu sauti ilipokoma nikagundua kuwa ilikuwa inatoka kwa shetani na hivyo nikasema:

"Achana na mimi ewe uliyelaaniwa. Mwanga ulionionyesha ni giza la milele".

Baada ya haya shetani akasema:

“Kwa mara nyingine tena umeweza kuniepuka kutokana na hekima na utambuzi aliokujaalia Mola wako. Lakini nimefanikiwa kuwatoa mamia ya watu katika njia kwa kutumia njia hii”. Kisha akatoweka.

Nikanyanyua mikono yangu mbinguni na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili neema hii aliyonijaalia.

Mtu mmoja aliyekuwa akisikiliza haya maneno yangu aliniuliza:

“Ewe Abdulqadir, ulijuaje kuwa yeye ni shetani?”

Nikamjibu:

“Kutokana na alichokisema cha kuhalalisha vilivyo haramu kwa ajili yangu...”

Huu ni aina ya utambuzi ambao kila mmoja wetu anauhitaji katika maisha yake yote.

❁

Wakati wa kipindi kigumu cha dola ya Uthmainiyya, wakati ambao watoto wa mfalme wanashindana kwa ajili ya kiti cha enzi, jamii ilikuwa na ustahimilivu na ufahamu mkubwa wa historia kwa kiwango ambacho watu wa leo hawakifikii. Hawakuonyesha upendeleo miongoni mwa wale wana wa mfalme, na waliamua kusubiria matokeo ya ule upinzani uliokuwa umejitokeza kati yao. Ndio maana pindi Musa Chelebi alipowasili katika vitongoji vya Bursa ambao ulikuwa mji mkuu kwa wakati ule, watu waliwatuma wawakilishi wao waende kwake na kumwambia:

“Hakuna yeyote kati yetu ambaye anakuunga mkono wala anayekuchukia. Kama ndugu wewe lishughulikie suala hili mwenyewe. Wala usituhusishe sisi katika huu upinzani wenu usije ukafungua vidonda ambavyo havitawezekana kupona tena. Utii wa askari walio chini yako ni deni la dhamiri yako kwa wana wa

mfalme. Hata hivyo ombi letu kwako ni kuwa usije ukaruhusu huu mtafaruku ukaligawa taifa letu…"

Na hivyo ikawa nguvu kubwa iliyozuia mgawanyiko wa dola ya Uthmainiyya imetoka kwa hawa watu waliokuwa na uoni wa mbali, utambuzi, busara na tabia njema. Kinyume chake kama inavyoweza kuonekana katika mataifa mengine mengi kungelitokea umwagaji wa damu na vurugu miongoni mwa watu kutokana na uungaji mkono mbaya na kumfuata kiongozi mmoja.

❁

Timurlane ambaye alimshinda Yildirim Bayazid pale Ankara, aliagiza watu wa dola ya Uthmainiyya wawalipe fedha ya ulinzi wao, jambo ambalo liliendelea kwa miaka mingi.

Baada ya pale Ilhans akaendeleza makubaliano haya akidai kuwa yeye amechukua nafasi ya Timur. Makubaliano haya yaliendelea mpaka kipindi cha Murad Han wa pili. Wakati wa utawala wake dola ya Uthmainiyya ikapata tena nguvu yake na watu wakamuambia Sultani maneno yafuatayo:

"Ewe Sultani wetu. Kwa nini bado unaendelea kuwalipa hawa watu fedha za ulinzi?

Si tuachanane nao tu…"

Murad wa pili ambaye alikuwa mtawala mwenye akili na busara nyingi alitoa jibu lifuatalo kutokana na ombi lao:

"Wao bado hawafahamu kupanda kwetu na nguvu yetu ya sasa. Kama hatuwapatia fedha wanayoihitaji watakusanya jeshi ingawa litakuwa dogo na kupambana na sisi. Ingawa tutawashinda lakini damu ya waislamu itakuwa imemwagika…Hivyo acheni tuendelee kuwalipa hizo fedha wanazozihitaji. Sitaki kumwaga damu ya waislamu kwa ajili ya fedha…

Hata hivyo mnaweza kuonyesha uimara wa jeshi letu kwenye misafara ya Ilhans ili muwafanye wafahamu nguvu yetu na uimara wetu. Kwa namna hii hawatathubutu kuchukua fedha ya ulinzi kutoka kwenye taifa lililostawi na bora kuliko lao..."

Na kwa namna hii mambo yakawa kama ambavyo Murad wa pili alitabiri.

❁

Sababu moja wapo iliyomfanya Murad wa pili asisitize kutaka kwake mwanae aliyeitwa Mehmed Fatih wa pili aje kukalia kiti chake baada yake ilikuwa ni uwezo aliokuwa ameuona ndani yake. Kwani wakati bado ana umri mdogo mwana mfalme Mehmed alikuwa akitafakari na kufanya mambo ambayo hata watu wazima hawakutarajia kuwa angeliweza kuyafanya. Alikuwa akimuuliza baba yake maswali mazito mno. Siku moja alimuona baba yake akiwa katika bustani la kasri akamkimbilia. Baada ya kumuulizia hali yake alimwambia:

"Ewe baba yangu Sultani. Sifahamu hekima yake lakini nakuona licha ya majukumu makubwa na mzigo ulioko mabegani mwako hakuna dalili za uzee kwako tofauti na ninavyoona kwa watu wengine walio na umri mkubwa. Umezeeka kama watu wengine lakini wewe hujapinda kama wao. Ingawa umepitia misukosuko mingi lakini bado una nguvu, ushupavu na uhodari kama wa kijana na bado unaweza kutumia akili yako na uwezo wako kwa usahihi. Naangalia na nakuona wewe ni mshindi kwenye uwanja wa mapambano. Naangalia na nakuona wewe ni mwalimu mwenye busara katika uwanja wa kujifunza. Naangalia tena na nakuona wewe ni daruwesh ambaye unawatumikia watu kwa moyo safi...hakuna masiku yanayopita ambayo ni yako mwenyewe. Unawezaje kukusanya nguvu na kuyafanya yote haya bila ya kupinda mgongo wako. Wewe ni kama kijana mwenye msimamo na ufahamu. Umeweza kuihifadhi hiyo roho yako laini. Jambo hili

limewezekanaje baba? Akili kuendelea kushughulishwa inatosha kumchakaza na kumchosha mtu, lakini kwako hakukuleta mabadiliko yoyote wala hakukuvuruga hali yako ya amani. Ni dawa gani unayoitumia kwa ajili ya hali yako hii isiyo ya kawaida? Ni dawa gani unayokunywa kwa ajili ya uwezo wako huo mkubwa wa akili? Tafadhali nifundishe na mimi ili niweze kufuata njia yako..."

Huku akiwa ameshtushwa na maswali kutoka kwa mtoto wake mdogo lakini wakati huo huo akiwa amefurahishwa mno Murad wa pili alitoa maneno yafuatayo ya kihistoria kama ushauri kwa mwanae:

"Ewe mwanangu mpendwa. Umenifurahisha sana. Namuomba Mola wetu Mtukufu ambaye anaabudiwa na ulimwengu mzima na kila kilichomo ndani yake akuzidishie vipawa vya kipekee ambavyo amekujaalia. Mwenyezi Mungu akujaalie uendelee na mwenendo wako huo huo.

Ewe mwanangu. Bila kujali ni kipi kinasemwa na yeyote, ninaamini kuwa wale watu wanaoishi kulingana na misingi ya usawa na kuiaga hii dunia kwa moyo safi watakutana na neema zisizo na kifani ambazo ni vigumu kuzifikiria. Sina shaka juu ya hili. Ndio maana ninajaribu kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa moyo safi na kwa moyo wangu wote. Ninaamini kuwa Mwenyezi Mungu atanilipa kutokana na magumu ya hii dunia niliyoyapitia na ninajikinga kwake katika kila jambo. Kwa kuongezea ni kwamba ninaamini kuwa katika makadirio aliyoniandikia kuna wepesi mkubwa na furaha kwa ajili yangu.

Ewe mwanangu. Hauna budi kujiepusha na kuamini au kupumbazwa na kila neno linalosemwa. Ni muhimu kuchukua na kuchunguza undani wa kila jambo na kulileta karibu na ufahamu wako.

Kama ilivyo kwa tunda haliwezi kuliwa mpaka likomae, pia wale watu walioishi kwa muda mrefu na walio na ujuzi na uzoefu daima ni wale wanaochaguliwa miongoni mwa wenzao. Kinyume chake kula zabibu ambazo hazijakomaa wakati zilizokomaa zipo ndani ya uwezo wako ni udhaifu wa akili yako.

Ewe mwanangu. Muda baada ya muda huwa ninawakumbuka mababu zangu waliotangulia. Na wakati mwingine ninatafakari namna utakavyokuwa mwisho wa vizazi vinavyokuja baada yangu. Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia kufikia siku hii ambayo tuna mapenzi, heshima na utii juu yake. Ninatumani nitaendelea kufuata njia hii hii baada ya siku ya leo. Namna nilivyokuja katika dunia ndivyo ambavyo ninataka niondoke.

Fahamu kuwa- kuendelea kwa jambo lolote hakutegemei nguvu kubwa, upanga, ushujaa au ukali. Cha muhimu ni akili, busara, tahadhari, subira, utambuzi na kupewa mitihani mbalimbali. Mbinu ya kwanza daima haifai na ina madhara makubwa. Na ya pili haiwezi kukufikisha popote yenyewe. Hauna budi kuzitumia zote ili kufikia kwenye mafanikio makubwa. Usisahau ushindi mkubwa wa mababu zetu. Ingawa juu juu wanaoneka walipata ushindi chini ya kivuli cha upanga lakini ukweli ni kwamba hayo yaliwezekana kwa kupitia akili, mantiki na upendo.

Ewe mwanangu. Usijitenge na haki hata kama kwa kiasi kidogo. Kwani Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi ni muadilifu na anawapenda waadilifu. Kwa namna moja wewe ni mwakilishi wake hapa ardhini. Ameamua kukujaalia neema na fadhila nyingi na amekufanya uwe kiongozi wa watu. Kamwe usisahau jambo hili...

Ewe mwanangu. Katika dunia hii kuna watu wa aina tatu:

Kundi la kwanza ni la wale watu wenye akili na wenye kutafakari katika mambo yao, na ambao wanafikiria mambo yajayo na ambao ni wa kawaida na si watu wa ajabu.

Kundi la pili ni la wale ambao wamejiweka mbali na kufahamu ni njia ipi iliyonyooka na ni ipi iliyopinda. Hata hivyo hawakufikia kwenye hali hii kwa kutaka wenyewe bali ni matokeo ya ushawishi wa wale wanaowazunguka. Pindi wanaposhauriwa huwa wanarudi katika njia iliyonyooka; wanakubali ukweli na wanatafakari juu ya maneno wanayoambiwa. Lakini wakati mwingi wanaishi kulingana na wanayoyasikia kwa watu wanaowazunguka.

Kundi la tatu ni la wale ambao hawafahamu chochote kinachoendelea na wala hawazingatii ushauri na tahadhari wanazopewa. Wao wanafuata matamanio yao pekee na wanajiona wanafahamu kila kitu. Hawa ni watu hatari mno.

Ewe mwanangu. Kama Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi amekuumba ili uje kuwa miongoni mwa watu wa kundi la kwanza basi ninafurahia sana na ninamsifu na kumtukuza Yeye. Na kama uko katika kundi la pili basi ninakushauri usikilize ushauri na tahadhari unazopewa. Lakini jihadhari! Usiwe miongoni mwa watu wa kundi la tatu. Wao hawapo katika hali nzuri si mbele ya Mwenyezi Mungu wala machoni mwa watu.

Ewe mwanangu. Masultani ni kama watu ambao wameshikilia mizani mikononi mwao. Hata hivyo Sultani wa kweli ni yule ambaye ameushikilia mzani wake kwa usahihi. Nakushauri pindi utakapokuwa Sultani uweke uwiano sawa katika mzani wako. Hapo Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi atakutakia kheri. Atakufanya uwe miongoni mwa watu wema. Na Yeye ni mjuzi wa mambo yote...”

Uzuri ulioje wa utambuzi na akili isiyo ya kawaida ya baba na mwanae...

❁

Zaidi ya aina mbalimbali za huduma alizoziasisi Bayazid Wali wa pili kama vile vituo vya misaada, majengo makubwa na zahana-

ti, pia aliweka umuhimu mkubwa kwenye sayansi na utamaduni wa kiislamu. Kipindi alichotawala kilikuwa ni kipindi ambacho misingi ya utamaduni na ustaarabu wa dola ya Uthmainiyya ilikuwa imewekwa. Pindi Muitalia maarufu ambaye alikuwa na fani ya usanifu majengo na uchoraji aliyeitwa Leonardo da Vinci alipomuandikia Bayazid wa pili barua ya kumuomba amruhusu abuni miradi ya ujenzi wa misikiti na majengo mengine ndani ya Istanbul, mawaziri wa Kubbealti walifurahi sana. Hata hivyo Bayazid wa pili ambaye alikuwa na uelewa wa ndani wa tasawwuf alikataa ombi lake:

"Kama tutakubali ombi lake basi majengo ya taifa letu yatakuwa kama makanisa kimuundo na kiroho. Usanifu wa majengo yetu ya kiislamu hayatapata hadhi yake".

Mtazamo huu unadhihirisha akili, busara na usafi wa moyo wa Muislamu. Baada ya Bayazid wa pili ardhi za waislamu ziliongezeka na kufikia kilomita za mraba milioni 24. Kwa namna hii sanaa ya Uislamu ilifikia kilele chake. Ilikuwa ni kutokana na mtazamo huu itikadi ya Uislamu iliweza kuonekana katika majengo mbalimbali ya ibada kama vile Selimiye and Sulaymaniye, majengo ambayo thamani yake imeweza kuhifadhiwa na itaendelea hivi mpaka siku ya kiama.

❁

Bila shaka muhanga wa kwanza wa Palestina ni Abdulhamid Han wa pili. Alionyesha umuhimu mkubwa katika suala la Palestina na aliwaendea wayahudi ambao walikuwa wanaonekana kama hawana hatia kwa tahadhari na busara katika kupambana na matakwa yao. Abdulhamid Han wa pili alimwambiaTheodore Hertzl ambaye alitaka kuilipia dola ya Uthmainiyya madeni yake yote ya nje ili wawaachie waichukue ardhi ya Palestina:

“Sitauza hata kiasi kidogo cha udongo wa Palestina. Kwani ardhi hii si yangu, ni ya watu wangu. Na watu wangu waliipata ardhi hii kwa kumwaga damu yao. Kipande cha ardhi ambacho kimepatikana kwa damu ya shahidi hakiwezi kuuzwa kwa ajili ya fedha. Fahamu kwamba kamwe sitaruhusu ulaghai wako wa upasuaji unaotaka kuufanya katika mwili wangu”. Pia alichukua tahadhari kubwa ili kuiondoa hatari hii kubwa kuliko hatari zote.

Kwa kufahamu tunayoyafahamu leo hii tutaweza kuelewa vizuri uoni wa mbali na hekima ya Abdulhamid Han wa pili.

Mpaka leo hii jina lenye kutumiwa na wavulana wengi wa Palestina ni Abdulhamid. Wapalestina wanampa heshima kwa maneno: “Sisi ni yatima wa Abdulhamid”.

❁

Kwa ufupi ni kwamba uoni wa mbali na utambuzi ni sifa muhimu mno kwa muumini. Shah Al-Kirmani anasema:

“Yeyote anayeyachunga macho yake kutokana na haramu, na akaiweka roho yake mbali na matamanio na raha za kidunia zenye kudanganya; yeyote ambaye ni muangalifu kwa kile kilichoko ndani yake, na ambaye kwa nje anafuata *sunnah* au mwenendo wa Mtume; na yeyote ambaye anakula kwa kipato cha halali- mtu huyu kamwe hatapunguziwa uoni wake wa mbali na utambuzi wake”.

**22. Kuutakasa moyo na roho**

Hatua ya kwanza katika kuelekea kwenye tabia njema ambayo inampelekea mtu kuwa na sifa ya Uislamu ni kuitakasa *nafs*[104] yako na kuusafisha moyo wako. Pia kusafisha na kutakasa huku

104. *Nafs* ni roho ya mwanadamu ambayo imeegemea kwenye maasi. Hii ni asili ya kiunyama na matamanio ya mwanadamu. Neno nafs litaendelea kutumika katika kitabu hiki (Maelezo ya mfasiri).

ni kigezo kikubwa katika kujua kuwa mwisho wa mtu utakuwa mbaya au wenye furaha.

Ili kuitakasa nafsi na kuusafisha moyo kwanza kabisa mtu hana budi kujisalimisha kutokana na matamanio ya nafsi na tabia nyingine mbaya. Kila muumini hana budi kutambua udhaifu wake, kasoro zake, udhalili wake na ujinga mbele ya ukuu, nguvu na ukamilifu wa Mola wake. Hawana budi kuyaelekeza mambo yao kama ambavyo Mola wao anaridhia. Pindi jambo hili litakapofanikiwa basi nafsi itafikia mahali panapokubalika, itakuwa imejiweka mbali na sifa yake yenye kulaumiwa ambayo ndani ya Qur'an imetajwa kama "nafsi yenye kuamrisha mambo maovu"[105].

Kufanya juhudi katika kuitakasa *nafs* yako na kuendelea kuwepo kwenye hali hiyo kwa moyo safi inachukuliwa kuwa ndio 'jihadi kubwa', kutokana na umuhimu wake na kiwango cha ugumu wake. Haya ndiyo maneno aliyoyatumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pindi waliporejea kutoka kwenye vita vigumu vya Tabuk. Katika vita hivi maswahaba walikuwa wamesafiri umbali wa kilomita elfu moja kabla ya kurejea nyumbani. Walivumilia njaa na kiu miongoni mwa magumu mengine. Nywele na ndevu zao zilivurugika na ngozi zao zilishika kwenye mifupa kutokana na njaa. Ni wakati huu walipokuwa katika hali hii ndipo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaambia maswahaba zake:

*"Sasa hivi tunarejea kutoka kwenye jihadi ndogo na kuelekea kwenye jihadi kubwa; tunatoka kwenye vita kutokana na matakwa na msimamo wa nafsi zetu".*[106]

Katika hadith nyingine nyingi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ amesema:

105. Angalia Yusuf, 12:53
106. Angalia Suyuti, Jamiu as-Saghir, II, 73

"*Mujahid* au mpambanaji wa kweli katika njia ya Mwenyezi Mungu ni yule anayepambana na nafsi yake mwenyewe" (Tirmidhi, Fadailu al-Jihad, 2/1621; Ahmad, VI, 20).

*"Mtu mwenye akili ni yule ambaye anayeingoza nafsi yake kwa kuiwajibisha na kujiandaa kwa kile kinachokuja baada ya kifo. Mpumbavu ni yule ambaye anafuata matamanio ya nafsi yake lakini bado anaendelea kutarajia kheri kutoka kwa Mwenyezi Mungu"* (Tirmidhi, Qiyamah, 25/2459; Ibn Maja, Zuhd, 31).

*"Kitu ninachohofia zaidi kwa umma wangu ni kwamba watafuata matamanio ya nafsi zao"* (Suyuti, I, 12).

Mafunzo ya kiutume ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yalitokana na kuendelea kupambana na nafsi yake. Matokea yake kutokana kuitakasa huku nafsi na kuusafisha moyo maswahaba ambao walikuwa nyuma yake wakawa watu wema ambao wamesafishwa dhidi ya uchafu wa aina zote na kuwa kizazi cha mfano.

Ibn Mas'ud ؓ alikulia chini ya maelekezo na muongozo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ hivyo alipitia katika hali ya kumsifu, kumshukuru na kumtaja Mwenyezi Mungu kwa wingi. Licha ya kuwa kwake na ufahamu mkubwa wa hadith aliokuwa nao kutokana na ukaribu wake kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ lakini alisimulia hadith 848 kwa sababu alikuwa ni wa kipekee mno katika kusimulia kitu chochote kilichosemwa na Mtume. Ibn Mas'ud ؓ alidhihirisha namna alivyokuwa chini ya uongozi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kama ifuatavyo:

"Tuliathirika mno na hali ya kiimani ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kiasi kwamba tukaweza kukisikia chakula tulichokila wakati tukifanya *dhikr* ya Mwenyezi Mungu" (Angalia Bukhari, Manaqib, 25).

Mwanzoni Ibn Mas'ud ؓ alikuwa mchunga kondoo. Lakini baada ya kuongozwa kwenye Uislamu na kupitia kwenye mafunzo

ya kiimani ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ moyo wake ukawa kama bahari yenye kina kirefu, safi na laini na kuwa kioo chenye kudhihirisha utukufu wa Mwenyezi Mungu. Shule maarufu ya Kufa ni zao la swahaba huyu maarufu. Mwanasheria wa kiislamu maarufu katika dunia hii, Abu Hanifa alipata mafunzo yake katika shule hii. Wanasheria wengine wanaochukuliwa kuwa maarufu katika dunia hii kama vile Solon and Hammurabi hawakuweza kumfikia Abu Hanifa. Kadiri pote la Hanafi lililoasisiwa na Abu Hanifa lilivyoendelea ndivyo ambavyo malipo yenye kuendelea yanavyoenda kwa Abu Hanifa. Hivyo Ibn Mas'ud ﵁ na maswahaba wengine kama yeye wanaendelea kukumbukwa licha ya miili ya kuzikwa chini ya ardhi. Utawala wao utaendelea kukumbukwa katika nyoyo za watu katika umma wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mpaka siku ya kiama.

Njia muhimu waliyoitumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ pamoja na marafiki wa Mwenyezi Mungu katika kuilea nafsi na moyo kiimani ni '*suhbah*'[107]. Maneno ya mtu aliyeitakasa nafsi yake kuusafisha moyo wake yanakuwa yamejawa na mguso mkubwa. Hisia na maneno haya ambayo yanatolewa kwa moyo safi yanaingia moja kwa moja kwenye moyo wa yule anayeambiwa na matokeo yake yanasababisha muitikio chanya na kuwa sababu ya kuenea kwa mafanikio na imani.

Wanachuoni na wenye elimu ni warithi wa Mitume, kwanza uandae moyo wako kwa kuulainisha na kuufanya uwe tayari kubadilika kabla ya kukufikishia ujumbe. Wanaandaa mazingira kwa ajili ya pepo mwanana za majuto kuvuma na kutuliza hasira na dhoruba ya ghadhabu za nafsi.

107. Neno *Suhbah* linatokana mzizi wa neno wenye kumaanisha uswahaba, mahusiano ya kijamii na urafiki. Hapa na kuendelea neno hili litatafsiriwa kama mahubiri (Maelezo ya mfasiri).

Mafanikio yatokayo kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mpaka kwenye nyoyo za viongozi wema ambao walifuata nyayo zake huwafikia waumini kwa kupitia mshikamano wetu na wao na mafundisho yao. Kwa njia hii mwenendo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ unakuwa umeingizwa kwenye nyoyo za waumini kulingana na uwezo wa nyoyo zao.

Kadiri mafundisho haya yatakavyotolewa kwa hamasa ya ibada ndivyo mafanikio yatakavyoongezeka. Mahubiri ya mtu huchukuliwa kulingana na moyo wa yule anayefikishiwa. Kumhubiria mtu ni sawa na kumuandikia maelekezo ya kiimani yule unayezungumza naye. Mahubiri yanayotolewa na kusikilizwa kwa moyo safi ni jambo lenye mafanikio makubwa; kueleweka kwake kutategemea hali ya moyo wa yule anayesikiliza.

Njia muhimu kuliko zote ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliitumia katika kuwafunza na kuwaongoza maswahaba zake ilikuwa ni mahubiri. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimueleza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yafuatayo:

"**Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa Waumini** " (Dhaariyaat, 51:55).

"...**Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji** " (Ghashiya, 88:21).

Jambo la kuzingatia ni kwamba maneno haya *'sahabi'* (Swahaba) na *'suhba'* (uswahaba) yanatokana na mzizi mmoja. Hisia za mapenzi, heshima na adabu waliyokuwa nayo maswahaba juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ ni mifano mizuri ya manufaa yanayopatikana kutokana na mazungumzo na muongozo wa kiimani. Katika hali ya kuelezea manufaa ya uswahaba na majadiliano na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na matokeo yake yenye kuleta amani katika nyoyo za watu yafuatayo yamesemwa:

"(Tulikuwa tukimsikiliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ huku vichwa vyetu vimetulia) kana kwamba ndege alikuwa ametua juu yake na sisi tunahofia kuwa tukijitingisha ndege huyo atakimbia zake" (Angalia Abu Dawud, Sunnah, 23-24/4753; Ibn Majah, Janaiz, 37; Ibn Sa'd, I, 424).

Hivyo madarasa duara ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ yalikuwa yakiendeshwa kwa hamasa kiasi hiki. Pindi alipokuwa akiongea wale waliomzunguka walikuwa wakimsikiliza kwa shauku na umakini mkubwa kiasi kwamba hali ya amani na raha iliweza kushuhudiwa na wengine. Maadili na adabu iliyotoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ mpaka kwa maswahaba zake iliwafanya waone ni karaha kumuuliza swali. Ndio maana walikuwa wakisubiria mabedui kutoka majangwani waje na kumuuliza Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ maswali ambayo yatamfanya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ atoe maneno ambayo watanufaika nayo.

Maswahaba waliobarikiwa ambao mwanzoni walikuwa katika ujinga walifikia katika hali hiyo kutokana na kuingia kwao kwenye Uislamu na kupata mafanikio yaliyotokana na mazungumzo, mafunzo ya kiimani na muongozo uliotolewa na Mtume, na baada ya kutakasa nafsi zao na kusafisha nyoyo zao kiasi kwamba wakawa watu wema katika dunia hii. Visa vya wema wao ambavyo vimepita katika midomo ya watu na kukita katika nyoyo zao vimeshinda karne zote na ardhi zote.

Hivyo matendo ya kuitakasa nafsi na kuusafisha moyo yana nafasi muhimu katika kujenga Uislamu. Kwanza kabisa mtu hana budi kujisafisha mwenyewe kutokana na kutoamini, ujinga, hisia za uovu, msimamo potofu na sifa chafu. Hivyo mtu hana budi kujitakasa kutokana na namna zote za makosa yanayotokana na imani, tabia na matendo, makosa ambayo yanapingana na dini hii ya wazi. Baada ya kuusafisha moyo na kuulinda kutokana na

namna zote za maovu, mtu hana budi baada ya hapo kuufunza na kuupamba kwa sifa za kiuchamungu kama vile imani, elimu, busara, hisia chanya na tabia hivyo kumpelekea kuendana na imani yake. Kwa kuwa mwanadamu ameletwa hapa duniani kwa ajili ya kujaribiwa hivyo atakutana na mateso makubwa yatakayo-sabishwa na *'nafs'* mpaka kufa kwake. Tabia hii imejaa maovu elfu moja. Hata kama atafikia daraja la juu la wema lakini bado ataendelea kuwa katika hatari ya hila, miito ya ulaghai na mitego ya nafsi na Shetani. Utukufu wa mja utaanza pale atakapojiweka mbali na hatari hizi na kujiepusha na mapambo ya dunia yenye kulaghai na kujipamba na uchamungu na mwishowe kurudi kwa Mwenyezi Mungu moja kwa moja.

Jalaluddin Rumi anaelezea kwa kina raha na mitihani ya mwanadamu kama ifuatavyo:

"Mtu anayeimiliki nafsi yake ni kama nabii Musa عليه السلام. Lakini mwili wake ni kama wa Firauni. Mtu anayemilikiwa na nafsi yake huisahau nafsi yake mwenyewe na kuanza kutafuta maadui nje.

Ewe msafiri katika njia ya haki! Kama unataka kuufahamu ukweli ni kwamba Musa na Firauni hawakufa; bali wanaishi ndani yako. Wamejificha kwenye uwepo wako na wanaendeleza mapambano yao ndani ya moyo. Ndio maana huna budi kuwasimamia watu hawa wawili ambao ni maadui wao kwa wao, waliopo ndani ya nafsi yako"

Rumi anasema tena:

"Usiunawirishe na kuukuza mwili wako moja kwa moja. Kwani ni muathirika ambaye anasubiria kuingia kaburini. Unachotakiwa kukifanya ni kuustawisha moyo wako. Mwisho wake ni Mtukufu na kitu ambacho kitasifiwa.

Upatie mwili wako mafuta na sukari kidogo tu. Kwani yeyote anayeulisha mwili wake kupita kiasi ataishia kuwa windo la matamanio ya nafsi yake na kuangamia.

Istawishe nafsi yako kwa chakula cha imani. Ipatie fikra chanya, uelewa mkubwa na chakula cha imani ili iende kwenye mafikio yake ukiwa imara"

Ukweli ni kwamba nafsi inafanya kazi mara mbili, pindi itakapotakaswa na kufunzwa itampelekea mwanadamu kupanda daraja na kufikia kwenye daraja lenye kuheshimika miongoni mwa viumbe vyote. Na kinyume chake kama haya hayatafanyika basi itaweza kuporomoka na kuwa chini ya walio chini. Kiuhalisia ni kama upanga wenye ncha mbili.

Nafsi yoyote isiyokuwa na muongozo wa kiimani ni kama kizuizi chenye kuleta maumivu ambacho kimefunika ukweli kwa ujinga. Pale tu mwanadamu atakapojiweka mbali na sifa hizi zenye kulaumiwa licha ya kuzuiwa na nafsi yake na kufikia mahali akaweza kuitakasa na kuisafisha nafsi yake na moyo wake, basi hapo ataweza kumkurubia Mwenyezi Mungu na wema na hata kuwapita malaika ambao hawana nafsi. Heshima ya ushindi huo inatokana na juhudi anayoifanya mtu katika kuitafuta.

Matokeo yake kuitakasa nafsi na kuusafisha moyo ni mambo ya lazima ili kujiepusha na maasi ambayo ni sehemu ya asili ya mwanadamu na badala yake kupanda mbegu za uchamungu. Kila mwanadamu atahukumiwa kutokana na namna alivyojitahidi katika kumfahamu Mwenyezi Mungu na kuongeza ujuzi juu yake na kufikia kiwango kikubwa cha kumfahamu Yeye kadiri ya uwezo wako na nafasi yako. Pia atahukumiwa kutokana na namna alivyotekeleza amali njema na kumsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi. Huu ndio 'utumishi' wa kweli. Kwa mtumishi wa Mwenyezi Mungu kufikia malengo haya itategemea na namna atakavyovuka vikwazo vya nafsi na kuijaza hisia za utukufu utakaopatikana kwa kuitakasa nafsi na kuusafisha moyo.

Kuitakasa nafsi ni suala lililopewa umuhimu mkubwa kiasi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anaapa kwayo mara kwa mara. Mwenyezi Mungu anasema yafuatayo katika Surat Shams:

"**Naapa kwa jua na mwangaza wake! Na kwa mwezi unapo lifuatia! Na kwa mchana unapo lidhihirisha! Na kwa usiku unapo lifunika! Na kwa mbingu na kwa aliye ijenga! Na kwa ardhi na kwa aliye itandaza! Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake, Hakika amefanikiwa aliye itakasa, Na hakika amekhasiri aliye iviza**" (As Shams, 91:1-10).

Pindi Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi anapoapa kwa kitu huwa ni ishara ya heshima na thamani ya kitu hicho na pia anaonyesha umuhimu na utukufu wa jambo litakalofuata baada ya kiapo. Aya zote hapa ni sawa isipokuwa kuna tofauti moja:

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa mara kumi ndani ya aya hizi, moja baada ya nyingine. Kisha baada ya hapo ili kuweka uzito katika maana Ametumia neno 'qad' ambalo linamaanisha uhakika zaidi, baada ya neno hilo anatufahamisha kuwa:

"…**Hakika amefanikiwa aliye itakasa (nafsi), Na hakika amekhasiri aliye iviza**"

Jambo la kuzingatia ni kwamba hakuna sehemu nyingine yoyote ndani ya Qur'an tukufu na katika jambo lolote lingine kinyume na kuitakasa nafsi ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa kiapo mara kumi mfulululizo. Ukweli huu unatosha kumdhihirishia mwanadamu namna ulivyo umuhimu na ulazima wa kuitakasa nafsi kwa ajili ya kumuongoa mwanadamu.

Katika *tasawwuf* kujitakasa inamaanisha kupunguza mahitaji ya nafsi na kuvunja utawala wake juu ya mwili na hivyo kuiruhusu imani kutawala mwili wake. Jambo hili litawezakana pale tu tutakapoongeza nguvu katika kupambana na nafsi kwa kupitia njia

ya riyazat, ambayo inahusiana na kula, kunywa, kulala na kuongea katika njia ya wastani. Hii ndio sababu inayopelekea katika *tasawwuf* nafsi inaongozwa kwa '*qillatul taam*' (kula kidogo), *qillatul manaam* (kulala kidogo) na *qillatulkalaam* (kuongea kidogo). Hizi ni njia za kwanza zinazotumika katika kuingoza nafsi. Lakini kama ilivyo katika mambo mengine, ni muhimu kutojiweka mbali na kuzipitia njia hizi kwa wastani pia. Kwani mwili ni amana ambayo Mwenyezi Mungu amemjaalia mwanadamu.

Kwa namna yoyote ile katika mapambano dhidi ya nafsi mwili hautaachwa kujaliwa bali utakuwa chini ya muongozo maalum. Kinachotakiwa si kuusahau mwili kabisa bali kuulinda dhidi ya kuvuka mipaka na kuuzoesha kwenda kama ambavyo Mwenyezi Mungu anaridhia.

Jambo lingine la muhimu katika kuitakasa nafsi ni kuufanya moyo uwe katika hali ya usafi. Kutokana na kuwa kwake kito katika msingi wake moyo ni sehemu ya kupaangalia kwa umakini mkubwa. Moyo ni sehemu tukufu ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anapaangalia sana. Kama isivyowezekana kwa mtu mwingine kinyume na mfalme kukaa katika kiti cha enzi cha kasri, vivo hivyo kasri la mwili ambalo ni moyo hauna budi kusafishwa dhidi ya uchafu wa aina yoyote ile na kumuacha Mwenyezi Mungu pekee, na hivyo kufuta aina zote za matamanio yenye kuangamiza ya hapa duniani na mambo mengine maovu. Kinyume cha haya yote ni kwamba moyo utakuwa umefungiwa kupokea neema za Mwenyezi Mungu. Haya hayamaanishi kuwa mtu hatakiwi kuwa na hisia za mapenzi kwa mwingine kinyume na Mwenyezi Mungu. Wale waliofanikiwa kuzitakasa nafsi zao na kuzisafisha nyoyo zao na kufanikiwa kuwa na moyo wa upambanuzi watakuwa wamejiweka mbali na mapenzi mengine kinyume na Mwenyezi Mungu. Lakini watu wengine hawawezi kufuta moja kwa moja mapenzi juu ya mali, watoto na vitu vingine. Ukweli ni kwamba mapenzi ya namna hii yanakubalika ili mradi hayavuki mipaka.

Ili kuweza kuelewa vizuri umuhimu wa kuusafisha moyo inatosha kuangalia hali yake ya kimaumbile na kiroho katika maisha. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliashiria umuhimu wa moyo kama ifuatavyo:

*"Kuna kipande cha nyama katika mwili wa binadamu ambapo kikitengemaa basi na mwili mzima utakuwa umetengemaa, lakini kikiharibiwa na mwili mzima utakuwa umeharibiwa. Kipande hicho cha nyama ni moyo"* (Bukhari, Iman, 39).

Rumi anasema kuwa ni jambo la ajabu kuujaza mfuko ambao una tundu bila ya kuliziba kwanza. Vivo hivyo ni wazi kuwa pindi amali zitakapotekelezwa kwa moyo safi zinaweza kuwa sababu ya furaha na uongofu kwa mwanadamu. Haya ni kwa sababu matendo yanahesabiwa kutokana na nia ya mtu. Na nia ni kitu ambacho mahali pake ni moyoni. Kutokana na haya tunagundua kuwa ni jambo la msingi kurekebisha nia ya mtu na kuifanya iwe ni kwa moyo safi.

Kiwango hiki kinaweza kufikiwa kulingana na mwalimu anayeupa moyo mafunzo.

Lengo la wale marafiki wa Mwenyezi Mungu ambao wanajaribu kuupa moyo mafunzo ni kufikia daraja la *ihsan* au utambuzi wa kuwa na Mwenyezi Mungu wakati wote. Kwa namna hii watakuwa na moyo wenye uhai. Ili moyo ufikie daraja hili hauna budi kusafishwa dhidi ya mapenzi na mategemeo ya yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu.

Moyo ambao utakuwa umefikia daraja hili utakuwa umepandikizwa mambo mazito. Moyo utakuwa ni kioo cha majina matukufu ya Mwenyezi Mungu na siri zake kulingana na kiwango ambacho utakuwa umesafishwa dhidi ya uchafu wa aina yoyote na kuwa safi. Kwa namna hii mtu anaweza kufikia daraja la *marifatullah*, daraja linaloweza kufikiwa pale ambapo moyo utakuwa

umemtambua Mwenyezi Mungu kwa uhakika. Kisha maarifa hayo yanakuwa ni ujuzi mkubwa kwa mwanadamu.

Ni wale tu ambao wataenda mbele ya Mwenyezi Mungu huku wakiwa na nyoyo zilizotengemaa na ambao nyoyo zao zitakuwa zimetakaswa dhidi ya madhaifu yote ya kiimani na ambao watakaokuwa na nyoyo safi ndio watakaookolewa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an:

"...siku ambayo mali wala watoto..........." (Shu'ara, 26:88-89).

Kuna masharti kadhaa ambayo ni lazima yatimizwe kama mtu anataka kuwa na moyo uliotengemaa na nafsi iliyofikia katika hali ya kutosheka. Masharti hayo ni:

1. Kipato cha halali
2. Kuomba msamaha na kuomba dua nyinginezo.
3. Kusoma Qur'an na kufuata maamrisho yake.
4. Kutekeleza ibada kwa unyenyekevu wa hali ya juu.
5. Kutoa katika vile ulivyoruzukiwa.
6. Kuamka kufanya ibada nyakati za usiku.
7. Dhikrullah (kumtaja Mwenyezi Mungu) na kumtambua.
8. Kuendelea kumtumia maamkizi ya amani na baraka Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ na kumpenda.
9. Kutafakari juu ya mauti.
10. Kuongozana na watu wema na waaminifu.
11. Kuwa na tabia njema.

Kama kweli mtu atayatimiza masharti haya na kufanya juhudi ya kuyadumisha atafanikiwa kuwa na moyo uliotengemaa, ambao utakuwa umetakaswa dhidi ya yeyote yule kinyume na Mwenyezi

Mungu na atakuwa kama kioo safi ambacho kitakuwa kikidhihirisha sifa tukufu za Mwenyezi Mungu.

Mola wetu ni muumba na mmiliki wa kila kitu. Ndio maana hategemei kiumbe chochote. Hakuna zawadi yenye thamani kubwa ambayo inaweza kupelekwa mbele yake na ikawa imekosekama katika hazina yake isiyo na mipaka. Yeye ndiye mwema kupita viumbe vyote, na ndiye chanzo cha wema na uzuri wa aina zote. Ndio maana kitu kizuri na chenye thamani kupita viumbe vyote ni moyo safi ambao unadhihirisha majina yake matakatifu. Hivyo zawadi yenye thamani kubwa ambayo inaweza kupelekwa mbele ya Mola wetu ni moyo uliotengemaa, kitu ambacho ndicho anachokihitaji kutoka kwetu wakati wote.

***Matukio ya wema***

Pindi vilipokuwa vikipiganwa vita vya Mûta Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa juu ya mimbar ndani ya msikiti wake huku akiwaarifu maswahaba zake matukio yote yaliyokuwa yakitokea katika kila hatua ya vita. Uwanja wa mapambano ulikuwa ukionekana mbele yake. Uuaji uliokuwa ukiendelea ulikuwa ukisimuliwa kwa maswahaba kwa majonzi na huzuni. Katika kuzungumzia namna yalivyokuwa mapambano kati ya adui upande mmoja, shetani upande mwingine na nafsi zao wenyewe, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akisema yafuatayo:

*"Zayd ibn Harith amechukua bendera. Shetani amemsogelea upesi na anajaribu kumuonyesha namna uhai na hii dunia vinavyovutia na namna mauti yasivyopendeza na yalivyo mabaya. Lakini Zayd anamwambia yafuatayo na kuendelea na mapambano:*

*'Wakati huu ni muda wa kuimarisha imani ndani ya nyoyo za waumini. Lakini wewe unajaribu kunishawishi niipende dunia'. Ndio ameingia kwenye mapambano na mara ameuawa. Muombeeni msamaha kwa Mwenyezi Mungu".*

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaendelea:

*"Sasa hivi yuko peponi na anakimbia na kucheza kwa furaha huku na kule. Sasa hivi Jafar amechukua bendera. Upesi shetani amemkimbilia. Anajaribu kumuonyesha namna uhai na hii dunia vinavyovutia na namna mauti yasivyopendeza na yalivyo mabaya. Hata hivyo Jafar anamwambia:*

*''Wakati huu ni muda wa kuimarisha imani ndani ya nyoyo za waumini', kisha anakimbia na kwenda kushambulia jeshi la maadui na sasa ameuawa. Ninashuhudia kuwa kwa hakika yeye ni shahidi wa kweli".*[108]

Kisha akaendelea:

*"Muombeni Mwenyezi Mungu amsamehe ndugu yenu. Ameingia peponi kama shahidi. Sasa hivi yuko peponi, anaruka na kwenda popote anapopataka kwa kutumia mbawa mbili zilizotengenezwa kwa rubi".*

*"Sasa hivi Abdullah ibn Rawaha amechukua bendera"*, baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ kusema hivyo alikaa kimya kwa muda kidogo. Nyuso za Answar zikabadilika kutokana na kuanza kufikiria kuwa labda Abdullah ibn Rawaha amefanya jambo ambalo halimpendezi Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake. Hata hivyo wakati ule Abdullah alikuwa amechukua bendera na anawakimbilia maadui na wakati huo huo anapambana na nafsi yake:

"Ewe nafsi yangu. Niliapa kuwa nitakufanya ujisalimishe kwangu. Ama ufanye hivyo kwa kutaka mwenyewe au nitaku-

108. Ibn Omar ؓ anasimulia: "Tulimtafuta Jafar na kumkuta ni miongoni mwa mashahidi. Alikuwa katika hali ambayo tuliweza kuhesabu majeraha ya mishale na mikuki zaidi ya tisini [kifuani mwake]. Kati ya majeraha haya hakukuwa na hata jeraha moja mgongoni mwake" (Bukhari, Maghazi, 44). Jafar ؓ aliuawa akiwa na miaka thelathini na tatu (Ibn Hisham, III, 434).

lazimisha kufanya hivyo. Ninakuona huipendi pepo. Wewe si chochote bali chombo kilichojaa maji, ewe nafsi yangu. Unafikiri kama hutakufa sasa hivi hutakuja kufa tena? Kama utafanya kama walivyofanya wale wawili waliotangulia na kufa shahidi basi utakuwa umefanya jambo zuri. Kama utaacha kufanya hivyo utakuwa miongoni mwa wenye bahati mbaya".

Wakati ule kidole cha Abdullah kilikuwa kimejeruhiwa. Alishuka kwenye farasi wake na kukiangalia kidole chake kilichojeruhiwa na kuanza kusoma shairi lililokuwa na maana ifuatayo:

"Je wewe si kidole chenye kuvuja damu tu? Na yamekutokea haya wakati unapambana katika njia ya Mwenyezi Mungu" Kisha akakivuta kwa nguvu kidole chake na kukichomoa. Kisha akaendelea kupambana. Alikuwa akipambana kwenye jihadi ndogo dhidi ya maadui na wakati huo huo akipambana kwenye jihadi kubwa dhidi ya nafsi yake:

"Ewe nafsi yangu. Kama una wasiwasi kuwa utakuwa umetengana na mke wako basi fahamu ya kuwa tayari nimeshampa talaka. Na kama ni kwa sababu utakuwa umetengana na watumishi wako basi fahamu ya kuwa tayari nimeshawaacha huru. Na kama una wasi wasi kuwa utaacha bustani na miti yako basi fahamu ya kuwa nimevitoa kwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake".

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akaendelea kusimulia matukio yaliyokuwa yakiendelea kwenye uwanja wa vita:

"Abdullah ibn Rawaha akakusanya nguvu zake na huku ameshikilia bendera mkononi akaendelea kupambana na maadui mpaka akafa shahidi. Kisha akaingia peponi baada ya kusita kwanza. Muombeni Mwenyezi Mungu amsamehe".

Answar waliumizwa na kusikitishwa waliposikia kuwa Abdullah رضي الله عنه aliingia peponi baada ya kusita kwanza. Wakamuuliza Mtume:

"Ewe Mtume! Ni kwa vipi alisita?"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawajibu:

"Pindi alipojeruhiwa alisita kuendelea kupambana na maadui. Kisha akailaumu nafsi yake na kukusanya nguvu na kufa shahidi. Kisha aliingia peponi. Nilionyeshwa wote wakiwa peponi huku wamepumzika kwenye viti vya dhahabu. Lakini kiti cha Abdullah kilikuwa chini kidogo ukikilinganisha na viti vya wenzake wawili. Nilipouliza ni kwa nini niliambiwa:

"Abdullah alianza kupambana huku akiwa na wasiwasi kiasi fulani".

Ukweli kuwa Abdullah alikufa shahidi na kuingia peponi uliwafurahisha na kuwatuliza Answar.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa anazidi kusononeka kadiri alivyokuwa akiendelea kusimulia matukio yale na machozi kama lulu yalianza kutiririka kutoka katika macho yake yaliyobarikiwa. Kisha akasema:

"Sasa hivi upanga katika panga za Mwenyezi Mungu umechukua bendera. Matokeo yake Mwenyezi Mungu amewajaalia mujahid wawatawale maadui zao kwa urahisi" (Angalia Bukhari, Maghazi, 44; Ahmad, V, 299, III, 113; Ibn Hisham, III, 433-436; Waqidi, II, 762; Ibn Sa'd, III, 46, 530; Ibn Asir, Usdu al-Ghabah, III, 237).

Kama inavyoweza kuonekana kwamba Shetani na nafsi havimuachii mtu mpaka afe. Hivyo hatuna budi kuwa katika hali ya tahadhari wakati wote na kuwa katika hali ya kupambana na kujikinga kwa Mola wetu. Mwenyezi Mungu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an tukufu:

"**Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini**" (Al-Hijr, 15:99).

❁

Abdulqadir Jaylani, mmoja miongoni mwa watu wema alikuwa amefikia katika daraja la juu katika fani ya sayansi ya nje. Hata hivyo ili kuhakikisha kuwa anakuwa katika hali ya 'udhalili', yani kujiepusha na majivuno na kuikumbatia nafsi aliamua kujitenga na maovu yaliyokuwa ndani ya Baghdad kwa kipindi cha muda mrefu ili kuulinda moyo dhidi ya chochote ambacho kinaweza kumuweka mbali na Mwenyezi Mungu.

Katika miaka yake ya kwanza ya kuwa na Sheikh wake aliyekuwa akiitwa Nakshibend ili afikie hali ya 'udhalili mbele ya Mwenyezi Mungu' jambo ambalo ni kinyume na majivuno na kujiona, na hivyo kuitakasa nafsi yake, Abdulqadir Gaylani alianza kuwahudumia wagonjwa na watu waliokuwa na matatizo na wanyama waliokuwa wamejeruhiwa na hawana wamiliki. Aliwasimamia wote hawa na kufagia mitaa ya mji kwa kipindi cha miaka saba. Aliamua kuishi katika maisha ya kuwahudumia wengine.

Hivi ndivyo ulivyo ugumu wa kuitakasa nafsi na ndivyo ukubwa wa malipo yake unavyokuwa.

❁

Ingawa Imam Ghazzali alikuwa juu ya wanasayansi wote katika kipindi chake lakini aliishi kana kwamba alikuwa si kitu kwa muda mrefu na alijitenga na matamanio yote ya nafsi yake.

Imam Ghazzali anaelezea namna ufahamu wake ulivyokuwa juu kama ifuatavyo:

"Nilikuwa na ufahamu wa sayansi ya kiakili na kisheria. Nilikuwa na wanafunzi wengi sana. Nilianza kutafakari juu ya hali yangu. Niliona kuwa nilikuwa nimepumbazwa na raha mbalimbali. Nilikiria juu ya malengo ya elimu yangu. Nilikuta kuwa sikuwa naitoa kwa moyo safi na kutarajia radhi za Mwenyezi Mungu, kinyume chake nilikuwa nimechanganya na mapenzi ya wadhifa na umaarufu. Niligundua kwa hakika kuwa nilikuwa katika

maporomoko hatari ya maji tena katika ncha yake. Nilijisemea katika nafsi yangu:

"Fanya haraka na changamka kwani umebakiza muda mfupi wa kuishi. Kama ujuzi uliokuwa nao hauwi wa kweli kwa kuanza kuutumia kivitendo basi utakuwa si chochote bali uongo mtupu. Kama hutaachana na mambo yasiyo ya msingi na huondoi vikwazo vyote mwisho wako utakuwaje?"

Kisha kuna kitu kikatokea. Kwa kipindi cha miezi sita nilijikuta katika bonde la kushangaza, bonde lililopo kati ya kujitenga na dunia na mapambo yake na kuikimbilia akhera. Nililia na kusononeka kwa miezi sita. Moyo wangu ulikuwa katika shida. Niliuona na kuuelewa udhaifu wangu. Niliuona uwezo wangu wa kupambana na nafsi ukiniteleza kutoka mikononi mwangu. Nilikuwa kama mtu aliyekuwa na ugonjwa usiotibika au tatizo lisilo na suluhu. Nilimuomba Mwenyezi Mungu huku ninatokwa na machozi na nikamuomba ulinzi wake kwa unyenyekevu mkubwa. Matokeo yake kulingana na aya ifuatayo Mwenyezi Mungu akakubali maombi yangu na kuuamsha moyo wangu:

"…Yeye ambaye anawaitikia wenye shida pindi wanapomuita na kuondoa shida zao…" (an Naml, 27:62).

Niliondolewa matamanio ya kupenda mali na wadhifa. Niliyapa kisogo mambo yote hayo. Nilianza kujizoesha dhikr, upole, juhudi katika dini, kujizuia na machafu, kuitakasa nafsi yangu na kuirekebisha tabia yangu. Niligundua kuwa wale wanaoenda kwa Mwenyezi Mungu na ambao ni wasafiri katika njia ya uongofu ni watu wema wa *tasawwuf*. Wana tabia njema na heshima. Haya ni kwa sababu hali zao za ndani na nje zimechukua nuru kutoka kwa Mitume. Na hakuna nuru nyingine katika uso wa dunia ambayo inaweza kupita nuru ya Mitume" (Angalia, Ghazzali, "al-Munkidhu mina al-dalal," Istanbul, 1994 uk 35-39).

❁

Kisa cha namna Ibrahim ibn Adham ambaye alikuwa Sultani wa Balh alivyoanza katika kuitakasa nafsi yake na kuusafisha moyo wake ni kama ifuatavyo:

Siku moja Ibrahim ibn Adham alipitiwa na usingizi juu ya kiti chake katikati ya usiku. Mara ukelele mkubwa ukasikika kutoka juu ya dari la kasri. Makelele yakazidi kiasi kwamba yakamuamsha Sultani. Sultani akajiweka sawa upesi na kuita huku ameelekea kwenye dari:

"Ni nani wewe na unafanya nini juu ya dari katika nyakati hizi?"

Sauti kutoka darini ikasema:

"Tunamtafuta ngamia wetu aliyepotea ewe Sultani wetu".

Ibrahim ibn Adham akawafokea kwa hasira:

"Enyi wajinga na wapumbavu! Mmeona wapi mtu anamtafuta ngamia juu ya dari?"

Wakati huu jibu lililotolewa lilikuwa katika namna yenye kueleweka zaidi kutokana na uongofu na onyo lililopatikana:

"Ewe Ibrahim! Unafahamu kuwa ngamia hatafutwi juu ya dari lakini je hufahamu kuwa huwezi kumpata Mwenyezi Mungu wakati umekaa katika kiti chako huku umevaa joho la hariri, huku ukiwa umevaa taji kichwani na huku ukiwa na mjeledi mkononi mwako?"

Tukio hili liliamsha hamasa ya kiimani ambayo ilikuwa imeshaanza kupanda ndani ya moyo wa Ibrahim ibn Adham kwa muda mrefu. Lilimuacha katika hali ya mshangao na isiyo ya kawaida. Hata hivyo Sultani hakuweza kuachana moja kwa moja na mfumo wa maisha aliokuwa nao hapo mwanzoni.

Ibrahim ibn Adham alikuwa ametawaliwa na mapenzi ya kuwinda na alilifanya jambo hili kuwa desturi yake. Katika moja miongoni mwa safari zake za kuwinda alipata onyo lingine la kiimani, mwishowe onyo hili likamfanya awe msafiri wa kweli katika njia ya haki:

Siku moja alipokuwa mawindoni juu ya farasi wake alianza kumfukuzia swala. Alimkimbiza swala yule kiasi kwamba akaenda mbali na askari wake. Farasi wake akawa anatokwa na jasho na huku pumzi zimemuishia. Alikuwa amefika mbali na swala yule, mara mnyama yule mdogo na mzuri akamgeukia na kumwambia:

"Ewe Ibrahim! Je haya ndiyo uliyoumbiwa kwayo? Je Mwenyezi Mungu alikuumba si kwa lolote bali uweze kuniwinda mimi? Na nini utakachopata baada ya kunikamata? Ni kipi kingine utakachokipata zaidi ya kumaliza uhai wangu?"

Pindi Ibrahim ibn Adham alipoyasikia maneno haya akajihisi moyo wake unaungua kiasi kwamba akajirusha chini. Akaanza kukimbia kuelekea jangwani. Baada ya muda mfupi akaangalia na akawa hamuoni yeyote katika jangwa lile kubwa zaidi ya mchungaji. Upesi akamkimbilia na kumsihi:

"Tafadhali chukua vito hivi, joho hili la Sultani, hizi silaha na huyu farasi wangu na unipe hilo joho lako nilivae. Na usiiulize nafsi".

Huku yule mchungaji akiwa amepigwa na butwaa Sultani akalivaa lile joho la mchungaji na kuondoka. Yule mchungaji akamtazama na kujisemea katika nafsi yake: "Sultani amechanganyikiwa". Lakini ukweli ni kwamba Ibrahim ibn Adham alikuwa hajachanganyikiwa bali alikuwa amepata fahamu. Alienda kumuwinda swala lakini badala yake Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akamuwinda yeye kwa swala.

Haiwezekani kuidhibiti na kuitakasa nafsi bila ya kufanya juhudi na kufanya kila ambacho nafsi inakipenda. Juhudi ya makusudi inahitajika ili kuifanya nafsi iende kama ambavyo Mola wetu anaridhia na kuifikisha akhera kwa amani. Na mtu hana budi kuianza juhudi hii mara moja bila ya kupoteza muda, kwani kifo kinaweza kukufikia wakati wowote...

❁

Siku moja mmoja miongoni mwa marafiki wa Mwenyezi Mungu aliyeitwa Najmaddin-i Kubra alihudhuria mazishi ya mtu mmoja mwema pamoja na baadhi ya wanafunzi wake. Pindi imam alipoanza kumuandaa maiti kwa ajili ya maswali ambayo ataulizwa kaburini, Najmaddin akatabasamu. Wanafunzi wake wakastaajabu kumuona anatabasamu katika wakati ule na hivyo wakamuuliza juu ya hekima yake. Hata hivyo Najmaddin alitaka kubakia kimya.

Alipoona wamesisitiza sana akawajibu:

“Moyo wa yule anayemuandaa maiti ni mjinga lakini moyo wa maiti ndani ya kaburi uko hai na ni mzima kabisa. Nilistaajabisha na namna mtu mjinga anavyoweza kumuandaa mtu ambaye moyo wake uko hai na ni mzima kabisa”.

Muumini ambaye ameitakasa nafsi yake na kuusafisha moyo wake huwa anaendelea kuishi hata baada ya kufa. Wale wasioweza kufanya hivyo hawana tofauti na maiti hata kama bado wanaishi.

❁

Siku moja Mawlana Khalid-i Baghdadi aliondoka pamoja na baadhi ya marafiki kwa ajili ya kwenda kumtembelea Sheikh Abdullah-i Dahlawi. Baada ya safari yao iliyochukua miezi kadhaa-inasemekana kuwa safari yao ilichukua mwaka mzima- mwishoni wakafika Dahli (Jihanabad). Mawlana Khalid hakuweza kuchelewesha kwenda kumuona Sheikh wake hivyo akaenda kwenye nyum-

ba ya daruweshi wake pamoja na marafiki zake. Wale waliokuwa pamoja naye wakamwambia daruweshi aliyewafungulia mlango:

"Al-Hajj Mawlana Khalid Ziyauddin na marafiki zake ambao ni wanachuoni kutoka Sulaymaniye, Damascus na Baghdad wamekuja kumtembelea Sheikh".

Abdullah-i Dahlawi ambaye alikuwa na taarifa juu ya ujio wao alituma ujumbe ufuatao:

"Muacheni Khalid abaki! Na waambieni wengine warejee kwenye ardhi zao baada ya ziara fupi waliyoifanya"

Maagizo haya yalitiiwa na kisha yakafuata maagizo mengine:

"Muambieni Khalid aanze kusafisha ukumbi wa kuchukulia udhu mara moja"

Kwa kutambua kuwa hii ndio njia pekee ya kukubaliwa kuwa mwanafunzi wa Sheikh na hata bila ya kumuona Sheikh Mawlana Khalid hakukataa hata kidogo licha ya kuwa alikuwa mtu maarufu mno katika ulimwengu wote wa kiislamu na pia alikuwa na elimu kubwa. Alichukua ndoo na ufagio na kuanza kazi yake mara moja.

Alianza kukusanya maji yaliyokuwa yanahitajika kwa ajili ya kazi ile ya usafi kutoka kwenye kisima ambacho kilikuwa mbali kutoka kwenye nyumba ya daruwesh. Alikuwa akijaza ndoo yake kwa maji na kisha akiibeba mabegani mwake kwa kutumia fimbo nene. Alikuwa akitembea mara nyingi katika siku kwa ajili ya kutekeleza jukumu hili la usafi. Kwa njia hii alionyesha juhudi kubwa na ushupavu katika kuipa mafunzo nafsi yake. Pale nafsi yake ilipoonyesha dalili ya kusita au kulaumu alikuwa akitubu na kuomba msamaha upesi. Ikapita miezi mingi kwa namna hii.

Siku moja alikuwa amechoka sana kutokana na kusafisha vigae vya choo. Kipindi kile nafsi ikawa imepata sehemu ya udhaifu wake na hivyo ikaanza kumshawishi:

“Ewe bahari pekee ya elimu ya ardhi za Baghdad na Damascus. Ewe mtu mkubwa kutoka katika watu wakubwa, Mawlana Khalid! Umesafiri umbali mrefu mpaka hapa kwa ajili ya maneno ya mtu ambaye hufahamu kuwa ni Mtukufu au mwendawazimu tu. Na je umepata ulichokuwa unakitafuta? Angalia hapo ulipo, hakuna Sheikh wala safari ya kiroho. Je wamekufanyia chochote zaidi ya kukufanya usafishe vyoo kwa miezi kadhaa sasa? Je hii ndio elimu ya ndani uliyokuwa ukiitafuta...?

Khalid-i Baghdadi alishtushwa sana na ushawishi huu wa hatari uliotokana na nafsi na hivyo akaionya upesi kwa onyo lifuatalo ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa moyo safi:

“Ewe nafsi yangu. Kama hautakubali jukumu hili tukufu ambalo mwalimu wangu amenipatia kwa kushukuru na ukajaribu kuniweka nalo mbali hata kwa nchi moja basi nitakufanya ufagie sakafu si kwa kutumia ufagio bali kwa kutumia ndevu zangu mwenyewe...”

Abdullah-i Dahlawi alikuwa akiishuhudia hali yake hii kutokea mbali na huku anatabasamu. Kutokana na jambo hili la mwisho Mawlana Khalid alifanikiwa kuidhoofisha nafsi yake na baada ya hapo akaanza kuona malaika wakiwa wamebeba ndoo na ufagio wake. Cha zaidi ni kwamba nuru ilianza kung’aa kutoka kwenye mabega yake ambayo yalikuwa yamedhoofika na kuumia kutokana na kubeba maji mengi, pia nuru ile ilimulika hadi mbinguni. Kutokana na kufurahishwa mno na jambo hili Abdullah Dahlawi alimuita karibu yake mwanafunzi wake huyu asiye na mfano na kisha akamwambia:

“Mwanangu Khalid! Umefikia kiwango cha juu cha ufahamu. Hata hivyo ulitaka kuupamba kwa imani zaidi. Hivyo ukataka kuitakasa nafsi yako na kuusafisha moyo wako. Kinyume chake nafsi yako ingelikukokota mpaka kwenye mashimo ya majivuno na kujiona na kukuharibia kabla ya kumaliza. Sifa zote njema

anastahiki Mwenyezi Mungu kwa kukujaalia kuweza kuifagia nafsi yako chini ya nyayo zako na kukuwezesha kupanda vilele vya wema. Sasa hivi malaika wanakutekelezea majukumu yako".

"Mwanangu, Walimu wetu ambao ndio tumewafuata ni wale watu ambao walifanikiwa kupata undani wa sheria, njia, haki na kumfahamu Mwenyezi Mungu. Sasa hivi umejiunga nao na kuingia kwenye duara lao kama mhuishaji wa dini hii. Kwa sasa uongofu wa maduara mengine ya kiimani yanakusubiria wewe. Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi akuongezee matumaini".

Kutokuwepo kwa nafsi ghafi ambayo haijatakaswa na moyo uliozingirwa na mawingu ambao haujasafishwa, elimu yote iliyoko duniani haiwezi kumuongoza mtu. Ni baada ya masharti haya mawili muhimu kukamilishwa ndipo ambapo mtu anaweza kunufaika na imani yake.

❁

Aziz Mahmud alikuwa qadi (jaji) mkuu kabla ya kuingia kwenye mafundisho ya kiimani ya Muhammad Muhyiddin Uftada. Kwa sababu hii Muhammad Muhyiddin

Uftada akamuagiza auze maini katika masoko ya Bursa na pia asafishe vyoo vya nyumba ya daruwesh ili kwanza kabisa amfanye ahisi udhalili wake. Kutokana na mafunzo haya ya nafsi yake Qadi Mahmud akawa na daraja la juu kiasi kwamba akaweza kuwaongoza masultani na akapewa jina la *'Hudayi'* (lenye kumaanisha mwenye kuongoza) na mwalimu wake.

Siku moja mtu mmoja aliyekuwa amesikia kuwa Aziz Mahmud Hudayi alikuwa mzuri katika elimu ya alkemia alimjia na kumuuliza:

"Mwalimu nimesikia kuwa unaifahamu sayansi ya alkemia, unasemaje kuhusu jambo hili?

Bila ya Aziz Mahmud Hudayi kutosema lolote akanyoosha mkono wake kwenye mzabibu uliokuwa karibu yake na kuchuma majani matatu. Kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu yale majani matatu yakageuka na kuwa majani ya dhahabu.

Mtu huyu dhaifu aliyekuwa akishuhudia tukio lile kwa mshangao na yeye alijaribu kufanya kitu kile kile lakini hakufanikiwa. Aziz Mahmud Hudayi alimwambia:

"Mwanangu! Fahamu ya kuwa kujifunza sayansi ya alkemia inahusiana na kujifunza alkemia ya nafsi".

Lengo na dhumuni la maisha na utumishi si kuweza kufanya maajabu na miujiza bali ni kuitakasa nafsi yako, kuusafisha moyo wako na kujiepusha na sifa mbaya na hivyo kuwa muumini wa kweli.

Mshairi mkubwa na mtu aliyekuwa na upeo mkubwa wa kufikiria aliyeitwa Muhammad Iqbal anaelezea katika shairi lake umuhimu wa kuipa nafsi mafunzo na kuujaza moyo upendo:

Siku moja nilipokuwa maktaba nilimsikia nondo mmoja akimwambia nondo mwingine:

"Niliingia kwenye vitabu vya Ibn Sina nikaona kazi za Farabi. Nilipaa na kuzunguka kwenye sentensi zake zisizo na mwisho na herufi zilizofifia katika maneno yake na kisha nikazitafuna kurasa zake. Nilisafiri kwenye mitaa na vitongoji vya 'mji wa watu wema' wa Farabi. Hata hivyo sikuelewa falsafa yake. Nikawa msafiri katika jinamizi lao la mitaa isiyo na mwisho. Hakuna jua la kumulika siku yangu..."

Katika kujibu kilio cha yule nondo wa kwanza, yule nondo mwingine akamuonyesha mabawa yake yaliyoungua:

"Angalia", akasema. "Angalia nimeunguza mabawa yangu kwa ajili ya mapenzi". Kisha akaendelea:

“Kinachoyafanya maisha yawe na uhai zaidi ni juhudi na upendo; na kinachoyapa maisha mbawa ni ari na uaminifu katika mambo”.

Baada ya nondo wa pili kumuonyesha yule wa kwanza mbawa zake zilizoungua akaendelea kusema:

“Jiokoe dhidi ya kuangamizwa kwa msaada wa hii mitaa ya falsafa isiyo na kikomo. Pata faida katika upendo, hamasa na mafanikio yanayotokana na Mathnawi, bahari ya ufahamu na fungua mbawa zako na uingie kwenye makutano...”

Hivyo ili kuitakasa nafsi yako na kuusafisha moyo wako huna budi kushikamana na imani na kuzama ndani yake kwa upendo, uaminifu na kuonyesha juhudi na kuishi katika maisha ya utumishi.

❁

Pindi Mahiz Iz Hodja (Mturuki wa kisufi aliyeishi katika karne ya 20, na ambaye alikuwa akifundisha somo la usufi katika mashule ya kidini) alipoona kuwa vina vya moyo wake vilikuwa vimekosa ufahamu wa kweli, akagundua kuwa tiba pekee ya kuondoa upungufu huu ni uongozi wa kiroho, na hivyo akatumia miaka ya mwisho wa uhai wake katika safari ndani ya njia ya mafunzo ya kiroho. Aliielezea hali yake kama ifuatavyo:

“Kwa kuwa haiwezekani kuyakusanya sehemu moja yote ambayo watu wameyasema kuhusiana na ujuzi, mtu hana budi kuendelea kujifunza na kufanya upembuzi wa ujuzi wake. Na ninaamini kuwa ukweli unaweza kupatikana kwa kupitia uongozi wa wataalamu. Ndio maana nilipogundua kuwa niko katika hali ya kutojitambua nilijishikisha katika ujuzi na hekima za mwalimu Ramazanoglu Mahmud Sami ili nipande kuelekea kwenye mbingu za ujuzi.

Ili kufungua mbawa zako katika anga ya ujuzi huna budi kushikamana na jua la utambuzi ili uweze kupanda ngazi za upendo, uwezo na kutoa huduma.

❁

Kwa kumalizia ni kwamba kuitakasa nafsi na kuusafisha moyo ni amali ambayo haina budi kuendelezwa bila ya kusita katika kipindi chote cha uhai. Muumini hana budi kuwa katika hali ya kuichunguza nafsi yake wakati wote, na asifikirie kamwe kuwa ameshafaulu ili isije ikampelekea kuzidiwa nguvu na ushawishi na ulaghai wa nafsi yake. Rumi anatahadhirisha juu ya suala hili kama ifuatavyo:

"Hii nafsi dhalili na ovu inatamani kukuingiza katika faida ya muda mfupi ya hapa duniani. Ni kwa muda gani utaendelea kushughulishwa na manufaa haya yenye kupita? Je haitoshi kuwa umeshajivuruga mwenyewe vya kutosha?"

"Ingawa nafsi yako imekupa ahadi za wema tena na tena, lakini imeshazivunja ahadi hizo zaidi ya mara elfu moja na pia imeshavuruga toba yako"

"Hata kama ungelikuwa umepewa miaka elfu moja ya kuishi nafsi yako ingelikuwa ikitafuta dharura tofauti tofauti kila siku".

"Kama hiyo nafsi yako inayostahili kuchukiwa inataka upate manufaa ya kiroho, yani inataka utekeleze amali njema, usidanganyike nayo kwani nyuma yake kuna mtego wa adui yako huyo".

"Katika mkono wa kulia wa nafsi kuna ushanga na Qur'an iliyojificha kwake ni upanga na sime"

Tasawwuf ambayo inatilia umuhimu katika kuitakasa nafsi na kuusafisha moyo ni bahari isiyokuwa na kina. Ni ujuzi ambao unauzunguka ulimwengu mzima. Haiwezi kuelezewa bali kila mtu anaweza kuiongelea kulingana na uelewa wake na daraja lake.

Watu wa tasawwuf ni watu wenye tabia njema, wakarimu, wenye huruma, wapole na wanyenyekevu. Wanapatana na kila mtu na wanayaangalia maisha ya baadae kwa tahadhari kubwa. Matendo yao yote ni kulingana na maamrisho ya Qur'an tukufu na mwenendo, maadili na matendo ya Mtume. Wanampenda Mwenyezi Mungu aliye juu zaidi na kipenzi chake zaidi ya wanavyojipenda wao wenyewe, mali zao, utajiri na watoto.

Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie na sisi tuishi katika namna nzuri ya utumishi kama wao na utujaalie tutumie mtaji wa uhai wetu katika njia bora na yenye kukupendeza Wewe...

Ewe Mola wetu, zipambe nyoyo zetu kwa mapenzi ya imani. Tujaalie tuwe miongoni mwa wale ambao wanaweza kuona ubaya wa ukafiri na uasi na kujiweka nao mbali. Tujaalie tushikamane na mwenendo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ- na kuwa Qur'an iliyo hai. Tujaalie tuishi katika hali ya *ihsan* na kama mifano ya kuigwa katika wema. Zijaze nyoyo zetu kwa upendo. Tujaalie tuwe na hadhi ya kuitwa 'waja wako' vipenzi na kuitwa 'ndugu zangu' na kipenzi chako. Tujaalie tuvikuze vizazi vyema ambavyo vitakuwa ni vyenye kukupendeza katika hii dunia na kesho akhera na ambavyo vitatuombea baada ya kufa kwetu.

Ewe Mola wetu! Lilinde taifa letu na watu wetu dhidi ya kuicha Qur'an na imani na tulinde dhidi ya mwenendo mbaya. Tujaalie tuishi maisha ya peponi wakati bado tupo ndani ya dunia hii yenye kupita na utujaalie tujipambe kwa utukufu wa Qur'an. Tujaalie tukutumikie Wewe kwa namna ambayo itaruhusu vizazi vijavyo vinufaike na Qur'an...

Amin...

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

# FOR FREE IN PDF FORMAT

# ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT
**1350 BOOKS** IN **60 LANGUAGES** FOR FREE




Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org